# UAMBIE ULIMWENGU KWAMBA YESU ANAKUJA

Mervyn Maxwell

UAMBIE ULIMWENGU KWAMBA MASIHI ANAKUJA

(TELL IT TO THE WORLD THAT THE MESSIAH IS COMING BACK AGAIN)

https://youtu.be/szPRP-JN3KM

https://youtu.be/Eu8QkxXOQYE

USIACHE WATU GIZANI

Tafadhali tusaidie kuhakiki, tuwasiliane

Na Mervyn Maxwell

Uhamishoni.Ughaibuni.Mtandaoni.Majumbani

JE, UNAJUA KWAMBA MASIHI ANARUDI HIVI KARIBUNI ?

Kwa nakala ya kidijitali ya kitabu hiki, tafadhali tembelea RohoYaUnabii.Org, RohoYaUnabii.Net, MaarifaMtandaoni.Com, MaarifaMtandaoni.Africa

Asante kwa Wasomaji, Watafsiri, Wahariri, Washauri, Waombezi, Wanaufundi na wote ambao wanasaidia hii kazi ya Machapisho duniani kote:

Eline Mrema-Bariadi, Tanzania

Elias Luwela-Rukwa, Tanzania

Musa Budodi-Shinyanga, Tanzania

Mbusi Mpagalushu-Arusha, Tanzania

Nhandi Masunga-Iringa, Tanzania

Isaac Msusu-Kigoma, Tanzania

Ezekiel Ojwang-Tarime, Tanzania

Gerard  Nyafanga-Mara, Tanzania

Paul Momadi Masaka-Jersey, Marekani

David Jabez Masaka-New Jersey, Marekani

Daniel Nyangaresi Masaka-Kisii, Kenya

Grace Momadi-Masaka-Jersey, Marekani

# YALIYOMO

SURA YA 1.....4
"HAPANA, MUNGU. SIWEZI KUHUBIRI!" "HAPANA, MUNGU. HAPANA! "UNAJUA KWAMBA SIWEZI KUHUBIRI. "SIWEZI KUHUBIRI!".....4
SURA YA 2.....9
UAMSHO MKUU WA UJIO WA PILI.....9
SURA YA 3.....17
WAKATI WA KUKAWIA.....17
SURA YA 4.....22
KILIO CHA USIKU WA MANANE.....22
SURA YA 5.....27
"KWA NINI BABA HAKUJA?".....27
SURA YA 6.....33
KUINGIA KWA USHINDI II.....33
SURA YA 7.....39
"KLEOPA KATIKA SHAMBA LA MAHINDI ".....39
SURA YA 8.....44
NURU MPYA KUTOKA KWA NENO LA MUNGU.....44
SURA YA 9.....48
"TAZAMA JUU ZAIDI KIDOGO".....48
SURA YA 10.....54
“YESU ANAFANYA NINI SASA? ".....54
SURA YA 11.....59
MASHAHIDI WAJANE.....59
SURA YA 12.....67
KAPTENI AENEZA NENO.....67
SURA YA 13.....78
UJUMBE WA MALAIKA WA TATU.....78
SURA YA 14.....87
GAZETI LETU ZURI LA ZAMANI NA LA KWANZA KWENYE HISTORIA YETU YA MACHAPISHO- “REVIEW AND HERALD ".....87
SURA YA 15.....100
JE, WAADVENTISTA WANAWIWA NA WAKRISTO WENGINE?.....100
SURA YA 16.....108
YESU NA "HUKUMU YA UPELELEZI".....108
SURA YA 17.....119
KATIKA UHITAJI WA “AGIZO LA INJILI/INJILI YENYE UTARATIBU”.....119

SURA YA 18.....128
KUMPA MTOTO JINA.....128
SURA YA 19.....142
LAODIKIA.....142
SURA YA 20.....149
HISIA ZA UTUME.....149
SURA YA 21.....156
ALIYEKUWA PADRI WA KIKATOLIKI.....156
SURA YA 22.....164
FAMILIA YA WAMISHENARI WA NG'AMBO.....164
SURA YA 23.....173
HARAKATI ZA UTUME ULIMWENGUNI.....173
SURA YA 24.....184
WANAWAKE WANAOONGOZA.....184
SURA YA 25.....196
AMEVUVIWA KUOKOA ROHO.....196
SURA YA 26.....208
MAAZIMIO YA FURAHA, TAKATIFU NA YENYE AFYA.....208
SURA YA 27.....214
ZAWADI YA KRISMASI.....214
SURA YA 28.....223
KWA FURAHA YA HUDUMA.....223
SURA YA 29.....236
SUMAKU YA WEMA NA UCHESHI USIOLINGANISHWA WA KRISTO.....236
SURA YA 30.....248
MIAKA KUMI NA SITA YA MGOGORO.....248
SURA YA 31.....257
MDUARA WA UPENDO.....257
SURA YA 32.....268
KUNG'AA KWA UTUKUFU WAKE.....268

MWITO KWA MPENDWA MSOMAJI…

Hitaji letu kuu katika huduma hii ya Machapisho Uhamishoni ni Roho Mtakatifu, Ushauri, na Maombi yako msomaji. Wako watu wanaoishi nje ya Afrika wanahitaji pia kusoma kwa Lugha ya asili. Toka mtambo wa kuchapa ubuniwe kule Ujerumani mwaka 1456 na Johannes Gutenberg, Neno la Mungu limefikia mabilioni, ila bado kuna makundi karibu 6000 hayajafikiwa, angalia Joshugaproject.org na habari za '1040 window'.

'Sambaza Biblia popote,' ndiyo kauli mbiu ya muumini; sambaza Neno la Mungu kote.

Jiunge nasi katika kuandika vitabu, kutafsiri, kuhakiki, na kuhariri. Ikiwa kuna kosa lolote la kiuandishi au kiutafsiri, tafadhali wasiliana nasi na endapo ukiamua kuchapa, usibadilishe chochote labda typos tu.

Sasa umefika wakati wa kuandika vitabu ambavyo vinaendana na muktadha wa mazingira na utamaduni wetu, kwani ulimwengu wa Kikristo sasa umehamia Afrika na Amerika ya Kusini. Kwa hapa Kwetu Afrika Mashariki, tumekuwa wazito kuandika kuhusiana na Mada mbalimbali ambazo zinaendana na mazingira yetu; mada za afya, lishe, mahusiano kama ndoa, kilimo na mazao yake, kulea na kukuza watoto, aina za biashara zinazoendelea, hali ya kisiasa na muumini, utendaji wa kufikia watu na kujenga makanisa, nyimbo zetu na noti zake; haya yote tunayasoma na kuyaiga kwenye vitabu na mitandano ya magharibi na ni mema tu, lakini kama ulimwengu wa Kikristo umehamia kwetu, tunabidishwa pia kuwa waandishi kwa sababu tunajua hali yetu katika kufikia wengine au kuboresha afya na jamii kuliko mtu mwingine.

Kwa nini nyimbo zetu nzuri zenye ujumbe mzito zisichaguliwe kwa makini, nyimbo zenye ujumbe na zilizopendwa, zilizoimbwa miaka 50 hivi na kuwekwa kwenye vitabu na kisha watu waimbe? Tenzi tunazoimba za magharibi ni nzuri, ila hata wao wanaendelea kuziongeza vitabu, nasi hapa tuna nyimbo nzuri na zinaendana na utamaduni wetu na mtindo wetu wa kuchukua mafungu na kuelezea kisa fulani. Kwa nini basi tusijiongeze nasi, ili tuongeze kwenye maktaba yetu vitu vizuri, ikiwemo nyimbo za watoto?. Tuna wataalamu wengi wa nyimbo. Pia umefika wakati wa 'Reverse Mission' Watu wa Amerika ya Kusini sasa ni wainjilisti kila mahali duniani, ikiwemo magharibi kama vile Ulaya, Marekani na hata Asia, Australia, Mashariki ya kati na Afrika! Sisi Afrika tuna Waumini wengi kuliko Amerika ya kusini, na tunajua lugha nyingi kubwa kama Kifaransa na Kingereza, ila bado tunaona kwamba tupate waandishi kutoka nchi zenye Wakristo wachache kuliko sisi ambao hawaandiki kwa muktadha wa mazingira yetu na watoto wetu, na wanaona pengine wawe na vile vitu walivyo navyo nchi zingine au wawe na mwenendo kama ule.

Mfano mdogo sana ni, waandishi wengi wa nje huandika vitu vingine visivyoendana na muktadha wetu, mfano vyakula kama Pizza, Tambi, Kimchi, Taco, Panzit, Empanada, Manicotti, Tortellini, Sushi, au Falafel. Je viwanda vyetu hutengeneza vitu hivi? Kila chakula duniani kinacholimwa hufanana tu, ila jinsi ya kukitengeneza hupishana. Mwafrika atatumia ngano kupika ugali, Mhindi chapati, Mchina Noodle, Mzungu mkate au makaroni, nk.

Ni kweli Kiswahili ilikuwa lugha ya kuzungumzwa na siyo ya Maandishi, ila wakati umefika maandishi kuongezwa kwenye mambo mazuri! tunaelewa kwamba si utamaduni wetu kuandika, ila si utamaduni wetu kufanya mambo mengi ambayo sasa tunayafanya!

Si kila kitabu tunachoandika ni lazima kiuzwe, vingine ni vya kusaidia jamii; wewe hautaweza kuuza kila kitu katika dunia hii kama unataka kufanya uinjilisti au kubariki watu. Kitabu cha Jando na Unyago kwa Waumini ni vizuri tupate watu wa kutusaidia kuandika, kwani jamii inaishi sehemu tofauti, na hii inafanya kusiwe na Mafundisho au kujifunza kwa mambo fulani muhimu toka kwa Kabila la mtu kama ilivyokuwa, na wakati huo huo pengine serikali haiwezi kukidhi hitaji hili kwa urahisi.

Watu husema utamaduni wa mtu mweusi ni kusaidia jamaa na ndugu zake wa damu tu na wala sio umma. Yawezekana ni kweli ila tuna la kujifunza kutoka kwa kila mwanadamu. Wenzetu wa Nigeria wameanza kuweka vitabu vyao mtandaoni ili watu wasome na kufaidika katika nyanja mbalimbali kama vile uchumba, maombi ya kuondoa laana kwenye familia nk. Joel Nanauka ni mfano mzuri katika Ulimwengu wa Kiswahili kwenye kuandika na kugawia watu ujuzi wake. Tumevisoma vitabu vyake vizuri ambavyo ametubariki kwenye ujasiliamali nk. Ukiwa na chochote, hata ikiwa ni kama senti mbili za Mjane, ujuzi, uwezeshaji wa aina fulani, tafadhali usisite kuutoa na pia kama una ujuzi wa kuandika vitabu au kufundisha wengine kuandika vitabu, fundisha wengine, maana ulimwengu wa Kiswahili una umasikini wa Maandishi yaliyoandikwa kwa muktadha wa utamaduni, nyenzo, na maisha yetu ya kila siku.

UhamishoniUghaibuniMtandaoni@gmail.com au simu -1-908-343-3022- Bwana atubariki sote ili tukae Ndani Yake

YESU Anarudi! Roho na Bibi arusi waseme, “Njoo!” Kila mtu asikiaye hili, na aseme, “Njoo!” Aliye na kiu na aje; anayependa, na achukue maji ya uzima bila malipo. Amina. Njoo BWANA!

DIBAJI

Waadventista Wasabato hawajifikiri wenyewe kama watu wanaounda "jamii yoyote ya kidini." Wanalitazama kanisa lao kama tu vuguvugu lenye nguvu ya kiroho lililokabidhiwa ujumbe muhimu na kuchochewa na hisia ya utume. Ujumbe wao unamhusu Yesu: “Injili ya milele” Kuzaliwa Kwake, huduma Yake, kufa na kufufuka Kwake Kristo ili kuwapa watu wenye mioyo mipya; "tumaini la marejeo" katika ujio wa Kristo mara ya pili, kuwapa watu makao mapya; na “Ukweli wa Leo” kuhusu huduma ya wakati ule ya Kristo mbinguni, ikifuta dhambi kwa njia ya pekee na kutoa kafara/sadaka kuliko wakati mwingine wowote ili kuwafanya watu kuwa na afya njema, watakatifu, na wenye furaha. Dhumuni lao ni kuchukua habari hii iliyo njema sana na kuipeleka kwa ulimwengu-kwa kuwa habari hii sio tu ya watu ambao ni Waadventista Wasabato, bali ni ujumbe wa ulimwengu wote, wa kila mwanadamu, na kila mahali. Unapaswa kupelekwa kwa “kila taifa na kabila na lugha na jamaa”; kwa miji yote, na vijiji vyote; kwa kila nchi, jumuiya, koloni, na "kiumbe." Hiyo inamaanisha "mtu" (Marko 16:15). Kitabu kimoja hakiwezi kusema yote kuhusu Waadventista Wasabato. Kwa kuchagua, mwandishi huyu anaelezea zaidi jinsi harakati zao zilivyoanza, kwa sababu hiyo inaelezea vyema kile kinachofanya harakati hizi ziende mbele, na jinsi zinavyotarajia kumalizika, hivi karibuni.

## SURA YA 1
## "HAPANA, MUNGU. SIWEZI KUHUBIRI!" "HAPANA, MUNGU. HAPANA! "UNAJUA KWAMBA SIWEZI KUHUBIRI. "SIWEZI KUHUBIRI!"

Kabla William Miller hajajisalimisha kwa Bwana na kuwa kiongozi wa Uamsho mkuu wa Majilio ya Pili ya Yesu huko Amerika, alibishana na Mungu na dhamiri yake ikahangaika kwa miaka kumi na tatu. Twahitaji kusisitiza kuwa mwanzoni, hakutaka kuuambia ulimwengu kwamba Kristo anakuja upesi. Katika enzi ambazo moja ya kumi ya watu wa Marekani waliishi mashambani, William Miller pia alikuwa mkulima. Lakini hakuwa mtu wa kawaida. Akiwa bado mvulana, baada ya familia kwenda kulala usingizi, alikuwa anasoma vitabu, kwa mtindo wa Lincoln, kwa nuru ya nishati ya mafundo ya lami katika kibanda chake cha magogo huko Low Hampton, New York. Alioa mnamo 1803 na kukaa kati ya Milima ya Kijani ijulikanayo Appalachians, huko Poultney, Vermont, alimaliza haraka kusoma vitabu vya maktaba ya mahali hapo. Mke wake mpya, Lucy, alifanya kazi nyingi za shambani yeye mwenyewe, ili William Miller apate muda wa ziada wa kusoma.

Akiwa ni mtu wa kuchangamana na jamii na mwenye ari ya kazi na vile vile msomaji wa vitabu, Miller alichaguliwa mfululizo kuwa naibu msimamizi wa sheria, na msimamizi wa haki ya amani. Haikuchukua muda, naye akawa mtu tajiri vya kutosha kumiliki farasi wawili, mwenye hekima ya kutosha kuwa na urafiki wa karibu na vyama vyote viwili vya kisiasa vya wakati huo—na wa kilimwengu kiasi cha kuacha imani yake ya ujana, kama ilivyokuwa, na kugeukia imani zilizokataa mafunuo ya Mungu katika Biblia. Alilelewa katika nyumba ya Wabaptisti, William akiwa mvulana alikuwa  mwenye wasiwasi sana kwa muda, kuhusu nafsi yake. Alijaribu kupata amani kwa kuwatii sana wazazi wake na kwa kutoa sadaka ya mali alizothamini, lakini hakupata amani. Aliendelea kuamini Biblia, lakini alihangaika kwa sababu alihisi haikumpa msaada na aliona kana kwamba ilijipinga. Lakini baada ya kufunga ndoa yake, siku hizo ambazo Marekani ilikuwa changa, Miller alisoma vitabu ambavyo Thomas Jefferson, Benjamin Franklin, na Mababa Waanzilishi wengine wa taifa la Marekani, walikuwa wamesoma.

Haya yalikuwa maandishi ya watu kama David Hume, Voltaire, na Thomas Paine. Watu wengine wenye fikra za kina huko Poultney walisoma vitabu hivyohivyo, na punde si punde akakubali imani ya Udeisti, falsafa yao ilikuwa ya kuvutia lakini isiyokidhi kujibu hoja kuhusu ulimwengu na uumbaji wake. Kulingana na Dini hii ya Udeisti, Mungu aliuumba ulimwengu na kuuweka ufanye kazi chini ya sheria zisizoweza kubadilika za athari na matokeo. Ili kupatana na sheria hizi, wanadamu wanapaswa kuishi maisha safi, yenye fadhili, na ya uaminifu; lakini hawaamini

sala/maombi, Mwokozi, au maisha baada ya kifo bali huona haya kama ni ushirikina wa kijinga/kitoto. Miujiza, msamaha, na ufufuo wao waliona kuwa vingehitaji Mungu atende kinyume na sheria Zake za asili, na hilo lilikuwa jambo lisilo katika mawazo yao. Mungu alikuwa amemaliza kuiumba dunia kama saa, na kuiacha ijiendeshe yenyewe.

Sio Ukristo bali Umarekani wenye heshima, sheria-na-utaratibu ndiyo vingeweza kuleta ubora wa mtu, Miller alihitimisha; na nyumba yake mpya, pakawa mahali pa kawaida, pa kukutania wazalendo na wenzi wa ndoa wasio na dini. Huko Hampton, mama yake Miller alisikia kilichokuwa kikiendelea huko Poultney na alikuwa na wasiwasi sana. Alimsihi shemeji yake na baba yake mzee, wote wawili wakiwa makasisi wa Kibaptisti, wamtembelee William mara kwa mara, naye akaahidi kwamba sala zake zingeenda pamoja nao. William alimkaribisha kwa uchangamfu Mjomba Elihu na Babu Phelps, lakini baada ya kuondoka alifuatiliza jinsi walivyokuwa wakiongea kama kimchezo-mchezo au kwa upotovu na kufurahia sana na marafiki zake masimulizi hayo.

Akiwa amesadiki kwamba kupenda nchi yake, badala ya kumpenda Kristo ndilo tumaini kuu zaidi la wanadamu, Miller alijitoa kutumikia nchi yake, katika Vita vya 1812. Wengine arobaini na saba wakajitoa pia, kwa sharti kwamba lazima watumike moja kwa moja chini ya amri ya William Miller! Vita vya 1812, vita vya pili vya kijeshi vya Marekani kwa ajili ya uhuru kutoka kwa Uingereza, vilikuwa ni jambo lisilo na mashiko, na lisilo na mantiki wakati mwingi. Mapigano ya Plattsburg, yaliyopiganwa kwenye ufuo wa Ziwa Champlain, ambapo palikuwa karibu kutoka nyumbani kwa Miller, yalikuwa ya kipekee. Asubuhi ya Septemba 11, 1814, Waingereza walijivunia jeshi la nchi kavu la askari 15,000 wa kawaida na jeshi dogo la majini lililo na vifaa vya kutosha ziwani. Wamarekani walikuwa 5500 tu, na hivyo walikuwa na uhakika wa kushindwa.

Matokeo yalikuwa ni mshangao. "Bwana: Imekwisha, imekamilika," afisa mmoja Mmarekani mwenye ari akaripoti saa nane na dakika ishirini alasiri hiyo. "Meli za Waingereza zimepiga bendera ya Marekani. Uchinjaji mkubwa umetokea pande zote mbili - mambo yako wazi, ambapo ninaandika sasa .... tukio lilikuwa la ajabu kutazama, lilikuwa la heshima, lilikuwa nzuri. Asubuhi ya leo, saa kumi, Waingereza walitufungulia moto mzito sana wa makombora na wa kuangamiza, majini na ardhini. Roketi zao ziliruka kama mitupo ya mawe .... Hakika hujapata kushuhudia vita .... Lazima ufikirie kile sisi tunachohisi, kwa maana siwezi kuelezea vyema hali hiyo."

1. Afisa huyo alielezea kwa fahari kushiriki kwake. "Nimeridhika kwamba mimi naweza kupigana. Najua mimi si mwoga.... Watu wangu watatu wamejeruhiwa na gamba la bomu ambalo lilipasuka ndani ya umbali wa futi

mbili kutoka kwangu." "Huzza! Huzza!" Alisema katika msisimko wake wa kuridhishwa; na kisha, wafungwa ishirini au thelathini hivi walipoingizwa kwenye ngome ya jeshi, alitia sahihi jina lake: "Wako milele, William Miller." Vita viliisha mwaka wa 1815. Kapteni William Miller alikuwa ameonyesha uwezo wake wa kuongoza miaka mingi kabla ya kuanzisha vuguvugu la kidini bila yeye kupenda. Lakini aliporudi nyumbani kukamua ng'ombe na kulima na kupanda na kuvuna, akili yake ilichunguza bila kutulia dini ya wazalendo. Kwa kanuni ya sababu na matokeo, alitoa hoja, kwamba ushindi wa Plattsburg ulipaswa kwenda kwa Waingereza. Wanajeshi wao walikuwa mashujaa/maveterani ambao walikuwa wamemshinda Napoleon, na waliwazidi Wamarekani kwa uwiano wa watatu kwa mmoja 3:1.

Mwanahistoria wa kisasa ameita Plattsburg "hatua madhubuti" ya vita, na kapteni mwandamizi wa Amerika, katika ripoti yake kwenye ofisi ya vita wakati huo, alimpa utukufu Mungu: "Mwenyezi Mungu ameridhika kutujalia ishara ya ushindi." Je, iliwezekana, labda, kwamba Mungu alikuwa amependezwa na Marekani? Na Je, lile ganda lililomlipukia miguuni mwake bila kumuumiza wala kuwaua marafiki zake, hivi ilikuwaje? Je, Yupo Mungu aliyejali? Alihama kutoka Poultney kurudi Low Hampton. Baba yake akiwa amefariki, alilipa mkopo wa nyumba ulioishikilia nyumba yao rehani. Haya yalikuwa makazi aliyoishi toka utotoni ili mama yake aweze kuishi mahali hapo bila deni; kisha akakaa kwenye ekari 200 jirani. Ili kuonesha tabia njema, Miller alihudhuria kanisa la Kibaptisti wakati wowote mjomba wake alipokuwa na mahubiri. Vinginevyo alikaa mbali na shuguli za kanisa. "Tulikukosa kwenye ibada Jumapili iliyopita," mama yake alisema kwa upole. "Siwezi kuhudhuria huko wakati Mjomba hayupo, mama." "Kwa nini mwanangu?" "Ni jinsi mashemasi wanavyosoma mahubiri." "Wanajitahidi kwa kadiri wawezavyo, nina uhakika." "Mama, Wakati mjomba yuko mbali, kwanini wasiniruhusu niyasome hayo mahubiri?" Hivyo Miller bila kujua alijiwekea mtego, na wale ndugu wema aliowacheka kwa furaha walihakikisha kwamba amenaswa humo.

Mahubiri waliyompatia yalimfanya kusoma (Kutoka kwa Maongezi ya Utendaji Hai ya ya Alexander Proudfit) yaliamsha akili yake. Mashaka yake juu ya dini ya Udeisti yaliongezeka. Septemba 11, 1816, ilifika, kumbukumbu ya pili ya ushindi huko Plattsburg. Disko la umma lilipangwa likitanguliwa na mahubiri, usiku mmoja kabla. Mwinjilisti mgeni aliwatuma watu nyumbani wakiwa wamebubujikwa na Uamsho ambao ulifanya lile disko au dansi kuondolewa. Jumapili iliyofuata ilikuwa zamu ya Miller kusoma tena, safari hii hubiri katika Proudfit lenye kichwa, "Wajibu wa Wazazi kwa Watoto Wao." Akiwa amezidiwa na hisia katikati ya somo, hakuweza kufika mwisho.

Akiwa amekata tamaa juu ya dhambi zake, Miller aliwaza jinsi ingekuwa vyema kujitupa mikononi mwa Mwokozi na kutumaini kabisa neema Yake. Alimhitaji

Mwokozi. Ulimwengu ulimhitaji Mwokozi pia. Lakini je, Nafsi hiyo ya ajabu ilikuwepo? Basi Akarudi kwenye Biblia; na katika kurasa zake akampata Mwokozi aliyemtafuta. “Nililazimika kukiri kwamba lazima Maandiko ni ufunuo kutoka kwa Mungu,” aliandika baadaye. "Basi Maandiko yakawa furaha yangu, na katika Yesu nilipata rafiki."

Mara moja alianza ibada ya familia kwa utaratibu kila siku. Lakini marafiki zake w wenye udunia moyoni, walimdhihaki sasa, kama ambavyo hapo awali alivyokuwa amewadhihaki Wakristo wengine mara nyingi. Walimtania wakisema, Je, "Unajuaje kwamba Biblia ni Neno la Mungu?.” "Vipi kuhusu utata wake?" "Ikiwa Biblia ni Neno la Mungu,” Miller alijibu kwa uthabiti, "basi kila kitu kilicho ndani kinaweza kueleweka, na sehemu zake zote kupatana kabisa. Nipe muda, nami nitafafanua utata wake unaoonekana au la nitaacha imani na kushikamana na Udeisti." Akiweka kando kila kitabu isipokuwa Biblia yenyewe na Concordance ya Cruden, alianza na aya 13 za kwanza za Mwanzo sura ya kwanza na hakuendelea haraka zaidi kuliko vile alivyoweza kushughulikia maswali/hoja zilizotokea. Akitumia marejeleo yaliyo pambizoni, na kuyalinganisha hivyo aliacha Biblia ijieleze/ijifafanue yenyewe.

Tofauti zake nyingi zilizoonekana kutoyeyuka zilififia moja baada ya nyingine. Zaidi ya yote, aligundua kwamba Yesu, Rafiki na Mwokozi wake mwenye upendo, alikuwa ameahidi kuja tena duniani! Aligundua zaidi kuwa ahadi nyingine nyingi za unabii zilikuwa zimetimizwa, kwa nini basi hii? Ndipo siku moja akakutana na Andiko ambalo lilipaswa kumtia alama katika maisha yake yote, Danieli 8:14: “Hata siku elfu mbili na mia tatu, ndipo Patakatifu patakapotakaswa.” Masomo yake yaliongezeka kwa kasi, wakati mwingine yakadumu mchana kutwa; wakati mwingine usiku kucha. Kwa usahihi, aliamua (akitumia Ezekieli 4:6 na Maandiko mengine) kwamba siku 2300 zilikuwa miaka 2300, na kwamba zilianza mwaka 457 KK. Kwa makosa alidhani kwamba “kusafishwa kwa Patakatifu” ulikuwa mwisho wa dunia na ujio wa pili wa Kristo.

Mnamo mwaka wa 1818, baada ya miaka miwili ya umakini usiopungua, alifikia hitimisho la kushangaza kwamba Kristo angerudi "karibia na mwaka 1843" (Miaka 2300 baada ya 457 KK), na kwamba "katika miaka ishirini na mitano ……. mambo yote. Ya hali yetu ya sasa itaisha." Hivi mwisho wa ulimwengu umo ndani ya miaka ishirini na mitano? Ikiwa ndivyo basi ulimwengu lazima uonywe. Sauti ilimchoma ndani ya nafsi yake, "Nenda ukauambie ulimwengu." Ndiyo agizo, lenye kipaumbele, kutoka kwa Bwana, lililosikika moyoni mwake!

Kwa miaka mitano Miller alipuuzia wito huo na kupembua msimamo wake kwa nguvu. Aliogopa, na kuandika baadaye, "kusije kukawa na uwezekano fulani wa mimi kuwa na makosa, na nikawapotosha wengine." Vipingamizi vingi vilitokea akilini mwake kuliko wapinzani wake wowote waliotokea baadaye. Wakati miaka ya utafiti

iliondoa shaka yote, hofu ya kuzungumza mbele ya watu iliigubika nafasi yake. "Nilimtaarifu Bwana sikuwa mzuri katika malumbano ya mhadhara/hoja na sikuwa na sifa zinazohitajika (debate)." Miller alitimiza vizuri majukumu yaliyokuwa yakiongezeka katika kanisa lake mahalia. Alizingatia zaidi kuongoka kwa wadhambi. Na alishiriki imani yake juu ya kuja kwa Kristo na marafiki na waandishi wa habari.

Lakini hakuna kitu ambacho kingeweza kuzima kiu na wito wake wa kuendelea wa kuhubiri. Kufikia tarehe 15 Agosti 1831, baada ya miaka kumi na tatu ya kuahirisha mambo, mzigo kwenye nafsi yake ulionekana kutoweza kubebeka tena kwani alitindikiwa na msukumo wa "Nenda ukauambie ulimwengu." "Nimekuweka kuwa mlinzi. Uambie ulimwengu!" Alitazama juu kutoka katika Biblia aliyokuwa akiisoma, akifadhaishwa sana na wito wa Mungu. Hivi huu ulikuwa ni wito wa Mungu?

Aliona ni lazima ajihakikishie bila shaka kuwa ni wito wa Mungu. Akapiga ngumi kwenye meza yake. Akasimama. Akapiga magoti na kuomba, “Hapana, Mungu. Hapana! Unajua kwamba mimi siwezi kuhubiri. Siwezi kuhubiri. "Lakini labda ni mapenzi Yako kwangu kwenda. "Ee Bwana, nitaingia agano Nawe. Ukipenda kufungua njia; Namaanisha, kama Wewe utaniletea mwaliko wa kuhubiri, basi, Ee Mungu, nitakwenda.” Akaketi kitini mwake kwa raha akiendelea kusema kuwa “nikipokea mwaliko, nitajua kwamba Mungu amenitembelea na uwepo Wake; lakini uwezekano wa jambo hili ni mdogo sana,” naye akatabasamu kwa kuridhia, “kwamba mtu yeyote atamwomba mkulima mwenye umri wa miaka hamsini kama mimi kweli, eti ahubiri juu ya ujio wa pili wa Bwana, hakika haiwezekani.”

Ndani ya dakika thelathini kukasisika hodi inayobishwa kwa nguvu mlangoni, jambo ambalo lilimchochea. "Nani anaweza kuwa na harara hivyo siku ya Jumamosi asubuhi?" kengele ya mlango ililia tena. “nitakwenda nione kuna nani” Habari za asubuhi mjomba, alisalimia kijana Irvin kwa uchangamfu "Mpwa Irving” alishangaa Miller "Hivi unaweza kuwa unafanya nini maili kumi na sita kutoka nyumbani mwako asubuhi hii na mapema?" Nimeondoka kabla ya kifungua kinywa asubuhi na nimekuja kukujulisha kuwa mhubiri wetu wa Kibaptisti aliyetakiwa kuhubiri huko Dresden, hawezi kuhubiri kwenye ibada kesho. Baba amenituma nilete ombi kwako. Anataka uje kuzungumza nasi kuhusu mambo ambayo umekuwa ukijifunza katika Biblia. Kuhusu kuja kwa Kristo mara ya pili. Unajua. "Je, utakuja?"

*Maelezo:*

*1. The story of William Miller and the great Second Advent awakening has been told and retold many times by the Advent Shield, by Miller himself, by former Millerite Adventists such as Sylvester Bliss, Isaac C. Wellcome, Joseph Bates, and James White; and by J. N. Loughborough, M. Ellsworth Olsen, Everett N. Dick. F. D. Nichol. LeRoy Edwin Froom, Arthur Whitefield Spalding, Whitney R. Cross. Jerome Clark, David Tallmadge Arthur, and others. Letters,*

*publications, and other primary source materials are preserved in the Orrin Roe Jenks Memorial Collection of Adventual Materials, Aurora College Library, Aurora, Illinois; in the Heritage Room, James White Library, Andrews University, Berrien Springs, Michigan; in the Ellen G. White Estate; in various other libraries; and (microform) in Vern Carner, ed., The Millerites and Early Adventists (Ann Arbor, Mich.: University Microfilms, forthcoming)*

*2. Samuel Eliot Morison, The Oxford History of the American People (New York: Oxford University Press, 1965), p. 398*

*3. In Sylvester Bliss, Memoirs of William Miller (Boston: Joshua V. Himes, 1853), p. 47*

*4. Bliss, Memoirs, pp. 6 ff, says that Miller was assigned to read a sermon called, "Importance of Parental Duties," from "Proudfoot's Practical Sermons," This seems to be a slip of memory for "The Duty of Parents to Their Children," in Alexander Proudfit, Practical Godliness in Thirteen Discourses (Salem, 1813)*

*5.The story of Miller's conversion and call is told by himself in his Apology and Defence (Boston: Joshua V. Himes, 1845)*

## SURA YA 2
## UAMSHO MKUU WA UJIO WA PILI

Miller aligeuka nyuma bila kusema neno, akakimbia nje kupitia mlango wa jikoni na kuanguka kwenye kichaka cha michongoma kilichosimama karibu, huku akishindana mweleka na Bwana kwa maombi. Alijikuta anajikasirikia mwenyewe, ana hasira na Mungu, na hofu nyingi sana. Kwa muda wa saa moja aliomba kuachiliwa kutoka kwa ahadi yake. "Ee Mungu wangu, tuma mtu mwingine, naomba!" Hata alipokuwa katika dini yake ya ukana Mungu alikuwa amelishika Neno Lake Bwana kwa uaminifu, Je Atakapokuwa Mkristo angeweza kufanya kidogo zaidi?

Baada ya machozi ya uchungu kumbubujika, hatimaye alijisalimisha kwa Mungu. Kisha, furaha ilijaa katika nafsi yake! Miaka kumi na tatu ya kusitasita na hatimaye kupata ushindi. Ni furaha iliyoje kujisalimisha! Utukufu uwe juu ya Jina Lake Bwana! Kwa namna isiyo ya kawaida, aliruka-ruka, akimsifu Mungu kwa sauti kubwa. Lucy Ann, binti yake mdogo, akitazama kwa wasiwasi, alikimbilia nyumbani. "Mama, Mama, njoo haraka!" Mara tu baada ya chakula cha mchana Miller alikuwa njiani pamoja na Irving kando ya Ziwa Champlain (ziwa ambalo aliishi ufukoni mwake, miaka kadhaa kabla ya kupigana kwenye Vita vya Plattsburg), kuelekea mahali alipoishi dada yake huko Dresden.

Ili kumfanya awe huru kuzungumza, mkutano ulifanyikia jikoni huku Miller akiwa ameketi mezani kwenye kiti kikubwa chenye mahali pa kuegesha mikono. Mwamko

mkuu wa Ujio wa Pili wa Bwana huko Amerika ulikuwa sasa umeanza![1] Ujuzi wake wa kina wa Biblia ulikuwa wenye kuvutia sana, maombi yake ya kutoka moyoni yalikuwa yenye kugusa mioyo sana kiasi kwamba watu katika Dresden walimshawishi ahubiri kila usiku kwa juma moja. Taarifa zilienea kutoka kijiji hadi kijiji. Mahudhurio yaliongezeka. Zaidi ya familia kumi na mbili ziliongoka na kujitoa kwa Kristo. Bila shaka walikuwa wametoka katika nyumba ya Guildford na kuingia kanisani. Na aliporudi nyumbani mwaliko ulimngoja kutoka kwa mchungaji ambaye alikuwa bado hajasikia kuhusu mfululizo wa masomo yake ya kwanza.

Agano la Miller na Bwana lilithibitishwa kwa jinsi ya kupindukia. Hakika, alikuwa ameitwa kwenye huduma, kama tu vile Petro, Yakobo, na Yohana walivyoitwa. Kwa uhakika sawa; kwa Yeye Bwana YuleYule. Tangu mwanzo Miller alipokea mialiko zaidi ya ile ambayo angeweza kuhudumu. Walokole, Wamethodisti, Wabaptisti, Wapresbiteri walishindana wao kwa wao ili kumvuta kutoka shambani mwake ili aende kwenye mimbari zao. Ili kusaidia kukidhi mahitaji hayo alichapisha kijitabu cha mahubiri yake kwa gharama zake mwenyewe. Hili liliongeza tu hamu ya hitaji la kupanua ufahamu wa watu kuhusu kazi yake.

Mchapaji mmoja alichapisha kitabu cha mahubiri yake kwa gharama yake. Mnamo 1833 Mbaptisti wa eneo hilo ambaye alimjua Miller vizuri alimsaidia kuwekewa mikono au kupata leseni ya kuhubiri kwa kumwekea sahini, Na baadaye, cheti cha kumpendekeza kama mhadhiri wa unabii kilitiwa sahihi na wachungaji kadhaa wa Kibaptisti na viongozi kadhaa katika madhehebu mengine.[2] Karibu kila mahali Miller alipohubiri, watu waliongoka. Mara nyingi kulikuwa na uamsho; wakati mwingine miji yote ilibadilishwa-iliongolewa. "Unacheka, Ndugu Hendryx?," alimwandikia rafiki yake mapema katika kazi yake hii mpya, "kufikiri Ndugu mzee Miller anahubiri! Lakini wewe cheka tu; ... ni sawa - ninastahili kuchekwa, kwani hakuna aliyejua kwamba ningeweza kuhubiri Ukweli!, Ila kuhubiri ndiyo bora na yote ambayo ningeweza kumwomba Bwana anipe."

Siku hizo kila kijiji kilikuwa na ukafiri wake; baadhi ya jamii ndogo ziliungana nao. Makafiri walikuwa kama wakana Mungu lakini wakiwa na mashaka na utata mkubwa zaidi. Huko, makafiri walimwona Miller kama mtu ambaye alikuwa ameuliza maswali yao, na ambaye alikuwa ameyajibu. Katika sehemu moja makafiri mia moja waliukubali ujumbe wake kwa wiki moja.[3] Karibu na mwisho wa maisha yake Miller alihesabu kwamba alikuwa amehubiri katika miji isiyopungua 500 kutoka Massachusetts hadi Michigan, kutoka Montreal hadi Maryland, katika mingi ya hiyo miji, alikuwa ameihubiria mara kadha wa kadha, na binafsi alikuwa amesaidia kujipatia wongofu wa zaidi ya roho 6000.[4]

Lakini tunaendelea na kisa chetu. Kwa miaka yake minane ya kwanza, Miller, ambaye aliweka kanuni ya kwenda tu pale ambapo Bwana "alifungua njia," alikuwa

na shughuli nyingi sana katika makanisa madogo katika miji midogo. Mnamo mwaka 1839, mwishoni mwa ibada huko Exeter, New Hampshire, alikutana na mtu ambaye alibadilisha maisha yake ya kazi. Joshua V. Himes[5] akiwa na umri wa miaka thelathini na nne alikuwa tayari anajulikana sana huko New England kama mpiganaji wa vita dhidi ya utumwa, vileo na vita. Huyu akitafuta kila njia kuifanya dunia kuwa mahali pazuri pa kuishi, aliguswa moyo sana aliposikiliza ujumbe wa Miller kuhusu siku 2300. Mara tu mkutano ulipoisha, Himes alisimama kwa kasi na kumwalika Miller arudie mahubiri katika kanisa lake la Chardon Street huko Boston.

Kwa hivyo mnamo Desemba 8, 1839, Miller aliwasilisha mfululizo wa mahubiri yake ya kwanza katika jiji hili kuu. Mahubiri yalivutia kiasi kwamba mikutano ilipangwa mara mbili kwa siku, hata hivyo mamia ilibidi warudishwe kwa kukosa nafasi. Himes aliguswa moyo. Daima alimwona Miller kama kamanda aliye na utayari katika kutafuta askari na kusudi kujitayarisha kwa ajili ya dunia iliyofanya upya kwa wengine na sababu ya kukomesha mambo yote maovu.[6] "Je, wewe unaamini kweli yale ambayo umekuwa ukituhubiria?" alimwuliza Miller usiku mmoja nyumbani kwake.

Kwa makusudi na kwa dhati Miller alijibu, “Naam, naamini hivyo, Ndugu Himes, la sivyo nisingekuwa naihubiri habari njema.” "Basi unafanya nini ili kuieneza duniani kote?" Miller alisimulia majaribio yake ya kufikia kila mji na kijiji kilichomtumia mwaliko. Himes alishangaa. Kila mji mdogo na kijiji? Je ni vipi kuhusu miji? Je, Baltimore, Rochester, Philadelphia, na New York--hakika, Je, watu milioni kumi na saba wa Marekani--wakae bila kuonywa? Na vipi kuhusu ulimwengu mwingine? Alizungumza kwa kishindo na kusema, "Ikiwa Kristo atakuja katika miaka michache kama unavyoamini, basi hakuna wakati wa kupoteza katika kutuma ujumbe kwa sauti za radi ndogondogo ili kuwaamsha kujiandaa!" "Naelewa, Ndugu Himes," Miller alijibu kwa uchovu, "lakini mkulima mzee kama mimi anaweza kufanya nini kweli? Sikuzoea kuzungumza mbele za watu. Ninasimama peke yangu." Akashusha pumzi.

"Wachungaji wengi, wanapenda kunifanya nihubiri makanisani mwao ili kuongeza idadi ya watu katika makutaniko yao, na hivyo ndivyo inaishia, na wengi wao bado. Nimekuwa nikitafuta msaada." Himes iliwaka moto. Mara (alisema baadaye) alijiweka mwenyewe, familia yake, sifa yake, na yote aliyokuwa nayo juu ya madhabahu ya Mungu ili kumsaidia Miller kufikia kikomo cha uwezo wake hadi mwisho. Mara moja akawa meneja wa Miller yaani msaada katika kuboresha huduma yake, wakala wa utangazaji, na mtaalamu aliyewekwa wakfu kuhusiana na huduma ya ukuzaji. "Je, ukipata mwaliko utaingia mijini?" "Hakika nitaweza kuingia, Mungu akinisaidia." "Basi, Baba Miller, jiandae kwa ajili ya kampeni. Milango itafunguliwa katika kila mji katika muungano wa nchi hii, na onyo la Marejeo ya Yesu litaenezwa hata miisho ya dunia." (Jina “Baba” lilitumiwa siku hizo kama ishara ya upendo na heshima kwa wanaume wazee.) Himes alitimiza ahadi yake na unabii wake.

Punde si punde, Miller alikuwa akitembea katika majiji muhimu zaidi ya nchi, na jina lake likawa maarufu katika taifa zima. Njia moja ambayo Himes alimfanya Miller kuingia katika miji mikubwa zaidi ilikuwa ni kwa kuwashawishi wachungaji wa madhehebu yake mwenyewe, katika jumuiya za kikristo, kumfungulia mimbari zao. Mmoja wa wachungaji hawa alikuwa Lorenzo Dow Fleming wa Portland, Maine. Katika Fleming's Casco Street Church, ujumbe wa Miller uliwafikia familia ya Robert Harmon; na hivyo binti yao, Ellen, ambaye alikuwa mwanzilishi wa baadaye wa Kanisa la Waadventista Wasabato, alikabidhi maisha yake kwa tumaini la marejeo ya Yesu mara ya pili. Himes alitoa michango mingi yenye nguvu. Labda mchango wake mkubwa zaidi, ulikuja kupitia machapisho.

Mnamo Februari 1840, bila fedha au orodha ya usajili wa machapisho, alizindua jarida la kwanza la Waadventista, Ishara za Nyakati (Signs of the Times). Gazeti hili liliongoza kwa umashuhuri miongoni mwa Waadventista. Kwa kitambo Himes aliyahariri magazeti haya ya Ishara za Nyakati, mwenyewe. Vuguvugu hilo lilipoenea, aliwahamasisha wengine kubaki ofisini kushughulikia gazeti, huku yeye mwenyewe akiendelea kuanzisha majarida mengine katika miji mingine au kuwahimiza watu wenye vipaji kuchapisha machapisho yao wenyewe. Ndani ya miaka minne ujumbe wa marejeo ulitangazwa katika miji mbalimbali na Kilio cha Usiku wa manane kikatolewa, na Habari Njema, Ishara za Nyakati za kurejea kwa Yesu mara ya pili, Baragumu ya Yubile, Kengele ya Filadelfia, Sauti ya Eliya, Kilio cha Usiku wa manane Kusini, Kilio cha Usiku wa manane Magharibi, Lia Usiku wa manane wa Kweli, na mengine kadhaa—mengi yao yameandikwa kwa uwazi, yakiwa yameharirwa vizuri, na kuchapishwa vyema kwenye karatasi nzuri.

Kulikuwa na vitabu vyenye mfululizo wa zaidi ya arobaini pia vinavyojulikana kama "Maktaba ya Ujio wa Yesu mara ya pili." Kabla ya kukatishwa tamaa kukubwa kwa Oktoba 22, 1844 (Great Disappointment), nakala milioni nane za machapisho ya Waadventista zilienezwa kwa watu na kueneza Neno la Mungu. Usajili wa magazeti kwa kawaida ulishughulikiwa siku hizo na wasimamizi wa posta. Mkuu wa posta huko Canton, Iowa, aliripoti kwamba wakati machapisho ya wafuasi wa Miller yalipowadia mahali, kulikuwa na "kukimbilia nakala hizo ili kufanya manunuzi" ya nakala zozote za ziada. Unaweza kunitumia nakala zaidi? Watu walisihi. "Wewe hujui thamani" ambayo machapisho haya yanayo.[7]

Ujumbe wa Miller hauhusu "mzozo mwingi au malumbano kuhusiana na tarehe iliyobainishwa." Bali ulikuwa ni ujumbe wa malaika wa kwanza: "Injili ya milele" na "saa ya hukumu Yake Bwana imekuja." (Ufunuo 14:6, 7) Roho ya uinjilisti ndiyo ilitaka kuwasaidia watu kujitayarisha kukutana na Bwana. Kupitia uinjilisti, makanisa ya Methodisti yakaonekana kupata washiriki wapya 40,000 kufikia mwaka wa 1844, na Wabaptisti 45,000.[8] Ratiba moja ya wiki sita, ya mhudumu mmoja kijana mfuasi wa Miller, iliongeza idadi ya watu ndani ya  makanisa ya mtaa kwa

maelfu![9] Huko Portland, Maine, wakati Miller alipokuwa huko, kijana mlegevu alikimbilia na kupiga kelele kwa marafiki zake, "Wavulana wenzake, akisema, kuna mhubiri kwenye Mtaa wa Casco ambaye anasema ulimwengu unakaribia mwisho. Je! Mwaweza kuacha kucheza kamari na msikie anachosema?" Huko Portsmouth, New Hampshire, uamsho uliendelea kwa wiki baada ya Miller kuondoka. Kengele za kanisa zililia kila siku kwa maombi kana kwamba kila siku ilikuwa ni Jumapili. Maduka ya Grog yakawa vyumba vya mikutano.

Mamia kadhaa waliongoka, na maelfu wakakusanyika kwenye ukingo wa maji ili kuwaona watu wakibatizwa. Wachungaji wa madhehebu mengi walimiminika kusaidia kazi hiyo. Joshua V. Himes alikuwa mmoja tu wa hawa. Viongozi wengine mashuhuri waliojiunga na Miller ni pamoja na Josiah Litch, Mmethodisti ambaye tayari alijulikana sana kama mkalimani wa unabii na ambaye alikubali imani ya Miller baada tu ya kuwa na uhakika kwamba haikubaliani na Umethodisti. Alihubiri sana, kisha akachapisha kitabu cha kurasa 200 kuhusu mihadhara ya Miller, na, miongoni mwa mambo mengine, alisaidia kumshawishi Charles Fitch ajiunge pia.

Fitch alikuwa mchungaji wa kanisa la Congregationalist huko Boston, ambaye wakati fulani alikuwa msaidizi mkuu wa mwinjilisti maarufu Charles G. Finney. Kwa usaidizi wa Apollos Hale, Mmethodisti aliyejulikana sana, alitayarisha “Chati ya 1843,” ambayo huenda wahadhiri wote walitumia, ikionyesha unabii mwingi wa Biblia uliotokea mwaka wa 1843. Pia alifanya ubunifu wa chati ya picha ya Danieli 2 iliyotenganisha ufalme baada ya ufalme.. Kando na viongozi hawa mashuhuri kulikuwa na wengine waliofika zaidi ya 30. Tunamfikiria James White, kama Himes, mhudumu wa Christian Connection; na Joseph Bates, pia mshiriki wa dhehebu hilo, mlei ambaye alichukuliwa kuwa mhudumu. Lakini hakuna anayejua ni wasaidizi wangapi! Makadirio ya wakati ule yalianzia 700 hadi 2000. Kati ya Wachungaji 174 waliojulikana, karibu nusu walikuwa Wamethodisti, wanne walikuwa Wabaptisti, na waliosalia nandi walikuwa Washiriki wa Congregational, Wakristo, Wapresbiteri, Waepiskopi, Walutheri, Wanamageuzi wa Uholanzi, Waquaker, na wengine kadhaa.

Haiwezi kusisitizwa kuwa Miller hakuwa pekee anayeongoza! Kundi kubwa la watu wenye uwezo, wenye kufikiri kutoka katika madhehebu makubwa walimuunga mkono, si wachache ambao walikuwa wamebarikiwa kwa mafunzo mengi ya kitaaluma. Ilikuwa ni ushuhuda wa kuvutia kwa "mkulima mzee." Imani ya Millerism/Wamiller ilikuwa ni mapinduzi yaliyomhusu Kristo ambayo yalikubaliwa kwa uchangamfu na wengi, washiriki na viongozi, katika makanisa yaliyoheshimika ya wakati huo, na maelfu ya makafiri, na nafsi zisizojali katika ulimwengu usio na utulivu wa nje. Wafuasi waliendelea kuongezeka zaidi hadi Miller, Himes, na viongozi wengine walikuwa wakizunguka karibu bila kukoma kati ya New York na Boston, Albany na Utica, Rochester na Buffalo, kaskazini hadi Montreal, magharibi hadi Cincinnati, Saint Louis, na Louisville, na chini. kusini hadi Washington na

Baltimore. Robert Winters alipeleka neno hilo Uingereza. Barua zilipelekwa katika kila ofisi ya posta nchini Marekani na kila kituo cha misheni kinachojulikana kote ulimwenguni.[10]

Huko Washington, DC, hata tangazo la uongo lilileta watu 5000. Huko Philadelphia vyombo vya habari vya kilimwengu viliripoti umati "mkubwa" wa Waadventista wapatao 15,000. Kuwepo katika vuguvugu la Wafuasi wa Miller la viongozi wengi kutoka makanisa mengi tofauti kulifanya mikutano ya wafanyakazi kuwa muhimu. Kuanzia mwanzoni mwa 1840, zaidi ya "mikutano mikuu" ishirini[11] iliitishwa katika sehemu mbalimbali, wakati mwingine kwa kiwango cha mikutano miwili hadi mitatu kwa mwezi. Mkutano mkuu wa kwanza ulifanywa na Joshua V. Himes's Chardon Street Chapel mwezi Oktoba. Homa ya matumbo ilimpata Miller na mkutano ulifanyika kwa mafanikio bila yeye, ndivyo ule wa pili, wa tatu, na wa nne pia ulivyofanyika. (Mkutano wa tano ulipangwa kufanyika Low Hampton ili Miller aweze kuhudhuria).

Akiwa amesikitika kwa kulazimika kukaa mbali na mikutano kwa ajili ya ugonjwa, Miller alianza kuelewa kwamba harakati aliyokuwa ameanzisha kwa mwito wa Mungu ilikuwa ikikua zaidi yake, yaani kwa uwezo wa Mungu Kwamba awepo au asiwepo, Kazi itasonga mbele. Mikutano mikuu ilifanyika kwa njia ya mikutano mikubwa ya hadhara. Mahudhurio katika mikutano hii na mingineyo ya Wafuasi wa Miller yalipoongezeka, mkutano uliofanyika Boston chini ya uongozi wa Joseph Bates mnamo Mei 1842 ulipiga kura kujaribu kufanya mikutano ya kambi na kupanga mikutano mitatu wakati wa msimu wa joto (Summer). Mkutano wa kambi ulioanza Juni 28 huko East Kingston, New Hampshire, ulimkuta Joshua V. Himes akisimamia kazi kwenye uwanja, wakiwemo watu elfu saba hadi elfu kumi kwenye uwanja huo.

Gazeti la Boston Daily Mail liliangazia tukio hilo na kupongeza umati kwa mikakati, hulka, mavazi, uungwana, mpangilio, na mtindo wao wa maisha (decorum). Hata mshairi maarufu aitwaye John Greenleaf Whittier alishuka huko kwa saa moja au mbili kuangalia mambo. Miaka mingi baadaye bado alikuwa anakumbuka wahubiri wenye ufasaha waliokita kwenye lugha ishara ya Biblia, michoro ya kambi ya sanamu ya Nebukadreza na wanyama wa Ufunuo—na matao yenye mwanga hafifu kwenye misitu, duara jeupe la hema, moshi wa mioto ya kambi ulioikuwa ukipanda kama uvumba na nyuso zilizoinuliwa juu kwa shauku/ari.

Haikuchukua muda, na mikutano ya kambi ikaanza kufanywa katika sehemu nyingi, mara nyingi ikiitishwa na halmashauri za watu waliojitolea sehemu mahalia. Wanaume, wanawake, na watoto walimiminika kutoka kila upande, boti za injini ya mvuke zikisongamana, magari ya reli yaliyokuwa yakifurika kwa watu, na treni zenye msongamano; watembea miguu waliingia ndani kutoka kila upande wa barabara, huku watu wote, wale wacha Mungu na pia wadadisi, wakielekea kwenye

mikutano muhimu kwenye uwanja wa kambi wa Marejeo ya Bwana kwa mara ya Pili. Ilionekana kwamba karibu kila muumini alikuwa na Biblia mkononi mwake.[12]

Mafanikio makubwa ya mikutano ya kambi yalisababisha Wafuasi wa Miller, au Millerites kuchangia fedha kwa ajili ya hema kubwa linalotosha watu, kwani umati ulikuwa mkubwa katika jumuiya ambapo mikutano ya kambi haikuwezekana na kumbi zilikuwa ndogo sana. Waliagiza hema kubwa zaidi lililotengenezwa Marekani, hadi wakati huo na kulipa jina "hema kubwa." Palihitajika timu ya kudumu ya watu wanne kuisimamisha kila ilipohitajika kufanya hivi. Nguzo yake ya katikati ilikuwa futi 55, kipenyo chake futi 120, na kulikuwa na nafasi ndani yake, ya kutosha kukaa watu 4000.[13]

Hema kubwa likawa agizo, nalo likasimikwa, na kutumika ndani ya siku thelathini. Hawakuwa na wakati wa kupoteza ikiwa Kristo alikuwa anakuja "mnamo mwaka wa 1843." Magazeti yalishangazwa na kasi ambayo hema hilo lilipanguliwa, na kufungwa kama mzigo ili kusafirishwa kwa gari ya farasi, boti ya mvuke, au gari-moshi, na kupelekwa katika mji mwingine. Liliposimikwa chini tena, watu walipiga makelele kuwa watu hawawezi kujaa humo, kwamba ni kubwa sana. Mikutano ilipoanza, walishangaa kuona kuna msongamano. Mamlaka za reli Zilipanga treni maalum ili kuchukua umati wa watu.

Huko Rochester, dhoruba za upepo ghafla ulikata minyororo kumi na tano ya hema ila likaanguka kwa taratibu—kwenye vichwa vya watu. Wananchi kwa kushukuru walichangisha fedha kwa ajili ya kuikarabati, kwa sharti kwamba mfululizo huo wa mikutano uendelee. Wakati huohuo, Jumapili Himes alihubiri katika soko la jiji kwa vikundi vitatu kwa saa nane. Waadventista hawa, yaani watu waliotarajia Yesu kurudi, hawakuhudhuria tu makanisa yao wenyewe siku ya Jumapili lakini pia walikutana mara kwa mara katika mikutano ya madhehebu mbalimbali na mikutano ya maombi wakati wa juma. Punde wakajenga "mahema" imara lakini ya gharama ndogo na ya kukaa maelfu huko Boston, Akron, Cincinnati, na Cleveland. Wakati wenye dhihaka waliposema kwamba majengo yalikana imani yao katika kurudi kwa Kristo upesi, waumini walimnukuu Yesu: endeleni kufanya shuguli au biashara hadi nitakaporudi “occupy till I come."

Mkutano mkuu wa Mei 1842 ulikuwa umepiga kambi mikutano mitatu ya kambi ilikuwa imefanywa mwaka huo. Mikutano thelathini na moja ilifanyika. Mnamo 1843, mikutano arobaini. Mwaka 1844, mikutano hamsini na nne, na kisha jumla mikutano 125 ilifanyika. Jumla ya mahudhurio, yalikuwa angalau nusu milioni, mbali na maelfu na maelfu waliohudhuria mikusanyiko mingine katika "kambi lile kubwa” na katika makanisa, makazi ya watu, na kumbi za kukodiwa. Mungu alitaka ujumbe wa malaika wa kwanza uhubiriwe kwa “kila kabila, na lugha, na jamaa.” Alimwita Miller

“kuuambia ulimwengu.” Yeye hakutaka ujumbe huu, ufungiwe katika eneo fulani tu au kwa mtu fulani tu!

*Maelezo:*

*1. See Arthur Whitefield Spalding, Pioneer Stories of the Advent Message, rev. ed. (Nashville, Tenn.: Southern Publishing Association, 1942), pp. 40-49. Spalding claims to base his details on a conversation with an eyewitness*

*2. Miller, Apology, pp. 19, 20*

*3. See James White, Sketches of the Christian Life and Public Labors of William Miller (Battle Creek, Mich.: Steam Press of the Seventh-day Adventist Publishing Association, 1875), pp. 111, 112*

*4. Miller, Apology, pp. 22, 23*

*5. The best biography now of Himes is David Tallmadge Arthur, "Joshua V. Himes and the Cause of Adventism, 1839-1845" (master's thesis, University of Chicago, 1961).*

*6. The characterizations are from Arthur, "Joshua V. Himes," pp. 168, 51*

*7. Midnight Cry, May 25, 1843. p. 74*

*8. Everett N. Dick arrived at these figures by comparing the growth of the Methodists and Baptists in the early 1840s with their normal growth curve and with the decline which they suffered immediately after 1844. He concluded cautiously that those who fell away had been influenced by Millerism. The evidence is striking. See Dick, "William Miller and the Advent Crisis, 1831-1844" (doctoral dissertation, University of Wisconsin, 1930), pp. 263, 264.*

*9. The young minister was James White. See his Life Incidents, in Connection With the Great Advent Movement, as Illustrated by the Three Angels of Revelation XIV (Battle Creek, Mich.) Steam Press of the Seventh-day Adventist Publishing Association, 1868), p. 96*

*10. Midnight Cry, August 24,1843, p. 1*

*11. See Arthur, "Joshua V. Himes," pp. 61, 62. Arthur disagrees with the 16 counted by LeRoy Edwin Froom and thinks he can find between 23 and 26. See Froom, Prophetic Faith of Our Fathers, 4 vols. (Washington, D.C.: Review and Herald Publishing Association, 1946-1954), vol. 4, p. 555*

*12. See Joseph Bates, Second Advent Way Marks and High Heaps (New Bedford, Mass.: Press of Benjamin Lindsey, 1847), pp. 11, 12 38*

*13. It may be that the Adventists didn't have to pay for the great tent. In 1892 Loughborough wrote that E. C. Williams of Rochester, New York, told him in the 1850s that he presented the tent to Miller as a gift. But there are difficulties in the details of the account. See J. N. Loughborough, Rise and Progress of the Seventh-day Adventists (Battle Creek, Mich.: General Conference Association of Seventhday Adventists, 1892), p. 41*

## SURA YA 3
## WAKATI WA KUKAWIA

Sio kila mtu, aliishi bila kumshuku mzee Miller, siyo kila mtu alikubaliana na William Miller au alimchukulia mzee huyu kwa uzito. Wengine walisema alikuwa tu akitafuta pesa. Mbunge wa nchi aliwasilisha muswada bungeni wa kuahirisha mwisho wa dunia hadi 1860. Maigizo ya kuchekesha yalitoa viti vilivyohifadhiwa kwenye parachuti ya kutorokea watu kwa Dola 200. Tangazo lilitangaza, "Wakati Umefika" - yaani, wakati wa kuchukua dawa mashuhuri ya mitishamba ya kikohozi ambayo watu huiamini "Balsam ya Winstar ya Wild Cherry." Katuni ilionyesha "Kupaa kwa hema la fahari la ibada linaloitwa “Miller Tabernacle" huku Shetani akimshika mhubiri Himes kwa nguvu na kupiga kelele, "Joshua V., lazima wewe ubaki nami!"

Matumaini yalitawala Amerika wakati Miller alipoanza kuhubiri, na, kwa akili nyingi, mazungumzo juu ya mwisho wa ulimwengu unaokaribia yalikuja kama wazo jipya. Wafuasi wa demokrasia ya Jacksoni walionekana kutangaza ukamilifu wa mwisho wa jamii ya wanadamu hapa duniani, na hivyo ndivyo jumuiya za kimishenari, jumuiya za Biblia, na Shule za Jumapili zilivyoongezeka kwa idadi. Uvumbuzi wa sayansi na teknolojia wa ajabu wa hivi karibuni, uliongeza ushahidi kwamba ulimwengu ulisimama kwenye kizingiti cha enzi ya dhahabu.

Akisafiri kwa boti chini ya Mto Hudson akielekea kwenye miadi katika kipindi cha kupukutisha majani cha 1833, William Miller alisikia kikundi cha wanaume wakistaajabia maendeleo ya miaka ya hivi karibuni. Taa zinazotumia gesi! Mashine za kusokota pamba na kutengeneza majora! Vyakula vya makopo vinavyosindikwa! Upigaji picha! Mashine ya McCormick ya kuvuna nafaka! Magari moshi! Hata zile mashua za mvuke walizokuwa wakisafiria, za kurukaruka, na yenye kumwaga moshi ndiyo zilikuwa zinavumbuliwa. "Mambo hayawezi kuendelea hivi," mmoja wa watu hao alisema kwa mshangao, "Vinginevyo katika miaka thelathini mwanadamu atakuwa zaidi ya mwanadamu (ataendelea na kuwa kitu kingine)." Miller alisogea karibu. ““Mabwana,” akasema, “uvumbuzi huu unanikumbusha Danieli 12:4. Katika siku za mwisho, ‘Wengi wataenda huko na huko, na maarifa yataongezeka. “Alipowaona wanapendezwa, aliwapa uchunguzi wa historia kufuatana na nuru ya unabii wa Danieli 11 na 12.

Kisha ghafla tu, akajikuta akisema, "Waungwana, sikuwa nimedhamiria kuingilia mazungumzo yenu kwa muda mrefu hivi." Lakini alipoamua kwenda upande mwingine wa mashua, kikundi kizima kilimfuata na kuomba wapate mafundisho zaidi ya unabii. Hapo ndipo alipowafundisha kitabu chote cha Danieli - kichwa cha dhahabu, pembe ndogo, siku 2300, karibu kila kitu kutoka falme nne hadi hukumu na ujio wa pili. "Je, umeshayachapisha haya mahubiri?" wakauliza; na alipotoa nakala zilizochapishwa za mahubiri yake, walinyakua kila nakala aliyokuwa nayo.[1]

Japokuwa wasafiri-wenza wa Miller, hatimaye walikubali mafundisho yake. Wachungaji wengi wa wakati huo na wanatheolojia hawakuyakubali. Badala yake,

wakiongozwa na "postmilenia au baada ya miaka 1000" ya ajabu iliyoenezwa na Daniel Whitby, walijielekeza kwenye uvumbuzi na maendeleo ya kimishenari yaliyowazunguka na kusema, "Tazama, ulimwengu unazidi kuwa bora zaidi. Ujio wa pili wa Kristo hata sasa unafanyika, kiroho, ndani ya mioyo ya watu na tuko kwenye mwanzo wa miaka elfu ya amani! (Enzi za Postmillenia zinasema Kristo atakuja wakati kuna amani na maendeleo, na wakati imani ya Mwenyezi Mungu itakuwa imesheheni kwa wengi). Ingawa nadharia hii inaweza kuonekana kuwa ya kushangaza, wachungaji walioiamini, hawakuwa wachache ila ni wachache sana walioiamini miaka 2300 ya Danieli 8:14. Baadhi yao walisema kwamba enzi mpya kweli ingeanza katika miaka ya 1840.

Mchungaji George Bush, profesa wa fasihi ya Kiebrania na Mashariki katika Chuo Kikuu cha New York City, alikuwa mfano wa wengi. Akikubali kwamba uelewa wa Miller wa siku 2300 ulikuwa sahihi, hata hivyo alisisitiza kwamba "tukio kuu mbele ya ulimwengu sio moto wake wa kimwili, lakini kuzaliwa upya kwake kimaadili." [2] Miller alijibu kwa kunukuu Maandiko: “Katika siku za mwisho,” alisema “watu waovu ... wataendelea kuwa waovu zaidi, wakidanganya na kudanganyika” (2Timotheo 3:1, 13 ); lakini si kila mhudumu alitaka kusikia Maandiko kama hayo. Kadiri muda ulivyosonga mbele, hawa walianza kumpinga Miller kwa nguvu kwenye mimbari zao. Wanaume wengine walipinga kwa njia zingine. Phrenolojia ilikuwa maarufu katika miaka ya 1840 (Phrenolojia ni nadharia ya sayansi ya uongo, ambayo inajaribu kuoanisha haiba na hulka ya mtu na matuta na mitaro ya kwenye fuvu la kichwa, haya yalikuwa mawazo maarufu katika karne ya 19).

Elimu hiyo ilidai kwamba tabia ya mtu inaweza kusomwa kutokana na umbo la kichwa chake, na lilikuwa jambo la kawaida sana siku hizo, mtu kwenda kuchunguzwa kichwa chake. Mnamo Machi 1842, wakati Miller alipokuwa akihubiri huko Medford, Massachusetts, karibu na Boston, Mkristo ambaye alikuwa amekubali imani ya Waadventista, yaani ujio wa Yesu wa upesi, alimshawishi Miller kumtembelea mtaalamu wa frenolojia, aliyekuwa rafiki yake, akitumaini, bila shaka, atamgeuza mtaalam huyu wa nguvu za giza, ambaye hakuthamini wanamarejeo, naye hakuwa amekutana na Miller na wala hakumtambua.

Miller alipofika kwa huyu mtaalamu wa Frenelojia, alianza kuchunguzwa kichwa chake, alikishika kichwa alisema "Ah, hapa kuna kichwa kilicho na balansi/usawaziko mzuri," alisema huku akipitisha vidole vyake vyenye uzoefu juu ya fuvu la Miller. "Nitakuambia, bwana, huyu Bw. Miller hakika litakuwa jambo gumu kumwongoa mtu kama wewe!" Aliendelea na kuangalia katika uso wa Miller, akisema, "Una akili nyingi sana na uvumilivu mwingi kiasi kwamba huwezi kuchukuliana au kuvumilia upuuzi wa Bwana Miller!"

Mtaalamu huyu aliendelea, akifanya mfululizo wa ulinganisho, huku akiongeza chumvi katika maelezo yake akilinganisha kati ya kichwa alichokuwa akikichunguza na kichwa cha Miller jinsi alivyodhania kilivyo. "Oh, ningependa kuchunguza kichwa cha Bwana Miller," alivuta pumzi akiwatazama wanaume walioketi kwenye safu ya viti kando ya ukuta wakimngojea atoe huduma hiyo kwao pia. "Hakika ningekikandamiza kidogo!" Kisha akiweka mkono wake juu ya sikio lake shupavu," alisema kwa sauti na kwa dhihaka, "Nina uhakika tutakapopata nafasi ya kupima kichwa cha mzee William Miller atakuwa na tuta kubwa la unafiki na ushupavu kichwani mwake kama hii ngumi yangu!"

Mtaalamu wa frenolojia alipoitunisha ngumi yake mara mbili kama njia ya kielelezo, safu ya wanaume hawa walicheka naye kwa furaha, wakayapiga mapaja yao, huku wakitikisa vichwa na kugonga ngumi zao wenyewe kwa kumwiga daktari wa frenolojia. Mtaalamu wa frenolojia aliangua kicheko kuliko watu wote. Uchunguzi ulipokamilishwa, mtaalam wa frenolojia aliuliza kwa upole, "Bwana, naomba jina lako, tafadhali, ningependa kuliweka kwenye faili lako?" "Oh," alijibu Miller kwa huruma, "Jina langu halina maana yoyote. Wee acha Lipite tu." "Lakini bwana, kwa kweli ningependa kuambatanisha jina lako na kichwa kizuri sana kama chako. Isitoshe, ninalihitaji kwa kumbukumbu zangu." "Vizuri sana," mtahiniwa alikubali kwa kusita, "unaweza kuniita Miller, ukichagua." "Miller? Miller?"

Mtaalam alipata kigugumizi. "Lakini hebu naomba kuuliza, ni jina lako la kwanza?" "Wananiita William Miller." Yule mtaalamu wa frenolojia akauliza "Mzee ambaye anatoa mihadhara juu ya unabii?" "ndiye huyo haswa." Miller akajibu. Hapo ndipo mtaalam wa frenolojia alipotulia kwenye kiti chake, akitetemeka kwa mshangao na kufadhaika.[3] Lakini ikiwa baadhi ya watu walimpinga Miller na wengine kumdhihaki, wengine, ingawa hawakukubaliana naye, walitetea udhati/unyofu wake kwa nguvu. Na kulikuwa na watu wengi sana—wakulima, akina mama wa nyumbani, wafanyakazi wa viwandani, watu wenye elimu—ambao, ingawa hawakutaka kumwamini, moyoni mwao walikuwa na uzito fulani moyoni na tashwishwi kuhusu mafundisho yake.

Taarifa za mashahidi wa matukio ya ajabu zilienea kwenye magazeti. Mfano: Jupiter ilizungukwa na duara la nuru -halo), Farasi na mpandawake walionekana mwezini. Msalaba mweusi kwenye mwezi wa damu, nyimbo kusikika angani. Watu wanaotembea angani. Malaika watatu wakilia, "Ole, Ole, Ole." Matukio haya yote ya ajabu hakuna yaliyoripotiwa na wafuasi wa Miller. Kwa kuwa macho yao yalikazwa kwenye Maandiko, hivyo hawakuwa na nafsi ya kuyashuhudia hayo! Makafiri waliziripoti na kuzitangaza sana habari hizi kwenye vyombo vya habari. Mnamo 1833, miaka miwili baada ya Miller kuanza kuhubiri, nyota zilianguka kama vipande vya theluji. Kisha, wakati wa baridi kali mwishoni mwa Februari 1843, kulitokea bila kutangazwa katika anga ya kusini-magharibi kimondo (comet) chenye miali ya moto ambacho kilionekana mchana pakiwa kweupe. Wengine walisema “Mjumbe kutoka

anga za juu.” Wengine wakasema “Jicho la adhabu au jicho la uharibifu.” Hata wenye mashaka na dini walitetemeka.[4]

*Vidokezo:*

*1. Adapted from Bliss, Memoirs, p. 106*

*2. George Bush, Reasons for Rejecting Mr. Miller's Views on the Advent, with Mr., Miller's Reply (Boston: Joshua V. Himes, April 15, 1844), p. 11*

*3. Adapted from Midnight Cry, November 23, 1843, p. 2. Reprinted without adaptation in Francis D. Nichol, The Midnight Cry (Washington, D.C.: Review and Herald Publishing Association, 1944), pp. 98, 99*

*4. William Miller, Evidence From Scripture and History of the Second Coming of Christ, About the Year 1843; Exhibited in a Course of Lectures (Boston: Joshua V. Himes, 1842), pp. 174, 175*

# SURA YA 4
# KILIO CHA USIKU WA MANANE

Katika mkutano wa makambi usioweza kusahaulika huko Exeter, New Hampshire, mnamo Agosti 1844, kilio cha usiku wa manane hatimaye kilisikika.[1] Nahodha wa bahari aliyestaafu Joseph Bates, mtu ambaye alikuwa amewekeza mali yake katika kazi hiyo njema, alikuwa akiwahimiza Wafuasi wa Miller kwa nia iliyogawanyika, akiwaambia waendelee na safari na kuwatia moyo na hamasa kwa dokezo la siku zake za zamani za ubaharia.

Kusanyiko lilihangaika katika joto kali, bila raha, na bila kusadiki yale yaliyokuwa yanahubiriwa na Bates. Hapo ndipo mpanda farasi alipotokea, naye akashuka, na kuketi kwenye safu ya mwisho, kila mtu aligeuka na kumtazama. Wale waliokuwa karibu naye zaidi, walimshirikisha katika mazungumzo ya kiroho. Lakini Joseph Bates alikaa bila kuonyesha shauku yoyote. Mara Bibi John Couch alisimama dede kwa miguu yake. Huyu alikuwa dada yake Samuel Snow, mpanda farasi ambaye alikuwa amewasili tu. Alizungumza kwa uungwana na adabu lakini kwa uhakika.

"Ndugu Bates! Tumechelewa sana kutumia wakati wetu juu ya Ukweli huu ambao umekuwa kama mazoea tu kwetu. Muda uliobaki sasa ni mfupi. Bwana anao watumishi hapa ambao wana chakula kwetu, kwa wakati wake kwa ajili ya nyumba Yake. Waache hao basi ili wanene, na watu wasikie." Alipokuwa akiongea hivi, shahidi aliyejionea anaripoti, Roho wa Bwana alitembea juu ya kusanyiko kama upepo mwanana unaovuma juu ya ziwa lililokuwa na utulivu papo hapo. Vilio vya njaa vilisikika, “Amina, Dada; ndiyo, ndiyo,” sauti zikainuka pande zote. Hapa na pale wanaume na wanawake walitokwa na machozi ya papo hapo, wakitazamia jibu la sala zao. Bates aliiacha mimbari kwa ujasiri. "Ikiwa Ndugu Snow ana Ukweli kwa ajili yetu kutoka kwa Bwana, hebu na aje na kutoa ujumbe Wake."

Akiwa kwenye gari-moshi kwenda Exeter alikuwa amevutiwa kwamba maendeleo kama hayo yangetukia. Snow alikuwa tayari; na alikubaliwa kuzungumza wakati akili zikiwa mpya katika mkutano wa asubuhi. “Bwana wetu aliyebarikiwa ameahidi kwamba atakuja tena na kuwapokea watu Wake Kwake Mwenyewe,” Snow aliwakumbusha maelfu ya wasikilizaji wake waliokusanyika kwenye anga tulivu asubuhi iliyofuata.[2] “Kuhusu wakati wa kurudi Kwake, Yesu aliwaambia wanafunzi kwamba ‘siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbinguni, wala Mwana, ila Baba. (Marko 13:32)

Snow aliendelea kusema, “Watu wengi hufikiri kwamba fungu hili linathibitisha kwamba wanadamu hawatawahi kujua wakati, lakini pia huthibitisha kwamba

Mwana wa Mungu, hatajua kamwe wakati wa kuja Kwake, kwani tamko hili kuhusu Mwana ndilo ambalo limetamkwa kuhusu wanadamu na malaika! mara ya kwanza," Snow aliendelea kusema kuwa, "Yesu alikuja kwa wakati na Alikuwa na ujumbe kuhusu wakati. Alisema, 'Wakati umetimia.' (Marko 1:15 ) Ninawauliza ninyi, akina dada, ni wakati gani ulitimia?" Umati ukajibu, "Wakati wa unabii." "Majuma sitini na tisa kati ya yale majuma sabini ya Danieli." "Sawa, sawa,"

Snow akawatia moyo. Sote tunajua unabii wa Danieli 8 na 9 kuhusu siku ambazo ni miaka 2300 na kuhusu majuma sabini ya miaka ambayo 'ililiamriwa (au 'kukatiliwa mbali') kutoka kwa zile siku 2300. Na imekuwa kitu cha kawaida miongoni mwetu kubeba miaka hii miaka 2300 hadi kufikia 'karibu mwaka wa 1843.' "Lakini tumepuuza baadhi ya mambo! Naam ile amri ya kurudi na kujenga Yerusalemu upya. (Danieli 9:25). Sasa Ezra 7:8 inatuambia kwamba amri hiyo haikufika Yerusalemu hadi mwezi wa tano wa mwaka, ikiwa miaka ya Biblia ilianza na kuisha katika majira ya kuchipua, na ikiwa amri hiyo haikuanza kutumika/kuhusika hadi miezi mitano baada ya mwanzo wa mwaka, je, miaka 2300 haipaswi kuendelea mbele angalau miezi mitano zaidi ya mwanzo wa majira ya kuchipua?" "Amina." "Hiyo ni kweli."

"Kwa kweli lazima iwe hivyo," watu walijibu. "Kisha tulikosea kutarajia kurudi kwa Kristo katika msimu wa kuchipua majani wa 1844!" "Ndiyo, ndiyo! Asante Mungu!" "Je, huu si ukweli unaofuata unaozaa wakati wa kurudi kwa Kristo"?--Snow aliendelea katika hoja yake kwa uhakikisho wa shauku--" ni ufahamu kamili zaidi wa aina za majira ya kuchipua majani na kupukutisha majani katika sheria ya Musa. Sherehe ilikuwa Pasaka, iliyofanyika katika 'mwezi wa kwanza' wa mwaka wa Biblia. Sikukuu kuu ya sherehe za kupukutika kwa majani (Autumnn) ilikuwa Siku ya Upatanisho, katika 'mwezi wa saba' wa mwaka.

Je, ni siku gani ambayo Yesu alikufa msalabani?" Umati wa watu ukamjibu, "Pasaka, wakimfuatilia kwa makini. "Sawa! 'Kristo Pasaka wetu' alisulubishwa kwa ajili yetu (1 Wakorintho 5:7) katika mwezi wa kwanza, katika majira ya kuchipua ya mwaka, siku ile ile ambapo mwana-kondoo wa Pasaka alichinjwa. Lakini si hayo tu. Mwana-kondoo wa Pasaka alichinjwa muda gani?" "Wakati wa jioni," watu wakajibu, "Ndiyo; kwa usahihi zaidi, 'katika saa za jioni' kama Kiebrania inavyoelezea; si wakati wa machweo, lakini saa sita mchana. Hebu Niambie, Kristo Pasaka wetu alitoa uhai Wake kwa ajili yetu saa ngapi?" "Saa tisa kamili," jibu likaja."

Snow akirejelea mwanahistoria wa kale wa Kiyahudi Josephus na mwanahistoria mahiri, William Hales, aliweka tarehe ya Kifo cha Kristo kama majira ya kuchipua ya mwaka wa 31 BK, katikati ya juma la sabini la miaka ya Danieli (Daniel 9), "Ndugu zangu, ninawatangazia kutoka katika Neno la Mungu, kwamba Yesu alipokuja mara ya kwanza, alikufa kama Pasaka wetu katika mwaka ule ule uliotabiriwa katika unabii wa Danieli na siku ile ile iliyoamriwa katika nuru ya sherehe/kaida—hakika,

katika saa ile ile iliyowekwa katika sheria hiyo. Hakuna hata nukta moja ya sheria iliyoshindwa. Kila nukta na nukta ilitimia. Muda ulizingatiwa sana!

"Sasa, ndugu, kama vile Pasaka ilivyokuwa, yaani kivuli/mfano wa majira ya kuchipua, vivyo hivyo Siku ya Upatanisho ilikuwa kivuli/mfano wa majira ya kupukutisha majani. Je, kuhani mkuu alifanya nini katika Siku ya Upatanisho?" "Alisafisha Patakatifu." "Ndiyo, kwa kweli! Na ni kazi gani ambayo Yesu atakamilisha mwishoni mwa siku za miaka 2300 za Danieli 8:14?" "Utakaso wa Patakatifu!" Umati ulirudia tena. "Haswaa! Naam, kama wakati ulizingatiwa sana wakati Yesu alikufa kama dhabihu yetu ya Pasaka, je, hautazingatiwa kwa uthabiti wakati Kuhani wetu Mkuu atakapotimiza utakaso wa Patakatifu? Je! Si iko wazi kwamba Yesu atatimiza ahadi za unabii wa Danieli 8:14 si tu katika mwaka wa Danieli 8 bali, kwa usahihi zaidi, katika tarehe kamili ya Siku ya Upatanisho?"

Wafuasi wa Miller walipekua Biblia zao wakitazamana, kwa mshangao na kwa shukrani nyingi. Snow aliendelea, akithibitisha uhakika wa ujumbe wake. "Na ni lini, ndugu zangu, Siku ya Upatanisho inaangukia katika kalenda ya kaida/sherehe za Biblia?" "Siku ya kumi ya mwezi wa saba," walijibu, kwa umoja. "Sawa tena! Mambo ya Walawi 23:27 yasema, 'Siku ya kumi ya mwezi huo wa saba kutakuwa na siku ya upatanisho.' Ndugu, ikiwa tukio la kutakaswa lilikuja siku ya kumi ya mwezi wa saba, ni lini katika mfano huo Yesu atakamilisha utakaso wa Patakatifu?" Ari yake ilikuwa kubwa sana, "mwezi wa saba."

Snow alitulia na kuvuta pumzi kabla ya kutoa ushahidi wake wa mwisho. "Kwa hesabu ya uangalifu zaidi iliyohifadhiwa katika maandalizi ya Bwana na Wakaraite/Wayahudi, siku ya kumi ya mwezi wa saba inaangukia mwaka huu tarehe 22 Oktoba." Ndipo Snow akanyamaza, kisha akaleta uamsho kwa wito wake kwa kuhitimisha. "Ndugu, lifikirieni jambo hilo. Sasa ni wiki ya pili ya mwezi Agosti. Katika muda usiozidi miezi mitatu Bwana atakamilisha upatanisho na kutoka katika Patakatifu ili kuwabariki watu Wake wanaongoja (Mambo ya Walawi 9:22, 23). Katika muda usiozidi miezi mitatu kazi ya Mungu itakamilika. Hakuna msimu mwingine wa baridi yenye theluji (Winter) tena kwenye dunia hii ya zamani, yenye ubaridi. Katika muda usiozidi miezi mitatu, Bwana-arusi atakuwa hapa kumchukua bibi-arusi Wake anayesubiri.

Je! huu sasa sio wakati wa kilio cha usiku wa manane, kilio cha usiku wa manane, 'Tazama Bwana arusi anakuja; hebu tokeni nje kumlaki'?" Machozi ya shukrani na shangwe yalitiririka kwa uhuru. Snow aliombwa kurudia hotuba yake siku iliyofuata ili wote wahakikishe kwamba wameelewa. Viongozi wengine waliwahimiza watu kutumia vizuri ile hesabu ya siku zilizobakia. Wakitilia mkazo, na kuweka uzito, wakiwa wanyenyekevu, na waliopata nguvu mpya kama umeme, waumini walipanda treni, mashua, na mabehewa walipokuwa wakirudi nyumbani kwao, kila mahali

walibeba habari hiyo ya Kambi. Punde kilio cha usiku wa manane, kilisikika kama mwitikio wa kusisimua kikiruka kwenye milima ya granite huko New England."

Magharibi ya Kati ya nchi wakati huo huo (Midwest), walitamka kwa kauli moja "harakati za miezi saba" zilienea hadi kila jiji, kijiji, na kitongoji kilisikia habari hiyo, Himes alipinga hizi harakati, lakini baadaye alichukua uamuzi wa kuliunga mkono vuguvugu hili. Alihakikishiwa kwamba Mungu alikuwa ndani ya vuguvugu hilo, William Miller aliichunguza habari hizi kwa makini, akaomba kwa kina na bidii juu yake, kisha akaandika hivi kwa furaha: “Ninaona utukufu katika ‘mwezi wa saba’ ambao sikuwahi kuuona. Ninakaribia nyumbani. Utukufu! Utukufu! Utukufu!" Oktoba 22!

Tuna siku chache tu, ili tufikie mwisho wa wakati. Jamani, ni wakati wa ajabu iliyoje kuwa hai katika kipindi cha historia kama hiki! Jinsi hizi siku walizoziita siku za mwisho zilivyokuwa zikiyoyoma, wafanyabiashara Waadventista walifunga maduka yao; mafundi magari wakafunga maduka yao; wafanyakazi waliacha kazi zao. Watu wengi wakafika kwenye mikutano ya makambi wengi waliungama makosa yao na kukusanyika mbele kwenye mimbari kwa ajili ya maombi, pesa nyingi zilitolewa ili maskini waweze kulipa madeni yao na pia wanunue makaratasi ili waweze kutoa machapisho kuhusu mambo haya-mpaka wachapishaji wakasema hawawezi kutumia hizi pesa tena, na ndipo wale waliotaka kuwa wafadhili waligeuka na kurudi kwa huzuni.

Katika mashamba baadhi ya wakulima waliacha bila ya kutoa mavuno yao mashambani ili kuthibitisha imani yao,[3] tufaa/matunda yakaachwa kuoza kwenye bustani. Huko mijini walimu wengi wa mashule, majaji kadhaa wanalinda amani, hata mahakimu wa Norfolk - walijiuzulu kazi zao. Huko Philadelphia fundi cherehani kwenye Mtaa wa Tano alifunga duka lake kwa" heshima ya Mfalme wa wafalme ambaye angetokea tarehe ishirini na mbili ya Oktoba." Shirika kubwa la Brooklyn liliwaruhusu wafanya kazi wake waende zao makwao.

Watu wa imani ya Methodisti, Wapresbiteri, na Congregationalisti wakaharakisha kwenda kwenye maji ya ubatizo. Mashua za injini ya mvuke zinaendeshwa usiku na mchana kuwahimiza watu na Kilio cha Usiku wa manane na kusambaza machapisho mengine. Mamia elfu ya nakala yakaendelea kuchapishwa huko New York na Boston kwa wiki tatu. Kando na maelfu mengine huko Rochester, Topsham, Philadelphia, Lancaster, Utica, Cleveland, Cincinnati, Detroit, na Toronto.

Oktoba 15, siku saba tu zilikuwa zimebakia. Mnamo Oktoba 19 mitambo ya uchapaji iliacha kufanya kazi. Hema kubwa lilikuwa tayari limekunjwa kwa mara ya mwisho. Familia za Wahubiri zilikuwa zimerudi majumbani mwao ili kuwa pamoja na familia zao. Joshua V. Himes aliharakisha kwenda Low Hampton ili kuwa na Miller. Waumini

walikuwa wakingojea ndani ya majumba yao kwa furaha. Kijana Ellen Harmon baadaye aliandika, "Huu ulikuwa mwaka wa furaha zaidi maishani mwangu. Moyo wangu ulikuwa umejaa matarajio ya furaha."[4] Huko nje, ulimwengu pia ulikuwa ukisubiri kwa tashwishwi. Maelfu ambao hawakuwahi kujiunga na vuguvugu hilo waliichunguza mioyo yao kwa kuhofia inaweza kuwa kweli.

Oktoba 22 ilipoanza, Wafuasi wa Miller walikusanyika katika makundi makubwa na madogo; walikusanyika katika mahema yao, katika makanisa, katika hema za kukutania, katika nyumba za watu binafsi; katika mikutano ya makini na sala, ya ari, shangwe na sifa kwa Bwana. Huko Low Hampton, New York, marafiki wa Miller walikusanyika kando ya miti ya Canada (maple trees)  kando ya nyumba yake, mahali ambapo leo panajulikana kama mwamba wa kupaa juu kwenda mbinguni au Ascension Rocks. Walikuwa wakikesha mchana kutwa, kwa maana hawakujua ni saa ipi atakayokuja Bwana wao.

Jua lilichomoza upande wa mashariki, kama "bwana arusi atokaye chumbani mwake." Lakini Bwana-arusi hakutokea. Jua likasimama katikati mchana, kukawa na joto lenye kutoa uhai "pamoja na uponyaji katika mbawa zake." Lakini Jua la Haki lilishindwa kuangaza, likashuka upande wa magharibi ikawa machweo, ya ukali, "ya kutisha kama wenye bendera ?" (Wimbo wa Sulemani 6:10). Lakini Yeye aliyeketi juu ya farasi mweupe hakurudi kama kiongozi wa majeshi ya mbinguni. Vivuli vya jioni vilinyemelea taratibu na kuleta ubaridi katika nchi nzima. Saa za usiku zilisonga taratibu. Katika nyumba za wafuasi wa Miller wenye huzuni, kengele ya usiku wa saa sita iligonga ikiashiria siku mpya imengia. Oktoba 22 ilikuwa imefika. Yesu alikuwa hajaja. Jamani, Hakuwa Amekuja!

*Vidokezo:*

*1. The story is well told in James White, Life Incidents, pp, 153-168*

*2. Snow's studies in Exeter climaxed a development that had been emerging in so many ways and places that the Millerites considered it supernatural. See J. N. Loughborough, The Great Second Advent Movement (Nashville, Tenn.: Southern Publishing Association, 1905), pp. 157-159. Snow's presentation as given here is adapted from his own articles in the True Midnight Cry and in the Advent Review and Signs of the Times Reporter, October 16, 1844, and from James White, Life Incidents, pp. 159-168, and Joseph Bates, Second Advent Way Marks, pp. 30, 31*

*3. Heaven watched over the potatoes. In one instance in New Ipswich, New Hampshire, a blight affected the potatoes dug at the usual time, but the potatoes dug late by Leonard Hastings were protected in the soil and sold for an extra-good price.*

*4. Ellen G. White, Testimonies for the Church, 9 vols. (Mountain View, Calif.: Pacific Press Publishing Association, 1885-1909, 1948), vol. 1, p. 54 63*

## SURA YA 5
## "KWA NINI BABA HAKUJA?"

Mfuasi mwaminifu wa Miller, Charles Fitch hakukatishwa tamaa. Alikuwa tayari amekufa—siku nane kabla ya kukatishwa tamaa kukubwa— tarehe 14 Oktoba 1844. Alikuwa na umri wa miaka thelathini na minane tu, baba wa watoto sita. Fitch, kama utakumbuka, alikuwa mhudumu wa kusanyiko la Miller ambaye alitengeneza sanamu ya Danieli 2 ambayo inaweza kugawanywa, na "Chati ya 1843." Fitch alijiunga na harakati za ujio wa Yesu kwa mara ya pili. Mnamo 1838 alikuwa mmoja wa wachungaji wa kwanza kuchukua msimamo wake upande wa Miller, hadharani. Alipendezwa na tafsiri za kinabii za Miller; lakini alipoona kwamba upinzani ungemnyima utambulisho kwenye kanisa lake la kisasa huko Boston, alirudi nyuma.

Muda mfupi baadaye, hata hivyo, alipohamia katika parokia ya huko New Jersey, aligundua Yesu ni Mkweli, na Yesu kama Mwokozi wa Kweli na binafsi. Kisha aliachana na dhehebu lake kwa furaha ili kupeleka habari njema juu ya Kristo na uadilifu Wake kwenye makutaniko mengine mengi. Barua zake za upendo kwa mke wake, alizoandika alipokuwa akisafiri, zinaonyesha jinsi alivyoziandika kwa njia nzuri na kama kawaida, upendo kwa watu na upendo kwa Yesu. Sasa Josiah Litch alipoelekeza fikira za Fitch kwenye mihadhara ya Miller kwa mara ya pili, Fitch aliona katika siku zile 2300 zina ujumbe mzuri kuhusu kurudi kwa Bwana wake wa ajabu, naye alijitoa moyo na roho yake, kwa ajili ya mahubiri hayo.

Kifo cha kutisha cha watoto wake wanne kati ya sita kilizidisha hamu yake ya kuja kwa Masihi kwa mara ya pili. Muda mfupi kabla ya Oktoba 22, 1844, Fitch alibatiza vikundi vitatu vilivyofuatana vya waongofu nje, katika siku yenye baridi kali. Yaonekana kwa sababu hiyo, aliugua na, Jumatatu, Oktoba 14, akafa. Jarida la wafuasi wa Miller, Midnight Cry, liliripoti kwamba "mjane wake na watoto wasio na baba sasa wako Cleveland, wakitazamia kwa ujasiri kuja kwa Bwana wetu

kuwakusanya washiriki waliotawanyika wa familia" katika siku chache. "Dada Fitch atakuwa…... anatabasamu na mwenye furaha." kwa vile Yesu atakuwa amerudi.

Si vigumu kufikiria vichwani mwetu watoto wawili waliobakia, wakiuliza kwa machozi baada ya mazishi, "Mama, Je, tutamwona Baba yetu tena?" "Ndiyo, wapendwa," Bibi Fitch alijibu kwa ujasiri. "Baada ya siku chache tu, Yesu atakaporudi, atamwamsha Baba, na kaka na dada zenu waliolala usingizi wa mauti , na kisha tutakuwa pamoja familia yote nzima, yenye furaha tena milele!" Usiku wa Jumatatu, Oktoba 21, watoto waliuliza, "Mama, tutaonana na baba tena kesho?" "Ndiyo, wapenzi!" Siku ya Jumanne usiku walilia, "Kwa nini baba hakuja leo?"

Kulikuwa na familia nyingi kama hizo siku hizo. Wakiwa na watoto au wazazi wachanga ambao walikuwa wamekufa kwa kifua kikuu, kipindupindu, kifaduro, na magonjwa mengine ya kutisha, wengi walitazamia kuungana tena kwa furaha na wapendwa wao wakati Yesu angekuja tena. Sio bila sababu kwamba Oktoba 22, 1844, iliingia katika historia kama siku ya "Kukatishwa tamaa na kuvunjika moyo sana." James White aliandika miaka mingi baadaye, “Wakati Mzee Himes alipotembelea Portland, Maine, siku chache baada ya kupita kwa wakati huo, na kusema kwamba akina ndugu wajitayarishe kwa majira ya baridi kali na theluji, hisia zangu zilikuwa karibu kushindwa kudhibitiwa. Niliondoka mahali pa mkutano na kulia kama mtoto mdogo."

Katika mji mwingine, Waadventista sabini waliopigwa na butwaa walikaa pamoja katika nyumba kubwa ambamo walikuwa wamekusanyika ili kumlaki Bwana, wakihimizana kutotupilia mbali imani yao, na kushiriki gharama kwa kuweka pesa zao zote zilizobaki kwenye bakuli la pamoja na kupika au kufanya shughuli zao pamoja ili kujitegemeza na hali. Kiongozi wa wafuasi wa Miller alifanikiwa kuwashawishi kurudi nyumbani na kuendelea na maisha ya kawaida. Idadi nzuri ya waamini hawa hata hivyo, haikuweza kuzoea maisha haya kwa urahisi. Wengine hawakuwa hata na nyumba ambazo wangerudi na kukaa tena. Walikuwa wameuza mashamba yao na kuchangia mapato kwa ajili ya kazi hiyo ya injili.

Huko Paris, Maine, Edward Andrews aliialika familia maskini ya Stowell kuja na kuishi naye, tendo la ukarimu ambalo Mungu alilizawadia sana, kama tutakavyoona katika sura inayofuata. Kila mahali waumini waliokata tamaa waliulizana, "Je, tuko wapi sasa? Je, tumekosa nini?" Miller na viongozi wengine walikiri waziwazi kwamba walikuwa wamefanya makosa; lakini walifichwa kujua uthibitisho wa wazi kabisa kuhusu “kilio cha usiku wa manane” (kwamba Kristo angekuja tarehe 22 Oktoba) na “harakati ya mwezi wa saba” (kuenea kwa hamu kwa ujumbe huu na mwitikio wa dhati wa watu) ulibarikiwa sana na Mungu. Himes alizungumza akimtetea Miller na kwa ajili ya wengine wengi: "Tumekosea katika imani ambayo tulifikiri kuwa inaendeshwa kwa Neno na Roho, na majaliwa ya na ukarimu wa Mungu."

Katika harakati ya mwezi wa saba "Palionekana kuwa na nguvu isiyozuilika ..... ambayo ilinyenyekeza wote mbele Zake Bwana." na Ujumbe Wake "uliifikia mioyo katika sehemu tofauti, za mbali na karibu wakati huo huo, na kwa namna ambayo inaweza kuhesabiwa tu kwamba hakika ni Mungu tu, Ndiye alikuwa ndani yake. Palitokeza kila mahali uchunguzi wa kina zaidi wa moyo na kujinyenyekesha nafsi mbele za Mungu wa mbinguni, na hata kusababisha watu kuacha upendo kwa mambo ya ulimwengu huu—kuponywa kwa mabishano na uadui—ungamo kwa makosa, kujidhili mbele za Mwenyezi Mungu, na dua na maungamo Kwake kwa ajili ya msamaha na kukubaliwa.” "Lakini tuliweza kusema, 'Hivi sisi tulikuwa nani, hata tumpinge Mungu?'"[5] "Mungu mkuu ametutendea kwa njia ya ajabu," aliandika F. G. Brown, Mwadventista mwingine mashuhuri.

"Ubaguzi wetu, elimu, mapendeleo yetu, kiakili na kimaadili, vyote vilipinga fundisho hili la kuja kwa Bwana. ... Roho Mtakatifu alitenda ... katika nafsi zetu za ndani," mpaka ujio wa pili wa Bwana, ukawa "tumaini letu, furaha yetu sote." "Biblia tunaisoma, na kila ukurasa umejaa kuja kwa Bwana mara moja."[6] Brown aliposema kwamba kila ukurasa wa Biblia umejaa ujio wa upesi wa Bwana, alitia chumvi kidogo tu.

Agano Jipya pekee linataja ujio wa mara ya pili wa Bwana mara 300! Yesu aliahidi, "Nikienda ... , nitakuja tena." (Yohana 14:3) Malaika walitabiri, "Yesu huyu ... atakuja jinsi vile vile mlivyomwona akienda Zake." (Mdo. 1:11) Petro alizungumza kuhusu wakati ambapo “Mchungaji mkuu atatokea.” (1Petro 5:4) Paulo alisema, “Bwana Mwenyewe atashuka kutoka mbinguni. (1 Wathesalonike 4:16) Yohana alisema waziwazi, “Yeye anakuja na mawingu.” (Ufunuo 1:7)

Hata kama ahadi hiyo haikutajwa waziwazi popote pale, inaweza kueleweka kwa urahisi kutokana na mambo mengine yote ambayo Biblia husema kumhusu Mungu. Mungu mwenye upendo, Mwenye uwezo wote wa Biblia hataacha kosa kwenye kiti cha enzi cha dunia milele. Siku moja Yeye atafanya mabadiliko! Miller alikuwa sahihi bila shaka katika kuhubiri ujio wa pili. Alikuwa sahihi bila shaka, pia, alipowataka watu wajitayarishe. Yesu alisema, “Kwa hiyo ninyi nanyi jiwekeni tayari, kwa maana katika saa msiyodhani Mwana wa Adamu Yuaja. (Mathayo 24:44 ).

Miller alikazia sana kujitayarisha, kiasi kwamba kwake wakati wa kurudi kwa Kristo, ingawa lilikuwa jambo muhimu, hili lilikuwa na umuhimu wa pili. “Lengo langu kuu lilikuwa ni kutaka nafsi za watu ziongolewe kwa Mungu,” aliandika baada ya kukatishwa tamaa, “na nilitaka kuwahamasiha wanadamu wenzangu kufanya matayarisho hayo ya moyo, ambayo yatawawezesha kukutana na Mungu wao kwa amani. Katika moja ya safari zake za mapema alimimina mzigo wa moyo wake kwa watu wa nyumbani. "Ee Mwenyezi Mungu waamshe watu wa Mungu huko Hampton. ....., Baba yangu, waongoe watoto wangu!" Wengi wa majirani zake

walimkubali Kristo; na kuhusu familia yake, kufikia 1843 aliweza kufurahi, “Nina mke na watoto wanane na nina sababu ya kuamini kwamba wao ni watoto wa Mungu na waamini wa Mafundisho yale ya Neno la Mungu ninayofundisha.

Mkazo wa Miller ulikuwa mkubwa zaidi juu ya utayarishaji wa moyo, kuliko kuhesabu wakati, kwamba hata wakati ambapo Yesu hakuja Oktoba 22, aliweza kusema kwa uaminifu wote, "Natamani kuuliza kama mafundisho yangu yameathiri na kuleta mashiko" kuongeza shauku ya kurudi kwa Yesu. Miller, hakika alikuwa amekosea tukio ambalo lilitimia yaani "kutakaswa kwa Patakatifu" mwishoni mwa siku 2300; lakini hakuwa na haja ya kuona kuwa amekosea kuhusu hesabu yake ya wakati.

Tafsiri yake ya siku 2300 kama miaka 2300 ilitokana na dhana (Ezekieli 4:6) kwamba siku moja ya mfano katika unabii ni sawa na mwaka mzima-(siku moja=mwaka mmoja.) Unabii mwingi katika Biblia una lugha ya mfano kama hiyo. Wanawake wanawakilisha makanisa, wanyama wanawakilisha himaya au falme, maji yanawakilisha watu, na kadhalika. Hata wapinzani hodari wa Miller, kama vile Mchungaji George Bush, walikiri na kukubaliana na kuchukua siku moja kama neno la kinabii, lililowakilisha mwaka mmoja, ... hata Isaac Newton, Askofu Newton, Kirby, Scott, Keith, na wengine wengi walikubaliana na hili." Katika kukubali hili, Bush alikuwa sahihi. Siku 2300 zilitambuliwa kuwa miaka 2300 na watu wengi kabla ya Miller, kurudi nyuma hadi mwanzoni mwa karne ya tisa, karibu miaka elfu moja kabla ya William Miller kuzaliwa!

Martin Luther na Wanamatengenezo wengine wengi waliamini kanuni ya siku moja kusimamia mwaka, kama alivyofanya Sir Isaac Newton, mmoja wa wanasayansi wakuu katika historia. Newton kweli alisoma theolojia na historia ya kanisa maisha yake yote na aliandika maneno zaidi (1,300,000) juu ya masomo haya kuliko katika uwanja wa sayansi. Akili yake iliyopenda hisabati, ilipelekea kuvutiwa na unabii wa muda mrefu kwa namna ya pekee. Katika karne ya kumi na nane ugunduzi mkubwa ulifanywa chini ya uongozi wa Mungu kupitia Johann Petri (1718-1792), mchungaji wa Kanisa la Reformed huko Ujerumani. Petri alikuwa wa kwanza (1768) kutambua kwamba siku 2300 za Danieli 8:14 zilianza kwa wakati mmoja na unabii wa majuma sabini wa Danieli 9, hivyo kufanya iwezekane mwishowe kuhesabu kwa uhakika fulani kuhusu, mwisho wa siku hizo. Uhalali wa hoja ya Petri--ambayo ina mantiki nzuri—unathibitishwa na ugunduzi wa njia na hoja zilizoendana na Hans Wood huko Ireland (1787), John A. Brown huko Uingereza (1810), na W. C Davis, mchungaji wa Presbyterian huko South Carolina (1811)—hawa wote walifanya uchunguzi huu kabla ya William Miller, mlei wa Kibaptisti huko New York, kufikia hitimisho la jumla katika utafiti wake uliojitegemea katika mwaka 1818.

Kulingana na pointi zao za kuanzia na usahihi wa hesabu yao, watu hawa wote walihitimisha kwamba siku 2300 zingefungwa katika miaka ya 1840 au (katika kesi ya Hans Wood) miaka ya 1880. Manuel de Lacunza, Padre Mjesuti; Joseph Wolffe, Myahudi Mkristo; Henry Drummond, mfanyakazi wa benki na Mwingereza na mbunge; William Cunningham; Heinrich Richter; Mortimer O'Sullivan; Louis Gaussen; William Pym; George Croly; Henry Manning; Alexander Keith; James A. Begg; George Stanley Faber; na wengine wengi huko Scotland, Ireland, Ufaransa, Ujerumani, Uholanzi, Uswizi, Amerika ya Kusini, Mashariki ya Kati, na (idadi kubwa zaidi) kule Uingereza waliandika vitabu, walitoa mahubiri, walichapisha majarida, na kufanya mikutano ya uamsho kuhusu ujio wa pili wa Bwana yaani zaidi au sambamba kidogo na uamsho wa pili wa Miller wa ujio wa pili katika Amerika ya Kaskazini.

Uamsho wa Ulaya haukuwa na umoja kama wa Marekani, na haukubainisha tarehe ya ujio wake kama ile ya  Marekani ya Oktoba 22, 1844; lakini kufikia mwaka wa 1844 idadi kubwa ya wachungaji, wakiwemo mapadre 700 wa Kianglikana, walikuwa wakitangaza ujio wa pili katika makanisa makubwa ya mawe na makanisa madogo katika vijiji vya Waingereza, wakichukua kama maandishi yao ya kauli mbiu, ujumbe wa malaika wa kwanza katika Ufunuo 14, “Saa ya hukumu Yake imefika." Thomas B. Macaulay, mwanahistoria mashuhuri na mjumbe bungeni, aliandika mnamo 1844 kwamba idadi ya wale walioamini katika kurudi kwa Kristo ilijumuisha watu wa aina mbalimbali "waliotofautishwa kwa vyeo, mali, na uwezo. ... Waheshimiwa," aliongeza; "na wabunge wameandika kuitetea hoja hii."

Jambo la kuvutia kwa njia ya kipekee ilikuwa ni kuonekana kwa "wahubiri watoto" katika nchi ya Sweden katika kipindi hiki. Ilipokaribia mwaka 1841 na kuendelea hadi majira ya joto mwaka 1844, vijana na hata watoto wadogo walitoa wito kwa ujasiri kwa ajili ya matengenezo ili kujitayarisha kwa ajili ya kurudi kwa Kristo.  Kwa mujibu wa sheria, hakuna mtu mzima ambaye angeweza kuhubiri nchini Swideni bila ruhusa ya kanisa na serikali. Ili kukwepa hili, Mungu aliwaita watoto. Hata hivyo, wengine walinyanyaswa. Ole Boqvist, kwa mfano, alipigwa bila huruma mbele ya dada yake, kisha akaachiliwa bila kutarajiwa, kwamba aendelee kuhubiri. Msichana mmoja mdogo sana alicheza kwa njia ya kawaida na wanasesere wake huku majirani wakikusanyika nyumbani kwake. Kisha akahubiri kwa mamlaka kwa muda wa saa moja hivi, kisha akarudi kucheza na wanasesere wake.

Dk. Sven Erik Sköldberg, ofisa wa tiba wa serikali kwa miaka thelathini, alichunguza “ugonjwa wa kuhubiri” wa watoto hawa,” kama alivyouita kama maadui wake walivyouita, na kuripoti kwamba baadhi ya watoto hao walihubiri wakiwa wamelala chini na  kufumba macho, bila fahamu, na yaonekana hawakupumua (kama maono ya Danieli 10:17). Lis Andersdotter, Mary Swensdotter, na pengine vijana wengine wadogo wa miaka kumi na kitu, ikiwa midomo na pua zao vilikuwa vimefungwa

wakiimba, waliendelea kuvumisha wimbo huo (humming). Dk. Sköldberg aliripoti kwamba watoto walitangaza mambo muhimu ya Ukristo--Kristo, sala, toba, na wongofu—lakini hakutoa maelezo yoyote ya maonyesho yao ya kimwili. Watoto walipoulizwa kutoa maelezo yao wenyewe, walinukuu Yoeli 2:28, “Itakuwa, baada ya hayo, ya kwamba nitamimina roho Yangu juu ya wote wenye mwili, na wana wenu na binti zenu watatabiri.”

Na mada ya ujumbe wao ilikuwa nini? Kimsingi ilikuwa ni sawa na wafuasi wa Miller na Waadventista waliokuwa wakihubiri kwa Kingereza,’ ujumbe wa malaika wa kwanza wa Ufunuo 14: "Saa ya hukumu Yake imekuja." Haijalishi sababu yoyote inayoweza kutolewa kuwa “ni kwa nini Baba hakuja" katika familia ya Charles Fitch mnamo Oktoba 22, 1844, haikuwa kwamba Miller alikuwa amevumbua nadharia iliyobuniwa kwa msingi wa tafsiri za mtazamo wake binafsi. Hakika ujumbe wake ulikuwa sahihi kabisa katika mambo yake mengi muhimu. Na ilikuwa ni sehemu ya mwamko mkuu wa Marejeo ya Kristo ya Pili—harakati ya mabara tofauti, ya madhehebu mbalimbali ambayo ilitangaza Ukweli mkuu wa kinabii ambao wakati wake ulikuwa umefika.

*Vidokezo:*

*1. Arthur Whitefield Spalding, Origin and History of Seventh-day Adventists, 2 vols. (Washington, D.C.: Review and Herald Publishing Association, 1961), vol. 1, p. 113, note 4; Seventh-day Adventist Encyclopedia (hereafter, SDA Encyclopedia), art, "Fitch, Charles."*

*2. Midnight Cry, October 31, 1844, p. 142.*

*3. James White, Life Incidents, p. 182*

*4. Luther Boutelle, Sketch of the Life and Religious Experience of Elder Luther Boutelle ([Boston]: Advent Christian Publishing Society, 1891), pp. 68, 69, in Arthur, "Joshua V. Himes," pp. 146, 147*

*5. Midnight Cry, October 31, 1844, p. 140*

*6. Letter of November 11, to Advent Herald*

*7. Miller, Apology, p. 24*

*8. William Miller to his son William, November 17, 1838, in Nichol, The Midnight Cry, pp. 65, 66*

*9. William Miller, February 4, 1843, to Signs of the Times, in Bliss, Memoirs, pp. 180,181 78*

*10. Miller, Apology, p. 34*

*11. Rush, Reasons for Rejecting, p. 6*

*12. Nahawendi began the 2300 years in 942 BC with the destruction of the tabernacle at Shilohand ended it at the projected coming of the Messiah in AD 1358. See Froom, Prophetic Faith, vol.1, p. 713; Seventh-day Adventist Bible Commentary, vol. 4, p. 54*

*13. H. McLachlan, ed., Sir Isaac Newton: Theological Manuscripts (Liverpool: University Press, 1950), pp. 1-25*

*14. Petri began the 70 weeks in 453 BC, ending the 2300 days in 1847. See Froom, Prophetic Faith, vol. 2, pp. 713-719*

*15. Froom, Prophetic Faith, vol. 2, pp. 719-722; vol. 4, pp. 210-221*

*16. Mourant Brock, Glorification (American Millennial Association reprint, 1845), p. 134, in Froom, Prophetic Faith, vol. 3, pp. 705, 706*

*17. Thomas B. Macaulay, Critical and Miscellaneous Essays (Philadelphia: Cary and Hart), vol. 5, p. 324, in Froom, Prophetic Faith, vol. 3, p. 268*

*18. Ellen G. White, "Notes of Travel," Historical 79 Sketches of the Foreign Missions of the Seventh-day Adventists (Basle: Imprimerie Polyglotte, 1886), pp. 201-207; Ole Boqvist, Review and Herald, October 7, 1890, p. 612; Froom, Prophetic Faith, vol. 3, pp. 671-686*

## SURA YA 6
## KUINGIA KWA USHINDI II

"Tulitumaini kwamba ni Yeye ambaye angewakomboa Israeli" (Luka 24:21, NASB). Inasaidia kujikumbusha wenyewe kwamba tukio la Oktoba 22, 1844, halikuwa tukio la kwanza la kukatishwa tamaa kukubwa au mvunjiko wa moyo mkuu kwa watoto wa Mungu. Fikiria ile huzuni iliyokuwepo wakati Yesu alipokufa msalabani! Siku ya Jumapili mara tu baada ya kifo cha msalaba, bila watu kujua kwamba Yesu amefufuka kutoka kwa wafu, wafuasi Wake wawili walikuwa wakienda huko vijijini kwenye mashamba, wakati Yesu alipokutana nao njiani. Bila kutarajia kumwona tena, walishindwa kumtambua na kuzungumza kwa huzuni juu ya kusulubishwa Kwake. Kleopa, mmoja wa wasafiri hawa, aliugua kwa huzuni ya moyoo=, "Tulitumaini kwamba Yeye Ndiye atakayewakomboa Israeli."

Miaka elfu mbili na maelfu ya maili ya kuondolewa kutoka wakati huo na mahali hapo, bado tunadaka kwikwi za kilio katika sauti ya huzuni ya msafiri. Na machozi yake hayakuwa yake peke yake. Hebu fikiria wanandoa wachanga ambao siku chache tu zilizopita walikuwa wamemleta mtoto wao aliyekuwa mahututi kwa ugonjwa kwenye Pasaka. Kila kitu kilitegemea kumweka hai maili chache zaidi za uchovu, saa chache zaidi za wasiwasi, mpaka waweze kufika Yerusalemu mbele ya Yule Mponyaji mkuu, ambaye kwa miaka kadhaa alikuwa amehudhuria Sherehe hiyo kama desturi ya Kiyahudi ilivyokuwa. Nao walitembea maili nyingi ya safari hiyo yenye kuchosha, na siku hiyo ya kuogofya.

Kwa bahati wanawasili wakati mtoto bado yuko hai, lakini wanagundua kwamba Mponyaji Mwenyewe yaani Masihi amekufa, Maelfu waliambiana wenyewe kwa wenyewe huzuni yao. “Kila upande kilio kilisikika, Tunamtaka Kristo Mponyaji!...Lakini watu walirudishwa nyuma kutoka kwenye nyua za hekalu, na askari wakawekwa kwenye malango....Walioteseka…wakainama chini kwa masikitiko na kukatishwa tamaa. ... Matabibu waliulizwa bila mafanikio kama Je, hapakuwa na ujuzi na uweza kama huo wa Yeye aliyelala kaburini mwa Yusufu?. "Sisi tulikuwa tukitumaini ya kuwa Yeye Ndiye atakayewakomboa Israeli." Hapa, hakika kulikuwa na "Kukatishwa tamaa Kukubwa!" Sasa, huzuni ya mwishoni mwa juma la kusulubishwa iliongezwa na ukweli kwamba, siku chache tu kabla ya kifo Chake, Yesu aliingia kwa sherehe ya kusisimua inayojulikana kama ‘kuingia kwa kishindo cha ushindi Yerusalemu” na kushangiliwa kwa Hosanna. Hatupaswi kupuuza hili. Jambo hili litatusaidia sana katika ufahamu wetu wa kukatishwa tamaa kwa wafuasi wa Miller.

Siku ya Jumapili kabla ya kifo Chake Yesu, Yeye aliwatuma wanafunzi Wake wawili kutafuta mwana punda, kisha kumfungua, na kumletea. Walipoonekana kushangaa, Yesu aliwaambia wamwambie mmiliki wa punda, "Bwana anamhitaji." Kwa hiyo wanafunzi wakamchukua mwana punda, na Yesu akapanda juu yake hadi Yerusalemu—katika utimizo wa unabii wa Agano la kale wa Biblia unaosema: “Furahi sana, Ee binti Sayuni; piga kelele, Ee binti Yerusalemu; Tazama, Mfalme wako anakuja kwako; Ni Mwenye haki, Naye ana wokovu; Ni mnyenyekevu, amepanda punda, Naam, mwana-punda, mtoto wa punda” (Zekaria 9:9). Watu walipomtazama Yeye akipanda mwana punda katika utimizo wa unabii wa Zekaria, walipata uhakika kwamba Yeye alikuwa karibu kujiweka Mwenyewe kuwa mfalme wa kidunia, awafukuze Warumi waliokuwa wakiwachukia, watoke migongoni mwao, na kufanya Yerusalemu kuwa mji mkuu wa ulimwengu na sio Rumi.

Kwa wazi, Kristo alichukua hatua ya kwanza katika shughuli iliyowaacha watu na maoni yasiyofaa sana kumhusu Yeye, ambayo matokeo yake yalifuatiwa na kukatishwa tamaa kwa jinsi ya kuogofya. Yawezekanaje basi, kwamba Kristo, njia, kweli, na uzima, awe sehemu ya udanganyifu uliopangiliwa hivyo? Je, Mfalme wa

Amani awezaje kweli, kudhamiria namna hii, na hata kuweka jukwaa la huzuni iliyofuata? Au maswali haya ni ya kupotosha? Je, Yesu alikuwa “Yeye ambaye angewakomboa Israeli”? Hakika! Alikuwa Mwokozi wa ulimwengu wote! Je, Yesu, alipokuwa ameketi juu ya punda, alikuwa mfalme kweli? Pasipo shaka alikuwa Mfalme wa sayari zote! (universe)

Je, Yesu alipowaongoza watu wamtazame Yeye kama mfalme, alikuwa amewadanganya? La! Bila shaka sivyo hivyo! Ni nini basi kiliwafanya wachanganyikiwe juu Yake na, baadaye kidogo, wakakatishwa tamaa ndani Yake Yeye? Ilikuwa sababu ya kutokuelewa kwao wenyewe. Ili kufanya iwe wazi kabisa katika akili zetu kwamba Yesu hakuhusika na kutoelewa kwao na kukatishwa tamaa kwao hapo baadaye, basi tuulize swali lingine: Je, Yesu aliwahi kuwaonya wafuasi Wake kwamba Yeye hakuwa mfalme wa aina ile waliyomdhania na kwamba angeenda kuuawa? Jibu ni kwamba, kama miezi tisa kabla ya kusulubishwa “Yesu alianza kuwaonyesha wanafunzi Wake ya kwamba imempasa kwenda Yerusalemu, na kupata mateso mengi kwa wazee na wakuu wa makuhani na waandishi, na kuuawa, na kufufuka tena siku ya tatu." (Mathayo 16:21)

Kristo hangeweza kuwa wazi zaidi kuliko hivyo! Hata hivyo mbingu ilifanya hata zaidi ya haya kuwajulisha watu Ukweli mapema. Yesu alitambulishwa na Yohana Mbatizaji katika dakika ya kwanza ya huduma Yake rasmi kama Mwana-Kondoo wa Mungu (Yohana 1:29). Kila mtu alijua kwamba katika utumishi wa Patakatifu wana-kondoo wa Mungu walikufa kama dhabihu kila siku ya mwaka na kila mwaka kwenye Pasaka. Danieli 9, iliyoandikwa miaka 500 kabla ya kuzaliwa kwa Kristo, ilifunua kwamba "katikati" ya juma la mwisho la yale majuma sabini (ya miaka 490), Masihi "angekatiliwa mbali." Isaya 53, iliyoandikwa miaka 700 hivi kabla ya kuzaliwa kwa Kristo, ilitabiri kwamba Mtumishi wa Mungu, kama ilivyokuwa mwana-kondoo, ‘angeongozwa kwenye machinjo (Mstari wa 7, RSV)

Mwanzo 3:15, ahadi ya kwanza kabisa ya Mwokozi, ilionya kwamba adui “angeuponda” uzao wa mwanamke. Hivyo kwa muda wa miaka 4000 mbingu ilifanya kila iwezalo kuzuia kutokuelewa kwa watu na matokeo ya kukata tamaa! Lakini kwa nini basi Yesu aliweka jukwaa la kuingia Yerusalemu kwa ushindi? Kwa nini hakukaa tu kwenye mbao Zake za useremala kule Nazareti na kuepuka kila fursa ya kutoeleweka? Unajua ni kwa sababu gani? Wakati ulikuwa umefika wa Yeye kufanya tendo la muhimu sana katika historia yote. Alipaswa kufa msalabani kama upatanisho kwa ajili ya dhambi za ulimwengu, kufanya msamaha uwezekane kwa kila mwanadamu duniani, na kurejesha imani katika tabia na serikali ya Mungu katika malimwengu yote.

Katika asubuhi ile ya Jumapili ya kuingia kwa ushindi na shamra na shangwe, Yesu alijua ya kwamba katikati ya juma la sabini na la mwisho la unabii la miaka

iliyotabiriwa katika Danieli 9—hasa, katika Ijumaa ile ya Pasaka inayokuja katika saa ile ile, yaani saa tisa alasiri. wakati mwana-kondoo wa Pasaka alipotakiwa kuchinjwa—Yeye, Muumba wa mbingu na dunia, alipaswa kufa juu ya msalaba nje ya kuta za Yerusalemu ya kale. Alijua kwamba kwa tendo hili angeonyesha upendo wa Mungu bila kosa, akifungua njia kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu na kufanya uzima wa milele uwezekane kwa kila mtenda dhambi mwenye hatia.

"Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele." Lakini ingesaidia nini kuonyesha upendo huo ikiwa hakuna mtu atakayepata kusikia kuhusu huu upendo? Wema kama huo ulidai kuhubiriwa sana ili mtu mdhambi mwenye hatia ajifunze, na kuamini, na kuishi tena. Hii ndiyo sababu Yesu aliandaa kuingia kwa ushindi Yerusalemu na kuimbiwa Hosanna. Alifanya yote aliyoweza kuwazuia watu kutoelewa. Lakini walipong'ang'ania katika kutoelewa kwao, hata hivyo Yeye aliendelea, akijua kwamba baada ya muda, wengi wangekuja kuelewa waziwazi ambapo vinginevyo wasingejali kujua jambo hilo kamwe. Lakini kabla hatujaondoka kwenye "kuingia kwa kishindo Yerusalemu," lazima tujiulize maswali mawili zaidi kuhusu hilo na kuhusu "Kukatishwa tamaa kukubwa" kulikofuata.

Katika barabara ya Emau, Yesu alieleza ni nini kimetokea na kwa njia gani kilichotokea? Je, unaweza kutaja majina ya wale wanafunzi wawili waliokwenda kijijini/shambani? Je, unamfahamu Kleopa. Je, hukumbuki jina la mtu mwingine wa pili aliyekuwa anatembea naye? Hapana, hakika Biblia haitoi jina hilo. Baada ya kukatishwa tamaa sana katika juma lile la kusulubishwa, Yesu alijifunua kwa namna ya kipekee sana, maelezo yenye manufaa zaidi ya kile ambacho kilikuwa kimeenda vibaya, hayakutolewa kwa wanafunzi wakuu kama Petro, Yakobo, na Yohana, bali kwa walei Wakristo wawili ambao wasingejulikana kwa njia nyingine, ila kama walei waliojitolea. Na ni kwa njia gani Yesu alielezea jinsi walivyokatishwa tamaa? "Akawaambia, Enyi msiofahamu na wenye mioyo mizito kuamini yote waliyonena manabii! haikumpasa Kristo kuteswa na kuingia katika utukufu Wake? Na kuanzia Musa? akawaeleza katika maandiko yote mambo yaliyomhusu Yeye Mwenyewe” (Luka 24:25-27)

Hivyo ndivyo ilivyokuwa. Yaonekana aliwakumbusha mafungu ya Biblia kama tulivyozungumza muda mfupi uliopita—Mwanzo 3:15, kuhusu nyoka kuponda uzao wa mwanamke; Isaya 53, kuhusu kuongozwa kwa Mwana-Kondoo kwenye machinjo katika utaratibu wa Patakatifu kutokana na taratibu au kaida; Danieli 9, kuhusu Masihi "kukatiliwa mbali;” na bila shaka Aya zingine nyingi. Alipokuwa akifanya hivi, bila shaka Kleopa na mwenzake lazima walisema, "Tumesikia hili jambo mara mia! Kwa nini basi hatukuweza kuliona hapo awali?" Na nyoyo zao zikawaka ndani yao alipowafunulia Maandiko. Baadaye kidogo, walipomtambua Yesu, Yeye aliwaacha. Waweza kufikiria jinsi walivyokimbia kurudi Yerusalemu, wakijikwaa kwenye njia ya

mawe katika mwanga wa mbalamwezi wakati wa Pasaka, wakikimbilia, kuwaambia wanafunzi wakuu kile walichokuwa wamejifunza na Yule Ambaye walikuwa wamemwona! Viongozi walijichunguzia upya Maandiko kwa uangalifu. Punde, wakiwa wamewezeshwa na neema ya Mungu, walianzisha vuguvugu jipya la kidini, kanisa la Kikristo.

Hakika tukio hili la 1844 ni Kuingia kwa Ushindi II (Kuingia kwa Ushindi na Shangwe kwa pili), tunaweza kuhusisha kama mwendelezo wa "Kuingia kwa Ushindi I" na kisha, "Kukatishwa tamaa Kukubwa kwa kwanza." Lakini kama tuwezavyo kufikiri, ikiwa tutaweza, kuita huzuni ya Oktoba 22, 1844, ni "Kukatishwa Tamaa Kukubwa kwa pili," hivyo tunaweza kufikiria mwamko mkuu wa Majilio ya Pili kama "Kuingia kwa Ushindi kwa kwanza." Kama tutakavyoona katika sura zinazofuata, Mnamo Oktoba 22, 1844, Yesu alianza kazi mpya ya upatanisho muhimu katika njia Yake kama upatanisho wa Kalwari. Katika mpangilio wa neema ya Mungu, pale Yesu alipokufa msalabani, saa tisa mchana ya Ijumaa ya Pasaka karibu na mwisho wa majuma sabini, ndivyo Yesu alianza huduma hii nyingine ya upatanisho katika Siku ya Upatanisho ya sherehe/kaida (ceremonial), Jumanne, Oktoba 22, 1844, mwishoni mwa miaka ile 2300—siku za Danieli 8:14.

Na kama vile awali Alipotundikwa msalabani nje ya Yerusalemu ya kale, vivyo hivyo wakati huu Yeye alisimama kando ya mbao za torati katika Patakatifu pa Patakatifu pa mbinguni katika Yerusalemu Mpya. Huduma hii mpya ya upatanisho ni, kama tutakavyoona, mchakato wa kipekee wa neema tele wakati mwingine unaitwa "kuondolewa au kufutwa kwa dhambi," huduma iliyokusudiwa kuondoa dhambi zote kutoka kwenye mioyo na maisha na kumbukumbu za waamini wapendwa wa Kristo na kuwatayarisha kwa maisha ya milele. Kuwa na umoja wa milele na "upatanisho" wa milele na Baba (At-one-ment). Tendo kubwa na la neema sana la upatanisho lilidai kutangazwa hadharani kwa bidii zaidi, ili watu waweze kujifunza tena, na kuamini, na kuishi. Na mlipuko mkubwa wa utangazaji wa habari hizi njema ulipokelewa kama tulivyoona, katika Ulimwengu wa Kale na mpya. Lakini Mungu angewezaje kumwita hivyo Miller na wengine wengi kuhubiri ujumbe ambao haukuwa wa Kweli?

Tumeona kwamba ujumbe wa Miller ulikuwa uko karibu sana na ile kweli. Alikuwa amepatia juu ya uhalisia wa ujio wa pili, aina ya maandalizi yaliyohitajika, umuhimu wa kuongoa roho, na hesabu ya siku 2300, hakika alikuwa sahihi zaidi kuliko watu wa wakati wake. Kile tu ambacho alikuwa amekosea ni mahali pa tukio, kufikiri kwamba Patakatifu pa kutakaswa katika Danieli 8:14 palikuwa duniani, na katika kuhitimisha kwamba utakaso wa Kristo wa Patakatifu ungetimizwa kwa kuja Kwake duniani kuusafisha ulimwengu na kuhukumu kanisa kama Mfalme wa wafalme. Hakufanya kosa kubwa zaidi kuliko lile wanafunzi walilofanya walipofikiri kwamba unabii aliotabiri ulihusu kuja kwa Kristo kama mfalme katika mwaka wa 31 BK.

Lakini ikiwa ni hivyo, kwa nini basi Yesu hakufafanua suala hilo kwa Miller na kuhakikisha kwamba alikuwa na ujumbe ulionyoka mbele za watu!? Jibu ni kwamba alijaribu, kama vile alivyojaribu na wanafunzi wake mwenyewe kabla ya kuingia Yerusalemu kwa ushindi mara ile ya kwanza. Angalia Aya za Maneno katika Danieli 7, Luka 12, Waebrania 8 na 9, Ufunuo 10, na Ufunuo 11, zinavyoeleweka vyema sasa, ambavyo zingezuia kukatishwa tamaa pale 1844, kama vile ambavyo Aya zingine za Agano la Kale zingeweza kuwaokoa wanafunzi kutokana na kukatishwa tamaa kwao.

Pia, kuna ulinganifu wa kustaajabisha wa Yesu pale alipokuwa akiwaonya wanafunzi Wake kwamba angeteseka sana, na kisha kufa, na kufufuka tena siku ya tatu. Mapema miaka ya 1840 Bwana Aliwachagua Wafuasi wawili wa Miller, William Foy (mhudumu Mmarekani mweusi ambaye alikuwa na ngozi nyeupe) na Hazen Foss, na katika maono ya kinabii aliwaonya kwamba wakati ungeendelea zaidi ya Oktoba 22, 1844! Kwa mara nyingine tena kutokuelewa kulikuwa katika akili za watu—**na sio katika mapenzi ya Mungu**. Lakini ikiwa katika maelezo haya Miller alikosea, kwa nini basi Mungu alimtaka ahubiri hata kama ni kwa udogo kuhusu kurudi Kwake? Kwa nini hakumwacha tu aendelee kulima nafaka na kukamua ng'ombe wake, maisha yake yote? Hakika hata Miller ndivyo alivyotaka. Kama ingekuwa hivi, basi hata kusingekuwa na kukatishwa tamaa kukubwa kwa 1844..

Tumetoa sababu kwa nini Bwana aliruhusu hili. Yesu alikuwa karibu kuingia katika mchakato mkubwa wa upatanisho ulio sawa katika neema na ufanisi kwa kifo Chake msalabani—na ulimwengu ulihitaji kujua juu ya jambo hili zito ili watu waweze kujifunza na kuamini na kuishi. Na ni kwa nani, wapi, na jinsi gani Yesu alieleza kwa mara ya kwanza kutoelewa jambo hili baada ya kukatishwa tamaa mwaka huo wa 1844?

Mnamo Oktoba 23, asubuhi ile iliyofuata tu siku ya Oktoba 22, Mwadventista mwenye bidii, ila asiyejulikana sana, Hiram Edson kwa jina, alikuwa akipitia njia ya mkato, ili kuvuka shamba la mahindi, akiwa na rafiki yake, wakati mara moja jambo hilo likaangaza akilini mwake, naam, Ukweli ulio thabiti. maelezo ya matamko muhimu katika Danieli 7, Luka 12, Ufunuo 10 na 11, na (saa chache baadaye, akiwa nyumbani) alionyeshwa katika Waebrania 8 na 9, ambayo Wafuasi wa Miller nayo pia hawakuielewa vizuri au waliiruka na laiti wangeyapitia mafungu haya, basi mambo yangeeleweka vizuri na kusingekuwa na kukatishwa tamaa kukubwa au kukosea sana kama ilivyokuwa imekwisha kutokea.

Kwa maneno mengine, Yesu alimfungulia Hiram Edson kutoka katika Maandiko mambo yaliyomhusu Yeye Mwenyewe. Hiram Edson akisafiri na mwenzake katika shamba la mahindi alikuwa kama “Kleopas shambani, alipokuwa akitembea na rafiki yake walipokutana na Yesu, Naye akawafunulia.” Edson alikuwa kama Waadventista wa wakati wa Yesu, akisafiri kuingia vijijini na mashambani pamoja na

mwenzake. Kristo alipowakaribia aliwapa mafunuo ya Patakatifu kama fungu la Daniel 8:14 linavyopasa kufafanuliwa! Mafunuo ya Edson yalisomwa, yalichunguzwa na kukaguliwa upya tena na tena. Kutoka kwake na kwa wakati sahihi, lilianza, vuguvugu kubwa jipya la kidini duniani kote—Kanisa la Waadventista Wasabato.

*Vidokezo:*

*1. Ellen G, White, The Desire of Ages (Mountain View, Calif.: Pacific Press Publishing Association, 1898, 1940), p. 776*

*2. Tazama T. Housel Jemison, A Prophet among You (Mountain View, Calif.: Pacific Press Publishing Association, 1955), uk. 485-489.*

## SURA YA 7
## "KLEOPA KATIKA SHAMBA LA MAHINDI "

"Baba, Je, naweza kubatizwa usiku wa leo? Tafadhali naomba kubatizwa" "Tayari muda umeenda sana, unajua, Ophelia, na tuna maili kumi na mbili ya kupanda katika gari la theluji lililo wazi kabla hatujafika mahali pa kulala!" Alijibu babaye. "Najua, Baba; lakini ningependa sana kubatizwa kabla hatujarudi nyumbani." "Je,

unatambua kwamba maji ya ziwa pengine yameganda kuzunguka kingo, na kwamba itatupasa kusafiri maili mbili au tatu kwenye baridi kali kwenda huko na kurudi?" "Ndiyo; lakini ni sawa," msichana alijibu. "Naweza kuvumilia." Alipoona azimio lake, mchungaji aliyepo katika kundi alimgeukia rafiki yake na kumwuliza, "Mzee, je, ungependa kwenda ziwani pamoja na Ophelia na baba yake na kumbatiza?" “Ningefurahi kufanya hivyo,” yule mtu mwema akajibu. Na hapo Hiram Edson aliongozana na binti yake mwenye umri wa miaka kumi na miwili hapo kwenye maji ya barafu, akashuhudia ubatizo wake gizani, na alifika nyumbani saa moja jioni sana, hakika,akiwa na baridi kali, lakini akiwa na furaha sana katika Bwana.

Tukio hili, lililotokea mwishoni mwa uamsho mwaka wa 1855, miaka kumi na moja baada ya kukatishwa tamaa kukuu, jambo hili linamtambulisha Hiram Edson kwetu kama baba Mkristo mwaminifu. Kwa ujumla alikuwa na watoto sita, akiwemo mmoja aliyekufa akiwa mtoto mchanga. Katika uamsho huo huo Edson aliwekewa mikono kama mzee wa kanisa wa eneo hilo—akitambulishwa kwetu kama mlei wa Kikristo mwenye bidii. Kwa miaka mingi baada ya kukatishwa tamaa kukuu, kwa kadiri afya yake ilivyoruhusu, Edson alichunguza Kweli mpya, akajidhabihu kuichapisha Kweli hiyo, na kusafiri kuieneza.

Mapema miaka ya 1850 aliandamana na Joseph Bates, John Andrews, John Loughborough, na idadi ya wachungaji wengine, wakitafuta waumini watarajiwa, waliovutiwa na mafundisho bila kuchoka, mara nyingi wakisafiri mamia ya maili, mara kwa mara kwa miguu, kwa kawaida wakati wa majira ya baridi kali. Majira ya joto alilima ili kujikimu katika gharama za maisha. Mara mbili aliuza shamba, mara moja kundi la kondoo, kusaidia kazi hiyo. Alipozeeka, alitunukiwa sifa za kuwekewa mikono, kama mchungaji katika kazi ya Bwana. Alikufa mwaka wa 1882.

Lakini kabla ya kwenda mbele zaidi, hebu tueleze maisha yake ya nyuma. Mke wa kwanza wa Edson alikufa mnamo 1839, alipokuwa na umri wa miaka thelathini na mbili. Ili kuwaandalia watoto wake wadogo watatu mama mpya, alioa upesi na kumleta mke mwingine kwenye shamba lake karibu na Port Gibson, New York (Kwenye Mfereji wa ziwa Erie). Mnamo 1843 ujumbe wa marejeo ya Bwana kwa mara ya pili ulifika Rochester, umbali wa maili thelathini.

Punde habari ikaenea hadi Port Gibson. Edson, ambaye kwa wakati huo alikuwa Mmethodisti, alikubali ujumbe wa marejeo wakati wa mfululizo wa mahubiri hayo. Usiku ule ule ambao mfululizo huu ulihitimishwa, Edson alifurahishwa na sauti iliyosikika kwa uwazi masikioni mwake, ikimwambia aende nyumbani kwa jirani aliyekuwa mahututi na kumponya kwa Jina la Bwana. Hilo lilimsumbua, kwa kuwa alifikiri kwamba miujiza ya uponyaji iliishia katika nyakati za Biblia.

Hata hivyo, hakuweza kutengua usadikisho huo, hivyo aliingia nyumbani kwa rafiki yake usiku sana. Edson alisogea mpaka kwenye mishumaa iliyokuwa inawaka kando ya kitanda, na akaweka mikono yake juu ya mgonjwa, na kusema, “Ndugu, Bwana Yesu anakuponya nawe umekuwa mzima. Kwa furaha kubwa ya Edson, mtu huyo aliketi mara moja, akatupa blanketi nyuma ya kitanda, kisha akainyoosha miguu yake kwenye ukingo wa kitanda, na kuzunguka chumbani mle, huku akimsifu Mungu.

Haikupita muda na watu wengine wote wa familia wakawa wamesimama, wakimsifu Mungu. Jioni hiyo hiyo Edson alisikia sauti ikimwambia, "Nenda ukaongee ile kweli [kuhusu marejeo ya pili ya Bwana] kwa majirani na wenzako." Aliona kushuhudia ni kazi ngumu zaidi kuliko kusaidia mtu kupona! Alijitahidi kwa siku nyingi. Lakini hatimaye alipojisalimisha, yeye, kama ilivyokuwa kwa mzee William Miller, aligundua kwamba Mungu angeweza kumtumia vizuri. Alitembelea nyumba kwa nyumba mchana kutwa, akasaidia kwa mikutano ya usiku, na haikuchukua muda, na akashuhudia majirani zake mia tatu au nne na watu wenzake wakimkubali Yesu na kujiunga na vuguvugu la marejeo ya Yesu mara ya pili. Akiwa ameshughulika kwa njia hiyo, yeye na familia yake walifikia siku ya Oktoba 22.

Siku hiyo ya tukio kuu la kumlaki Kristo lilipowadia, na usiku kuzidi kuingia na bila ishara yoyote na kisha saa ikazidi kuwapa tahadhari kwamba wakati unasonga bila tukio lolote, sisi tunaweza kuwa na hakika kwamba wao na marafiki waliokuwa wamejiunga nao katika tukio hilo walipitia upya ushahidi wa imani yao: zile siku 2300 kuanzia msimu wa kupukutisha majani wa 457 KK hadi msimu wa kupukutisha majali wa 1844 BK; uamsho wa ujio wa Yesu mara ya pili kama utimilifu wa jumbe za malaika wa kwanza na wa pili; "muda wa kusubiri na Kukawia" baada ya kukatishwa tamaa kwa majira ya kuchipua, na "kilio cha usiku wa manane" kwenye mkutano wa kambi mwezi Agosti; na hasa baada ya kupata maelezo yaliyo wazi ya Samwel Snow ya kutakaswa kwa Patakatifu katika nuru ya Siku ya Upatanisho.

Leo, walijiambia, Oktoba 22, “siku ya kumi ya mwezi wa saba,” Yesu alikuwa akimaliza kazi Yake ya mwisho ya upatanisho katika Patakatifu pa Patakatifu pa mbinguni na bila shaka bado angeondoka mahali hapo na kuja duniani kubariki watu Wake wanaomsubiri. “Tulitazamia kwa uhakika kumwona Yesu Kristo na malaika wote watakatifu pamoja Naye,” Edson aliandika baadaye, “na kwamba sauti Yake ingewaita Ibrahamu, Isaka, na Yakobo, na watu wote wa kale wenye kustahili, na marafiki wa karibu na wapendwa ambao walikuwa wamechukuliwa kutoka kwetu na kifo ….... Matarajio yetu yaliinuliwa juu, na hivyo tukamtazamia Bwana wetu ajaye hadi saa sita usiku ikafika."

Wakati kengele ya saa ilipokuwa ikilia ilipofika saa sita ya usiku, familia ya Edson na marafiki, kama ilivyokuwa kwa Wafuasi wa Miller kila mahali, walihesabu mapigo ya moyo sasa, ya ile mioyo ya watu iliyokuwa ikizama kwa kasi kwa kukatishwa tamaa.

Wakati ambapo hakuna sauti yoyote ambayo ingeweza kusikika ila mdundo wa kutatanisha na ile saa,iliyokuwa inatoa sauti ya tiktok, tiktok,ndipo walibaini kwamba sasa "siku ilikuwa imepita" na Yesu hakuwa amerudi, hivyo "kukata tamaa kwao kukawa hakika." Edson alisema, "Matumaini yetu na matarajio yetu yalipasuka-pasuka, na roho ya kulia machozi ikatujia, ambayo sikuwahi kuiona hapo awali…. Tulilia, na kulia, mpaka kupambazuka." Lakini saa zilivyozidi kwenda, Edson alijikuta akili yake ikipitia njia ambazo Mungu alimbariki tangu alipokubali tumaini la marejeo ya pili. Alikuwa amepewa uwezo wa kuponya katika Jina la Kristo; alikuwa ameona mamia ya maisha yamebadilishwa na kuwa bora; alikuwa amefurahia amani ya ajabu. Na ujasiri wake ulianza kurudi.

“Twendeni ghalani,” aliwaambia wale watu waliokuwa bado nyumbani mwake. Na katika anga la kijivu na kijibaridi cha mwisho wa Oktoba alfajiri, kundi la watu wa kawaida, wakiwa wamechanganyikiwa lakini bado wakiwa wanajitahidi kuamini, waliingia kwenye ghala, na wakafunga mlango, na kupiga magoti ili kuomba. “Tuliendelea katika maombi ya bidii hadi ushahidi wa Roho ulitolewa kwamba maombi yetu yamekubaliwa, na kwamba nuru itatolewa, na kukatishwa tamaa kwetu kufafanuliwe, na kufanywa wazi hadi turidhishwe mioyo yetu.”

Hakuna maelezo yaliyokuja wakati huo tu; lakini uhakika ulizuka mioyoni mwao ya kwamba Mungu ni pendo, na ya kwamba ingawa hawakuelewa kilichotokea, Yeye angekiweka wazi siku moja. Wakiwa wamejisikia vizuri mioyoni mwao, walirudi jikoni na kupata kifungua kinywa. Edson alipendekeza kwa mmoja wa marafiki zake wa karibu na aliyekuwa na uhakika naye, O. R. L. Crosier, kwamba watembelee baadhi ya majirani, ambao kwa sasa wamekuwa wafuasi wa Miller ambao walikuwa wamewasaidia kumpata Kristo, ili waweze kuwatia moyo katika usadikisho wao mpya. Labda ili kuokoa muda walichukua njia ya mkato kuvuka shamba la mahindi yaliyosimama. “Kwa mshtuko, nilipokuwa nikipita kwenye shamba la mahindi,” Edson anatuambia, "Nilisimamishwa nilipokuwa karibu na katikati ya shamba.

Mbingu ilionekana wazi mawazoni mwangu, na pia nikaona waziwazi na kwa uwazi, kwamba badala ya Kuhani wetu Mkuu kutoka Patakatifu pa Patakatifu pa mbinguni na kisha kuja duniani (tarehe 22 Oktoba], ….. kwamba kwa mara ya kwanza aliingia siku hiyo chumba cha pili cha Patakatifu pale; na kwamba alikuwa na kazi ya kufanya katika Patakatifu pa Patakatifu kabla ya kuja hapa duniani." Jambo sahili sana; lakini ni kati ya matukio ya ajabu sana katika historia ya kidini. Ibrahimu alikuwa mchungaji wa ng'ombe tu, ambaye alihamahama wakati Mungu alipomwita kuwa baba wa watu Wake wateule. Danieli alipokea wito wake wa pekee kama kijana mateka katika nchi ya kigeni.

Yesu alikuwa Rabi msafiri katika jimbo la mbali la Kirumi pale kifo Chake kiliokoa ulimwengu, Kleopa alikuwa mfuasi asiyejulikana wakati Kristo alipompa mafunuo ya

Biblia ambayo yaliongoza kwenye msingi wa kanisa la Kikristo na Hiram Edson, ambaye ni “Kleopas” wa Wanamarejeo, alikuwa mkulima wa jimbo la New York—na Mwinjilisti mlei aliyejitoa kusoma Biblia, na kuongoa roho—wakati Mungu alipompa ufahamu wa huduma ya mbinguni ya Kristo ambayo ilikuwa mpya kabisa katika historia ya theolojia. Kwa maana ya pekee sana Kanisa la Waadventista Wasabato lilizaliwa wakati huo, na katika shamba hilo, wakati mkulima huyo alipomtafakari Kristo.

*Vidokezo:*

*1.Review and Herald, December 27, 1855, p. 101; J. N. Loughborough to Elder H. M. Kelley, December 23, 1919, p. 1*

*2. The chapters on Hiram Edson are based in part on an undated, untitled manuscript fragment by Hiram Edson deposited in the Heritage Room, James White Library, Andrews University, and in part on other materials collected and analyzed in James Nix, "The Life and Work of Hiram Edson" (research paper, Andrews University, 1971)*

*3. P. Z. Kinne to F. E. Bowen, January 21, 1930, in W. A. Spicer, Pioneer Days of the Advent Movement (Washington, D.C.: Review and Herald Publishing Association, 1941), pp. 219, 220*

# SURA YA 8
# NURU MPYA KUTOKA KWA NENO LA MUNGU

Uadventista wa Wasabato kimsingi ni ujumbe kuhusu Yesu, kuhusu kile anachofanya sasa kuwapa wanaume na wanawake, wavulana na wasichana uhuru kutoka kwenye dhambi na kuwageuza kuwa waangavu, wakarimu, na watu wa kujali wengine kama Yeye. Wakristo wote wa Biblia wanaamini kwamba Yesu alikufa kwa ajili ya wenye dhambi msalabani na kwamba tangu kufufuka Kwake "Yeye Yu hai sikuzote ili kuwaombea" (Waebrania 7:25). Wanatheolojia wengi, hata pale ambapo wamefikiria jambo hilo kwa umahususi mdogo, kawaida wamekuwa wakidhania kwamba siku zote Yeye ameendelea na maombezi haya katika Patakatifu pa Patakatifu pa mbinguni.

Waadventista Wasabato, hata hivyo, wanaamini kwamba baada ya kupaa Kwake, Masihi alianza kazi Yake ya maombezi katika Patakatifu, eneo la kwanza la Patakatifu pa mbinguni, na kwamba ni mwaka 1844 tu ndipo Aliposogea mbele hadi katika eneo la pili, la ndani, lililo takatifu zaidi.  Tofauti hii kwa vyovyote haiko kwenye jiografia. Sivyo kabisa! Ijapokuwa huduma ya Kristo ya ukuhani mkuu katika Patakatifu pa mbinguni ilikuwa ya ajabu sana siku zote, kazi yake mpya ya pekee katika Patakatifu pa Patakatifu sana, inaipita kwa mbali kazi hiyo iliyotangulia, katika katika kubadilisha neema na nguvu. Tutatoa sura kadhaa kwaajili ya mada hii sasa na tutairejelea mara nyingi katika kitabu hiki. Kleopa na mwenzake walipokuwa wakienda mashambani, Yesu aliwakemea kwa kutoamini “yote” ambayo manabii walikuwa wamezungumza kumhusu Yeye (Luka 24:25 )

Wanafunzi na Wafuasi wa Miller vilevile, ingawa walisifiwa sana kwa kugundua zile Kweli kuhusu Kristo ambazo watu wengi walizipinga au kuzipuuza, hata hivyo walipuuza au hawakuelewa Aya ambazo zilikuwa zimesimama kwa karne nyingi Katika Maandiko Matakatifu. Kweli hii maalum kuhusu Kristo ambayo Hiram Edson na wengine vivyo hivyo waligundua, ilibaki katika Biblia bila kugunduliwa kwa muda mrefu.

Kila Mkristo anawiwa kuelewa jambo hili. Je, Hiram Edson,  alikuwa na maono ya kinabii katika shamba la nafaka, kama wengine wanavyodai? Jambo hili linaweza kuwa kweli kabisa. Hata hivyo, hasemi kwamba alimwona Yesu akiingia Patakatifu pa Patakatifu. Badala yake, katika maelezo yake yanayojulikana zaidi, anasema kwamba aliona "kwamba" Yesu aliingia Patakatifu pa Patakatifu mnamo Oktoba 22.

Katika maelezo tofauti hasemi chochote kuhusu "kuona" chochote, lakini badala yake anakumbuka kwamba alisikia sauti ikisema naye. Labda yeye mwenyewe hakujua jinsi ufahamu huu wa thamani ulivyomjia, lakini kujaribu kuthibitisha kile

kilichotokea sio lazima. Jambo la maana ni kwamba alijifunza jambo ambalo sisi pia tunaweza kujifunza kutoka katika Biblia (kutoka kwako na kwangu, na kwake pia).

Hebu tunukuu kidogo zaidi yale anayosema kisha tuyachambue. "Niliona ..... kwamba [Kristo] alikuja kwenye arusi wakati huo [Oktoba 22, 1844]; kwa maneno mengine, kwa Mzee wa siku, kupokea ufalme, mamlaka, na utukufu; na lazima tungojee kurejea Kwake kutoka arusini; na akili yangu ilielekezwa kwenye sura ya kumi ya Ufunuo ambapo niliweza kuona ono lile lililokuwa limesema na wala halikusema uongo; tulikuwa tumekula kitabu kile kidogo na kilikuwa kitamu vinywani mwetu, na sasa kilikuwa kichungu tumboni mwetu, kikileta uchungu mwilini mwetu mwote, Kwamba ni lazima tutoe unabii tena, n.k., na kwamba malaika wa saba alipoanza kupiga baragumu, hekalu la Mungu lilifunguliwa mbinguni, ikaonekana katika hekalu Lake sanduku la agano Lake, n.k."

Wakati Wamiller/Wamila waliposoma Danieli 8:14 ("Hata siku elfu mbili na mia tatu; ndipo Patakatifu patakapotakaswa"), walidhani kwamba Patakatifu palikuwa duniani na kwamba unabii wa muda mrefu kama zile siku 2300 ulifikia hadi mwisho wa dunia. Katika 2 Timotheo 4:1 Kristo "atawahukumu walio hai na waliokufa kwa kufunuliwa Kwake," na walidhani kwamba hukumu hii katika ujio wa pili ndiyo hukumu pekee ambayo itatokea, Kisha wakageukia Danieli 7:10-13 na kusoma kimakosa, "Hukumu iliwekwa... Mmoja kama Mwana wa Adamu alikuja na mawingu ya mbinguni [duniani]." Hata hivyo, Katika shamba la nafaka, Edson ghafla alitambua kwamba Danieli 7:13 haisemi, "dunia" bali "kwa Mzee wa siku"!

Ingawa hukumu hakika itatokea wakati Kristo atakapokuja duniani (2 Timotheo 4:1), Biblia inatabiri hapa hukumu nyingine itakayotukia kabla ya ule mwisho, ambapo Yesu, baada ya kuja kwa Baba juu ya mawingu ya mbinguni, anapokea. "utawala, na utukufu, na ufalme." Hii ni muhimu sana na tutajifunza tena katika sura inayofuata. Wamiller walikazia sana fikira zao kwenye mfano wa Kristo (katika Mathayo 25) wa wanawali kumi wanaongoja bwana arusi aje kwenye arusi, kiasi kwamba walipitiwa na hivyo hawakuona mfano mwingine wa harusi ya Kristo katika Luka 12.

"Wakati wa kungojea" baada ya kukatishwa tamaa wakati wa majira ya kuchipua, "kilio cha usiku wa manane" mnamo Agosti, na "wakatayarisha utambi wa taa zao kwa kutoa masinzi" wakati wa harakati ya kiroho ya mwezi wa saba ikiendelea, wote walifanana, na mfano huu wa mabikira ni wa kusadikisha sana kiasi kwamba bila shaka waliamini Bwana—arusi angekuja Oktoba 22. Naye alikuja—lakini si duniani. Alikuja kwenye arusi, kama mfano ulivyosema angefanya. Alikuja juu ya mawingu kwa Baba ili kupokea ufalme Wake, yaani "kuuoa." (Ni nahau ya zamani ya Biblia) Edson akiwa huko nje kwenye shamba la nafaka, na huku pumzi yake ya msisimko ikitoa mvuke katika hewa yenye baridi kali, alielekeza akili yake kwenye maneno ya Kristo katika Luka 12:35, 36: "Viuno vyenu na viwe vimefungwa na taa zenu

zinawaka; nanyi iweni kama watu wanaomngojea Bwana wao atakaporudi kutoka arusini." Edson alistaajabu sana hata alipoandika maelezo haya, alisisitiza maneno, "aliporudi kutoka harusini." Mtu anaweza kupiga picha ya Edson akipaza sauti kwa haki shambani!, "Tunapaswa kungoja hadi Yesu arudi kutoka arusini! Harusi ni ndoa ya Kristo na bibi-arusi Wake Yerusalemu mpya, mji mkuu wa ufalme wake mpya (Ufunuo 21).

Mnamo Oktoba 22 tulikuwa tunapaswa kuingia naye arusini kwa imani, Arusi itakapokwisha, ndipo atakapokuja kutupeleka kwenye karamu ya arusi (Ufunuo 19). Wao hawakuliona hilo, bila shaka, nao walikatishwa tamaa; lakini tamaa kubwa yenyewe ilikuwa uthibitisho kwamba walikuwa kwenye njia! Biblia inasema hivyo katika Ufunuo 10, kifungu ambacho usikivu wa Edson ulivutwa baadaye. Katika Ufunuo 10 malaika mwenye nguvu anasimama juu ya nchi kavu na baharini, akiashiria harakati ya kinabii duniani kote. Kwa mkono mmoja anashikilia "kitabu kidogo ambacho kinaonekana wazi"; na mkono mwingine anauinua mbinguni, na anaapa kwamba "hapatakuwa na wakati tena." Kama inavyopaswa kuwa, Wamiller walikiona kile kitabu kidogo kama ishara ya unabii wa wakati wa kitabu cha Danieli ambao haukuwa umeeleweka vya kutosha ("Na kwamba umefungwa"; Angalia Danieli 12) hadi siku yao wenyewe, lakini ambao wakati wa ufufuo mkuu wa marejeo ya pili ulitangazwa na harakati ya kinabii katika mabara yote.

Katika sehemu ya kwanza ya Ufunuo 10:10, Yohana anasema kwamba katika maono yake “Nikakitwaa kile kitabu kidogo katika mkono wa yule malaika, nikakila; nacho kilikuwa kitamu kinywani mwangu kama asali." Kwa uwazi hii ilifananishwa na shangwe ya Wanamarejeo walipokuwa wakingojea marejeo ya pili ya Mfalme. "Wako katika tumaini lenye baraka," walitia sahihi barua zao. "Mwaka wa furaha zaidi wa maisha yangu," alikumbuka Ellen White. Katika furaha yao walishindwa kuelewa maneno yaliyofuata: "Na mara tu nilipokula, tumbo langu lilikuwa chungu," Lakini asubuhi iliyofuata Oktoba 22, Maneno haya hayakuwa tena magumu kueleweka.

Edson aliandika, "Hakika mimi niliweza kuona ono ambalo lilikuwa limezungumzwa na sikusema uongo; ... tulikuwa tumekula kile kitabu kidogo; kilikuwa kitamu kinywani mwetu, na sasa kimekuwa uchungu tumboni mwetu, na kuutia uchungu miili yetu wote." Je, hili tukio la kukatishwa tamaa kukubwa kwa Oktoba 22, 1844, lilikuwa limetabiriwa mapema karibu Miaka 2000? Ndiyo, lilitumika kuthibitisha kuwa utimizo wa Kweli wa unabii Baada ya maneno kuhusu tumbo kuwa chungu, Ufunuo 10 unamalizia kwa mstari huu: “Imempasa kutabiri tena mbele ya watu wengi, na mataifa, na lugha, na wafalme." Hapa palikuwa na tamko ambalo hata Edson hakuwa tayari kulimeza!

Hakika, Waadventista wasingelielewa kikamilifu jambo hili kwa miaka mingi. Lakini kwa wakati huo ilitosha kuona yale walipaswa kujua, kama Edson alivyofanya,

kwamba lazima tutoe unabii tena, nk." Vipindi vya wakati wa kinabii viliisha tarehe 22 Oktoba, lakini wakati halisi wa kuhubiri injili ungeendelea hadi siri ya Mungu ikamilike. Hatimaye, Edson anatuambia, aliona katika shamba la nafaka kwamba "malaika wa saba alipoanza kupiga baragumu, hekalu la Mungu mbinguni likafunguliwa, na Sanduku la Agano lake likaonekana." Hii inarejelea Ufunuo 11:15-19. Malaika wa saba anapopiga baragumu yake, “falme za ulimwengu huu” zinakuwa falme za Kristo. "Wakati umewadia wa wafu kuhukumiwa,” watakapo "hukumiwa." Na “hekalu la Mungu” likafunguliwa mbinguni, na “Sanduku la Agano Lake” likaonekana.

Miller na wenzake, walihusianisha haya yote kwenye hukumu katika marejeo ya pili ya Oktoba 22. Edson aliona kwamba mengi zaidi yalihusika; na sasa akaanza kustaajabu, kwa kuwa Yesu alikuwa ameingia kwa mara ya kwanza Patakatifu pa Patakatifu pa hekalu la mbinguni ambapo Amri Kumi zimehifadhiwa ndani ya Sanduku la Agano, pengine kwa ajili ya nuru mpya ambayo ingetokea upesi kuhusu utunzaji wa amri zote. Ikiwa wazo jipya lilikuwa linaletwa, lakini haikuwa wazi kwake Edson wakati huo. Muda wote huo, Edson akiwa amesimama kwenye shamba la mahindi huku akisisimka sana juu ya ule uelewa wake mpya wa Biblia alioupata, rafiki waliyeandamana naye alikuwa akitembea huku akiwa amezama katika mawazo yake ya kina, hata hakugundua kwamba yuko peke yake. Mara moja akasimama, akageuka akauliza swali kwa kusema kwa sauti, "Hiramu, kwa nini unasimama hapa kwa muda mrefu?" Edson alijibu, "Bwana anajibu maombi yetu ya asubuhi, akitoa mwanga kuhusiana na kukatishwa tamaa kwetu."

## SURA YA 9
## "TAZAMA JUU ZAIDI KIDOGO"

"Nilipokuwa nikiomba kwenye madhabahu ya familia, Roho Mtakatifu aliniangukia na nilionekana nikipanda juu na juu, mbali sana na ulimwengu wa giza. Niligeuka kuwatafuta Wanamarejeo, watu waliokuwa wanangojea marejeo ya Masihi kwa mara ya pili ulimwenguni, lakini sikuweza kuwapata au kuwaona, wakati sauti iliponiambia, “Angalia tena, na utazame juu kidogo.”

Haikuwa kwa Hiram Edson pekee kwamba Kristo alileta nuru mpya baada ya kukatishwa tamaa. Kufuatia kusulubishwa na kufufuka Kwake Yesu alionekana sio tu kwa Kleopa na mwenzake kwenye barabara kuelekea vijijini huko mashambani, bali pia kwa Mariamu bustanini, kwa wanafunzi kumi na mmoja wakati wa chakula cha jioni, kwa waumini 500 huko Galilaya, kwa Paulo katika maono, na kwa wengine. Vivyo hivyo, baada ya Oktoba 22 Alileta nuru mpya kwa Edson katika shamba la mahindi, kwa Joseph Turner katika utulivu wa chumba chake cha kujisomea, na kwa Ellen Harmon katika maono ya kinabii. Joseph Turner alihariri jarida la Wamiller. Kufikia tarehe 15 Desemba 1844 yeye pia alikuja kuona kwamba watakatifu lazima wangoje hadi Bwana-arusi atakaporudi kutoka arusini. Yeye na Apolo Hale, Mwanamarejeo mwingine mashuhuri, walichapisha haraka nuru yao katika jarida la The Advent Mirror.

Ellen Harmon alilelewa huko Gorham na Portland, Maine. Baba yake, Robert Harmon, mshona kofia, na mama yake, Eunice, walikuwa watu wa kawaida katika Kanisa la Maaskofu la Methodisti. "Walikuwa na furaha ya kuwaona watoto wao, wanane kwa idadi, wote wameongoka na kukusanywa katika zizi la Kristo." Akiwa mwanafunzi wa shule ya msingi, Ellen alijeruhiwa katika ajali isiyo ya kawaida usoni mwake, iliyosababishwa na msichana mmoja, alipomrushia jiwe. Ajali hii ilisababisha umwagaji mwingi wa damu wakati huo na uharibifu wa kudumu katika mfumo wake wa kupumua. Kwa kukosekana kwa huduma za kisasa za matibabu, hali yake ilidhoofika sana, na kwa miaka mingi maambukizi yoyote ya kawaida kabisa, yangeweza kusababisha shida. Wakati nguvu na ujasiri wake haukuweza kustahimili tena kuendelea masomo, aliacha shule kwa huzuni.

Alipokuwa na umri wa miaka kumi na miwili, familia yake ilimsikia William Miller akihubiri na kukubali ujumbe wake. Alipotoa wito wa kujitoa kwa Kristo, Ellen

akaenda mbele; lakini akihisi kwa ukali sana hali yake ya dhambi, hakuwa na hisia kwamba ameokolewa. Katika mkutano wa makambi ya Kimethodisti katika majira ya joto yaliyofuatia alisali kwa bidii sana kiasi kwamba alihisi mzigo wake wa hatia ukiondolewa kwa ghafla kiasi, naye akajisikia kana kwamba dhamira inamshtaki! Kisha taratibu hisia tamu za kukubaliwa na Bwana zililimjia na kuchukua nafasi yake. Upesi yeye na wengine kadhaa walibatizwa karibu na Portland kwenye Ghuba ya Casco. Alijaribu tena kupata elimu kwa kuhudhuria shule ya wasichana ya eneo hilo, lakini kwa mara nyingine tena ilimbidi kujiondoa shuleni. Miller alirudi Portland.

Ellen alimwona mzee Millerakisimama katika mahubiri yake ili kuwakaribisha wazee kwenye viti vya mkusanyiko uliokuwa na watu wengi. Alimpenda kwa matendo yake; naye alivutiwa sana na mahubiri yake yaliyokita kwenye Biblia, ya dhati na yenye ari. Lakini shangwe yake kuhusu kuja mara ya pili kwa Yesu iliharibiwa upesi na mahubiri ya moto wa mateso ya Jehanamu, kutoka kwa mhudumu asiyekuwa Mwadventista ambaye alimfanya Mungu kuwa mkatili sana kiasi kwamba mashaka yake yakamrudia. Alikesha usiku kucha, akiomba rehema. Mama yake alimpeleka kwa Mzee Stockman.

Mzee Levi Stockman, mchungaji mchanga wa Kimethodisti ambaye, kama akina Harmons, alikuwa amekubali tumaini la marejeo ya Yesu, alimwambia Ellen kwamba Mungu si dhalimu bali ni Baba wa mbinguni Mwenye upendo ambaye anatamani kuwavuta watoto Wake karibu Naye kwa imani rahisi/sahili ya kumtumaini na kumtegemea Yeye. "Nenda jisikie huru, Ellen," alisema. "Mungu anakupenda!" Pia alisema kwamba Mungu lazima ana mpango wa pekee sana katika mapenzi Yake, kwa ajili yako, akitaka kukuza katika binti mchanga kiasi hiki uzoefu wa huu wa kidini. Alimwombea, na Ellen akaondoka akiwa msichana mwenye furaha zaidi. Akiwa na usadikisho kwamba muda mfupi tu ulisalia kabla ya kuja kwa Yesu mara ya pili, Ellen alijitahidi sana kuboresha huduma ya kuleta roho kwa Mungu, na akasaidia wongofu wa wengi wa wale aliofanya nao kazi ngumu ya injili.

Muda wote uliosalia wa maisha yake marefu alikumbuka kwa vyema kabisa yale majuma yaliyotangulia Oktoba 22, 1844. "Kwa kuchunguza moyo wake kwa bidii" na kufanya maungamo ya unyenyekevu, tulifikia wakati wa kutazamia marejeo ya Bwana kwa sala. Kila asubuhi tulihisi kwamba ilikuwa kazi yetu ya kwanza kupata uthibitisho kwamba maisha yetu yalikuwa sawa na Mungu ... Tuliomba pamoja na kuombeana sisi kwa sisi ...

Furaha ya wokovu ilikuwa muhimu zaidi kwetu kuliko chakula na vinywaji vyetu. Yesu alipoacha kutokea tarehe 22 Oktoba, familia ya Ellen ilivunjwa moyo kama wengine. Kati ya watoto wanane wa Harmon, ni wanne tu wa mwisho ndio waliokuwa bado nyumbani: Sarah, mwenye umri wa miaka 22; Robert, 18; na Ellen

na dada yake pacha, Elizabeth, wote wawili walikuwa na umri wa miaka 16. Kati ya wale waliokuwa wameondoka, ni dada wawili walioolewa, ambao walikwenda kuishi Poland, Maine, yapata maili 30 kutoka hapo. Robert na Elizabeth hivi karibuni walikuwa wamekatishwa tamaa kuhusiana na ujio wa pili wa Kristo, ingawa Robert aliirudia imani yake baada ya miaka michache, na inaonekana kwamba, huenda Elizabeth alikufa akiwa Mkristo. Lakini wakati wa Novemba na mapema Desemba 1844, Ellen, Sarah, na wazazi wao waliishi siku baada ya siku wakiwa na tumaini, ila imani ilikuwa ikipungua siku kwa siku, kuhusu kurejea kwa Yesu upesi.

Katika hali hii ya akili Ellen, sasa akiwa na umri wa miaka kumi na saba (siku ya kuzaliwa kwake ilikuwa Novemba 26), alienda kwa gari la farasi mnamo Desemba kumtembelea Bi. Haynes, rafiki yake. Asubuhi moja kikundi kidogo cha wanawake wengine wa Kiadventista walijiunga nao katika maombi—kwa ajili ya kupata nuru, bila shaka, juu ya kukatishwa tamaa kwao, na kwa rehema kwa wapendwa wao ambao imani yao haikuwa na nguvu tena. Walipopiga magoti, Roho Mtakatifu alisogea karibu kwa hali ya kusadiki kabisa.

Wakati huo, Ellen alipata maono yake ya kwanza.  Maono yalipoisha, aliwaambia wanawake aliokuwa nao jinsi alivyowatafuta Waadventista ulimwenguni kwa bidii katika maono, na kisha asiwaone, ndipo malaika alipomwambia, "Angalia tena, na utazame juu kidogo." Hapo, ndipo aliona njia, juu ya dunia, ambayo waumini walikuwa wakisafiri kuelekea Mji Mtakatifu. Watu, njia, na jiji, hata hivyo, vilikuwa vielelezo tu vya ujumbe halisi ambao maono hayo yalikusudiwa kuwasilisha. Kwa usikivu na shukrani, Ellen alivutiwa na "mwanga mkali uliowekwa nyuma yao mwanzoni mwa njia, ambayo malaika aliniambia kuwa ni kilio cha usiku wa manane."

Hili lilikuwa jibu la maombi yao! Mbingu zilisema kwamba kilio cha usiku wa manane - tangazo la kuja kwa Bwana-arusi mnamo Oktoba 22 - ilikuwa nuru, nuru ya Kweli. Hakuna maelezo ya kukatishwa tamaa kulikotokea yaliyotolewa, lakini hapa palikuwa na  uhakikisho kwa kweli! Nuru iliwekwa "mwanzoni mwa njia." Hili lilikuwa wazo jipya. Walitumaini kilio cha usiku wa manane kingeashiria mwisho wa njia. Ni dhahiri Mungu alitarajia wafuasi Wake kusafiri njia mpya ya uzoefu na huduma. Nuru "iliangaza njiani kote na kutoa mwanga kwenye miguu yao njiani ili wasijikwae." Lakini haikuwa chanzo chao pekee cha mwanga. Daima Yesu alikuwa mbele yao tu, akiwaongoza hadi mjini, na kuwatia moyo kwa nuru kutoka kwa "mkono Wake wa kuume wa utukufu."

Kwa kusikitisha, Ellen aliona kwamba baadhi ya Wanamarejeo "waliikataa kwa ujinga nuru iliyokuwa nyuma yao na kusema kwamba si Mungu aliyewaongoza kutoka awali, walipokuwa hawamjui, hadi sasa." Nuru iliyokuwa nyuma ya watu hawa, waliosema kwamba zile siku 2300 hazikuwa na maana na kwamba Oktoba 22 ilikuwa

ni kosa, ilizimika, na miguu yao ikaachwa katika giza totoro, nao “wakajikwaa, wakakosa kuiona ile alama na wakashindwa kumtazama Yesu, na wakaanguka kutoka kwenye njia chini katika ulimwengu wa giza." Kabla ya maono kufungwa, Ellen alikuwa na mambo mengine ya kushangaza ya kuwaambia wanawake aliokutana nao.

Mzee Stockman, kama Mzee Charles Fitch, alikufa wakati fulani kabla ya Oktoba 22. Karibu na mwisho wa maono alioneshwa kwamba wakati wa marejeo ya Yesu utakapotukia hatimaye, wote wawili watachukuliwa kwenda mbinguni. Hii pia ilikuwa habari njema, na ilitoa uthibitisho wa ziada kwamba Mungu alikuwa pamoja na harakati ya ujio wa Yesu mara ya pili. Wiki moja baada ya maono haya ya kwanza ya furaha, Ellen alipokea maono mengine ambapo Mungu alimwita rasmi kumfanyia kazi kama nabii. Alimwonya juu ya dhabihu kuu ambayo ingehusisha kazi hii, na pia aliahidi wingi wa neema Yake. Ellen alijikunja kwa hofu.

Akiwa mgonjwa sana kiasi kwamba hangeweza kutembea kuvuka toka upande mmoja wa chumba mpaka mwingine au kuzungumza kwa sauti zaidi ya kunong'ona, alifurahi kutoa kila kitu, hata kile kilichobakia mwishoni, ili kuokoa wale waliopotea, lakini aliogopa upinzani na kuwakilishwa isivyo. Mkutano wa waumini Wanamarejeo ulipangwa ufanyike nyumbani kwake. Kwa kuwa hakutaka kukabiliana nao, alitoroka kwa gari la kuteleza kwenye theluji (snowmobile) hadi kwenye nyumba ya jirani. Lakini baada ya muda kidogo alijisalimisha. Katika ibada ya maombi, nuru inayoonekana kwa macho, ilimulika. Alitoa ushuhuda wake kwa Wanamarejeo wa Portland na mwishowe akasikia takriban watu sitini kukiri kwamba walikuwa wameacha imani katika “kilio cha usiku wa manane” lakini sasa walikuwa wamesadikishwa tena kwamba kilio hiki kilitoka kwa Mungu.

Muda mfupi baadaye, alipokuwa akimtembelea dadake Mary, aliwasilisha maono yake kwa kikundi cha Waadventista katika kilima cha MacGuire, karibu na Poland. Alianza kwa kunong'ona, ila Mungu alimpa sauti yenye nguvu kwa karibu saa mbili. Alipomaliza na watu wakamwuliza maswali baada ya mkutano, akarudia kunong'ona tena. Akiwa bado mgonjwa sana hata asiweze kusoma, Ellen alitoka katikati ya majira ya baridi kali ya New England kuwatembelea Waadventista wengine walioishi "mashariki" kando ya pwani ya Maine.

Katika mkusanyiko mdogo huko Exeter, Maine, alikuwa na maono ya umuhimu wa kipekee. “Niliona kiti cha enzi,” aliwaambia watu wakati mkutano ulipoisha,” na juu yake aliketi Baba na Mwana. Hadi wakati huu alikuwa amejua tu kwamba Oktoba 22, 1844 ilikuwa siku muhimu sana; ila hakujua ni kwa sababu gani. Sasa alionyeshwa ndani ya Patakatifu pa mbinguni. Alipokuwa akitazama, "alimwona Baba akiinuka kutoka kwenye kiti cha enzi, na katika gari la moto akiingia ndani ya Patakatifu pa Patakatifu, na kuketi." Yesu, pia, alitoka kwenye kiti cha enzi.

Na alipokuwa akifanya hivyo, aliinua mkono Wake na kuwaambia wafuasi Wake waliowakilishwa kama wamwabuduo pale, “Ngojeni hapa; naenda kwa Baba yangu ili niupate ufalme; tunzeni mavazi yenu, yasiwe na mawaa, na bado kitambo kidogo nitarudi kutoka arusini niwakaribishe kwangu.” Akiwa amevutiwa sana, alitazama “gari la vita la mawingu, lenye magurudumu kama mwali wa moto, likizungukwa na malaika, lilipofika mahali Yesu alipokuwa. Aliingia ndani ya gari na kubebwa hadi Patakatifu pa Patakatifu, ambapo Baba aliketi.” “Hapo,” akasema Ellen, “nilimwona Yesu, Kuhani Mkuu amesimama mbele ya Baba”

Hii ilikuwa zamu ya Ellen kujifunza kuhusu Bwana-arusi akienda arusini mnamo Oktoba 22, 1844 na kurudi kutoka kwenye hiyo arusi, wakati wa kurejea mara ya pili. Lakini kwa uwazi zaidi kuliko Edson au Turner, aliona utimizo kamili wa Danieli 7:9-14. Baada ya wale “Wanyama” wanne wa Danieli 7, zile “pembe kumi” na ile “pembe ndogo” ya kutisha zimemaliza mwendo wao wa kutisha na historia inakaribia mwisho wake, Danieli aliona kwamba viti vya enzi kuu vingewekwa na yule Mzee wa Siku angekuja achukue kiti Chake. "Hukumu ikawekwa, na vitabu vikafunguliwa." Kisha “mmoja aliye mfano wa Mwanadamu” angekuja “pamoja na mawingu ya mbinguni” kwa Mzee wa Siku ili kupokea mamlaka na ufalme. Hivyo Biblia ilitabiri kwamba kabla ya Ujio wa Yesu mara ya Pili wakati wa hukumu utakapofika, Baba angeondoka sehemu moja ya mbinguni hadi nyingine na Mwana angemfuata huko.

Huko Exeter, Maine, Februari 1845, Ellen alionyeshwa, naye akapata mshangao haswa, kwamba unabii huu ulikuwa umetimizwa sasa. Kwa hivyo hii ndiyo sababu Oktoba 22 ilikuwa muhimu sana! Pia alipata maono ya ukuu wa hekalu na Patakatifu pa mbinguni lililokuwa Kubwa vya kutosha kwa ajili ya magari ya moto na makundi ya malaika, "hakuna muundo wa jengo la kidunia unaoweza kuwakilisha ukubwa wake." Katika majira hayo ya joto, afya yake ilikuwa imeboreka kwa kiasi fulani, yeye na dada yake Sarah walianza ziara ya miezi minane kati ya Waadventista wa Massachusetts, wakikaa baadhi ya nyakati na familia ya Otis Nichols huko Dorchester, na mara kwa mara walifanya safari za muda mfupi nyumbani kwao Portland.

Mnamo Oktoba, huko Carver, Massachusetts, alipata maono maalum ya tatu, kama nyongeza ya "Kilio cha Usiku wa manane" na maono ya "Bwana arusi.” Katika maono hayo aliona siku za mbeleni, wakati Kristo angekamilisha huduma Yake ya ukuhani katika Patakatifu pa Patakatifu na “wakati ambapo taabu ya Yakobo” ingeanza. Alikuwa hajawahi kusikia haya kabla. Wazo la kwamba wanadamu wangelazimika kuishi wakati fulani bila mpatanishi lilikuwa jambo la kusikitisha. Ellen alipokuwa akisafiri, akifuatana na dada yake Sarah, na pia wakati mwingine na watu wengine ikiwa ni pamoja na James White na ndugu yake wa karibu Louisa Foss, alihubiri

maono yake kwa kila Mwanamarejeo yeyote Mmilleri/Mmila aliyekuwa tayari kusikiliza, na kuleta ufahamu na furaha kwa wengi wao.

*Vidokezo:*

*1. Ellen G, White, Life Sketches of Ellen G. White (Mountain View, Calif.: Pacific Press Publishing Association, 1915, 1942), p. 17*

*2. Ellen G. White, Christian Experience and Teachings of Ellen G. White (Mountain View, Calif.: Pacific Press Publishing Association, 1922), p. 53*

*3. Cf. Review and Herald, April 21, 1868, p. 287*

*4. J. N. Loughborough, "A Sketch of Individual Experience" (1918), manuscript deposited in the Heritage Room, James White Library, Andrews University*

*5. Ellen G. White, Early Writings of Ellen G. White (Washington, D.C.: Review and Herald 127 Publishing Association, 1882, 1945), pp. 14, 15*

*6. James White, A Word to the "Little Flock," p. 22; idem, to Joseph Bates, July 13, 1847*

*7. Ellen G. White, Early Writings, pp. 54, 55*

*8. Ellen G. White, Patriarchs and Prophets (Mountain View, Calif.: Pacific Press Publishing Association, 1890, 1958), p. 357*

*9. Otis Nichols to William Miller, April 20, 1846, original deposited in the Orrin Roe Jenks Memorial Collection of Adventual Materials, Aurora College Library; Cf. Ellen G. White, Spiritual Gifts, 4 vols. (Battle Creek, Mich.: [vols. 1, 2] James White, 1858, 1860; [vols. 3, 4] Steam Press of the Seventh-day Adventist Publishing Association, 1864), vol. 2, pp. 67-82. See below, chapter 13, note 2*

*10. Letter from Sister Harmon, Falmouth, Mass., Feb. 15, 1846, in Day-Star, March 14, 1846, p. 7; republished with some alteration in Francis D. Nichol, Ellen G. White and Her Critics (Washington, D.C.: Review and Herald Publishing Association, 1951), pp. 625, 626 128*

## SURA YA 10
## “YESU ANAFANYA NINI SASA? "

Kwa hiyo sisi tunajua Yesu alipo sasa; Yeye Yuko katika Patakatifu pa Patakatifu pa mbinguni. Na tunajua anachofanya huko; anahudhuria 'harusi' na kushiriki katika 'hukumu' ya awali kabla ya marejeo. Lakini, kwa lugha rahisi, yote haya yanamaanisha nini kuhusu kile ambacho Yesu anafanya sasa? Edson na Crosier walikuwa wameketi kwenye meza katika shamba la Edson's Port Gibson, ambapo Crosier alifanya makazi yake kwa muda. Rafiki wa tatu alikuwa amejiunga nao, Dk. F. B Hahn wa Canandaigua, katibu wa jumuiya ya tiba ya jimbo lake.

Biblia, nakala moja au mbili za Concordance ya Crudence yaani gombo la ufafanuzi wa Biblia, na pengine machapisho fulani ya wafuasi wa Miller yalikuwa mbele ya nyuso zao. Muswada/makala ya Joseph Turner katika gazeti la The Advent Mirror ilikuwa bado ina wiki kadhaa kuchapwa katika siku zijazo, na maono ambayo Ellen alikuwa ameonyesha yangebaki bila kujulikana kwao kwa zaidi ya mwaka mmoja; hivyo wakiwa Port Gibson watu hawa watatu walitafuta jibu lao katika sehemu bora zaidi, katika Biblia zao. Watu watatu hawa walipokutana mara baada ya muda kujifunza na kuomba kwa ajili ya nuru mpya, ufahamu wao wa Patakatifu pa mbinguni ulizidi kuongezeka.

Walisadikishwa, mfano, kwamba mbinguni palikuwa ni mahali halisi, halisi kama “mji wenye misingi” (Waebrania 11:10) na halisi kama “makao mengi” ambayo Kristo amekwenda kuandaa katika nyumba ya Baba Yake (Yohana 14:1-3). Lakini somo lao liliongozwa hasa na sentensi kuu katika Waebrania 8 na 9: “Tunaye Kuhani mkuu wa namna hii, aliyeketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Ukuu mbinguni, mhudumu wa Patakatifu, na mhudumu wa Patakatifu pa ile hema ya kweli." "Kuna makuhani ... wanaotumikia kwa kielelezo na kivuli cha mambo ya mbinguni." "Maskani ya kwanza ilikuwa kielelezo." “Basi ilikuwa sharti nakala za mambo yaliyo mbinguni zisafishwe kwa hizo [dhabihu za wanyama]; bali mambo ya mbinguni yenyewe yasafishwe kwa dhabihu zilizo bora kuliko hizo. Kutokana na Aya kama hizi walikuja kutambua kwamba dhabihu ya Kristo msalabani na ukuhani Wake mbinguni vilionyeshwa kiishara katika taratibu za kaida/sherehe za Agano la Kale (Ceremonial occassions of the sanctuary sacrifice).

Walijifunza kwamba Mungu alimwagiza Musa atengeneze hema ya kukutania na huduma zake ili kuwa somo la kufundisha Kweli kuu kumhusu Yesu Kristo. Na waliona kwamba ikiwa tunataka kujua kile Yesu Kuhani wetu Mkuu anafanya katika Patakatifu pa mbinguni leo, ni muhimu kugundua kile makuhani walifanya katika Patakatifu pa Agano la Kale zamani. Hapa kulikuwa ufunguo wa hazina kubwa! Ukisoma katika kitabu cha Kutoka na Mambo ya Walawi, isingeweza kuwachukua muda mrefu kujua kwamba Patakatifu pa kidunia (au “hema la kukutania” kama lilivyoitwa mara nyingi) lilikuwa hema la kubebeka la vyumba viwili lililotumiwa na Waisraeli wakati wa safari yao ndefu kupitia jangwani, wakitokea Misri, kwenye Nchi ya Ahadi.

Kila siku, watu walipokuja kuungama dhambi zao walitoa dhabihu ya mnyama na kusamehewa. Kisha kuhani, ama moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja, alipeleka kiasi kidogo cha damu ya mnyama ndani ya chumba cha kwanza ("mahali Patakatifu"), akiiweka juu ya madhabahu ya dhahabu, ndogo na nzuri iliyokuwa pale. Kwa kufanya hivi alibeba ndani ya Patakatifu kumbukumbu ya dhambi iliyoungamwa; na kwa sababu dhambi ni najisi kwa jinis ya kutishaa, hata hii kumbukumbu ya dhambi iliyoungamwa bado ilichafua au "kunajisi" Patakatifu.

Mara moja kwa mwaka, katika Siku ya Upatanisho, kuhani mkuu alibeba damu ya dhabihu moja kwa moja hadi kwenye chumba cha pili (“mahali Patakatifu pa Patakatifu”), na kunyunyiza sehemu yake juu ya Sanduku takatifu, lililopakwa dhahabu (“Sanduku la Agano”) ambalo lilikuwa na Amri Kumi ambazo, kwa kufanya dhambi, watu walikuwa wamezivunja. Kwa Edson, Crosier, na Hahn, Siku ya Upatanisho ilionekana kuwa tukio muhimu kuliko yote.

Ilikuwa ni Siku ya Upatanisho ambayo ilikuwa imempa Samuel Snow uthibitisho wake katika mkutano wa kambi ya Exeter, New Hampshire, kwamba siku 2300 ziliisha

mnamo Oktoba 22, 1844; na ni dhahiri kabisa lilikuwa tukio tukufu na muhimu zaidi la kalenda ya kaida/sherehe za kale (ceremonial calendar). Lakini kabla hatujapata kujua walichojifunza kuhusu Siku ya Upatanisho, hebu tuangalie kwa muda neno “upatanisho” kama lenyewe. Neno hili la kuvutia linatokana na nahau upatanisho au "kuwa pamoja at-one-ment."

William Tyndale, ambaye alitafsiri Biblia katika Kiingereza, kwa gharama ya maisha yake mwanzoni mwa miaka ya 1500, alitumia "upatanisho" kwa ajili ya kurejesha mahusiano ya kirafiki (at-one-ment) kati ya Mungu na wenye dhambi, na pia kwa njia ambayo uhusiano mzuri hupatikana. Kutoka katika Biblia ya Tyndale tafsiri hii ilihamishwa karne moja baadaye hadi kwenda katika King James Version, na kutoka hapo ikaingia katika msamiati wa kila mwanafunzi wa Neno aliyezungumza Kiingereza (Asilimia 83 ya tafsiri ya Tyndale iliingia kwenye King James Version). Wenye dhambi "wanapingana/wanatofautiana" na Mungu, na wametengwa Naye kwa dhambi zao. (Isaya 59:2)

Kwa sababu hawawezi kujirejesha au kujirekebisha wenyewe, ni lazima mtu mwingine awafanyie upatanisho (Awafanye wawe na umoja). Ili kutimiza hitaji hilo, Yesu alitoa maisha Yake; na hii ndiyo sababu wanatheolojia wengi wa Kiprotestanti wanazungumza juu ya kifo cha Kristo kama “upatanisho.” Wanamarejeo hata hivyo, katika shauku yao ya kujifunza yote wawezayo kuhusu Yesu, wamekuja kuelewa upatanisho kwa maana muhimu na pana zaidi. Hiram Edson na marafiki zake, kwa mfano, waliona kwamba katika ibada za Patakatifu pa kidunia, watu walipokuwa wakitoa dhabihu zao na kuungama dhambi zao siku baada ya siku, walisamehewa na upatanisho ulifanywa kwa ajili yao (Angalia Mambo ya Walawi 4:26, 31, 35).

Bila kujali hilo, kila mwaka dhambi zao zilizosamehewa zilipitiwa upya na kusafishwa katika Siku ya Upatanisho. Katika Siku hii kuu ya Upatanisho (Mambo ya Walawi 16), Mungu alihitaji kuhani mkuu mwenyewe kufanya huduma na ibada hii. Hakuna kuhani wa kawaida ambaye angeifanya. Katika siku hii moja katika mwaka wote kuhani mkuu aliingia Patakatifu pa Patakatifu, ambapo uwepo wa Mungu ulifananishwa na nuru ing’aayo, na isiyo ya kawaida au asili juu ya Sanduku la Agano. Na kusudi la kuhani mkuu katika siku hii ya pekee katika mahali hapa pa pekee lilitamkwa kwa mkazo katika Maandiko: “kufanya upatanisho kwa ajili ya Patakatifu,” na “kufanya upatanisho kwa ajili yenu [watu wa Mungu], ili kuwatakasa ninyi, mpate kuwa safi na dhambi zenu zote mbele za BWANA." (Mambo ya Walawi 16:33, 30) Utakaso wa Patakatifu na utakaso uliohitimishwa wa watu waliosamehewa ulienda sambamba katika nyakati za Agano la Kale.

Hivyo, Edson na marafiki zake walitoa hoja kwamba, kutakaswa kwa Patakatifu pa mbinguni na kutakaswa kabisa kwa watakatifu waliosamehewa na Mungu lazima iwe ndiyo maana ya huduma ya pekee ya Kristo katika Patakatifu pa Patakatifu pa

mbinguni tangu Oktoba 22, 1844. Kwa msaada wa konkodansi zao au magombo ya ufafanuzi wa Biblia, Edson, Crosier, na Hahn wakatafuta maneno "fidia ya dhambi" na "upatanisho" kila mara yanapotokea katika Biblia ya (KJV), na wakagundua kwamba yanahusishwa na maneno kama vile "kusafisha, kupatanisha, kutakasa, kusamehe, kufanya takatifu, kutoa haki, kusamehe, kuhalalisha, kukomboa [na] kufuta. "Walitilia maanani hasa ahadi iliyo katika Matendo 3:19-21 kwamba kwa maana ya mwisho, dhambi zote "zitafutwa" kabla tu ya Mungu kumtuma Yesu tena duniani mwishoni mwa ulimwengu.

Walifikiri kwamba upatanisho wa kila siku ulikuwa mfano wa kifo cha neema cha Kristo msalabani na cha huduma Yake katika Patakatifu pa mbinguni, na kuwezesha msamaha wa dhambi upatikane kwa kila mwenye dhambi; na kwamba Siku ya Upatanisho ya kila mwaka ilikuwa ishara ya huduma ya Kristo katika Patakatifu pa Patakatifu pa mbinguni, akifuta dhambi za kila mwamini ambaye amebaki mnyofu tangu kuungama kwake. Hivyo wakasitawisha hitimisho la ushindi: Kwa vile wenye dhambi wametafuta msamaha katika vizazi vyote, Yesu amebeba kumbukumbu ya dhambi zao zilizoungamwa hadi Patakatifu, ambapo pametia unajisi Patakatifu pa mbinguni. Na kama vile ilivyokuwa lazima kwamba “mifano ya mambo yaliyo mbinguni isafishwe” kwa dhabihu za wanyama, ndivyo ilivyokuwa lazima baada ya muda “vitu vyenyewe vya mbinguni” visafishwe. (Waebrania 9:23)

Kusafishwa kwa Patakatifu kunakoendelea sasa, hakika ni kazi kubwa kwelikweli ya kuungama na kupatanishwa; na jambo hilo sio kitu pungufu, yaani kuondolewa na kufutwa kwa mwisho kwa kila dhambi inayowatenganisha watu wa Mungu kutoka Kwake. Crosier, mwandishi bora katika kikundi, aliagizwa na wengine kuandika matokeo ya utafiti wao. Enoch Jacobs, mhariri na rafiki wa Waadventista huko mji wa Cincinnati, alikubali kuchapisha makala yake kwa gharama zao katika nambari maalum (au "ziada") ya jarida lake la The Day Star. Gharama ilikuwa karibu dola 30.00, na hali zao zilikuwa ngumu sana kiasi kwamba hata Edson na Hahn, ambao walikubali kulipia gharama ikiwa Crosier angeanza kuandika, walipata ugumu wa kuja na hata nusu ya hiyo pesa. Bi. Edson aliuza baadhi ya vyombo ikiwemo sahani na vijiko vyake ili kusaidia.

Walitarajia pesa iliyobaki ingechangwa na wasomaji wenye shukrani. Baadhi ya Waadventista ambao miongoni mwao akiwamo, Ellen Harmon walikuwa akisafiri wakati huo huko Massachusetts na sehemu nyinginezo za New England kwa dhahiri alikuwa kwenye orodha ya wale wanunuaji wa gazeti kwa njia ya posta; na gazeti la Day Star Extra la Februari 7, 1846, lilipowasili, alifurahi. Maelezo haya yalipatana sana na maono alilokuwa amepokea. Shauku yake iliidhinishwa haraka na maandishi haya.

Katika maono mengine muda mfupi baadaye, Bwana alimwonyesha kwamba “Ndugu Crosier alikuwa na nuru ya Kweli, juu ya kutakaswa kwa Patakatifu, na kwamba yalikuwa mapenzi Yake kwamba Ndugu Crosier aandike maoni ambayo angetupa sisi katika nyongeza ya Gazeti la The Day Star, Februari 7, 1846." Alitoa maoni, "Ninahisi nimeidhinishwa kikamilifu na Bwana kupendekeza hiyo sehemu ya Ziada, iliyokuwa katika gazeti kwa kila mtakatifu." Miaka mingi baadaye, baada ya kupata nuru zaidi juu ya somo hilo, bado alizungumza kama walivyofanya kuhusu "kazi hii kuu ya upatanisho," "kufutwa kwa dhambi." Pia aliita dhana yao mpya kama moja ya "alama-landmark" za ujumbe wa Waadventista Wasabato. Tusipoelewa hili, alisema, "haitawezekana" kwetu "kuzoesha na kuonyesha imani iliyo muhimu kwa wakati huu." Karibu na mwisho wa maisha yake alikazia tena kile alichosisitiza: "Patakatifu ndiyo msingi wa imani yetu." Patakatifu ndio msingi wa imani yetu!

Waadventista Wasabato wapo ili kuuletea ulimwengu ujumbe kuhusu ile kazi ambayo Yesu anaifanya kwa sasa kwa hivi, wale wanaoweka imani yao Kwake, yaani wale wanaomtegemea na kumtumaini Yeye, naam kwa wale wanaomtumaini Yeye. Hata katika nyakati za Agano la Kale, Kuhani mkuu aliposafisha Patakatifu, aliwatakasa watu pia, kama vile Bwana alivyofanya kupitia Musa, na kuwaambia watu, “ili mpate kutakaswa na dhambi zenu zote mbele za Bwana.” Kupita kwa wakati katika 1844, Ellen White aliandika katika 1889, “ilikuwa kipindi cha matukio makubwa, yaani kufunguka kwa macho yetu yaliyoshangazwa.yaliyotekewa.”

Naam, utakaso wa Patakatifu unaoendelea mbinguni, ambao baadaye utaamua uhusiano na watu wa Mungu duniani. "Jinsi uhusiano huo ulivyo wa utukufu sana na jinsi ulivyomhusu kila mtu binafsi, naam watu wote wa Mungu duniani, alidokeza katika Kitabu cha The Great Controversy, ukurasa wa 485 (Pambano Kuu): “Hivyo kutatimizwa utimizo kamili wa ahadi ya agano jipya, ‘Nitausamehe uovu wao, na kuwasamehe maovu yao; sitazikumbuka dhambi zao tena……Katika siku hizo, na wakati huo, asema Bwana, uovu wa Israeli utatafutwa, wala uovu hapana; na dhambi za Yuda zitatafutwa wala hazitaonekana’ (Yeremia 31:34; 50:20)

Edson na marafiki zake walijifunza mambo mengi kumhusu Yesu; lakini hebu sisi tungojee hadi sura za baadaye ili kupata ufafanuzi wa njia muhimu ambazo huduma ya Kristo kama kuhani mkuu inahusiana na arusi na hukumu, kama vile ujumbe wa malaika wa tatu ulivyo na muhuri wa Mungu, roho ya unabii, na, haswa haswa, Sabato ya siku ya saba.

*Maelezo.*

*1. O.R.L. Crosier, "The law of Moses," Day Star Extra, February 7, 1846, p. 38*

*2. In many cases the priest ate a portion of the people's sacrifices, thus transferring their guilt to himself. Later, when he made his own sacrifice, he carried blood into the holy place, thus transcribing there a record not only of his own but also of the people's sins. (See Leviticus 4:27-35; 1-7, 13-20; 6:24-30)*

*3. Seventh-day Adventists regard the entire plan of salvation, from beginning to end, as the atonement. See SDA Encyclopedia, art. "Atonement." See also Seventh-day Adventists Answer Questions on Doctrine (Washington, D.C.: Review and Herald Publishing Association, 1957), pp. 341-390. The cross is Christ's supreme atoning act. His ministry in heaven, however, is considered "equally essential" (Ellen G. White, The Great Controversy between Christ and Satan [Mountain View, Calif.: Pacific Press Publishing Association, 1888, 1911, 1950], p. 140 489), and is called "atonement" by Ellen White in many passages, such as Spiritual Gifts, vol. 1, p. 158; Testimonies for the Church, vol. 5, p. 575; The Great Controversy, pp. 420, 489, 623; Testimonies to Ministers (Mountain View, Calif.: Pacific Press Publishing Association, 1923, 1961), p. 37*

*4. Crosier, "The Law of Moses," p. 40*

*5. James White, A Word to the "Little Flock," p. 12*

*6. Ellen G. White, Patriarchs and Prophets, p. 358*

*7. Ellen G. White, Counsels to Writers and Editors (Nashville, Tenn.: Southern Publishing Association, 1946), p. 30*

*8. Ellen G. White, The Great Controversy, p. 488*

*9. Ellen G. White, Manuscript 20, 1906*

*10. Ellen G. White, Counsels to Writers and Editors, p. 30*

## SURA YA 11
## MASHAHIDI WAJANE

Katika Mkutano Mkuu wa 1843 wa Waadventista wa Sabato Wabaptisti wa Marekani, kura Ilipigwa kuhusu utendaji wa jambo ambalo linastahili umakini wa jicho letu kwa karibu. "Wajumbe" kadhaa walihudhuria kikao, wakiwakilisha baadhi ya

wanachama 5,500 wanaoishi hasa katika majimbo ya Rhode Island na New Jersey na kutawanyika katika majimbo mengine kadhaa. Msururu wa miswada/manuscripts za Jumapili katika mabunge ya majimbo na shirikisho hivi majuzi ulikuwa umeongeza maslahi ya umma katika Sabato. Nyakati zilionekana kuwa mwafaka kuendeleza kazi ya siku takatifu ya Mungu; na konferensi ilipiga kura pendekezo lisilo la kawaida kwa kanisa lao: "Kwamba siku ya kwanza ya Novemba ijayo itunzwe na makanisa yetu kama siku ya kufunga na kuomba kwamba Mwenyezi Mungu asimame na kusihi mioyo ya watu kwa ajili ya Sabato Yake takatifu.

Wabaptisti waaminifu waliotunza Siku ya Saba ya juma, ambao walizingatia pendekezo hili mnamo Jumatano, Novemba 1, 1843, hawakutarajia jinsi, au ukubwa, wa jibu ambalo Mungu Alikuwa amelitayarisha kwa karne nyingi awali, au kabla ya hapo. Hata walipokuwa wakifunga na kusali, mmoja wao, Bi. Rachel Oakes (ambaye baada ya kuolewa tena, aliitwa Bi. Preston) wa kutoka Verona, wa kata ya Oneida, New York, alikuwa akifikiria kuhamia kijiji cha mlimani cha Washington New Hampshire. Binti yake mwenye umri wa miaka kumi na minane, Delight, alikuwa amekubali kazi ya ualimu kwenye shule ya serikali huko na kwa vile yeye mwenyewe alikuwa mjane, ilionekana kuwa jambo la busara kwa Bi Oakes akae huko wakati wa majira ya baridi ya theluji na bintiye Delight, Washington, New Hampshire. Kwanini asifanye hivyo? Isitoshe, angeweza kupata fursa ya kushuhudia huko.

Angeweza kuchukua ugavi wa machapisho ya Sabato. Akiwa angali anafikiria hatua ya kutekeleza mawazo yake, Bi Oakes, alijikuta akihudhuria ibada katika kijiji chake kipya na ndugu wa Kikristo. Kutaniko lao lilikuwa lile lisilofungamana na madhehebu na ambalo, pamoja na mchungaji wao, lilikuwa limekubali ujumbe wa marejeo ya Yesu ambao William Miller alihubiri. Lilikuwa pia, kwa hakika, kutaniko lililotunza Jumapili, na kwa kuwa hapakuwa na kanisa la Wasabato karibu, Bibi Oakes aliishika Sabato kadiri alivyoweza pamoja na binti yake Delight, na kisha akahudhuria kanisa la Jumapili kwa ajili ya ushirika wa Kikristo. Jumapili hii mahususi ilikuwa siku ya kushiriki meza ya Bwana (Komunio), na mchungaji, Frederick Wheeler, mpanda farasi wa Kimethodisti, mwenye umri mdogo wa kutoka mji wa Hillsboro, maili kumi na mbili kutoka hapo, alikuwa akihubiri.

Mara moja alisema kitu ambacho kilikaribia kumfanya Bi Oakes asimame kutoka kwenye kiti chake. Alijizuia hadi Wheeler, mchungaji mzuri huyu, alipokuja kumtembelea paroko wake mpya kutoka New York. "Ulipokuwa unazungumza, Mzee Wheeler," alimwambia kwa ghafula, "nilishindwa kujizuia. Ulisema kwamba ni lazima tuzishike Amri zote Kumi, na bado wewe mwenyewe huvunja moja kati ya hizo mara kwa mara!" “Kwa nini, Dada Oakes,” akasema yule mtu mwema, “Je, unamaanisha nini?” "Ninamaanisha kwamba amri ya nne inasema, 'Siku ya saba ni Sabato ya Bwana, Mungu wako,' lakini wewe unashika siku ya kwanza. Unaitunza

Jumapili ya papa badala ya Sabato ya Bwana!" Hatujui kama mchungaji aliudhika au la, lakini tunajua kwamba wakati fulani wakati huo wa majira ya baridi kali, yawezekana mnamo Machi 16, 1844, alifanya uamuzi wake wa kushika siku ya saba kama Sabato.

Hivyo ndivyo ilivyokuwa, kwamba Frederick Wheeler, Mmethodisti wa Kiadventista na mfuasi wa Miller, wa Hillsboro, New Hampshire, akawa mchungaji wa kwanza wa Waadventista Washika Sabato katika Amerika ya Kaskazini. Na ingawa wakati huo hakuhubiri kuhusu Sabato katika kanisa lake la Washington, inaonekana kwamba alifanya hivyo katika shule iliyo karibu na nyumbani kwake, na kwamba alizungumza jambo hilo faraghani na kulikuwa na angalau mchungaji mmoja ambaye, kama yeye, alikubali tumaini la ujio wa Kristo kwa mara ya pili. Kufikia Agosti 1844 Thomas M. Preble, aliyekuwa Mbaptisti wa Freewill ambaye alichunga kusanyiko la watu 145 katika kitongoji cha kutengeneza viatu cha Weare, New Hampshire, kama maili kumi na mbili mashariki mwa Hillsboro, akawa mchungaji wa pili wa Waadventista Washika Sabato katika Amerika Kaskazini.

Kufikia mapema Oktoba 1844 kulikuwa na angalau mwadventista mwingine Mshika Sabato, jina lake aliitwa Dada S. Blake huko Rhode Island, ambaye inaweza kuwa, alikuwa Bibi wa Kibaptisti wa Siku ya Saba kama Bi. Oakes. Nje ya Amerika Kaskazini Waadventista wengine wachache wa awali waliikubali Sabato ya siku ya saba takriban wakati huohuo au mapema zaidi. Mmoja wao alikuwa Francisco Hermogenes Ramos Mexia (1773-1825) wa Argentina, mwanasiasa mashuhuri aliyechanganya matengenezo ya kisiasa, kilimo cha mashamba makubwa, biashara na uinjilisti kwa Wahindi wekundu. Alifanya idadi kubwa ya waongofu, na alikamatwa mwaka 1821 kwa kushika Sabato.

Mwingine, James A. Begg (1800-1868) wa Scotland, anayejulikana sana katika Visiwa vya Uingereza kama mwandishi wa unabii na Marejeo ya Yesu mara ya Pili, alianza kushika Sabato yapata mwaka 1832. Lakini lazima turudi Washington, New Hampshire. Inaonekana kwamba Delight Oakes aliishi katika shamba kubwa la Farnsworth. Basi kuna uwezekano mkubwa kwamba mama yake alikaa huko pia. Lazima kulikuwa na maoni mengi kuhusu Sabato na Jumapili ambayo lazima yalimfikia Bi Oakes moja kwa moja na wenyeji wake wakarimu na waaminifu. Inaonekana, zaidi ya hayo, kwamba Cyrus, mmoja wa vijana wa Farnsworth, alikuwa amempenda mwalimu huyu wa shule, yaani Delight Oakes. (Hapo Baadaye walioana) Lakini jambo lililoshamiri kupita kila jambo jingine lilikuwa mwisho wa ulimwengu unaokaribia.

Kristo alikuwa anakuja, na kulikuwa na muda mfupi kwa Waadventista wengi kuzingatia wajibu mpya wa siku takatifu ya Sabato. Hivyo ilikuwa kwamba miongoni mwa wale waliotazamia kwa hamu ujio wa pili mnamo Oktoba 22, 1844, kulikuwa na

angalau watu watatu walioshika Sabato, ikiwemo Frederick Wheeler huko Hillsboro, Thomas Preble wa Weare, na Dada Blake katika Kisiwa cha Rhode—isipokuwa Bi. Oakes, ambaye hadi wakati huo, yaonekana alishindwa kuwashawishi watu wa Washington pale alipofikia, kuwa washika/watunza Sabato, ila alikuwa kwa wakati huu, amewaruhusu wao kumshawishi yeye binafsi kuwa Muadventista. Pamoja na huyo, kulikuwa na angalau washika Sabato wanne. Baada ya "kupita kwa wakati ule waliotegemea Yesu kuja" mnamo Oktoba 22, Waadventista huko Washington hawakuacha imani yao, lakini waliendelea kwa subira kungojea kurudi kwa Kristo.

Kwa wakati huu walielekeza mawazo yao kwa hamu zaidi kwenye Sabato ya Bi. Oakes. Muda mfupi baadaye, wakati kanisa dogo imara la Christian Brethren lilipokuwa na ibada tulivu siku ya Jumapili asubuhi, William, kijana mkubwa wa watoto wa Farnsworth, alisimama dedewakati wa mkutano wa kijamii na akatangaza mbele ya watu waliomjua tangu kuzaliwa kwake kwamba alikuwa amefanya uamuzi wake wa kuishi tangu sasa akishika Sabato ya amri ya nne. Yesu Kristo hakuwa amebadili siku hiyo, lakini papa alikuwa amefanya hivyo katika utimizo wa unabii. William alisema alitaka kuhesabiwa miongoni mwa watunza Sabato ya Bwana na si miongoni mwa wafuasi wa Papa, ambao ni wavunjaji wa Sabato.

Kabla ya kuketi chini, kaka yake Cyrus  alisimama na kutoa ushuhuda ule ule. Bi. Oakes na binti yake kila mmoja alitoa machozi na kumsifu Bwana. Lakini, sio kila mtu aliyefurahia. Sehemu kubwa ya kutaniko halikukukubali Sabato kwa wakati huu, ingawa wengi wao waliikubali baadaye. Wale waliofanya hivyo, waliacha kutumia kanisa kwa wakati huo na badala yake walikutana Sehemu yenye eneo kubwa hapo mjini Farnsworth—

## KUTANIKO LA KWANZA LA WAADVENTISTA WASHIKA SABATO KATIKA AMERIKA KASKAZINI.

Lakini kabla hatujafuatilia mustakabali wa Sabato wa siku zilizofuata, inavutia zaidi na inasaidia kutazama nyuma kwa muda. Baada ya yote, Waadventista Wasabato walipata Sabato kutoka kwa Bibi Oakes naye huyu mama ambaye alikuwa Mmethodisti wa zamani, aliipata kutoka kwa Wabaptisti wa Siku ya Saba. Je, Sabato inaweza kufuatiliwa mpaka wapi huko nyuma? Je, ilianzia wapi Sabato kwenye ulimwengu wetu huu? Kwenye uumbaji, bila shaka! Lakini katika karne za hivi majuzi ni jambo la thamani kurejea angalau miaka ya 1520, wakati Matengenezo ya

Kanisa yalipokuwa yakipamba moto katika Ulaya ya kati. Hapa Martin Luther na wale Wanamatengenezo wengine waliokuwa viongozi, wote wakisema kwamba Kweli sharti itafutwe katika “Biblia na Biblia pekee,” haishangazi kwamba mazungumzo yalizuka kati ya wafuasi wao juu ya suala la Jumapili na Sabato.

Sabato inafundishwa kwa uwazi katika Maandiko kama fundisho jingine lolote la imani. Kulikuwa na Wakristo huko Ulaya katika miaka ya 1520 ambao waliuliza, "Ikiwa Luther anasema ni lazima tufuate Biblia na Biblia pekee, kwa nini yeye hashiki Sabato? Je, yeye mwenyewe hashiki amri za Mungu?" Miongoni mwao walikuwako waamini wengine waliokubali ubatizo wa kuzamishwa majini mtu akiwa mtu mzima, kama ilivyokuwa kwa Yesu mto Yordani, badala ya ubatizo wa watoto wachanga, na kujipatia jina la Anabaptist.

Kutoka miongoni mwa Wa-Anabaptisti kukatokea wanaume wawili wenye kisa cha kusisimua hasa. Wote wawili waliwahi kuwa makasisi wa Kikatoliki. Katika kutafuta kwao ile Kweli waliacha kazi zao za upadri na kuwa Walutheri. Walipoendelea kujifunza, wakawa Wanabaptisti. Baada ya kujifunza zaidi, waliikubali Sabato na kuwa "Wa-Anabaptisti wa Kisabato" wa kwanza. Luther aliwatumia wanatheolojia ili kuwakatisha tamaa. Kutokana na ripoti zao tunajifunza kwamba watu hawa wawili, Oswald Glait na Andreas Fischer, hawakuwa wamefanya uamuzi wao kwa ajili ya Sabato kijuu juu. Walikuwa wamepima na kufikiriia mambo kwa uangalifu kuhusu msimamo wao unaohusu Sabato, walisema, haiwezi kuwa sehemu ya sheria ya kimapokeo/kaida kwa sababu ilianzishwa wakati wa uumbaji kabla hata ya hitaji la sheria za kaida kutokea (Sabbath law came before the fall or ceremonial laws of sacrifice); kwa hiyo ni sehemu ya sheria ya kimaadili na bado ni ya lazima kwa vile ipo katika zile Amri Kumi za Mungu, ambazo ni nakala ya tabia ya Mungu (Sheria ya Bwana ya Sabato ilikuja kabla ya mwanadamu kuanguka na kaida za sherehe za kuchinja dhabihu au kafara).

Wakinukuu Mathayo 5:17, 18, walionyesha kwamba Yesu alikataa kubadili hata nukta moja au sehemu ndogo ya sheria; na kurejelea Yakobo 2:10. Waliongeza kwamba mitume hawakuibadilisha Sabato pia. Walisema kuwa ibada ya Jumapili, ilikuwa ni utimilifu wa unabii wa kazi ya pembe ndogo (Danieli 7:25) ambayo iliazimu "kubadili majira na sheria." Katika siku hizo wanadamu hawakuweza kuchukua msimamo kama huo, hata katika nchi za Kiprotestanti, na kutumaini kuishi maisha yao ya kawaida. Mnamo 1529 Bwana na Bibi Andreas Fischer walihukumiwa kifo, bibi Fischer kwa kuzamishwa katika maji, na Bwana Andreas Fischer kwa kunyongwa. Hukumu ya Bibi Fischer ilitekelezwa na alikufa maji, lakini mumewe alipokuwa katika harakati za kunyongwa, alianguka chini na kutoroka. Kwa bahati mbaya hakutoroka milele kwani mnamo 1539 au 1540 Bwana Fischer naye alikamatwa na askari wa Knight aliyekuwa jambazi na akavutwa ndani ya ngome yake, na kurushwa kutoka juu ya ukuta.

Oswald Glait alinusurika matukio mengi alipokuwa akisafiri huko Ulaya ya kati kuwatia moyo waamini na kuwafanya watunza Sabato wapya. Mnamo 1545 alitekwa nyara. Baada ya mwaka mmoja na wiki sita gerezani aliamshwa usiku wa manane na kelele zinazosukasuka za askari kwenye ukumbi nje ya chumba chake. Mlango ukafunguka ghafla. Kwa mwanga wa kupepea wa mienge ya moto ambayo walishikilia, alisoma katika nyuso zao ukatili mbaya wa juu na hatima yake inayokuja. Aliongozwa kupitia jiji lililo kimya hadi kwenye ukingo wa Danube, akiwa amefungwa mikono na miguu, na kutupwa mtoni. Askari waliposikia mlio wake, hawakutambua kwamba Ukweli ambao kwake alijitolea maisha yake ungeishi kwa karne nyingi huko Ujerumani, nao uingie katika maisha mapya huko Uingereza, Scotland, Wales na Ireland, na kuhamishiwa katika makoloni ya Amerika, na katika karne ya ishirini ukaishika Mioyo ya mamilioni ya watu duniani kote.

Washika Sabato wengine kutoka kipindi hiki wanaojulikana waliishi Uholanzi, Uswizi, Moravia, na Sweden na kulingana na utafiti wa hivi majuzi, huko Seville, Spain Kila mtu anajua kwamba Wapuritani ambao ni washika dini wa awali wa Kimarekani, hawa walikuwa wakitunza kwa umadhubuti sana siku ya Jumapili, wakiamini kwamba Jumapili inapaswa kuwekwa katika utimilifu wa amri ya nne. Washika dini wa Uingereza walikuwa sawa na Wapuritani pia; na wakati wa miaka ya 1600 kulitokea msukosuko huko Uingereza kuhusu amri ya nne kiasi kwamba watu kadhaa waliongozwa kushika Sabato. Wabaptisti wanaotunza Siku ya Saba ya juma, wanathamini kumbukumbu zao kama waanzilishi wa harakati ya kutunza Sabato ya Jumamosi iliyoandikwa katika Biblia.

Miongoni mwa watu wa kwanza hawa walikuwa John na Dorothy Traske. John alikuwa mchungaji mcha Mungu mwenye bidii na Dorothy, mwalimu mwenye kipawa ambaye alikuwa na ustadi wa kuwasaidia watoto wadogo sana kutoka katika nyumba za matajiri kujifunza kusoma. Wote wawili walifungwa gerezani kwa ajili ya kushika Sabato. Bw. Traske alihukumiwa (mwaka 1617) "kwa kuwekwa juu ya mkatale huko Westminster, na kutoka huko alichapwa na kisha kuwekwa katika gereza la Fleet ambapo angebaki huko kama mfungwa." Ilikuwa maili mbili tu kutoka Westminster (bunge la Uingereza) hadi gereza la Fleet. Ni mateso makubwa kiasi gani aliteseka, kufungwa nyuma ya gari akiburuzwa na kuchapwa viboko njia nzima. Lakini alipokaribia kumaliza kifungo chake cha miaka mitatu, alighairi na kuacha Sabato. Hata hivyo, mke wake alipata ujasiri kutokana na woga wake. Hivyo aliendelea kukaa katika gereza lake chafu, lililojaa viroboto na panya na aliendelea kuwa mwaminifu kwa miaka kumi na tano au kumi na sita hadi kifo chake.

Francis Bampfield, kasisi wa Kanisa la Uingereza, alifungwa gerezani mwaka wa 1662 kwa kukataa kula kiapo kinyume cha dhamiri yake. Akiwa gerezani, akawa mshika Sabato punde, kwa sababu ya funzo binafsi la Biblia. Kwa kuhubiri karibu kila siku katika kipindi kilichosalia cha kifungo chake cha miaka tisa, alianzisha kikundi

cha watunza Sabato gerezani! Mara alipoachiliwa, alifungwa tena kwa muda mfupi. Akiwa ameachiliwa tena, alihamia London ambako alikamatwa mara tatu zaidi kwa ajili ya kuhubiri Kweli kuhusu Sabato, hatimaye akamaliza maisha yake katika unyevunyevu na ubaridi wa gereza la Newgate.

John James, mhubiri mwingine na mshika Sabato, alikuwa akihubiri Sabato mchana, Oktoba 19, 1661, wakati polisi walipoingia kanisani mwake na kudai kwa jina la Mfalme Charles wa Pili kwamba akome. Mtu huyu aliyejawa na Roho Mtakatifu, aliendelea kuhubiri. Zogo likazuka. James alikamatwa, na kuhukumiwa na baraza lililojaa watu kwa mashtaka ya uongo, na kuhukumiwa kama msaliti kwa kunyongwa, kuvutwa kwa gari, na kukatwa katwa. Ijapokuwa mke wake alimsihi mfalme mara mbili kwa ujasiri, John James aliwekwa kitanzi shingoni huko Newbury, kisha kitanzi kikatolewa baada ya kufa na mwili wake ukakatwakatwa kama wauza nyama wafanyavyo kwenye bucha, moyo wake ukatolewa nje ya kifua chake na kutupwa kwenye moto, na kichwa chake kutundikwa nje ya kanisa lake, kama onyo la kuhuzunisha kwa yeyote anayeweza kutamani kushika siku ya saba kama Sabato.

Kwa Wabaptisti wengi wa Siku ya Saba yaani Jumamosi, Sabato ilikuwa siku yenye thamani sana, hata kuweza kuifia. Sio washika Sabato wote wa Uingereza katika karne ya kumi na saba walitakiwa kupewa mateso. Dk. Peter Chamberlen, daktari wa magonjwa ya wanawake na aliyekuwa akisaidia kuzalisha akina mama aliyependwa na wanawake kadhaa wa familia za kifalme na watu mashuhuri nchini Uingereza, aliitunza sabato kwa usalama kwa zaidi ya miaka thelathini na miwili. Alizungumza lugha kadhaa, alipendekeza maji ya moto na baridi katika matibabu ya magonjwa, na, kwa bahati, aligundua gari lisilo na farasi linaloendeshwa na upepo. Kwa uzuri na uwezo wake, alikuwa wa thamani sana kiasi kwamba viongozi wa Uingereza hawakutaka kumtesa.

Maadhimisho ya siku ya saba yalihamishiwa Marekani na Stephen Mumford, ambaye alihama kutoka Uingereza mnamo 1664 na kupanga (organize) kanisa katika Kisiwa cha Rhode, mnamo 1671, hili ni kanisa la kwanza la Wabaptisti washika Sabato huko Amerika ya Kaskazini. Mapema miaka ya 1700 kulikuwa na watunza Sabato wa Moravian, pia, huko Bethlehem, Pennsylvania.

Baada ya kuwatembelea, Count Nicolaus von Zinzendorf aliazimia kushika Sabato na pia Jumapili. Na bado kulikuwa na watunza Sabato Wajerumani wengine katika sehemu mbalimbali za makoloni. Wabaptisti washikao Siku ya Saba ya juma, yaani Jumamosi huko Amerika ya Kaskazini walijipanga vizuri katika Kongamano lao Kuu (General Conference) mwaka 1802 wakiwa na washiriki karibu 1200. Ingawa waliongezeka kwa idadi, hawakuwahi kuwa na juhudi nyingi kuhusu uinjilisti. Kwao, Sabato ilikuwa siku ya kutunza na kuthamini badala ya kuwashirikisha watu wengine

pia ili waijue na kuishika. Lakini baadhi waliwaambia watu wengine--jambo ambalo linaturudisha kwenye General Conference yao au Mkutano Mkuu wao muhimu wa 1843, na azimio lake likitenga Novemba 1, 1843, kama siku ya kufunga na kuomba kwamba Mungu "atasimama na kusihi watu, kwa ajili ya Sabato Yake takatifu."

**Kupitia mjane Rachel Oakes, sala yao ilijibiwa zaidi ya ndoto zao pendwa zaidi.**

*Vidokezo:*

*1. Seventh Day Baptists in Europe and America, 3 vols. (Plainfield, N.J.: The Seventh Day Baptist General Conference, 1910-1972), vol. 1, p. 185. (See also Froom, Prophetic Faith, vol. 4, pp. 942, 943)*

*2. Early fragmentary accounts of how Mrs. Oakes brought the Sabbath to the Adventists in Washington differ considerably in their small details and have been the subject of much study by Adventist historians. Interested students can compare the story as related here with other accounts in Froom, Prophetic Faith, vol. 4, pp. 944-951, and Spalding, Origin and History, vol. 1, pp. 115-117, 397-400*

*3. S.W. Bartle to W.A. Spicer, September 4, 1935, original deposited in the W.A. Spicer Collection, the Heritage Room, James White Library, Andrews University. Bartle's authority is George Wheeler, presumably Frederick Wheeler's son*

*4. Sister S. Blake, Richmond, Rhode Island, letter, Advent Herald and Signs of the Times Reporter, October 2, 1844, p. 72*

*5. Froom, Prophetic Faith, vol. 4, pp. 920-940*

*6. For information about early Sabbatarian Anabaptists see Gerhard F. Hasel, "Sabbatarian Anabaptists of the Sixteenth Century," part 1, Andrews University Seminary Studies 5 (July 1967), pp. 101-121, and part 2, AUSS 6 (January 1968), pp. 19-28*

*7. See SDA Encyclopedia, art. "Sabbath"*

*8. Mario Veloso, "Reformation in Seville, 1530- 1560" (master's thesis, Andrews University, 1972), pp. 143-145. The Spanish Sabbath keeper was Constantino de la Fuente*

*9. Information about prominent seventeenthcentury British Seventh Day Baptists can be found in Seventh Day Baptists in Europe and America, vol. 1, pp. 63-111; Froom, Prophetic Faith, vol. 4, pp. 906-917; and J.H. Andrews and L.R. Conradi, History of the Sabbath and First day of the Week (Washington, D.C.: Review and Herald Publishing Association, 1912), pp. 717-734*

## SURA YA 12
## KAPTENI AENEZA NENO

Kulikuwa na kitu kuhusu namna ambapo Sabato ilivyohama kutoka kuwa Wabatisti wa Siku ya Sabato na kutengeneza njia yake, hadi kwa Waadventista Wasabato ambapo ilifananishwa na namna moto unavyokuwa ukisonga mbele kutoka kwenye kamba iliyounganishwa na fyuzi iliyopo kwenye pipa la kulipulia baruti.

Bi. Oakes aliipitisha/aliambukiza Sabato ya Kweli, ya Amri ya Nne kwenye Maandiko yaani siku ya saba ya juma, Jumamosi, kwa Frederick Wheeler na Waadventista wachache wa Washington. Wheeler aliihubiri bila ubishi mwingi sana wakati huo na (inaonekana) akaipitisha kwa Thomas M. Preble. Preble aliandika juu yake katika Hope of Israel ya Februari 1845 - Gazeti lililoharirіwa, na Joseph Turner yule yule ambaye mnamo Desemba 1844 aligundua Ukweli uleule ambao Edson na Ellen waligundua juu ya kungojea kurudi kwa Kristo kutoka kwenye harusi. Mara tu Preble alipoweza, alirekebisha makala yake na kuichapisha tena kama chapisho lenye kichwa, “IMEFAA VYA KUTOSHA,” Chapisho linaloonyesha Kwamba Siku ya Saba ya juma, yaani Jumamosi, ndiyo inapaswa kuadhimishwa kama Sabato.

Alihitimisha ujumbe wake kwa nguvu kwa kutumia herufi kubwa na italiki nyingi. “Hivyo tunaona Danieli 7:25 ikitimizwa, ile ‘pembe ndogo’ ikibadili ‘sheria na majira.’ Pembe ndogo ilibadilisha amri ya Nne, kutoka ‘ikumbuke siku ya saba ya juma’ na kwenda ‘siku ya kwanza ya juma’ ambayo watu wengi ndiyo hutunza kwa kuabudu katika siku hiyo. Kwa hiyo inaonekana kwangu kwamba wote wanaoshika siku ya kwanza ya juma kama 'Sabato' ni Watunza Jumapili wa Papa na WAVUNJA SABATO YA MUNGU!!! Makala na vipeperushi/trakti hizo zilipata matokeo. Hii inaweza kuwa sababu kwa nini J. B Cook, mwanatheolojia Mfuasi wa Miller, alitetea Sabato kwa miaka michache.

Bila shaka nakala ya chapisho hilo ilifika Paris, Maine, ambako ilisadikisha watu kadhaa, na kuingia ndani yafamilia ya Edward Andrews, na hilo lilikuwa jambo lenye

matokeo, kama tutakavyoliangalia. Nakala ya makala hiyo pia ilisomwa na nahodha huyo wa bahari aliyegeuka kuwa kiongozi wa Wamiller, aitwaye kwa jina la Joseph Bates. Na kupitia juhudi zake moto wa injili uliwaka, moto kwenye fataki. hakika Bates hakuwa mtu asiye na vitendo, pale aliposikia kitu na kilikuwa sawa, yeye hakukaa kimya, bali aliingia kwenye utendaji, alishirikisha wengine wakipate hicho kitu mara moja. Mara moja Bates aliacha kila kitu alichokuwa akifanya na kuipekua Biblia kwa bidii, kujifunza haswa. Alisafiri maili 140 kwa gari la farasi, reli, na miguu —na pengine kwa miguu safari yote—hadi Hillsboro kukutana na Frederick Wheeler.

Akiwa amechelewa kufika, aliamsha familia yake, na kujifunza naye kwa kusoma usiku mzima. (Mtoto wa Wheeler, George, alisimulia tukio la usiku huo muda wote katika maisha yake.) Asubuhi iliyofuata, Bates na Wheeler walienda Washington na kuzungumza kuhusu Sabato hadi adhuhuri na baadhi ya watu wa familia ya akina Farnsworth chini ya kituo cha miti ya mshira/maple. Kisha Bates akarudi nyumbani kwake Fairhaven, Massachusetts. Ndipo akiwa njiani alipambana moyoni na matokeo ambayo mabadiliko ya Sabato kwa upande wake yangeweza kuhusisha majirani, familia, na marafiki zake. "Ni nini hicho kwako? Wewe Nifuate Mimi" ndiyo sauti ambayo ilisikika bila kuchoka au kukoma masikioni mwake. Akivuka daraja kati ya New Bedford na Fairhaven, Bates alijipatia mwongofu wake wa kwanza kutoka kwa mmoja wa marafiki zake Waadventista. "Habari gani, Kapteni Bates?" aliuliza James Madison Monroe Hall. "Habari," akajibu jemadari, "siku ya saba ni Sabato ya Bwana, Mungu wetu." Hall aliitunza siku ya saba iliyofuata kama Sabato.

Katika mwaka huo wa1845 Wabatisti wa Siku ya Saba wanaweza kuwa hawakuwa wainjilisti sana kuhusu Sabato, yaani walikaa nayo moyoni, na wala hawakuitangaza sana, lakini Joseph Bates alikuwa nahodha wa zamani wa bahari, mtu mwenye hulka ya uongozi wa asili kwa kumfafanua. Hata hivyo alikuwa Mwanamarejeo, yaani alikuwa anangojea kurejea kwa Yesu mara ya pili, kuwachukua watu kwenda mbinguni na kuishi Naye. Zaidi ya kuwa Muadventista, alikuwa na shauku ya kuwasaidia watu kujitayarisha kukutana na Bwana. Katika mawazo yake, alisema kwamba yeye hakuweza kuwaza kamwe, “kwamba Kamanda wetu mtukufu na Bwana wetu, alipanga kwamba sisi tujishughulishe tu na kuteketeza dhabihu zetu kwake na kuziacha zifuke moshi kwenye madhabahu ya Mungu, Katikati ya nchi ya adui peke yake, lakini badala yake tuwe tunasukuma mbele kutoka ushindi hadi ushindi wa injili." (Hebu Tusimwabudu Mungu tu wenyewe bila ya kuwajulisha wengine wajiunge kumwabudu na kwenda mbinguni)

Mnamo 1846 alisoma makala ya Crosier katika gazeti la Day-Star Extra la Februari 7 na kusadikishwa kwamba Patakatifu pa kutakaswa ni mbinguni na ni hekalu halisi kama vile Yerusalemu mpya lenyewe. Aliketi na kuandika kipande kiandamani, chenye chapisho lenye kichwa, “The Opening Heavens—Mbingu zilizofunguliwa,” ambamo aliongeza uthibitisho zaidi kutoka kwa elimu ya unajimu na Biblia. Hata

hivyo hakuridhishwa na hatua hizi na ndipo aliposafiri mwendo mrefu hadi Port Gibson ili kulinganisha maelezo na Edson, Crosier, na Hahn, na kuwafanya wote wawe watunza Sabato. Wakati huohuo, aliandika chapisho lake maarufu zaidi, "The Seventh Day Sabbath, A Perpetual Sign—Sabato ya Siku ya Saba ya juma, ni Agano la Milele," (Kutoka 31:16)

Mungu alibariki dhabihu,usomaji na ujifunzaji ambao uliingia katika kazi hiyo ndogo. Hakika ilifanya waongofu wengi washika Sabato, ambao miongoni mwao walikuwa James na Ellen White, ambao walikubali ujumbe wake muda mfupi baada ya arusi yao mnamo Agosti 30, 1846. Kwa kuzingatia haya yote na kazi yake ya baadaye, Joseph Bates anaweza kuonwa kuwa baba wa Ukweli wa Sabato miongoni mwa Waadventista Wasabato—watu hawa ambao wanashika Sabato, leo idadi yao ni mamilioni duniani kote (nusu yao ni kutoka Bara la Afrika na asilimia 11% wanazungumza Kiswahili, na ndiyo sababu ya kutafsiri historia hii kwako msomaji!, Angalia video pia ya kitabu hiki—Tell it to the World!).

Hebu tusimame na kutafakari kidogo ili tufahamiane na Joseph Bates. Huyu alikuwa mtu jasiri kwa namna iliyoje, mbunifu, asiyechoka, mvumilivu, mwenye nidhamu, aliyejitoa, mwenye kuikana nafsi, mwenye maisha yasiyoboesha na mwenye fadhila kwa watu. Mzee wa imani miongoni mwa waanzilishi wa kanisa la Waadventista Wasabato, alisafiri kupita wengi ila hakupata magonjwa ukilinganisha na waanzilishi wengine wa kanisa (pioneers of the church). Aliishi hadi kufikisha umri wa miaka 80. Bates alizaliwa mwaka wa 1792 maili kumi na mbili tu kutoka kwenye mandhari, sauti, na harufu za New Bedford, Massachusetts, bandari iliyopanuka kwa kasi na kuwa kitovu cha wavuvi wa nyangumi duniani, ambao walifanya biashara ya mafuta ya nyangumi, mifupa na nyama yake. Bila shaka aliingia kwenye mawimbi ya bahari akiwa na umri wa miaka 15 kama mvulana msaidizi melini (cabin boy). Baba yake alitumaini kwamba Joseph angekuwa na wakati mgumu na usio na furaha na hivyo angeacha. Hakika alikuwa na wakati mbaya sana lakini aliendelea na kazi hiyo.

Wakati wa safari yake ya kwanza alianguka kutoka katika mlingoti wa meli kwenye bahari ya Atlantiki lakini aliokolewa kabla papa aliyekuwa mbele yake akitafuta chakula upande wa pili wa meli kummeza, hakika angeweza kuwa chakula cha papa. Katika safari yake ya pili, akiwa pwani ya Liverpool Uingereza, alikamatwa kwa nguvu ili kuingizwa katika Jeshi la Wanamaji la Kifalme la Uingereza lililokuwa katili, likifanya mazoezi jambo ambalo lilifanya Uingereza kuharakisha vita na Marekani mnamo 1812, *(Vita hii ilijulikana sana na hapo ndipo wimbo wa taifa wa Marekani, ulitungwa, Uingereza iliivamia Marekani ambayo ilikuwa tayari nchi huru kufuatilia mapinduzi ya Ufaransa; Angalia the war of 1812).*

Miaka mitano ilipita kabla ya Bates kuachiliwa. Nusu ya wakati huo alitumia kama baharia baharini na nusu kama mfungwa wa vita POA, katika meli ya 'Man Of War" au kwenye Gereza la Dartmoor. Mara kadhaa alijaribu kutoroka upande wa meli yake au kupitia sehemu yake ya ndani, lakini kila wakati alikamatwa, hakufanikiwa. Alipokuwa huru tena, alifanya safari kumi kati ya 1815 na 1828. Mnamo 1818, katikati ya safari hzo, alimwoa mpenzi wake wa utotoni, Prudence Nye. Maisha yake yalikuwa yenye matukio mengi ya kustaajabisha. Akiwa anakagua minyororo ya nanga mara moja katika siku zake kama mfanyakazi, aliona barafu ikitokea kwa ghafula karibu na mashua yake ya makasia na kumpeleka katika giza kuu hadi baharini. Nahodha wake alisoma ibada kwa ajili ya mazishi yake! Katika kipindi kingine, akirudi na shehena nzito ya chuma kutoka Ulaya na siku tatu tu fupi kutoka nyumbani, meli yake ilighubikwa na tufani kali na ya muda mrefu. Meli hiyo ilirudishwa ndani ya Bahari ya Atlantiki kwa wiki kadhaa, huku nyasi ndefu za baharini na jamii ya kaa wengi wakubwa waliojaa mbele ya kuta za meli wakirudisha nyuma maendeleo ya hiyo meli, ili isiende mbele kirahisi.

Mara saba nahodha wake alipunga mkono kwa meli zinazopita kuomba maji na mahitaji mengine. Joseph Bates aliamini hadi wakati wa kifo chake kwamba sala ya yule mpishi mweusi, sala ya kwanza aliyopata kusikia kwenye meli, ilikuwa sababu moja iliyowafanya mwishowe wafike nyumbani salama. Mmoja baada ya mwingine watoto wake watano walizaliwa, ila wa kwanza alikufa akiwa mchanga, hivi ndivyo wakazi wa familia yake walivyoongezeka kwenye nyumba ya akina Bates; wakati huohuo, vileo, divai, lugha chafu au matusi na tumbaku viliondolewa kimoja baada ya kingine kutoka kwa maisha binafsi ya Joseph Bates. Alitafakari zaidi kuhusu wokovu.

Prudy (kama alivyomwita mke wake) aliweka Agano Jipya kwenye kifua cha baharia wake. Kitabu hiki Kizuri kilimvutia sana nahodha. Mwanzoni, akiwa amehuzunika juu ya nafsi yake, hata alifikiria kujidhuru kwa kuruka juu ya bahari. Kule katika ufuo wa Amerika Kusini alipanda mti ili kujilinda na nyoka na akaomba kwa sauti. Amani ilikuwa ikinyemelea taratibu moyo wake, lakini imani kamili katika Mungu bado ilikuwa imemchenga. Baada ya kurudi nyumbani huko Fairhaven alianzisha ibada ya kawaida ya familia na kuanza kuhudhuria kanisani. Katika ujana wake, kabla ya kwenda baharini, alikuwa ametoa moyo wake kwa Mungu na alihudhuria mikutano ya maombi kwa furaha.

Uzoefu huo sasa ulikuwa wa muda mrefu uliopita na alikuwa anaanza upya tena maisha haya ya imani. Mara moja hofu yake ikaondoka na furaha ikaingia kwa kasi. "Ulimi wangu ulilegezwa ili kumsifu Mungu. ... Mashaka yote na giza kuhusu wongofu wangu na kukubalika kwangu na Mungu, vilipita kama umande wa asubuhi, na amani kama mto, kwa wiki na hatimaye miezi ilitawala moyo na akili yangu." Ndani ya merikebu katika siku hizi bora zaidi alimwomba Mungu kwa maandishi, "Ee Bwana,

nakuomba, nitumie kama chombo cha utumishi wako; unihesabu miongoni mwa watu Wako wa pekee." Katika miaka ijayo, maombi haya yangetimizwa kwa njia ya ajabu. Siku ya ubatizo wake alianza kuandaa chama na jamii inayozingatia kiasi (temperance), ya kwanza katika Amerika ya Kaskazini.

Katika safari yake ya mwisho, iliyofuata mara moja, aliamuru watu wake, wageni kutoka Boston, waepuke matusi yote, wajiepushe kabisa na pombe, na kushika Sabato (ambayo kwake wakati huo, bila shaka, ilimaanisha Jumapili). Walifurahia safari isiyo na ugomvi sana katika kazi zao. Punde si punde, meli nyingine arobaini na baadaye meli sabini na tano kutoka New Bedford na Fairhaven zilikuwa zikifuata mfano uliowekwa na Bates na watu wake. Mnamo 1828, baada ya miaka ishirini na moja baharini, Joseph Bates alistaafu kutoka taaluma ya nahodha wa meli na kuuza meli yake. Alikuwa amemwahidi Prudence mkewe, kwamba angeishi na kutulia nyumbani sasa, akiwa amejiwekea akiba ya $10,000.

Inaonekana alikuwa amefikia lengo lake. Kulikuwa na sababu nyingine ya kustaafu. Alitaka kupata nafasi zaidi za kumshuhudia Bwana. Alipokuwa akiendeleza shughuli ya shamba la hariri na kuuza mali zisizohamishika, alikuwa mshiriki hai wa kanisa la ndani la Christian Connection na wa jamii kadhaa za mageuzi/matengenezo ya kiroho, ikiwa ni pamoja na kikundi cha wapinga utumwa (wakomeshaji utumwa—antislavery or abolitionist group). Lakini shamba lake la hariri lilipokuwa likianza kuzalisha mali vizuri, alisikia mahubiri ya kwanza ya Wafuasi wa Miller na mara akajiingiza pamoja na kila kitu alichokuwa nacho katika harakati za marejeo ya Masihi.

Akiwa amekwisha kufanya kazi tayari na J. V. Himes katika kufundisha sababu za kuwa na kiasi katika miaka ya 1820, alivutwa haraka katika uongozi wa Waadventista. Aliongoza moja ya mikutano yao mikuu-General Conference. Mnamo 1843 Bates aliungana na H. S. Gurney, mhunzi mwenye nguvu, rafu-rafu na mwenye sauti nzuri ya kuimba, kwa ziara ya uinjilisti kwenye Kisiwa cha Kent karibu na pwani ya Maryland. Kufikia wakati huu alikuwa ameachana na harakati za ukomeshaji wa biashara ya utumwa, akiamini marejeo ya pili ndiyo jibu pekee la ufanisi kukomesha utumwa. Alitaka sasa kuwaongoza watumwa kwenye uhuru katika Kristo. Lakini wamiliki wa watumwa wakamsalimu kwa kumtilia shaka.

Mmoja wao alimwambia "Ninaelewa kuwa wewe ni mtu wa harakati za kukomesha utumwa, na umekuja kuchukua watumwa wetu." "Ni kweli nimekuja kuwachukua watumwa wako - na wewe pia!" alijibu Bates. "Nataka ninyi nyote mwokolewe." Mtu huyu mkali na mkorofi alikatiza mkutano na kutishia kuamsha umati wa watu na kuwaweka juu ya farasi yeye na Gurney na kuwatoa nje ya mji kupitia uzio wa reli. Bates alijibu kwa upole, "Ikiwa utaweka matandiko juu ya farasi, tungependelea kupanda farasi kuliko kutembea." Wasikilizaji wake walicheka na kumfanya yule mtu

mkorofi aketi. Bates na "mwinjilisti wake mwimbaji"waliendelea kuwatafuta waongofu wengi kutoka kwenye kundi la watu weusi na weupe kwa namna sawa.

Kabla ya masika ya 1844, aliuza shamba lake na mali isiyohamishika yaani ardhi na majumba, na alilipa madeni yake kwa ajili ya marejeo ya Masihi wake, na akaendelea kutoa karibu mali yake yote iliyobaki kwa ajili ya kazi hiyo. Prudence mkewe alipopinga kwamba hakuwa na busara katika matumizi ya mali, alijibu kwa ujasiri, "Bwana atatoa." Ingawa Bwana hakuja kama ilivyotarajiwa, aliipatia mahitaji familia ya Bates, mara nyingi kwa njia zisizotarajiwa. Jumanne, Oktoba 22, 1844, ilimkuta Joseph karibu hana hata senti, na bila mwanawe wa pekee.

Kijana wake aliyechagua kufuata matukio ya kumfurahisha ya ujana kuliko usadikisho na imani ya babaye ya Ukristo, kijana huyu, Mdogo wa miaka kumi na minne, alisafiri baharini kwa meli inayovua nyangumi siku ya Jumatatu, Oktoba 21. Katika miaka yake ya ishirini, Joseph mdogo (junior) alijeruhiwa na nyangumi; Na alipofika miaka thelathini, alikufa baharini. Siku moja baada ya Oktober 22, 1844, siku ya kukatishwa tamaa kukubwa, ilimkuta Kapteni Bates akiwa ameaibika sana. Kabla ya hapo, alikuwa mwanajamii anayeheshimika sana, na aliwataka majirani zake kujiandaa kwa ajili ya marejeo ya pili. Sasa walimdhihaki na kumzomea mitaani hadi akatamani ardhi ipasuke na kummeza. Upesi alielewa hilo, hata hivyo, na kujihesabu kuwa miongoni mwa Waadventista ambao walitumaini kuwa hesabu zao hazikuwa sahihi na kwamba Yesu bado angekuja hivi karibuni.

Tayari tumeona kile kilichochukua sehemu ya maisha na muda wake katika 1845 na 1846. Aliikubali Sabato kutoka kwa Preble na Biblia na nuru mpya kuhusu Patakatifu iliyogunduliwa na Edson, Crosier, na Hahn. Alisadikishwa mwishoni mwa 1846 kwamba Ellen White alikuwa nabii wa kweli. Kisha akaendelea kuwa, pamoja na James na Ellen White, mmoja wa viongozi watatu wa juu katika vuguvugu lililokuwa linaibuka la Waadventista Wasabato. Akiwa amezoea kusafiri safari zisizo na kikomo kwenye bahari kuu, Bates msafiri wa baharini asiye na kituo, na asiyehitimisha safari zake, aliendelea kusonga mbele. Hadi 1852 alipotafuta kuleta nuru mpya kwa wafuasi wa Miller kutoka Maine hadi Michigan; baada ya hapo alisafiri mbali zaidi, akishuhudia kwa yeyote ambaye angesikiliza, kuanzia kwa wasafiri waliochoka kando ya barabara hadi kwa gavana (W. H Crapo, wa Michigan) katika jumba lake la kifahari.

Treni wakati huo zilionekana kama ndege leo. Alitumia hizi nyakati fulani, akiwagawia abiria machapisho. Wakati mwingine alitembea; hii ilikuwa njia ya nafuu kwa gharama, na angeweza kukutana na watu wengi kwa njia hiyo. Wakati fulani, akiwa hana pesa za nauli, alilazimika kutembea kwa miguu. Mara nyingi alitembea urefu wa maili nyingi kwenye theluji ili tu kutafuta familia moja ili

aishuhudie ile Kweli. Kwa nyakati tofauti alifika kwa wakati ili kumwombea mtoto aliyekuwa mgonjwa mahututi na kuona amepona.

Mara moja, baada ya miezi kadhaa, barabarani, alirudi Fairhaven, na kuanza safari ya mbali tena kutembelea "waumini waliotawanyika" baada ya kukaa wikendi moja tu nyumbani! (Bi. Bates kwa miaka mingi alikuwa akiandamana na mama yake mjane na kisha binti yake aliyeolewa). Ingawa aliweza kushikilia umati mkubwa wa watu wenye matamanio ya kusikia mada aliyowakilisha, utaratibu wa kawaida wa Bates ulikuwa kuhutubia vikundi vidogo-vidogo katika makanisa, shule za umma au serikali, au nyumba zilizo mashambani na vijijini. Watu waliopendezwa na masomo yake ya Biblia, waliwaalika majirani zao kutoka maili nyingi huko vijijini, ili kumpa Bates mahali pa kulala siku moja au mbili—kisha mara nyingi waliongeza idadi ya washika Sabato wapya wachache kama matokeo ya wito wake.

Hali ya hewa ilikuwa ni kikwazo kidogo tu kwa mtu huyu ambaye alikuwa amekabiliwa na dhoruba za bahari. Alipokuwa na umri wa miaka sitini na tano, alibatiza watu saba mtoni, wakiwa wamesimama kwenye shimo lililokatwa mahali penye futi tatu za barafu ili wapate kuyafikia maji. Joto lilikuwa digrii thelathini chini ya sifuri (yaani $-30^0$ C). Akiwa amebarikiwa na nguvu za asili na busara na alikuwa ni mkubwa kwa James White karibia miaka thelathini akiwa mwandamizi wa James White, Bates alichaguliwa kuwa mwenyekiti wa mikutano mingi muhimu zaidi iliyofanywa na Waadventista Washika Sabato, zoezi ambalo liliendelea hadi kuundwa rasmi kwa Konferensi Kuu (GC) mnamo Mei 1863.

Hivyo nahodha wa meli aliendelea na uongozi hata katika safari yake ya maisha ya imani. Mwanamatengenezo huyu aliendelea kufanya matengenezo. Kwa maboresho na matengenezo kwenye njia yake ya mtindo wa maisha ambayo aliyafanya katika miaka ya 1820, pia alikuwa kufikia 1844 aliongeze amengine mkakati huu wa afya katika maisha yake kama vile kuacha kutumia chai, kahawa, nyama, na vyakula vingine visivyofaa kwa afya. Akipendelea ashuhudie kwa mfano, Bates alisema machache sana kuhusu mlo wake hadharani hadi maono ya matengenezo ya afya yalivyotolewa kwa Ellen White ya 1863. Baada ya hapo alizungumza kwa uhuru zaidi juu ya somo hilo. Watu walipomtazama tu, walibidishwa kumsikiliza! Alikuwa mgonjwa mara chache na kwa muda mfupi sana tu, katika maisha yake yote. Aliweza kusema akiwa na miaka sabini na tisa, "Sina maumivu kabisa!"

James White, ambaye mwenyewe ni mara chache sana alikuwa mzima, angeweza kusema kuhusu Bates, "Angesimama akiwa amenyoka wima kama mnara na angetembea kando ya barabara kwa wepesi kama mbweha." Baada ya kujitia ile nidhamu kama afisa wa meli, ili kudumisha kumbukumbu inayoendelea kuhusu kazi yake na wafanyakazi wake, Bates licha ya safari zake za kila mara, aliweza kutuma mamia ya ripoti katika makala zilizoingia katika ofisi ya uchapaji ya Review and

Herald. Watu waliojiunga, ambao wengi wao alikuwa amewabatiza yeye binafsi, walimshukuru kwa ajili ya kazi yake. Uwezo wake huu kama mwandishi unaturudisha pale tulipoanzia.

Bates, nahodha mcha Mungu na Mtunza Jumapili, yaani siku ya kwanza ya juma, akawa Mwadventista Msabato mcha Mungu zaidi, aliyeishika siku ya Saba ambayo ndiyo ipo katika amri ya nne ya Mungu (Kutoka 20:8-11). Na, kama tulivyoona, kilikuwa ni kijitabu alichoandika mwaka 1846 kiitwacho “The Seventh Day Sabbath, A Perpetual Sign—Sabato ya Siku ya Sabato Alama ya Mungu ya Kudumu” kilichowaongoza James na Ellen White, na wengine wengi, kugundua Sabato ya kweli. Mnamo 1855 alimweleza J. N. Loughborough uzoefu aliokuwa nao alipokuwa akiandika moja ya vitabu vyake vitatu kuhusu siku ya Sabato.

Ni kisa maarufu na kinafaa kusimuliwa tena. Kabla ya maendeleo ya migodi ya fedha ya magharibi mwa nchi, katika miaka ya 1870, fedha ilikuwa bidhaa adimu nchini Marekani, na fedha/sarafu za Kiingereza na Kihispania ndizo zilitumika kwa kawaida. Wakati tukio katika kisa hiki kilipotokea, akiba ya fedha za Bates ilipungua hadi shilingi ya York.

Hebu turejelee upya kisa chetu kama  alivyokuwa anakisimulia yeye mwenyewe Bates: *"Nilipokuwa nikiomba siku moja, hakika usadikisho ulinijia moyoni kwamba ni lazima niandike kitabu kuhusu Sabato na kwamba Mungu atanipa mbinu na fedha. Niliketi kwenye meza yangu huku nikiwa na Biblia yangu na konkodansi, yaani ufafanuzi wa Biblia na nikaanza kufanyia kazi hili na baada ya kama saa moja hivi, mke wangu Bi. Bates akaja na kusema, 'Joseph, sina unga wa kutosha kuoka.' "Kuna kitu gani, ambacho hakipo nyumbani ambacho unakihitaji ' niliuliza. " 'Takriban ratili nne ya unga,' akajibu.*

*"Nilitoka nje na kununua unga, nikaleta nyumbani, na kuketi tena kwenye dawati langu. Punde Bibi Bates aliingia tena na kusema, 'unga huu umetoka wapi?' " 'Kwa nini,' niliuliza, 'hautoshi?' "'Lakini sielewi,' alisema. 'Je, wewe, Kapteni Bates, mtu ambaye alisafiri kwa meli kutoka New Bedford hadi sehemu zote za dunia, umetoka na ukanunua ratili  nne tu za unga?' "Hadi sasa Bi. Bates [ambaye bado hakuwa mshika Sabato] hakujua hali yangu halisi ya kifedha. Kwa kutambua kwamba lazima sasa nimjulishe jambo hilo, nilisema kwa utulivu, 'Mke wangu, kwa kununua chakula hiki, nilitumia pesa ya mwisho, niliyokuwa nayo duniani.'*

*"Bi. Bates alianza kulia kwa uchungu na kuuliza, 'Tutafanya nini?' "Nilisimama kwa miguu yangu kana kwamba nilikuwa nahodha bado nikiongoza chombo changu na*

*kusema, 'Nitaandika kitabu na kueneza Ukweli wa Sabato mbele ya ulimwengu.' "'Lakini tutaishije?' " 'Bwana atafungua njia.' “ ‘Oh, Bwana atafungua njia! Bwana atafungua njia!' Hivyo ndivyo unavyosema kila mara.' Na akaangua kilio na kutoa machozi, kisha akatoka chumbani.*

*"Niliendelea kuandika kwa muda wa nusu saa, wakati hisia iliponijia moyoni kwenda posta. Nilikwenda, na hakika kulikuwa na barua—lakini ilihitaji malipo ya posta ya senti tano kwani aliyetuma hakuweka stempu. Ilininyenyekeza kumwambia msimamizi wa posta, Bw. Drew, rafiki yangu, kwamba sikuwa na hata senti tano, lakini alikuwa mwenye fadhili na kusema, 'wewe chukua tu, na ulipe wakati mwingine.' 'Hapana,' nilijibu, 'Sitachukua barua hadi malipo ya posta yalipwe. Nina maoni, hata hivyo,' niliendelea, 'kwamba kuna pesa ndani ya hii barua. Je, unaweza kuifungua? Ikiwa kuna pesa humo, toa ya posta kwanza.' "Msimamizi wa posta alitii —na akapata hundi ya dola $10. Ilitoka kwa mtu ambaye alisema Bwana alikuwa ametia mguso mkali na kwa nguvu sana akilini mwake kwamba Kapteni Bates alihitaji pesa ambazo alinitumia mara moja.*

*"Kwa moyo mwepesi nilienda kwenye duka la chakula, na kununua pipa la unga kwa $4.00, na viazi, sukari, na vitu vingine muhimu. Nilipomweleza muuza duka ambaye alikuwa na huduma ya kuvipeleka kwa farasi nyumbani, kwa kumweleza mahali ambapo vyakula vilipaswa kupelekwa, nilimpa tahadhari, 'Pengine mwanamke huyo mwenye nyumba atakwambia hizi bidhaa sio zake, lakini wewe usiweke umakini kwa kile atakachosema cha aina hiyo. Wewe pakua tu bidhaa kwenye kibaraza cha mbele.' “Kisha nilienda kwa Benjamin Lindsey, mchapishaji, na kupanga kuchapisha kitabu changu kwa makubaliano kwamba ningelipia kazi hiyo haraka, yaani mara tu nitakapopokea pesa, na kwamba vitabu hivyo havingekuwa vyangu hadi gharama yote ilipwe.*

*"Nilijua kwamba hakuna mtu anayenidai chochote, lakini nilihisi kuwa ni wajibu wangu kuandika kitabu na kwamba Mungu angesonga mbele ya watu kutuma fedha. Nilinunua karatasi na kalamu kwa ajili ya kutoa muda ili bidhaa za chakula zifike nyumbani kabla mimi sijafika. Kisha nikaendelea, kwa kuingia ndani ya nyumba kimya kimya kupitia mlango wa nyuma, na kuketi tena kwenye kazi yangu. Punde Bibi Bates alikuja kwenye chumba changu na kusema kwa furaha, 'Joseph, tazama kwenye ukumbi wa mbele! Bidhaa hizo zimetoka wapi? Nilimwambia mtu aliyevileta hapa na kwamba siyo vitu vyangu, lakini alisisitiza juu ya kuvishusha*

*hapa. "'Naam,' nikasema, 'nadhani ni sawa.' "'Lakini Je, vilitoka wapi?' "'Bwana Ndiye aliyevituma.' "'Bwana alivituma. Bwana Ndiye aliyevituma, ndivyo usemavyo siku zote Bates!*

*"Nilimpa barua niliyokuwa nimepokea. Aliisoma na akalia tena, lakini kilio tofauti sana na kile cha kwanza. Kisha akaniomba msamaha kwa kukosa kwake imani. "Na hakika pesa ziliingia, nyakati fulani kutoka kwa watu ambao sijawahi kukutana nao. Kwa kweli, kiasi cha mwisho cha fedha tulichohitaji—sikujua kilitoka wapi au kitatoka wapi—- nacho kilifika siku ile ile ambayo vitabu vilikamilishwa kuchapwa."*

Ingawa Joseph Bates hakuwahi kujua malipo hayo ya mwisho yalitoka wapi, J. N. Loughborough, 1884, aligundua kwamba H. S. Gurney, rafiki mwimbaji wa Joseph Bates na mhunzi wa Kisiwa cha Kent, waliyesafiri naye, ndiye aliyekuwa ametoa. Wakati Gurney alikuwa katika safari hiyo, mwajiri wake alimfukuza kazi na kwa hasira akakataa kumlipa ujira wake wa nyuma aliokuwa akistahili. Sasa, kwa wakati ufaao, Bwana alimwongoza mwajiri kujutia jambo hilo. Kwa majaliwa ya Mungu katika kumsaidia Kapteni Bates kueneza Neno kuhusu Sabato katika mwaka 1846 na 1847 na kuimarishwa kwa Sabato ya awali Gurney alimtumia pesa Bates.

Hili liliwaimarisha na kuwaweka Waadventista katika imani, baada ya kuthibitishiwa sana kwamba Mungu alikuwa pamoja nao. Fataki iliwasha baruti. Nuru mpya ya Siku takatifu ya Mungu ilikuwa inawajia juu yao

*VIDOKEZO:*

*1. Historia hii ya Bates imetolewa hasa kutokana na maandishi yake mwenyewe, pamoja na wasifu wake, ambao ulichapishwa tena na Chama cha Uchapishaji cha Kusini mwaka 1970; pia kwenye Godfrey T. Anderson, Outrider of the Apocalypse (Mountain View, Calif.: Pacific Press Publishing Association, 1972); na 181 Spalding, Origin and History, juz. 1, ukurasa wa 111- 130;*

*2. Pia imechukuliwa kutoka kwa Loughborough, The Great Second Advent Movement, ukurasa wa 251-254. Loughborough anasema tukio hilo lilitokea wakati Bates akiandika kitabu chake cha kwanza cha Sabato mnamo 1846; lakini James White, Matukio ya Maisha, uk. 269, akisema Bates alifilisika hadi kubaki na shilingi ya York alipokuwa akiandika kitabu chake cha tatu kuhusu somo hilo katika vuli ya 1847. Inaonekana kwamba kitabu hiki cha tatu kilikuwa "A Vindication of the Sabbath and The Commands of God: With a Further History of God's Peculiar People". , kutoka 1847- 1848 (New Bedford: Press of Benjamin Lindsey, 1848), ambayo ilionekana Januari, 1848, na kwa hakika ilikuwa imechukua miezi kadhaa kujiandaa. Godfrey T. Anderson wa Chuo Kikuu cha Loma Linda hivi majuzi aligundua nakala katika maktaba ya Jiji la Boston; 3. Review and Herald, Juni 28, 1923, ukurasa wa 9, 10. Tunaweza*

*kusema kwamba Mungu aliweka pesa hizo “katika escrow juu ya kukata tamaa kusaidia kuanza kusambaza ujumbe wa malaika wa tatu," Spalding, Origin and History, vol. 1, uk. 401*

# SURA YA 13
# UJUMBE WA MALAIKA WA TATU

Walipokutana na mzee Bates kwa mara ya kwanza mapema mwaka wa 1846, Ellen Harmon hakuamini katika Sabato ya kweli, yaani Jumamosi ambayo Joseph Bates alikuwa akifundisha. Wala nahodha hakuamini maono ya kinabii ya Ellen Harmon. Ellen alimwona Bates kama baba, kwani alikuwa amemzidi umri kwa zaidi ya miaka thelathini, hivyo akawa kama baba yake wa pili na mtu mkarimu kwake. Hata hivyo, alishangaa sana kwamba Mkristo wa kweli hivyo kwa nini anaweka mkazo mkubwa tu kwenye hiyo amri ya nne. Hivi mzee huyu hakujua kwamba kulikuwa na amri zingine tisa?, (alishangaa).

Kwa upande wake, Bates alimkubali Ellen kama kijana Mkristo mzuri sana, na japokuwa hakupata chochote kilicho kinyume na Maandiko katika maono yake, "alihisi hofu na kujaribiwa sana kuhusu mtu kupata maono" na maandishi na maono ya binti huyu, alifikiri kwamba yalitokana tu na hali yake ya afya iliyodorora. Alimhoji yeye na dada yake kwa karibu nje ya mikutano ya hadhara. Mnamo Novemba mwaka huo alikuwa na maono kuhusu nyota na sayari. Alijua Ellen alikuwa hajui somo hili, ambalo yeye, kama baharia, alijua mengi kuhusu nyota na sayari. Alivutiwa sana na maono yake, kiasi kwamba hatimaye alikubali kipawa chake kuwa Roho ya Kweli ya unabii.

Wakati huohuo, Waadventista, Wafuasi wa Miller, ambao walikuwa wamesimama kwa umoja kwa utukufu katika imani yao kwamba Kristo angekuja kutakasa “Patakatifu” pa dunia na kanisa mnamo Oktoba 22, 1844, walikuwa wamegawanyika katika matabaka kadhaa tofauti. Idadi kubwa ilikuwa imeikataa dhana hiyo ya marejeo ya Yesu ama kurudi kwenye madhehebu yao ya awali au kuiacha imani ya Kikristo. Kinyume chake, idadi ndogo tu lakini yenye nguvu ya Wamiller ilichagua kuamini kwamba walikuwa sahihi kuhusu wakati wa kurudi kwa Kristo. Wengine walihitimisha kwamba ni sawa kabisa kwamba Yesu alikuwa amekuja tarehe 22, Oktoba, lakini alikuja bila kuonekana na kwa waumini wote ila wale wa kweli tu— yaani kwao wenyewe. Kulingana na watu hawa, Yesu alikuwa amesafisha Patakatifu Pake (nafsi zao wenyewe) kutokana na kila doa la dhambi, na matokeo yake kwamba wasingeweza kutenda dhambi tena.

Kwa mshangao wake mkuu, Ellen aliitwa na Bwana kusaidia kuwaongoza watu hawa kutoka katika upotofu wao. Alipoona kwamba madai yao ya utakatifu yaliambatana na upumbavu na hata ukosefu wa maadili kama vile uasherati, alisitawisha chuki kali kwa kila aina ya ushupavu wa kidini au misimamo iliyopitiliza. Kwa miaka iliyofuata mara nyingi alionya watu dhidi ya kudai kuwa huru kutoka kwenye dhambi. Kundi kubwa la Wamiller (Takribani 40,000 au zaidi) waliendelea kuamini kwamba Kristo

angekuja kulisafisha kanisa na dunia mwishoni mwa zile siku 2300, lakini walisema walikuwa wamekosea ile tarehe waliyoiweka mara ya kwanza katika mahesabu yao (457 KK).)

Waadventista hawa walikusanyika tena mnamo Aprili 1846 kwenye mkutano huko Albany, New York. Kwa miongo mingi waliendelea kuweka tarehe mpya za kurudi kwa Kristo. Bado idadi yao iliendelea kuongezeka na takriban watu 30,000 kwa idadi, kama Kanisa la Kikristo la marejeo, hawa walikuwa ni miongoni mwa Waadventista waliokatishwa tamaa. Ilikuwa katika hili kundi la waamini ambapo nuru ilitolewa kwa Edson na Crosier (Nuru juu ya Patakatifu), na, Ellen Harmon (pamoja na nuru yake juu ya Patakatifu na roho ya unabii), na Bates (pamoja na nuru yake juu ya Sabato) na kisha wakaweka juhudi zao.

Kabla ya mwisho wa mwaka 1846 makundi kadhaa yenye mshikamano na umoja ya waumini katika Sabato, Patakatifu, na Roho ya Unabii yalikuwa yameundwa katika maeneo yaliyotawanyika karibu na New England na jimbo la New York huko Fairhaven na Port Gibson, na hataa katika mji wa Topsham, Maine, hata chini ya uongozi wa mhandisi wa wilaya aitwaye Stockbridge Howland na huko Dorchester, Massachusetts, kusini mwa Boston, chini ya Otis Nichols, mwandishi anayenakshi picha na michoro (lithographer).

Pengine Waadventista wa kwanza kukubali ufunuo wote wa mambo matatu yaani wa Sabato, Patakatifu, na Roho ya Unabii ilikuwa familia ya Otis Nichols. Watu hawa waliosimama imara, walimkaribisha Ellen na dada yake Sarah mwaka wa 1845, wakati wote walikuwa watunza Jumapili. Waliikubali Sabato kutoka kwa Joseph Bates miezi mingi kabla ya Ellen kufanya hivyo. Labda tuwape watu hawa heshima ya kuitwa “Waadventista Wasabato” wa kwanza.

Kwa bahati mbaya Otis Nichols, alimwandikia William Miller barua mnamo Aprili, 1846, akimhimiza kumkubali Dada Ellen kama nabii wa Mungu na nuru yake mpya juu ya Patakatifu kama Kweli ya Mungu. Miller, kwa huzuni alisema, alikuwa mzee sana na amechoka kuelewa mambo. Hatuwezi kamwe kuamua kwamba ni nani walikuwa Waadventista Wasabato wa kwanza. Tuachane na hayo basi, ila, James White na Ellen Harmon walifunga ndoa huko Portland mnamo Agosti 30, 1846. Wakiwa wametengwa na ushirika wa kanisa kwenye makanisa yao ya zamani kwa sababu ya imani yao ya marejeo ya Yesu mara ya pili, waliweka nadhiri zao za kiapo cha ndoa kwenye ofisi za hakimu wa serikali.

James alikuwa amefanikiwa sana kama mwinjilisti wa Kiadventista. Ni yeye ndiye ambaye ziara yake ya uinjilisti wa wiki sita ilirejelewa katika sura ya pili wakati wa baridi kali ya theluji, mkutano huu aliofanya ulisababisha watu 1000 kuongoka. Alipotembelea Portland mara kwa mara alivutiwa na ripoti kwamba Dada Ellen

alikuwa akialikwa na wachungaji mbalimbali kushuhudia katika makanisa yao. Baada ya kukatishwa tamaa pale 1844, alikutana na Ellen tena kuhusu wakati alipokuwa na maono ya "Bwana arusi." Baada ya hapo James na Ellen walisafiri pamoja mara kwa mara, wakiongozwa na watu wazima kama vile, Sarah Harmon au Louisa Foss au wakati mwingine watu zaidi ya sita, ili kuwatia moyo Waadventista waliokata tamaa.

Sasa – walikuwa wameoana wakiwa ni kama hawana hata senti. Bw. na Bi. Robert Harmon, ambaye alikuwa kakaye Ellen, walikuwa wamerudi Gorham, na waliwaalika kuishi nyumbani mwao, nao wakakubali kwa furaha. Mara moja, James na Ellen walisoma kitabu kipya cha Joseph Bates kuhusu siku ya Sabato na Sabato ya Kweli, wakakilinganisha kitabu kile na Biblia, na wakagundua kwamba siku ya saba kwa hakika ni Sabato ya Kweli ya Mungu. Miezi michache baadaye ilikuwa baada tu ya Bates kukubali maono yake - aliugua sana kiasi kwamba watu wengine walidhani angekufa. Wazazi wake, dada zake, na mume wake waliomba kwa bidii, lakini hapakuwa na nafuu yoyote hadi Otis Nichols alipomtuma mwanawe Henry kutoka Dorchester kuwaelezea hofu yao kwao.

Wakiwa na Henry pale, walifanya awamu nyingine ya maombi, na Henry Nichols kijana mdogo, aliguswa moyo sana kiasi kwamba aliinuka kutoka magotini pake, naye akatembea ndani ya chumba, na kuweka mkono wake juu ya kichwa cha Ellen. "Dada Ellen," akasema, "Yesu Kristo anakuponya." Siku iliyofuata Ellen alikuwa mzima vya kutosha kupanda farasi na kwenda maili thelathini na nane pamoja na James kwenye mkutano. Na kwa muda mrefu baadaye alijisikia vizuri kuliko alivyokuwa kwa miaka kadhaa. Mtoto wao wa kwanza alipozaliwa, mnamo Agosti 26, 1847, walimwita Henry Nichols White ili kumkumbuka kijana huyo na msimu huo uliowaletea furaha.

Wakati huo huo wa msimu wa majani kupukutisha wa 1846-47, baada ya kuwatembelea Edson na Crosier huko Port Gibson na kutazama Ellen akiwa na maono yake juu ya unajimu huko Topsham, Bates alienda nyumbani kwake Fairhaven kuhakiki na kupanua kitabu chake cha kwanza kuhusu "Siku ya Sabato," ambacho fedha za kukiandaa zilikuwa karibu kwisha ila kilikuwa na soko kubwa. Katika toleo la pili la "The Seventh Day Sabbath, A Perpetual Sign—Sabato ya Siku ya Saba, Agano la milele la Mungu na watu wake" (Kutoka 31:16) Bates aliendeleza ufafanuzi wa wazi wa ujumbe wa malaika wa tatu akiwa na nuru angavu zaidi. Pia alisitawisha wazo la Hiram Edson kwamba labda Ufunuo 11:18, 19 ilikuwa inatimizwa wakati huo.

Alibainisha kwamba Preble, Cook, na wengine, akiwemo yeye mwenyewe, walikuwa wamevutiwa kuchapisha nuru kuhusu hoja ya Sabato. Naye alidokeza kwamba huenda sababu ilikuwa kwamba wakati "malaika wa saba alipoanza kupiga

baragumu yake” mwaka wa 1844, “hekalu la Mungu lilifunguliwa mbinguni,” na “Sanduku la Agano Lake” (lenye Amri Kumi) lilikuwa likionekana wakati huo. Bates alikuwa mnyenyekevu kuhusu hatua hii ya pili. "Sisemi kwamba maoni haya ni chanya," alionya, "lakini nadhani ni hoja yenye nguvu." Kufikia mapema majira ya kuchipua, hata hivyo, mashaka yake yaliondolewa.

Ellen alikuwa amepokea maono mawili ya kushangaza na ya waziwazi kabisa kuhusu Sabato. Maono ya kwanza aliyapata Machi 6, 1847, na maono ya pili Aprili 3, 1847. Haya yalifanana vya kutosha kiasi kwamba unaweza kuyaelezea yote mawili kwa kusimulia kisa cha maono ya pili peke yake. Hebu tuweke fikra zetu kwenye tukio hilo, lililoundwa upya kutoka kwenye maelezo ya awali. Karibu na majira ya kuchipua mimea, alikuwa njiani kuelekea Topsham, Maine. Bila shaka theluji ilikuwa ikiyeyuka, maua yalikuwa yakichanua, na ndege wadogo walikuwa wakiwinda wadudu kwenye nyasi. Ndani ya nyumba huko mjini Stockbridge Howland, waumini walikuwa wamepiga magoti katika sala siku ya Sabato, Aprili 3, wakitafuta nuru na kweli ya Mungu.

Mara moja Ellen, kwa sauti yake ya utulivu,  na ya kupendeza, akalia, "Utukufu! Utukufu!" Kila mtu alijua alikuwa na maono mengine. Hali ya wakfu wenye kusisimua ilitanda juu ya kikundi. Tayari maombi yao yalikuwa yakijibiwa. Walijua kwamba maono yake yakiisha, Ellen angekuwa na jambo la msaada la kuwaambia. Akiwa bado kwenye maono Ellen aliinuka na kuiendea meza ambayo walikuwa wameweka Biblia zao na vitabu vingine kabla ya kupiga magoti.  Miongoni mwa watu waliokuwa katika kundi hilo waliinuka pia kutoka magotini mwao na kuketi kwenye viti vyao kutazama na kuomba kimoyomoyo baraka za Mungu. Bila kusita, Ellen alichukua Biblia na kuinua juu ya kichwa chake. Aliiweka mahali pale ambapo hangeweza kuisoma, alianza kushughulikia ahadi za Biblia.

Kisha akamwendea mtu aliyehitaji kutiwa moyo na Andiko hilo, akanukuu mstari huo huku akitazama mbinguni, na kuikandamiza Biblia kwa upole kifuani mwake. Mtu huyo alipochukua Biblia ili kujisomea kifungu hicho, Ellen alirudi mezani kwa sasa, na akachukua Biblia nyingine, na kurudia utaratibu huo kwa ajili ya mtu mwingine tofauti. Alifanya hivi mara kadhaa. Kisha akaketi na maono yakaendelea. Baada ya muda alivuta pumzi kwa nguvu, pumzi yake ya kwanza tangu maono hayo yaanze. Kila mmoja alikuwa na shauku ya kutaka kujua atasema nini. Alitazama kuzunguka chumba huku macho yake yakijaribu kulizoea giza la dunia tena, baada ya mwangaza wa mbinguni.

"Je, unaweza kutuambia sasa kile Bwana amekuonyesha?" James aliuliza kwa sauti ya taratibu. "Ndiyo, naweza," Ellen alijibu. "Nimeona malaika akiruka kwa kasi kuja kwangu. Akanichukua upesi kutoka duniani hadi kwenye Mji Mtakatifu. Katika mji huo nikaona hekalu, ambalo niliingia. Kisha nikapita kwenye Patakatifu. "Yesu

akainua pazia na nikaingia ndani ya Patakatifu pa Patakatifu. Hapo niliona sanduku, lililofunikwa kwa dhahabu safi kabisa. Yesu alisimama kando yake. Ndani yake kulikuwa na mbao za mawe zilizokunjwa pamoja kama kitabu. Yesu akaifungua, naye alipofanya hivyo; Niliona Amri Kumi. Juu ya meza moja ziliandikwa amri nne na juu ya meza ile nyingine ziliandikwa amri sita. Zile nne kwenye mbao ya kwanza ziling'aa zaidi kuliko zile nyingine sita, lakini ile ya nne, yaani ile amri ya Sabato, iling'aa juu ya zote (Kutoka 20:8-11).

Sabato takatifu ilionekana yenye utukufu. Mng'ao wa utukufu wake, ulikuwa umeizunguka pande zote." Kwa sababu ya hili, watu walitazamana kwa mshangao, na Ellen aliona jinsi walivyoitikia. "Mimi pia nilistaajabu," alikubali. "Sikujua kwamba Sabato ilikuwa ya pekee sana machoni pa Mungu." Baada ya kupumzika akaendelea. "Nikaona kwamba Sabato takatifu ni, na itakuwa, ukuta unaotenganisha Israeli wa Kweli wa Mungu na wasioamini; na kwamba Sabato ni hoja kuu ya kuunganisha mioyo ya watakatifu wapendwa wa Mungu, wanaongojea."

Tena palionekana mshangao ukiendelea kughubika chumba kile. akasema: "Niliona ya kuwa Mungu ana watoto wasioiona na kuitunza Sabato. Hawakuikataa nuru iliyo juu yake. Na katika kuanza kwa wakati wa taabu, tulijazwa na Roho Mtakatifu tulipotoka na kuitangaza Sabato kikamilifu zaidi. Hili lilikasirisha makanisa na Waadventista wa majina tu, kwani hawakuweza kukanusha Ukweli wa Sabato. Kwa wakati huu wateule wa Mungu wote waliona wazi kwamba tulikuwa na Ukweli, nao walitoka na kustahimili mateso pamoja nasi." "Je, kulikuwa na kitu kingine chochote ulichoonyeshwa Ellen?" "Ndiyo, kilikuwepo," alijibu. "Ilikuwa kuhusu malaika wa tatu. Niliona kwamba anawakilisha watu wanaoipokea Sabato na kwenda nje kuuonya ulimwengu kushika sheria ya Mungu kama mboni ya jicho Lake. Nikaona kwamba tukiiacha Sabato, tutapokea chapa ya mnyama. Pia niliona," naye akatabasamu, "kwamba kwa kuitikia onyo hilo, watu wengi wangeikubali Sabato ya Kweli."

Ellen White aliandika maono haya mara moja, na baada ya siku chache Joseph Bates alikuwa na nakala elfu moja zilizochapishwa kama karatasi pana moja iliyochapishwa upande mmoja. Chapisho alililoiita "Neno kwa Kundi Dogo" Baadaye (mwaka 1851) alichapisha maono hayo katika kijitabu kiitwacho 'A Sketch of the Christian Experience and Visions of Ellen G. White (Uzoefu wa Kikristo na maono ya Ellen White).' Maono haya yanapatikana leo katika kitabu cha Maandiko ya Awali (Early Writings).

Waumini waliposoma maono ya Aprili 3, 1847, wengine walitatanishwa na walielewa kwamba baada ya wakati wa taabu kuu kuanza, rehema ya kila mtu itaondolewa na kesi zao kuamuliwa; wakasema "Itasaidia nini basi kuwahubiria watu Sabato wakati huo? Ellen White alielezea katika kitabu chake kinachofuata (sasa pia

kimejumuishwa katika Early Writings, angalia RohoYaUnabii.Org au MaarifaMtandaoni.Com): “Kuanza kwa wakati wa taabu au dhiki kuu,’ kulikotajwa hapa, hakurejelei kwenye wakati ambapo mapigo yataanza kumwagwa, bali ule muda mfupi kabla tu ya kumwagwa, wakati Kristo anapoingia katika Patakatifu. Wakati huo, wakati kazi ya wokovu inakaribia kufungwa, taabu itakuwa inakuja duniani, na mataifa yatakuwa na hasira, lakini yatazuiliwa ili yasizuie kazi ya malaika wa tatu. Wakati huo 'mvua ya masika,' au kuburudishwa kutoka kwa uwepo wa Bwana, kutakuja, na kutoa nguvu kwa sauti kuu ya malaika wa tatu, na kuwatayarisha watakatifu kusimama katika kipindi ambacho mapigo saba ya mwisho yatamwagwa.

Waadventista wa kwanza wa Sabato walivutiwa na utabiri kwamba walipaswa "kuitangaza Sabato kikamilifu zaidi." Kwa ukamilifu zaidi kuliko nani? Kikamilifu zaidi kuliko nini? Kikamilifu zaidi kwa njia gani? Umuhimu wa maswali haya hauwezi kuelezwa kwa kwa mkazo zaidi kama ilivyo. Huko nyuma katika mwaka 1847 jibu lilikuwa angalau hili: Walipaswa kuambatanisha na Sabato maana kubwa zaidi na uzoefu binafsi wa ndani zaidi kuliko Waabaptisti wa Kisabato waliokuwa nao katika siku zao au Wabaptisti wa Siku ya Saba ambao Waadventista walipokea Sabato kutoka kwao.

Wabaptisti wa Siku ya Saba na Wabaptisti wa Kisabato, Je, unakumbuka kuwa walikuwa wamesema kwamba Sabato ini jambo la lazima kwa sababu zifuatazo: Ni sehemu ya sheria ya maadili, Yesu na mitume waliiadhimisha, na kanisa lililoasi liliibadilisha katika kutimiza unabii. Je, kulikuwa na kosa lolote katika msimamo wao? La. Ilikuwa ya kibiblia, na ilionyesha heshima kubwa kwa utimizo wa unabii katika historia ya zamani. Lakini kulikuwa na mengi zaidi katika Ukweli huu wa Sabato kuliko haya. Na leo si jambo lisilo wazi -na sio lingine linalowatofautisha Waadventista Wasabato na washika Sabato wengine. Kuna njia tofauti kabisa ya kuishi na kufikiri inayohusika hapa, uelewa mpana zaidi wa kwa nini tunaishi na kile tunachotarajiwa kufanya na kuwa. Tofauti hiyo inahusisha ufahamu wa maneno ya Biblia kama vile “muhuri wa Mungu,” “jumbe za wale malaika watatu,” “alama ya mnyama,” “Patakatifu,” na “hukumu.”

Waadventista Wasabato wanakubali kimsingi yote ambayo Wabaptisti wa Siku ya Saba walifundisha, lakini kutokana na kujifunza Biblia wameongeza dhana za vitendo zinazohusiana na unabii wa siku za mwisho. Wale waanzilishi wachache wa Waadventista waliposoma jumbe za malaika watatu wa Ufunuo 14, walipata uthibitisho mzito kwamba wao wenyewe walikuwa wakichukua jukumu maalum kwa wakati maalum uliotabiriwa katika Maandiko. Wafuasi wa Miller katika miaka ya mapema ya 1840 walikuwa wamesaidia kutangaza ujumbe wa malaika wa kwanza kuhusu saa ya hukumu na injili ya milele (Ufunuo 14:6, 7). Katika mwaka 1843 na 1844 walikuwa wamesaidia kutangaza ujumbe wa malaika wa pili, kwamba Babeli

ilikuwa imeanguka na kwamba watu wa Mungu lazima kama sababu sababishi, watoke katika makanisa ambayo yaliwakilisha Babeli, (Ufunuo 14:8; 18:1-4 ).

Basi Mnamo 1846 waliona kwamba malaika wa tatu alitangaza ujumbe uliokita kwa Kristo kama kiini cha kushika Sabato, ya siku ya saba ya juma—Kweli ileile ambayo wakati huo ilikuwa ikivutia umakini wao (Ufunuo 14:9-12). Kwa mshangao wao walikuja kutambua kwamba walikuwa wakiitwa kutimiza ujumbe wa malaika wa tatu, kama vile walivyosaidia kutimiza ujumbe wa malaika wa kwanza na wa pili. Ugunduzi wao ulithibitishwa na maono ya Ellen White ya Machi 6 na Aprili 3, 1847. Hapa palikuwa na maendeleo makubwa zaidi ya Wabaptisti wa Siku ya Saba. Jambo hili lilitoa hisia mpya ya hatima na ufahamu kwamba walikuwa wakiitwa kutimiza unabii mwingine ambao wakati wake ulikuwa umefika.

Hisia yao ya kubainisha wakati iliimarishwa zaidi katika njozi ya Machi na Aprili kwa ishara/dalili kwamba tangu Oktoba 22, 1844, Yesu alikuwa amesimama kando ya Sanduku la Agano, akionyesha sheria na kufunua nuru ya utukufu kuhusu Sabato. Maono mengine yalikuja miaka miwili baadaye, mnamo Machi 1849, yakibainisha ujumbe maalum kwamba “wakati amri iliyong’aa ilikuja pamoja na umuhimu wake wote….. ulikuwa ni wakati mlango ulipofunguliwa katika Patakatifu pa Patakatifu [yaani, tarehe 22 Oktoba, 1844], ... mahali ambapo Yeye [Yesu] anasimama sasa karibu na Sanduku la Agano."

Katika maono mengine Ellen White aliona malaika akinukuu ujumbe wa malaika wa tatu, na alipokuwa akifanya hivyo, alielekeza juu kwenye Patakatifu pa mbinguni. Sasa, Yesu hatakaa katika Patakatifu pa Patakatifu milele. Kama tulivyoona katika sura ya tisa, mnamo Oktoba 1845 Ellen aliona wakati ukifika ambapo Kristo ataondoka mahali hapo na kupiga hatua kwenye wingu ambalo litampeleka duniani huku hukumu za Mungu zikiwaangukia wenye dhambi. Ufunuo 15 na 16 pia hutabiri wakati huu na kuonyesha kwamba hukumu za Mungu zitaanguka kwa namna ya mapigo. Ujumbe wa malaika wa tatu hauongelei tu juu ya utunzaji wa Sabato bali pia unaeleza hasa ni nani watu ambao watalazimika kuteseka na mapigo haya ya mwisho. Ni wale wasioizoeza imani yao kwa jinsi ya kutosha kushika amri za Mungu, na ambao badala yake wanaikubali “alama ya mnyama” akilini mwao.

Ikawa wazi kabisa kwa Waadventista wa mapema kwamba kitabu cha Ufunuo kinazungumza juu ya alama mbili tofauti ambazo watu watapokea katika akili zao kabla ya kufungwa kwa rehema, ile “alama ya mnyama” na “muhuri wa Mungu.” Kwa sababu chapa ya mnyama inabandikwa kwa wale wasiozishika amri, Waadventista wa kwanza walianza kuona kwamba muhuri wa Mungu ni kwa ajili ya wale wazishikao Amri na za Mungu - wale wanaozishika zote, ikiwa ni pamoja na Sabato. Waligundua, kwa hakika, kwamba muhuri wa Mungu ni Sabato, inayotunzwa

ipasavyo kwa njia ya imani katika Yesu. Na fasiri yao hii ilithibitishwa kwa kujifunza Biblia kwa kina na kwa maono moja au zaidi aliyopewa Ellen White.

Walipochunguza Ufunuo 7, waliona kwamba malaika mwingine maalum alitumwa katika siku za mwisho kushuhudia "kutiwa muhuri" huku kwa watu wa Mungu katika tukio la Sabato. Waliona pia kwamba mapigo saba ya mwisho hayataanguka hadi kila mfuasi wa kweli wa Yesu awe ametiwa muhuri. Waanzilishi wa imani walipokuwa wakitafakari haya yote na zaidi, hisia ya utendaji wa dharura na kukusudia iliibuka kulingana na ufahamu kwamba Sabato ni muhimu kwa sababu muda ni mfupi na Kristo anakuja hivi karibuni. Akiwa anafanya kazi Yake mbinguni Kristo anaelekeza uangalifu kwenye Sabato. Katika siku hizi za mwisho Yeye anafuta dhambi;, na kuvunja Sabato bila shaka ni dhambi. Wakati mawingu meusi ya wakati wa mwisho wa taabu yanapokusanyika angani na dhoruba inayokuja inakaribia kupasuka kwa ghadhabu, pambano kuu kati ya Kristo na Shetani linafikia upeo wake duniani.

Malaika wema na wale malaika wa mashetani waovu, au mapepo, wako ng'ambo wakitafuta wanadamu, ili kuwavuta wawe watiifu kwa Mungu au kwa mnyama. Katika mchakato huo, wahusika wanaundwa bila kubatilishwa ama kwa sura ya Mungu au kwa mfano wa yule mwovu. Hakuna anayeweza kuepuka kuhusika. Wote lazima wawe na upande wa kusimama. Ni wale tu wanaochagua Kweli ya Mungu ndio watakaoepuka mapigo na kushiriki furaha ya marejeo ya pili ya Kristo. Katika pambano hili kila mshika Sabato ambaye anaelewa nyakati anaitwa kuingia kwa nguvu zake zote, hazina, na talanta zake zote: "Acha ujumbe uenee, kwa maana wakati ni mfupi!"

Ni jinsi gani ulivyokuwa tofauti msisitizo huu na ule Bi. Oakes aliokuja nao Washington, New Hampshire! Wakati yule bibi mwema wa Kibaptisti wa Siku ya Saba alipowasilisha kile alichotaka kusema, Waadventista, kwa kweli, walijibu kwamba kwa sababu Yesu alikuwa anakuja upesi, hapakuwa na wakati au haja ya kufikiria kuhusu amri ya Sabato. Lakini kama vile Bates, Gurney, Edson, James na Ellen White, David Arnold, Stockbridge Howland, na Waadventista wengine wa Sabato walikuwa wamejihusisha vizuri katika utafiti wao, waligundua kwamba ni kwa sababu Kristo anakuja upesi na wakati ni mfupi kwamba ni lazima tuikubali Sabato ambayo ni jaribio kuu la utii wa kweli/dhati kwa Yesu—na tuitangaze kila mahali Sabato.

Hii, basi, ni angalau sehemu ya kile kilichomaanishwa kuhusu "kuitangaza Sabato kikamilifu zaidi." Pia ni kiini cha ujumbe wa malaika wa tatu. Na malaika wa tatu wa Ufunuo 14 anatangaza ujumbe wake "kwa sauti kuu." Ili sehemu hii ya unabii itimie ili ujumbe uweze kuenea kwa wale ambao hawakujua, waamini walianza kuhisi wajibu wa kuzindua uchapaji wa machapisho na vitabu kwa mikakati endelevu.

*VIDOKEZO:*

*1. According to different traditions, Rachel Oakes, Frederick Wheeler, and William Farnsworth are each ascribed the honor of being known as the "first Seventh-day Adventist." However at the time when each of them accepted the Sabbath, they knew nothing about that "foundation of our faith," the new light on the sanctuary. And being unacquainted with the modern manifestation of the spirit of prophecy in Ellen Harmon White, they could scarcely be numbered among those who "keep the commandments of God, and have the testimony of Jesus," in this special latter-day meaning. Otis Nichols held to all three doctrines (Sabbath, sanctuary, and spirit of prophecy) some years before Wheeler, Farnsworth; or Mrs. Oakes did, and somewhat earlier than Bates, Edson, and the Whites. Another early believer (possibly even earlier than Nichols) was H. S. Gurney.*

*2. Otis Nichols to William Miller, April 20, 1846, written on the back of a copy of the April 6, 1846, broadside of Ellen Harmon's first visions*

*3. Joseph Bates, The Seventh Day Sabbath, A Perpetual Sign, 2d. ed., rev. and enl. (New Bedford: Press of Benjamin Lindsey, 1847), p. iv*

*4. The vision of the Sabbath in the sanctuary that begins on page 100 of Life Sketches is the April 3 vision, and is the same as the one described in Early Writings, pp. 32-35. It is also the one that Joseph Bates published in his broadside, A Vision, vol. 1, no. 1 (April 7, 1847). In his "Remarks" in this same broadside Bates refers to a "similar vision" given to Ellen White on March 6, 1847, and it may be assumed that it is this vision which is described? in Life Sketches, pp. 95, 96. Careful examination of these two pages tends to confirm this conclusion.*

*5. Adapted from Loughborough, The Great Second Advent Movement, pp. 244,245*

*6. The statements attributed here to Ellen White are slightly adapted from Early Writings, pp. 32, 33, 85, 86; Life Sketches, pp. 95, 96, 100- 103; and Spiritual Gifts, vol. 2, pp. 82, 83. They combine elements from both the March 6 and April 3 visions*

*7. Its title and date: Supplement to the Christian Experience and Views of Ellen G. White, 1854*

*8. Ellen G. White, Early Writings, pp. 85, 86*

*9. Ibid., p. 42*

*10. Ibid., p. 254*

*11. See especially ibid., pp. 36-38; also SDA Encyclopedia, art. "Seal of God."*

*12. Present Truth, no. 4 (September 1849), p. 28*

## SURA YA 14
## GAZETI LETU ZURI LA ZAMANI NA LA KWANZA KWENYE HISTORIA YETU YA MACHAPISHO- “REVIEW AND HERALD "

Jarida ambalo James White alizindua mnamo Novemba 1850 kwa zaidi ya karne moja limejulikana kwa watu wa zamani kama "The Good Old Review." Limesajiliwa na ofisi ya posta kama “The Advent Review and Sabbath Herald.” Adventist Review anaamanisha kweli Kupitia tukio la Marejeo ya Yesu? Ikiwa “Marejeo” haya ni ujio wa pili wa Kristo, Je, ni kwa namna gani wanapitia tukio hili la kuja kwa Yesu katika gazeti kabla halijatokea? Jibu la mwaka 1850 lilikuwa kwamba ujio ambao Unahakikiwa hapa ni ule mwamko mkuu wa Marejeo ya Yesu mara ya Pili (The Great Second Advent awakening).

Baada ya kukatishwa tamaa katika masika ya 1844, Josiah Litch alikuwa ameanzisha Gazeti liitwalo The Advent Shield, akifuatilia majaliwa na mipango ya Mungu, na utimilifu wa unabii katika harakati za marejeo ya Kristo mara ya pili, hadi wakati huo. Katika majira ya joto ya 1847 Joseph Bates aliandika makala iitwayo Second Advent Waymarks and High Heaps, historia iliyo na nyongeza juu ya mada hiyo hiyo. Ellen alikuwa ameona katika Maono yake ya kwanza kwamba nuru angavu ya kilio cha usiku wa manane ilikuwa iangazie njia ya kuelekea Mji Mtakatifu. Hii ni sababu moja kwa nini kumekuwa na historia nyingi kuhusu Uadventista wa awali, ikiwa ni pamoja na unayosoma sasa.

Hii ni sababu moja, pia, ya Jarida ‘The Advent Review’ na ‘Sabbath Herald.’ Jarida jipya lilikuwa na kazi ya kutangaza ujumbe muhimu kutoka kwa Yesu katika Patakatifu pa Patakatifu palipopangwa kuwatenganisha wanaume na wanawake kutoka kwenye dhambi na kuwavuta Kwake Bwana Mwenyewe. Kati ya uvumbuzi wa awali wa Sabato—katika—Patakatifu na uzinduzi wa Jarida la Review na Herald, miaka miwili na nusu muhimu na ya uundaji ilipita, ambayo iliadhimishwa na zaidi ya mikutano ishirini ya ‘mwishoni mwa juma-weekend’ ambayo iliendelea hadi mikusanyiko ya mwishoni mwa majuma ya mwanzoni mwa mwaka 1846.

Mikutano hii ilifanywa katika nyumba zilizochaguliwa katika vituo mbalimbali vya kijiografia vya Utunzaji wa Sabato vilivyokuwa vikiendelea, ilifanyika jikoni, sebuleni, vyumba vikubwa ambavyo havijakamilishwa katika ujenzi,” na katika ghala kadhaa zilizotelekezwa (barns). Kongamano lililofanyika mwezi wa Aprili 1848 lilikuwa muhimu sana. James White akiwa amezoea kuhudhuria mikutano zaidi ya 12 huko huko Topsham,  na aliguswa moyo sana wakati watu wapatao hamsini walipowasili kwa ajili ya mkutano katika nyumba ya Albert Belden huko Rocky Hill, Connecticut. Miaka mingi baadaye aliutathmini mkutano huo kama "mkutano mkuu wa kwanza uliofanywa na Waadventista Wasabato.

Kuhusiana na idadi  ya watu na mvuto, mkutano huu uliashiria kufunguliwa kwa ukurasa mpya katika msimu, kazi na historia ya Uadventista." Kongamano lingeweza kudumu kutoka Ijumaa hadi Jumapili au kutoka Alhamisi alasiri hadi Jumatatu asubuhi. Kongamano moja lilifanyika siku ya Jumapili na Jumatatu. James White, alikuwa kama nembo hai ya "Advent Review,” aliwasilisha ushahidi kwamba matukio ya kweli yaliyohubiriwa na vuguvugu la Wafuasi wa Miller yalifikia kilele chake pale Kristo alipoingia Patakatifu sana au kama tunavyojua kutokana na Kutoka 25 na Kitabu cha Waebrania, Patakatifu pa Patakatifu. Joseph Bates, yeye mwenyewe pia alikuwa alama/ishara/nembo ya “Mhubiri wa Sabato” aliye hai, huyu alihubiri siku ya Sabato ndani ya kusanyiko juu ya Sanduku la Agano la ushuhuda Wake Bwana na juu ya hitaji la kuupokea ujumbe wa malaika wa tatu.

Wanaume na wanawake waliohudhuria mikutano hii walikuwa wamepitia matayarisho ya kuja kwa Yesu na kukatishwa tamaa pale Oktoba, 22, 1844. Sasa, miaka kadhaa ikiwa imepita, na wakiwa hawako tena katika tukio hilo la furaha na uchungu wakati huo-huo, waliulizana kama ni kweli? Je, ni kweli kwamba Siku 2300 zilifikia mwisho wake mnamo 1844? Je, ni  kweli Yesu aliingia katika ua wa ndani wa Patakatifu pa mbinguni? Je, ni kweli tulihubiri ujumbe wa malaika wa  kwanza na wa pili? Je, sio "wajibu" wetu sasa kuiithisha kwa kupitisha kwa watu ujumbe wa malaika wa tatu?

Walikuwa na uzoefu katika dhabihu iliyohusika katika kuunga mkono theolojia isiyopendwa na watu wengi, theolojia isiyo maarufu. Hawakuwa na uzoefu katika

mabadiliko ya falsafa za kiliberali (vagaries of liberal philosophies). Vigezo vyao vilikuwa sawa na vya Luther kwenye Diet of Worms - Maandiko, hekima na dhamiri. Walipogundua kwamba Biblia ilisema waziwazi juu ya madai ya Sabato ya siku ya saba, wengi wao walihatarisha maisha yao kwa hiari yao wenewe.

“Wengi wa watu wetu,” aliandika Ellen White katika 1904, “hawatambui jinsi msingi wa imani yetu ulivyowekwa imara. Mume wangu, Mzee Joseph Bates, Baba Pierce, Mzee Hiram Edson, na wengine ambao walikuwa waangalifu, waungwana, na wa kweli, walikuwa miongoni mwa wale ambao ... walitafuta ile Kweli kama hazina iliyositirika, na tulijifunza na kusali kwa dhati na bidii. Mara nyingi tulibaki pamoja hadi jioni usiku, na nyakati nyingine usiku kucha, tukiomba kwa ajili ya nuru na kujifunza Neno, tena na tena ndugu hawa walikusanyika ili kujifunza Biblia, ili wapate kujua maana yake, na kuwa tayari kuifundisha kwa nguvu kwa wengine.”

Jukumu la Ellen White mwenyewe lilikuwa na mipaka lakini la thamani. “Walipofikia hatua katika somo lao ambapo walisema, ‘Hatuwezi kufanya lolote zaidi,’ Roho wa Bwana angekuja juu yangu,” Ellen aripoti, “ nami ningechukuliwa katika maono, na maelezo ya wazi juu ya jambo hilo, na kupewa Mafungu ya Biblia tuliyokuwa tukijifunza ningepewa, pamoja na maelekezo ya jinsi tulivyopaswa kufanya kazi na kufundisha kwa ufanisi." Mara moja ndugu katika Kristo waliyaangalia yale madokezo ya Aya za Biblia alizopewa katika Biblia na konkodensi zao na wakasisimka kuona kwamba kwa kweli zilifafanua mambo yaliyozungumziwa. Michango hii ya Ellen White ilionekana kuvutia hasa kwa sababu "ndugu walijua kwamba wakati Ellen hakuwa katika maono," angetuambia, "Mimi siwezi kuelewa mambo haya."

Muhtasari wa jumla aliopewa ulikuwa wazi vya kutosh kwa hakika. Lakini mara nyingi hakuelewa. Ellen hakuelewa Maandiko ya Biblia au hoja ya dhati au yenye nguvu ambayo akina ndugu waliitumia ili kuunga mkono maoni yao mbalimbali. “Nilikuwa katika hali hii ya akili,” anasema, “mpaka mambo yote makuu ya imani yetu yalipofanywa kuwa ya thamani akilini mwetu, kwa kupatana na Neno la Mungu.” Ilikuwa wazi kwamba lilikuwa ni kusudi la Mungu kwamba ndugu hawa waelewe kwa kinagaubaga kuwa Ukweli aliokuwa akiwaita waukumbatie na kuutangaza, huu ulikuwa na mizizi katika Biblia yenyewe tu na si—kama wengine wanavyoweza kushawishika kusema—katika ndoto za binti tu.

Katika mkutano uliofanyika nyumbani kwa David Arnold karibu na Volney, New York, katika majira ya joto ya 1848, Ellen White anaripoti kwamba "karibu watu thelathini na watano walihudhuria,-marafiki wote ambao wangeweza kukusanywa katika sehemu hiyo ya Jimbo. Lakini kati ya idadi hii ya watu, hapakuwa na hata watu wawili waliokubaliana kwamba walikuwa na makosa mazito, na kila mmoja alisisitiza maoni yake mwenyewe kwa msukumo, akitangaza kwamba maoni hayo,

yalikuwa kulingana na Maandiko.  Walipoanza kusherehekea Meza ya Bwana, mmoja wa ndugu alisimama na kusema kwamba aliamini inapaswa kuadhimishwa mara moja tu kwa mwaka—kama ilivyokuwa wakati Yesu Mwenyewe alipoiadhimisha. Mtu fulani alifundisha kwamba milenia ilikuwa tayari imepita,  katika siku za nyuma.

"Tofauti hizi za ajabu za maoni zilizidisha mzigo mkubwa juu yangu," Ellen White alikumbuka miaka mingi baadaye. "Niliona," aliandika, "kwamba makosa mengi yalikuwa yanawasilishwa kana kwamba ndiyo Ukweli. Ilionekana kwangu kwamba Mungu hakuheshimiwa/hakutukuzwa. Huzuni kubwa iligandamiza roho yangu, na nilizimia chini ya mzigo huo mzito. Wengine waliogopa kwamba nilikuwa naelekea kufa. Ndugu Bates, Chamberlain, Gurney, Edson, na mume wangu waliniombea sana, na upesi ufahamu wangu ukanirudia tena, Nuru ya mbinguni ikatulia juu yangu, na nikapotea kutoka kwenye mambo ya hapa duniani."

Katika maono yake alionyeshwa kile ambacho kilikuwa kibaya kuhusu mawazo ambayo watu hawa walikuwa wakiwasilisha, na msimamo wao wa kweli ulivyopaswa kuwa. "Aliamriwa kuwaambia wayasalimishe makosa yao na kuyaondoa, na kuungana juu ya Kweli za ujumbe wa yule malaika wa tatu.” Matokeo yake yalikuwa kwamba mkutano huo “ulifungwa kwa ushindi. Kweli ilipata Ushindi,” na vuguvugu hilo likapata washiriki wapya kadhaa. Iligharimu kitu kuendesha makongamano hayo. Ellen ndiye alilipia gharama nyingi zaidi. Akiwa na hakika kwamba Mungu alikuwa akimwita aende, alimwacha mtoto wake mchanga Henry kwa machozi pamoja na marafiki zake wapendwa, Stockbridge. Howlands, akimtembelea mara kwa mara kwa miaka kadhaa, kama Hana, na zawadi- 1Samweli 2:18-20.

Ili kupata pesa za kuhudhuria mkutano katika shamba la David Arnold, James White alipata dola arobaini kwa kukata nyasi na mundu—kwa senti themanini na saba na nusu tu kwa ekari. Alipokuwa akienda nyumbani chini ya Mfereji wa Erie, unaotoka katika maziwa makuu matano ya Marekani, pamoja na ndugu wa familia ya White baada ya mkutano katika ghala la Edson huko Port Gibson, Ndugu mpendwa Bates alijaribu kuingia kwenye mashua mtoni, na dola ya thamani kwa ajili ya kulipia safari yake. Akiwa na nauli tayari mkononi mwake wakati boti iliposhindwa kusimama Bates alipepesuka na kuanguka mtoni. Bila woga, nahodha wetu wa zamani wa baharini alianza kuogelea "hali ameshikilia kijitabu chake kidogo cha mfukoni kwa mkono mmoja, na dola yake kwa mkono mwingine. Kofia yake ilianguka, na katika kuiokoa alipoteza fedha, lakini akashikilia sana kijitabu chake cha mfukoni.”

Baadaye kidogo yeye na ndugu za familia ya White walitembelea kwa kushtukiza familia ya washika Sabato wapya, Ndugu na Dada William Harris, wakitumaini kwamba Bates angeweza kupata namna ya kukausha mavazi yake yaliyolowa maji.

Kusanyiko la mwisho mnamo 1848 lilifanyika katika nyumba ya Otis Nichols huko Dorchester mnamo Novemba 18 na 19. Kwa namna fulani ulikuwa mkutano muhimu sana wa namna yake. Waumini walipokuwa wameingia katika umoja wa karibu zaidi juu ya ile mada kuu waliyokuwa wakisoma na kujifunza, mzigo uliwekwa mbele yao sasa kwamba yapasa mtu fulani aongoze katika kuzichapisha mada hizo. Siku ya Jumapili, Bibi White alipata maono ambayo alizungumza kwa sauti juu ya Sabato kama muhuri wa Mungu (Ufunuo 7) ikichomoza mashariki kama jua na kuongezeka kuwa na joto na mwanga zaidi, iking'aa zaidi hadi watakatifu watakapopewa kutokufa.

Baada ya maono hayo alimwambia Ndugu Bates achapishe kile alichosema. Akimgeukia mume wake, aliongezea kuwa “Nina ujumbe kwako. Ni lazima uanze kuchapisha kigazeti kidogo na kukituma kwa watu." Kigazeti kidogo- auchapisho dogo. Vitabu ni vizuri, bila shaka, lakini mara nyingi hupata shida ya kupuuzwa. Magazeti yanastahimili zaidi. Bibi White alijadili karatasi iliyopendekezwa: "Acha kiwe kidogo kwanza mwanzoni; lakini watu wakisomapo,” aliahidi, “watakutumia fedha ya kuchapisha, na utafanikiwa toka hapo unapoianza kazi ndogo ya kwanza.” Baada ya kupumzika akaongeza, “ Nilionyeshwa kuwa kutoka kwa huu mwanzo mdogo kutakuwa na vijito vya nuru vinavyoangaza kotekote ulimwenguni.”

Huo ulikuwa unabii wenye kuvutia na kugusa moyo sana ulioweza kuwasilishwa kwa wabeba nuru wachache waliokuwa maskini! Kulikuwa na wakati wa kujaribiwa kukubwa uliofuata. Watu wengi waliotaka jarida hilo lichapishwe walitaka mtu mwingine alipie gharama zake. Mzee White hakuwa na pesa za kuchapisha mwenyewe kwa kuwa aliishi maisha ya kujitolea kabisa kwa huduma yake, akitegemea mapato kwa kazi za hapa na pale alipokuwa hajaenda kwenye misafara ya uinjilisti na michango midogo midogo ya watu. Alipotafuta kuungwa mkono kwa chapisho lililopendekezwa matokeo yalikuwa ya kukatisha tamaa kwa kiwango kikubwa. Basi mzee Joseph Bates aliingia kwenye hilo pengo na kwenye maandalizi ya kitabu kipya cha A Seal of the Living God, A Hundred Forty-Four Thousand of the Servants of God Being Sealed— Muhuri wa Mungu aliye hai, Watumishi wa Mungu Mia Arobaini na Nne Wakitiwa Muhuri, mwaka wa 1849.

Mwaka mmoja baadaye, mwanzoni mwa 1850, akishikilia upana wa njozi za “mikondo ya nuru ya Ellen White kuzunguka ulimwengu,” alitabiri kwa ujasiri kutangazwa kwa Sabato huko Ufaransa, Uingereza, Urusi, na nchi za mashariki ya mto Frati. Mwaka mmoja baadaye, mwanzoni mwa 1850, James White pia alichapa kitabu cha nyimbo cha kurasa 48, ‘Hymns for God's Peculiar People, That Keep the Commandments of God, and the Faith of Jesus—Nyimbo za tenzi za watu wa pekee wa Mungu wanaotunza amri kumi za Mungu na imani ya Yesu.’ Hilo, pia, lilibeba ujumbe kuhusu muhuri wa Mungu, “ujumbe uliokuwa wazi, ulikuwa ukipanda na kwenda juu kutoka mashariki” na sala, Ee Mungu, Mungu uliye hai, utuwekee Muhuri

wako unapopita! utulinde na fimbo ya uharibifu tusije tukafa, ilipanda kuelekea juu pia.

Wimbo unaoitwa "Second Advent History—Historia ya Marejeo ya Yesu mara ya pili" ulifuatilia historia na maendeleo ya jumbe za malaika wa kwanza na wa pili hadi "ujumbe wa malaika wa tatu ulio mzito, sasa unatangaza adhabu ya mwisho." Wimbo mwingine uliadhimisha maono ya awali zaidi ya Ellen White. Huu uliandikwa na W. H. Hyde, ambaye alipokea uponyaji wakati Ellen alipomwombea katika miezi ya kwanza ya huduma yake ya kinabii. ‘Tumesikia kutoka nchi angavu, takatifu; Tumesikia, na mioyo yetu inafurahi.’ Wimbo mashuhuri uliimbwa na waamini!

Katika miaka yake ya uzeeni, Bibi White alisikika mara kwa mara akiimba wimbo huu peke yake. ‘Vitabu vya aina tofauti ni vizuri, lakini Bwana alisema anahitaji waanze na Jarida!’ Mnamo 1848, James White alikata nyasi za ng’ombe (hay), kwa senti themanini na saba na nusu kwa ekari ili kupata pesa za kuhudhuria mkutano. Mnamo Julai 1849, baada ya miezi kadhaa ya kusihi kwa ajili ya Jarida bila mafanikio, aliamua kujaribu tena. “Nitakwenda kutafuta shamba la kukata nyasi,” alimpasha habari mke wake.

Kisha alipokuwa akitoka katika majira ya asubuhi, mzigo mkubwa ulimsonga Ellen na akazimia. Sala ilitolewa, na punde si punde alijisikia nafuu. Maono yalikuja. "Maono yalikuwa kuhusu nini?" James aliuliza baadaye. "Kuhusu wewe ‘James’." "Ulionyeshwa nini?" "Bwana alinionyesha kuwa alikubariki mwaka jana ulipotoka kukata nyasi, lakini ikiwa utajaribu jambo lile lile sasa, Yeye atakuacha uwe mgonjwa. Kazi yako ni kuandika, kuandika, kuandika na kutoka nje ya makazi, na kutembea kwa imani. "Masharti ya hiyo njozi yalitimia, James alichukua kalamu na karatasi na, akiwa na Biblia yake na konkodansi, alianza kutayarisha makala na tahariri bila kukawia. Aliposoma na kujifunza Maandiko, nyakati fulani aliona ni vigumu kuyaelewa. Kisha yeye na Ellen wakapiga magoti na kumwomba Mungu awaelezee. Kisha akaendelea kuandika. Wakati huu Mzee na Bibi White walikuwa wakiishi kwa muda katika nyumba mpya, ya vijijini ya Albert Belden karibu na Rocky Hill, Connecticut.

Mkutano wa kwanza wa 1848 ulikuwa umeitishwa katika "chumba chake kikubwa ambacho hakijakamilika kujengwa" (kama futi 20 x 30) kwenye ghorofa ya pili. James na Ellen, baada ya kuishi karibia miaka mitatu ya ndoa, bado hawakuwa na samani/fanicha. Kila kitu walichokuwa nacho kiliingia kwa urahisi kwenye sanduku la futi tatu-trunket. Kila senti ya ziada iliingia kwenye kusudi la wito wao. Bi Clarissa Bonfoey wa Middletown mji uliokuwa jirani, mwanamke mwenye tabia ya uchangamfu na furaha ambaye mama yake alikuwa ameaga dunia, alijitolea kumletea vitu vya mamaye na kuwaambia wahame navyo. Walifurahi. Samani zake zililetwa kwa gari, na sehemu yake kubwa iliwekwa kwenye ghorofa ya pili, na kazi

ilianza ya kugawa vyumba na kupangilia samani. Ulikuwa mpangilio wa kipekee, Bi Bonfoey alikuwa akiishi kwa akina White, nao akina White wote waliishi na akina Belden.

Mnapokuwa na imani moja mnaweza kuweka urafiki wa karibu zaidi kuliko ule wa ndugu wa damu. Ushikamanifu huo ulidumu, na dada yake Ellen, Sarah baadaye aliolewa na mwanaume aitwaye Steven Belden, na akawa mama wa Frank E. Belden, mwandishi wa nyimbo (mfano ‘atakuja kwa vile tukeshe nk). Katika mwezi ule ule ambapo chapisho lilitolewa (Julai 1849) mtoto wa pili wa White alizaliwa pia. Mtoto huyu aliitwa James Edson. Jarida jipya waliliita Present Truth. Neno hili au jina la gazeti lilitoka katika 2 Petro 1:12.

Katika tahariri yake ya kwanza White aliandika, "Wakati wa Petro kulikuwa na Ukweli wa sasa, au Ukweli uliotumika kwa wakati huo, yaani sasa yao. Kanisa daima huwa lina Ukweli wa sasa. Ukweli uliopo sasa, ni ule unaoonyesha wajibu wa sasa, na nafasi sahihi kwa ajili ya sisi ambao tunaenda kukaribia kushuhudia wakati wa taabu, ambao haujawahi kutokea.” "Ukweli wa sasa" wakati huu ulikuwa bila shaka, Sabato. Machapisho hayo yalipokamilika, James White aliingia Middletown kwenye joto kali la Julai, kisha akapanda hadi ofisi ya juu ya mchapaji ya ndani, na kuomba nakala elfu moja.

James alikuwa akisumbuliwa na maumivu makali kwenye mguu wake. Alichechemea maili nane kwenda na maili nane kurudi. Mchapishaji, Bw. Charles Hamlin Pelton, alipotazama kwanza kichwa cha mada kilichopendekezwa na kisha kwenye vichwa vya makala katika nakala iliyoandikwa kwa mkono ya James White, alishangaa. "Sabato ya Kila Wiki Iliyoanzishwa Wakati wa Uumbaji, na sio Sinai," alisoma. "Je, huu ni 'Ukweli wa sasa, Ukweli wa leo?" Lakini kazi ni kazi. Aliinua mabega yake na kuelekeza kidole chake kwenye mstari wenye nukta ili mzee White aweke sahihi yake. White alitia saini mkataba huo na kuchechemea akishuka chini kwa mwendo mrefu wa "ngazi. Lakini Pelton alipoanza kuweka herufi ndogo kwa mkono, fumbo hilo lilitatuliwa. "Dhoruba inakuja," alisoma. "Vita, njaa na tauni tayari viko nchini, uwanja wa machinjio ya watu. Sasa ndio wakati, wakati pekee wa kutafuta kimbilio katika Kweli ya Mungu aliye hai.”

Makala nyingi katika matoleo matatu ya kwanza, ingawa zilikuwa mpya kabisa kwa mchapishaji, hakika yalikuwa mafundisho ya awali na zamani ya Kibaptisti ya Siku ya Saba na suala la tatu na la nne la dhana ya Waadventista iliibuka: Yesu katika Patakatifu, ujumbe wa malaika wa tatu, Sabato kama muhuri wa Mungu, na mazungumzo ya Isaya 58:12-14, ambapo siku za mwisho, watunza Sabato wanaitwa "watengenezaji wa mahali palipobomoka" katika sheria ya Mungu.

"Wakati umefika," alitangaza James White, "kwa ajili ya kutangazwa kwa Sabato kwa ukamilifu zaidi" akiendelea kuchechemea kwa ajili ya ulemavu wake aliendelea kuthibithisha na kuhakikisha kwamba habari hiyo iliwekwa na kuchapishwa katika umakini wake. Nakala zilipomalizika kuchapwa, aliazima gari la kubebea mizigo la farasi la Ndugu Belden ili ayalete nyumbani machapisho hayo.

Waliweka rundo la machapisho sakafuni, na kisha waumini waliitwa kutoka kila mahali. Hawa walikaribishwa kutoka mashamba ya karibu, na kwa machozi Walipiga magoti na kuomba kwa dhati ili Mungu awabariki. Walikunja masomo yale, na kukata kona zisizotakiwa, na kuanza kuyatuma kwa kila waliyefikiri kwamba angeweza kuyasoma. James aliyaweka machapisho mengine katika mfuko na kuyapeleka Middletown kwa ajili ya kuyatuma kwa njia ya posta.  Punde barua na michango iliingia ili kumtia moyo aendelee kuchapisha majarida haya.

Baada ya kuchapisha matoleo manne kutokea Middletown, Familia ya Whites walihama kutoka kwa Albert Beldens, na walitumia siku chache za furaha na mtoto wao Henry wa miaka mitatu katika nyumba ya Stockbridge Howlands huko Topsham, Maine; kisha, wakaazima samani kutoka kwa ndugu wenyeji,  na wakaishi kwa muda huko Oswego, New York. Binti wa Bonfoey alikuja pamoja na familia ya White ili kukaa na mtoto Edson, na kumlea wakati Ellen White alienda kusafiri na mumewe. Wakiendelea kusambaza Ukweli wa Sasa  kote, walichukua miezi kadhaa.

Mzee White alipopata mashine mpya ya kuchapa na kuchapa toleo la Desemba, aligundua kwamba shauku ya chapisho hilo ilikuwa karibu kufa. Hata Bates, kwa hakika, alipingwa (ilikuwa kwa muda mfupi tu), pengine akitoa sababu kwamba kuendana na tarehe za machapisho na kuchapa kwa wakati na kuwapa watu machapisho kwa wakati humweka mhariri katika kazi ngumu daima kwenye dawati. Sadaka nazo zilikuwa chache sana kwa muda, kiasi kwamba White alilazimika kutangaza kwamba, "Wakati huu mimi sina fedha, na nina deni."  Ellen White aliongeza kutoka katika maono, “Mimi nilivyozitazama roho maskini zikifa kwa kukosa Ukweli wa sasa, na baadhi ya wale wanaodai kuamini Ukweli wanajiwekea fedha zao kibindoni na kuwaacha watu wafe, kwa kuzuilia rasilimali zinazofaa za kuendeleza Neno la Mungu; basi kwa kutazama tu haya nilipatwa na uchungu sana, na nikamwomba malaika aondoe mandhari na kazi hii kutoka kwangu."

Sasa pesa zilianza kuingia. Kutojali kulibadilishwa na bidii—na James White punde alijikuta akihariri machapisho mawili! Pamoja na jarida la “The Present Truth” aliongeza jarida la “The Advent Review.” Kisha mnamo Novemba 1850 baada ya Familia ya White  kuhamia Centerport, New York, na kisha Paris, Maine, idadi ya kwanza ya toleo la kwanza ilitoka kwenye “The Second Advent Review and Sabbath Herald—Mapitio ya Ujio wa mara ya Pili na Ujumbe wa Sabato, ikiwa ni mwendelezo wa majarida yote mawili yaliyounganishwa katika moja. Mbali na makala kuhusu

Sabato na Patakatifu, walichapisha vitu vingine, bila shaka, juu ya mada mbalimbali za Biblia; pia barua kutoka kwa watunza Sabato, na taarifa juu ya mahali na shughuli za wahudumu wao wachache, wanaosafiri daima.

Usajili, bila malipo mwanzoni, uliwekwa na baada ya muda kuwa dola $1.00 kwa mwaka kwa wale ambao wangeweza kulipa, ingawa bado ingekuwa bure kwa wale ambao hawakuweza kutoa hizi pesa. Karibu kila nyumba ya Waadventista ililipokea jarida, na wengi wao walilipia. Hii ikawa kiungo cha upendo kinachounganisha harakati za pamoja na kuiongoza mbele. Sasa chapisho la "The Good Old Review," lilikuwa limeboreshwa sana na kupanuliwa, na bado linasaidia hata leo kuwa kiungo kilicholiweka Kanisa la Waadventista Wasabato katika umoja na kusonga mbele huku likikumbuka yale yaliyopita.

Kwa kweli, katika miaka ya hivi majuzi, ukuaji mkubwa wa washiriki nje ya Amerika Kaskazini umesababisha kuzinduliwa kwa matoleo maalum yaliyorekebishwa kwa wasomaji katika maeneo mengine, kama vile Ulaya na Amerika ya Kusini. Baada ya kuanza chapisho jipya White aliendelea kusafiri sana, kufanya kazi kwa bidii, na kulipwa kidogo sana. Kulikuwa na ujumbe mkubwa wa kubebwa na ni wajumbe wachache tu ndio waliubeba. Mnamo 1851, James White alivunjika moyo sana kutokana na kufanya kazi kupita kiasi na alipanga siku moja kumpa mpiga chapa barua ya kuingizwa katika jarida la Review linalofuata, kwamba hilo liwe toleo la mwisho la gazeti hilo. Lakini Ellen alizimia tena wakati James alipokuwa akitoka nyumbani, na akageuka nyuma ili kumsaidia. Waliomba, na imani yao ikafufuka, na machapisho yakaendelea kusambazwa.

Akiwa anaishi Saratoga Springs, Mzee White aliamua kwamba ingefaa kuacha kuchapa kwa watu wengine na kwamba badala yake wanapaswa kuanzisha ofisi yao ya uchapishaji. Kilichokuwa kibaya zaidi ni pale alipofikiri kwamba Jarida linalotolewa kwa ajili ya kutangaza Sabato mitambo ya watu wa dunia hulichapisha siku ya Sabato yaani Jumamosi kama ilivyokuwa inatokea wakati mara kwa mara. Alihisi, pia, kwamba waumini wangefanya kazi hiyo kwa uaminifu mkubwa kuliko wasioamini, na alitumaini kuwa wakichapa wenyewe, wanaweza kuweka akiba fulani ya pesa kwa ajili ya kazi hiyo. Ili kununua vifaa muhimu, angelazimika kwanza kutafuta pesa.

Maombi ya fedha yalitumwa, pesa zikaanza kuingia, na White akanunua mashine ya “Washington handpress,” iliyofanana na ya vyombo vya habari ambavyo Gutenberg alitumia katika karne ya kumi na tano. Wakati huo huo hatua nyingine ilikuwa imesababisha familia ya White kuhama na kampuni hiyo ya Review huko Rochester. Nyumba kuu kuu ya zamani inayotikisika kidogo ilikodishwa (kwa $175.00 kwa mwaka). Hii likuwa kubwa vya kutosha kuhifadhi magazeti, mashine ya uchapaji, karatasi za akiba, na pia mahali pa kuishi familia ya White, watoto wao wachanga,

na watu wapatao kumi na wawili waliojitolea. Hawa walipata chumba cha kulala na chakula—bweni na  mara nyingi mlo wao haukuwa na chochote zaidi ya nafaka iliyokorogwa kama ugali au maharagwe, mlo baada ya mlo.

Mtu mashuhuri miongoni mwa wale waliojiunga na watendakazi katika siku hizo za mapema walikuwa Annie Smith na baadaye kidogo akamwita kaka yake Uriah Smith. Annie alisaidia popote alipohitajika, hasa kama mhariri wa nakala na msahihishaji na wakati mwingine kama mhariri msaidizi wa Mzee White alipokuwa hayupo. Alikuwa na kipawa cha utunzi wa nyimbo, na kumi kati ya nyimbo zake zinapatikana katika kitabu cha Nyimbo za Kanisa (U mwendo gani nyumbani ndiyo wimbo wake ambao sisi wazungumza Kiswahili tunaujua sana!). "Nilimwona Mtu Aliyechoka, Mwenye Huzuni, na Kuchakaa—I Saw One Weary, Sad, and Worn" ni mojawapo ya mashairi yake mengi tu yanayojulikana zaidi ambayo yalipamba ukurasa wa mbele wa jarida la 'The Review"

Wengi wao walitafsiri mwendo huo katika mistari ya sauti kama hii: 'We are going, we are going, now a lonely Pilgrim Band, To a brighter world of glory, to a fair and happy land/Twaenda, twaenda, sasa tukiwa wasafiri wapweke, Kuelekea nchi yenye utukufu zaidi, kwenye nchi ya haki na yenye furaha.' Kifo chake cha ghafla kutokana na Kazi nyingi  na huzuni ya kukatishwa tamaa katika kutafuta mwenzi wa maisha, akiwa na umri wa miaka ishirini na saba kilihuzunisha wengi na kusababisha maombolezo makubwa. Uriah Smith pia alikuwa mtunga mashairi, mwenye ladha ya mifumo ya kitambo zaidi lakini yenye manufaa sawa kwa "The Advent Review:" 'Tazama Bwana-arusi anakuja, tokeni mwende Kumlaki—Behold the Bridegroom cometh, go ye out to meet him!"

Uriah alikuwa na umri wa miaka ishirini alipoacha mipango yake ya elimu ya kwenda Harvard na kuhamia katika nyumba kubwa ya White huko Rochester. Akiwa na umri wa miaka ishirini na tatu, mnamo 1855, alifanywa kuwa mhariri wa kiwanda cha uchapaji. Kwa mabadiliko machache tu ya hapa na pale, alitumika kwenye idara ya Uhariri kama mhariri  miaka hamsini, na mara nyingi kama mhariri mkuu, lakini pia kwa miaka mingi kama mhasibu, meneja wa ofisi, au mhakiki. Smith alikuwa stadi wa kutumia zana na mshine na kalamu pia. Kwa muda mrefu alikuwa mchapaji (engraver) pekee kwenye vyombo vya habari aliyehusika na vielelezo kwenye machapisho yaani wood-cut illustrations.

Alitengeneza madawati yake mwenyewe, mawili ambayo yamehifadhiwa. Alipata hati miliki ya mguu wa bandia—kwani alikuwa amepoteza mguu katika ujana wake na akajitengenezea mguu bandia ambao ulimwezesha kupiga magoti wakati anaomba. Baadaye alipata hati miliki ya dawati la shule lililoboreshwa. Kwa miaka mingi Uriah Smith alijaza nafasi ya katibu wa Konferensi Kuu. Alipata muda wa kuandika vitabu tatu usiku. Mojawapo ya maandishi yake maarufu ni Unabii juu ya

Danieli na Ufunuo (Thoughts on Daniel and the Revelation), ambayo yalibaki kuwa tafsiri maarufu iliyotumiwa kwa kawaida na Waadventista miongoni mwa vitabu viwili vikuu vya unabii hadi miongo kadhaa baada ya kifo chake.

Akiwa mwenye sura ya kuvutia, mwenye adabu, na mtu aliyejituma, alikuwa mmoja wa viongozi wa Waadventista waliojulikana sana wakati wa uhai wake. Alikufa kutokana na kiharusi alichopata alipokuwa akienda kazini siku ya Ijumaa Machi 1903 akiwa na umri wa miaka sabini na moja.

Lakini tukirejea nyuma kidogo; Mnamo 1855 waumini wa jimbo la Michigan waliialika familia ya White kuhama kutoka Rochester hadi Battle Creek, Michingan na wakajitolea kuwajengea kiwanda kidogo cha uchapaji. Ofa hiyo ilikubaliwa kwa furaha na wote, na kiwanda kidogo cha mbao chenye orofa mbili kilijengwa haraka. Katika miongo iliyofuata, vifaa vinavyoendeshwa kwa mvuke vilichukua mahali pa mashine ya kugandamiza kwa mkono (kutoka hand pressed equipment na kuingia kwenye Steam pressed equipment]

Majengo yenye nafasi kubwa zaidi yalichukua nafasi ya lile jengo dogo la kwanza, hadi Seventh-day Adventist Steam Press ya Battle Creek ikawa taasisi kubwa zaidi na iliyo na vifaa bora zaidi vya uchapishaji katika jimbo zima la Michigan. Lakini Waadventista hawajawahi kusahau kwamba makao yao makuu ya kwanza ya Uchapaji yalikuwa katika ofisi iliyokuwa nyumbani huko Rochester, na kwamba hapa ndipo taasisi yao ya kwanza iliyokuwa kampuni ya uchapishaji ilianza. Ilikuwa ni katika kuisajili kampuni hii kiserikali kama chama cha uchapishaji kisheria ndipo ambapo viongozi waliketi chini mnamo 1860 na kuchagua Jina la dhehebu (Seventh Day Adventist. Na kipindi chote ambacho ofisi za Makao Makuu ya Konferensi, zilikuwa hapo Battle Creek (kutoka 1863 hadi 1903), zilitumia vyumba vya kiwanda cha Review And Herald. Yote haya ni ishara kwamba Kanisa la Waadventista Wasabato liliitwa kwa kusudi la kuwajibika katika kutoa ujumbe maalum wa siku za mwisho. Kusudi la kanisa hili, ni kuuishi ujumbe huo na kuwajulisha wengine kuhusu ujumbe huo (kupitia vitabu na machapisho na kwa njia nyinginezo) ili nao waweze kuuishi (Je, mimi ninafanya hivyo leo kwenye ujirani wangu, yaani kuwagawia wengine machapisho na kushiriki habari njema?)

*VIDOKEZO:*

*1. This chapter is based primarily on Ellen G. White, Life Sketches, pp. 110-128; James White, Life Incidents, pp. 264-296; contemporary correspondence by James and Ellen White; and Spalding, Footprints of the Pioneers (Washington, D.C.: Review and Herald Publishing Association, 1947), pp. 99- 103*

*2. Seven conferences of various size and significance are known from contemporary sources to have been held in 1848; at Rocky Hill and Bristol, Connecticut; Oswego and Port Gibson, New York; Rocky Hill (again); Topsham, Maine; and Dorchester, Massachusetts. Several of these 1848 meetings have become known familiarly among Seventh-day Adventists as "Sabbath Conferences," a term apparently coined by Arthur L. White, who, in his Messenger to the Remnant (Washington, D.C.: Board of Trustees, Ellen G. White Publications, 1954), p. 38, lists five "Sabbath conferences," omitting the gatherings at Bristol and Dorchester. The SDA Encyclopedia, art. "Sabbath Conferences," adds Dorchester to make six--and goes on to say that sixteen similar meetings were held in 1849 and 1850. Bates is known to have attended a "conference" in Middletown, Connecticut" in 1847*

*3. James White, Life Incidents, p. 271, where he puts the number in attendance at "less than thirty." In Ellen G. White, Spiritual Gifts, vol. 2, p. 93, a contemporary letter of his is quoted which gives the number "about fifty"*

*4. Ellen G. White, Selected Messages, 2 vols. (Washington, D.C: Review and Herald Publishing Association, 1958), bk. 1, pp. 206, 207*

*5. Joseph Bates, A Seal of the Living God. A Hundred Forty-Four Thousand, of the Servants of God Being Sealed, in 1849 (New Bedford, [Mass.]: Press of Benjamin Lindsey, 1849), p. 233*

*6. Ellen G. White, Life Sketches, pp. 110, 111*

*7. Ibid., p. 116, footnote 8. Ibid., pp. 124, 126*

*9. This hymnal bears the date 1849 but did not appear until early 1850. Apparently the type for the first signature(s) was set in 1849 but not for the last one till later. Present Truth, December 1849, p. 47; March 1850 (no. 7), p. 56; March 1850 (no.8), p. 64; cf. Ellen G. White, Letter 4, 1850*

*10. Ellen G. White, Testimonies, vol. 1, p. 70; Arthur L. White, Messenger, p. 127*

*11. Frank E. Belden wrote a large number of hymns and gospel songs, twenty-two of which may be found in the The Church Hymnal. His Christ in Song was loved and widely used for many years*

*12. James White, Oswego, New York, to Bro. Hastings, January 10, 1850. Arthur L. White, Messenger, p. 49*

*13. Present Truth, December 1849, p. 47*

*14. Present Truth, April 1850, p. 71*

*15. Changed in the second volume, August 5, 1851, to the Advent Review and Sabbath Herald*

*16. Ellen G. White, Life Sketches, p. 140*

*17. One is housed at the Review and Herald Publishing Association in Washington, D.C., and the other in the James White Library, Andrews University.*

# SURA YA 15
# JE, WAADVENTISTA WANAWIWA NA WAKRISTO WENGINE?

Waanzilishi wa Waadventista Wasabato waliuita ujumbe waliougundua, "Kweli." Waliipa mada hiyo ya jarida lao la kwanza- Ukweli wa Sasa. Waandamizi wao hata leo bado huzungumzia juu ya washiriki wapya kama watu "waliongia au waliokuja kwenye Kweli" na waasi-wa imani kama "watu walioiacha ile Kweli" (2 Timotheo 4:10). Katika mwaka 1881 Ellen White aliandika, "Ni hakika kwamba tuna Kweli kama vile Mungu anavyoishi; na Shetani, pamoja na sanaa yake yote na nguvu za kuzimu, hawezi kubadilisha Ukweli wa Mungu kuwa uongo." Inakaribia kuonekana kana kwamba Waadventista Wasabato wanafikiri wao pekee ndio walio na Ukweli! Kinyume chake, hata hivyo, wanakubali kwamba wanawiwa kwa hali ya juu na Wakristo wengine wengi katika enzi zote ambao wamethamini na kuwarithisha/kuwapasia hizi Kweli kutoka kizazi kimoja hadi kingine, mara nyingi kwa hatari ya maisha yao.

Tayari tumefuatilia deni la kipekee ambalo Waadventista wanadaiwa na Wabaptisti wa Siku ya Saba. Hebu tuangalie kwa ufupi kuwiwa huko kwaajili ya wokovu wa wengine. Lakini kwanza, Ukweli ni nini? Yesu anajibu, "Mimi Ndimi ... KWELI" (Yohana 14:16), na "Neno Lako ndiyo Kweli" (Yohana 17:17). Kwa hiyo Kweli ni “Kristo” na hili ni “Fundisho kuu la imani, au Fundisho la Biblia -Bible Doctrine.” au "Mafundisho" maana yake ni "Somo au Mada zilizomo katika Maandiko ya Bwana." (Doctrine)

Mfano, Biblia inafundisha Ukweli kumhusu Mungu. Yesu pia alifundisha Kweli kumhusu Mungu. Wakati ambapo wengi walimwona Mungu kama Mwenye Nguvu kupita yeyote yule, ama mwenye kukasirika isivyofaa kwa sababu ya kasoro za wanadamu au mwenye ukatili na yule asiyejali mateso ya mwanadamu, Yesu alimtangaza kuwa Huyu Baba wa mbinguni ni Mwenye upendo.

Yesu alisema kwamba Mungu ni Mwenye neema na mkarimu sana kiasi kwamba anatoa wokovu kwa yeyote anayemtumaini tu kwa moyo wake wote. “Kila amwaminiye” anao uzima wa milele (Yohana 3:16). Yeye Aliahidi kwa sauti ya upole, bila ya kuipaza juu au kugumia, “Iwekeni mioyo yenu yenye dhiki katika raha.... Mimi nikienda ..., nitakuja tena niwakaribishe Kwangu, ili Nilipo Mimi nanyi mwepo (Yohana 14:1-3, NEB). Yesu pia aliahidi kwamba hadi tufikie siku hiyo yenye furaha, Yeye Angekuwa pamoja na wanadamu kwa njia ya binafsi kabisa na kipekee, kupitia mwakilishi Wake, Roho Mtakatifu, ambaye ni kama Yeye tu (Angalia Yohana 14:15-18, 25-29; 15:26,27; 16:7-14).

Ili kuwahakikishia watu jambo hili, Aliwaalika wafuasi Wake kula mlo rahisi pamoja Naye (Meza ya Bwana), wakati huo akiwakumbusha. Anatamani kuwa "ndani" yao na kuwa sehemu yao. Yesu alifundisha kwamba mtu anapokufa, Mungu hamtesi mtu huyo katika mahali fulani pasipoonekana, bali humwacha apumzike, kwa amani "alale usingizi," usingizi usio na fahamu au ndoto mpaka pale katika ufufuo! (Yohana 11:11-14; 5:28, 29). Yesu pia alifundisha Ukweli kuhusu Mungu ambaye anataka kila mtu awe huru. Hakuna hata mtu mmoja anayepaswa kulazimishwa kuwa Mkristo. Watu wanapaswa kufundishwa kwanza na kisha kubatizwa ikiwa tu wamechagua kuamini (Mathayo 28:18-20; Marko 16:16).

Alifundisha zaidi kwamba, ikiwa tungependa kuendelea kuwa marafiki Zake, basi tunapaswa kushika amri za Mungu. Alituahidi msaada unaohitajiwa ili kufanya hivyo, akiongezea kwamba kuishi kwa kupatana na Mungu kungetuletea furaha. (Yohana 15:1-11). Yesu alisema Kweli za ajabu nyingi kumhusu Mungu kiasi kwamba watu waliomsikiliza "walishangazwa na Maneno ya neema yaliyotoka midomoni Mwake" (Luka 4:22 NIV). Hata kwa kuhatarisha kazi zao na maisha yao wenyewe, polisi au wanausalama wa hekalu wakati fulani walikataa kutii amri ya kumkamata Masihi, "hakuna Mwanadamu aliyewahi kunena kama mtu huyu," walikuwa wakisema (Yoh. 7:46)

Yesu alipoondoka duniani, aliwapa mitume Wake "Roho ya Kweli" ili waendelee kufundisha fundisho la Kweli—Kweli kuhusu Kweli. Cha kusikitisha ni kwamba mambo yalikwenda mrama. Kama vile Paulo alivyokuwa ameonya, walimu wa uongo walitokea (Matendo 20:28-31; 2 Timotheo 4:3, 4). Baada ya muda mfupi, Ukweli wa Kristo ulipotoshwa vibaya sana. Mafundisho ya uongo yalileta dhana potofu kumhusu Mungu; nayo yakaleta upotevu wa kiroho. Haki kwa imani haikusahaulika kabisa, na baadhi ya Wakristo katika kila zama walishikilia kwa uthabiti imani yao kwa Mungu. Lakini katika mkanganyiko wa zama za Kati, watu waliotamani kupata amani pamoja na Mungu mara nyingi walifundishwa kwamba pamoja na "kumwamini," Mungu kwamba alitaka waende kwenye hija ngumu, kutembelea mahali Patakatifu, na kufanya toba nyingine za aina mbalimbali.

Zaidi ya yote waliambiwa wabaki na uhusiano mzuri na wachungaji wao, kwa maana ilisemekana kwamba makuhani waliteuliwa na Mungu kushikilia funguo za mbinguni na kuzimu, na kuzifunga mbingu dhidi ya yeyote aliyefanya makosa. Kwa kuwa makuhani wengi wa siku hizo walikosa uaminifu na walikuwa wafisadi, watu wengi walikuja kumdharau Mungu kama walivyowadharau makuhani. Watoto walibatizwa mara tu walipozaliwa, wakageuzwa kuwa washiriki wa kanisa kabla ya kujua maana ya kuwa Wakristo. Marejeo halisi ya Kristo mara ya pili hayakukataliwa, lakini wanatheolojia wengine waliamini marejeo haya yalikuwa umeshatendeka kiroho.

Wakitumia vibaya Maandiko ya Ufunuo 20:4, walisema Kristo alikuja na kuwaweka maaskofu wake kwenye viti vyao vya enzi (cathedra) katika makanisa yao (Cathedrals).[3] Badala ya kufundisha kwamba katika kifo mtu hulala, ilisemekana kwamba watu ambao hawajabatizwa, walipokufa walikwenda moja kwa moja kwenye mateso ya milele katika jehanamu na kwamba hata waaminifu mara nyingi waliwekwa toharani (Pagatorio), mahali pa kati ya mbingu na Jehanamu, ambapo walichomwa moto fulani wa mateso kwa kipindi kisichojulikana kabla ya kusonga mbele kwenda mbinguni. Hekaya hizi zilibuniwa ili kuunga mkono nadharia hizi.

Kwa kielelezo walisema kuwa kuna kaburi huko Uingereza, lilisemekana kupanda juu na kushuka chini mara kwa mara, kama uthibitisho kwa wacha Mungu kwamba nafsi iliyozikwa humo ilikuwa ikiteswa kwa hali ya juu. Vijana walipouliza ikiwa wangeweza kuwasaidia wazazi wao waliokufa aidha babu na bibi zao kupita upesi zaidi kutoka toharani hadi mbinguni, walipewa mgawo wa toba na kuambia watoe malipo kwa ajili ya kutubia zaidi. Ikiwa wangeuliza, "Tumefanya vya kutosha?" jibu lilikuwa, "Hakuna anayejua."

Shajara za zamani na kazi za ibada za watawa na watakatifu, zinafunua siri kwamba kwa Wakristo wengi Meza ya Bwana iliendelea katika zama za Kati kuwa tukio la ushirika mtakatifu au meza ya Bwana, mahali penye ukaribu sana, na Mwokozi binafsi. Wakati huo huo, Maneno rahisi ya Yesu, “Huu ni mwili wangu”—yaliyotafsiriwa katika Kilatini, "Hoc est corpus meum," yaliaminika kugeuza mkate wa ushirika au meza ya Bwana kuwa mwili halisi wa Kristo,[4] na kuifanya mvinyo kuwa takatifu sana kiasi kwamba, ilibidi watu wa kawaida kukatazwa kuinywa wasije kwa bahati mbaya kumwaga "damu ya Mungu." Washirikina waliingia makanisani usiku wa manane ili kuiba vipande vya mwili wa Kristo na kunyunyiza kwenye kabichi zao mashambani kwa ajili ya kupata bahati njema.

Ilihisiwa na wengi kwamba kulikuwa na uhitaji mdogo wa mahubiri au, hata kwa hakika, waliona hakuna hitaji la ibada yoyote isipokuwa wakati ambapo kengele ya mkono ililia na mchungaji kutamka maneno, "Hoc est corpus meum." Huduma za ibada ziliharakishwa ili kufanya wakati huu wa ajabu za kishirikina uje kwa haraka. Maneno ya Kristo ya ushirika wa kiroho yakawa kwa mamilioni kama uchawi tu. Wakati Ukweli kuhusu Mungu uliposahauliwa na mafundisho ya uongo kuchukua mahali pake, watu wakazidi kuwa wazembe, wasiojali na wenye ushirikina kuhusu dini yao binafsi.

Kwa ujumla, walimwona Mungu kuwa mwenye hasira au asiyejali, asiye na hisia—kama vile Wayahudi walivyofanya kabla ya Yesu kuja na kuleta ujuzi sahihi wa Mungu na kuweka mambo sawa. Jinsi Mungu alivyokuwa na matamanio makubwa ya kuwasilisha ulimwenguni kwa mara nyingine tena na kwa kutumia ushahidi halisi kumhusu Yeye! Je, alikuwa na furaha iliyoje, pale John Wycliffe alipofungua akili

yake kwa ajili ya Kweli mpya! Wycliffe, mwanatheolojia mkatoliki mwaminifu alimpenda Bwana Yesu na aliamini kwamba Kristo Ndiye Chanzo cha Ukweli wote. Aliwasihi Wakatoliki wenzake waweke kando mapokeo mbalimbali yenye ubunifu wa wanadamu na kufuata Maandiko kama mwongozo pekee wa Mkristo. Maadui walitishia kumwua.

Wakati fulani alipokuwa amelala kitandani kwa ugonjwa, walikuja kumdhihaki. Lakini akainuka na kuketi kitandani, naye akasema, "Sitakufa, bali nitaishi, na nitatangaza tena matendo maovu ya mababa  au wazee wa dini." Wycliffe akawa baba au mwanzilishi wa tafsiri ya kwanza ya Biblia nzima kwa lugha ya Kiingereza cha zama za Kati (1150-1456 BK). Mamia ya nakala zilizonakiliwa kwa mikono zilisambazwa. Wahubiri maalum walioitwa Lollards walitumwa kote Uingereza wakiwa wamevalia mavazi ya kipekee wakisoma Biblia hii kwa watu na kuwafundisha watu kuyaweka Maandiko kama kipaumbele, yawe juu ya mapokeo.

Karne moja ilipita na Martin Luther akaja, mara nyingi alikuwa akipiga  magoti mbele za Mungu akitafuta Ukweli. Akiwa profesa katika chuo kikuu cha Kikatoliki, alitakiwa kufundisha Biblia kama Neno la Mungu. Lakini toba au vitubio vingi vilitakiwa kutoka kwake, vilivyohusisha toba na kujitesa mwenyewe kwa hiari, kiasi kwamba mbingu ilionekana kuwa haiwezekani kufikiwa, na Mungu akaonekana kwake kama hakimu mwenye hasira. "Je, mimi nampenda Kristo?" Alijiuliza katika wakati wa uchungu. "Namchukia"alijijibu mwenyewe. Maandishi ya Mtakatifu Augustino yalimsaidia. Kisha kwa msisimko mkubwa aligundua katika Biblia kwamba wenye dhambi hawaokolewi kwa “matendo yao” bali kwa imani sahili katika maisha, kifo, na ufufuo wa Yesu.

Aligundua Fundisho la Biblia la Ukuhani wa Kifalme (1Petro 2:9), Ukweli wa kusisimua kwamba kila mtu anaweza kuja kwa Kristo moja kwa moja bila uptanisho wa makuhani na watakatifu. “Milango ya Paradiso ilifunguka kwa upana/uwazi,” akasema, “nami nikaingia ndani moja kwa moja. Luther alikubaliana na Wycliffe kwamba Biblia na Biblia pekee ndiyo kanuni ya imani. Katika Baraza lililofanyika kwenye mji wa Worms, lijulikanalo kama Diet of Worms, mwaka 1521 alitangaza kwa ujasiri mkamilifu, "Nisipohukumiwa na Maandiko na sababu zilizo wazi, siwezi kufanya jambo lingine. Dhamiri yangu imefungwa kwa Neno la Mungu."

Luther pia alikubali kile ambacho Wycliffe aligundua kuhusu Meza ya Bwana, yaani, mkate haugeuki kuwa mwili na damu halisi ya Kristo.[5] Alisisitiza kwamba mlo/chakula hiki cha meza ya Bwana, ni tukio kuu ambalo Kristo anatuhakikishia msamaha wa bure wa kila dhambi. Hivyo Luther alikubali maarifa ya Wakristo waliotangulia katika ugunduzi upya wa ile Kweli, akaongeza mafunuo yake mwenyewe, na kurarithisha/kuyapitisha kwa mamilioni, nayo yakafundishwa hata baada yake. Ulaya yote ya kaskazini, maelfu ya Wakatoliki walishangilia pamoja na

Martin Luther. Idadi kubwa ya watu walitoa maisha yao kwa ajili ya imani yao. Wahudumu wa Kilutheri nyakati fulani walitundikwa kwenye miti kwa makundi. Ilionekana kwao kuwa ni rahisi vya kutosha kutoa vyote kwa ajili ya Ukweli kuhusu Mwokozi wao.

Katika Ufaransa na Uswisi Wakatoliki wengine waliojitoa waliendelea na mafunzo yao na kugundua Ukweli wa ziada ambao ulikuwa umefichwa katika zama za Kati. Mashuhuri zaidi kati ya hawa, ni John Calvin, baba wa Presbyterian na Congregationalists, mtu huyu alikuwa na akili yenye mantiki kama ya Luther ilivyokuwa na shauku. Aliupanga vyema Ukweli wa Kibiblia wa kusisimua uliokuwa umeanza kudhihirika.

Ni bahati mbaya kwamba jina la Calvin leo linahusishwa kwa dhihaka na fundisho la hatima ya uzima wa milele wa mtu, kuamuliwa mapema kwa wokovu wa mtu, bila hata hiari yake mwenyewe huyo mtu, (Predestination)." Ni kweli alifundisha jambo hili, lakini kwa watu wa wakati wake haikusikika kama inavyosikika kwetu leo. Wakati huo watu walikuwa wamefundishwa kwamba hatima yao ilitegemea utii kwa makuhani na maaskofu ambao "walikuwa na funguo" za ufalme wa mbinguni. Calvin alisema kwamba hatima ya watu kwa hakika iliamuliwa mapema— hata hivyo, si na wanadamu, bali na Mungu, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu!

Ni vigumu leo kuelewa kitulizo kikubwa sana ambacho makutaniko ya Calvin yalipata walipojifunza kutoka kwenye Biblia yenyewe, kwamba hatima yao ilikuwa mbali sana na mielekeo ya uroho na tamaa zisizo na busara na zenye kubadilika-badilika, kwa kutotabirika, za wachungaji na makasisi kiasi kwamba ilifumbuliwa wazi na Mungu maelfu ya miaka kabla ya watu hao kuzaliwa. Calvin hakuwa sahihi kabisa. Alifundisha kwamba mara tu mtu anapokuwa amechaguliwa na Mungu kwa ajili ya wokovu, hata mtu huyo mwenyewe hangeweza kuchagua kupotea, hata afanyeje. Hata hivyo, alipoweka hatima ya mwanadamu mikononi mwa Mungu badala ya mikononi mwa wanadamu wengine, aliwasogeza watu wake karibu zaidi na Kweli ya Biblia.

Calvin aliweka mbele ya wafuasi wake uwezekano wa ushindi juu ya dhambi zaidi ya Luther alivyofanya na kuwapa uthubutu wa kuishi kila siku kwa ushindi kuliko walivyokuwa wameishi siku iliyopita. Ingawa Luther alirejesha hasa fundisho la hali yetu ya kubadilishwa mbele za Mungu (kuhesabiwa haki kwa njia ya imani), Calvin alisisitiza mabadiliko ya tabia (utakaso kwa imani) ambayo neema ya Mungu hufanya iwezekanavyo. Maelfu ya Wakatoliki walikubali kwa shukrani ile Kweli iliyorejeshwa ambayo Calvin aliwafundisha, na wengi wao pia walitoa maisha yao kwa Mungu kupitia mafundisho hayo.

Katika Uingereza wafuasi wa Calvin walikuja baada ya muda kujulikana kama Wapuriti kwa sababu  walihangaikia kutakasa kile kilichoonekana kwao kuwa Ukristo usiokomaa zaidi wa Kanisa jipya la Anglikana. Kwa watu wa imani ya Wapuriti, leo tunawiwa (deni) la toleo la Biblia ijulikanayo kama King James (King James Version). Mnamo 1603 walimwomba Mfalme James wa Kwanza asaidie kutoa tafsiri mpya ya Biblia, ili itumike katika ibada. Mfalme akakubali na akateua wasomi arobaini na saba wa ulimwengu wa wakati wake kutekeleza jukumu hilo

Miaka minane baadaye, yaani mwaka wa 1611, tafsiri maarufu ya King James Version ilitoka kwenye mitambo ya uchapishaji na kufikia watu. Je, ni nani kweli, anayeweza kukadiria kile ambacho tafsiri hii imefanya, kwa utukufu wa Mungu? Katika bara la Ulaya Wa-Anabaptisti wacha Mungu walitoa wito wa "ubatizo wa mtu anayeamini." Na waliyatoa maisha yao kwa ajili ya jambo hili kwa Mungu pale ilipobidi. Mwana-Anabaptisti wa kwanza kufa inaonekana alikuwa msichana mzuri wa Uswisi ambaye kichwa chake kilishikwa na kushinikizwa chini ya maji kwenye bwawa la farasi kama dhihaka ya kuigiza ubatizo wa waamini.

Wengine walikufa kwa njia hii au kwa kuzamishwa kwenye mito au kuchomwa moto kwenye chanja za miti au kuchomwa kando ya moto kama mishikaki. Wengine walilazwa kwenye majeneza yaliyo wazi ambayo yalikuwa madogo sana kwao. Wanajeshi waliwapiga teke na buti zao zenye misumari. Wanaofanana na Wa-Anabaptisti katika bara la Ulaya walikuwa Wabaptisti wa Uingereza na Amerika.[6] Hawa pia walisisitiza ubatizo wa mtu aliyefundishwa na kuamini tu na kwamba watoto wachanga hawapaswi kubatizwa. Lakini tofauti na Wa-Anabaptisti wengi wao walisonga mbele hadi "kubatizwa kwa kuzamishwa." Katika karne ya kumi na nane mafundisho juu ya hatima ya uzima wa milele iliyoamuliwa mapema yalianza kufifia na kupoteza nguvu..

Mamilioni ya watu ambao hawakuwahi kuhisi woga wa makuhani walianza kuogopa kwamba huenda Mungu Mwenyewe Ndiye aliyewachagua wapotee! John Wesley alirejesha Ukweli wa Agano Jipya kwamba wokovu ni bure kwa wote - kwa "yeyote aaminiye" (Yohana 3:16). Wesley alianzisha Kanisa la Methodisti, ambalo lilikubali kanuni za “Biblia na Biblia pekee,” “ukuhani wa waumini (1 Petro 2:9), hali ya Meza ya Bwana kuwa ukumbusho unaoletwa kupitia imani, hisia ya uponyaji wa Kristo na uwepo wa Kristo, na fundisho kwamba maisha ya Mkristo yanapaswa kugeuzwa, kuwa na mabadiliko (Warumi 12:2). Wesley daima alishikilia Fundisho la ubatizo wa watoto wachanga, lakini yeye na kanisa lake waliruhusu ubatizo kwa kuzamishwa kwa wale walioutaka (Ellen Harmon alibatizwa kwa kuzamishwa ndani ya maji katika Kanisa la Methodisti)

Walichofanya Wamethodisti kilikuwa mfano kwa Wakristo wengine. Walikubali Ukweli kutoka kwa wale waliotangulia na kuongeza nuru mpya zaidi, na kwa njia hii

Ukweli wa Mungu ulionekana wazi zaidi. Kulikuwa na Wakristo mmoja-mmoja, pia, kwa karne nyingi, ambao walijifunza kwamba Mungu hawatesi wenye dhambi baada ya kifo bali huwaacha wapumzike (Hakuna kukaa toharani au pugatori). Wycliffe aliamini katika "usingizi usio na fahamu kati ya kifo na ufufuo yaani-kutoka pale mtu anakufa mpaka Yesu anapokuja na kufufua watu kwenda kuishi nao mbinguni milele mtu analala usingizi wa mauti, anakuwa hana ufahamu." Martin Luther alifundisha kwamba kifo katika Kristo "ni usingizi mzuri, mtamu na mfupi."

Huko Uingereza, Mwanglikana aitwaye Francis Blackburne, Mbaptisti Matthew Caffyn, na mshairi Mpuritani John Milton walishiriki imani hiyo. Huko Marekani mtumishi katika kanisa la Methodist aitwaye George Storrs ambaye alikuwa mtumishi wa kanisa la Congregationalist, Charles Fitch pia walifundisha kuwa kifo ni usingizi (1 Wathesalonike 4:13-14). Hii ni mifano michache ya idadi kubwa ya walioamini.[7] Rejea za Storrs na Fitch zinatukumbusha kwamba mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa kulikuja mwamko mkuu wa marejeo ya pili ya Yesu kwenye madhehebu mbalimbali, ambapo Ukweli kuhusu marejeo ya pili ya Yesu yaling'aa kwa mng'ao mkuu kuliko ulivyokuwa tangu karne ya pili. Kutoka katika mwamko huo liliinuka Kanisa la Waadventista Wasabato.

Annie Smith alikuwa Mbaptisti. Rachel Oakes alikuwa Mbaptisti wa Siku ya Saba. Hiram Edson, Frederick Wheeler, na Ellen Harmon walikuwa Wamethodisti, Joseph Bates na James White walikuwa washiriki wa Christian Connection. Stockbridge Howland alikuwa Congregationalist. Hawa wote na maelfu ya wengine waliongezeka na kuwa Waadventista Wasabato katika siku za mwanzo za vuguvugu jipya, hawakuacha Ukweli mzuri kuhusu Mungu ambao walikuwa wamejifunza katika madhehebu yao ya awali. Badala yake, walipata utukufu mpya ndani yake kwa vile walijifunza dhana tajiri, zilizosheheni kwa thamani zaidi.

Kuhesabiwa haki kwa njia ya Yesu Kristo, ushindi kwa Roho Mtakatifu, wokovu kwa njia ya imani pekee, Biblia kama kanuni pekee ya imani, ukuhani wa waamini, ubatizo wa kuzamishwa, marejeo ya  Kristo yaliyo karibu - yote haya (yaani Mafundisho haya makuu ya imani kutoka kwenye safari ya imani, na mengine mengi) Waadventista Wasabato waliyatoa kutoka kwenye makanisa yao ya zamani. Katika haya mafundisho ya imani (Doctrines) waliongeza fundisho la Sabato (kutoka kwa Wabaptisti wa Siku ya Saba) na kukoka huo moto wa hili fundisho mpaka likawa mwenge/tochi angavu. Zaidi ya wote waliowatangulia, watu hawa walifundisha kwamba Mungu Mkarimu na Mwenye neema huwaacha wafu walale usingizi mpaka ufufuo. Kwa njia kuu zaidi, waliuhubiri ulimwengu habari zenye kusisimua kuhusu kazi kubwa mpya ambayo Yesu anashiriki sasa mbinguni.

Kwa hivyo Waadventista Wasabato wanaposema kwamba wanayo "Kweli," wanamaanisha kwamba wana Ukweli ambao Wakristo wengine waliushikilia mbele

yao, na pia Ukweli wa sasa, Ukweli maalum wa ziada ambao unatumika hasa kwa wakati huu wa sasa. Ujuzi wa kwamba Yesu Yuko mahali Patakatifu sana, akifuta dhambi, haungekuwa Ukweli katika siku za Martin Luther. Yesu hakuwa katika Patakatifu pa Patakatifu wakati huo. Lakini Yeye Yuko huko sasa. Na matokeo au hatima yake ni kubwa sana.

Waadventista wanapomwalika rafiki aache dhehebu lake na kuwa Msabato, hawatarajii aache kila kitu anachojua kama Mmethodisti au Mbaptisti au Presbyterian au Mkatoliki. La hasha! Mbali kabisa na wazo hilo Kila kipengele kizuri cha Ukweli kuhusu Yesu katika kanisa lake la awali, anapaswa kukithamini hata kwa uchangamfu zaidi na jotojoto kwa upendo, anapokuwa katika Kanisa la Waadventista Wasabato, akiongeza mambo ya utukufu ambayo tayari anajua ukweli mkuu na muhimu uliogunduliwa na Waadventista Wasabato.

Msabato anaposema ana “Ukweli,” hajisifu. Huo Sio Ukweli wake. Ni Kweli ya Mungu; Ukweli ambao Mungu ameufunua, sio ili kuridhisha udadisi tu, bali ili uenezwe kila mahali kwa kila mtu atakayesikiliza, kwa kila mtu ambaye Kristo alitoa uhai Wake kwa ajili yake na kila mtu ambaye Kristo anaishi ili kumwokoa. Mungu ameweka Kweli hii yenye kung'aa mikononi mwetu. Sasa Yeye anatutaka kuweka umakini wa dharura, akitarajia, tutakimbia na ujumbe huu, Ukweli huu na kuiambia dunia.

*Vidokezo:*

*1. Ellen G. White, Testimonies, vol. 4, p. 595*

*2. Penances, as the word is used in this paragraph, were various activities assigned by a priest and intended to show that a person was truly repentant for his sins. The most common penances consisted of reciting the Lord's Prayer and the Ave Maria a specified number of times. The Ave Maria is the prayer that begins, "Hail, Mary, Mother of God, blessed art thou above women"*

*3. Augustine taught that the millennium is going on now, and that the bishops have already been authorized to sit on their thrones in judgment*

*4. Catholics in the later Middle Ages taught that the "substance" of the bread turned into the "substance" of the body and blood of Christ, a process they called "transubstantiation." By "substance" their theologians did not imply the 254 common meaning of this term. Rather they meant that the "breadness" of the bread turned into the "bodyness" of Christ's body--while the appearance of the bread remained unchanged*

*5. Wycliffe and Luther believed that Christ's body was "really" present in the bread, a doctrine sometimes described as "consubstantiation." Nonetheless, by denying transubstantiation, they*

*made a significant advance in the direction of truth. (They did not believe that Christ was confined only to the bread, of course)*

*6. English Baptists have a complex origin. They seem to have arisen in part from roots in the British Isles, and are not to be regarded as merely a modification of the Anabaptists.*

*7. LeRoy Edwin Froom, The Conditionalist Faith of Our Fathers, 2 vols. (Washington, D.C: Review and Herald Publishing Association, 1965-1966), pp. 58, 78, 142, 205, 300-314*

## SURA YA 16
## YESU NA "HUKUMU YA UPELELEZI"

Ikiwa Daudi na Neema ambao ni Waadventista, wangeweza kutoka vitandani mwao mapema zaidi asubuhi ya Sabato ya kiangazi katika miaka ya 2025, na kisha wangeruka na kurudishwa nyuma katika wakati wa zamani au kale kuwahi kuwepo na kuhudhuria kanisani pamoja na Waadventista Wasabato wa mwaka 1851, wangehitaji kujitayarisha kupatwa na mshangao fulani mkubwa haswa. Ingawa wangegundua kwamba akina Howlands au Beldens au Chamberlain au Arnolds (au yeyote yule waliyeketi karibu naye wakati wa huduma kanisani) alithamini mafundisho mengi ambayo walikuwa wanayafahamu.

Daudi na Neema wangegundua upesi kwamba kwa namna ya ajabu baadhi ya vipengele vya Uadventista wa kisasa havikuwako hapo kabla, au huko nyuma. Mfano Jambo moja ni kwamba “ibada” isingefanyika kanisani. Waadventista Washika Sabato walijenga kwa mara ya kwanza majengo ya kanisa huko Battle Creek, Michigan, na Bucks Bridge, New York, mwaka wa 1855. Wakati James White alipojumuisha wimbo fulani alioupenda wa Kimethodisti katika Nyimbo zake za 1850

za Watu wa Pekee wa Mungu, aliyaacha nje maneno, " Katika siku yako hii, katika nyumba yako hii." [l]

Waadventista wa awali walikutana katika nyumba zao wenyewe, na familia kadhaa zikiabudu pamoja chini ya paa moja. Inaelekea kwamba pasingekuwa na mahubiri siku ya Sabato asubuhi wakati Daudi na Neema wanapotembelea kanisa au ushirika unaofanyika nyumbani mwa mtu. Kufikia 1851 wachungaji waliowekewa mkono kama watumishi wa kanisa walikuwa wameongezeka na kujumuisha William Ingraham, George Holt, na wengine kadhaa pamoja na Joseph Bates na James White; lakini hapakuwa na wahubiri wa kutosha kukidhi mahitaji ya mikusanyiko yote ya kila juma ya "makundi yaliyotawanyika."

Mahubiri ya Sabato asubuhi yalikuwa nadra sana; hakukuwa na hotuba. Ziliimbwa nyimbo za tenzi za kawaida za Sabato kwa kusindikizwa na kinanda cha organ (pump organ) (ikiwa familia inayoongoza ilibahatika kukimiliki hicho kinanda), Maandiko na Chapisho la Review yalisomwa kwa sauti na waumini wa eneo hilo na kujadiliwa, maombi yalitolewa, na, kulikuwa na uwezekano mkubwa kabisa, wa kuwa na “mkutano wa kijamii" ambapo waumini waliungamiana makosa yao wao kwa wao na kutoa ushuhuda wa imani yao. Ikiwa Daudi na Neema wangekumbuka kubeba Biblia zao, wangezitumia vizuri, kwani walizifungua na kuchunguza mno Maandiko. Lakini mikoba yao yaelekea ingebaki bila kufunguliwa (au hata wasingezishika simu kila mara humo).

Matoleo ya Sadaka leo, katika mikusanyiko ya kisasa huwa ni ya lazima kwa Waadventista Wasabato, siku zile za miaka 1851 katika matukio mengi, ni kama hukuweza kusikia kuhusu ukusanyaji wa sadaka. Misheni za kigeni hazikufikiriwa hadi miaka ya 1870, na wachungaji au wahudumu wa Kiadventista katika miaka ya 1850 mara nyingi walifanya kazi zao wakiwa na malipo duni sana—malipo ya chini sana kujikimu kimaisha.

Mshtuko mkubwa ungewapata Daudi na Neema katikati ya siku wakati wanapoalikwa kwenye chakula cha mchana, na kukuta nyama ya nguruwe imewekwa kwenye meza - na kuwaona baadhi ya watu wengine ambao pia walialikwa kwenye chakula cha jioni wakiwasha kiko na kuvuta tumbaku, wakati wakisubiri mlo wao! Uvutaji sigara, ingawa uliruhusiwa japo kwa shingo upande miongoni mwa ndugu, washiriki waliruhusiwa kwa moyo wa kusita-sita miongoni mwa waumini wa awali mnamo 1851, na maono ya kwanza ya Ellen White kuhusiana na matengenezo ya afya yalikuja miaka kumi na miwili baadaye.

Mshtuko mwingine ungekuja saa 12 jioni. Huku machweo ya majira ya kiangazi yakiwa bado yamesalia saa kadhaa, Daudi na Neema wangetazama bila kuamini kwamba wenzao wa 1851 mara moja wanaposoma kwamba saa inasema ni saa 12

jioni, wanaanza majukumu ya kazi zao za kawaida za siku za juma! Hawakugundua Fundisho la Masaa ya Sabato, ni kutoka jua linapotua Ijumaa hadi mpaka jua litakapotua Jumamosi, hadi Novemba 1855 ndipo ambapo waanzilishi wa Kiadventista walikuja kupata maarifa ya Biblia kwamba Sabato ni “tangu jioni hadi jioni, mtaishika hiyo Sabato yenu,” (Mambo ya Walawi 23:32) inamaanisha kuanzia machweo ya jua hadi machweo ya jua, kama walivyodhani, na sio saa sita hadi saa sita.

Na hata wakati wa chakula cha jioni kabla ya kurudi nyuma wakati wa miaka hii ya 2025, Daudi na Neema wangezungumza kwa wasiwasi kuhusu hali ya kuwa watu wa "Laodikia" ya mtu mwingine, wangekutana na macho ya watu ya mshangao kwa kutoelewa maana yake hiyo ni nini. Waadventista Washika Sabato walitumia ujumbe wa Walaodikia kwa Waadventista washika Jumapili hadi nuru iliyo wazi zaidi (na ya kufanya waone aibu) ilipokuja mwaka wa 1856. Yote haya yanaonyesha Ukweli kwamba ugunduzi wa nuru mpya haukufikia mwisho, kwa sababu tu ya kuanzishwa kwa Mafundisho ya "alama ya kihistoria-Landmark Doctrines"[2] kwenye miaka ya mwishoni mwa miaka ya 1840.

Kweli kuu mpya za Biblia ziliendelea kudhihirika, kwa kuwekwa wazi/nuruni katika miaka ya 1850—kama vile vile katika miaka ya 1860 (Kuishi Maisha yenye afya), miaka ya 1870 (Utume kwa mataifa mengine na Elimu), miaka ya 1880 (ufahamu wa kina juu ya haki kwa imani), na miaka ya 1890 (ufahamu zaidi  nafsi ya Kristo). Kwa hakika, uelewa wa Waadventista wa Biblia uliendelea sana baada ya miaka ya 1900 pia, na hasa katika miaka ya 1950, 1960, na 1970. Lakini tukirudi miaka ya 1850, inafaa kuchunguza imani fulani ambayo iliendelezwa katika muongo huo na ambayo ingekuja kuwa sifa au utambulisho wa vuguvugu la Marejeo. Hili ndilo fundisho la "hukumu ya upelelezi."

Alipoulizwa swali "Je, Yesu alianza kazi gani mpya mwaka 1844?" Mwadventista Msabato atajibu kirahisi sana bila hata kupepesa macho, "Hukumu ya upelelezi." Kwa kushangaza, wakati rafiki Wa Hiram Edson alipoandika ufahamu wao mpya mkuu wa Siku ya Upatanisho katika Gazeti la Day Star Extra--chapisho ambalo Ellen Harmon alihisi "limeidhinishwa kikamilifu na Bwana kupendekezwa kwa kila mtakatifu" - hakupumua au kutamka hata neno moja kuhusu hukumu ya upelelezi. Una maana hukumu?  Mkazo wake, badala yake, ulikuwa juu ya kazi ya Kristo ya kufuta dhambi katika Patakatifu na juu ya utakaso wa watu.  Pengine haya yalikuwa majaliwa na mipango ya Bwana.

Kusudi kuu la Siku ya Upatanisho ya kale lilikuwa hakika ni kufutwa kwa dhambi katika Patakatifu na kusafishwa kwa watu. Bwana (kupitia Musa) aliwaambia watu kwamba kuhani mkuu aliingia Patakatifu pa Patakatifu ili "kufanya upatanisho kwa ajili ya Patakatifu" na "kuwatakasa, ili mpate kuwa safi na  dhambi zenu zote mbele

za Bwana” (Mambo ya Walawi 16:33, 30). Lakini Siku ya Upatanisho pia ilikuwa siku ya hukumu. Waisraeli walitazamiwa “kuzitesa nafsi zao” siku hiyo. Yaani, walitakiwa kuchunguza mioyo yao hadi kwenye kiini cha mioyo yao ili kuona kama kweli walikuwa na majuto kwa ajili ya dhambi walizoungama siku baada ya siku katika mwaka uliotangulia.

Mwisraeli yeyote ambaye alikataa kufanya hivyo alipaswa kuchunguzwa na wazee na kukatiliwa mbali na kutaniko (Mambo ya Walawi 23:29). Lakini Siku ya Upatanisho kipaumbele chake hakikuwa siku ya hukumu. Kimsingi ilikuwa siku ya ushirika wa karibu na Mungu na ya utakaso wa mwisho kutoka kwenye dhambi. Watu waliorudi nyuma "walitengwa ushirika" siku hiyo sio kwa sababu ilikuwa siku ya hukumu ila kwa sababu ilikuwa siku ya fursa kuu ya kiroho - nao hawakujali ndio sababu ya kutengwa. Wafuasi wa Miller walihusisha hukumu na kutakaswa kwa Patakatifu si kwa sababu walikutana na hukumu katika Siku ya Upatanisho ya Mambo ya Walawi 16 bali kwa sababu mwisho wa siku 2300 za Danieli 8:14 unafanana na mandhari ya hukumu katika Danieli 7:9-14, tukio. ambalo walilitafsiri kimakosa kuwa ndio ujio wa pili.

Hii ndiyo sababu walihubiri ujumbe wa malaika wa kwanza, “Saa ya hukumu Yake imekuja,” Yesu alipokosa kufika tarehe 22, Oktoba 1844, baadhi ya wana Miller walidhani kwamba Bwana alikuwa ameanza kipindi kifupi cha hukumu mbinguni na mwishoni mwa kipindi hicho, angeshuka duniani. Lakini alipokosa kufika tena kuonekana kulingana na matarajio yao, waliacha wazo hilo. Wakati wa miaka ya 1850, hata hivyo, J. N Loughborough na Uriah Smith, ambao wote waliingia kwenye utunzaji wa Sabato mwaka wa 1852, walielekeza umakini wao kwenye kipengele hiki cha hukumu cha Siku ya Upatanisho.[3]

Mnamo 1857, miaka miwili baada ya ofisi ya Review and Herald kuhamishwa kutoka Rochester, New York, hadi Battle Creek, Michigan, James White alitumia neno "Hukumu ya Upelelezi." Ni dhahiri kabisa kwamba ikiwa ujumbe wa malaika wa kwanza (“saa ya hukumu Yake imekuja”) unatangulia ujumbe wa malaika wa pili na wa tatu, basi saa ya hukumu ya Mungu lazima ifike kabla ya mwisho wa dunia ili kuruhusu ujumbe wa malaika wa pili na wa tatu uhubiriwe baada ya hukumu kuanza. Hukumu ya Siku ya Upatanisho katika Israeli ya kale ilihusu tu watu wa Mungu. Ni wale ambao walikuwa wameungama dhambi zao katika mwaka huo. Hao ndio ambao dhambi zao zingefutwa. Na ni wao tu, na sio watu wa Mataifa, ndiyo ambao walikuwa chini ya kigezo cha "kukatiliwa mbali."

Yesu alirejelea hukumu hii maalum ya waamini katika mifano Yake. Alizungumza juu ya wavuvi wanaovua kila aina ya samaki (waongofu) katika nyavu zao (kanisa) na kisha kukaa chini (katika hukumu) kutunza samaki wazuri na kutupa wale wabaya (Mathayo 13:47-50). Alisimulia kisa cha mfalme aliyealika kila mtu kwenye karamu

ya arusi na kisha, kabla tu ya mlo huo, akawakagua wageni ili kuona ikiwa wale waliokubali mwaliko huo walikuwa wamevaa pia vazi la arusi walilopewa bure. Mwenye arusi alipompata mtu ambaye alifikiri kwamba mavazi yake mwenyewe yanatosha, bila vazi la arusi alilopewa bure, alimwamuru atoke nje (Mathayo 22:1-14).

Yesu pia alisimulia juu ya mtu aliyekuwa na deni la talanta 10,000 kwa mwajiri wake. Wakati mfanyakazi aliomba rehema, alisamehewa kwa uhuru. Lakini alipotoka nje na kumdhulumu mfanyakazi mwenzake aliyekuwa na deni lake la dinari mia mwajiri huyo aliamuru atupwe gerezani. “Vivyo hivyo,” Yesu akamalizia, “na Baba yangu wa mbinguni atawatenda ninyi, ikiwa ninyi hamsamehe kila mtu ndugu yake kwa mioyo yenu (Mathayo 18:23-35).

Wakati katika mwaka wa 1844 Yesu alienda juu ya mawingu ya mbinguni (Danieli 7) kuanza hukumu hii ya kabla ya kuja mara ya pili, Alianza upelelezi katika kumbukumbu za watakatifu ili kuona wale ambao walikubali Mwaliko Wake wa wokovu kama walikuwa wamevaa vazi la haki Yake; ili kuona kama wale waliosamehewa dhambi za talanta 10,000 wakati wa kuongoka wamewasamehe watu wengine waliokuwa na deni la dinari mia moja. Fundisho muhimu sana kama hili limekuwa likihusisha mawazo ya Waadventista Wasabato kwa miaka mingi tangu kugunduliwa kwake. Ellen G. White aliandika juu yake mara kwa mara na kwa uwazi. Alisema, kwa mfano, kwamba huduma ya mwisho ya Kristo katika Patakatifu pa mbinguni kwa hakika ni wakati wa hukumu ambapo kila jina lililoandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo linatwaliwa moja baada ya lingine, na ambapo baadhi ya majina yanahifadhiwa na mengine kufutwa (Tazama Ufunuo 3:5; 21:27; 22:19).

Sasa Danieli 7 inasema kwamba hukumu hii imewekwa ili kutoa "ufalme na mamlaka na ukuu wa ufalme chini ya mbingu zote" kwa "watu wa watakatifu Wake Aliye juu." Upeo wake mkuu, kwa hiyo, tofauti na ule wa mahakama nyingi za kidunia, ahuhusiani sana na hukumu ya mshitakiwa, kama kuhesabiwa haki kwa wale waliokombolewa. Kwa sababu Mungu anatamani sana kuwaheshimu watu Wake katika hukumu hii, anatoa amri rasmi, ya kitabu cha ukumbusho ili kiwe ushahidi (Malaki 3:16) ambapo “kila tendo la haki” lililotendwa na watu Wake, “kila jaribu waliloshinda, kila uovu walioushinda, kila neno la huruma nyororo lililoonyeshwa” Yote haya yameandikwa kwa uangalifu, pamoja na kila dhabihu na huzuni watuw waliyoistahimili kwa ajili ya Kristo.[4]

Hatuna shaka kuwa Mungu anajua hatima ya hukumu mapema. Yeye Anaendesha hukumu mbele ya malaika wasio na idadi (Danieli 7:10) ili nao waweze kuijua pia. Yeye Anataka kila mkaaji wa sayari zote ambazo hazikuanguka dhambini ajivunie juu ya watakatifu Wake wanaooishi katika dunia yetu hii, ila walio dhati na wenye

bidii ambao hivi karibuni watashiriki furaha za umilele pamoja nao. Hukumu, alisema Ellen White katika mwaka 1898, "inafanyika mbele ya malimwengu mengine yote pia (sayari zingine zenye viumbe wa Mungu wasioanguka), [ili] upendo, uadilifu, huduma, ya mwanadamu kwa Mungu, iweze kuheshimiwa kwa kiwango cha juu zaidi."[5]

Ajabu iliyoje enyi mbingu! shangilia , Ee nchi! "Watakuwa Wangu, asema Bwana wa Majeshi, katika siku ile niifanyayo"—sio changarawe Zangu, wala mawe Yangu—bali "vito Vyangu" (Malaki 3:17). Katika makadirio Yake ya tabia, Mungu hafanyi makosa. Angalia maneno ya Ellen White: "Wazo hili ni zito jinsi gani! Kwamba Siku baada ya siku ... matendo yetu, maneno yetu, hata nia zetu za siri zaidi, zote zina uzito wake katika kuamua hatima yetu ya tulivyonavyo au ole."[6] Wale "waumini" ambao hawajakua katika neema hawataruhusiwa kuingia katika mji mtakatifu. Lakini Kristo anapoona kwamba mtoto Wake ameshikamana Naye kwa uaminifu hadi mwisho, kwa ushindi Yeye anadai kwa niaba ya mtu huyo kuhesabiwa haki kwa kina na kwa ukamilifu.

Kuhusu wakati huo mtukufu ambapo dhambi za wenye haki zitafutiliwa mbali hatimaye, kikamilifu, na milele, Ellen White aliandika kwa uchangamfu mkubwa: "Kristo atawavika waaminifu Wake haki Yake Mwenyewe juu ya ahadi ya agano jipya, 'Nitausamehe uovu wao, na dhambi yao sitaikumbuka tena.' 'Katika siku hizo, na wakati huo, asema Bwana, uovu wa Israeli utatafutwa, wala hautakuwako" (Yeremia 31:34; 50:20)."[7] Inaonekana ni jambo lisiloeleweka kwenye ufahamu wetu: "Sitazikumbuka dhambi zao tena." Je, Mungu asiye na mwisho anaweza kusahau chochote? Je, yaliyopita, ya sasa, na yajayo yapo sawa, yaani yanafanana tu kwa ujuzi Wake Yeye Mwenye kujua yote?

Lakini Biblia haisemi kwamba Mungu hawezi kukumbuka dhambi zao tena. Inasema kwamba Mungu kwa kusudi Lake, Yeye hatakumbuka tena kwamba walikuwa watenda dhambi. Jinsi gani jambo linavyofunua mambo mengi kama nini kumhusu Baba wa mbinguni! Kwa hamu iliyoje Yeye Baba anatamani wakati huu wa kufutwa kwa dhambi ya kila mwanadamu ufike! Jinsi Alivyotamani sana wakati huu ufike, tangu wakati uasi ulipoanza, Yeye alitamani kuondoa dhambi ulimwenguni na kwa watu Wake mara moja na milele na milele! Atakapofunga kesi za watu Wake, Yeye hatazikumbuka dhambi zao tena - si kwa sababu hawezi kukumbuka, lakini kwa sababu ya mkazo Wake na nguvu ya upendo Wake, Yeye hatazikumbuka.

Dhambi zao zitakapofutwa, watakatifu hawatadai kuwa wao hawana dhambi. Hawahitaji kufanya hivyo. Wanadai na kutumainia kutotenda dhambi kwa Kristo na kukumbatia hili kwa nguvu. Kumbukumbu zao kwamba wamepungukiwa sana na utukufu wa Mungu na katika ufahamu wao wanamtegemea Yesu kabisa kwa ajili ya usalama na msaada inatosha kuzuia dai lolote la kujihesabia haki. Hata hivyo wakati

mlango wa rehema unapofungwa na wakati wa taabu ya Yakobo unapoingia,[8] ingawa watakatifu "wana utambuzi wa kina wa kutostahili kwao, hawana makosa yaliyofichika."[9] Dhambi zao zilizoungamwa zimefutwa, wala hawakuacha kuungama hata moja. Dhambi zao "zimetangulia hata hukumuni."[10] "Wamechukuliwa hadi katika nchi ya usahaulifu."[11] "Dhambi zao ... zimefutwa."[12]

Nao wajumbe wa mbinguni wanatangaza kwa furaha, wakisema, Mmetakaswa dhambi zenu zote mbele za Bwana. Lakini je, dhambi zinaweza kufutwa kutoka katika vitabu vya kumbukumbu vya mbinguni tu? Hebu tuseme ikiwa kwamba baada ya dhambi zao kufutiliwa mbali watakatifu walitenda dhambi mpya—"kufutwa" kungemaanisha nini? Mungu anaweza kufuta dhambi za wale wanaokufa katika imani kwa kuzingatia tu kumbukumbu zao. Watu hawa wamekufa na hawawezi tena kutenda dhambi. Lakini je, haitakuwa tofauti kabisa kwa wale walio hai wakati majina yao yanapoitwa katika hukumu? Je, dhambi zao zinaweza kufutwa mbinguni bila ya wao kuwa wameshinda kabisa hapa duniani? "Kufutwa kwa dhambi" lazima kufikiwe katika mioyo ya watakatifu walio hai kabla ya kutimizwa katika vitabu vyao vya kumbukumbu.

Ellen White aliandika kwa msisitizo sana kuhusu hili katika Kitabu cha 'The Great Controversy' au Pambano kuu, soma kwenye (RohoYaUnabii.Org): "Sasa, wakati Kuhani wetu Mkuu anafanya upatanisho kwa ajili yetu, tunapaswa kutafuta kuwa wakamilifu katika Kristo. Mwokozi wetu asingeweza kujisalimisha kwa nguvu ya mjaribu hata kwa wazo peke yake…... Hapakuwa na dhambi ndani Yake ambayo Shetani angeweza kuitumia kwa faida yake. Hii ni hali ambayo watu watakaokutwa wamesimama katika wakati wa taabu, wanapaswa kuwa nayo."[13]

Katika mwaka ule ule ambapo mistari hii ilionekana, Ellen White alitoa mahubiri[14] siku ya Sabato alasiri kwenye Mkutano Mkuu wa General Conference mwaka wa 1888 uliofanyika Minneapolis, Marekani, ambapo alikumbusha kutaniko lake kubwa kwamba "sasa Kristo Yuko katika Patakatifu pa mbinguni." Kisha akauliza, "Je, Anafanya nini humo?" "Yeye anafanya upatanisho kwa ajili yetu," jibu likafuatia, "Anasafisha Patakatifu kuondoa dhambi za watu," Ni nini kinachofuata? "Basi sisi tunapaswa kuingia kwa imani katika Patakatifu pamoja Naye, lazima tuanze kazi katika Patakatifu pa roho zetu. Tunapaswa kujitakasa kuondoa uchafu wote. Ni lazima 'tujitakase na uchafu wote wa mwili na roho, huku tukitimiza utakatifu, katika kumcha Mungu.' "Je, ni lazima tufanye hivi? Je, ni lazima tujitakase kutokana na uchafu wote? Je, hili liko kwenye Biblia? Hakika.

Alinukuu 2 Wakorintho 7:1. Na Yakobo 4:8 huongeza hivi: "Itakaseni mikono yenu, enyi wenye dhambi, na kuisafisha mioyo yenu, enyi wenye nia mbili. Akirejelea umati wenye mavazi meupe mbinguni, Ufunuo 7:14 huwaeleza si wale ambao Kristo alifua nguo zao bali ni wale ambao "wamefua mavazi yao, na kuyafanya meupe."

Waliziosha wapi? Hakika waliziosha katika damu ya Mwana-Kondoo. Hakuna chanzo kingine cha haki. Lakini walileta mavazi yao kwenye damu; Yesu hakuwaoshea watu hawa walipokuwa wamelala.

Ellen White, akiandika katika mwaka wa 1882, alisema kwa uwazi kwamba wengi “wanatamani kuvikwa haki kama vazi, lakini vazi jeupe la wale waliokombolewa, ni kwa wale walioosha mavazi yao, na kuyafanya yawe meupe katika damu ya Mwana-Kondoo. Yeye Amewasilisha jambo kama lilivyo: 'Jitahidini kuingia kwa mlango ulio mwembamba, kwa maana nawaambia ya kwamba wengi watataka kuingia, wasiweze"[15] Kila kitu kinategemea uhusiano wetu na Kristo, juu ya utii wetu wote kwa mapenzi na kazi ya Mwokozi. Wakati Kuhani wetu Mkuu anajishughulisha na upatanisho Wake wa mwisho, sisi, kama Waisraeli wa kale, lazima tuzitese nafsi zetu, ambazo zinapenda kujitosheleza kwa kiburi; kwa maana tusipofanya hivi, sisi, kama wao, tutakatiliwa mbali—si kwa sababu tumefanya dhambi (kwani kusudi hasa la upatanisho ni kusamehe dhambi), bali kwa sababu Yesu alijishughulisha na kazi hii ya kipekee sana ya neema, nasi hatukujali.

Asante Mungu, neema ya Kristo ni sabuni yenye nguvu ya ajabu. Ikiwa tutajisalimisha kwa neema hii, basi, tunaweza kufanywa kuwa na harufu nzuri ya milele na safi. “Yeye ni kama moto wa mtakasaji, na kama sabuni ya msafishaji,” Malaki 3:2 na kisha, akizungumza juu ya kazi ambayo Yesu anafanya sasa katika Patakatifu pa mbinguni, Malaki anaongeza katika mstari unaofuata, “Atawatakasa wana wa Lawi.” Katika Israeli ya kale makuhani walikuwa wana wa Lawi. Kwa kuwa waaminio wote katika Kristo sasa wanaitwa makuhani (1 Petro 2:9; Ufunuo 1:6), ahadi hii ya kutakasa “wana wa Lawi” pia ni ahadi ya kutakasa kila Mkristo anayekaa mkao wa kujipatia fursa hiyo. Basi, kutakaswa kwa Patakatifu kunahusisha kusafishwa kwa watu wanaotazamia Patakatifu.

Kufutwa kwa dhambi hakuhusiki tu na kutoa hesabu au uwajibikaji tu, bali pia mitazamo; sio tu na wingi wa dhambi zilizoungamwa bali pia na ubora wa maisha yaliyobadilika. Hapa ndipo Ukweli wa Sabato unapoingia. Sabato inadai utakatifu ule unaohitajika kwa ajili ya "kufutwa kwa dhambi" katika uzoefu wa mtu wa kila siku katika mtindo wa maisha yake. Ili kuitakasa Sabato, ni lazima wanadamu wenyewe wawe watakatifu.... Wakati amri ilipotolewa kwa Israeli, ‘Ikumbuke siku ya Sabato uitakase,’ Yehova aliwaambia pia, ‘Mtakuwa watakatifu Kwangu. Ili kuitakasa Sabato imewapasa watu wa Mungu kujitakaza nafsi zao kwanza"[16] (Kutoka 20:8; 22:31).

Sasa huu, "utakatifu sio kunyakuliwa: Bali ni kujisalimisha kikamilifu kabisa kwa Mungu kwa kudhamiria; ni kumtumaini Mungu katika majaribu ...; ni kutembea kwa imani ...;[17] Ili kuitakasa Sabato katika maana ya mwisho kabisa, ni pale mtu anapoishi siku nzima na huku mapenzi yake yapo katika kujitoa kikamilifu kwa

nguvu, uwezo na utakatifu wa Kristo—akiishi kwa Neno, akitembea kwa imani, akipumzika katika Upendo. Ni nani awezaye kufanya hivi siku nzima ya Sabato isipokuwa afanye hivyo kila siku juma zima? Hivyo utunzaji wa kweli wa Sabato na uzoefu wa "kufuta dhambi" ni kitu kimoja. Lakini Sabato haidai tu utakatifu, pia inaelekeza kwenye chanzo pekee kinachowezekana cha utakatifu. "Naliwapa Sabato Zangu, ziwe ishara kati ya Mimi na wao, wapate kujua ya kuwa Mimi, Bwana, Ndimi niwatakasaye" (Ezekieli 20:12)

Kristo anaposimama kando ya zile Amri Kumi katika Patakatifu pa Patakatifu sana, akizifuta dhambi mbinguni, kwa neema Yake anaangazia ulimwengu nuru ya thamani ili kuwasaidia wanaume na wanawake, wavulana na wasichana, kufikia kiwango cha kujiweka wakfu. Ushindi wenye ujuzi uliosheheni vyema ambao utawawezesha kusimama wakati wa taabu baada ya Yesu kuondoka Patakatifu pa mbinguni. “Kutoka Patakatifu pa Patakatifu,” aliandika Ellen White katika 1887, Hapa “kuna mwendelezo wa kazi kuu ya kufundisha.”[18] Kukubali, kuamini, kushirikiana na maagizo haya, haijalishi gharama ya malipo inaweza kuwa kiasi gani, ni sehemu ya kile kinachohusika katika kuleta maisha ya mtu kwa Kristo ili kuoshwa, na dhambi zake "kufutwa" katika uzoefu wa maisha halisi ya utendaji. "Lazima kuwe na utakaso wa roho hapa duniani, unaopatana na utakaso wa Kristo wa Patakatifu mbinguni."[19]

Maagizo kuhusu Patakatifu yanatufahamisha kile Yesu, Mwana-Kondoo wa Kalwari, anafanya sasa, na kwamba tunaishi katika wakati muhimu sana katika historia ya mwanadamu. Sabato na Patakatifu kwa pamoja hutukumbusha kwamba Yesu katika Patakatifu pa Patakatifu sana anavyoondoa dhambi katika kumbukumbu, pia anatafuta kwa namna ya pekee kuondoa dhambi katika maisha ya watu. Ujumbe wa kutia muhuri unaonyesha wakati wa kilele ambapo, kupitia uhusiano na Yesu usioweza kufutwa na ufahamu unaohusisha akili makini juu ya Sabato na Patakatifu, watu wa Mungu watakuwa wametulia katika Ukweli, kiakili na kiroho, ili wasiweze kuyumbishwa.

Fundisho la usingizi wa wafu linalinda dhidi ya dhana kwamba watu huenda mbinguni au motoni wanapokufa, imani ambayo haina maana kwa siku ya hukumu. Kwa nini Mungu awahukumu watu, wakati tayari amekwisha kuwapeleka mbinguni au motoni? Ndani ya jumuisho la muktadha, roho ya unabii inayodhihirishwa kupitia Ellen G. White inaonekana kama mfululizo wa jumbe zinazotumwa kutoka kwa Kuhani Mkuu, zikiwaongoza kwa upendo wafuasi Wake katika utakatifu halisi wa tabia ya Kristo ambao Yeye anatamani sana tuwe nao. Dhana hizi zote kwa pamoja zinajumuisha kazi kuu ya Kweli ya umoja, upatanisho, ambapo Yesu anatafuta kuunganisha watu Wake katika kifungo cha mwisho na cha milele cha umoja na Yeye Mwenyewe.

James White aliandika hivi mwaka wa 1868: “Waadventista Wasabato wanakita juu ya somo hili [la Kristo katika Patakatifu pa Patakatifu] kwa furaha kubwa…. Wanalishughulikia hili somo ... katika mahubiri na vitabu vyao, na kupata nafasi kwa hilo kati ya alama za unabii kwenye chati zao .... Ni kitovu kikuu ambacho Ukweli wote uliofunuliwa kuhusiana na makundi ya wokovu unajikusanya hapo pamoja, na huchangia zaidi katika kufafanua nafasi yao ya sasa, kuliko nyingine yoyote."[20] Ingawa Ukweli mkuu wa Yesu na hukumu ya upelelezi vilikuwa vya kwanza kuja wazi katika miaka ya 1850, vuguvugu lilikuwa likikua kwa kasi sana, na hitaji la uongozi mmoja ulio imara lilionekana, na ingawa wazo hili, liliogopwa sana na wengine, lilisisitizwa sana na wengine. Tunapinda kona sasa kwa kutoka kwenye safari ya mada za mambo ya imani, hadi kukua na kupangwa kwa Kanisa la Waadventista Wasabato kwa miaka mingi.

*Vidokezo:*

*1. For a comparison between the hymns James White selected and the possible antecedents of many of them, see Lyell Heise, "Hymns for God's Peculiar People: A Theological and Historical Study" (term paper, Andrews University, 1975). See also above, chapter 4, note 8*

*2. For a list of the "landmarks" see Ellen G. White, Counsels to Writers and Editors, p. 30;*

*3. See SDA Encyclopedia, art. "Investigative judgment." Certain historical details in this article are subject to correction*

*4. Ellen G. White, The Great Controversy, p. 481*

*5. Review and Herald, November 22, 1898, p, 745*

*6. Ellen G. White, The Great Controversy, p. 486*

*7. Ibid., p. 485*

*8. In Adventist terminology the "close of probation" as a last-day event refers to the time when Jesus leaves the most holy place and the cases of all have been settled irrevocably for life or death. See The Great Controversy, pp. 490, 491. The "time of Jacob's trouble" is the short but crucial period while the seven last plagues are being poured out, during which the saints, uncertain of their status with God, agonize for His blessing as Jacob wrestled with the Angel at Peniel. (See Genesis 32:24- 30; Jeremiah 30:5-7; The Great Controversy, p. 616) 9. Ellen G. White, The Great Controversy, p. 620*

*10. Ibid.*

*11. Ellen G. White, Spiritual Gifts, vol. 3, p. 135*

*12. Ellen G. White, The Great Controversy, p. 620*

*13. Ibid., p. 623*

*14. Ellen G. White, Manuscript 8, 1888, complete in A. V. Olson, ThroughCrisis to Victory (Washington, D.C: Review and Herald Publishing Association, 1966), pp. 260-269*

*15. Review and Herald, May 30, 1882, p. 338*

*16. Ellen G. White, The Desire of Ages, p. 283*

*17. Ellen G. White, The Acts of the Apostles (Mountain View, Calif.: Pacific Press Publishing Association, 1911,), p. 51*

*18. Idem, Letter 37, 1887*

*19. Ibid.*

*20. James White, Life Incidents, pp. 308, 309*

# SURA YA 17
# KATIKA UHITAJI WA "AGIZO LA INJILI/INJILI YENYE UTARATIBU"

"Lazima niseme, ndugu wapendwa, kwamba natumaini tutaamua ni jina gani tutakalokuwa nalo; Je, tunataka kuitwa nani. Mimi hukutana na marafiki mara nyingi sana ambao huniuliza jina la watu wetu ni nini na ni aibu kutokuwa na jina. Katika nafasi yoyote watoto wanapewa majina wanapokuwa na umri wa wiki chache au miezi michache tangu kuzaliwa. Tulipoanza kufanya kazi katika kusudi hili, kwa sababu kazi ilikuwa changa watu ambao walikuwa wameikubali bado walikuwa ni wachache, hivyo hatukuona umuhimu wa hatua hizo. Inaonekana kwangu kwamba mtoto sasa amekuwa sana kiasi kwamba haipendezi kutokuwa na jina lake."[1] Ndivyo alivyozungumza Mzee James White Jumapili asubuhi, Septemba 30, 1860, kwa mojawapo ya mikutano muhimu sana katika historia ya Waadventista Wasabato.

Miaka kumi na sita baada ya vuguvugu la Sabato-na Patakatifu kuzaliwa, ndipo hatimaye lilikuwa linaingia kwenye hatua ya kupiga kura ili kuchagua jina. Mkutano unaohusika ulikuwa umeanza kukutana usiku uliopita, mara baada ya kufungwa kwa Sabato, na mkutano uliendelea hadi shughuli yake ilipokamilika Jumatatu alasiri. Wajumbe walikutana katika kanisa la pili la Waadventista huko Battle Creek. Kanisa la kwanza, lilikuwa limejengwa miaka mitano tu kabla, na lilikuwa tayari limeonekana kuwa dogo sana. Jengo hili liliweza kutosha watu 300 na kwa sasa lionekana kuwa kubwa sana kwa kutaniko la mahali hapo. Lakini Waadventista hodari na wenye nguvu wa Battle Creek walikuwa wamepanga jengo hilo kuwa kitovu cha mikutano mikubwa ya Waadventista. Hata hivyo, hawakuwa na ndoto kwamba kanisa la tatu lingehitajika haraka sana, au kwamba la nne ambalo lingetosha mkusanyiko wa karibu watu 4000, pia ambalo pia lingehitajika hivi karibuni.

Waadventista wa Sabato wengi wa awali, walipinga kupanga taasisi ya madhehebu (hawakutaka organized church). Hili jambo halikuwa la kawaida siku hizo. Waprotestanti wa Marekani bado walijadiliana kwa ari ikiwa Roho Mtakatifu alifanya kazi vizuri zaidi kupitia makutaniko huru au kupitia madhehebu yaliyounganishwa na presbiteri, makongamano/makonferensi na mikusanyiko mikubwa. Wamethodisti na Wapresbiteri waliamini katika ushirikiano mpana wa madhehebu, lakini Wabaptisti na Wakongregational walibishana vikali kwa kufanana, juu ya uhuru wa kujisimamia katika utendaji na maamuzi wa kanisa mahalia *Kanisa mahalia liwe na uwezo wa kujitawala lenyewe katika mafundisho, uendeshaji wa ibada, mfumo wa uongozi na jinsi ya kutumia fedha au nyenzo (Autonomy of the local church).

Katika miaka ya 1850 James na Ellen White na wengine walisisitiza kutumia mfumo wa utaratibu wa dhehebu la aina ya presbiteri, lakini sio waumini wote hapo kwanza

waliokubaliana nao. Hasa, wale waliokuwa wamewahi kuwa Wamileri/Millerites, waliogopa kuanzishwa kwa madhehebu mapya. Walikuwa washiriki wa madhehebu ya Kiprotestanti ya wakati huo na, kwa kweli, walikuwa miongoni mwa washiriki wao waliojitolea sana. Lakini makanisa waliyoyapenda yalikuwa yamewageuka, yamedhihaki tumaini lao la kuja kwa Yesu mara ya pili, na kuwafukuza. Katika kuchanganyikiwa kwao, na wafuasi wa Miller walikuwa wametafuta maelezo katika Maandiko na wakayagundua katika Ufunuo 14:6-8.

Baada ya ujumbe wa malaika wa kwanza kuhusu saa ya hukumu imekuja, ambayo walikuwa wakitangaza wakati huo, waliuona ujumbe wa malaika wa pili, “Umeanguka, umeanguka; Ndipo walipounganisha hili na wito wa Kristo katika Ufunuo 18:1-4 , “Tokeni [kati yake [Babeli], watu Wangu,” na vifungu vingine mahali pengine katika Danieli na Ufunuo. Hitimisho lilionekana kuwa lisiloweza kuepukika. Makanisa ambayo yalikuwa yamewatendea kikatili sana yalikuwa yamekataa Ukweli muhimu na hivyo yakawa makanisa "yaliyoanguka,” kwa hakika "Babeli" kama kanisa kuu lililoanguka (au "kahaba") ambalo katika nyakati za Matengenezo na baadaye walikuwa wamejitenga.

Waliogopa kwa dhati kwamba ikiwa wangeanzisha taasisi nyingine ya kidini, wao pia baadaye wangeweza kukataa zile Kweli mpya za Biblia na kuwatesa watoto wakweli wa Mungu. Kwa sababu walikuwa wametoka hivi karibuni sana huko Babeli, inaeleweka kwamba hawakuwa na tamaa ya kujikuta mara moja katika Babeli mpya tena. Lakini ni nini kinachofanya kundi la Wakristo kuwa “Babeli”? Bila shaka ni Makosa katika Mafundisho ya imani (creed/dogma). Lakini je, kuna jambo jingine lolote lililokuwa sifa ya makanisa ambayo yaliwaondoa watu kwenye ushirika wao au kuwatenga?

Katika jarida kuu la wafuasi wa Miller, liitwalo The Midnight Cry, la Februari 15, 1844, George Storrs aliwaonya waumini ambao wakati huo walikuwa wakifukuzwa kutoka katika makanisa yao, “Jihadharini msitafute kuanzisha taasisi nyingine ya kanisa au dhehebu jingine. Hakuna kanisa lililopangwa kwa ubunifu wa mwanadamu lisilokuwa Babeli mara tu linapopangwa." Kwa hiyo kupanga (organization) kanisa kuliogopwa na wengi kwamba ndiyo alama mahususi ya Babeli. Wafuasi wa Miller walikuwa wametengwa kwa sababu imani zao za Kiadventista, zilichukuliwa kuwa kinyume na hitimisho na muhtasari wa mafundisho na kanuni za imani za madhehebu yao. Kwa hiyo Waadventista wengi walihisi kwamba ni lazima waepuke muhtasari huo wa mafundisho ya imani na kanuni la sivyo wangejikuta wako katika Babeli nyingine. Na siku moja, Roswell F. Cottrell, mwongofu hodari wa Wahuguenot ambaye hapo awali alikuwa Mbaptisti wa Siku ya Saba (na kama "muumini mwenye msimamo mkali sana), alichunguza tena Mwanzo 11 kwa kisa kuhusu kuanzishwa kwa jiji asilia la Babeli, alishangazwa na maneno ya wajenzi: “Nendeni, na tujijengee jiji

na mnara, ambao kilele chake kifike mbinguni; na tufanye tupate jina, tusije tukatawanyika juu ya uso wa dunia yote.

Mwishoni mwa Machi 22, 1860, Mzee Cottrell aliandika katika Review kwamba kwa maoni yake itakuwa ni makosa kujipa/kuchukua jina la dhehebu kwa vile desturi hiyo iko "kwenye msingi wa Babeli." Japokuwa hoja hizi kuhusu kupanga taasisi, kuwa na muhtasari wa mafundisho tunayosadiki, na kutoa jina zinakuwa ngeni masikioni mwetu, zina uhalali wake, kwani hakika zinatoa tamko la busara na kutupa tahadhari vichwani mwetu. Kahaba anayeitwa Babeli katika Ufunuo anawakilisha kanisa au kikundi cha makanisa. Na kanisa ni kundi la Kikristo la kimadhehebu lililopangwa rasmi, ambalo linashikilia seti fulani za mafundisho makuu ya imani, ama muhtasari wa mkusanyiko wa kanuni za imani. Zaidi ya hayo, ni wakati kanisa linashikilia Mafundisho fulani makuu ya imani ndipo linaelekea kuziita imani nyingine kuwa ni uzushi. Na ni kwa sababu kanisa limeunganishwa kupitia muundo wa shirika lililopangwa kwa utaratibu fulani, na hapo ndipo linakuwa nguvu ya kutesa watu.

Tunapotafakari juu ya huzuni na msongo ambao Wamiller walipata wakati walipofungiwa nje, na milango ya makanisa yao waliyoyapenda kufungwa wasiruhusiwe kuingia, tunaweza kuelewa vyema kusita-sita kwao. Upangaji wa shirika la kidini katika utaratibu fulani (organization), ikiwa na mkusanyiko wa kanuni au mafundisho ya imani na kuyaweka kwenye muhtasari, na kutoa majina kwa taasisi za madhehebu vinaweza kuwa na madhara.  Bila shaka pia ni kweli, kwamba kutokuwa na jina kwa taasisi au dhehebu kunaweza kuwa na madhara. Sio Waadventista wote wanaoshika Sabato walipinga utaratibu au kupangwa kwa kanisa (organization).

James White hakufanya hivyo. Mapema kama 1850 alionyesha tumaini [2] kwamba kanisa litakusanyika hivi karibuni na kusonga mbele katika mpangilio wa injili-kuweka utaratibu wa jinsi ya kuhubiri injili kwa pamoja kama ushirika. Alihubiri juu ya utaratibu wa injili katika Kongamano la Oswego mwaka wa 1851, na mwaka wa 1853 alichapisha mfululizo wa utaratibu wa injili katika Review. Alitumia neno "utaratibu wa injili au utaratibu katika kuifikisha injili" ili  kuwasilisha imani yake kwamba kanisa la kisasa lililopangwa kama taasisi (church organization) linapaswa kufuata mwongozo na mifano inayopatikana katika Agano Jipya.

Kijana J. N. Loughborough na mzee Joseph Bates waliunga mkono juhudi zake. Lakini watu wa kihafidhina (conservative) zaidi walipinga jambo hili. Na kwa hiyo, watu hawa waliishi na kufanya kazi katika ushirika wao bila jina,  taasisi, au mkusanyiko wa kanuni za mafundisho ya imani (creed), watunza-Sabato  hawa walijiita wenyewe kwa usahihi kabisa kama “kundi dogo,” “kondoo waliotawanyika,” “masalio,” “watakatifu,” au “rafiki” na kuendelea na injili.

Ijapokuwa walikuwa na hofu ya umoja wa kufanya utaratibu wa kupanga kanisa na kuunda taasisi na kufanya muhtasari wa mafundisho makuu ya imani waliyoamini, hawa Waadventista wa mapema walisadiki kabisa kutoka moyoni mwao kuwa walikuwa washiriki wa kanisa la kweli. Na walishikiliwa kwa nguvu pamoja, kana kwamba kwa gundi, katika umoja wa kweli kwa sababu mbalimbali.

Jambo moja la wazi lililowaweka pamoja, haswa katika miaka ya mapema ya 1845 hadi 1850, lilikuwa uzoefu wao uliofanana kwa wote. Karibu wote walikuwa Wafuasi wa Miller wa zamani ambao walipitia kukatishwa tamaa October 22, 1844. Mambo mengine yaliyowaunganisha ni pamoja na mikutano yao mingi waliyohudhuria pamoja, uongozi imara wa Joseph Bates na familia ya White katika ujana wao, maono ya Ellen, na, hasa, tabia ya mafundisho ya imani iliyoambatana na maono.

Kwa sababu "Ukweli wa sasa" ulikuwa umegusa mioyo ya wengi na ukawa muhimu sana, waliandika makala na vipeperushi ili kuchapisha na baadaye walivutwa kwa pamoja na kuwa karibu kwa ajili ya machapisho hayo. Kwa muda waliruhusiwa kutumia Gazeti la Day Star, lililoharirиwa na Enoch Jacobs wa Cincinnati. Wakati Jacobs alipokuwa mfuasi wa Shaker ambao walitoka kutoka dini ya Quaker/friends, walitumia gazeti la Crosier's Day-Dawn kwa muda mfupi. Lakini katika 1849 walianzisha jarida lao wenyewe, “Present Truth,” upesi gazeti hili nafasi yake ikachukuliwa na “Review and Herald.” Waumini walituma barua na makala kwa James White na walitiwa moyo waliposoma imani na uzoefu wa waumini wenzao, kupitia kurasa ambazo zilichapishwa katika jarida lao wenyewe.

Kulikuwa na gundi ya kutosha kuwaunganisha na kuwaweka pamoja wakati walikuwa mamia machache tu na hawakumiliki taasisi, lakini katika miaka ya 1850 walijipatia nyumba ya uchapishaji, na idadi yao iliongezeka kutoka karibu 200 hadi 3000 kwa wastani wa karibu asilimia 30 kwa mwaka, takriban mara sita ya ongezeko la wastani kiasilimia katika miaka ya 1970. Hakika, idadi inaonekana kuongezeka kwa kasi hadi kufikia 2000 ndani ya miaka miwili ya kwanza ya muongo huo,[3] kwa kiwango cha kushangaza, kwa zaidi ya asilimia 200 kwa mwaka ambacho kinaeleweka kwamba kilisimama na kwa bahati mbaya kilipungua sababu ya baadhi kurudi nyuma na kutawanyika.

Kwa ukuaji huu wa idadi kulikuja upanuzi wa kijiografia huko Michigan na Illinois na Wisconsin na Canada Mashariki na Canada Magharibi - na California ambapo idadi ya waumini ilikuwa inaruka na kusonga mbele. Bila shaka, hali hizi zilitengenezwa na kuhitaji vipengele vya ziada, nyeti na vya kisasa zaidi vya ushirika. Pia, watu wengine walijiunga na vuguvugu hilo ambao hawakuwa Wafuasi wa Miller na hawakuwa wamefukuzwa kutoka kwa makanisa yao na kwa hiyo hawakuogopa sana kuwepo kwa muundo wa kimadhehebu. Mnamo Novemba 1851 ripoti ilitumwa kwa Review kutoka kwenye kundi changa sana la Waadventista Washika Sabato,

Washington, New Hampshire, ikisema kwamba "kamati ya watu saba ilichaguliwa (Angalia mashemashi wa Matendo 6) kushughulikia mahitaji ya maskini."[4]

Waumini wa Washington hawakuruhusu hofu yao ya kupanga dhehebu au taasisi kuingilia kati wajibu wao wa Kikristo kwa watu wasiojiweza. Vivyo hivyo, walijiepusha kuwaita wanaume saba "mashemasi." Baada ya yote, Matendo 6 haikutumia neno "shemasi" pia! Hata hivyo, ripoti zilianza kuonekana punde baadaye kuhusu kuwekwa wakfu kwa wanaume hao waziwazi kama mashemasi, kama vile kule Fairhaven, mji alikozaliwa Joseph Bates. Muhimu zaidi kuliko kuwekwa wakfu kwa mashemasi ni kuwekwa wakfu kwa wachungaji kwa kuwekewa mikono na kupewa leseni kwa wahudumu. Kadiri ongezeko kubwa la washiriki lilivyokuja, ndivyo ongezeko linalolingana la ndugu wanaohubiri au ndugu walimu wanaofundisha Biblia, au ndugu wanaosafiri, au wajumbe, au wamishenari, au jinsi yoyote ile au vyovyote vile walivyoteuliwa kwa njia anuwai.

Zaidi ya arobaini na tano wametajwa kwa majina kwa uwiano wa washiriki 200 kwa mhudumu mmoja, katika  Magazeti ya Review ya 1852 na 1853. Kwa kuwa hakukuwa na chombo rasmi cha "kuwaita pamoja", wote walikuwa ni watu waliojitolea, wengi wao kama Hiram Edson ambaye alikuwa akihubiri katika majira ya hali ya hewa ya baridi ili wakati wa majira ya joto, aweze kujikimu kimaisha. Juhudi zao nyingi za kiroho hazikutumiwa kwa waumini wao waaminifu, bali waliwafikia washika Jumapili, ambao washika Sabato walipenda wawapelekee ujumbe wa malaika wa tatu. Walisafiri kwenda na kurudi kutoka Maine hadi Wisconsin, wakijibu maombi na maswali yaliyochapishwa katika Machapisho ya Review kutoka kwa watu wa kawaida, walei wenye bidii, au wapweke na katika maeneo yaliyojitenga.

Mwishoni mwa juma au wiki moja au mbili, ikiwezekana walifanya ubatizo wa watu watatu au wanne mtoni au ziwani, na wakiwa njiani wakaenda, kwenye miadi nyingine. Baadhi ya wanaume hawa walikuwa wamewekewa mkono kwa huduma (wamepewa leseni za uchungaji) na makanisa ambayo walikuwa wameshiriki hapo awali—Frederick Wheeler, kwa mfano, na Joseph Baker, na M. E. Cornell, na John Byington, na James White. Wengine, na pengine wengi wao, walikuwa watu wa kawaida waliojitolea –J. P Kellogg, Otis Nichols, H. S Gurney, Stockbridge Howland, na wengine wengi. Ni wachache, hata waliowekwa wakfu kwa huduma, waliopata mafunzo rasmi na sio wote waliodumu kwa muda mrefu katika juhudi zao za injili. Genial E.L.H Chamberlain alithibitisha kuwa ndiye mchanganyaji/mvurugaji mambo kwa ubora zaidi kuliko kundi la messenger, na baada ya kukifanyia majaribio kipaji chake kwa msimu mmoja alichukua pendekezo la Ellen White na kurudia kazi yake ya zamani.

Ilieleweka kwa ujumla kwamba hakuna mtu ambaye angeweza "kuendesha huduma za nyumba ya Bwana na kushughulika na taratibu zote," yaani, kuongoza katika Meza

ya Bwana na ubatizo kwa kuzamishwa,[5] bila kuwekwa wakfu kwanza. Hii bila shaka, ilikuwa ni kikwazo kikubwa kwa kazi iliyoendelea kukua kwa kasi kati ya majirani na marafiki. Kuwekwa wakfu kwa mchungaji kwa mara ya kwanza na Waadventista Wasabato, katika tukio lisilo rasmi kwa viwango vyao vya baadaye, kulitukia Vermont, mji wa Betheli ya Mashariki, katika majira ya joto ya 1851. Dada F. M Shimper baadaye aliripoti kwenye Review[6] ambapo Ndugu Washington Morse alikuwa “amewekwa wakfu” kwa kuwekewa mikono, kuwa msimamizi wa huduma na kaida kwenye nyumba ya Mungu.”

Yaonekana kuwekwa wakfu huku kulifanywa na George Holt, ambaye alikuwa ameteuliwa kuwa mtumishi katika dhehebu lake la awali. Kuwekwa rasmi zaidi[7] kulifanyika Jumatatu, Septemba 5, miaka miwili baadaye, katika kile kilichojulikana kama "Konferensi ya Potsdam" kwa sababu watu walikutana katika Daraja la Bucks huko katika Wilaya ya Potsdam ya kata ya Saint Lawrence, New York. John Byington alitengeneza mahali penye kivuli mbele ya nyumba yake ili itoshe kuketisha watu 300 kwa ajili ya mkutano wa "Siku ya Kwanza,” (Jumapili) mkutano ambao umma ungealikwa.

Mchungaji Byington na mkewe Bibi Byington walihisi kuzawadiwa kwa kazi yao hii wakati waumini themanini walipohudhuria siku ya Sabato, pamoja nao walikuwepo dada wawili waliosafiri maili sitini na tano kwa gari lao binafsi la farasi na baadaye kutoa ushuhuda na shukrani kuwa wamelishwa vyema kiroho katika sikukuu hii. James na Ellen White walikuja kutoka Rochester; lakini, kwa sababu Mzee White alikuwa mgonjwa kwa kiasi fulani, alimwacha kijana mahiri John Andrews afanye sehemu kubwa ya mahubiri. Jumapili usiku walifanya ibada maili mbili kwenye kilima juu ya Mto Grass kwenye Kanisa la Morley Wesleyan, ambapo Wafuasi wema wa Wesley walikusanyika ili kusikia mahubiri mazuri bila kuwa na kinyongo chochote dhidi ya John Byington kwa kuwaacha mwaka mmoja kabla, na kujiunga na Waadventista.

Lakini kilele kilikuja Jumatatu asubuhi, nyumbani kwa Byington. "Matamko yalitolewa kuhusiana na umuhimu wa kuweka utaratibu wa kanisa," labda na James White, ambaye lazima alikuwa anapata nafuu ya ugonjwa kwa sasa. "Ushuhuda wa wazi" ulitolewa na Ellen White na Machozi ya toba na ushirika yalimwagika. Na suala hilo lilizingatiwa na kumwekea mikono ya huduma mtumishi wa kujitolea mwenye umri miaka takribani ishirini, Horace W. Lawrence wa West Bangor, New York. Ndugu Lawrence alikuwa amebatizwa mwaka wa 1842 katika "Kanisa la Kikristo," kisha alijiunga na Wafuasi wa Miller mwaka 1843, alipitia hali ya kukatishwa tamaa ya Oktoba 22, 1844, na akapewa kibali cha kuwa mshauri na Waadventista wa Jumapili, alibatizwa tena katika ujumbe wa Sabato na Joseph Bates, na kuthibithishwa kuwa mlei mwenye ufanisi sana katika kazi ya injili, hata akasaidia

kumwongoa John Byington na mke wake kuanza kuishika Sabato ambayo ni Amri ya nne ya Mungu, ambalo lilikuwa ni tunu kubwa.

Zaidi ya hayo, majuma machache yaliyotangulia, akiwa amechukuliwa na ari kubwa na hisia za hitaji, alikuwa ameendesha huduma ya ubatizo na Meza ya Bwana kwa baadhi ya waumini walio maeneo ya mbali, yaliyojitenga bila kuwekewa mkono wa uchungaji. Wale waliomfahamu vyema walifikiri ulikuwa wakati wa “kumwekea mikono ya uchungaji.” Waamini wengine walikubali pia. Na kwa hivyo, Mzee White aliandika baadaye, ‘ilionekana vyema kwa Roho Mtakatifu na kwetu sisi,’ kumtenga Ndugu yetu mpendwa Lawrence kwa kazi ya huduma ya injili, ili aendelee kusimamia ibada za kanisa la Kristo, akiwa amewekewa mikono," White aliongeza, "Ni kwa kupatana kwa moyo mmoja, jambo hili limefanyika."

Hakuna aliyewazia kichwani mwake kwamba, ndugu hawa wakuu walipopiga magoti kwa ajili ya maombi ya kuwekwa wakfu kwa John Byington na H.G Buck, wachungaji waliokuwa wameongoka muda mfupi kabla ya hapo kutoka kwa wafuasi wa Wesley, James White, aliyetawazwa katika Christian Connection, na John Andrews kwamba hawa watatu kati yao wangeweza kuwa wenyeviti watatu wa kwanza wa halmashauri Kuu ya Waadventista Wasabato ijulikanayo na wengi kama General Conference of Seventh-Day Adventist Church. Wakati huo hapakuwa na General Konferensi (Halmashauri Kuu). Hakukuwa hata na Kanisa la Waadventista Wasabato, tukisema kama ilivyokuwa.

Mbali na kilio cha kuongeza nguvu-kazi katika harakati zinazokua, hali nyingine mbaya ambayo pia ilihitaji angalau mwonekano wa muundo shirika au utaratibu wa kanisa, lilikuwa hitaji la mara kwa mara la kukabiliana na watu wakorofi na wale waliorudi nyuma. Kwa kawaida James White au kiongozi mwingine anayetambulika alishughulikia matatizo haya alipokuwa akifanya ziara zake za mara kwa mara kwenye makutaniko ambamo watu waliosumbua waliishi. Shida zilizunguzwa kwa hekima, maombi na uwazi na kura ya wazi ikapigwa. Muda mfupi baadaye, Review nayo ingeweza kubeba masimulizi kwamba “ndugu” wa mahali fulani na kama vile ilivyokuwa “walihisi kutakiwa kuondoa ushirika kutoka kwa mtu ambaye alikuwa ameanguka kwa jambo fulani, na kufundisha makosa ya hatari au kutisha,” au mahali pengine wangesema “baada ya hali ya huzuni na mambo yalikuwepo, na kuleta matokeo ya ushawishi mbaya wa mmoja ambaye (alidai kuwa mwalimu) ambaye ilitubidi tumwondolee ushirika.”[8]

Muda mfupi baada ya ripoti kama hizo kuonekana, ungamo kama hili lingeweza kuchapishwa kutoka kwa mtu ambaye mwenendo wake wa dhambi ulikuwa umeshughulikiwa: "Sasa naweza kusema kwa uwazi, kwamba ... [nilichofanya] ni makosa. Pia, mimi sasa tazama, kwamba ilikuwa ni fursa yangu, na pia wajibu, kujisalimisha kwenye sauti ya kanisa”; au hivi: “Ningesema kwamba ninahisi moyo

wa shukrani sana kwa roho ya upendo ambayo imedhihirishwa kwangu mimi nisiyestahili, baada ya kumhuzunisha Roho wa Mungu, na kuleta lawama na jeraha juu ya mateso Yake.… nikakiri kwamba nina hatia ya makosa haya ... nasikitika kwa majaribu ambayo nimeleta juu ya watu wake."

Na kwa maungamo kama haya, matangazo kama yafuatayo yanaweza kutolewa kama mwitikio kutoka kwa wazee wa kanisa: “Kwa hiyo tunatumaini kwamba Ndugu na Dada … watarejeshwa kwenye imani ya ndugu zao kana kwamba kesi iliyotajwa haikuwepo kamwe. "[9] Ili kusaidia kuweka usafi kwenye harakati, katika matukio mengine Bwana aliingilia kati moja kwa moja. Tunarudi mwanzoni mwa majira ya kupukutisha majani ya 1852. Mnamo Septemba nyumba ya uchapishaji ya Review ilihamia kwenye nyumba kubwa ya Mount Hope Avenue huko Rochester. John Loughborough, ambaye alikuwa mhubiri kijana, mdogo kwa umri-mvulana wa Waadventista washika Jumapili na sasa alikuwa na umri wa miaka ishirini, alikuja kwenye chumba cha ibada katika makao hayo kumsikiliza John Andrews (mwenye umri wa miaka ishirini na tatu) akihubiri juu ya suala la Sabato na akasadikishwa.

Familia ya White walirudi kutoka safari ya Maine mnamo Ijumaa ya kwanza, Oktoba. ya Siku iliyofuata. Wakati wa ibada Loughborough alichangamsha kila moyo kwa msimamo wake wa hadharani ili kuitakasa Sabato. Oswald Stowell, ambaye alikuwa amekubali Sabato huko Paris, Maine, baada ya kusoma nakala ile ile ya chapisho la T.M. Preble lililomsadikisha John Andrews, alikuwa mgonjwa wa pleura-kubanwa kifua na kukohoa na hivyo alikuwa akisikiliza kutoka chumba kilichokuwa karibu. Madaktari walikuwa wamemkatia tamaa Oswald kwamba angekufa, lakini aliwaomba waumini wasali. Walipopiga magoti pembeni ya kitanda chake na kuomba, Mzee White alimpaka mafuta. Kufikia wakati wanainuka kutoka kwenye magoti yao, Oswald alikuwa ameketi kitandani, akipigapiga ngumi kwenye ubavu wake, ambazo zilikuwa na maumivu makali, na kusema, "Nimepona kabisa! Ninaweza kufanya kazi katika kiwanda cha uchapaji kesho!"

Ellen White alibaki amepiga magoti. Mumewe alimchunguza kwa muda na akasema "Ellen yuko kwenye maono. Hapumui akiwa katika hali hii. Ikiwa yeyote kati yenu anataka kujiridhisha na jambo hili la maono, basi, yuko huru kumchunguza." Alikuwa amepiga magoti huku macho yake yakiwa wazi, akitazama kwa akili vitu alivyoweza kuona tu. Kwa muda wa saa moja na dakika ishirini, muda wote maono hayo yalidumu, hakuna mtu aliyeweza kugundua ushahidi wowote wa kupumua, ingawa mara kwa mara alizungumza maneno au sentensi kama mwitikio wa kile alichokiona. Uso wake ulikuwa wa rangi ya asili, na ishara alizofanya kwa mikono yake zilikuwa za kupendeza.

Maono hayo yalipoisha, alimtafuta Loughborough, ambaye alikuwa amekutana naye kwa muda mfupi kwa mara ya kwanza usiku uliopita, na kumwambia mambo

yaliyomhusu yeye mwenyewe ambayo alifikiri kwamba hakuna mtu anaeyajua. Kisha akazungumza juu ya mtu ambaye hajawahi kukutana naye. Alisema alikuwa akisafiri mbali na nyumbani, akishuhudia mengi kuhusu amri ya nne lakini akivunja ya saba. Ilionekana kwamba mmoja wa waongofu wapya wa Andrews alikuwa Michigan wakati huo. Siku zote alionekana alikuwa mume mwaminifu na hakuna mtu aliyedhani maono hayo yalirejelea kwake.

Lakini majuma sita baadaye, ndugu huyu aliporudi nyumbani, Ellen White alimtambua mara moja tu, akakusanya watu kadhaa kama mashahidi, akamwambia kwa dhati kile ambacho Mungu alikuwa amemwambia, na akamalizia kwa maneno ya Nathani kwa Daudi: “Wewe ndiwe mwanaume huyo." Bila kuchelewa yule mwongofu mpya mwenye dhambi alipiga magoti mbele ya mke wake, akakiri kwa machozi kwamba yote yalikuwa ni ukweli wa kupindukia, akasema ilikuwa ni mara ya kwanza kutokea, na akaahidi kwa unyoofu kwamba itakuwa mara ya mwisho.[10]

Lakini ikiwa baadhi ya matatizo yanayokabili "kundi lililotawanyika" yangeweza kutatuliwa kwa machapisho ya kila juma, kuwekwa wakfu mara kwa mara, kutengwa na ushirika kwa maombi, na mafunuo ya wakati unaofaa, wengine wengi hawangeweza hilo. Na hivyo, kama James White alivyoona mwanzoni mwa sura hii, mapema tu au baadaye Waadventista wangesukumwa kuamua na kujipanga kama kanisa na hatimaye kulipa kanisa hilo jina—“mtoto huyu mpya lazima awe na jina”.

*Vidokezo:*

*1. Review and Herald, October 16,1860, p. 170*

*2. Letter to Brother Hastings, March 18, 1850*

*3. Review and Herald, May 6, 1852, p. 5*

*4. Review and Herald, November 25, 1851, p. 52*

*5. See Bates, The Seventh Day Sabbath, A Perpetual Sign, p. 22*

*6. Review and Herald, August 19, 1851, p. 15*

*7. Review and September 20, 1853, pp. 84, 85; conversation with John O. Waller, Andrews University, August 1975; see also Waller, "John Byington of Bucks Bridge: The PreAdventist Years," Adventist Heritage, July, 1974*

*8. Review and Herald, November 25, 1851, p. 52*

*9. Review and Herald, December 13, 1853, p. 183 10. Loughborough, Rise and Progress, pp. 169-173*

## SURA YA 18
## KUMPA MTOTO JINA

Baada ya saa kadhaa za kuzisugua nguo uchafu kwenye beseni la maji moto, bibi fulani wa Kiadventista katika kijiji cha Jackson, Michigan, alikuwa akianua nguo zake kutoka kwenye kamba siku hiyo ambapo jirani wa karibu, ambaye mara kwa mara alikuwa akitoa maneno ya hasira na kubeza dhidi ya watunza Sabato, alichukua ndoo ya maji na kumwaga maji yenye matope kupitia dirisha lake kwenye nguo safi na nzuri za bibi huyu mwadventista. "Wewe ... wewe mchawi!" Alitoa kilio yule mwanamke wa Kiadventista huku akibubujikwa na machozi, na huku akizitoa nguo kwa hasira kwenye kamba, kwa ajili ya kuzifua kwa mara ya pili.

Bila shaka neno lilienea; au tuseme, neno tofauti lilisambaa. Katika siku hizo sahili, wakati jina zuri la kanisa lilikuwa jambo la kipaumbele kwa kila mshiriki, mkutano wa kusikiliza kesi yake uliitishwa nyumbani kwa mhunzi Dan Palmer, kiongozi wa eneo aliyechukua nafasi ya wachungaji wa kanisa la Waadventista. H. S. Case na C. P. Russell, wawili kati ya wahudumu wengi waliojiteua, walimkemea mwanamke huyo vikali na kumshutumu kwa kutumia neno fulani. Lakini yeye alisisitiza sana kwamba hajalitumia neno hili, alisisitiza sana. Akili zilizotulia zilipendekeza upesi maombi.

Na wakati kundi likiwa limepiga magoti, Ellen White, ambaye alikuwa akipita pamoja na mume wake wakielekea magharibi, alipata maono. Kwa mwaliko wa Mzee White, Russell na Case walimchunguza kwa makini hadi waliposhawishika kwamba uzoefu wake wa maono, ulikuwa wa kweli. Maono hayo yalipofungwa, Bibi White alitangaza kwamba Mungu alikuwa amefichua ukweli kuhusu mwanamke anayehusika na kwamba alikuwa amefanya jambo baya. Hata hivyo, baada ya kufunua mengi hayo, Ellen alijikuta hawezi kukumbuka tena. Case na Russell walifurahi. Kwa msisitizo walijitangaza kuwa na imani thabiti katika vipawa vya

mbingu/Kiungu vya Dada White kama nabii, na wakadai kwamba mwanamke huyo aliyepatwa na hii bahati mbaya akiri!

Siku ya Ijumaa usiku, wakati wa ibada ya familia katika nyumba nyingine ya Waadventista, maono yale-yale yalirudiwa. Asubuhi ya Sabato, wakati wa mahubiri katika nyumba ya Dan Palmer, Bibi White alirudi tena kwenye hali hiyo. Mwanamke huyo alifanya makosa, alirudia—lakini Bwana pia alikuwa amefunua, Ellen aliendelea, kwamba hakuwa ametumia neno maalum ambalo Case na Russell walikuwa wamemshtaki kuwa alilitumia. Mungu alikuwa ameonyesha, zaidi ya hayo, kwamba Alichukizwa sana na ukosefu wa fadhili ulioonyeshwa na wahudumu hao wawili na badala yake akatamani wawe na huruma. Mwitikio huu ulikuwa wa kushangaza. Mwanamke huyo moyo wake uliyeyuka na huku akitokwa na machozi, aliungama alichokifanya na kuomba msamaha.

Lakini Russell na Case, kwa upande mwingine, walilalamika kwa hasira juu ya ukosoaji usio na msingi wa Bibi White kwao. Ilikuwa kwa namna hii mnamo Juni 1853 ambapo "watu wanaoenda kando ya imani au offshoot" wengi wao wale walio wa kwanza kufanya hivyo, hutoka kwa Waadventista Washika Sabato walizaliwa.[1] Watu hao wawili punde walizindua chapisho jipya la kuwashambulia familia ya White na viongozi wengine, na kutokana na jina lake, Messenger of Truth, wao na wafuasi wao wakaja kuitwa "The Messenger Party" Au “Chama cha Wajumbe.”

Wakati huo huo James White alikuwa mgonjwa sana kutokana na kufanya kazi kupita kiasi. Ilionekana kuwa na uwezekano mkubwa kwamba angekufa, hivyo wakati nyumba yake ndogo ya kwanza ilipojengwa huko Battle Creek, aliamuru hati hiyo iandikwe kwa jina la mke wake.[2] Mwanachama wa chama cha Wajumbe-Messengers Party walishangilia ugonjwa na unyonge wake, wakiutaja kama ushahidi tosha kwamba Mwenyezi Mungu ataruhusu mzee White, atoke njiani mwao, yaani alale mauti. Aliposikiliza maelezo yasiyo ya hisani/fadhila ya mwanachama huyu wa chama cha Wajumbe (Messengers Party), imani yake ilihuishwa, na kama Wycliffe wa kale aliketi kitandani na kusema, “Sitakufa, bali nitaishi, nami nitazitangaza kazi za Bwana, na bado ninaweza kuhubiri katika maziko yao."[3]

Kwa muda wa miaka miwili watumishi waaminifu waliona kuwa ni wajibu wao kuwatetea familia ya White na Ukweli kutokana na mashambulizi ya watu hawa. Lakini baada ya maono ya jioni ya Sabato huko Oswego, New York, Juni 1855, Ellen White aliwaagiza wasijibu mashtaka tena, bali watoe muda na nguvu zao kutangaza "Ukweli, Ukweli wa sasa."[4] Kwa Jina la Bwana, aliahidi kwamba kama wangefanya hivi, viongozi wa uasi, wanaopinga kanisa wajulikanao kama offshoots, wangeingia vitani wenyewe kwa wenyewe hivi karibuni; Magazeti yao yangeacha kuchapwa, na harakati zao zingetoweka. Pia aliahidi kwamba wakati huo utakapofika,

Waadventista (ikiwa wangefuata shauri la Mungu) wangekuta kwamba safu zao, au jeshi lao lingeongezeka maradufu.[5]

Kwa muda lazima ilionekana kwa wengi kuwa maneno yake hayangeweza kutimizwa, kwani mwishoni mwa mwaka huo huo kundi la pili lilijitenga chini ya uongozi wa J. M. Stephenson na D. P Hall. Mzigo wao ulikuwa kwamba fursa ya mwanadamu kujipatia wokovu itaendelea wakati wa "zama zijazo" (yaani, wakati wa milenia), imani ambayo iliwaletea jina, "The Age-to-Come Party"—"Chama cha Zama Zijazo." Stephenson na Hall walikuwa wameukubali Ukweli wa Sabato wakati J. H Wagoner alipotembea maili hamsini  ili kuwafundisha.

Hapo awali walikuwa wamemhukumu Russell na Case kwa "ufafanuzi ... wa ajabu" wa mafundisho katika "Messenger of Error" iliyomaanisha "Mjumbe wa Kosa."[6] Lakini baada ya muda Stephenson na Hall waligundua kwamba walikubaliana na Russell na Case katika kukataa uongozi wa James White na maono ya Ellen White, na hivyo wakajiunga nao. Chama cha Messenger kilionekana kukua zaidi. Lakini ndugu katika Bwana walitii  shauri la Ellen White.

‘Messenger Party’ (na chama saidizi cha Age-to-Come) vilisambaratika wakati ulipotimia, na mnamo Januari 14, 1858, White aliripoti katika Review kwamba kuandikishwa kwa watu ili kuchukua magazeti kila mwezi, namba yake ilikuwa imeongezeka katika miaka mitatu kutoka elfu moja hadi elfu mbili. Mwisho wa mhariri wa Messenger Party ulikuwa wa kusikitisha. Alijikuta amekosa kazi kwa sababu alikuwa hana wasomaji, hivyo alienda shule ya ualimu ili kujikimu kimaisha. "Lakini bila kujifunza kwanza kujitawala mwenyewe, alishindwa kabisa kuwatawala wanafunzi wake." Akiwa na hasira na mwanafunzi mkorofi, akavuta bunduki yake. Ili kuepuka kuuawa alikimbilia sehemu zisizojulikana.[7]

Kundi la wapinga imani wengine lilianzishwa, mwaka wa 1858, ambalo, kutokana na utendaji wake, linaweza kuitwa "The Smoke and Chew Party" yaani "Chama cha uvutaji sigara na utumiaji wa ugoro." Utumiaji wa tumbaku, ingawa haukuwa kigezo cha ushirika, ulionekana kama kitu kisicho na maana miongoni mwa washika Sabato wengi. Waumini wachache, hata hivyo, karibu na Otsego, Michigan, walipata mhudumu waliyempenda, Gilbert Cranmer, ambaye aliwahimiza kushika Sabato na tumbaku yao. Kwa pamoja, walichapisha gazeti la Hope of Israel na wakakanusha vikali uvuvio wa Ellen White. Hawa nao, pia, punde walitoweka kwenye eneo hilo.[8]

Ili kuepuka kurudia kwenye wapinga imani ya Kiadventista kwa muda, inaweza kuongezwa hapa kwamba mnamo 1865 mabaki ya vikundi hivi vitatu walipata nguvu tena kidogo wakati Wazee B. F. Snook na W. H. Brinkerhoff walipigiwa kura ya kuondolewa katika uongozi wa Mkutano wa Iowa. Snook na Brinkerhoff walitaka aina huru ya kusanyiko, lenye muundo wa madhehebu na waliwapinga Mzee na Bibi White

kwa nguvu. Kwa sababu walifanya makao yao makuu huko Marion, Iowa, wao na kikundi chao walikuja kujulikana kama "The Marion Party." Hivi karibuni Brinkerhoff ilianza tena upendeleo wake kwa sheria, na Snook akageuka kuwa mshiriki wa dhehebu la Universalist. Harakati zao bado zipo na zinajulikana kama “The Church of God, Seventh Day (Denver, Colorado) ikimaanisha “Kanisa la Mungu, Siku ya Saba” (Denver, Colorado).[9]

Loughborough mahali fulani alikutana na hadithi inayoleta udadisi lakini inayowezekana kutokea, kwamba watu hawa wanne walio na mafundisho ya imani ambayo yanatoka nje ya mpango ‘offshoots’ walichapisha machapisho yao kwenye mashine ndogo ya mkono. Kulingana na hadithi ya mapokeo, kila kikundi kilichofuata kiliinunua mashine kutoka kwa mtangulizi wake.[10]

Baraza kuu la Waadventista halikuweka vikwazo vya kisheria au kiuchumi kwa wale waliotaka kuondoka. Hakika  hawangeweza kufanya hivyo hata kama wangetaka. Lakini kulikuwa na athari za kiutawala ambazo zilikuwa ngumu kupuuzwa. Viongozi walioasi wa matawi haya mbalimbali walikuwa wamejulikana sana kupitia gazeti la Review wakati wa siku zao za uaminifu, na walijieleza katika jumuiya za mbali kama bado wao ni wafuasi wa vuguvugu la Waadventista. Ni nani alikuwepo kuthibitisha kwamba hawakuwa waaminifu?

Zaidi ya hayo, mwaka wa 1854 wakati umati mkubwa wa wainjilisti ulipofurika katika jengo la shule ili kumsikia John Loughborough akihubiri, swali lilizuka, "Kwa nini usitumie hema?" Walei wa eneo hilo mara moja walitoa pesa hizo, na Merritt Cornell akashuka kwenye gari-moshi na kurudi na hema moja baada ya siku chache. Punde waumini katika majimbo kadhaa walikusanya rasilimali zao ili kununua "hema za hadhi nzuri" ili zitumiwe na wahubiri wasafiri  katika maeneo yao, na mahudhurio na ubatizo wa watu viliongezeka kwa kutia moyo.

Huko Wisconsin wahudumu wa Age-to-Come na Messenger waliokuwa nje ya imani ya Waadventista Wasabato walichukua hema kwa matumizi yao wenyewe. Na ni nani aliyekuwepo kusema kwamba hawawezi? Kulikuwa na matatizo mengine pia ambayo yalihitaji kuwepo kwa mfumo wa uongozi. Njia pekee ya mawasiliano ya mara kwa mara kati ya ndugu waumini ilikuwa ni gazeti la Review. Ikiwa mhudumu alihisi kuvutiwa kusafiri hadi eneo fulani, alitangaza nia yake katika gazeti la kanisa. Matoleo yaliyofuata yalipotoka, angeazima nakala kutoka kwa muumini yeyote ambaye alikuwa akikutana naye wakati huo na kutafuta majibu yaliyochapishwa kutoka kwa watu waliokuwa wakiishi katika eneo alikokuwa akielekea. Barua hizi, ikiwa zipo, zilimwambia mahali ambapo huduma zake zilihitajika zaidi na mahali ambapo kuna uwezekano mkubwa wa mambo kufanikiwa.

Kwa upande mwingine, ikiwa waumini katika eneo fulani walitaka msaada wa mhudumu fulani, walijulisha watu habari hizo kupitia gazeti la Review. Notisi ifuatayo, kwa mfano, ilionekana katika toleo la Januari 21, 1858: "Je kaka na dada White, au Kaka Loughborough na Waggoner, au mtu mwingine aweza kuweka miadi ya mkutano huko Gilboa [Ohio], na kutoa taarifa yake katika Review? Tumekuwa tukitarajia ujio wa hawa wainjilisti kwa karibu majuma sita sasa. Je hamna matumbo ya huruma kweli, ya kufanya mje kutuona?

Haishangazi wahudumu hawa walijulikana kama "ndugu wanaosafiri." Kwenye boti za mito na magari ya reli, kwenye barabara za (magogo) na vinjia vya barafu, wengi wao walipanda, na mara nyingi kwa miguu yao, wakikanyaga huku na huko, juu na chini, kutoka Maine hadi Minnesota wakiamini walikuwa wakiongozwa na Roho Mtakatifu. Mara nyingi bila shaka waliongozwa hivyo. Lakini "Mungu si mwanzilishi wa machafuko." 1 Wakorintho 14:33.

Wakiwa na shauku ya kumaliza kazi hiyo, wanaume hawa walikubali mwito mmoja wa dharura baada ya mwingine wa kuharakisha kutoka jimbo hadi jimbo bila kungoja kwanza na kuhakikisha kama waongofu wao wapya walikuwa na msingi wa kutosha, au kama kuna mhudumu mwingine, anayefanya kazi karibu tayari, ambaye angeweza kushughulikia hitaji hilo kwa ufanisi zaidi. Kisha, pia, pamoja na wanaume walioitwa na Mungu kweli kama tulivyoona, kulikuwa na wahudumu wengine waliojiteua wenyewe, ambao kazi zao hazikuwa na matunda au zilikuwa mbaya zaidi. Kisha kulikuwa na wanaume wasiopevuka na wasio na uzoefu ambao walihitaji ushauri wa pekee ili kuwasaidia wakomae.

Ofisi ilihitajika kwa ajili ya kushughulikia changamoto hizi zote ambapo maamuzi yangeweza kufanywa kwa ajili ya ajira yenye ufanisi zaidi ya wafanyakazi; au, kutumia usemi mzuri wa Waadventista, kuweka "mgawanyo wa kazi" unaofaa zaidi. Tatizo jingine kubwa lilikuwa lile la kuwapa watumishi mshahara. Kimsingi katika uchumi wa kilimo waumini wengi walikuwa na pesa kidogo tu mfukoni. Baadhi ya waumini wasio na ubinafsi walitoa sadaka viwango visivyo na uwiano. Mfano kuna wakati Sarah Harmon alitoa mapato yake ya wiki tano yaani dola moja kwa wiki kusaidia kumfadhili Joseph Bates. Kellogg aliuza shamba, huku Edson kwa nyakati tofauti aliuza mashamba mawili na kundi la kondoo ili kusaidia kueneza ujumbe.

Lakini waumini wengi waliridhika kuwaacha wahudumu wajitoe mhanga, na kama waliwapa chochote, walikuwa na mwelekeo wa kufanya hivyo kwa kutoa mazao ya shambani au, pengine, kwa kutoa nguo zilizokaribia kuchakaa. Mara nyingi sana hawakutoa chochote. Wazo la hila, na la ubinafsi lilijificha kwa kujifanya siku hizo kuwa la Kimaandiko. Kwa sababu Yesu alikuwa ametofautisha mchungaji wa kweli, ambaye hutoa uhai wake kwa ajili ya kondoo, na mchungaji aliyeajiriwa; au "mwajiriwa anayepata mshahara," ambaye hukimbia mbwa mwitu ajapo, Wakristo

wengi katika madhehebu mbalimbali walihalalisha ukarimu wao kwa kutangaza kwamba kanisa halingeweza kuhudumiwa vyema na "huduma ya watu kuajiriwa na kulipwa mshahara."

Tokeo lilikuwa kwamba wahudumu wengi walilazimika kufanya kazi ili kujipatia riziki zaidi ya kuhubiri na kutembelea watu. Wengine walitegemea kazi za vibarua vya kutwa kwani wangeweza kuvipata kutoka sehemu moja hadi nyingine. Wengine walilima, wakisafiri umbali mfupi ili kuhubiri wakiwa huru na kisha, wakiwa wamefungwa kwa kazi zao za nyumbani, waliharakisha kurudi nyumbani—hali ambayo Loughborough alilinganisha kwa kebehi na kuchukia, kwamba ni sawa na kuwa farasi aliyefungiwa.[11]

Mnamo 1855 John Andrews, akiwa bado na umri wa miaka ishirini na, alijikuta akikaribia kuchoka sana kwa kujitafutia riziki akihubiri na kuandika kiasi kwamba alikuwa karibu awe kipofu, sauti yake ilikuwa karibu kutoweka, na wapendwa wake walikuwa wakimtabiria kifo cha mapema. Alirejea hadi Waukon, Iowa, ambako kulikuwa na jumuiya ya kwanza ya Waadventista wa Mashariki waliokuwa wanashughulika na kuendeleza udongo wenye rutuba wa nyanda za juu.

John Loughborough, mwongofu wake na mtendakazi mwenzake, pia alivunjika moyo mwaka mmoja baadaye, akahamia eneo lile lile, na kwa mshangao wake mwenyewe akajigeuza kuwa farasi aliyefungwa kamba. John Loughborough na Mary mkewe wanastahili huruma yetu.[12] Walihesabu gharama kabla ya kuingia katika huduma. Muda mfupi baada ya wao kuikubali Sabato, John Loughborough alihisi mwito wenye mkazo wa kuhubiri. Lakini alijua wazi nyakati ngumu ambazo zilikuwa na maana muhimu, na wakati huo alikuwa akifanya vyema katika kazi yake ya kuuza kufuli za dirisha, "Arnold's Patent Sash Locks."

Akiba yake ilifikia $35.00, —kwa kiwango cha wakati huo kwa vibarua (dola moja kwa siku)—Ilikuwa mshahara wa wiki sita au saba. Lakini, akipinga wito huo wa kuhubiri, aliona mauzo yake yakianza kupungua kwa kasi hadi katika wiki chache, alibakia na sarafu moja tu. Akipiga magoti, alitoa mustakabali wa maisha yake ya mbele kwenye mapenzi ya Mungu na akasimama kwa amani. Muda mfupi baadaye, Mary alipoomba pesa za kununua nyuzi na viberiti, John alimwomba anunue kwa senti moja tu ya kila kimoja na kumrudishia chenji ili asikose kabisa pesa taslimu—na kisha akamkabidhi zawadi kipande cha fedha cha senti tatu. (Sarafu kama hizo zilitengenezwa kutoka 1851 hadi 1873.)

"Tutafanya nini, John?" Binti huyu alilia.” Tuingie katika huduma na umtumaini Bwana katika kila jambo,” mumewe akajibu; ambapo Bi. Loughborough, kama Bi. Bates miaka michache awali katika hali kama hiyo, alienda mbali na kuangua kilio. Muda si mrefu John alimsikia mkewe akinyemelea na kutoka nje ya nyumba. Na

alipokuwa ametoka, mtu wasiyemjua alikuja, akajitambulisha mlangoni, na kumuuliza kama Bw. Loughborough angeweza kumpatia Dola 80.00 za kufuli za Arnolds Patent Sash Locks; alimwuliza Je, angeweza kweli kumpatia kiasi hicho cha fedha! Mary aliporudi alimkuta mumewe anaimba. Thamani yake ya kamisheni ilikuwa asilimia 33%, ilikuwa imepanda hadi Dola 26.00. Sasa mkewe alikuwa tayari kwenda naye popote na kumwamini Bwana.

Mke wa mhudumu anayekaa nyumbani huku mumewe akisafiri kwa wiki mfululizo na haoni kama mumewe anavyoona roho zikiwa hatarini kuokolewa kutoka katika dhambi, mara nyingi huona kwamba si rahisi kuendana na kuwekwa wakfu au wito wa mume wake. Ni kweli Mary alikuwa mwaminifu sawa, lakini hali ya mke wa mhubiri ilionekana kuwa ngumu katika kuvumilia hali hii. Na wakati, baada ya nyakati ngumu sana, waliposikia kuhusu familia za Waadventista ambao walikuwa wamehamia mji wa Waukon ili watoe ushuhuda wa injili kwa mifano huku wakipata pesa nyingi za kutoa kwa ajili ya kazi hiyo, alihimiza kwa urahisi shauku ya John kujiunga nao.

Lakini majira ya baridi kali ya theluji yalikuja mapema mwaka huo (1856), na kufanya ukulima usiwezekane. Na John alipoona kwamba karibu hakuna wenye dhambi waliokuwa karibu wa kuwashuhudia kwenye tambarare hii ya upweke na kwamba hata watakatifu hawa, badala ya kudumu kujitoa kwenye kazi, waligeukia kwenye shughuli za dunia za kulumbana wenyewe kwa wenyewe, akachukua kazi za useremala ili kujikimu kimaisha na kuanza kusali, huku dhamiri ikiwa inamshitaki, kujipatia njia adili ya kutoboa kutoka kwenye shida zake.

Mzee na Bi. White walikuwa mji wa Round Grove, Illinois, kama maili mia mbili kuelekea kusini, wakati katika maono alionyeshwa masaibu magumu ya watu huko Waukon. Mwitikio wao ulikuwa kuondoka mara moja na kwenda kusaidia. Lakini baridi isiyotegemewa kwenye msimu ambayo ilifanya shughuli ya kilimo isiwe na ufanisi huko Iowa pia ilikuwa imegandisha barafu kaskazini mwa Illinois, ikifuatiwa na kuyeyuka. Mvua kubwa ilikuwa imegeuza barabara kuu zisizo na lami kuwa matope. Kwa imani waliomba mwongozo. Punde mvua ilibadilika na kuwa theluji, na kufanya barabara zenye theluji iliyokuwa kama ujiuji kuweza kuganda zaidi na hivyo gari la theluji liliweza kuteleza juu.

"Hii ndiyo ishara yetu," Ellen alisema. "Mungu anapenda twende." Kupitia theluji inayodondoka na kuyumbayumba kwenye anga, walitoka nje, wakifuatana na Josiah Hartand na Elon Everts, na wahudumu wengine wawili ambao, ilitokea kwamba Mzee White alikuwa amewawekea mikono ya wakfu pamoja na Andrews miaka mitatu nyuma katika nyumba ya Everts. Theluji ilibadilika kuwa mvua. Na hivyo kipindi kipya cha barafu kuyeyuka kilitanda. Barafu kwenye mito ililainika na kuyeyuka. Mara kwa mara, walisikia onyo ili kuchukua tahadhari, "Usijaribu kuingia

mto Mississippi!" Kwenye ukingo wa Baba wa Maji, Ndugu Hart aliwavuta farasi, akasimama juu kwenye gari la theluji, na akasimama na kuinua mkono wake wenye mjeledi kuelekea mbinguni, na kulia, “Je, twende kuelekea Iowa, au kurudi Illinois, tumefika kwenye Bahari ya Shamu? Je, tutavuka?" Mrs White akajibu, "Nenda mbele, ukimtumaini Mungu wa Israeli." James White alimuunga mkono. "Ndiyo, ndiyo songa mbele!"

Njia nzima waliomba. Maji ya barafu yalizunguka pande zote, futi moja kwenye ya barafu isiyojulikana iliyokuwa chini. Wakati wowote wanaweza kuingia kwenye vifo vyao kwa baridi kali. Umati wa watu ulikusanyika kwenye ufuo wa pili. Lakini kama Waisraeli kwenye Bahari ya Shamu, wasafiri hao walivuka salama. Joto lilishuka chini tena. Ellen alikumbatia vazi lake la ngozi ya komba, kwani kwa siku nne zaidi wakiwa kwenye gari la theluji lililo wazi walikabiliana na upepo mkali. Usiku, katika hoteli ya Frontier iliyoko mipakani, walitundika chati zao kwenye ukumbi na kuhubiri ujumbe huo kwa wasikilizaji wenye kiu ya kusikiliza.

Siku ya Jumatano walifika mji wa Wsssaukon. Makaribisho yao huko yalikuwa ya ubaridi kama hali ya hewa ilivyokuwa. Sasa watu hawa walijua kwanini walikuja. Ili kuwahuisha waumini wa eneo hili. Ili kurudisha kujitoa kwao kwa Kristo kwa ajili ya huduma. Kuwasha upya moyo wa utauwa waliokuwa nao zamani. Hata John Loughborough alishangazwa na jibu la maombi yake. Hakutarajia kuwa Dada White angefika bila kutarajiwa kwa gari la kuteleza kwenye barafu (sleigh) huku akifanya kazi kwenye ngazi na kumwita kwa uchungu, "Unafanya nini hapa, Eliya?"

Lakini James na Ellen waliitisha mkutano, na kisha mikutano zaidi ikaendelea katika mfululizo kwa zaidi ya wiki. Uvumi ulikuwa umefanya kazi yake ya kutisha watu, na familia ya White walizungumza na wale watu wa "upande wa pili" kwa uvumilivu hadi kila mtu akaridhika. Jioni hadi jioni nyimbo za tenzi za ujio wa Yesu zilichochea kumbukumbu za dhati. Majadiliano yakageukia ahadi ambayo Kristo alikuwa amewapa Walaodikia hawa waliokuwa vuguvugu: "Mtu akiisikia sauti Yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake."

Kufuatia maono ya wakati ufaao, Ellen alitamka maneno ya ajabu, kutoka kwa Mungu Mwenye neema: "Nirudieni Mimi, Nami nitawarudia ninyi, asema Bwana, Nami nitaponya maasi yenu yote." Fadhili kama hizo zilikuwa nyingi sana kwa Mary Loughborough. "Ndugu na Dada White," aliangua kilio, "Nilidhani tumeenda mahali palipo mbali, pale ambapo haungeweza kutupata; lakini ninafurahi kuwa umekuja ... Mungu nisamehe! ... Ninafungua mlango wa moyo wangu. Bwana Yesu, ingia!" Ungamo lilifanywa, wakaomba radhi, na mkutano uliendelea hata baada ya saa sita usiku.

Kazi nzuri ilianza tena siku iliyofuata. Mary aliwasihi wengine, nao pia wakatoa wito kwa wengine. Hatimaye John Loughborough, pia, alisimama wima na kusema "Nimeweka jembe langu mpini!" alitangaza. "Nimepigilia msumari wa mwisho! Tangu sasa mkono wangu utashika upanga wa Roho na kamwe hautauacha. Kwa hiyo nisaidie, Mungu!"

Hatimaye Familia ya White ilipoondoka Waukon, machozi ya upendo yalitiririka kwa uhuru pande zote. Akimwacha Mary kwa muda na marafiki zake, Loughborough alirudi Illinois pamoja na Hart, Everts, na familia ya White, na mara moja akarudi kwenye lijamu—sio tena kama "farasi aliyefungiwa"—kuendesha mikutano ya injili kila mahali. Hakuacha kamwe huduma hadi alipofariki mwaka wa 1924; naye Mary hakuacha tena huduma muda wote alipokuwa hai.

John Andrews alijitolea tena katika huduma, lakini angeweza kuhubiri miezi michache tu baada ya muda kwa miaka kadhaa hadi afya yake iliporudi. Wakati huohuo msichana wa Kiadventista aliyemwoa huko Waukon, Angeline Stevens, rafiki wa utotoni, bila shaka alifanya alichoweza kumnenepesha na kumfanya anawiri. Lakini tatizo la kuwalipa mishahara wahubiri lilibakia pale pale, au tuseme tatizo lilizidi kuongezeka. Mavuno mazuri ya kipekee ya mnamo 1857, pamoja na uchumi mbaya kitaifa, ulishusha bei ya mazao chini hadi pesa taslimu haikuwezekana kupatikana.

Mnamo Aprili 1858, Andrews na Loughborough walipokuwa wakiishi kwa muda huko Battle Creek, Andrews aliongoza mafundisho ya darasa la Biblia nyumbani kwa Loughborough ili kuchunguza Maandiko ili kupata nuru juu ya namna ya kutegemeza huduma kwa mapato ya aina fulani. Dada White alikuwa ameonyeshwa katika maono kwamba Biblia ilikuwa na mpango kama huo, na ilikuwa ni azimio lao kuupata na kuulewa Mpango waliougundua wakati huo ulitokana na mchanganyiko wa Maandiko ya Agano la Kale juu ya zaka na 1 Wakorintho 16:2: "Siku ya kwanza ya juma [yaani, mara kwa mara] kila mtu [mmoja mmoja] ..."kutoa "kama Mungu alivyomfanikisha [kwa uwiano]."

Waliita mpango huo "Utoaji wa sadaka kwa ukarimu na mpango." Mwishoni mwa Sabato ya Januari 29, 1859, washiriki wa lile kanisa la makao makuu walikusanyika na kupiga kura kupendekeza kwamba “kila ndugu mwenye umri wa kuanzia miaka kumi na minane hadi sitini aweke akiba karibu naye siku ya kwanza ya kila juma kuanzia miaka mitano hadi mitano. senti ishirini na tano," kila kaka katika jamii wa umri huo, alihitajika kutoa senti mbili hadi kumi, na kila dada, "kutoa senti moja hadi tano kwa kila dola mia moja ya mali waliyomiliki." Pesa zilizokusanywa hivyo na kuwekwa mahali ili kuhifadhiwa, zilipaswa kutumiwa na makutaniko ya mahali hapo, hasa kuwasaidia wahudumu walipokuja kuhubiri na kufanya mikutano ya kiinjili karibu na hapo.

Kwa miaka mingi kutoa kwa mpango ulijulikana kwa herufi zake za mwanzo yaani ‘SB” yaani Systematic Benevolence au kwa jina pendwa la utani na kuvutia zaidi “Sister Betsy” Pia ilijulikana kwa usahihi mdogo kama "kutoa fungu la kumi au zaka." Bila shaka, kile walichotoa hakikuwa ni zaka halisi. Waadventista hawakukamilisha dhana yao ya kusaidia huduma kwa msingi wa zaka kamili kwa miaka mingine ishirini. Lakini kutoa kwa ukarimu na mpango ilikuwa hatua muhimu katika mwelekeo sahihi.

Utoaji wa utaratibu umewezesha Kanisa la Waadventista kutimiza mengi duniani kote. Kutokana na yale ambayo yamesemwa, je, inaonekana kwamba kuongoza kanisa kutumia mfumo wa kutoa kwa ukarimu kwa mpango ilinufaisha watendakazi wa kanisa pekee? Ikiwa unafikiri hivyo inakupasa utafakari upya. Wachungaji, au wahudumu wameitwa kuwatumikia watu wasiowajua na kurejesha waliopotea. Lakini wanawezaje kuhudumia watu hawa ikiwa, hawapati mshahara, watakuwa hawana uwezo wa kumudu maisha. Washiriki wanawezaje kuwaamini, ikiwa hawawezi kuwa na uhakika kwamba wanawakilisha imani moja nao?

Na watu wanawezaje kujisikia huru kutoa michango wakati viongozi huria wanaweza, kwa hiari yao, kuondoka na mali ambayo ni ya watu wote? Kwa kweli, lilikuwa ni tatizo la umiliki wa mali kama vile majumba n.k ambalo hatimaye lilishawishi wanachama na kuleta suala la kuweka mfumo wa uongozi katika mawazo yao. Waadventista mwishoni mwa miaka ya 1850 walimiliki aina tatu za mali za kanisa: mahema, majengo machache ya makanisa mahalia au makanisa ya mtaa, na jumba la uchapishaji la Battle Creek, pamoja na magazeti au makala, vitabu, na mashine zinazoambatana na uendeshaji wake.

Kwa usahihi zaidi, hata hivyo, kanisa halimiliki hata moja ya vitu hivi. Tayari tumeona jinsi hema linavyoweza kutekwa kirahisi na mhudumu wa uongo. Kwa habari ya makanisa, hayakuwa ya majengo yaliyojengwa na kuyalipia bali ya washiriki ambao walisimama kwenye mali yao. Wakati wa vuguvugu la Wafuasi wa Miller washiriki wawili kama hao waliasi, na moja ya nyumba zao za mikutano ikawa ghala la siki! Kanisa la Battle Creek lenyewe lilikuwa kwenye mali ya kibinafsi ya S.T. Belden. Kwa wale ambao bado walipinga kupanga kanisa, yaani kuanzisha taasisi ya dhehebu, James White aliona kwamba hata siku moja inaweza kuwa ghala la siki. Lakini kiwanda cha uchapishaji ndicho kilichomsumbua sana Mzee White. Ilikuwa taasisi pekee ya Waadventista iliyoendeshwa mpaka wakati huo.

Uinjilisti wao ulitegemea vitabu na makala ambazo walizalisha katika jengo hili, na harakati zao zote ziliunganishwa kwa kiasi kikubwa na jarida lake kuu, Review and Herald. Ila bado tashwishwi yote, jengo, vitabu, karatasi, na mashine, kisheria ilikuwa mali iliyomilikiwa binafsi na Mzee White.

Ndugu White alijua jambo hili na hakulipenda. Kwa uhamasishaji wake mwenyewe, mapema mwaka 1855 vyombo vya habari viliwekwa kwa njia ya maneno ya mdomo tu mikononi mwa "kanisa" na uangalizi wake kukabidhiwa kwa kamati ya uchapishaji. Maamuzi makuu kuhusu utendakazi wake, kama vile ununuzi wa 1857 wa nyumba ya Uchapishaji ya Adams au chombo cha habari, yalipigiwa kura kwenye "Mikutano ya Halmashauri kuu (General Conference)" ambayo wanachama kutoka kote walialikwa.

Katika mkutano wa Septemba 1860, White aliwakumbusha wajumbe tena kuhusu Taasisi ya uchapaji Review and Herald, ambayo yeye aliinzisha ila washiriki walikuwa wanaitegemeza. Alichosema ni kwamba "mali hii ambayo imesimamishwa kwa kwa sadaka zilizotolewa na watu. ... sikuzote mimi nimekuwa nikiiona kama mali ya kanisa. Ila mimi Ndiye mmiliki wake pekee kihalali na kisheria, na ninahangaika sana kuikabidhi mikononi mwa maafisa ili tuweze kuteua atakayeishikilia na kuisimamia kisheria." Je, ingekuwa vipi kama James White angekufa ghafla? Jimbo la Michigan lingefungia kila kitu ambacho ni mali ya shirika, angalau hadi mtoto wao wa kwanza Henry White, ambaye alikuwa na umri wa miaka kumi na tatu katika mwaka 1860, atimize miaka ishirini na moja kabla hajaruhusiwa kuwa mmiliki wa mali zile za uchapaji kisheria, na wakati huo Henry, pengine hata angeweza kuiacha imani, na kisha akachukua mtambo wa uchapishaji akaenda naona kutokomea na au hata pengine angekufa. Kama mambo yalivyotokea, Henry White, mtoto wa kwanza wa James na Ellen White alikufa akiwa na umri wa miaka kumi na sita. Suluhisho la kimantiki lilikuwa kuanzisha mfumo wa kanisa kisheria. Taasisi ambayo ni halali kisheria? Katika siku zile za zamani ambapo Review ilikuwa kana kwamba ni barua ya familia, Mzee R. F. Cottrell, ndugu yuleyule aliyatoa maisha yake ili kupinga "kuupa ushirika jina na kuanzisha dhehebu," aliwasilisha insha katika makala tulivu ili ichapwe lakini ilikuwa yenye uharibifu akisema kwamba kufanya ushirika wao kuwa taasisi ya kisheria na kuipa jina na hivyo iwe dhehebu, ingemaanisha utegemezi juu ya serikali kwamba lingekuwa jambo baya na lenye kupelekea muungano wa kanisa na jambo ambalo lingetoa kiti cha enzi ambacho siku moja mtu wa dhambi anaweza kuchukua kiti chake.

Cottrell punde alighairi pointi zote mbili, akikiri kwamba ni mambo ya kufikirika, ambayo kutokea kwake itakuwa nadra sana; lakini ilichukua miezi mingi ya jitihada kubwa za James White, Joseph Bates, John Loughborough, Merrit Cornell na watumishi wengine, kutengua uharibifu aliosababisha akilini mwa watu. Mzee White alidhamiria kulinda mali ya Waadventista kwa ajili Waadventista wote. Na hivyo ikawa kwamba karibu na mwisho wa Septemba 1860 kundi la viongozi na walei walikusanyika kwa mwaliko wake katika jengo la kanisa la Battle Creek - lile la pili, lile linalomilikiwa na S. T. Belden - na kujadili suala hilo ana kwa ana kwa muda wa

siku tatu. "Hatuko katika haraka sana," alielezea, "kiasi kwamba hatuwezi kusikia sababu zao ikiwa ni mtu yoyote atapinga."

Mazungumzo hayo yaliripotiwa katika Review la Oktoba 9, 16, na 23, 1860. Karibu mwanzoni kabisa John Andrews alitoa pendekezo ambalo wengine walikuwa wamedokeza zaidi ya miezi iliyotangulia lakini hakuna lililokuwa limeeleza vizuri hivyo. Alipendekeza kwamba ni kwa ajili tu ya madhumuni ya kumiliki mali, vinginevyo kanisa halihitaji kujipanga kisheria kama kanisa bali linapaswa kuteua wawakilishi wa “chama” ambao wangeweza kuwa taasisi au kampuni kisheria (incoroporated legally). Aliongeza kwamba hilo lilipatana na utaratibu wa injili, kwa vile Wakristo wa awali waliteua halmashauri ya watu saba kusimamia masuala ya kanisa ambao walijulikana kama mashemashi saba.

Aliweza kuwadokezea pia, kwamba mashirika ya uinjilisti na mashirika ya msaada yaliyotenganishwa kimuundo na madhehebu ni kitu ambacho ni cha kawaida katika Ukristo wa kisasa wa Marekani. Pendekezo hili lililobainishwa na Andrews, kwa bahati nasibu, lilionekana kusaidia sana katika kuondoa ukuta mawazoni mwa watu waliopinga kulipa jina kanisa na kuanzisha dhehebu. Mali katika jumuiya ya Waadventista hata leo kitaalamu hazimilikiwi na makonferensi au makanisa mahalia bali shirika lenyewe (GCSDA).

Baada ya siku mbili za majadiliano mnamo 1860 katiba sahili ya chama cha uchapishaji (bado likiwa bila jina) ilipigiwa kura. Lakini chini ya sheria za Michigan hakuna chama kinachoweza kuidhinishwa bila jina; hivyo suala hilo hatimaye lilipaswa kushughulikiwa, na kumfanya James White atoe maelezo yake ya kukumbukwa kuhusu uzao huo usio na jina kwa aibu-yaani mtoto huyo aliyezaliwa asiye na jina: "Inaonekana kwangu kwamba mtoto sasa ni mtu mzima sana kwamba ni vigumu sana yeye kutokuwa na jina lake. "

Jambo lisiloepukika lilifanyika. Kamati ilipiga kura kwamba wanapaswa kupitisha jina. Lakini waite jina gani? Wengine walipendekeza, "Kanisa la Mungu," wakati wengine walihisi hii ilionekana kama wanajivuna au kuonyesha kiburi tu. "Waadventista wa Siku ya Saba" ilipendekezwa. Walei, bila hata ya kupanga, ilitokea walikuwa na sauti kati ya wajumbe kumi na tisa wanaojulikana wa kamati hii ya mabadiliko.

Alikuwa mlei, Ezra Bracket, ambaye alianzisha hoja ya kwanza mwanzoni: "Ningependekeza kwamba lipangwe." Mlei mwingine aitwaye, David Hewitt, ambaye karibu na mwisho alianzisha hoja akaitikia, "Imekubaliwa, kwamba tutachukua jina la Waadventista Wasabato." "Kuchukua jina," hata hivyo, ilisikika kama "Kujitengenezea jina," na ili kukidhi hata kashfa zisizoweza kuchunguzwa kwa wale ambao bado hawajasadikishwa juu ya mfumo, ajenda/hoja hiyo iliondolewa na

nafasi yake kuchukuliwa na azimio la "kwamba sisi tunajiita Waadventista wa Siku ya Saba."

Maendeleo ya mafanikio makubwa ya kuandaa na kulipa jina Shirika la Uchapishaji la Waadventista Wasabato hadi shirika kamili la Halmashauri Kuu ya kanisa (General Conference) ilikuwa mchakato rahisi, ingawa haikukosa pingamizi kabisa. Katika msimu wa majira ya kuchipua ya 1861 viongozi wa Battle Creek walipendekeza kwamba makutaniko mbalimbali yaliyotawanyika yajipange kwa jina la "Waadventista wa Siku ya Saba."

Mnamo Oktoba 1861, majira ya kuchipua mimea, hatua za awali zilichukuliwa kuelekea kuunda Konferensi ya Michigan na uchaguzi wa kamati ya Halmashauri kuu iliyoongozwa na Joseph Bates. Wakati wa 1862 mikutano katika majimbo mengine kadhaa iliunda konferensi za majimbo. Michigan ilikamilisha ufunguzi wake mnamo Oktoba 1862 katika Kanisa la Monterey, ikimchagua mlei, William S. Higley, kama mwenyekiti wake wa kwanza.[13]

Hatimaye mnamo Mei 1863 wajumbe kutoka katika koferensi hizi walikutana huko Battle Creek na kutayarisha katiba rahisi kwa ajili ya Halmashauri Kuu ya kanisa ijulikanayo kama General Conference of Seventh Day Adventist church. James White aliteuliwa kwa shauku kubwa, kuwa mwenyekiti wa kwanza wa General Conference wa Kanisa la Waadventista Wasabato duniani. Alikataa wadhifa huo au nafasi hiyo, hata hivyo. Tangu 1850 alikuwa amehubiri, ameandika, amehojiana, na kusihi watu kwa ajili ya "kuweka utaratibu wa injili, kupanga kanisa na kuiweka katika taasisi ili kusiwepo na machafuko."

Alikuwa ameonekana sana kwenye kampeni kiasi kwamba alifikiri kukubali uenyekiti kunaweza kusababisha baadhi ya watu kuhoji nia yake. (Miaka miwili baadaye, mnamo 1865, James White alikubali jukumu hilo. Kwa ujumla alihudumu kama mwenyekiti wa Jimbo Kuu kwa miaka kumi—1865-1867, 1869-1871, 1874-1880. James White alipokataa kuchukua urais/uenyekiti wa Kanisa la Wasabato katika awamu ya kwanza, John Byington alichaguliwa, na hivyo kuwa mwenyekiti wa kwanza wa Konferensi Kuu ya Waadventista Wasabato tunayoijua wengi wetu kama General Konferensi ya Kanisa la Wasabato.

Ilikuwa nyumbani kwake huko Bucks Bridge, New York, ndipo ambapo Horace Lawrence alikuwa amewekewa mkono. Byington alikuwa ametumikia Wamethodisti katika nyadhifa mbalimbali na kisha Wafuasi wa Wesley (Wamethodisti waliohusika na kukomesha biashara ya utumwa) kama mhudumu na mjenzi wa kanisa. Mnamo mwaka wa 1852 alipata kuwa Mwadventista kwa kusoma gazeti la Review, na baadaye akajenga majengo ya kanisa ya kwanza kujengwa na Waadventista Wasabato. Alimfadhili binti yake Martha katika jaribio lake la kuendesha shule ya

kutwa ya nyumbani kwa watoto wa Kiadventista. Mnamo 1858 alihamia Battle Creek na alisafiri sana kama mhudumu anayejitegemea.

Baada ya kuchaguliwa kuwa mwenyekiti wa kanisa wa General Conference, aliendelea kusafiri sana, akihubiri na kubatiza, wakati wa vipindi vyake viwili vya mwaka mmoja. "Hakuna mtu anayeijua vizuri Michigan," watu walisema, "kama Baba Byington." Mbali na kupiga kura ya katiba na kumchagua mwenyekiti na maafisa wengine, kikao cha kwanza cha Mkutano Mkuu pia kiliweka utaratibu wa kuwalipa watumishi mshahara wa kawaida—kama $5 kwa wiki kutokana na sadaka zilizotolewa kwa ukarimu na kwa mpango.

Iliwalazimu wachungaji kubeba vyeti vya uchungaji au leseni rasmi za kuhubiri zilizowatambulisha kama wahubiri/wahutubu wa vuguvugu hilo. Na kikao kilisema kwamba mhudumu yeyote asisafiri kutoka konferensi moja hadi nyingine kwa kutaka kwake mwenyewe au kwa matakwa ya kanisa la mtaa/mahalia. Mwito wa kwenda kuhubiri lazima ushughulikiwe kupitia konferensi zote mbili zinazohusika, yaani ile anakotoka na kule anakokwenda. Tangu hapa makanisa hayakuwa tena katika hatari ya kuwa hazina ya siki! (mahali pa chuki na magomvi)

Wachungaji wanaweza kutumia muda wao wote kwa ajili ya kazi ya Mungu. Makutaniko yangeweza kuamua kwa urahisi ikiwa mhudumu anayezuru alikuwa Mwadventista Msabato halisi au mnenaji tu wa maoni ya mtu binafsi tu. Wahubiri wangeweza kuokoa muda na nguvu isiyoelezeka kwa kufanya kazi katika maeneo maalum badala ya kukimbilia bila kupumzika katika maeneo mbalimbali. Washiriki wa eneo hilo mahalia, wangeweza kukata rufaa kwa mamlaka ya juu ikiwa wangehisi kutendewa isivyo haki na makanisa yao ya nyumbani/mahalia. Na kila mtu angalau alijua hatimaye kwamba mtu huyu ni nani. Angeweza kusema kwa kujiamini/ujasiri, "Mimi ni Mwadventista Wasabato."

*VIDOKEZO:*

*1. For the story of the Messenger and Age-toCome parties, see Review and Herald, January 14, 1858, p. 77; Loughborough, Rise and Progress, pp. 188-192, and The Great Second Advent Movement, pp. 325, 326*

*2. Review and Herald, October 9, 1860, p. 163 3. Ellen G. White, Testimonies, vol. 1, pp. 95-97*

*4. Ibid., p. 123 5. Loughborough, The Great Second Advent Movement, pp. 325, 326 6. Review and Herald, March 20, 1855, p. 197*

*7. Loughborough, The Great Second Advent Movement, p. 326*

*8. Review and Herald, September 2,1858, p. 126; Loughborough, Rise and Progress, pp. 216, 217*

*9. SDA Encyclopedia, art. "Marion Party"*

*10. J. N. Loughborough, "A Sketch," pp. 67, 68*

*11. Review and Herald, February 26, 1857, p. 136*

*12. For the stories of the three-cent silver and the rescue at Waukon, see Loughborough, Rise and Progress, pp. 176-179, 2008, 211; Review and Herald, January 15, 1857, p. 84; Ellen G. White, Spiritual Gifts, vol. 2, pp. 217-222; Ella M. Robinson, Lighter of Gospel Fires (Mountain View, Calif.: Pacific Press Publishing Association, 1954), pp. 74-76, 105- 110; Spalding, Origin and History, vol. 1, pp. 279-289*

*13. Spalding, Origin and History, vol. 1, p. 306*

## SURA YA 19
## LAODIKIA

Neno hili la Laodikia ni la kushangaza kama linavyosikika, haswa baada ya yote ambayo tumekuwa tukiyajadili kwenye kitabu hiki. Waadventista Wasabato walijipa jina miaka minne kabla ya asubuhi ya Oktoba 1860 wakati David Hewitt alipopendekeza jina "Waadventista wa Siku ya Saba." Walifanya hivyo mnamo Oktoba, 1856; nao walilitoa moja kwa moja jina hili kutoka katika Biblia. Kisa hiki kina uhusiano wa moja kwa moja na Waadventista Wasabato leo. Tangu mwanzo kabisa, kama tulivyoona, Waadventista Washika Sabato walijiona kama watu wenye kusudi, lengo na harakati ya kufikia hatima. Kwa kuamini, kutokana na uzoefu na unabii, kwamba walikuwa na Ukweli wa sasa wa siku za mwisho, walihitimisha kwamba wao ndio kanisa la Kweli la siku za mwisho.

Walikuwa Israeli wa kiroho katika jangwa la kileo, wakipiga gwaride kutoka Misri ya “Babeli” hadi ulimwengu mpya wakati wa kuja mara ya pili kwa Bwana wetu Masihi, wakiirejesha Sabato ya Kweli njiani katika safari kama walivyofanya Israeli wa kale kwenye Mlima Sinai. Walikuwa nabii Eliya, ambaye Malaki aliahidi “kabla ya ile siku ya Bwana iliyo kuu na kuogofya,” akirudisha uaminifu-upatanifu kwa sheria ya Mungu juu ya mlima Karmeli wa Jumuiya ya Wakristo iliyoasi.

Walikuwa kanisa la sita la Ufunuo, “Filadelfia,” kanisa la upendo wa kindugu. Ilikuwa ni dhana ya msingi. Barua kwa gazeti la Review kutoka kwa walei waliotawanyika zilikariri na kurudia orodha ya sifa kwa nuru ya Ukweli. Katika nyakati hizo za zamani Wamarekani wengi walihisi kwamba wanapaswa kutunza siku takatifu, ingawa wengi wao hawakufanya hivyo. Mara tu chuki dhidi ya Waadventista waliokatishwa tamaa ilipofifia, waongofu wapya walimiminika. James White alikadiria kwa furaha kwamba idadi ya waumini ambayo ilikuwa inaendelea kupaa juu angani kama roketi kwa idadi, kutoka watu wachache hadi 2000 hivi katika miaka miwili ya kwanza ya miaka ya 1850.[1]

Tulijifunza kuhusu ukuaji wa kanisa katika sura ya 17. Sasa tunahitaji kuchunguza hasara ya kiroho inayohusiana na faida hii. "Ni dhahiri," James White aliandika kwenye kipande cha mhariri wa gazeti miaka michache baadaye, "kwamba pamoja na ongezeko la idadi ya washiriki ... hapakuwa na ongezeko linalolingana la watu kujitoa wakfu kwa Bwana au neema za Roho."[2] Hata baadhi ya wachungaji waliowekwa mikono ya wakfu waliacha kazi zao ili kushughulika na kazi za kilimo, Washington Morse na Horace Lawrence wakiwa miongoni mwao.

Kwa kushawishiwa baadhi ya viongozi wenye uchu wa mali na tamaa ya vitu, washiriki wengi walijali mambo yao ya kibiashara na kupuuza wenzao au kutiliana mashaka au kuoneana kijicho. Makundi mapya ya waumini yaliyokuzwa na wainjilisti yalielekea kupotea. Machapisho na vijitabu katika ofisi ya Review yalirundikana kwa maelfu kwa kukosa mtu yeyote wa kuvisambaza. nyumba za ibada zilikuwa na deni kubwa, na ni washiriki wachache sana walionekana kujali. Hakuna aliyefanya mauaji

au kuiba benki! Lakini wakiwa watu wanaojitayarisha kwa ajili ya kuchukuliwa kwenda mbinguni na wanaodai kuweka siku moja nzima ya juma kuwa takatifu, walikuwa katika hali ya kutia huzuni, walikuwa wameangukia pabaya.

Bila kukusudia James White mwenyewe alikuwa na sehemu ya kulaumiwa! Akiwa ameudhiwa na ukosoaji kwamba mafundisho aliyofundisha yalitokana na mawazo ya mke wake, kwa hakika alifunga safu za Maandishi ya kalamu ya mkewe hapo kwenye gazeti la Review. Kusudi lake lilikuwa jema vya kutosha. Alitaka waumini watarajiwa, waweze kutambua kwamba Sabato, Patakatifu, na usingizi wa wafu ni mafundisho ya Biblia. Lakini kwa kuthaminiwa isivyofaa, maono ya Ellen White yalipungua na kupungua zaidi, na kanisa lilinyimwa kwa kiasi kikubwa maonyo na mausia yake ya kina ya kiroho.

Baada ya kuhama kutoka Rochester hadi Battle Creek, watu wa eneo hilo waliitisha mkutano katika "Nyumba yao ndogo ya Maombi" na kukiri kwa dhati dhambi yao katika suala hili. Waliweka majina yao kwenye ungamo kwa ajili ya gazeti la Review na wakapiga kura ya kusisitiza kukabiliana na gharama ya Uchapishaji wa ‘mashauri ya wakati uliopo’ ya Ellen White. Kwa njia hii ilipatikana fedha ya kuchapisha Gombo la kwanza la kitabu “Shuhuda kwa kanisa.”

Kitabu hiki kilionekana mwishoni mwa mwaka wa 1855 kama kijitabu chenye kurasa kumi na sita—kiliunganishwa pamoja na Shuhuda zingine katika nusu karne iliyofuata pale Shuhuda zingine thelathini na sita zilipoongezeka, ambazo zimeunganishwa leo katika juzuu tisa zinazojulikana. Sasa, katika kitabu cha Ufunuo, Yohana aliagizwa kuandika barua kwa kila moja ya makanisa saba yanayowakilisha awamu saba au vipindi saba vya uzoefu wa Kikristo kuanzia siku yake hadi kuja kwa Masihi mara ya pili.

Wafuasi wa Miller walilichukulia ipasavyo kanisa la sita au la "Filadelfia" la upendo wa kindugu kama ishara ya harakati zao wenyewe. Baada ya kule kukatishwa tamaa kukuu kwa Oktoba 22, 1844, Wafuasi wa Miller waliokubali Sabato na mafundisho ya Patakatifu walifurahia ushirika mchangamfu wa Kikristo kiasi kwamba waliendelea kujiona kama Filadelfia - na wakawaita majina Waadventista wengine kama "Laodikia," kanisa la saba.[3] Maneno, “vuguvugu” na “mimi ni tajiri, ... wala sina haja ya kitu,” yalionekana kuwafaa watu waliofikiri wangeweza kuishi bila Sabato na roho ya unabii. Lakini kadiri hali ya kiroho ilivyoshuka katika safu zao wenyewe, ndivyo waumini walio dhati/wanyofu walivyozidi kuhisi kwamba “Filadelfia” ilikuwa haistahili kuwawakilisha sana washika Sabato.

Familia za watu wenye fikra mahiri zilijadili hapa na pale uwezekano wenye kuondoa faraja moyoni kwamba wao wenyewe walikuwa Walaodikia. Karibu na mwisho wa Gombo la Shuhuda namba. 1, Bibi White alisisitiza na kufikisha wito

wake kwa uwazi kwa maneno yaliyochukuliwa kutoka kwenye ujumbe wa Laodikia.[4] Kwa bahati mbaya maneno yake, ingawa yalithaminiwa, yalileta matunda kidogo kwa wakati huo.

Mnamo Mei 1856 aliandika maono kuhusu dhambi ya familia za Waadventista kujipatanisha na ulimwengu. Baada ya kusikia  Shuhuda hii ikisomwa, waumini wa Battle Creek walipiga kura kwa kauli moja kuichapisha, na kufikia Agosti ilikuwa kwenye barua kama Shuhuda kwa kanisa, Gombo la Pili). Shuhuda hii ilileta wasiwasi kwa wale watu waliokuwa  na dhamiri zinazojali, lakini kama gombo la kwanza la Shuhuda, bado gombo la pili lilikuwa na matunda machache yaliyoonekana papo hapo.

Njia ilifunguka mnamo Oktoba (kumbuka mwezi huu), wakati James White alipozindua mfululizo au makala zilizotafakariwa kwa umakini katika gazeti la Review, zikionyesha kwa kusadikisha kutoka katika Biblia kwamba Waadventista Washika Sabato, kanisa la mwisho kwa siku za mwisho, waliwakilisha bila mashaka kanisa la saba la Ufunuo, kanisa lenye vuguvugu lililojitosheleza la Laodikia.[5] Hapa kulikuwa na jina la mtoto anayekua! Hapa, pia, kulikuwa na ushahidi wa Biblia ambao ulithibitisha hofu zao wenyewe na maono ya Ellen White. Na jibu lilikuwa la kuleta furaha moyoni kweli kweli.

Ikiwa na washiriki chini ya 2000 waliojiorodhesha kulipata, Gazeti la Review lilipokea zaidi ya barua 300 kwa muda wa miezi michache iliyofuata, kumshukuru Mzee White kwa kuzungumza wazi na kuonyesha unyenyekevu na kujitoa wakfu upya. Uamsho wa kweli ulianza na ushindi mkubwa ulipatikana. Jukumu la Ellen White katika uamsho huu lilikuwa muhimu. Shuhuda zake zilifungua njia kwa hilo. Na alipokuwa akisafiri pamoja na mume wake, maono yalikuja, yakirekebisha ujumbe wa Laodikia kulingana na mahitaji ya mahali hapo. Huko Waukon—ambapo, unakumbuka, Familia ya White walizuru mnamo Desemba mwaka huo—picha ya Walaodikia ya Yesu akigonga mlango ilimfanya Mary Loughborough kulia kwa machozi, "Ninafungua mlango wa moyo wangu. Bwana Yesu, ingia ndani…."

Shuhuda mbili zikatolewa tena katika 1857 zilithibitisha zaidi uwasilishaji wa Mzee White. Baada ya maono, Ellen White aliripoti kwamba alikuwa ameonyeshwa marundo ya "takataka" ambayo watu walihitaji kuondoa kutoka katika milango ya mioyo yao - tofauti kati yao na ndugu zao, kupenda vitu vya dunia hii, ubadhirifu katika mtindo wao wa maisha, hasira zenye uovu, na kadhalika. Umakini wake pia uliitwa kwenye ahadi kwa Laodikia. "Ahadi hii ilikuwa ya thamani kama nini," alisema, "kama nilivyoonyeshwa katika maono! 'Nitaingia kwake, na nitakula pamoja naye, na yeye pamoja Nami.”[6]

Kwa kweli barua kwa Laodikia imejaa ahadi na pia uwapo Wake Yesu Kristo. Ni Yesu anayejitambulisha kuwa ni “Shahidi wa Kweli” na kuwaambia Walaodikia wanaojidanganya hali yao halisi. Yesu anasema kwamba wao ni vuguvugu. Yesu anasema wanahitaji dhahabu, mavazi meupe, na dawa ya macho. Yesu, “mfanyabiashara/mchuuzi wa mbinguni,” anabisha mlangoni akiwa na vitu hivi vya kuuzwa. Yesu anatoa ofa ya kuingia na kula pamoja nasi. Na Yesu, mwishoni, anaahidi kwamba kila mshindi "ataketi pamoja Nami katika kiti Changu cha enzi." Lakini kuna jambo tunalopaswa kufanya. Lazima tufungue mlango. Yesu hatawahi kuvamia au kujipenyeza kwa nguvu kwenye faragha yetu bila idhini yetu. Na ni lazima "tununue" kile Alicho nacho, ambacho anatuuzia sisi. Tunaweza kununua haki ya Kristo “bila fedha na bila gharama” (Isaya 55:1); lakini hakuna anayeweza kuwa mfuasi wa Kristo isipokuwa ametelekeza/ameacha kila kitu alicho nacho (Luka 14:33)

Katika maono ya pili, Ellen White aliona vikundi viwili vya washika Sabato wakiitikia ujumbe kwa njia mbili tofauti. Kundi moja lilikuwa la watu wasiojali na wazembe. "Malaika wa Mungu waliwaacha watu hawa." Kundi lingine lilikuwa linaukubali ujumbe. Kwa shauku waliondoa takataka - lakini si kwa nguvu zao wenyewe; waliteseka sana katika maombi ili Mungu awape nguvu. Na walipata ushindi! Wakishinda vitabia vya ukosoaji, ubinafsi, na kushuku wengine, walipigwa gwaride kwa utaratibu mkamilifu, wakiwa wamepangwa kama jeshi. Walijazwa na mvua ya masika (Roho Mtakatifu Yoeli 2). Waliushuhudia ulimwengu kwa mafanikio makubwa yenye kustaajabisha; na upesi wakamkaribisha Kristo katika ujio Wake wa mara ya pili.[7]

Ni fursa tukufu kama nini! Na ilitambuliwa kwa sehemu tu. Walipokutana katika vyumba vyao jikoni, ghalani, na kwenye makanisa madogo, watunza Sabato hawa waliungama kwa ajili ya ugumu wa mioyo yao, na chuki miongoni mwao na kuomba msamaha. Wazazi na watoto walijadili kutokuelewana kwa uwazi mpya na kumaliza tofauti zao. Kwa imani, watu walijitoa kwa kujinyima upya, na kujitoa kama dhabihu, hadi deni zito kwenye ofisi ya uchapishaji lilipogeuzwa na wakawa na ziada ya faida ya kutia moyo.

Kiwango cha ubatizo kiliongezeka. Mwendo mzima ulionekana kuwa na mashavu yenye unyevunyevu, yaani watu wakalia machozi ya furaha na majuto na nyuso zenye kung'aa, wakati Walaodikia waliotubu walipojisalimisha kwa Bwana, na kushangilia katika njia mpya ya maisha, na kila siku wakatazamia mvua ya masika. Kumruhusu Yesu moyoni ni sawa na kumpokea Roho Mtakatifu, kwa maana Roho Mtakatifu Ndiye mwakilishi binafsi wa Kristo. Watu wanapomleta “Kristo” katika kila sehemu ya maisha yao, Roho Mtakatifu huwajaza, akiwatayarisha kwa ajili ya mvua ya masika.

Mwonekano huu wa harakati za toba ulikuwa sio sahihi au wa kweli kabisa. Waumini wengi walibaki kuwa watu wa kutojali. Wengine waliuliza, “Kwa nini Ndugu na Dada fulani hawabadili mtindo wao wa maisha? Wengine walisisitiza juu ya uhuru wao na walikataa kuamini uongozi. Mvua ya masika ilichelewa kwa watu hawa. Na hata wale walio na bidii zaidi, baada ya kusahihisha mambo machache tu, waliona kwamba walikuwa wamefanya vya kutosha (wamefika). Maono ya Julai 15, 1859 (tena tafadhali angalia tarehe), yalifichua kilichokuwa kimeenda vibaya. "Kama wengine wao walivyokuwa, nao walishindwa kuona kazi ya nguvu iliyokamilishwa kwa muda mfupi, wengi walipoteza matokeo ya ujumbe."

Bibi White alisema: "Niliona kwamba ujumbe huu hautakamilisha kazi yake katika muda wa miezi michache."[8] Inaonekana kwamba Mungu alingojea kwa kukusudia msisimko upungue ili kuruhusu watu Wake kutenda kwa kanuni badala ya msisimko. Hivi ndivyo Mungu afanyavyo kazi sikuzote, Ellen White alieleza: “Ili watu Wake wasije wakadanganyika kuhusiana na wao wenyewe, Yeye huwapa wakati wa msisimko huo kuisha, na kisha huwathibitisha ili kuona kama watatii shauri la Shahidi wa Kweli."[9]

Ni dhahiri kazi iliyohitajika kuwafanya Waadventista kuwa tayari kwa mvua ya masika katika miaka ya 1850 haikupaswa kukamilishwa katika ibada moja ya maombi ya usiku kucha, au katika majuma kadhaa ya ibada ya kiroho, au hata katika ile “miezi michache, ambayo haikuwa mingi sana vile. " Kumtafuta Bwana kwa dhati kulihitajika kwa muda mrefu zaidi hadi tabia ilipokomaa katika viwango vipya vyenye kina na angavu. Lakini kama matengenezo ya kutosha yalihitaji zaidi ya miezi michache, je, miaka mingi ilihitajika kabla ya mvua ya masika kunyesha?

Katika ushuhuda uliotajwa hivi punde, maneno haya ya umeme , yaani nguvu kubwa pia yanaonekana, "Mungu ameupa ujumbe muda wa kufanya kazi yake." Ilikuwa Julai 1859 wakati Ellen White alipoandika maneno haya, pungufu ya miaka mitatu baada ya ujumbe wa Laodikia kufika kwa Waadventista Washika Sabato. Je, inawezekana kweli? Je, ina maana kwamba kabla ya Julai 1859 wafuasi wa upendo wa Mungu waliokosea wangeweza, kwa neema Yake, kuondoa takataka zote maishani mwao, kupata ushindi, kujazwa na Roho kama siku ya Pentekoste, na kuwa njiani kwenda kushuhudia kwa mafanikio makubwa kwa kila taifa, kabila, lugha, na watu kabla ya Julai 1859?

*Vidokezo:*

*1. For the story of the Messenger and Age-toCome parties, see Review and Herald, January 14, 1858, p. 77; Loughborough, Rise and Progress, pp. 188-192, and The Great Second Advent Movement, pp. 325, 326*

*2. Review and Herald, October 9, 1860, p. 163 3. Ellen G. White, Testimonies, vol. 1, pp. 95-97*

*4. Ibid., p. 123*

*5. Loughborough, The Great Second Advent Movement, pp. 325, 326*

*6. Review and Herald, March 20, 1855, p. 197 333*

*7. Loughborough, The Great Second Advent Movement, p. 326*

*8. Review and Herald, September 2,1858, p. 126; Loughborough, Rise and Progress, pp. 216, 217*

*9. SDA Encyclopedia, art. "Marion Party"*

*10. J. N. Loughborough, "A Sketch," pp. 67, 68*

*11. Review and Herald, February 26, 1857, p. 136*

*12. For the stories of the three-cent silver and the rescue at Waukon, see Loughborough, Rise and Progress, pp. 176-179, 2008, 211; Review and Herald, January 15, 1857, p. 84; Ellen G. White, Spiritual Gifts, vol. 2, pp. 217-222; Ella M. Robinson, Lighter of Gospel Fires (Mountain View, Calif.: Pacific Press Publishing Association, 1954), pp. 74-76, 105- 110; Spalding, Origin and History, vol. 1, pp. 279-289*

*13. Spalding, Origin and History, vol. 1, p. 306*

## SURA YA 20
## HISIA ZA UTUME

Bendera mia moja tisini na tatu! Ilivutia kuwatazama, wakiwaka kwa rangi, wakiruka kwenye mwangaza wa jumba la manispaa huko Vienna, Austria. Kila mtu aliwakilisha nchi tofauti ambamo Waadventista Wasabato walikuwa wakiendesha kazi iliyopangwa wakati wa kikao cha hamsini na mbili cha Konferensi Kuu -General Conference session, Julai 1975. Julai 1975 ilikuwa miaka 116 baada ya Julai 1859. Ikiwa watunza Sabato walikuwa wamejitayarisha kwa ajili ya mvua ya masika katika Miaka ya 1850, hawakupaswa kuchukua muda mrefu sana kuingia na injili katika nchi hizi zote. Hata hivyo kazi katika nchi 193 inawakilisha maendeleo ya kweli (kuna nchi 197 duniani, ila ukijumlisha na maeneo yanayojulikana kama territories, zipo nchi 215)

Makanisa yanayofuata ya Kiprotestanti yanayofanya kazi kwa utendaji hai yanafanya kazi katika nusu ya nchi hizo tu. Waadventista Wasabato daima wamehisi "hisia ya utume." Kifungu cha V cha katiba fupi ya General Conference au halmashauri Kuu ya kanisa la Wasabato ya 1863 kilihitaji kamati kuu ya watu watatu kufanya kazi kama "bodi ya wamishenari." Kabla ya hapo, mradi wa kwanza wa biashara wa Waadventista Washika Sabato ulikuwa ni ununuzi wa mtambo wa mkono wa uchapaji wa Washington kuchapisha Ukweli. Kabla ya hapo, katika mikutano ya 1848 huko Rocky Hill na Volney, watu walisikiliza maono ya Ellen White juu ya "jinsi tunavyopaswa kufanya kazi na kufundisha kwa ufanisi."[1]

Na kabla ya hapo, katika wakati ule ule uliovuviwa wakati Hiram Edson alipokuwa mtu wa kwanza kutambua huduma mpya ya Kristo ya mbinguni, Maneno ya Ufunuo yaliangaza akilini mwake: “Imekupasa kutoa tena unabii mbele ya watu wengi na mataifa na lugha; na wafalme." Tangu mwanzo kabisa Uadventista wa Sabato umekuwa zaidi ya jamii ya kidini tu. Hakika imekuwa harakati yenye ujumbe na hisia ya utume. "Hebu ujumbe upeperuke juu," aliandika James White katika mwaka 1849, "kwa maana wakati ni mfupi." "Kwa maana muda ni mfupi."

Kinadharia, imani kwamba Kristo anakuja upesi ingeweza kuzuia uenezaji wa ujumbe wa malaika wa tatu. Hii iliweka mipaka katika maono ya waumini wa

kwanza kwa udogo; lakini kwa shilingi ya York na senti tatu ya fedha walifanya bidii zaidi kadiri walivyoweza kwenye maeneo ya karibu, na milango ya fursa ilipofunguka, walijikaza na kusonga mbele, ili kupanua maono yao ipasavyo.

Mapema Februari 1845 Ellen White alipewa maono ya kazi kubwa sana ambayo Mungu alitaka ifanywe kabla ya kurudi kwa Kristo. Alichukuliwa mbinguni na kuagizwa atazame nyuma. Wanaanga huwa wanafurahi kuona dunia inang'aa kama yakuti samawi-sapphire; Lakini Ellen aliona ulimwengu katika giza la maadili. Alipotazama kwa makini, aliona "michirizi ya mianga ya nuru (jets) inayotokeza kwenye upenyo mdogo, na kuonekana kama nyota" zikiwaka moto huku na huko, kisha michirizi ya mianga mingine, na bado mingine zaidi katika sehemu nyingine, "ikizidi kung'aa, ikiangaza kutoka mashariki na kutoka magharibi, na kutoka kaskazini na kutoka kusini, na kuangaza ulimwengu wote: “Nuru ya mianga hii iliyoenda kwa kasi, ilitoka kwa Yesu, na ilisimama kwa watu waliokuwa na imani na wale waliolitii Neno, ambao walishikamana na ujumbe wa malaika wa tatu.[2]

Kisha mnamo Novemba 1848 yakaja maono ya Sabato iking'aa "kama vijito vya nuru vilivyopita wazi kuzunguka ulimwengu." Waumini walipomsikia Ellen akizungumza kuhusu mambo haya, baadhi yao walimtuhumu kwa kuahirisha ujio wa pili.[3] Lakini wengine walifurahi. Bates alichapisha akitabiri moyoni kwamba Sabato ingeenea mara moja hadi Ufaransa, Uingereza, Urusi, na Mashariki ya Kati.[4] James White kabla ya mwaka kwisha (1849) alishawishika kwamba Sabato "itagonga kengele yake katika mataifa, kuliko vile ujumbe wa marejeo ulivyowahi kuenea."[5] Huo ulikuwa utashi wenye ubunifu wa yale yanayoweza kutokea mbele!

Wakosoaji wa Uadventista wamefanya sehemu kubwa ya hatua ya awali ya kuvutia ya harakati inayojulikana kama "kipindi cha mlango kufungwa." Viongozi wa Wafuasi wa Miller mara nyingi walizungumza juu ya mlango kufungwa. Miller aliamini kwamba siku chache kabla ya Oktoba 22, 1844, mlango wa rehema ungefungwa dhidi ya wote waliokataa ujumbe wa malaika wa kwanza.[6] Baadhi ya Waadventista Washika Sabato waliendelea kushikilia maoni haya kwa muda mrefu tofauti-tofauti, baada ya kukatishwa tamaa.

Ellen White aliamini hadi alipopata maono yake ya kwanza.[7] James White aliamini kwa muda mrefu zaidi, na Joseph Bates kwa muda mrefu zaidi. Hata hivyo, kimantiki au la, Bates, Familia ya White, na wengine waliojiunga nao, walishiriki imani yao bila kuchoka na wote ambao wangesikiliza, kwa kuwa walikuwa chini ya hisia kubwa ya uharaka, naam, hali ya dharura katika kuruhusu ujumbe upeperuke kwa kuwa wakati ulikuwa mfupi. Inaeleweka, kwamba kwa vile ubaguzi mwingi ulikuwa dhidi yao, ilitokea kwamba hakuna mtu aliyewasikiliza hapo kwanza isipokuwa Wafuasi wa Miller wa awali. Lakini kama "walimwengu" wowote wangejitokeza kwa kuja kwenye mikutano yao, watu hao hawakusindikizwa nje.

John Wilcox aliiambia familia ya Loughborough kwamba aliongoka "kutoka nje ya ulimwengu" wakati wa mkutano wa Aprili 1848 huko Rocky Hill, Connecticut, na kwamba James White alimbatiza hapo hapo.[8] Mnamo 1850 Ellen White alimwandikia rafiki yake kwamba “watu walikuwa wakiingia kutoka pande zote" Oswego, New York.[9] Kufikia 1852, Wamethodisti na Wabaptisti walikuwa wakitoka "Babeli" ili "kuharakisha katika njia ya safari ya amri zote za Mungu."[10] Mara tu hawa watu wasio Waadventista walipotaka kujiunga na jeshi la washika Sabato walifanya jambo linalopaswa kutiliwa umakini.

Badala ya kung'ang'ania fikira za kutengwa zilizotokana na kutoelewa kwa namna fulani huduma ya Kristo katika Patakatifu pa Patakatifu sana, walichunguza theolojia yao ili kuona kama walikuwa wamepuuza jambo fulani. Waligundua kwamba ingawa kazi kuu ya Kristo tangu 1844 imekuwa ni kufuta dhambi za waumini, hata hivyo anabaki kuwa Kuhani Mkuu wa kila mwenye dhambi.[11] kwa hiyo, Ilikuwa ni sahihi kitheolojia kuwakaribisha waongofu waingie. Kwa kumbukumbu ya kukatishwa tamaa pale 1844 Oktoba kufifia, wale wasio Wafuasi wa Miller walizidi kuwa tayari kusikiliza. Kufikia majira ya kuchipua mwaka 1852 watu hao walifanya sehemu kubwa zaidi ya waongofu;[12] na kufikia katikati ya miaka ya 1850, kama tulivyokwisha kujifunza, mahema ya kiinjilisti yalisitawi kama uyoga katika jimbo moja baada ya nyingine.

Makutaniko ya mamia, hata elfu moja au zaidi, yalikusanyika ili kuwasikiliza Loughborough, White, Andrews, Cornell, Waggoner, Sanborn, Taylor, Hull, na wengineo wakihubiri Neno la Mungu. Lakini hata kuhubiria umati kutoka Maine hadi Minnesota hakufikii agizo la Kristo la kupeleka injili ulimwenguni kote (Mathayo 24:14; 28:18-20). Washika Sabato hawakukataa agizo la injili. Badala yake, waliona mfanano wenye kutokeza kati ya agizo lililo katika Mathayo 24:14 (“Injili hii itahubiriwa ili... kuwa ushuhuda kwa mataifa yote”) na ujumbe wa malaika wa kwanza katika Ufunuo 14:6, 7 ... (“injili ya milele. ... kwa kila taifa na kabila na lugha na jamaa"). Kwa muda walidhani kwamba walikuwa wametimiza agizo chini ya ujumbe wa malaika wa kwanza kwa kupeleka tumaini la ujio wa Masihi kwa kila kituo cha misheni kabla ya Oktoba 22, 1844.

Hata hivyo, wakichochewa na wale wasiokuwa Waadventista, na wengi waliosongamana kwenye hema zao, kwa mara nyingine tena walifanya hivyo, walichunguza theolojia yao. Ingawa walidhani kwamba ujumbe wa malaika wa kwanza ulikusudiwa kwa ulimwengu na ujumbe wa malaika wa tatu, kwa watakatifu tu, Ellen White aliwaongoza kuona kwamba ujumbe wa malaika wa tatu, pia, ulikusudiwa kwa "ulimwengu wenye hatia."[13] Na wakiwatazama tena wale malaika watatu, waliona ya kuwa wote watatu wanaenda sambamba mpaka kuja kwa Yesu mara ya pili,[14] na hivyo kufikia hitimisho kwamba Injili lazima iendelee kuhubiriwa kwa mataifa, na kabila, na lugha, na jamaa.

Hali ikiwa hivyo, kuhubiri Neno hata kwa Waamerika wa Kaskazini wote wanaozungumza Kiingereza ilionekana kutotosha tena. Mnamo 1855 Joseph Bates aliwahimiza waamini wenzake wapeleke kwa posta machapisho kwenye "baadhi ya vituo vya wamishenari vya kigeni, hasa kwenye visiwa vya Sandwich."[15] Mnamo 1856 James White alionya: "Roho ya umishenari inatafutwa kuinua kilio kwa upana zaidi katika nyanja mpya, na kupiga kengele kote kwenye ulimwengu wa Kikristo."[16]

Mnamo 1857 R. F. Cottrell alihubiri kupitia mkalimani kwenye kundi la Wahindi wekundu wa Seneca (walikuwa Wabaptisti) kando ya Mto Tonawanda, Niagara falls, New York.[17] Mwaka huo huo ndugu wa Bourdeau waliozaliwa nchini Canada, watu wenye lugha mbili (bi-lingual), A.C. na Daniel T., walianza kueneza injili kwa watu wanaozungumza Kifaransa huko Vermont, wakisaidiwa mwaka uliofuata na kasisi wa zamani wa Kikatoliki, M. B Czechowski, ambaye habari zake zitasemwa zaidi baadaye. John Fisher, mchungaji wa zamani wa kanisa la Baptisti, alitafsiri machapisho kwa lugha ya Kiholanzi kwa ajili ya wahamiaji karibu na Holland, Michigan.

Akitiwa moyo na maendeleo kama hayo, Uriah Smith alihariri katika Review ya mwaka 1859 kwamba “pengine” amri ya kutoa unabii kwa watu na lugha ingeweza kutimizwa katika Amerika Kaskazini![18] Smith alikuwa mwangalifu. Joseph Clarke, mwalimu mwenye bidii wa shule ya Ohio, hakuwa mwangalifu sana. "Kazi haipaswi kugawanywa," alionya. "Ireland iko karibu kama Ohio tu, na Urusi inapendwa kama Iowa."[19] Wengine pia wenye maono mapana zaidi kuliko mhariri wa Review, walikuwa tayari wamesafirisha vitabu na machapisho kwa jamaa zao ng'ambo.

Mapema miaka ya 1860 ripoti zilitoka kwa watu wa Ireland ambao walikuwa wameanza kushika Sabato mwaka wa 1859 na ambao walikuwa na shukrani nyingi kwa Review na Shuhuda za Dada White. "Mimi mwenyewe, na watoto wawili, na yaya wangu," aliandika mmoja wao, "tushike siku ya saba. Mtumishi wangu wa nyumbani namlazimisha asifanye kazi."[20] Ni rahisi kuelewa kwa nini katika miaka ya 1850 Waadventista walituma machapisho badala ya wahubiri kwenda ng'ambo.

Wachungaji waliokuwepo, waliokuwa na kazi nyingi, waliolipwa mishahara duni, na kuongozwa bila dira kamili, hawakuweza kabisa kukidhi mahitaji ya nyumbani. James White alifikiri moyoni kwamba wachungaji walikuwa na wito/miito kutoka kwa watu mara ishirini zaidi ya vile ambavyo wangeweza kuhudumia/kuhudumu. Na Je, wachungaji wangewezaje kutumikia nje ya nchi kwa shida kabla ya msingi wa nyumbani kupangwa vizuri katika utume wa kusaidia watu kuona nuru.

Kwa hivyo tunarudi kwenye taasisi ya Konferensi Kuu iliyoanza 1863 na mwanzo wa kamati yake tendaji kama bodi ya wamishenari. Ikiwa kwa hakika ilikuwa ni bodi ya wamishenari, iliyopewa jukumu la kuchagua wafanyakazi na maeneo kwa ajili ya

shughuli ya umishenari, kwa nini basi ilichukua miaka kumi na moja kutuma mmishenari wake wa kwanza wa kigeni, yaani J. N Andrews? Kwanza, kabisa, hii ilikuwa shughuli kubwa, yaani kuwatuma wamishenari nyumbani. Miongoni mwa hatua zake za kwanza zilichukuliwa mnamo 1863, hapo kura ilipigwa kwamba Isaac Sanborn apelekwe “kama mmishonari huko Minnesota." Alikuwa mmoja tu wa wachungaji/wahudumu kadhaa waliotumwa na mahema ya uinjilisti kwa msimu uliofuata na kujulikana kama wamishenari.[21]

Wainjilisti waliitwa wamishenari kama ipasavyo katika miaka ya 1850 na 1860. Mapema kama mwaka 1853 Loughborough na Cornell walikuwa wametumwa na kutaniko la kujitoa kwa kujinyima na kundi la mji wa Jackson, Michigan, kwenye "misheni" ya miezi kadhaa kwa walio wapweke, na maeneo yenye watu wachache, kwenye nyasi ndefu za Prairie huko Wisconsin na Illinois.[22] Sanborn kwenye misheni yake ya Minnesota 1863-64, alipitia maili 2400 zenye ugumu, na upweke katika miezi minane.

Na wakati J. N. Loughborough na Daniel Bourdeau walipojitolea kwenye Mkutano Mkuu yaani General Conference session ya mwaka 1868 kwa ajili ya uinjilisti wa hema huko California, yaani mahubiri ya hadhara au efoti (Tent meeting), walikwenda kama "wamishenari" Hakika. Walisafiri kuelekea kusini kwenye bahari ya Atlantiki, kisha wakavuka mpaka nchi ya Panama, na kisha kuelekea kaskazini hadi San Francisco, walisafiri maili 7000, mbali zaidi na makundi mengi kuliko vile ambavyo Andrews angeenda mnamo 1874 ili kufika Uswizi.

Ukweli ni kwamba, licha ya jukumu lake zito la misheni za nyumbani, Kongamano Kuu, yaani General Conference halikungoja miaka kumi na moja kabla ya kufikiria kutuma mmishenari katika nchi za kigeni. Akiwa na shauku kama mvulana mdogo shuleni, James White aliripoti kwamba kamati ya utendaji, yenye umri wa siku chache tu, ilikuwa tayari inafikiria kumtuma B. F. Snook kama "mmishenari Ulaya" kabla ya mwisho wa 1863.[23] Kwa majaliwa ya Mungu, lilikuwa na mawazo ya pili miongoni mwa watu, kwani kama unavyokumbuka, Snook hivi karibuni alikuwa amegeuka na kuwa Universalist.

Mnamo 1864 M. B. Chekowski alitafuta idhini kurudi Ulaya kama mmishenari. Kwa kusita kamati ilikataa ombi lake kwa matumaini kwamba wangeweza kumtuma hapo baadaye..[24] Chekowski, kama tutakavyoona katika sura inayofuata, alipata uungwaji mkono kutoka kwa Waadventista washika Jumapili na kwenda Ulaya hata hivyo. Miaka michache baadaye mmoja wa waongofu wake wa Uswisi, James Erzberger, alikuja Marekani. Wakati wa kukaa kwake aliwekwa wakfu na kupewa leseni ya uchungaji, ili aweze kurudi Uswisi "kushiriki katika kazi kubwa ya kuhubiri onyo la mwisho kwa wanadamu." Alitazamwa kama mmishenari na Ulaya ilizingatiwa kama uwanja wa misheni, mapema mwaka 1870.[25]

Wakati huo huo, na kwa kiasi kikubwa tunasema jambo lisilohusiana moja kwa moja na maendeleo haya ya kazi, kulikuwa na kundi la wanawake katika kijiji kilichosinzia kiroho cha Lancaster Kusini, Massachusetts, wakitiwa moyo na Stephen Haskell mwenye bidii na hawa wakiongozwa na Roxie Rice mwenye rasilimali au vyanzo vya kusaidia kazi, waliungana mnamo 1869 kuunda Jumuiya ya Wamishenari mahiri waliokesha.[26] Kwa namna fulani walipata wakati wa kusali, kuwaita jirani zao, kusaidia wagonjwa na wenye uhitaji, na pia kutuma maelfu ya machapisho na vitabu kwa watu kwenye nchi za Amerika Kaskazini na katika nchi nyingi za mbali. Walidumisha rekodi bora na waliandika mamia na mamia ya barua.

Mwaka uliofuata Haskell, mwenyekiti mpya aliyechaguliwa wa Konferensi ya New England, alianzisha chapisho lililoitwa New England Tract and Missionary Society, akichochea kupangwa kwa "T. na M." (Ikiwakilisha jumuia ya Tract and Missionary) kote New England (majimbo ya Connecticut, Maine, Massachusetts, New Hampshire, Rhode Island, and Vermont). Mnamo 1873 aliombwa kufadhili Vyama vya T. na M. kote Marekani. Katika hali nyingi zaidi kuliko mtu yeyote ajuaye, waongofu wa kwanza kwa ujumbe wa malaika wa tatu katika nchi za mbali walivutwa na wamishenari walei wa Jumuiya za T na M miaka kabla ya kuwasili kwa mmishenari ana kwa ana.

Tulianza sura hii kwa kutazama bendera kwenye Konferensi Kuu ya 1975-General Conference Vienna. Mwaka uliotangulia, 1974, ulichaguliwa na kanisa kuadhimisha "miaka mia ya utume wa Waadventista Wasabato ulimwenguni" kwa heshima ya kuondoka kwa J. N. Andrews mnamo 1874 kwenda Basel Uswiss. Lakini kwa sababu Waadventista Wasabato wamewahi kuwa vuguvugu lenye hisia ya utume, tarehe zingine zinaweza kutumika kwa kusudi lile la mmishenari wa kwanza (Hata hivyo Mmishenari wa kwanza ni Mungu Mwenyewe, alitaka kumfikia Adamu pale kwenye bustani ya Edeni baada ya dhambi!).

Kwa mfano, 1918 ingeweza kuwakumbusha 1818, wakati ambapo mwadventista wa awali, William Miller,  alisikia wito wa "kuuambia ulimwengu." Mwaka wa 1959 ulikuwa karne baada ya mtu wa kwanza wa Ulaya kuukubali ujumbe wa malaika wa tatu huko barani Ulaya. Na 1964 ilikuwa miaka 100 baada ya M. B. Czechowski kusafiri kama mmishenari wa kwanza wa Waadventista wa Sabato "wa kujitolea" huko ng'ambo.

*Vidokezo:*

*1. Ellen G. White, Selected Messages, bk. 1, p. 207*

*2. Review and Herald, July 26, 1887, p. 466*

*3. Ellen G. White, Selected Messages, bk. 1, p. 74*

*4. Bates, A Seal of the Living Cod, pp. 4, 35, 40, 45*

*5. James White to Brother Bowles, November 8, 1849*

*6. Midnight Cry, October 12, 1844, p. 122*

*7. Ellen G. White, Selected Messages, bk. 1, p. 74*

*8. Loughborough, "A Sketch," p. 50 361*

*9. Ellen G. White, Letter 4, 1850*

*10. Review and Herald, June 24, 1852, pp. 28-29. The tradition that David Hewitt was the first non-Adventist to accept the third angel's message is attested in Loughborough, "A Sketch," pp. 54, 55. It seems to be refuted by evidence in the voice of Truth that Hewitt was an Adventist in 1845*

*11. For example, Review and Herald, February 3, 1853, p. 148. The best history of the developments in SDA "mission theology" is Gerard Damsteegt, "The Rise of the Seventhday Adventist Message and Mission (Ph.D. dissertation, Free University of Amsterdam, 1976). Many references Cited below were called to my attention by this excellent study, soon to be published*

*12. Review and Herald, May 6, 1852, pp. 4, 5*

*13. Review and Herald, February 17, 1853, p. 155*

*14. Review and Herald, November 29, 1853, p. 164*

*15. Review and Herald, May 29, 1855, p. 240 16. Review and Herald, September 4, 1856, p. 141*

*17. Review and Herald, February 12, 1857, p. 117 362*

*18. Review and Herald, February 3, 1859, p. 87*

*19. Review and Herald, October 16, 1860, p. 175*

*20. Review and Herald, November 19, 1861, pp. 198, 199; cf. Review and Herald, December 15, 1863, p. 23*

*21. Review and Herald, May 26, 1863, p. 206; June 2, 1863, p. 8*

*22. Review and Herald, June 23, 1853, p. 21*

*23. Review and Herald, June 2, 1863, p. 8*

*24. Review and Herald, July 8, 1873, p. 29*

*25. Review and Herald, March 22, 1870, p. 109; January 25, 1870, p. 37; July 12, 1870, p. 32*

*26. Ella M. Robinson, S.N. Haskell, Man of Action (Washington, D.C.: Review and Herald Publishing Association, 1967), pp. 24-39*

## SURA YA 21
## ALIYEKUWA PADRI WA KIKATOLIKI

"Samahani, kijana, je, unaweza kuniruhusu kuvuka mpaka nikiwa chini ya gari lako la nyasi za ng'ombe?" Mkulima alitazama juu, akamchunguza kwa makini kasisi huyo wa kushangaza, ambaye alikuwa ameomba, akajibu kwa sauti ya chini, "Ndiyo, baba," na kwa uaminifu akaendelea kumficha chini ya gari lake jembamba la kukokotwa na farasi. Kasisi huyo, M. B. Czechowski, alikuwa akikimbia kuokoa maisha yake. Monasteri ya Wafransisko katika Ulaya ya kati ambayo yeye alikuwa mtawa humo, ilikuwa imejihusisha katika siasa za kitaifa kwa namna ya hatari.

Alikuwa karibu kufika mpaka wa kimataifa. Angekuwa salama ikiwa angevuka bila kuonekana na watu. Akiwa haonekani machoni mwa watu, anapokuwa chini ya nyasi kwenye gari la kumi na tisa la msafara mkubwa, Chekowski alirushwa-rushwa kwenye gari hili la nyasi katika mbali uliosalia hadi kwenye kituo cha ukaguzi mpakani na kisha alihisi gari ikisimama ili kusubiri ukaguzi. Akiwa anakodoa macho kwenye ufa ili kumwangalia ofisa wa forodha akifanya kazi yake, alishtuka sana kugundua kwamba mkaguzi huyo mzee alichunguza vilivyo ndani ya kila gari kwa kutumia upanga! Nguvu iliyohusika haikuonekana kumchosha hata kidogo licha ya joto kali la majira ya joto.

Alilichunguza lile gari la kumi na nane kwa nguvu kama alivyokuwa amelichunguza gari la kwanza. Chekowski aliomba kwa Mungu. Kisha, gari alilopanda, ambalo lilikuwa la kumi na tisa liliposogelea nafasi ya ukaguzi, inspekta alijiweka sawa, akamwita dereva, "Je, una chochote cha kusalimisha?" "Naapa sina hata mkate bwana!" mkulima akajibu. "Fanya haraka, basi, hebu vuta hatua," ofisa akaamuru. "Usiweke gari lako likiwa limeegeshwa hapa mpakani siku nzima!" Gari liliposogea mbele, Czechowski aliyekuwa ametokwa na jasho aliweza kutazama nyuma kupitia ufa mwingine. Alimwona mkaguzi akichunguza gari lililofuata kwa nguvu kama hapo awali.[1]

M. B. Chekowski hakika ni mmoja wa wahusika wa kupendeza zaidi katika harakati za umishenari, na labda mmoja wa wahusika-tata katika kisa cha Uadventista. Hata si mara zote watu walikubaliana kuhusiana na jina lake. Je, herufi zake za kwanza "M. B" zinasimamia Michael Belina au Michael Bonaventura? Na mtu hutamkaje "Czechowski"? (Alipendelea jina lake lisomeke "Chahofsky"[2]). Angeweza kusimulia visa kadhaa kama hiki hapo juu. Hata kama yote hayakutokea sawa na alivyowaambia, si vigumu kuelewa baada ya kusoma machache kwa nini, mara baada ya kuamua kurudi Ulaya, alitafuta njia yake ya kufika huko.

Mtumishi huyu alizaliwa Poland mwaka 1818, aliingia katika shirika la utawa la Mtakatifu Francisko akiwa kijana, akidhania kwamba watawa wa kisasa walikuwa wasafi, makapera na wenye kujikana kama Fransisko wa Asisi alivyokuwa. Akiwa amevunjika moyo, na alijaribu kufanya matengenezo kwenye makazi ya watawa, na tokeo lake likawa kwamba alipita kutoka sehemu moja ya kusisimua hadi nyingine. Kwa wakati ufaao alitoa rufaa-binafsi kwa papa huko Rumi, naye akafungwa gerezani kwa mwaka mmoja, kisha akapelekwa uhamishoni Ufaransa kwa miaka mitatu, na akafukuzwa kutoka huko hadi Uswisi.

Huko mnamo 1850 aliachana na kazi ya ukasisi na Ukatoliki na kisha akaoa. Mwaka uliofuata alisafiri kwa meli kuelekea Amerika ya Kaskazini, ambako, baada ya kufanya kazi kwa muda kwa ajili ya Wabaptisti katika nchi ya Canada, aliongoka mwaka 1857 wakati ujumbe wa malaika wa tatu ulipohubiriwa wakati wa mikutano ya makambi huko katika mji wa Findlay, Ohio. Majira ya kuchipua yaliyofuata, kwenye mkutano huko Battle Creek ulioshughulika na wahamiaji nchini wa makabila, nchi na lugha mbalimbali, Chekowski alipewa kufanya kazi ya huduma pamoja na akina ndugu wa Bourdeau miongoni mwa Wamarekani wanaozungumza Kifaransa.

Lilikuwa jambo la kupendeza, kuwa na padre kabisa wa Kikatoliki katika safu ya wainjilisti. Kujitolea kwake hapo awali na bidii yake ya sasa ilitajwa mara kwa mara katika Review, na kudumu kwake katika kuishi maisha ya chini kulileta mwitikio wa ukarimu miongoni mwa ndugu, haswa kutoka kwa Familia ya White. James White,

hata hivyo, ambaye alikuwa na watoto watatu wa kwake mwenyewe, alichanganyikiwa zaidi ni kwa nini Chekowski, ambaye alikuwa na watoto wanne, alikuwa akihitaji mara kwa mara posho nyingi za maisha. Muda si muda, White alikuwa anaandika katika Review kuhusu "ushauri" mzuri wa Chekowski unaohitajika kutoka kwa ndugu zake.[3]

Wakati akiandika ushauri huo Chekowski alihama kaskazini mwa New York, kwa ghafula na bila kushauriana  na ndugu, na kuanzisha misheni ya gharama kubwa lakini isiyo na matunda katika mji wa Brooklyn na New York City, kisha mambo yakawa magumu kwake. Mnamo 1861 James White alikuwa katika ziara ya Majimbo ya Mashariki akijaribu kuandaa mikutano lakini alikumbana na kiwango cha kukatisha tamaa cha upinzani. Hakika Chekowski, ambaye yeye na mke wake walikuwa wamefanya urafiki kwa ukaribu sana, angetii ushauri wake.

Kasisi huyo wa zamani alisisitiza, hata hivyo, kuendelea na mipango yake mwenyewe au kucheza ngoma yake mwenyewe kama ijulikanavyo kwa lugha ya Kiingereza, na kwa hasira, White aliandika katika chapisho la Review kuhusu misheni ya New York: “Tumesitisha kuendelea na shughuli yoyote inayohusiana na kusudi hilo hadi shughuli zetu zote zitakapoweza kukaa chini ya mfumo wetu wa uendeshaji.. ... Acha wengine wanaochagua kwenda mbele, wasukume vita hivyo bila mpangilio na kwa mkanganyiko."[4]  Hii ilikuwa hatua ya mabadiliko kwa Chekowski, alikuwa akimpinga sio  tu James White pekee yake,  bali pia C. O Taylor, A. C na D. T Bourdeau, na wengine, kwani alibaki New York, akihubiri katika lugha kadhaa na kuanza kikundi kidogo cha waumini. 'Lengo la kweli la Chekowski lilikuwa kufanya kazi Ulaya.

Wakati Halmashauri kuu ya kanisa, yaani General Conference ilipoandaliwa mwaka wa 1863, Gazeti la Review liliporipoti shauku yake ya kumtuma Snook huko kama mmishenari, Chekowski alitumaini ndoto yake ingetimia hivi karibuni. Wakati J. N. Loughborough alipokuja Brooklyn majira ya baridi kali yaliyofuata kufanya mikutano ya injili na kupanga kanisa (kanisa la watu kumi na sita), Chekowski alimsihi alitaje jina lake kwa kamati ya utendaji. Loughborough, badala yake, alimsihi asubiri kwa muda.

Miaka mingi baadaye, Loughborough alikumbuka kwamba hakuwa amejisikia huru moyoni kusema kwa uwazi na yule ambaye angekuwa mmishenari. Alikuwa amemwambia kwamba kanisa bado halingeweza kumudu gharama za kumtuma. Alitaka kusema kwamba mtu huyo mwenyewe alikuwa hana subira na ingekuwa si busara kumtuma awe mmishenari.[5] Mapema mwaka wa 1858 Chekowski, alikuwa amemweleza kwa siri Ellen White katika barua kwamba ilikuwa hamu yake kubwa "kutembelea nchi yangu niliyozaliwa, naam,  kuvuka maji mengi, na kuwaambia

wote kuhusu kuja kwa Yesu, na marejeo Yake yenye utukufu, na jinsi inavyowapasa kuzishika Amri za Mungu na Imani ya Yesu."[6]

Kwa upande wake Ellen White alimwandikia Czechowski barua kadhaa kumjibu kwa miaka hiyo. Mnamo 1861 alimwambia kwamba alikuwa ameonyeshwa katika maono kwamba kwa kukataa shauri la wahudumu wenzake alifanya makosa. Alimpongeza mmishenari kama mtu "mwenye dhamiri njema na mwaminifu kabisa mbele za Mungu" - pongezi isiyo ya kawaida kutoka kwa mjumbe wa Bwana—lakini alimkumbusha kwamba alikuwa amewapa ndugu zake sababu ya kufadhaika kwa uamuzi wake mbaya. Alimsihi “asijiwekee mwenyewe alama za kupita kwenye njia” bali angojee maamuzi ya kanisa; na alimwonya haswa asiwaache watu wanaomkana Mungu wazimishe mionjo yake ya kiroho kwa sifa za uongo.[7]

Uongozi ulizingatia ombi lake la kutumwa nje ya nchi na kwa kusita, ulimkatalia mmishenari kwenda kwa wakati huo, wakitumai bado angekua msimamizi mwenye busara ili waweze kumtuma wakati fulani baadaye.[8] Hapo ndipo Chekowski alifanya jambo lile lile ambalo Mama White alikuwa amemwandikia asifanye. Alienda kwenye mkutano wa kambi huko Wilbraham, Massachusetts,[9] uliofanywa na Wakristo wa Advent, akawaambia kuhusu ndoto yake, na akapewa sifa zao nyingi na kuidhinishwa kwa ari kubwa. Wakristo Waadventista walikuwa ni Wafuasi wake wa zamani wa Millers ambao walikataa Sabato na jumbe za Patakatifu lakini walikubali usingizi wa wafu, yaani mtu akifa haendi mbinguni ila anapumzika kaburini akingoja ufufuo, Masihi atakapokuja.

Walikuwa wamejipanga rasmi katika makao makuu yao huko Boston mwaka wa 1860, mwaka uleule ambao Waadventista wa Sabato walipata jina lao rasmi. Miles Grant, ambaye alihariri gazeti la “World's Crisis” (Mgogoro wa Ulimwengu), alikubali Chekowski aombe pesa, na kumpa ruhusa kupitia kurasa za jarida hilo. Tawi kuu la wafuasi wa Miller, lililodai kutoweza kufa kwa nafsi pale mtu akifa, lilikuwa limepanga kuwa Shirika la Milenia la Marekani, ambalo baadaye liliitwa Waadventista wa Kiinjili, katika mwaka 1858.

Mhariri wa Advent Herald pia alifungua gazeti lake kwa kasisi huyo wa zamani. (Yote yalisema, Waadventista wa siku ya kwanza idadi yao katika miaka ya 1860 ilikuwa ni kama mara kumi zaidi ya wanachama wa Waadventista Wasabato.) Hivyo walimuunga mkono Chekowski na wenzake, naye akaandamana na familia yake na Bibi Anna Butler, dada wa George I. Butler ambaye baadaye alikuwa mwenyekiti wa General Konferensi/Halmashauri kuu ya kanisa, na Michael Belina (au Bonaventura) Chekowski alisafiri kwa meli kuelekea Ulaya Mei 14, 1864.

Kwa muda wa miezi kumi na nne alifanya kazi kwa bidii karibu na Torre Pellice katika nchi ya Wawaldensia kwenye Milima ya Alps ya Italia. Huko aliwashawishi

watu kadhaa kwenye kuitunza Sabato, haswa J. D Geymet, Francis Besson, na baadaye kidogo, inaonekana, Bi. Catherine Revel.[10] Mwishowe akakubali upinzani mkubwa na kumchukua pamoja naye John Geymet—na, bila shaka, familia yake na Anna Butler—kisha alihamisha shughuli zake mnamo Septemba 1865 hadi Uswizi. Chekowski na Geymet walizuru nyumba kwa nyumba, wakahubiri katika majumba ya umma, wakachapisha na kuuza vipeperushi  na wakatoa gazeti liitwalo, L'évangile éternel ("Injili ya Milele").

Miaka mitatu baadaye, wakati Chekowski alipoondoka Uswisi kabisa, aliwaacha karibu waumini arobaini waliobatizwa wakiabudu katika makundi kadhaa. Kanisa lao kuu, huko Tramelan, lilipangwa mapema mwaka wa 1867, kanisa la kwanza la Waadventista Wasabato nje ya Amerika Kaskazini. Ili kupata utegemezo wa kifedha kutoka kwa wafadhili wake walio tayari kumfadhili, Chekowski aliwasilisha ripoti za kawaida kwa Adventist Herald na the World's Crisis, ambayo wahariri wake walizidi kumpenda, wakawahimiza wasomaji wao wamuunge mkono, na kupeleka michango yao kwake mara kwa mara.

Kwa kusaidiwa na Uhalisia kwamba Kiingereza kilikuwa lugha ngeni kwao, Chekowski alifaulu kwa miaka mitatu kuwafanya waongofu wake wasijue kuhusu vikundi vyote vya Waadventista nchini Marekani. Lakini siku moja yenye matukio mengi mwishoni mwa mwaka 1867, Albert Vuilleumier, ambaye alijua Kiingereza vya kutosha tu ili aweze kukifafanua kwa kutumia kamusi, aliona kati ya makabrasha ya Chekowski nakala ya Gazeti la Review ya Julai 16. Msisimko ulipokuwa ukiongezeka alisoma kifungu baada ya kifungu hadi akagundua kwamba kulikuwa na Waadventista Washika Sabato huko Amerika Kaskazini pia!

Haraka akapeleka barua—iliyoandikwa kwa lugha ya Kifaransa—kwenda Battle Creek; na baada ya kuchelewa kidogo kwa sababu ya lugha, watu wa Battle Creek walisoma kwa msisimko mkubwa kuhusu Waadventista Washika Sabato katika Uswisi ya mbali. Barua zilitiririka huku na huko, lakini shangwe ya pande zote mbili iliharibiwa na habari kwamba jengo na vifaa ambavyo Chekowski alikuwa amenunua kwa ajili ya kuchapisha L'évangile éternel vilikuwa vimewekwa rehani, tarehe ya mwisho ya kufanya malipo ilikuwa ikikaribia, na yule kasisi wa zamani alikuwa ameenda Italia kufanya kazi ya umishenari. Udhaifu wa Chekowski ulikuwa umejitokeza tena, kwa kuharibu kazi ya Mungu.

Wakati wadai wake walipoahirisha tarehe ya mwisho hadi Januari 1869, Wamarekani waliwaalika Waswizi kuwatumia mwakilishi, na kisha kuanza kutafuta pesa za kuwaokoa. Kulikuwa na masharti. Masharti yalitolewa kwamba katika hali hiyo ikiwa Wamarekani watatoa pesa taslimu, hatimiliki kwa waandishi wa habari isichukuliwe na mtu yeyote binafsi bali na waumini wa Uswizi kwa ujumla. Chekowski alisema Hapana! Na kiwanda na vyombo vya uchapaji vikapotea.[11]

Karibu wakati huo huo mmishenari huyu aliondoka Uswizi kabisa. Alifanya kazi kwa muda mfupi huko Ufaransa, Ujerumani, na Hungary; kisha akaishi Romania, ambako alijitegemeza na kufanya kikundi kingine cha waongofu. Chini ya mazingira yasiyojulikana, alikufa kwa "uchovu" mnamo Februari 23, 1876, huko Vienna, akiwa na umri wa miaka 57. Hatuna shaka juu ya bidii yake ya umishenari. Daima alikuwa maskini, akisafiri umbali wa ajabu kwa miguu. Angalau katika tukio moja, alihenyeka kwa maili nyingi baada ya giza na kuingia kwenye mashamba yenye matope katika mvua kubwa ya majira ya baridi kali.

Wakati mwingine, aliteleza kwenye theluji hadi kwenye ukingo wa genge. Aliamini kuwa Mungu amemwita kwa huduma yake maalum. Wakati mmoja, anaripoti, familia yenye ushawishi nchini Italia ilijiandaa kuhusu kuwasili kwake kupitia ndoto.[12] Ubora wa waongofu wake pia unastahiki. J. D Geymet, Francis Besson, Jonah Jones, na wengine  waliacha yote mara moja na kuwa wafanyakazi wenye ubora kwa kazi kwenye wakati wao wote wa umishenari.

Albert Vuilleumier, mtengenezaji wa saa, aliongeza  bidii maradufu, na hata akiwa mzee, nyakati fulani alikuwa akiwabatiza watu. James Erzberger, ambaye tayari alikuwa mhudumu katika mafunzo, alihamisha uaminifu wake kwa kanisa la Washika Sabato kwa maisha yake yote. Bibi Revel, licha ya upinzani mkali, nyumbani, alibaki mshika Sabato kwa zaidi ya miaka sitini hadi kifo chake akiwa na miaka 99. Bi. Pigueron, mmoja wa wale watatu wa kwanza kubatizwa katika ziwa huko Neuchatel, aliendelea kuwa Mwadventista kwa zaidi ya miaka sabini.

Familia kadhaa za wanandoa wachanga waliobatizwa na Chekowski, kupitia kwao, vizazi vyao bado wanafanya kazi na Waadventista Wasabato hadi leo. Wakati habari zilipoanza kuwa Czechowski alikuwa akihubiri Sabato huko Ulaya, Waadventista mbalimbali waliotunza siku ya kwanza yaani jumapili, wakiwa wamekasirika na kuumbuka sana walimwangusha chini na hawakumtegemeza tena. Waadventista Wasabato, hata hivyo, kwa kueleweka walifurahishwa na kumsifu kama "mtu huyu bora." Waligusia kidogo makosa yake na wakaelekea kujilaumu kwa kutomsaidia kuyashinda.

Kikao cha 1872 cha General conference, kilikubali rasmi "mkono wa Mungu katika kupanda Ukweli nchini Uswizi."[13] Lakini Andrews alipofika Uswizi mwaka wa 1874, aligundua kwamba wengi wa Waadventista wa Uswizi walimkumbuka Czechowski zaidi kwa "maumivu mengi na huzuni."[14] Madeni, kukatishwa tamaa, na Shetani alyekuwa amepanda mbegu za kuvunjwa moyo kwamba walikuwa wamemweka juu kwenye mambo ya uaminifu na kiroho ila…..

Waswisi walikuwa wakishikilia kwa uaminifu Ukweli kuhusu Sabato—lakini pia, walikuwa wakaidi katika kuamini uvumi  wa uzinzi wa kudhaniwa wa Chekowski na

ukengeufu wa mwisho.[15] Ingawa walimkaribisha Andrews kwa mioyo iliyo wazi, hawakuwa katika nafasi ya kuharakisha kazi ili kumsaidia kupata vyombo vipya vya uchapaji na kiwanda cha uchapaji alichohitaji sana,[16] na alikufa bila kukipata. Shauku kuhusu mambo ya Czechowski imeongezeka katika miaka ya hivi karibuni, ikichochewa kwa sehemu na miaka mia moja ya kifo chake.

Familia ya Watu wa Ulaya waaminifu wanajaribu, ikiwa wanaweza, kukanusha uvumi wote wa kusikitisha. "Tuna hazina hii," Paulo aliona juu ya kila mwinjilisti Mkristo, "**Lakini tuna hazina hii katika vyombo vya udongo, ili adhama kuu ya uwezo iwe ya Mungu, wala si kutoka kwetu** 2 Wakorintho 4:7-18."

Ellen White hakusema kwamba Chekowski akienda Ulaya Mungu angemwacha! La! Ni wazi kwamba Mungu alibariki mahubiri ya kasisi huyo ambaye awali alikuwa Mkatoliki. Walakini, bila kumhukumu mtu huyu, sisi tunajaribiwa kufikiria ni makuu mangapi na mema mangapi angeyafanya kama Chekowski angepunguza kiburi chake cha asili na kutafakari na hata kuhusisha maisha yake ya huko nyuma katika mwaka 1858, basi angetengeneza mapungufu yake ya kujisimamia na kujitegemeza na miaka yake katika nyumba ya watawa (ambapo kila hitaji la muda alipewa na shirika lake) na Je, mwisho wake ungekuwaje ikiwa angeheshimu shauri la kirafiki la wenzake na ushauri uliovuviwa wa Ellen White?

Katika kipindi hiki ambacho uinjilisti ulikuwa ukiongezeka kwa kasi, mmishenari huyu angeweza kujijengea haraka sifa thabiti kwa kazi ya umoja yenye ubunifu na timu ya watu walioamini kama yeye. Akiwa anaonekana na wengi na maarufu kama alivyokuwa, huenda angesaidia kwa kiasi kikubwa kubadilisha hali ya kupendelea mfumo wa kanisa katika wakati muhimu sana katika historia ya kanisa lake. Mkutano Mkuu, yaani General Conference ulipofikiria kumtuma B. F, Snook kwenda Ulaya, huenda ungemteua Chekowski badala yake, badala ya kungoja miaka kumi na kumtuma J. N. Andrews nje ya Marekani! Vyombo vyake vya habari huko Ulaya visingeshindwa kuendelea. Mtiririko wa wamishenari ungeweza kuanza miaka kumi mapema kuliko ilivyokuwa. Na kwa wakati ufaao M. B. Chekowski angeweza kumaliza siku za maisha yake kwa kuheshimiwa na kuthaminiwa zaidi pande zote mbili za Atlantiki yaani Marekani na Ulaya, basi huyu alikuwa mmishenari rasmi wa kwanza wa Waadventista Wasabato ng'ambo ya Marekani.

*VIDOKEZO: 1.*

*1. M.B. Czechowski, Thrilling and Instructive Developments: An Experience of Fifteen Years as a Roman Catholic Clergyman and Priest (Boston: Published for the Author, 1862), chap. 10*

*2. Advent Herald, January 3, 1865, p. 62*

*3. For example, in the Review and Herald, December 30, 1858, p. 48. Rajmund lady slow Dabrowski, "M.B. Czechowski, First Adventist Missionary to Europe" (seminar paper, Andrews University, 1972), provides a convenient collection of SDA published sources on Czechowski*

*4. Review and Herald, September 3, 1861, p. 108*

*5. J.N. Loughborough, "Sketches of the Past," no. 128, Pacific Union Recorder, June 20, 1912, pp. 1, 2*

*6. Review and Herald, September 23, 1858, p. 144*

*7. Ellen G. White, letter 3, 1864 379*

*8. Review and Herald, July 8, 1873, p. 29; January 11, 1870, pp. 21, 22*

*9. World's Crisis, July 28, 1869, p. 80*

*10. Mrs. Catherine Revel, a remarkable Christian lady, is sometimes considered to have been M.B. Czechowski's first European convert. (See, for example, J.N. Andrews, Review and Herald, October 14, 1875, p. 116) Czechowski, however, claimed John Geymet and another man as converts as early as January 1865 (World's Crisis, January 31, 1865, p. 78; March 28, 1865, p. 6), while in Review and Herald, May 6,1884, p. 295, G.I. Butler says that Sr. Revel had stood for the Sabbath for eighteen years, taking us back only to 1866 as the year of her conversion; and in a letter to Les signes des temps, December 1877, p. 144, she herself says that she had been in the true church for "ten or eleven years," which, again, indicates 1866 as the year of her conversion*

*11. Review and Herald, July 8, 1873,p. 29*

*12. World's Crisis, January 6, 1869, p. 68; April 22, 1869, p. 22*

*13. Review and Herald, November 30, 1869, p. 380 181; January 11, 1870, pp. 21,22; January 2, 1872, p. 20*

*14. Review and Herald, September 23, 1875, p. 92*

*15. J.N. Andrews, "Address to the Public," December 25, 1879, copy deposited in the Ellen G. White Estate*

*16. J.N. Andrews letter fragment, December 29, 1879, original deposited in the Ellen G. White Estate.*

# SURA YA 22
# FAMILIA YA WAMISHENARI WA NG'AMBO

Katikati ya karne ya kumi na tisa Amerika, ilichukua zaidi nguvu na ujasiri "kutunza Jumamosi badala ya Jumapili," na waongofu ambao walikubali siku ya jumamosi hawakukubaliana juu ya jambo jingine zaidi. Viongozi wao wenyewe waliwatazama kwa upole kama "Kasha la vifungo" vya kuvutia, vya maumbo tofauti tofauti, wenye imani tofauti miongoni mwao kuliko idadi ya vichwa na mapembe ya mnyama yoyote kwenye Biblia[1]

Kusema kwamba kila mshiriki alitembea kwa kasi sawa pamoja na wengine wote katika kujitolea kwa dhati kwa kusudi la kueneza ujumbe wa malaika wa tatu katika ulimwengu wote itakuwa uongo kabisa. Machapisho yalionekana yakirundikana kwenye vyombo vya uchapaji kwa sababu washiriki wengi hawakujali vya kutosha kuyanunua ili kusambaza, hali ambayo hatimaye ilimshawishi James White kwamba kanisa lilikuwa limeenda katika hali ya Laodikia. Na hata baada ya ripoti kuhusu kuanza kwa kazi huko Uswizi, ilichukua muda mrefu kabla ya kanisa kuanza kuchukua jukumu lake nje ya nchi.

Ellen White aliendelea kutoa wito kwa watu kuamka na kuwafikia watu walio nje. Alihimiza, watu wafanye jitihada za kipekee mahali ambapo malaika wa Mungu hufungua njia![2] Msitulie na kustarehe katika makoloni yenu ya Waadventista Wasabato![3] Usitarajie nuru ya Ukweli itakusaidia wewe isipokuwa "unapeleka nuru hiyo kwa wengine"![4] Maneno yake yaliangukia masikioni mwa watu wengi. Vivyo hivyo, habari kutoka Uswizi zilichochea watu kupendezwa na zaidi sana kuwasili kwa James Erzberger.

James alikuwa mwanafunzi wa seminari aliposikia kwa mara ya kwanza kuhusu washika Sabato. Ili kuonyesha chuki yake kwa kile alichokiona kuwa ni ushikaji wao sheria kwa kupitiliza au ushabiki wa sheria (legalism), alijitokeza kwenye mkutano wao wa Sabato huko Uswisi akiwa amevalia mavazi yake ya kazi. Mwishoni mwa 1868 Albert Vuilleumier alimbatiza. Mnamo Juni 1869 alifika kwenye kituo cha reli cha Battle Creek. Akiwa hawezi kuzungumza Kiingereza, aliinua bahasha iliyoandikwa, "J. N. Andrews, Battle Creek, Michigan." Mara Familia ya White wakamkaribisha nyumbani kwao.

Mara moja Willie, kijana wao, na Adeline Howe, mpishi wao, na John Kellogg, daktari wa baadaye, walianza kumpa masomo ya Kiingereza siku nzima. Ndani ya majuma matano kijana Erzberger alitoa hubiri kwa lugha ya Kiingereza. Ndani ya wiki tisa alisimama katika mkutano wa kambi la Ohio akihutubia na kutoa wito wa kupeleka ujumbe wa malaika watatu huko Uswizi wito ambao ulipokelewa kwa

machozi. Kwa mwitikio Waadventista Wasabato walikusanya kile ambacho kimeitwa matoleo au sadaka ya kwanza kwa ajili ya umishenari katika nchi za kigeni ($76.00).[5]

Katika muda wa zaidi ya mwaka mmoja Erzberger aliwekwa wakfu kwa huduma na kuelekea nyumbani kwake Uswisi. Wakati huohuo, kama tulivyoona, “Jumuiya ya Wamishonari ya Waadventista Wasabato” ilikuwa imeundwa kwa Kiingereza nayo ikiitwa a "Missionary Society of Seventh-day Adventists" ili kukusanya pesa kwa kazi ya injili. Gazeti la Review, zaidi ya hayo, mara kwa mara lilibeba habari zilizohusu Utume huko New England, huko kaskazini mwa Marekani, Misheni ya California, na Misheni ya Uswisi. Hata hivyo kuna Ukweli wa kutisha katika tahariri ya mwaka wa 1870: "Inaonekana kwamba Mungu anafungua njia ya ajabu kwa ajili ya kuenea kwa nuru. ... Mungu anatayarisha njia mbele ya watu Wake, hata kwa haraka zaidi kuliko kasi yao ya kujibu."[6] (Msisitizo umetolewa.)

Ademar Vuilleumier, binamu wa Albert, alikuja kuhudhuria shule hapo mjini Battle Creek. Uwepo wake ulifanya mabadiliko muhimu. Lakini wakati Mkutano Mkuu wa 1873 ulipotangaza kuchukua usimamizi wa kazi ya injili huko Uswisi, haukuchukua hatua yoyote kutuma mtu. "Mashamba yote ni meupe na tayari kwa mavuno," James White alisihi kwa nguvu "Lazima tutume watu Ulaya kuanzisha kazi huko. Ndugu katika Uswisi wamekuwa wakipiga simu, na bado wanaomba msaada. Na tunashauri kwamba Mzee J. N. Andrews aachwe ili aandamane na Ndugu Vuilleumier hadi Ulaya msimu huu wa kupukutisha majani."[7] Lakini hata hivyo haitakuwa msimu huu wa masika; Mwaka 1874 ungekuwa bora zaidi. Lakini, tunaposubiri hawa ndugu wafanye maamuzi, tuangalie tena mtu huyu ambaye Mzee White alimpendekeza na ambaye tayari tumekutana naye mara nyingi.

John Nevins Andrews, alizaliwa miaka kumi na tano kabla ya tukio la kukatishwa tamaa kwa Oktoba 1844 katika mji mdogo wa Poland, Maine (ambapo, kwa bahati, dada wawili wa Ellen Harmon walienda kuishi walipoolewa miaka mingi baadaye). Kwa wakati ufaao familia ya Andrews ilihamia Paris, Maine, na ilikubali ujumbe wa Miller, na baada ya Oktoba 22, 1844, waliikaribisha familia ya Stowell nyumbani mwao, ambapo walikuwa wameuza shamba lao kwa kutazamia kurudi kwa Kristo. Ukarimu huu wa wazazi wa John ulikaribisha baraka nyumbani. Kwa namna fulani nakala ya chapisho la T. M. Preble liliingia ndani ya nyumba yao. Hii ilikuwa ni makala ndogo, ya kukumbukwa iliyomwongoza Joseph Bates kwenye Sabato ya siku ya saba.

Marian Stowell mwenye umri wa miaka kumi na tano aliliona gazeti hili na akalichukua ili kujisomea. Akiwa amevutiwa, alimwonyesha Oswald, kaka yake mkubwa. Jumamosi iliyofuata wote wawili waliitunza Sabato—kwa siri kama walivyoweza, yaani, kwa kuwa waliogopa kuifanya waziwazi. Jumatatu iliyofuata,

Marian alimpa John mwenye umri wa miaka kumi na saba chapisho hilo. Alilisoma na kuuliza. "Je, baba yako na mama yako wamesoma hili chapisho?" "Hapana," Marian akajibu, "lakini mimi nimesoma. Je! uko tayari kushika Sabato ya kweli, John?" Wikiendi iliyofuata familia zote mbili, vijana na wazazi pamoja, walishika Sabato yao ya kwanza, wakifanya ibada katika moja ya vyumba vya nyumba yao. Wote walishiriki imani yao na watu wengine, na kwa uhakika, punde si punde familia nyingine saba zilikuwa zikikutana nao.

Mmoja wa wasichana katika kundi, Harriet Stevens, hatimaye akawa mke wa Uriah Smith; mwingine, dada yake Angeline, hatimaye akaolewa na kuwa mke wa J. N. Andrews.[8] Mnamo Septemba 1849 mkutano wa kushangaza ulifanyika kwa waumini walioishi Paris, Maine. Wakina White, Joseph Bates, Stockbridge Howland, na viongozi wengine kadhaa wa awali walihudhuria. Sala ilipotolewa, uso wa Ndugu Howland uling'aa kwa nuru ya mbinguni, Roho alishuka "kama alivyofanya siku ya Pentekoste," na wazazi na watoto, wakiungamiana makosa yao, waliunganishwa katika kuelewana na upendo. Washiriki wa familia ya Andrews walikuwepo. John alifurahishwa sana na ushahidi wa uongozi wa Mungu katika harakati ya Sabato na patakatifu hata akasema kwa bidii, "Ningebadilisha makosa elfu kwa Ukweli mmoja."

Baadaye Ellen White alisema kwamba baraka ya Mungu ilimwagwa katika tukio hili hasa kwa ajili ya kijana John. "Bwana alikuwa akimtoa Ndugu Andrews ili amfae kwa manufaa ya wakati ujao, na alikuwa akimpa uzoefu ambao ungekuwa wa thamani kubwa kwake katika kazi yake ya siku zijazo.[9] Karibu na mwisho wa mwaka uliofuata, James White alitoa kitabu cha kwanza cha Gombo la kwanza, la "The Second Advent Review and Sabbath Herald—Pitio la Ujumbe wa marejeo ya Bwana mara ya pili na Ujumbe wa Sabato;" kichwa cha juu kulikuwa na jina la J. N. Andrews nalo lilionekana waziwazi, kama mjumbe wa kamati ya watu watatu wa taasisi cha uchapishaji, Jambo hili lilionesha namna White alivyoweza kumwamini kijana John.

Ofisi ya uchapishaji haikukaa muda mrefu huko Paris, Maine, au Andrews. Mara moja aliingia shambani kama mhudumu, akishiriki uzoefu na dhabihu za wale "ndugu wasafirio. Baada ya ofisi ya Review kuhamia huko Rochester, alitumia sehemu ya wakati wake huko, ambapo, wasaidizi wengine pia mara nyingi walijikimu kimaisha kwa maharagwe na (mush) ugali mwepesi ambacho kilikuwa chakula duni kwa watu wanaolima mahindi kuliko nchi yoyote duniani, lishe hii pekee bila mbogamboga na matunda haitoshi huku akifanya kazi kupita uwezo pia waliishi kwa mlo uleule huku wakifanya kazi kupita uwezo wao, hali ambayo iliharibu afya ya watu kadhaa na kuchangia kifo cha Annie Smith Mnamo Oktoba 1851.

Wakati ofisi za Review zilipokuwa bado huko Saratoga Springs, John Andrews aliandika akiwa mji wa Cincinnati, "Katikati ya dhiki na mateso nafsi yangu ina furaha katika Mungu. Sikuwahi kuvutiwa zaidi na umuhimu wa kazi ambayo tunajishughulisha nayo, kuliko wakati huu wa sasa. Moyo wangu umefungwa ndani Yake, na katika kazi hii takatifu sana ningependa kutumia vyote kwa furaha kuokoa nafsi zinazoangamia, ambapo sasa ndiyo inaweza kuwa wakati wa taabu ni mfupi, usiku ambao hakuna mtu awezaye kufanya kazi umekaribia, basi, maadamu mchana upo, kwa nini basi tusifanye yale tuwezayo, ili kwa njia na fedha yoyote tuwezayo tupate kuwaokoa baadhi ya watu?[10]

Alimaanisha kila neno aliloandika. Ikiwa kuna chochote kilichoashiria tabia yake, mtu huyu alikuwa tayari kutumiwa na kutumika. Kwa muda mfupi alikaribia sana kutumia kila kitu alichokuwa nacho. Hii ndiyo sababu alirejea kwa muda huko Waukon; ambapo mwaka 1856 alimwoa Angeline. Ellen White alikuwa amesema kwamba Mungu alikuwa akimtayarisha John kwa ajili ya manufaa ya utumishi; na kuwa msaada kwa jambo hilo kwa hakika alithibitika kuwa alikuwa mhubiri, mwanafunzi, mwandishi, msimamizi, pamoja na mmishenari kiongozi.

Mnamo mwaka wa 1855 alithibitisha kwa uthabiti kwamba Sabato huanza wakati wa machweo ya jua na sio wakati wa jua kuchomoza kama Waadventista wachache walivyoshindana, au saa mbili jioni, kama Joseph Bates na wengine wengi walivyosisitiza. Utafiti wake miaka mitatu au minne baadaye ulisababisha zoezi la kutoa mpangokazi. Mnamo mwaka wa 1861 aliandika kazi ya kitaaluma iliyoitwa “History of the Sabbath and the First Day of the Week” (Historia ya Sabato na Siku ya Kwanza ya Juma), ambayo, ilirekebishwa kwa kupitiwa na kuchapishwa tena, ilibaki kuwa kiwango na utaratibu wa Waadventista Wasabato katika uwanja huo hadi kufikia karne ya ishirini (Walawi 32:23).

Ilisemekana kwamba Andrews angeweza kujifunza katika lugha saba, na alidai kuwa alikariri Agano Jipya lote. Andrews alikuwa mshiriki wa kamati ambayo mwaka 1860 ilipiga kura ya jina la "Seventh-day Adventist" na mwaka 1863 iliandaa Kongamano Kuu la kwanza-(General conference). Alihudumu kama mwenyekiti wa tatu wa Kongamano Kuu (1867 hadi 1869), na kwa miaka kadhaa alikuwa mhariri wa nyumba ya uchapaji ya Review and Herald.

Mnamo 1863 alikwenda Washington kuelezea serikali msimamo wa Waadventista kuhusu utumishi wa kijeshi unaohusu rasimu ya jeshi, kutoshika silaha, bali kusaidia majeruhi na huduma za kila siku jeshini (non-combatant position). Haishangazi kwamba Ellen White aliandika juu yake kwa waswisi katika mwaka 1878, "Tulikutumia mtu hodari katika jeshi letu lote"![11] Lakini hiyo ilikuwa muda mrefu baada ya Andrews kufika hapo! Ni wakati sasa wa mwaka 1874, mwaka wa bendera kusimikwa katika historia ya Waadventista.

Mnamo Machi 16, 1874, Jumuiya ya Kielimu ya Waadventista Wasabato ilisajiliwa, katika maandalizi ya kuanzishwa ndani ya mwaka huo, Chuo cha Battle Creek, taasisi ya kwanza ya Waadventista ya elimu ya juu ilihamia Berrien Springs na kuitwa J. N. Andrews university. Mnamo Juni 4, 1874, Signs of the Times ilizinduliwa, ikifungua njia kwa ajili ya kuanzishwa kwa kiwanda cha uchapaji cha Pacific Press mwaka uliofuata. Mnamo Agosti 1874, mkutano wa makambi ya pamoja na Mkutano Mkuu yaani General konferensi ulifanyika huko Michigan, huu ulikuwa mkusanyiko mkubwa zaidi wa watunza Sabato. Mpaka wakati huo, Uriah Smith, tunaweza kusema kuwa aliona kwa usahihi, siku za mbele watu wataweza kukutana popote duniani kwa karne nyingi kabla Yesu hajarudi.

Katika kambi hili na Mkutano Mkuu wa General konferensi James White alisisitiza tena kwa watu kubeba ujumbe wa malaika wa tatu kwa ulimwengu wote. "Misheni yetu ni ya dunia nzima," alisisitiza. Mnamo Jumatano, tarehe ya kwanza ya Aprili ya mwaka huo, ilikuwa siku ya kukumbukwa, wakati Familia ya White walikuwa wakiishi kwa muda huko Oakland, California, Ellen alikuwa amepata maono mashuhuri zaidi. Muda mfupi baadaye aliyaandika, akirekodi maneno aliyoambiwa na Mjumbe wa mbinguni: "Unakaribisha mawazo finyu sana ya kazi kwa wakati huu. Unajaribu kupanga kazi ili uweze kuikumbatia mikononi mwako. ... [Lakini] nyumba yako ni ulimwengu wote."

Alitaja hasa mabara ya Australia, Ulaya, na visiwa vya bahari kama maeneo yanayohitaji juhudi kubwa za kimishenari. Aliwahimiza viongozi kwa sentensi hii muhimu: "Mnapaswa kushikilia Neno la uzima, ili wote wapate fursa ya kupokea Ukweli ikiwa watapenda." Akichukua maneno ya mjumbe wa mbinguni tena, alisihi: "Usipoteze kamwe Ukweli kwamba ujumbe unaohubiri ni ujumbe wa ulimwengu mzima. Unapaswa kutolewa kwenye miji yote, kwenye vijiji vyote."[12] Tofauti na baadhi ya ndugu zake, Ellen White kamwe hakusahau sababu ya kuwepo vuguvugu la Waadventista Wasabato.

Yesu ameingia Patakatifu pa Patakatifu ili kushiriki katika kazi ya kuwaondolea watu Wake dhambi zao milele. Ili kuhimiza utakakaso kamili. Yeye Anasimama karibu na Sanduku la Agano akimwaga duniani utukufu wa utakatifu wa Sabato. Lakini hatakaa huko kwa muda mrefu, na atakapoondoka, kila kesi itakuwa imeamuliwa kwa ushindi au ole. Ujumbe wa Sabato, wa uaminifu na utiifu kwa Mungu unaotegemea uhusiano wetu muhimu na Yesu, lazima uende kwa kila nafsi iliyo hai, ili kila mtu apate nafasi ya kubadili njia zake kabla ya kipimo cha rehema, na kuanza kwa mapigo saba ya mwisho; na shambulio la kikatili la Shetani wakati wa taabu.

Aliandika, "Hakuna hata mmoja anayefanywa kuteseka kwa ghadhabu ya Mungu hadi Ukweli uletwe ndani ya akili yake na dhamiri yake, na kisha kukataliwa .... Kila mtu anapaswa kuwa na mwanga wa kutosha kufanya uamuzi wake kwa akili timamu.

Itakuwa mtihani mkubwa wa uaminifu."[13] Mnamo Agosti 14, 1874, General Konferensi ilijibu mwishowe maombi yake—na yale ya mumewe na Uswisi.

Chini ya turubai inayopeperushwa ya hema la mkutano wa kambi hatua ya kihistoria ilipigiwa kura ambayo ilifungua njia kwa Uadventista rasmi kutoka Amerika Kaskazini kwenda nje ya mipaka ya Amerika: "Imeamuliwa, Kwamba General Konferensi... agizeni Kamati ya Utendaji kumtuma Mzee. J. N. Andrews Uswisi haraka iwezekanavyo." Andrews alikuwa tayari kuondoka na kuanza umishenari. Mnamo Septemba 15, mwezi mmoja baadaye, alisafiri kwa meli kutoka Boston kupitia Liverpool, Uingereza, akielekea Uswizi. Pamoja naye ndani ya Meli ya Cunard, Atlas, walikuwa Ademar Vuilleumier, mkalimani wake wa kwanza wa Kifaransa, na watoto wake waliosalia, Mary, mwenye umri wa miaka kumi na miwili, na Charles, mwenye umri wa miaka kumi na saba.

Andrews alikuwa na umri wa miaka kumi na saba alipokubali kushika Sabato huko Paris, Maine kama ambavyo Amri ya Nne iagizavyo kukumbuka. Angeline, mkewe Andrews alikuwa amefariki Machi 1872. Watoto wake wawili wachanga pia walikuwa wamekufa. James White alitafakari kwa huruma, "Anaacha karibu nusu ya familia yake katika kaburi lenye ukimya." Kutokuwepo kwa mke na mama kungekuwa na matokeo mabaya kwa afya ya familia hii ya kimishenari, lakini Andrews alikuwa amekabili matatizo mengi sana akiwa mmishenari wa nyumbani, na aliona kuwa hakupaswa kuzuiwa kwa kufikiriwa kuwa ni mmishenari mgeni.

Watoto wake, pia, walijisalimisha kwenye mapenzi ya Mungu. Mara tu baada ya kuwasili, Andrews aliingia katika kazi yake. Aliitisha mkutano wa waumini na akapokea makaribisho ya kifalme. Alisafiri pamoja na Erzberger hadi Prussia ili kushirikiana na kundi la washika Sabato wasiokuwa Waadventista huko. Lakini mzigo mkubwa akilini mwake ulikuwa ni kuchapisha jarida la Kifaransa la Signs of the Times, "Les signes des temps." Akijua kwamba Wafaransa hawavutiwi na wageni wanaoharibu sarufi/sintaksi yao, alijitahidi sana kufahamu lugha yao kwa ukamilifu. Hakutaka kizuizi kisicho na maana kati ya ujumbe wake na watu. Mary na Charles walijiunga naye katika hili.

Baada ya miaka miwili walikuwa tayari kuingia katika agano zito, lililoandikwa na kutiwa sahihi ipasavyo, wakiahidi kuzungumza kwenye nyumba yao Kifaransa, pekee. Kijerumani wangeweza kutumia kwa nadra sana, ikiwa wangetaka. Kiingereza lazima kihifadhiwe, yaani wasikizungumze ila wakati wa dharua au dhiki pekee. Nyumba ya watatu hao ilikuwa ya ghorofa katika jiji la Uswizi linalozungumza Kijerumani pale mjini Basel. Hapa Andrews aliifanyia kazi tena "nakala ya Rochester-ofisi ya uchapaji ilikuwa nyumbani," kwa kutumia ghorofa kama ofisi ya uchapishaji na nyumba ya kuishi. Andrews aliandika nakala za chapisho lake kwa bidii, au alizitafsiri kwa usahihi kutoka kwenye Review na kwenye gazeti la

The California Signs. Charles, kwa bidii sana, alifanya uchapaji, Mary, ambaye alijifunza kuzungumza Kifaransa kwa ufasaha, alisaidia kuhariri machapisho. Kurasa zilizochapwa zilibebwa kwenye toroli hadi moja ya nyumba za uchapaji.

Andrews alikuwa amechagua mji wa Basel kutokana na sifa yake ya uchapishaji machapisho vizuri; lakini kwa jicho lake la ukamilifu, wachapishaji wote wazuri hawakuwa waaminifu na wale waaminifu hawakufanya kazi kwa ubora. Wakati fulani alisimamisha mashine ya uchapaji mara hamsini wakati mashine inachapa ili kusahihisha kazi ya uzembe ya mchapaji huyo. Aliomba Battle Creek wamsaidie kuwa na kiwanda chake mwenyewe na watu wa kukiendesha. James White alizindua mpango wa watu kutoa ufadhili wa $10,000 lakini ni fedha kidogo tu ilipatikana wakati huo.

Inaonekana kwamba Andrews hakupewa mshahara wa kawaida lakini alitarajiwa kuchukua gharama zake binafsi kutoka kwa michango ambayo ilitoka mara kwa mara kutoka Marekani. Kwa mtu ambaye alianzisha utaratibu wa kutoa kwa mpango, hii hakika ilikuwa kejeli. Akiwa Mkristo mwangalifu, aliona aibu kuchota senti zaidi ya kile alichoona kuwa muhimu kabisa. Kwa uhalisia, alichukua fedha kidogo kuliko ilivyokuwa ikihitajika. Kwa miezi kadhaa mwaka mmoja yeye na watoto wake hawakula chakula zaidi ya mkate, viazi, ugali mwepesi (mush), zabibu chache zilizokuwa kwenye msimu na mara kwa mara matunda mengine. Kama ilivyokuwa kule Rochester alikuwa makini sana katika mambo mengine pia.

Kufikia 1878, wakati Maude Sisley na akina William Ingses walipokuja kuwasaidia, Bibi Ings alianza kushuku kwamba mambo hayakuwa sawa kwa Mary. Taarifa ya kutisha ilifika Marekani kwamba familia za wamishenari huko Uswis ziliogopa "matumizi" yaliyokuwa yanawakabili. Andrews alialikwa kwenye Mkutano Mkuu wa 1878. Aliuliza kama angeweza kumleta Mary pamoja naye - na akaahidi atamlipia nauli. Bado alikuwa amebakiza fedha kidogo katika zile alizopata alipouza nyumba yake kabla ya kuondoka.

Hii ilikuwa ni safari ya mwisho ya Mary. Hata kijana aliyekuwa tabibu mahiri Dk. Kellogg hakuweza kuwapa tumaini lolote kuhusiana na afya zao kuwa njema. Mary alimkumbuka (alimmiss) mama yake na akamwomba baba yake aketi naye. Dk. Kellogg alimwonya juu ya matunda yanayoweza kupatikana; lakini Mariamu alikuwa amekwenda Ulaya kwa hiari bila mama na akasimama karibu naye kama mhimili, na hakutaka kumwangusha. Kabla ya mwaka kuisha, alifariki akiwa na umri wa miaka kumi na saba (kwa kifua kikuu). Andrews, ambaye afya yake ilidhoofika polepole pale mke wake alipokufa mnamo 1872, hakuwahi kufarijika kutokana na kifo cha binti yake. "Ninaonekana kumshikilia Mungu kwa mkono uliokufa ganzi," alishusha pumzi muda mfupi baadaye.

Mungu alimpenda katika upweke wake. Alimpa Ellen White ujumbe kwa ajili yake—kwamba Angeline, Mary, na watoto wawili waliolala usingizi wa mauti, walikuwa salama katika Yesu na wangefufuka ili waishi tena siku ya ufufuo wakati Masihi akija.[14] Majira ya joto yaliyofuata Andrews aligeuza hatua zake kwa hiari. Charles alifurahi kumwona! Walibuni njia mpya za kuvutia umakini wa umma, na usambazaji wa gazeti la Les signes ulipanda kutoka mia tano hadi elfu tano. Hata bila uwepo wa Mary alikuwa na wafanyakazi 12 sasa, na walikuwa wakitumia chumba chenye jua (sunroom), chenye vifaa vya uchapaji vyakutosha.

Walikuwa wakisambaza machapisho ya Kijerumani (kwa ajili ya Erzberger) na Kiitaliano, na pia katika Kifaransa. Les signes ilikuwa inaenda kuhutubia katika wilaya hamsini kati ya sitini na mbili za Ufaransa, na karibu nchi zote za Ulaya: Sweden, Austria, Hungary, Prussia, Saxony, Alsace, Belgium, Holland, England, Wales. Scotland, Italia, Sicily, na Uhispania—bila kutaja Uswizi, bila shaka, na pia Urusi, India, Misri, na Amerika Kaskazini na Kusini.[15]

Andrews alisafiri hadi Italia, Ujerumani, Uingereza, na Ufaransa, lakini karatasi pekee zilimpa jasho wa kutumia nguvu zake. Alianza kuona dalili za Mary zikijitokeza ndani yake, moja baada ya nyingine. Hali yake ilipozidi kuwa mbaya, Baraza Kuu yaani General Conference lilitangaza siku ya maombi ili kumwombea. J. N. Loughborough, mwongofu wake kutoka siku za Rochester, aliondoka Uingereza (ambako alikuwa akifanya uinjilisti) na kwenda kumpaka mafuta.

Andrews alijitolea kwa muda, lakini mwisho haukuwa mbali. Katika kiangazi cha 1883 mama yake mzee aliwasili kutoka Waukon akiandamana na Mzee B. L. Whitney, ambaye alikuwa ameteuliwa na ndugu "kumsaidia katika udhaifu wake." Akili ya Andrews ilibaki wazi na roho yake ikiwa na matumaini katika Bwana. Andrews alilala kitandani, kama mifupa hai, akiwaamuru wasaidizi wake wa karibu hadi mwisho kuhusu kuendelea na kazi ya uchapaji.

Aliaga dunia machweo ya Jumapili, Oktoba 21 1883, akiwa na umri wa miaka 54. Ukiwa amesimama kwenye kaburi lake kwenye Makaburi ya Wolf Cemetery nje ya Basel, mtu anaweza karibu kusikia sauti yake ikirudia maneno yake mwenyewe: "Nafsi zinaangamia, nani ambaye sasa anaweza kufikiwa na injili. Wakati wa taabu kuu uko karibu, usiku umekaribia ambao hakuna mtu awezaye kufanya kazi tena, je, tunaweza kuokoa baadhi ya watu?"

*VIDOKEZO:*

*1. S.N. Haskell to W.W. Prescott, August 23, 1907, in Robinson, S.N. Haskell, p. 26 2. Ellen G. White, Testimonies, vol. 1, pp. 147- 149*

*3. Ibid., vol. 2, pp. 113-116; 631-636; 669*

*4. Ibid., p. 123*

*5. Review and Herald, August 12, 1937, pp, 4, 5*

*6. Review and Herald, March 22, 1870, p. 108*

*7. Review and Herald, August 26, 1873, p. 84*

*8. Biographical data about Andrews are based primarily on correspondence deposited in the 401 Ellen G. White Estate. See also Mrs. Marian C. Stowell Crawford, General Conference Bulletin, 1901, p. 116, and Watchman, April 25, 1905, p. 278, for the story of Andrews's conversion to the Sabbath. See also Everett N. Dick, Founders of the Message (Washington, D.C.: Review and Herald Publishing Association, 1938), pp. 299-333*

*9. Ellen G. White, Life Sketches, p. 127; Spiritual Gifts, vol. 2, pp. 116, 117*

*10. Review and Herald, November 25, 1851, p. 54*

*11. Ellen G, White, letter 2, 1878 12. Ellen G. White, Life Sketches, pp. 208-215; Testimonies, vol. 7, pp. 34-36*

*13. Ellen G. White, The Great Controversy, p. 605*

*14. Ellen G. White, Letter A-71, 1878, in In Heavenly Places (Washington, D.C.: Review and Herald Publishing Association, 1967), p. 272*

*15. Review and Herald, May 20, 1880, p. 332*

## SURA YA 23
## HARAKATI ZA UTUME ULIMWENGUNI

Baada ya kifo cha Mzee Andrews, hakuna tanzia ya sifa na heshima iliyoandikwa katika gazeti la Review. Hivi ndivyo alivyotaka; na wahariri wa jarida hilo walitii takwa lake hilo bila kupenda. Lakini hotuba kubwa za sifa za Mzee Andrews hata hivyo zimeandikwa. Wamishenari na familia za wamishenari ambao wameacha nyumba zao katika mkondo unaotiririka daima kumtumikia Bwana katika mazingira ya hali isiyojulikana nao wamemfanyia Mungu heshima kuu ya kufuata kule alikoongoza. Hapa kunaweza kuwa na tofauti kubwa ya ubora kati ya utumishi wake Andrews wa umishenari na ule wa M. B. Czechowski. Kwa sababu Andrews aliondoka nchini kwa makubaliano na kwa agizo la waumini wenzake, Waumini wote kwa njia fulani walienda pamoja naye, na kwa muda mfupi kanisa kwa ujumla lilijiona kuwa katika harakati ya wamishenari wa ulimwengu.

Sio kwamba lilielewa wazo kikamilifu wakati wa mwanzo na Sio kwamba linafanya hivyo bado. Lakini mara moja lilianza kuchukua jukumu lake la kupeleka ujumbe ulimwenguni kote kwa umakini. Mwaka uliofuata kanisa lilimpigia kura James White wa Battle Creek, John Loughborough wa California, na John Andrews wa Uswisi kama kamati yake kuu ya watu watatu, ambayo pia ilikuwa bodi yake ya wamishenari. Mpangilio huu ulionekana "unafaa sana" kwa mhariri Uriah Smith, na alisema, "ujumbe ambao Waadventista wa Sabato wanatoa ni ujumbe kwa dunia nzima."[1]

Baada ya kumtaja Czechowski tena na mapungufu yake, inaweza kuwa haki kusema hata Andrews alikuwa ni chombo cha udongo tu, Inaonekana kwamba hakuhitaji kufa mapema hivyo. Ellen White kama mjumbe wa Bwana alimshauri mara kwa mara kutofanya kazi kupita kiasi, na badala yake atunze afya yake vizuri zaidi. Andrews aliahidi kujaribu, kisha akahalalisha kazi yake iliyopindukia kwa kusema kwamba kufanikiwa kwa kusudi hili la ujumbe wa injili, kulihitaji yeye kufanya kazi kwa bidii.

Tukitazama  nyuma ni rahisi sana kumhurumia lakini si rahisi sana kukubali uamuzi wake. Karibu na mwisho wa maisha yake, alikiri kwa kutubu kwamba alikuwa amefanya makosa.[2]  Lakini Mungu akambariki kwa jinsi ya ajabu. Naye alitumia roho yake yenye nguvu ya maamuzi na isiyo na woga ili kuvutia maelfu ya vyombo vingine vya udongo kutumika kwa bidii katika sehemu za mbali. Sadaka ya Mary binti yake pia ilikuwa na mvuto wenye nguvu. Mazishi yake yaliita mkutano mkubwa zaidi kufikia tarehe hiyo kwenye historia ya Battle Creek na, pamoja na wito mzito wa baba yake kwa vijana katika hafla hiyo, vijana wengi wa kiume na wa kike waliohudhuria Chuo cha Battle Creek walivutiwa kuiga kujitoa wakfu kwake.[3]

Kuishi katika enzi hii ya safari za ndege, ni vigumu leo kufikiria kwamba muda mfupi kabla ya kuondoka kwa familia ya Andrews kwenda Ulaya, mwenyekiti wa Jimbo Kuu yaani General konferensi, George I. Butler alikuwa ametolea udhuru kusita kwa umishenari kwa upande wa vijana wengine kwa kutamka kwamba "vijana wetu wangeangalia shughuli kama hiyo kwa hofu kubwa."[4] Miaka kumi baadaye, wakati Butler alipokuwa tena ofisini kama mwenyekiti wa General Konferensi, alikuwa ameshinda woga wake na kufanya safari ya Ulaya yeye mwenyewe, ambapo alisaidia kuanzisha mashirika ya uchapishaji nchini Uswizi, Norway, na Uingereza, na kuboresha usimamizi wa kazi nzima huko. Huo ulikuwa mwaka uliofuata, baada kifo cha J. N. Andrews.

Kufikia wakati huo kulikuwa na Waadventista Wasabato elfu Ulaya, na wamishenari walikuwa wakifanya kazi sio katika nchi ya Italia, Ufaransa, na Uswisi tu (nchi ambako Andrews na Chekowski walikuwa waanzilishi wa kazi -pioneers), bali pia katika nchi ya Denmark, Norway, na Sweden, ambako akina John Mattesons na wengine walikuwa wakifanya kazi ya umishenari, na huko Uingereza, chini ya William Ingses na John Loughboroughs na wengine.

Mnamo mwaka wa 1882, Stephen Haskell aliyejulikana kwa umaarufu wa kutoa machapisho na utume alisaidia kuitisha Baraza la kwanza la Ulaya la Misheni za Waadventista Wasabato (hapo awali, ikijulikana kama Konferensi ya Ulaya) huko Basel, baraza lililokuwa na uwakilishi kutoka maeneo ya Uingereza, Skandinavia, na Ulaya ya Kati. Kusimulia kisa cha Uadventista katika kila nchi mpya kungehitaji vitabu vingi. Takriban kila nchi ilikuwa na "Joseph Bates" wake mwenyewe, aliyejitoa hadi kubakia na shilingi ya York, lakini akisonga mbele dhidi ya upinzani wa wazi au  wa hila kupitia milango Mungu aliyoifungua mbele yake.[5] (York shilling senti 12 za NY)

Kama Andrews, John G. Matteson alifuata mtindo wa Rochester katika huduma yake hadi Skandinavia. Alikuwa amejifunza jambo fulani kuhusu uchapaji huko Amerika. Waongofu wake huko walipoomba machapisho kwa lugha ya Kidenmaki na ofisi ya Review ikawakatisha tamaa, alikuwa amechangisha dola 1000 kutoka kwa

Wadenmark na Watu wachache wa Norway, ndipo akapanda gari-moshi hadi Battle Creek, na akajifunza jinsi ya kukiweka kitabu kwenye mitambo ili kichapwe (typeset), kuandika makala, na kuitayarisha mwenyewe.

Huko Norway aliweka kiwanda cha uchapaji katika jengo ambalo familia yake iliishi. Bila kufahamu malighafi za mahali alipoishi alichanganya wino na kuweka kwenye karatasi tofauti, kwa kutooanisha wino na karatasi katika toleo lake la kwanza na nakala zake za karatasi zilichelewa kukauka. Kwa msaada wa familia yake alitundika kurasa hizo kwenye kamba za kuanikia nguo kwa wiki moja. Lakini usumbufu mdogo haukumzuia Matteson na washirika wake kuweka msingi thabiti wa Uadventista huko Skandinavia.

Miongoni mwa Waadventista wa kwanza wa Siku ya Sabato nchini Urusi walikuwa Romualdo Bartola,[6] msafiri mfanyabiashara wa Kiitaliano, na Gerhard Perk, Mmennonite wa zamani. Aidha Andrews au Chekowski walikuwa ndiyo msaada katika kumwongoa Bartola; ndugu za wale wanaozungumza Kijerumani huko Amerika walikuwa wametuma machapisho kwa marafiki wa mji wa Perk wanaozungumza Kijerumani, ambao walikuwa wameyatazama machapisho kidogo tu na kuwaonya wakisema, "Haya maandishi ni hatari sana, yanaweza kumdanganya hata Mmennonite."

Roho ya udadisi aliyokuwa nayo Perk ilishinda. Akiwa amejificha kwenye nyasi, Perk alisoma nakala ya Ujumbe wa Malaika wa Tatu, akakubali ujumbe wake, na kutuma maombi Battle Creek, ili kupata maelezo na machapisho zaidi. Mtu aliyefanya kazi Ujerumani wakati wa wongofu wa Perk alikuwa L. R. Conradi, kijana Mjerumani ambaye alikuwa amehamia Marekani, huyu alikubali Sabato alipokuwa akikata kuni huko Iowa, alivunja rekodi ya kuhitimu muda mfupi huko Chuo cha Battle Creek, na kwa haraka akaonyesha kipaji cha kushangaza kwa kuongoa idadi kubwa ya wahamiaji wengine walioingia Marekani (Huyu ndiye aliwatuma wale wamishenari wa kwanza Tanzania, wakina Enns).

Ofisi kuu ya kanisa yaani General Konferensi walimwomba arudi Ulaya kumsaidia Mzee Erzberger. Akiwa amevutiwa na mawasiliano ya Perk, Conradi alipanda gari-moshi hadi Urusi na kufanya kazi kubwa huko pamoja na Perk, wakawatafuta watunza Sabato wakiwangoja katika sehemu nyingi, wakiwabatiza, na katika matukio mengi, walitupwa gerezani (pamoja na Perk). Kwa miongo kadhaa baadaye Conradi akawa kiongozi wa Waadventista katika Ulaya ya kati na mmishenari wa ulimwengu katika Ukweli kabisa, akiendesha misheni ya uinjilisti katika Afrika na Amerika Kusini na pia Ujerumani, na kuandika idadi ya vitabu muhimu.

Mwadventista wa kwanza wa Sabato nchini Uturuki anaonekana kuwa Theodore Anthony, Mturuki ambaye, kama Conradi, aliondoka mahali alipozaliwa na kuikubali

Sabato huko Amerika. Alikuwa akitengeneza viatu huko San Jose, California, wakati Roho wa Mungu alipomwita arudi nyumbani kwake. Hong Kong ikawa shamba la misheni ya Waadventista chini ya hali ambazo zimekuwa mashuhuri na kujulikana.

Abram LaRue, wakati fulani akiwa baharia na mchungaji wa wanyama, na kisha mkata magogo ya miti huko Sonoma, California, alimsikia John Loughborough akihubiri ujumbe wa malaika wa tatu wakati wa siku za mwanzo za Uadventista huko Golden West. Akiwa ameelemewa na  mzigo wa mahitaji ya kiroho ya China, aliwasihi ndugu wamruhusu afanye kazi kati ya mamilioni ya nchi hiyo kubwa. Hakuuliza ujira; Bali kibali pekee. Lakini uongozi ulikataa kwa  kigezo cha umri wake. Alikuwa na umri wa miaka sitini. Akiwa ameshindwa lakini  hakuwa na woga wala kukata tamaa, alipata sehemu mbadala kwa ajili ya kazi ya injili katika "moja ya visiwa vya Pasifiki."

Kwa sababu hapo awali alikuwa akiishi Hawaii, ilidhaniwa kuwa angeenda huko; Naye alifanya uinjilisti wa vitabu huko Honolulu kwa muda, alitokea kupendwa sana na ujumbe wake kupokelewa kiasi kwamba mwinjilisti William Healey alitumwa kuvuna mavuno yake. Kisha akasogea kimya kimya mahali ambapo moyo wake ulikuwa ukimwita sana, hadi Hong Kong, kisiwa cha China cha Pasifiki.

Afrika, bara ambalo wengi hulifikiria kwanza mtu anaposema anaenda kuwa "mmishenari," lilikaribisha Waadventista wa kwanza kabisa mwaka 1863! Bibi Hannah More, alipokuwa akizuru Connecticut, alipokea kutoka kwa Stephen Haskell nakala kati ya mambo mengine ya kazi mpya ya John Andrews, History of the Sabbat —Historia ya Sabato. Aliporudi Liberia akiwa mmishonari wa madhehebu mengine, alisoma kila kitu kwa uangalifu, na pia machapisho mengine yote ambayo Haskell alihakikisha kwamba alipokea kupitia barua.

Akiwa Mkristo wa dhati aliyeshika jumapili, mwanzoni aliona vigumu kufanya badiliko la kutunza Sabato, lakini kufikia wakati alipoandika barua yake ya kwanza iliyochapishwa katika gazeti la Review, Januari 2, 1864, tayari alikuwa amehusika kumwongoa mmishenari mwingine Mwaustralia kwa ujumbe wa malaika wa tatu, Alexander Dickson. Lo, aliwahakikishia wasomaji wa Review kwamba, wako watu wamekuwa "Waadventista Wasabato" kwa moyo wote huko Afrika!

Ni wakati wa kiangazi hapa, aliendelea (mnamo Januari): "Ndege wanaimba, vyura wanachungulia, wadudu wanavuma na maua yanachanua, na uumbaji wote vinatabasamu. Mwanadamu peke yake ni mwovu. Lo ni huruma iliyoje kwamba mwanadamu mwovu anapaswa kustahimili wakati viumbe vyote vikiimba. "[7] Ni huruma iliyoje, pia, kueleza mwisho wa kusikitisha wa mwanamke huyu wa kuvutia. Jumuiya yake mwenyewe ya wamishenari, ilipogundua imani yake mpya, ilimfariji.

Lakini bila kuvunjika moyo hata kidogo, alitembelea vituo vingine vya misheni kwenye pwani ya magharibi ya Afrika na kuacha machapisho kwa kila kimoja.

Aliporudi Marekani, Hannah More alibatizwa huko Lancaster Kusini, Massachusetts, na akaendelea kusambaza vitabu, ambavyo baadhi yake vilizaa matunda, alipokuwa akienda Battle Creek.[8] Huko Battle Creek, hata hivyo, alikuta mawazo ya waumini yakiwa yameegemea mambo ya kidunia. Familia ya White walikuwa mbali safarini.

Dada More, akiwa na upungufu wa fedha, alitafuta kazi kati ya watu ambao hawakujali. Kwa kuwa walichelewa sana kumkaribisha kwenye nyumba zao hapo Battle Creek, alikaribishwa kuishi pamoja na mmishenari mwingine wa imani yake ya zamani kwenye rasi ya Michigan na akaaga dunia huko, hata kabla ya wakati wake, akiwa amechanganyikiwa na kukosa ukarimu wa Wasabato huko Battle Creek, lakini akiwa Mwadventista Msabato mwaminifu.

Aliposikia tukio hili la uchungu, Dada White alilikemea kanisa huko Battle Creek kama nabii wa kweli, si kwa kuwa lilikuwa baya zaidi kuliko makanisa mengine bali kwa kutokuwa bora zaidi ukilinganisha na nuru waliyonayo. Watu hawa wameshindwa kumkaribisha malaika bila kujua, aliandika (Ebrania 13:2).[9] Pengine Hannah More, mmishenari katika Afrika, akishiriki imani yake katika Kristo juu ya Sabato na Patakatifu mwaka 1863, anapaswa kuheshimiwa kama mmishenari wa kwanza wa Waadventista Wasabato ng'ambo. Kwa nini isiwe hivyo?

Nuru ya "Ukweli wa sasa" iliwashwa tena katika Bara la Afrika na Romualdo Bartoli, ambaye tulikutana naye muda mfupi uliopita huko Urusi na ambaye alianzisha kundi la waumini - na kuwabatiza - wakati wa safari ya biashara yake huko Alexandria. Kisha nuru ikabebwa na Dr. H.P. Ribton, daktari wa Kiingereza aliyekubali Sabato kutoka kwa mmishenari wa Kiamerika, Andrews, wakati alipokuwa akiishi katika jiji la Italia la Naples, na kuelekea Misri mwaka 1878 kwa ajili ya afya ya binti yake. Baada ya kufanya kazi nzuri, Ribton aliuawa pamoja na walinzi wake wawili wa kisabato mwaka 1882 wakati wa ghasia dhidi ya wageni ilipoibuka mjini.

Afrika Kusini inaweza kusimulia kuhusu William Hunt, mchimba madini ambaye alibeba nuru ya Sabato pamoja naye kutoka kwenye mashamba ya dhahabu ya Nevada hadi kwenye uchimbaji wa almasi wa Kimberly. Kama LaRue, naye alikubali Sabato wakati Loughborough alipokuwa akifungua kazi kaskazini mwa California; na, kama LaRue pia, alimtumikia Bwana kwa gharama yake mwenyewe. Wakati huo huo, nchini Afrika Kusini, Peter Wessels na G. J. Van Druten, wakulima wa Kiafrika, walikuwa wakijifunza kuhusu Sabato peke yao.

Wessels, mshiriki mshikamanifu wa kanisa la Dutch Reformed, alihangaikia sana kukamua ng’ombe wake siku ya Jumapili kiasi kwamba akamfanya jirani yake, Van

Druten, ajifunze naye swali la Sabato katika Biblia. Punde watu wote wawili walikuwa wakiishika siku ya saba, bila kuwajua washika Sabato wengine wowote ulimwenguni. Kwa muda waliwasiliana na William Hunt (ama kwa njia ya maandishi au kwa kukutana kwa "bahati nasibu" katika uwanja wa almasi - maelezo hutofautiana), na kupitia Hunt Waafrika hao wawili kwa furaha yao waligundua madhehebu ya Waadventista Wasabato.

Washiriki wengine wa familia ya Wessels mbali na Peter pia wakawa Waadventista Wasabato. Ukarimu wao, uliotokana na uuzaji wa shamba lenye almasi, uliandika sura katika kisa cha Uadventista sio tu barani Afrika bali pia huko Australia na hata huko Chicago, ambapo walimsaidia Dk. Kellogg kufadhili huduma yake kwa maskini wa mijini. Kufikia sasa, kazi ya injili katika Afrika hususan Misri, Liberia, na Kusini ilikuwa imefanywa hasa na wahamiaji walio Wakristo na vizazi vyao na watu wengine wasio weusi. Mfanyakazi wa kwanza aliyejitolea haswa kwa weusi Waafrika wasio Wakristo alikuwa George James, mpiga fidla Mwingereza ambaye alikuja kuwa Mwadventista Msabato huko Amerika.

Mapema miaka ya 1890, alipojitolea mwenyewe kwa utumishi wa umishenari, Halmashauri ya Misheni ya Kigeni ya Konferensi Kuu (ambayo ilikuwa imechukua nafasi ya kamati tendaji katika wadhifa huu) ilikataa kumtuma kwa msingi wa ukosefu wa fedha za kutosha. Mara moja, James aliuza kila kitu alichokuwa nacho isipokuwa fidla yake na nguo zake na kujilipia pesa ili kwenda kutekeleza utume. Kwa miaka miwili katikati ya bara la giza alivutia wenyeji kwa kucheza "fidla yake ambayo ingeweza kuimba wakiliita boksi linaloimba."

Moyo wake ulichangamka aliposikia kwamba dhehebu lilikuwa limezindua kituo cha misheni cha kawaida huko Solusi, na akaondoka kwa furaha kwenda kuwasalimia ndugu zake huko. Lakini akiwa njiani kuelekea Solusi ndani ya meli ndogo ya mto alikufa kwa ugonjwa wa malaria, na akazikwa katika kaburi la upweke, na lisilojulikana kando ya mto.

Mnamo 1894, mwaka ambao, kwenye ardhi iliyoidhinishwa na Cecil Rhodes, Waadventista Wasabato walifungua kituo chao cha kwanza cha misheni kati ya watu wasio Wakristo (Matebeles).[10] Miaka ishirini baadae 1874, Karibu nusu karne baada ya 1844 walifungua kituo cha pili kwa watu wasio Wakristo (Wahindu) huko Calcutta India. Mapungufu ya kitabu hiki yanatuzuia sisi kusema mengi juu ya asili ya Uadventista katika sehemu nyingi, hata huko Australia, kile kisiwa kikubwa zaidi ya visiwa vyote na bara dogo zaidi kati ya mabara yote, ambayo Alexander Dickson aliupeleka ujumbe huu wa kutia joto moyo kutoka moyoni mwa Hannah More, na kuuhubiri katika miaka ya 1860, lakini alikata tamaa na matokeo yake akaacha kuhubiri.

Mnamo 1886, S. N. Haskell aliyesafiri kila mahali pamoja na familia yake na kikundi kizuri cha waumini pamoja na familia zao na, wakiwa na mashine ya uchapishaji, walipata ujumbe na kuhamia huko Australia. Kuanzia 1891 hadi 1900 Ellen White alifanya kazi huko mwenyewe, Lakini tuangalie tena katika bara la Afrika kwa muda. Karibu wakati huo huo ambapo George James alienda huko peke yake, General Konferensi ilimwomba Mzee Lawrence Chadwick kuchunguza uwezo wa umishenari wa pwani ya magharibi. Meli yake iliposogea hadi kufika  kwenye bandari ndogo ya Apam, Gold Coast (sasa inaitwa nchi ya Ghana), alikaribishwa kwa shauku na watu takribani 36 mpaka 48, ambao walikuwa  Waadventista Wasabato!

Hakika, kiongozi wao, Francis Dolphijn, mzaliwa wa kabila la Fanti, alitoka nje hadi kwenye meli ili kukutana naye na akaruka juu ya ngazi ya kamba safu kadhaa wakati akipiga kelele kwa sauti ya juu, "Je, Mzee Chadwick yuko hapa?" Chadwick pia alikuwa amepata makundi mengine ya waongofu yakimngoja, moja huko Sierra Leone likiongozwa na Mchungaji Coker, na lingine huko Liberia, likiongozwa na Bw. Gaston. Inaonekana kwamba Dolphijn na Coker walikuwa wamejisomea wenyewe nuru ya Kweli kupitia machapisho yaliyosafirishwa na washiriki wa “Tract and Missionary Society” huko USA. Gaston alikuwa amesikia Neno kwenye safari ya Afrika Kusini na akarudi kuwaambia watu wake.[11]

Tulirejelea Afrika kama njia moja tu ya kutilia maanani, tena, kwa kazi ya walei katika juhudi ya kimishenari ya Waadventista Wasabato. Dolphijn na Gaston hawakuwa wahudumu, lakini walishiriki imani yao kwa matokeo kabla ya kukutana na mmishenari aliyewekwa wakfu. Ribton, LaRue, Anthony, Bartoli, Hunt, wote waliondoka nyumbani na kuwa wamishonari katika nchi za kigeni bila kuwekewa mikono ya uchungaji—au hata kulipwa!

Ni jambo la kustaajabisha, lenye  Ukweli sahili, kwamba watu wengi walivutwa kwa Kristo wa Sabato na Patakatifu huko Amerika na ulimwenguni kote wamevutwa kabisa au kwa sehemu kupitia kufikiwa na wamishenari, nyumbani au nje ya nchi, na watu ambao hawajawekwa wakfu, walei wa Kikristo wenye dhati na bidii. Hii inatukumbusha kutoa heshima kwa aina hiyo maalum ya wahudumu walei au wainjilisti wa vitabu wa Kikristo, walioitwa kwa heshima kwa karne nyingi, wakijulikana kama "kolpota au canvassers"

Katika nchi nyingi, wainjilisti walikuwa mstari wa mbele. Nchini Chile, kwa mfano, waumini wa kwanza kabisa nchini Chile walikuwa wahamiaji wanaozungumza Kifaransa ambao walikuwa wameikubali Sabato baada ya kusoma Les signes des temps nchini Algeria! Lakini “watendakazi” wa kwanza (1894) walikuwa Claire Nowlen, kolpota kutoka Argentina, na Frederick Bishop na Thomas Davis, makolpota kutoka California. Bishop na Davis walisafiri kwa meli kupitia  daraja la Golden Gates.California wakiwa na vitu vichache sana zaidi ya nguo miilini mwao na baadhi

ya vitabu kwenye sanduku. Hawakujua Kihispania na hawakubeba pesa taslimu; lakini miongoni mwa waongofu wao walikuwapo ndugu wa wanaofurahisha moyo, nao ni Thomann, Edward na Victor, ambao Mungu aliwatambulisha kwao kwa ndoto.

Edward na Victor wakawa makolpota, wakivumilia nyakati za ufukara sana kwa muda kiasi kwamba waliishiwa pesa hadi kubaki na jozi moja tu ya viatu kati yao. Lakini walivaa viatu hivyo kwa zamu huku mmoja akibaki nyumbani kusali wakati mwingine alipovaa viatu kwenda kushuhudia. Baadaye Edward akawa kiongozi katika nchi yake mwenyewe, na wote wawili walitumika kama wamishenari. Ikiwa Claire Nowlen aliondoka Argentina kwenda Chile mnamo 1894, basi Argentina ilikuwa "makao makuu ya wamishenari wa kigeni ambao walikuwa Waadventista Wasabato" mnamo 1894! Hakika.

Italia ilikuwa imekuwa makao yasiyo rasmi ya Waadventista Wasabato mwaka wa 1865, wakati Chekowski alipomshawishi Geymet kuandamana naye kama mmishenari wa kigeni kwenda Uswizi. Chini ya Czechowski, Uswizi ikawa kituo rasmi cha makao makuu ya kazi ‘homebase’ cha Erzberger na Albert Vuilleuimier kwa kazi zao huko Ujerumani na Ufaransa. Ikawa makao makuu rasmi ya utumishi wakati B.L. Whitney na G. I. Butler walipopanga Konferensi ya Uswizi mwaka 1884.

Katika miaka ya 1890 Ellen White alitabiri kwamba Australia, pia, ingekuwa kitovu cha misheni za kigeni.[12] Ilikuwa kama sehemu ya kutekeleza utabiri huu wa kusisimua kwamba washiriki wachache na maskini wa Australia waliojitolea sana kufanya chuo chake kuwa kitovu cha kazi ya umishenari kwelikweli. Chini ya L. R. Conradi, Ujerumani ikawa kitovu cha kazi ambacho kilipeleka wamishenari wengi sana, hasa kwa makoloni ya Kijerumani barani Afrika. Makoloni haya yalipoanguka chini ya Milki ya Uingereza katika vita vya kwanza vya dunia, Uingereza ikawa makao makuu ya kazi, huku ikiwa na hali mbaya kiuchumi.

Mnamo 1920 mtu na mke wake, kama seti za wanandoa ishirini walitumwa nje, na wengi zaidi katika mwaka 1922, kati yao walikuwa W. T, Bartlett na S. G Maxwell. Hawa walikuja kuwa mashuhuri sana. Kazi hii ilikua kwa nguvu sana "ng'ambo ya Marekani," hadi kufikia mwishoni mwa miaka ya 1920, Waadventista Wasabato wengi waliishi nje ya Amerika Kaskazini. Kwa mtazamo wa miaka ya 1970, hii ina maana kwamba Waadventista Wasabato imekuwa kwa kiasi kikubwa dini isiyo ya Kiamerika kwa nusu karne. Leo zaidi ya asilimia 80 ya washiriki wanaishi nje ya nchi ile ambapo kanisa lilizaliwa (Kwa sasa asilimia 51% ya Wasabato wanatoka Afrika).

Ingawa mnamo 1863 kulikuwa na washiriki 3500 Waadventista Wasabato waliopatikana karibu wote kutoka Kaskazini-Mashariki na kati ya Marekani, leo zaidi ya washiriki 22,000,000 wanaishi katika zaidi ya nchi na maeneo 212; idadi hii ni kubwa sana ambayo hakika imekuwa makao ya wamishenari wa kigeni.

Waadventista Wasabato leo ni vuguvugu la kimishenari la ulimwengu wote. Na kwa kuwa Yesu alisema, “Injili hii ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; hapo ndipo ule mwisho utakapokuja” (Mathayo 24:14), je, sio jambo la kawaida sisi kutazamia kurudi kwa Kristo upesi sana? Labda ndani ya wiki moja au mbili zaidi? Labda, ni nani anayejua, hata usiku wa leo?

Mnamo 1892 Ellen White aliwaonya Waadventista Wasabato wasibainishe tarehe kwa kusema kwamba Kristo angerudi ndani ya mwaka mmoja au miwili au hata mitano.[13] Mnamo 1892, walipokuwa wakifanya kazi katika nchi nyingi tu, walikuwa wakimtarajia kwa muda mfupi! Hakika hawakuonekana kuelewa. Je! Watu wanaelewa leo? Yesu alisema injili lazima iende kwa kila "taifa." Neno la Kigiriki linalotumika hapa katika maandishi ya kale zaidi ni ethnos. Kutokuelewana imeleta udadisi katika ulimwengu unaozungumza Kiingereza, kwa msingi labda wa toleo la King James Version?

Tafsiri ya neno hili, imewapotosha Wakristo wengi wenye shauku kutazamia ujio wa pili muda mrefu kabla masharti hayajatimizwa. Ingawa neno ethnos kama lilivyotumiwa katika siku za Yesu lilimaanisha "taifa," pia lilimaanisha "watu," "kundi la watu," "tabaka," na "kabila." Ilimaanisha hata "taifa" kwa maana ndogo ya "taifa la wafua shaba," ni kusema, chama au chama cha wafanyikazi wa mahali hapo. Umbo la wingi, ethne (na hili ndilo tulilo nalo katika Mathayo 24:14), lilimaanisha "wageni"—kwa Wagiriki, "wasio Wayunani," na kwa Wayahudi, "Mataifa." Ni wazi kabisa, Yesu hakuwa anazungumza tu kuhusu nchi 200 au zaidi, bali hata jumuiya za watu, makoloni, nchi zisizo huru na zilizo huru, maeneo, na mali zilizoorodheshwa katika kalenda za almanak za kisasa.

Na kwa hakika hakumaanisha kwamba mara tu familia ya wamishenari inapowasili katika nchi, jumuiya, koloni, au nchi isiyo huru, n.k., na kusambaza vijuzuu vichache kwamba, nchi hiyo nzima, pamoja na wakazi wake wote, vikundi vya lugha, makabila, vikundi vidogo na tamaduni ndogondogo, zinaweza kuangaliwa kama zimehubiriwa injili.

India ina watu bilioni 1.5 sasa wanaozungumza lugha na lahaja 880 tofauti na Jiving katika vijiji 550,000. Nigeria, yenye watu milioni 230, nayo ina makabila 250 tofauti, Tanzania ina makabila 124 tofauti na kila moja likizungumza lugha yake, ni wachache sana ambao ni Wakristo. "Kamwe usipoteze mtazamo wa Ukweli kwamba ujumbe unaohubiri ni ujumbe wa ulimwenguni pote. Huu unapaswa kutolewa kwa miji yote, kwa vijiji vyote,[14] asema Mjumbe wa mbinguni. Kwa maana pana na ya neema zaidi, Yesu alimaanisha kwamba injili inapaswa kuhubiriwa kwa kila Myahudi, kwa kila Mmataifa, kwa kila mtu, na hapo ndipo mwisho unapoweza kufika.

Yeyote anaweza kuokolewa. Kristo hakufa kwa ajili ya Wamarekani tu kama watu, au Uchina kama taifa, bali kwa ajili ya kila mwenye dhambi ambaye mapafu yake yanavuta pumzi waziwazi kana kwamba hapakuwa na mtu mwingine ambaye Yeye alimtolea Maisha Yake. Naye hayuko tayari kuja tena hadi kila mtu anayeishi wakati huo apate nafasi ya kusikia na (kama anapenda) kuamini na kuishi. “Kuhubiri Injili kwa kila kiumbe,” aliamuru katika Marko 16:15 "Nenda ukauambie ulimwengu! Kila kiumbe" kama miaka kumi au ishirini hivi, alisema Mnamo 1892. Hebu fikiri jambo hili.

Ilionekana kuwa jambo la busara kwa nabii, ambaye zaidi ya mtu mwingine yeyote alijua juu ya kazi ya ulimwenguni pote inayokabili kanisa, kwamba mwisho ungeweza kufika ndani ya miaka kumi au ishirini baada ya 1892. "Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa Roho wangu, asema Bwana" (Zekaria 4:6). Mungu alivunja vizuizi vya lugha siku ya Pentekoste kwa mara moja na anapokuwa na watu tayari, atafanya hivyo kwa urahisi tena. Yeye Hatamaliza kazi peke yake; kama angetaka kufanya hivyo kungekuwa katika mpango Wake angeweza kufanya hivyo zamani na kuimaliza kazi. Agizo ni, "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili" (Marko 16:15).

Wakati waamini wa kweli wa Mungu wanajitoa wenyewe kwa ajili ya utumishi wa misheni, katika ujirani wao na pia katika ulimwengu wote, Wakristo wanapohisi shauku kwa ajili ya nafsi iliyopotea ambayo Yesu anasikia uchungu kwa ajili yake, ‘wanapoondoa takataka’ kutoka moyoni mwao, na kumwacha Kristo Mwokozi aingie, Roho Wake ataijaza mioyo yao kuliko hapo awali, na kazi ya Mungu itaenea duniani kote kama moto kwenye makapi.

Yesu yuko katika kazi ya kufuta dhambi. Anafanya kazi ya kutakasa dhambi na ubinafsi kutoka katika mioyo na maisha ya watu. Na watakapomwacha asafishe dhambi zao na ubinafsi mpaka nje, Yeye atajileta mwenyewe ndani kabisa. Yeye Atawajaza kwa Roho Wake - lakini si kama maji yanavyojaza kikombe. Atawajaza Roho Wake kama vile maji chini ya shinikizo la mpira! Yeye Atamimina wema Wake kwa wingi kupitia kwao kwenda kwa ulimwengu. Na atakapokuwa na kundi la wanaume na wanawake, wavulana na wasichana, duniani kote, ambao wamejazwa Roho Mtakatifu kama vyombo vilivyowekwa wakfu mkononi Mwake, ndipo watu watasema, “Tazama, mvua ya masika inanyesha, na dunia imejaa maji ya utukufu wa Bwana." "MUNGU atafanya kazi," Ellen White aliahidi karibu na mwisho wa maisha yake, "ikiwa tutampa miili yetu, nyenzo zetu- naam, tutampa nafsi zetu."[15]

*Maelezo:*

*1. Review and Herald, August 26, 1875, p. 60*

*2. Ellen G. White, Testimony to the Battle Creek Church (Battle Creek, Mich.: Steam Press of the Seventh-day Adventist Publishing Association, 1872); J. N. Andrews to Ellen G. White, September 17, 1883*

*3. Reported in the Review and Herald, December 5, 1878*

*4. True Missionary, March 1874, pp. 20, 21*

*5. For reports on how the SDA work began in countries around the world (see the SDA Encyclopedia articles on these countries. See 426 also Spalding, Origin and History) 6. J. N: Andrews to S. N. Haskell, December 23, 1879, gives the spelling "Bertola"*

*7. Review and Herald, March 29, 1864, p. 142*

*8. Review and Herald, December 17, 1872, p. 8*

*9. Ellen G. White, Testimonies, vol. 1, pp. 632, 666-680*

*10. The first regular mission station for black Africans was opened a few weeks earlier among the Fantis of the Gold Coast (now Ghana). The Fantis, however, were already Christianized, leaving Solusi to be the first SDA station for non-Christians*

*11. George Elmer Bryson, "The Beginning of the Seventh-day Adventist Church in Ghana (Gold Coast), 1888-1905" (term paper, Andrews University 1975)*

*12. Ellen G. White, Life Sketches, pp. 372-376*

*13. Ellen G. White, Selected Messages, bk. 1, p. 189*

*14. Ellen G. White, Testimonies, vol. 7, pp. 35, 36*

*15. Ibid., vol. 9, p. 107*

## SURA YA 24
## WANAWAKE WANAOONGOZA

"Kiko wapi kile 'kila kiumbe' ambacho wito wa injili lazima uende kwacho?" iliuliza sauti ya kike ya kuvutia katika Mkutano Mkuu wa 1899 huko Lancaster Kusini, Massachusetts. "Ni wapi hicho kila kiumbe kinapatikana?" "Katika ulimwengu wote," sauti zingine zilijibu kutoka kwa wanamkutano. "Ndiyo, ndiyo, katika ulimwengu wote," msemaji alikubali, "lakini pia kuna mahali pengine. kwani Dunia ni kubwa sana!" "Je, ni Hapa karibu" Karibu kwa kiasi gani?" alisisitiza mzungumzaji; kisha, akijibu swali lake mwenyewe: "Hapa nyumbani kwako mwenyewe!" Msemaji wa tukio hili hakuwa Ellen White. Dada White bado alikuwa mbali huko Australia. Badala yake alikuwa Sarepta Myrenda Irish Henry, mmoja wa wanawake wa kipekee sana kujiunga na harakati za Waadventista.

Bi. S. M. I. Henry alikuwa mhamasishaji mashuhuri wa maisha ya kiasi na matengenezo mengine kwa miaka thelathini kabla ya ugonjwa mbaya kumpeleka

Battle Creek. Matibabu na maombi yalisababisha uponyaji wake katika mwaka wa 1896, na pia katika wongofu wake hadi kuwa mshika Sabato. Alijiunga na Waadventista akichukulia kwamba watu wenye ujumbe wa ajabu namna hii lazima wawe wanaelekea kwenye ukamilifu. Akiwa amevunjika moyo lakini hakukata tamaa hata kidogo, katika miaka michache iliyobaki ya maisha yake alitoa ushahidi wenye matokeo.

Katika tukio hilo linalozungumziwa, alijishughulisha na moja ya mada anazopenda zaidi. "Nyumba ni moyo wa kanisa," alisema, "na mama nyumbani ndiye kitovu cha maisha. Mama alivyo ndivyo nyumba ilivyo pia." Kabla ya injili kupelekwa kwa kila kiumbe kilicho nje ya nyumba, aliendelea kusema, nyumba za waamini lazima ziwe na uwezo; na nguvu zinazohitajika zinapatikana kwa urahisi kwa wazazi na watoto vile vile. Biblia inasema katika kitabu cha Matendo kwamba ahadi ya Roho "ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu."[1]

Bibi Henry, ingawa alikuwa bora zaidi kuliko wengi, alikuwa mmoja tu wa maelfu ya wanawake ambao talanta yao na kujitolea kumechangia mafanikio ya harakati za ujio wa Masihi. Tayari tumekutana na wanawake kadhaa, mfano Bibi John Couch, utakumbuka, alikuwa na ujasiri wa Kikristo wa moja kwa moja lakini kwa adabu alimkatiza Mzee Joseph Bates na kumtambulisha Samuel Snow katika kutaniko, ambaye naye aliwafundisha kutaniko kuhusu kilio cha usiku wa manane.

Bi. Rachel Oakes alitambulisha Sabato kwa Waadventista huko Washington, New Hampshire. Annie Smith alishangilia waumini wa mwanzo kabisa kwa nyimbo za furaha. Hannah More alikuwa wa kwanza kuthamini ujumbe wa malaika wa tatu katika bara la Afrika. Annie Butler na kijana Mary Andrews walikuwa wamishenari wa kike wa kwanza kwenda Ulaya. Bibi Armstrong na Bi. Catherine Revel walikuwa miongoni mwa waongofu wa kwanza wanaoshika Sabato huko. Na, bila shaka, Ellen G. White, aliyevuviwa na mwenye msukumo wa harakati nzima ya waadventista, yeye mwenyewe alikuwa mwanamke madhubuti!

Hawa wote na wengine tumekutana nao. Lakini kulikuwa na wengine wengi.[2] Wanawake wametoa ushawishi mkubwa katika mwendo na safari ya Uadventista kupitia kujitolea kwao kwa huduma, aina mbalimbali za michango yao, uaminifu wao, na unyenyekevu wao. Wametumikia wakiwa makatibu, walimu, wauguzi, wamishenari, na wafanyakazi wa Biblia, na pia kama waandishi, wahariri, watunzi, waanzilishi, wasimamizi, wafadhili, na wahubiri. Bado kwa sehemu kubwa wametumikia kwa kutambuliwa kidogo. Mishahara yao kwa kawaida ilikuwa chini sana ukilinganisha na ile ya wanaume. Ni mara chache sana wameomba majukumu ya juu au vyeo. Wamefanya karibu kila kitu, wameomba bila malipo, na kupokea thawabu yao kwa kujua kwamba wamefanya walichoweza.

Hebu tukutane na baadhi ya mifano mashuhuri. Ingawa jina lake karibu kusahaulika leo, Minerva Jane Chapman, dadake Mzee J. N. Loughborough, alijulikana sana katika safu ya Waadventista wakati wa uhai wake. Mnamo 1877 alichaguliwa kuwa mweka hazina wa Halmashauri Kuu -General Konferensi. Wakati huohuo alikuwa mhariri wa "Youth's Instructor," katibu wa Shirika la Uchapishaji, na mweka hazina wa machapisho na the Vigilant Missionary Society! Alihudumu kwa miaka tisa kama mhariri wa gazeti la Youth's Instructor, akikataa kupokea mshahara wowote kwa huduma zake katika wadhifa huo.

Mzee na Bi. Chapman walihamia Battle Creek mwaka wa 1866 muda si mrefu baada ya General Konferensi kuandaliwa na Vita vya wenyewe kwa wenyewe kumalizika. Alifanya uchapaji kwa mikono kwa muda lakini kwa kasi ya juu alipanda ngazi hatua kwa hatua hadi kuwa mweka hazina wa Review and Herald, na kisha kwenye majukumu ambayo tayari yametajwa. Baada ya kustaafu mwaka wa 1893 aliendelea kuishi Battle Creek, akiwa mzima wa afya na mwenye bidii hadi siku aliyofariki akalala usingizi wa mauti akiwa na umri wa miaka 94.[3]

Maria L. Huntley alizaliwa katika mojawapo ya familia za kwanza za Waadventista washika Sabato huko Washington, New Hampshire. Baada ya muda akawa katibu mahiri wa the Vigilant Missionary Society, kundi lile la wanawake wenye bidii na waliojitolea wenye nia ya kimishenari huko Lancaster Kusini, Massachusetts, ambalo tulisoma kuwahusu katika sura ya ishirini. Jumuiya ya wenyeji ilipopanuka na kuwa Shirika la "General Tract and Missionary Society" kwa ajili ya dhehebu zima mwaka wa 1874, akawa katibu wake na aliendelea kushikilia wadhifa huu muda wote alioishi—akiongeza wa kwanza, kisha mwingine, halafu wa tatu, na hatimaye kumi na moja, makatibu wasaidizi sambamba wa kumsaidia.

Wakati wa Mkutano Mkuu (GC) wa 1888 huko Minneapolis aliombwa kuhutubia mkutano juu ya shughuli za uendeshaji za kawaida za kanisa. Alisisitiza kwamba "wengi wangefanya kazi kwa furaha kama wangejua jinsi ya kufanya hivyo," na akawasihi wachungaji waandae mipango madhubuti ya kutoa mafunzo kwa watu wa kawaida.[4] Kinyume na Bi. Chapman, Bi Huntley *ambao walifariki wakiwa na umri wa miaka 43 pekee, walipokuwa akiandaa shughuli za ku*ongoa roho huko Chicago.[5]

Mnamo 1866 msichana wa miaka kumi na tano aitwaye Maud Sisley, alikuja Battle Creek na kupata kazi katika Review and Herald. Baba yake alikufa miaka kadhaa kabla wakati familia ilikuwa bado Uingereza. Ndugu mkubwa alikuwa wa kwanza kuondoka kwenda Marekani. Wengine walipofuata, walimkuta "akiitunza Jumamosi kama siku ya Sabato" na wakajiunga naye kufanya vivyo hivyo. Pamoja na Maud na kaka yake, kulikuwa na jumla ya watoto saba katika familia ya Sisley. Kati ya wasichana hao wanne, Josephine akawa mwalimu wa mmishenari huko Australia.

Martha alifanya kazi kama mchapaji katika Review and Herald, na Nelly alisoma katika Battle Creek Sanitarium, akawa muuguzi, akaolewa na Mzee George B. Storr, na pamoja naye wakaandamana na Ellen White hadi nchi ya Australia. Na vipi kuhusu Maud? Alikuwa mmoja wa Waadventista wa kwanza kutoa zaka kamili. Alikua aina ya mmishenari mwanafunzi, akichukua likizo ya miezi sita bila malipo kufanya kazi ya utume huku akijitegemea huko Ohio. Mnamo 1877 alienda Uswisi kutumika akiwa mmishonari mseja nje ya nchi. Huko alitoa machapisho kwa Kiitaliano, ingawa hakujua lugha hiyo. Baadaye alirudi Amerika, na kuolewa na C. L. Boyd, msimamizi wa Konferensi ya Nebraska, akaandamana naye hadi Afrika Kusini akiwa sehemu ya kikundi cha kwanza cha wamishenari Waadventista kwa wasio Wakristo katika bara hilo.

Inastahili kutajwa kuwa wavulana watatu katika familia hii pia walikuwa wafanyakazi katika kusudi la injili. John akawa mhubiri. Robert alikuwa mmishenari anayejitegemeza na akafa katika uwanja wa utume. William (William Conqueror Sisley) akawa mbunifu na mjenzi, akibuni na kujenga baadhi ya majengo makuu katika Chuo cha Battle Creek, Chuo cha Walla Walla, chuo cha Muungano, na katika taasisi nyinginezo nchini Australia, Afrika Kusini, na Uingereza.[6]

Kile ambacho familia ya Sisley ilifanikisha ni ishara ya weledi wa mama yao na kujitoa wakfu. Kama akina mama, maelfu ya wanawake wengine wa Kiadventista ambao pia wamewalea watoto wao kwa ajili ya Mungu wamechangia kwa kiasi kikubwa mafanikio ya harakati hiyo. Ikumbukwe kwamba wakati Mkutano Mkuu ulipoanzisha Bodi ya Misheni ya Kigeni mnamo 1879, ukitegemea uangalizi wa kimishenari ambao hapo awali ulikuwa chini ya Kamati ya Utendaji, wajumbe wake watatu kati ya tisa walioteuliwa walikuwa wanawake ambao tumewataja hivi punde: Minerva Jane Chapman. Maria L. Huntley (umri wa miaka 32), na Maud Sisley (28).[7]

Familia nyingine maarufu katika Uadventista wa awali iliundwa na "Rankin girls" karibu 12 kati yao kwa pamoja, Wengi wao walikuwa walimu, baadhi yao walifanya kazi isivyo kawaida. Ida Rankin alikuwa mkuu wa kwanza wa wanawake leo tunaita matron au dean wa wanawake ("preceptress" katika siku hizo) katika Battle Creek College. Mary Rankin akawa mama wa Dk. E. A. Sutherland, mtu ambaye, pamoja na Percy Magan, walisaidia kubadilisha Chuo cha Battle Creek kuwa Chuo cha Umishenari cha Emmanuel (sasa ni shule ya shahada mbalimbali kama vile Bachelors, Masters na PHD ya Chuo Kikuu cha Andrews) na baadaye akaanzisha Chuo cha Madison kinachotegemeza watu (self supporting school).[8]

Msichana mashuhuri zaidi kati ya wasichana wote wa Rankin alikuwa ni Helen, ambaye baada ya ndoa yake na Alma Druillard alikuja kujulikana kama "Mama D." na "Shangazi Nell." Kwa kawaida akiwa mzuri katika takwimu, Bi. Druillard alichaguliwa

kuwa mweka hazina wa Konferensi ya Nebraska. Baada ya ndoa yake alikuwa mke mmishenari kwa miaka kadhaa. Mnamo 1901 alikuwa mweka hazina wa Chuo cha Umishenari cha Emmanuel. Wakati mumewe alifariki mnamo 1904, alikuwa na baraka kubwa ya kuweza kuongoza familia yake, alikuwa na umri wa miaka sitini na alikuwa karibu kuchukua majukumu mapya katika kazi.

Katika mwaka huo huo, 1904, E. A. Sutherland (mtoto wa dada yake Mary) na Percy T. Magan, mtendakazi mwenzake, walijiuzulu kutoka kuwa Chancellor au mkuu wa Chuo cha Umishenari cha Emmanuel na kuhamia Kusini ili kuanzisha kazi ya elimu ya Waadventista huko. Bibi White pia alikuwa Kusini wakati huo, akimtembelea mwanawe mwinjilisti, Edson. Edson alipendekeza kwamba wote wapande meli yake ya umishenari, Morning Star. Siku ya kwanza, walipohitaji kufanya matengenezo, Bibi White alichukua fursa ya kuchelewa kutazama ekari ambazo ndugu walikuwa wakifikiria kuwa mahali pa kujenga shule mpya ya vijana wasiojiweza.

Sehemu kubwa ya ardhi ilionekana kuwa duni, lakini Ellen White alikuwa ameshawishika kuwa ndipo mahali ambapo Mungu alitaka wanunue, si kwa ajili ya shule tu bali pia kwa ajili ya hospitali au jengo la afya. Ndipo baada ya kurudi kwenye mashua, kila asubuhi kwa siku tatu aliwaita Sutherland na Magan na kuwasihi watafute pesa na kununua ardhi hiyo. Sutherland na Magan walirudi tena kutazama mahali hapo. Hapa palionekana kuwa pabaya sana kiasi kwamba walikaa chini na walilia kweli-kweli!

Lakini waliamua kufuata mwongozo wa Bwana na wakaazimia kwamba Sutherland amwendee shangazi yake, Bi. Druillard katika Chuo cha Umishenari cha Emmanuel, na kumwomba atoe pesa hizo. Alienda Berrien Springs na kufanya ombi lake. Alimjulisha kwamba alifikiri mradi huo ni upumbavu kabisa. Sutherland aligeuka kuondoka. "Unaenda wapi?" Aliuliza Bi. Druillard "Ili kupata mtu mwingine ambaye atatusaidia. Ninaenda kumtii Bwana, hata iweje." Punde alikuwa amesimama kando ya Bibi White, akiitazama ile ardhi. Kwa msingi wa uhakikisho wa Bibi White, yule bibi tajiri aliamua kusonga mbele kwa kusponsor injili. Hakuna aliyekatishwa tamaa.

Chuo cha Madison na Madison Sanitarium vilikua na kufanikiwa, vikitoa mafunzo kwa maelfu ya wanafunzi, vikitoa mamia ya wahitimu, na kuchochea uanzishwaji wa taasisi zinazofanana yaani zinazojitegemea kote Kusini na katika nchi mbalimbali ulimwenguni- (self supportive institutes). Siku ambayo Bibi Druillard alikuja kusaidia katika mradi huu, Dada White alimwambia, "Nelly, unafikiri wewe una umri mkubwa wa kustaafu sasa. Ikiwa utakuja na ushiriki kura yako na kazi hii, ikiwa utapenda, waangalie hawa vijana wa kiume [Sutherland na Magan, wangali katika miaka ya thelathini] na wewe uwaongoze, na kuwategemeza katika yale Bwana anayotaka wafanye, ndipo Bwana ataufanya upya ujana wako, nawe utafanya mengi zaidi siku zijazo kuliko ulivyowahi kufanya huko zamani katika maisha yako."

Maneno yaliyonenwa yalikuwa kweli. Mama D. alitoa mchango wake kwa ajili ya maskini wa Kusini. Mungu alimtegemeza katika uzee wake uliokomaa na wenye bidii. Alifariki akiwa na miaka 94 baada ya kuanzisha taasisi nyingine, hii ilikuwa ni ya watu weusi, Riverside Sanitarium.[9] Kate Lindsay alikulia katika familia kubwa katika eneo moja la kilimo la Wisconsin na wasichana wa Rankin. Huyu alikuwa mjukuu wa binamu ya David Livingstone na alivutiwa na kile Florence Nightingale alikuwa akifanya huko Uingereza na Crimea, aliondoka nyumbani hadi Battle Creek mnamo 1867 ili kutoa huduma zake kwa Taasisi ndogo ya Matengenezo ya Afya ya Magharibi ambayo Waadventista walikuwa wameanzisha mwaka mmoja kabla.

Haikuchukua muda, naye alienda New Jersey kwa kozi ya uuguzi ya miaka miwili, na kisha katika Chuo Kikuu cha Michigan huko Ann Arbor kama mshiriki wa kundi la pili la wasichana waliowahi kuruhusiwa kuchukua kozi ya tiba huko. Mmoja wa wasichana kumi kati ya wanaume 1300, alipokea kejeli na matamshi ya kumpa mashaka na kumtilia mashaka, lakini alipotetea hoja yake kuunga mkono haki ya wanawake kusoma kozi ya tiba, alishinda siku hiyo na akapata heshima kwa vijana wa kiume. Hatimaye alimaliza kozi ya udaktari na akiwa wa kwanza katika darasa lake zima.

Aliporudi katika Taasisi ya Matengenezo ya Afya ya Magharibi (Western Health Reform Institute), ambayo sasa imepewa jina la Sanitarium ya Tiba na Upasuaji, alibobea katika magonjwa ya wanawake na watoto karibu wakati ule ule John Harvey Kellogg alipokuwa mkurugenzi wa tiba wa taasisi hiyo. Akiwa mtu asiye na woga na mwenye kusonga mbele, hatimaye alimshawishi Kellogg na bodi kuanza shule ya uuguzi mwaka 1883, ambayo aliendelea kuisimamia na kuiongoza hadi alipoondoka kuelekea Afrika mwaka wa 1897.

Baadaye alihudumu katika Boulder Sanitarium huko Colorado. Akiwa wakili mzuri wa muda, mtu makini, na mwenye moyo mwororo, Dk. Lindsay alikuwa na mvuto kwa maelfu ya wauguzi, madaktari, na wagonjwa bila ya kusahaulika. Katika miaka yake huko Battle Creek nyumba yake pekee ilikuwa ni chumba kidogo karibu na ofisi yake! Alitamani huduma ipatikane kila wakati. Na ni kwa sababu ya kujitolea kwake kwamba amepewa heshima ya bweni kuitwa kwa heshima yake, yaani Kate Lindsay Hall, bweni la wanafunzi wauguzi katika Chuo Kikuu cha Loma Linda.[10]

Georgia Anna Burrus alijitolea kwa huduma kama mmishenari mwanamke na akawa mmoja wa wafanyakazi wa kwanza wa Waadventista Wasabato nchini India. Ilikuwa ni ujasiri kwa upande wake kwenda mbali bila mume au familia. Kabla tu hajatua, upweke mbaya ukampata. Katika kina cha kutamani kwake nyumbani alidondosha saa yake kwenye deki ya meli na ikaacha kufanya kazi. Alikuwa amempoteza rafiki yake wa mwisho! Alifikiri kwa uchungu kwamba ikiwa tu angesikia tena mshale wa saa ukitembea angeweza kuendelea na kuwa mmishenari! Akiwa amepiga magoti

katika chumba chake, alimwomba Mungu amhurumie na kuifanya saa hiyo kufanya kazi tena. Mungu alimpenda na kujibu ombi hilo kirahisi sana (Hakuomba kurudi nyumbani. Hilo kamwe halikumwingia akilini). Kwa woga na kwa kuamini alichukua saa yake na kuishikilia sikioni. Ilisikika ikifanya kazi tena! Na haikuacha kamwe kufanya kazi tena. Hakuwa na shida nayo tena hivyo aliendelea moja kwa moja hadi India, hamu yake ya nyumbani iliondolewa kabisa.

Baadaye aliolewa na Luther Burgess, mmishonari mwingine, na pamoja walitumia miaka 32 wakisimamia kazi ya injili miongoni mwa watu mbalimbali wa bara hilo dogo. Katika safari hadi Amerika iliyofanyika ili kwamba Mzee Burgess aweze kupokea matibabu, waligundua kwamba ofisi kuu ya kanisa haikuwa na pesa za kuwarudisha. Bi. Burgess alienda barabarani na kuuza nakala 20,000 za "Shule ya Mafunzo ya Biblia" kwa senti kumi kipande ili kununua tiketi zao yeye mwenyewe.[11]

Tukizungumza kuhusu wamishenari wanawake nchini India, hatupaswi kumsahau Anna Knight, mmishenari wa kwanza mweusi katika nchi hiyo. Akiwa mtoto huko Mississippi alikuwa amejifunza kusoma mapema zaidi kuliko wenzake wowote na aligeuka kuwa Mwadventista kwa kusoma gazeti la “Signs of The Times” na Steps to Christ.” Baada ya muda wa masomo katika akademi ya Waadventista huko Graysville (mtangulizi wa Chuo cha Misheni cha Kusini), alirudi nyumbani maili 380 kwa likizo ya majira ya joto. Jamii ilimdhihaki.

Siku za Sabato alichukua Biblia yake, pamoja na vitabu vifuatavyo: Sabbath School Quarterly, Sabbath School Worker, Review and Herald na Youth's Instructor. Akiongozana na mbwa wake, alichukua na bastola kwenda msituni. Mbwa alitakiwa kuwalinda dhidi ya nguruwe mwitu. Bastola ilikuwa ya kuwakinga dhidi ya watu! (Akiwa mtoto alikuwa amejitengenezea pinde na mishale na alijulikana kuwa na uwezo wa kugonga fundo kwenye yadi 100).

Baadaye huko mjini Battle Creek Sanitarium, akawa muuguzi. Dk. Kellogg alichukua tahadhari maalum na akamteua mjumbe wa General Konferensi 1901. Katika mwaka huo huo alitoka nchini na kwenda kama nesi India. Huko India alifanya uinjilisti wa vitabu yaani Colpoteur, akafundisha shuleni, akauguza, na alichangamana na matajiri na maskini vilevile katika sehemu zote za kaskazini na mashariki mwa nchi. Bila kuchoka, akidumishwa na maombi ya kila mara, aliongozwa, kuponywa, na hata kulishwa na mfululizo wa miujiza.

Akiwa dhaifu kutokana na njaa baada ya saa thelathini na sita bila chakula wala maji akiwa anasafiri kwa treni, alitazama nyuma yake kwenye chumba chake na alistaajabu kuona kwenye kiti sahani ya mkate na kikombe cha kinywaji cha joto. Alipokuwa akila kwa shukrani, alitazamia kwamba wakati wowote mgeni huyo aliyevalia isivyo kawaida na akizunguka-zunguka kwenye jukwaa angeweka kichwa

chake dirishani na kuomba malipo yake. Lakini alipomaliza na kujaribu kumrudishia vyombo, alikuwa ametoweka. Baada ya muda Bibi Knight alirudi kwenye kazi yake ya shule huko Mississippi; kisha akaendelea na kuanzisha YWCA ya kwanza ya watu wenye rangi nyeusi huko huko Atlanta.

Alihudumu kama Mmishenari wa Nyumbani, Mmisionari wa Kujitolea, Msimamizi wa Elimu, na katibu wa Shule ya Sabato nafasi zote kwa wakati mmoja kwa Majimbo ya Kusini-mashariki na Kusini, ofisi yake pekee wakati fulani ilikuwa katika buti ya gari lake na mkoba wake. Hatimaye alitulia na kuwa mama katika Chuo cha Oakwood. Alikuwa amesafiri, bila kuhesabu muda wake nchini India, maili nusu milioni, alikuwa ameendesha karibia mikutano 10,000, na alikuwa ameandika kwa mkono au kuandika barua 49,000.[12]

Wanawake wengine wengi wamechangia historia ya Kanisa la Waadventista Wasabato, na kusaidia kutimiza utume wa kuuambia ulimwengu." Hatuwezi kumwacha kabisa Lora Clement, binti wa Melissa Rankin (ambaye alikuwa msichana wa Rankin mwenyewe), ambaye alihariri Youth's Instructor, gazeti lililotangulia liitwalo Insight, kwa miaka ishirini na tisa ya kushangaza, ambapo makala yake, "Let's Talk It Over," ilikuwa mojawapo ya mada iliyothaminiwa zaidi.

Ni maelfu mangapi ya wanawake wametoa michango kama viongozi na walimu wa Shule ya Sabato. Flora Plummer, katibu (ambaye ni mkurugenzi) wa Idara ya Shule ya Sabato ya General Konferensi kutoka 1913 hadi 1936, aliandika vitabu vingi, na, bila shaka, alisaidiwa na wanawake na wasichana wasiohesabika katika Shule za Sabato za maeneo mengi ulimwenguni kote. Vipi kuhusu walimu wa shule za msingi, akademia na vyuo? Katika elimu ya Waadventista ni nani anajua ni maelfu mangapi ya wanawake waliotumika kanisani, bila kuacha pale mimbarini?

Ida Riggels Burden, kwa mfano, katibu wa Shule ya Sabato ya Konferensi ya Oregon mwanzoni mwa karne ya ishirini, alikuwa mzungumzaji wa mara kwa mara katika ibada, na alikuwa mmoja tu wa wahubiri wanawake. Mke wa Mzee E. B. Lane alijulikana sana kama mhubiri na alibeba leseni ya huduma kwa jina lake mwenyewe, ingawa sio "sifa" za huduma za mhudumu aliyewekwa wakfu. Kuwekwa wakfu kwa wanawake kulijadiliwa katika General Konferensi la 1881, ambako inaweza kuwa kulichochewa na Ukweli kwamba Wabaptisti wa Siku ya Saba walikuwa wamewaweka wakfu wanawake muda mfupi.

Huko Amerika wakati wa Anguko kuu la uchumi (Great Depression-inflation) na huko Ulaya wakati wa Vita vya dunia vya pili wanawake walitumika kama wachungaji wa ndani bila kuweka wakfu. Kuwekewa kwao wakfu ili kuwa wachungaji kwa huduma ya injili kunajadiliwa sana kwa miaka kama 50 sasa, nchi zingine wamewekewa mikono kuwa kama wazee wa makanisa katika maeneo mahalia. Wakati huo huo

shauku kubwa imeonyeshwa katika taarifa iliyotolewa na Ellen White mnamo 1895 ambayo inaonekana akiidhinisha kuwekwa wakfu kwa wanawake kwa aina ya jukumu la ushemasi au mfanyikazi wa ustawi: "Wanawake ambao wako tayari kuweka wakfu wakati wao kwa huduma ya Bwana wanapaswa kuteuliwa kutembelea wagonjwa, kuangalia vijana, na kuhudumia mahitaji ya maskini na hawa wanapaswa kutengwa kwa kazi hii kwa sala na kuwekewa mikono.[13]

Kulikuwa na vuguvugu lenye nguvu la uhuru wa wanawake au ufeministi nchini Marekani katika karne ya kumi na tisa na vilevile katika karne ya ishirini; vuguvugu la karne ya kumi na tisa lilitoa wito bora zaidi wa kurejeshwa kwa haki halali na lilipiga kelele mbaya zaidi kuhusu ngono huru na kupinga uzazi. Jibu la Waadventista Wasabato karne moja iliyopita, lilikuwa na msisitizo juu ya jukumu la wanawake kama wenye ofisi wenye uwezo na kama walimu na waelekezi wa vijana kanisani, shuleni, na zaidi sana nyumbani.

Baada ya yote, si kwa kamba wakina mama wamefungwa minyororo kwa majukumu tu ya nyumbani bali kama watu wadogo walioumbwa kwa mfano wa Mungu na wenye uwezo, wakati wa ukomavu, kueneza ujumbe duniani. Hakika, hata wakiwa wachanga, watoto ni miongoni mwa "kila kiumbe" ambaye injili lazima iende kwao, kama Bibi S. M. I. Henry alivyoona inafaa. Ellen White mara kwa mara alikuwa na msisitizo katika kuinua vipengele hivi vya mwanamke wa kuheshimiwa, lakini hakufanya hivyo kwa kuegemea upande mmoja. Pia alitoa wito wa kushughulikiwa kwa malalamiko ya wanawake na kudai, katika jina la Bwana, malipo yenye uwiano kwa kazi ya wanawake.

Aliandika: "Bwana ana kazi kwa ajili ya wanawake, na vilevile kwa wanaume. Wanaweza kuchukua nafasi yao katika kazi Yake katika shida hii, na Bwana Atafanya kazi kupitia wao."[14] Mungu ni Mungu wa haki, na ikiwa watumishi wanapokea mshahara kwa kazi yao, wake zao, ambao hujishughulisha na kazi kama watenda kazi pamoja na Mungu, wanapaswa kulipwa sambamba na mshahara wa waume zao, walakini hawawezi kudai malipo haya."[15] "Swali hili si la wanaume kusuluhisha. Bwana amelitatua. Wewe [aliandika kwa uongozi] unapaswa kufanya wajibu wako kwa wanawake wanaofanya kazi katika injili."[16]

Wakati James White alipomwekea mhudumu mikono ya uchungaji kando ya ziwa katika majira ya joto ya 1867, alimwomba mke wa mhudumu apige magoti kando ya mumewe kwa msingi kwamba alikuwa akitengwa kama msaidizi wake. Alifikiri kwamba utaratibu kama huo unapaswa kufuatwa katika kuwekwa wakfu kwa wahudumu wote.[17] Wakati Robert H. Pierson alipokubali kuchaguliwa kwake tena katika kikao cha General Konferensi ya mwaka 1975 huko Vienna, alimwomba mkewe asimame kando yake kama ishara ya wake za watendakazi wote wanaoshiriki mizigo ya waume zao. Ana furaha mke anayeweza kushiriki mizigo ya mumewe moja

kwa moja. Wengi, hasa watoto wanapokuwa wadogo au waume zao hawapo, lazima washiriki mizigo yao kwa bidii. Kwa heshima tulisoma mistari nyororo ambayo

Angeline Andrews (wakati huo akiwa katika miaka ya mwisho ya thelathini) aliandika katika shajara yake siku baada ya siku karibu mwaka wa 1860:[18] "Ninamkumbuka sana mume wangu. Inaonekana kana kwamba sikuweza kuvumilia wazo lake kuwa mbali kwa miezi kadhaa zaidi." "Siwezi kuridhika na kutokuwepo kwake kwa muda mrefu. Jinsi moyo wangu ungetamani sana kukutana naye tena. Yeye ni mmoja wa waume wema na bora zaidi." "Nataka John afanye vyema." "Ni shauku yangu kwamba mkono wa Mungu umwongoze." "Kuna haja moyoni mwangu ambayo bado haijatimizwa. Sionekani kuridhika sana ama katika kuandika au kupokea barua." "Mume wangu mpendwa amekuja! Jinsi ulivyo wa thamani muda wa kukutana." "Mume wangu mpendwa aliondoka asubuhi hii akienda kujiunga na kambi la Minnesota. Wakati wa kusikitisha, katika matukio haya ya kuagana!"

*Vidokezo:*

*1. Slightly adapted from an apparently verbatim report of her sermon "Woman's Work" General Conference Bulletin, 1899, pp. 172- 174*

*2. A useful study on the subject of this chapter is John G. Beach, Notable Women of Spirit: The Historical Role of Women in the Seventh-day Adventist Church (Nashville, Tenn.: Southern Publishing Association, 1976). See also appropriate articles in the SDA Encyclopedia*

*3. Obituary notice by A. G. Daniells, Review and Herald, January 3, 1924, p. 22; SDA Encyclopedia, article Chapman, Minerva Jane (Loughborough)" 451 4. General Conference Daily Bulletin, 1888, p. 3*

*5. Review and Herald, April 29, 1890, p. 271; SDA Encyclopedia, art. "Huntley, Maria L*

*6. Spalding, Origin and History, vol. 2, p. 50; SDA Encyclopedia, art. "Sisley, William Conqueror"; E. K. Vande Vere, The Wisdom Seekers (Nashville, Tenn: Southern Publishing Association, 1972), p. 52*

*7. Review and Herald, December 4, 1879, p. 184*

*8. Spalding, Origin and History, vol. 2, pp. 45-47*

*9. Ibid., vol. 3, pp. 107-175*

*10. Kathryn Jensen Nelson, Kate Lindsay, M.D. 1842-1923 (Nashville, Tenn.: Southern Publishing Association, 1963)*

*11. SDA Encyclopedia, art. "Burgess, Georgia Anna (Burrus)"*

*12. Anna Knight, Mississippi Girl, An Autobiography (Nashville, Tenn.: Southern Publishing Association, 1952)*

*13. Review and Herald, July 9, 1895, p. 434*

*14. Ellen G. White, Evangelism (Washington, D.C.: Review and Herald Publishing Association, 1946), p. 464*

*15. Ellen G. White, Manuscript 43, 1898; manuscript release no. 267*

*16. Ellen G. White, Evangelism, p. 493*

*17. Review and Herald, August 13, 1867, p. 136*

*18. Slightly edited from Angeline Andrews, Diary, manuscript deposited in the Heritage Room, Vernier Radcliffe Library, Loma Linda University*

# SURA YA 25
# AMEVUVIWA KUOKOA ROHO

Mrs James White au kama tumjuavyo Mama Ellen, au Dada White, au Bibi White alikuwa mama halisi vilevile "mama katika Israeli." Aliwaacha wavulana wake chini ya uangalizi wa mpishi na mfanyakazi wa nyumbani wakati yeye akisafiri na mumewe kwa wito wa Bwana, hii ilikuwa chanzo cha tashwishi ya mara kwa mara kwake na, wavulana wake (James Edson na Willie mdogo wake) wakiwa katika mazingira hayo, mara nyingi walijipatia fursa ya kujiingiza mara kwa mara katika tabia mbaya.

Hasa kwa James Edson. Muda mfupi kabla ya siku ya kuzaliwa ya kutimiza miaka kumi na sita kwa Edson, mama yake alimwandikia barua ya dhati kwa huzuni nyingi. Aliandika hivi: “Wakati wote wanaonizunguka wakiwa katika usingizi, mimi hukesha kwa mahangaiko” kuhusu hali yako ya kiroho na “mimi huwa ninaweza kupata utulivu katika sala ya kimya-kimya tu.” "Wewe Edson ukiwa mbele ya nyuso zetu, unaweza kufuata matakwa yetu, lakini ... unatuasi wakati hatupo. Umefuata mapenzi yako na mipango yako mara nyingi sana, ukificha yote kutoka kwetu, ukienda kinyume na ushauri wetu wote na makatazo yetu, jambo ambalo linatufanya kutoweza kukutegemea (hautegemeki ….)

Badala ya wewe kuwa faraja, wewe ndiyo chanzo cha wasiwasi wenye uchungu na fadhaa. "Miiba na michongoma imeota katika bustani yangu na kuzisonga mbegu nilizojaribu kupanda." Mbaya zaidi, "ni giza ambalo siwezi kuelezea linalofunika kwenye akili zetu kuhusiana na ushawishi na mvuto wako kwa Willie (mdogo wako). Wewe unamwongoza katika mazoea ya kutotii na kujificha na kuficha ukweli, au kuzungumza maneno na tabia yenye utata... ... "Oh, Edson, ni kujua mambo haya ndiko ambako hunichosha na kuleta juu yangu kukata tamaa” jambo ambalo linaweza kunifanya hata niache kazi zangu za utume ninazozifanya hadharani.

Wakati Ellen White akiwasihi wazazi kuwaombea watoto huku vidole vyao viking’ang’ania kwa nguvu ahadi za Biblia na sauti ya kusihi katika namna ambayo ni sauti ya mzazi tu inaweza kutenda hivyo na kwa unyenyekevu mkubwa, na kwa kusihi kusikokoma na kwa Imani isiyoyumba, alijua fika alichokuwa anakizungumza.[2] Alijua pia kwa uzoefu binafsi inamaanisha nini kuwaadikia vijana, kwa "wanafunzi katika shule zetu" na aliandika akisema "kwa marafiki zangu wadogo" na kwa Paul na Delbert na Anne na Mary na kwa vijana wengine, wakiwemo vijana wake, na wengine ambao Bwana angeweza kuwaweka akilini mwake.”

Alipowasihi hawa vijana kutoa mioyo yao kwa Kristo na kujitayarisha kwa ajili ya kurejea Kwake Masihi na kumtumikia, lazima alijiuliza mara mia kwa nini ni vijana wachache sana walionyesha nia ile ile ya kuongoa roho kama aliyokuwa ameonyesha

wakati yeye akiwa kijana. Rudi kwenye utoto wa Ellen. Nyemelea taratibu masaa ya usiku sana, nawe utamwona  Mrs Harmon au mama wa Ellen White, kisha sogea hadi hadi kwenye mlango wa chumba cha kulala cha Ellen pamoja na pacha wake Elizabeth na kusikiliza wanachosema.

Ungemsikia Ellen akinong'ona kwenye chumba chake "Ee Bwana Mungu, Martha bado hajawa tayari!" sauti ya Ellen inanong'ona chumbani. "Tafadhali, tafadhali nisaidie kujua ninachoweza kufanya ili kumsaidia Martha. "Tayari umenisaidia kuleta marafiki zangu kadhaa kwa Yesu," sauti inaendelea baada ya kutulia, "Rebecca, na Rachel, na Suzanne, na Viola na mumewe, na Anna na mumewe, na Lois, na Fannie, na Patience. Nina furaha sana kwa kila mmoja wao. Ninakushukuru, ninakushukuru sana. ... Nami nina furaha sana kwamba Yesu anakuja hivi karibuni.

Lakini Martha lazima awe tayari! Tafadhali, nisaidie kujua jinsi ninavyoweza kumsaidia." Bi Harmon (mamaye Ellen) anajua kwamba Ellen amesubiri Elizabeth apate usingizi na kisha atoke nje ya blanket lake na kupiga magoti karibu na kitanda. Pia anajua kwamba ana uwezekano wa kuendelea kusihi kwa njia hii usiku kucha, na kwamba kesho jioni ataomba ruhusa ya kwenda nyumbani kwa Martha na dada yake mkubwa Sarah, na kwamba hatarudi mpaka Martha ampe Bwana moyo wake, hata kama itachukua usiku wote. Juhudi na umakini huu unaweza kudhoofisha afya ya Ellen vibaya sana, lakini msichana huyu haonekani kujali, Ni kitambo kidogo tu watapokea miili mipya isiyoharibika yaani kwa yule ambaye yuko tayari, wakati Yesu anakuja.

Kwa namna hii, maombi ya Ellen kwa ajili ya Martha na wengine yanaendelea na mamaye, Bi. Harmoni anasikiliza bintiye akiomba, mpaka anachoka na anarudi hadi kwenye chumba chake mwenyewe, na anapiga magoti kuomba, na kulala.

Sura yetu ya mwisho ya kitabu hiki Ilisema machache kuhusu wanawake mashuhuri zaidi miongoni mwa Waadventista wote. Ellen G. White alikuwa na majukumu mengi kwa Kanisa la Waadventista Wasabato: Mwandishi, nabii, mshauri, mchangishaji fedha (Fund-raiser), na mwanzilishi mwenza wa taasisi. Lakini ili kumwelewa, ni lazima mtu ajue alikuwa mtu wa aina gani kimsingi. Muhimu kuliko yote Ellen White alikuwa mwongoaji wa roho, alitaka kuona watu wakiokolewa - si tu kama kijana, lakini maisha yake yote.

Miaka mingi baada ya ndoa yao, yeye na James walipotea mara moja msituni. Familia ya mlowezi mmoja iliwapa chakula na maelekezo ya njia ya kupitia, naye akawaachia machapisho na kuwaelezea imani yake. Muda mrefu baadaye, alikutana na watu wale wale tena kwenye mkutano wa kambi, wote wakiwa Waadventista waongofu. Katika kipindi kingine, akiwa amecheleweshwa kwa saa tano kwenye kituo cha gari-moshi, alifanya mazungumzo marefu ya kiroho pamoja na mwanamke

mmoja aliyekaa karibu naye, na kumpa mtu mwingine somo la Biblia. Akikarabatiwa saa yake huko Uswisi, alimwalika karani kijana kwenye duka la saa kumtembelea nyumbani kwake. Alipokuja, alipata uamuzi wake wa kuacha kazi yake, kwa kuwa ilihusisha kuvunja Sabato, na kutoa moyo wake kwa Bwana.

Hakuona kwa namna yoyote mawazoni mwake, kwamba huduma inapaswa kuwa ndani ya kanisa tu. Kinyume chake, mara nyingi aliona mahitaji ya kanisa yakimfungia mahali na kumzuia kutimiza wito wake wa kuongoa roho, na kumzuia kutimiza utume wake wa kweli. "Sijafika sehemu hii ya Australia," alisema kwa kundi la waumini wapya kwa unyenyekevu, "kutoa wakati wangu na nguvu zangu ili kuwafanya ninyi kuwa wachangamfu na kuwaweka katika hali ya furaha.... Dhamira yangu mimi, ni kwenda katika maeneo yaliyo nje ya nchi, kwa wale walioketi gizani, nao hawana nuru."[4]

Katika Kongamano Kuu la 1901 aliwaambia viongozi waliokusanyika, "Moyo wangu una shauku na kutamani wokovu wa roho."[5] Lakini tukirejea nyuma kwa dakika moja katika ujana wake, Ndani ya mwezi mmoja baada ya kufikisha umri wa miaka 17, Ellen Harmon alipata maono yake ya kwanza.[6] Katika maono haya watakatifu walichukuliwa kutoka katika hali ya kukatishwa tamaa hadi kwenye mti wa uzima. Aliimba "Aleluya" pamoja na malaika na akawa na shauku zaidi kuliko hapo awali kuona watu wakiokolewa. Alikuwa ameona mbinguni! Alijua kwa kuona kwamba hakuna mavazi ya kilimwengu, starehe, umaarufu, au ufikirio wa kifedha, ungeweza kulinganishwa na maisha katika Jiji la Mungu.

Lakini kuwa nabii mwenye kuleta roho za watu ilikuwa vigumu zaidi kuliko kuwa kijana mdogo mwenye kuleta roho kwa Bwana na kama nabii angeitwa kwa kazi ya ukomavu zaidi. Kama nabii Yohana angekuwa na furaha ya kutembelea mbinguni na kuzungumza na Yesu; lakini kama Isaya angehitajika pia "kuwaonyesha watu wa Mungu dhambi zao." Kama Yeremia wakati mwingine alilia kutopendwa kwake. Kama Paulo angelazimika kusafiri sana, mara nyingi katika hatari na usumbufu, na ndivyo ilivyokuwa.[7] Alipendwa na kuthaminiwa na watu wengi, alidhihakiwa na baadhi ya watu kama mshupavu, msumbufu, mwingiliaji mambo ya watu, au tapeli.

Mwanzoni Mungu alipomwagiza afanye dhambi ya mtu iwe wazi kwake, nyakati fulani alilihafifisha karipio hilo, na kuliweka kwa ulaini ili kulifanya lionekane kuwa lenye kukubalika zaidi. Kisha Yesu akatokea mbele yake kwa mguso mzito sana. Alisoma mahangaiko ya upendo katika uso wa Yesu na aliona kwamba ikiwa watu wataendelea kutenda dhambi kwa sababu tu alishindwa kuwarekebisha, basi hawa watu wangepoteza roho zao.[8] Ujumbe huu uligusa moyo wake. Alikuwa amesali usiku kucha kwa ajili ya watu na kisha akawasihi usiku kucha. Ikiwa kuwaambia dhambi zao ilikuwa muhimu kwa wokovu wao, angefanya hivyo bila shaka.

Hata hivyo, kusita kwake kulijitokeza mara kwa mara, hasa alipokuwa hajui jinsi ya kuwashawishi watu wagumu sana. Kwa mchungaji mmoja maarufu na aliyeheshimiwa lakini aliyekasirika kwa urahisi alikuwa akiendelea kuurekebisha ushuhuda wake mara kwa mara bila kumfikishia kwa wakati hadi akajikuta anafikisha ujumbe kwa kuchelewa wakati mchungaji akiwa kitandani mgojwa sana akisubiri mauti.[9]

Lakini kwa kawaida alishinda kusita kwake na kusambaza /kurithisha Neno la Mungu kama mjumbe Wake mwaminifu. Hakuna dhabihu iliyokuwa kubwa sana - ikiwa ilimaanisha roho zingeweza kuokolewa. Leo Ellen White anajulikana zaidi kwa vitabu vyake na alikuwa hodari. Alichapisha zaidi ya kurasa 40,000 za maandishi na zaidi ya kurasa 50,000 za barua na muswada/manuscript-maandishi ambayo yaliandikwa bila kuchapwa. Aliandika juu ya maadili, maisha ya familia, na theolojia; juu ya kanuni za elimu, usimamizi wa biashara, na afya; juu ya tafsiri ya historia na maelezo ya Maandiko; na mengi zaidi ya hapo.

Ili kupata wakati wa kufanya hivyo mara nyingi alikwenda kulala mapema na kuamka nyumba ikiwa tulivu, saa kumi na moja alfajiri, au saa tisa alfajiri, au hata saa saba usiku. Japokuwa anajulikana kwa ajili ya umaarufu wa vitabu vyake, Bibi White anastahili kujulikana zaidi kama mzungumzaji wa hadhara/umma.[10] Katika ujana wake mara nyingi alikumbwa na changamoto ya sauti kukwaruza ambayo kwa imani ingemwacha kwa ghafla na kwa namna ya ajabu, baada ya kuanza kuhutubia kutaniko. Jambo hili lilionekana tena mara nyingi katika maisha yake yote. Mungu angeweza kumponya moja kwa moja, lakini ni wazi alipendelea kutoa uthibitisho huu wa ukaribu wake aliposimama kuzungumza.

Ellen White aliishi kwa afya nzuri kadiri alivyoweza, kisha akamtegemea Mungu kufanya mengine. Angeomba, “Nimefanya yote niwezayo kufanya, Bwana, kwa kutumia njia Yako mwenyewe, na sasa ninaomba baraka maalum ambayo Wewe peke yako unaweza kunipa ili kunitegemeza.” Mara nyingi alimwambia James alipokuwa angali hai, "Laiti ningeweza kupata uhakikisho hapo awali, ingekuwa vyema kiasi gani kwangu!" Akajibu, "Mungu hajawahi kushindwa kukubariki wakati unaposimama kuzungumza; kwa hivyo vyovyote vile hisia zako zinavyoweza kuwa, lazima uweke imani yako Kwake, ukiiweka nafsi yako isiyojiweza juu ya ahadi Zake." "Hii nimejaribu kufanya," alisema. "Nimejifunza kwamba ni lazima tutekeleze sehemu yetu, tukishirikiana na Mungu. Bwana Anatoa nguvu kwa kila wajibu."[11]

Wakati mwingi wa miaka yake ya ukomavu Dada White alihubiri kwa sauti ya ajabu na yenye nguvu. Muda mrefu kabla ya uvumbuzi wa vipaza sauti aliweza kusikika kwa urahisi na umati wa watu elfu tano na zaidi ya mara moja kwa kumi na tano au ishirini elfu.[12] Mgonjwa katika Sanitarium ya Washington aliwahi kukaa kwenye kibaraza cha ghorofa ya pili (balcony) na kumsikia kwa uwazi alipokuwa akihutubia

hadhira ya mkutano wa kambi katika hema lililowekwa msituni karibu. Yeye hakupiga kelele.

Wasikilizaji waliokuwa mbele walifikiri alikuwa akizungumza nao tu. Hakuuelezea uwezo wake kama muujiza pia, ingawa alimpa Mungu utukufu. Badala yake, alifanya mazoezi ya usaidizi wa diaphragm ya kisayansi na alizingatia kwa uangalifu utamkaji na utengenezaji wa sauti. Lilikuwa jambo la kiroho kwake. Utoaji unaofaa ungeongeza ufanisi wake katika kuwasilisha ujumbe wa malaika wa tatu. Kupumua kwa kina kungeimarisha mapafu yake na kurefusha maisha yake ya huduma. Kuzungumza kwa usahihi kungemsaidia kuokoa roho zaidi. Alifundisha kwamba mtu yeyote angeweza kujifunza kuzungumza vizuri hadharani ikiwa alisoma na kufuata sheria zilezile alizozifuata.[13]

Watu waliomsikia walitoa maoni baadaye juu ya "usikivu wenye heshima" ulioonyeshwa na watazamaji wake, "usikivu wenye shauku ya hali ya juu," "usikivu unaofanya mtu kukosa pumzi," wa "ukimya wa kina" wa mkutano" ulifanya wao kuvutwa na maneno kama sumaku ivutavyo,” na "kimya chenye kicho" kilikuja kwa kusanyiko pale alipokuwa akiingia kwenye mimbari.” Tabia yake wakati akizungumza ilikuwa ya kutilia mkazo wa hatima na ya dhati lakini yenye tabasamu la kupendeza usoni mwake. Baada ya mahubiri huko Ulaya kutolewa kupitia mfasiri, watu hao, kwa kuwa hawakuweza kuzungumza Kiingereza, walimpa mkono kwa machozi ya shukrani na upendo wao papo hapo.

Mwandishi wa gazeti la Detroit Post alielezea mojawapo ya mahubiri yake ya Mkutano Mkuu huko Michigan kama tukio "la ajabu na la kusisimua.” "Ingawa ufasaha wake na nguvu za ushawishi zilijulikana sana na watazamaji," aliandika, "bado hawakuwa tayari kwa ajili ya wito wa kusihi wenye nguvu ambao haukuweza kujibiwa ambao aliutoa. Kwa hakika alionekana kuvuviwa alipokuwa akiwasihi wenye dhambi kukimbia dhambi zao. Athari ya hotuba yake yenye kufanya watu watekewe na namna yake ya kuitoa hii hotuba, ilikuwa ya kushangaza zaidi."[14] Maombi yake ya hadhara wakati mwingine yalikuwa na matokeo zaidi kuliko mahubiri yake.

Huko Colorado katika miaka yake ya themanini na zaidi, alisikika waziwazi kwenye mkutano wa uinjilisti wakati mvua ikipiga paa la  mabati kama vile kwaya.[15] Mwishoni alialika kila mtu kupiga magoti. Wapresbiteri, Wamethodisti, Wabaptisti, washiriki wa madhehebu mengi, walitokwa na machozi karibu mara moja na uaminifu mtamu wa maombi yake kwa niaba yao. Baharia mmoja wakati fulani alitoa maoni yake kuhusu sala yake, "Alimleta Mungu pale pale tulipoketi, na kutuwasilisha Kwake kwa ajili ya baraka Zake na sasa, mimi ni lazima niwe mtu bora zaidi."[16]

Mara moja moja, kwa wakati mzuri angeleta jambo la kuchekesha au kuchangamsha watu (humor). Alipokuwa akiongea katika kanisa dogo la Saint Helena Sanitarium katika siku zake za baadaye, mwanawe, W. C. White, alilala kwenye kiti chake nyuma yake kwenye jukwaa wakati mamaye akizungumza . Alipomwona mwanawe, Bibi White alisimama kwa muda na kusema, "Wakati Willie alipokuwa mtoto mchanga, nilizoea kumpeleka kwenye jukwaa na kumwacha alale kwenye kikapu kando ya mimbari, na hajawahi kuiacha tabia hiyo." Burudani (fun) ya Bi. White kuhusu mwanawe ilikuwa ucheshi (humor) wa "familia," na hii inatukumbusha kwamba kwa sababu ya kazi yake ya umma na kazi yake kama mama wa nyumbani, anayeitunza nyumba yake (ambayo sura hii ilianzia hapa) mara nyingi hupuuzwa.

Vitabu vyake Child Guidance, The Adventist Home, na Messages to Young People (Malezi ya Watoto, Nyumba ya Mwanamarejeo na Ujumbe kwa Vijana), vilikuja kutokana na uzoefu wake na pia kutoka kwa maono yake. Aliwaambia wazazi wasiwazomee watoto wao au kuwachapa kwa hasira bali watulie kwa saa chache kisha wawapeleke kando kwa ajili ya maombi (na kuchapwa ikibidi). Kabla hajatoa ushauri huu aliufanyia kazi-binafsi kwanza.[17]

Aliamini kwamba mama anayepika chakula chenye afya jikoni humtumikia Mungu kwa hakika kama vile mhudumu anayehubiri mahubiri kwenye mimbari,[18] na mara nyingi alitamani kwamba yeye mwenyewe angebaki nyumbani kumtumikia Bwana badala ya kuhitajika kwa kusafiri na kuhubiri sana.

Mtoto wake wa kwanza alipokuja, alifikiri kwamba sasa angeweza kukaa nyumbani kwa muda. Yeye na James walikuwa wamekutana wakati wa ziara za uinjilisti, na walikuwa wamesafiri karibu kila mara tangu wakati huo. Lakini Mungu alisema alimhitaji awashuhudie Waadventista waliotawanyika, na waliokuwa wanapambana na changamoto. Kwa kusikitisha, alimkabidhi mtoto wake Henry mdogo, kwa Stockbridge Howlands, akirudi kumwona na zawadi mara moja kwa mwaka kama Hannah alivyofanya katika Biblia.

Aliweka sheria ya kutolalamika kamwe kuhusu jambo lolote ambalo watu wasiokuwa wema walimfanyia; lakini alipokuwa mama kijana na kusikia watu wanasema kwamba ana bahati kwa sababu hakulazimika kukaa nyumbani na kubadilisha nepi za watoto, hakuweza kabisa kujizuia kulalamika.[19] Kwa sababu ya umashuhuri wake, pia mara nyingi hupuuzwa kwamba aliolewa na mtu maarufu pia![20]

Ijapokuwa Ellen White alimpa mumewe msukumo wa kuanzisha chapisho na kupata kuijua Sabato ya kweli ya  siku ya saba ya juma, Katika Nyumba ya uchapishaji ya Waadventista, ilikuwa ni Mzee White ndiye ambaye alifanya kazi karibu zote, kukusanya na kupanga malighafi/nyenzo na wafanyakazi.  Nyumba yake ya uchapaji na mashine vilisonga mbele na kukua na kuwa Taasisi ya Uchapishaji ya Review and

Herald, ambayo leo inaingiza takriban $20,000,000 kwa mwaka (Kiwanda hiki kilifungwa mwaka 2015 sasa ni Pacific Press ndiyo inafanya kazi, Ila Review and Herald ipo online, unaweza kuulizia jinsi ya kuwapata katika makao makuu ya kanisa).

James White pia alianzisha Pacific Press, shirika ambalo leo ni kubwa pia. Kwa nguvu aliunga mkono na kuongoza Taasisi ya Matengenzo ya Afya ya Magharibi (Western Health Reform institute huko Battle creek), ambayo ilikuwa katika Sanitarium kubwa ya Battle Creek. Alisaidia kuzindua Chuo cha Battle Creek na alikuwa mwenyekiti wake wa kwanza.[21] James White alikuwa mwandishi mwenye msukumo na mahiri, mzungumzaji mwenye ufanisi na ufasaha/umbuji, na rafiki mchangamfu. Pia alikuwa meneja bora. Wakati fulani katika mwaka (1869) alipokuwa mgonjwa sana na kushindwa kusimamia Review, shirika la uchapishaji lilipoteza $3,000. Mwaka wa kwanza alipoirudisha (1870) ilipata $7,000.[22]

Nyakati nyingine kufanya kazi kupita kiasi na hamu ya kupindukia ya kuona kazi imekamilika ilimfanya audhike kirahisi (irritable) na kuchukulia mambo kwa unyeti sana. Ugonjwa ulileta toba. Shuhuda ilikuja ya kukubali toba yake. Ilianza kwa maneno, "Nilionyeshwa katika maono, Desemba 25, 1865, suala la mtumishi wa Bwana, mume wangu, Eld. James 468 White."[23] Mtumishi wa Bwana, Mzee James White, alikuwa amekuwa mume wa Ellen kutoka Agosti 30,1846. Alikuwa amemwona miaka kadhaa kabla ya hapo wahudumu katika Portland, Maine, walipomwomba ahubirie mikutano yao wakati wa siku njema za Wafuasi wa Miller.

Hakumtambua hadi walipokutana huko Orrington, Maine, muda mfupi baada ya Bwana kumwambia asafiri na kuwaambia watu maono aliyompa. Walishiriki matukio mengi ya kuwatembelea Waadventista waliokata tamaa lakini hawakuwa na mawazo ya kuoana, kwa sababu walidhani Bwana angekuja upesi sana. Kwa Muda, Mwinjilisti White alitoa mwito binafsi kwa uamuzi wa kutaka kumwoa Ellen Harmon, alikazana sana, kiasi cha kumshawishi "ndipo tulifunga ndoa," Bibi White alisema miaka mingi baadaye, akiongeza kwa upendo, "Ninahisi kwamba yeye ndiye mwanamume bora zaidi aliyewahi kutembea kwenye hii ardhi!."[24]

Watu wengi walimfikiria vyema. "Yeye ni rafiki wa maskini kama wengi wanavyoweza kushuhudia kwa mioyo yenye shukrani," aliandika B. F. Snook mwaka wa 1863. Alisisitiza kuwalipa watu waliomfanyia kazi zaidi ya mishahara yao, huku akijilipa mwenyewe kiwango cha chini cha mshahara  kuliko ambavyo mshahara wake ungepaswa kuwa. Mara nyingi alirudisha pesa na riba ambayo ilikuwa imekopeshwa kwa Review bila riba. Mara moja yeye binafsi alimkopesha mchungaji maskini pesa bila riba yoyote ingawa alikuwa akilipa asilimia 10. Mara kadhaa alikataa michango ya watu kusaidia uchapaji, ikiwa aliona kuwa mtoaji alikuwa na wakati mgumu.[25]

Ili kuwa mkarimu sana, na pia ili aweze kumlipa mpishi na mwangalizi wa nyumba ambaye huduma zake ziliwezesha Ellen kuandika, kushauri, na kusafiri, alifanya kazi kwa saa nyingi za uchovu akinunua na kuuza vifaa vya kuandikia, vitabu, na mambo mengine; lakini watu wa kusaidiwa walikuwa wengi na daima ilionekana kuwa hakuna kiasi cha kutosha kutimiza huduma yake ya fadhila. Katika moja ya matembezi yao ya mwisho pamoja Mzee na Bibi White walijadili kisa cha mwanamke mwamerika mweusi aliyefanya kazi ya kuosha nguo za watu, ambaye walipita nyumbani kwake. "Mke wangu," Mzee White alisema, "lazima tumtunze mwanamke huyu maskini. Tusisahau, katikati ya masumbufu na shughuli zetu nyingi, watu maskini ambao wana taabu sana kuishi .... Kama ningekuwa na uwezo kwa amri yangu, Ningejenga nyumba zinazofaa ... kupangisha watu hawa maskini.[26]

James na Ellen walikuwa na watoto wanne, wote wavulana. Henry alirudi katika familia yao alipokuwa na umri wa miaka mitano kutoka mahali alipokuwa analelewa, "mvulana aliyefunzwa vizuri, na anayesali." Wakinda ndugu Howlands walikuwa wametenda kulingana na imani yao, walitegemeka kwa kutunza neno lao, kwa kumlea huyu mtoto.[27] Wavulana wa familia hii waliugua magonjwa ya kawaida yaliyokuwa yanawapata watoto wengi katika siku hizo za maarifa ya chini kuhusu tiba. Mama yao alijifunza mengi kuhusu tiba za nyumbani na thamani ya maji safi na hewa safi. Pia alijifunza maana ya kuombea mtoto anayechungulia kaburi, na kujua faraja inayotokana na kuwa na mwenzi mwenye imani sawa.

Mara nyingi watoto wao waliponywa kama jibu la maombi; walakini, wawili kati yao walikufa wakiwa wachanga—jambo la kawaida katika siku hizo. John Herbert, mtoto wa nne, alikufa alipokuwa na umri wa miezi mitatu. Henry aliishi hadi akatimiza umri wa miaka 16 tu. Alikuwa mvulana mchangamfu na mwenye sauti nzuri ya kuimba, na walimkosa sana (Sweet singer). Willie alionekana kuwa mvulana mwenye nia sahihi tangu mwanzo. Baada ya Mzee White kufa kwa malaria na kufanya kazi kupita kiasi mwaka 1881 akiwa na umri wa miaka 60, Ellen White alimwalika Willie White, kitinda mimba wake, kuwa mwandani/mwenza wake wa kudumu katika huduma.

Mungu alimwonyesha katika maono kwamba alikuwa amemtayarisha kwa ajili ya kazi hiyo kwa “roho ya hekima na akili timamu.[28] Kama baba yake, akawa msimamizi aliyebarikiwa kuifanya kazi hii kwa ufanisi. Ilikuwa Edson, mvulana aliyezaliwa wakati Ukweli wa Sasa ulipoanza, ambaye kwa miaka mingi alikuwa huzuni ya wazazi wake. Hata barua ambayo mama yake alimwandikia kabla tu ya kutimiza miaka kumi na sita haikumbadilisha sana. Labda hata alizidi kuwa mbaya.

Waumini wa Battle Creek walipobidishwa na dhamiri mnamo 1870 kuomba msamaha hadharani kwa kushindwa kuwaunga mkono Mzee na Bibi White kama walivyopaswa, Edson naye aliwasilisha ombi lake la msamaha. Inasikitisha kwamba ilimbidi kufanya

hivyo kutokana na hali ila ilionyesha kwamba moyo wake ulikuwa unaanza kuelekea kwenye njia sahihi. Ilikuwa vigumu kwa Edson kutulia. Alijaribu kwa mkono wake kuanza uchapishaji na akaanzisha kampuni yake ya uchapishaji kama baba yake, ingawa aliitumia kama biashara yake binafsi. Alitoa vitabu kadhaa vya nyimbo kwa kushirikiana na Frank Belden, binamu yake. Alijaribu tasnia nyingine pia katika upigaji picha wa kibiashara katika siku zake za majaribio. Na kwa muda alifanya kazi kwenye boti inayotumia mvuke katika mto. Ingawa siku zote alikuwa Mwadventista, aliona ni vigumu kujiweka wakfu kikamilifu kwa Bwana.

Kisha mara moja mambo yalibadilika, muda mfupi baada ya mama yake kuondoka kwenda Australia, Edson alijikuta na Bwana wake katika njia mpya.[29] Alikutana na shuhuda zilizopuuzwa ambazo Bibi White alikuwa ameandika akiita mtu kuinjilisha watu weusi wa Marekani Kusini (soma the Southern work, miongoni mwa Wamarekani weusi waliokuja kama watumwa). Shuhuda hizi zilisema kwamba watu weusi wanapaswa kufundishwa kusoma ili waweze kuelewa Biblia wao wenyewe, na kwamba zaidi ya yote wanapaswa kuchukuliwa kama watoto wa Mungu kabisa. Uzoefu alioupata Edson katika safu zake mbalimbali za kazi sasa ulijikita kwenye kusudi kubwa. Alitengeneza boti inayotumia mvuke, ambayo ingetumika kwenye mto, akaiwekea mashine ya uchapishaji mwishowe, chumba cha giza cha picha (dark room for negatives), kanisa, na makazi yake na wasaidizi wake. Kisha akaondoka kwenda kusini mwa nchi, huko Mississippi. Ili kufadhili mradi wake aliendeleza uuzaji wa kitabu chake cha kwanza cha Injili, kitabu cha shule ya msingi cha kujifunza kusoma kwa kutegemea Biblia, ambacho kilichapishwa kwa ajili yake huko Battle Creek.

Alitayarisha slaidi za picha ili zisaidie kuvutia wasikilizaji wasiojua kusoma na kuandika, na kwenye kiwanda chake kidogo cha uchapaji ndani ya mashua alichapisha vijuzuu. Haikuchukua muda, naye akawa anawafundisha watu weusi kusoma na kuielewa vizuri Biblia. Katika miaka mitano alianza makanisa hamsini! Mafanikio yake, kwa bahati mbaya, hayakupendwa na ulimwengu wote. Mzungu mmoja mwenye hasira alizuiwa kumpiga mmoja wa wasaidizi wa Edson ili amuue, ndipo mzungu aliyekuwa rafiki zaidi alipochomoa bunduki yake na kumlinda.

Kufikia 1900 ubaguzi wa rangi ulikuwa umeenea sana kiasi kwamba katika sehemu nyingi familia ya White hawakuweza tena kufanya kazi kwa usalama kwa ajili ya watu weusi. Kwa majaliwa na mipango ya Mwenyezi Mungu—hasa kupitia Edson White—Mungu alikuwa amewainua Waadventista weusi kuleta ujumbe wa malaika wa tatu kwa jamii yao wenyewe. Mashine ya uchapaji ndani ya mashua ya Edson ilihamishiwa kwenye banda la kuku na baadaye ikatumiwa katika Southern Publishing Association, huko Tennessee—Jumuiya ya Uchapishaji ya Kusini, nyumba ya tatu ya uchapishaji iliyoanzishwa na familia ya White huko Amerika.

Kitabu chake cha kwanza cha Injili kiliuza zaidi ya nakala milioni moja. Inasemekana kilikuwa kitabu cha kwanza cha aina yake katika nchi ya Marekani, kilikuwa na mchango wa kipekee kwa Waadventista katika kuwaendeleza Wamarekani weusi. Kama tulivyoona, miaka ya awali ya Bibi White ilitumika kusafiri na mume wake kuzunguka majimbo ya Kaskazini-mashariki. Mnamo 1853 walitembelea hadi magharibi mwa nchi na kufika Michigan, na mnamo 1855 walihamia Battle Creek. Safari zao zilienea zaidi katika Magharibi ya Kati, na kisha hadi Magharibi ya Mbali. Mnamo 1872 walifanya safari yao ya kwanza kwenda California, ambapo mnamo 1874 na 1875 walianza gazeti la Signs of the Times na Pacific Press.

James White alikufa mwaka 1881. Miaka minne baadaye Ellen White alisafiri kwa meli hadi Ulaya kama mmishenari kwa miaka miwili (Agosti 1885-Agosti 1887), akifuatana na mwanawe, W. C. White. Mnamo 1891 alianza safari kwenda Australia, akitumikia akiwa mstari wa mbele huko kwa miaka tisa. Aliporudi mwaka wa 1900, alifanya makazi karibu na Sanitarium ya Saint Helena, ambapo alinunua nyumba huko mashambani, "Elmshaven" kama ilivyoitwa, Ilikuwa kubwa vya kutosha kuwaweka makatibu muhtasi wake, na kuwapa malazi, idadi kubwa ya wageni waliofika mara kwa mara kutafuta ushauri.

Mwishoni mwa miaka yake ya sabini na themanini alisaidia kuanzisha taasisi ya Paradise Valley Sanitarium, Chuo cha Wainjilisti wa tiba (Medical Evangelists) huko Loma Linda (sasa ni Shule za Uuguzi na Tiba katika Chuo Kikuu cha Loma Linda), na Chuo cha Pacific Union, maili chache juu ya kilima kutoka nyumbani kwake. Katika makazi yake ya "Elmshaven" alikamilisha mfululizo wa vitabu vinne vya "Conflict of the Ages" na aliandika makala na barua nyingi zaidi ya kuandaa vitabu vingine saba ikiwemo (Wazee na Manabii, Manabii na Wafalme, Tumaini la Vizazi vyote, Matendo ya Mitume na Pambano Kuu).

Kutoka hapo mwaka wa 1909 alisafiri kwa treni hadi Washington DC, kuhudhuria kikao cha General Konferensi kwa mara ya mwisho, akawahutubia wajumbe kwa sauti yake ya kawaida iliyo wazi. Katika safari hiyo hiyo pia alirudi Portland, Maine, palipokuwa mahali ambapo palikuwa makazi yake wakati wa usichana, ambako alikuwa amengoja marejeo ya Yesu mnamo Oktoba 22, 1844, na alikuwa amepata maono yake ya kwanza wiki chache baadaye. Kama ajuza, aliendelea kufanya kazi kwa bidii kwenye vitabu na mawasiliano yake. Lakini katika saa zake za mapumziko alipenda kuwasimulia visa/hadithi watoto huku wakichana nywele zake, na wakimwimbia nyimbo za furaha kuhusu ujio wa pili wa Kristo, na kuwatembelea majirani zake katika Kristo.

Familia katika Bonde liitwalo Napa Valley zilimkumbuka kwa muda mrefu "yule mwanamke mzee mwenye nywele nyeupe, ambaye sikuzote alizungumza kwa upendo sana juu ya Yesu."[30] Alikuwa bado anatafuta kuongoa roho. Aliaga dunia,

akiwa mwenye ushindi katika imani, Ijumaa alasiri yenye jua, Julai 16, 1915. Maneno yake ya mwisho kwa mwanawe yalikuwa, "Namjua yule niliyemwamini."[31] Alikuwa ameona Waadventista Washika Sabato wakikua kwa idadi, kutoka watu wachache hadi 137,000.

Gazeti la New York Independent lilimheshimu likisema: "Aliishi maisha na kufanya kazi ya nabii wa (kike) anayestahili." kuonekana kwake mara ya mwisho katika kusanyiko ilikuwa kwenye ibada ya kanisa katika Chuo cha Pacific Union. Akiwa dhaifu huku akisaidiwa kusogea na wahudumu wawili kufika kwenye mimbari (baada ya kuanguka na kuvunjika paja.) Ujumbe wake siku hiyo ulikuwa changamoto kwa vijana wa Kiadventista kuamka na kumaliza kazi ya kuongoa roho, ili Yesu aje tena upesi.

*Vidokezo:*

*1. Ellen G. White, Letter 4,1865; manuscript release no. 224*

*2. Ellen G. White, Testimonies vol. 5, pp. 322, 323*

*3. The prayer and the names of persons are conjectural, based on Ellen G. White, Life Sketches, pp. 17-46. For the personal life of Ellen White see Arthur L. White, Messenger, pp. 99-127, and SDA Encyclopedia, art. "White, Ellen G."*

*4. Review and Herald, May 29, 1894, p. 348*

*5. General Conference Bulletin, 1901, p. 26*

*6. Ellen G. White, Early Writings, pp. 13-17. Note that the bottom paragraph on p. 17 begins a later vision about the new earth. Cf. Spiritual Gifts, vol. 2, p. 52*

*7. Among the dangers she faced while preaching were at least four physical attacks by deranged persons. One would-be assailant leaped at her from a balcony. In no case was she harmed. On each occasion she resumed her sermon after the briefest pause, apparently unruffled. 478 Horace J. Shaw, "The Speaking of Ellen White," pp. 509, 510.*

*8. Ellen G. White, Early Writings, pp. 76, 77; Life Sketches, pp. 90, 91*

*9. Ellen G. White, Letter 1, 1883*

*10. The chief study on Ellen White as a public speaker is Horace I. Shaw, "The Speaking of Ellen G. White" (Ph.D. dissertation, Michigan State University, 1959)*

*11. Manuscript 111, 1901, in Shaw, "The Speaking of Ellen G. White," pp. 495, 496*

*12. "The Eminent and Self-made Men of Michigan," in In Memoriam, A Sketch of the Last Sickness and Death of Elder James White" (Battle Creek, Mich.: Review and Herald Press, 1881)*

*13. Ellen G. White, Evangelism, pp. 665-670*

*14. Detroit Post, in Review and Herald, August 18, 1874, p. 68*

*15. Recollection of H. M. S. Richards, presented at a meeting at Andrews University, 1969*

*16. Shaw, "The Speaking of Ellen G. White," pp. 513, 628*

*17. Ellen G. White, Child Guidance (Nashville, 479 Tenn.: Southern Publishing Association, 1954), pp. 244-247*

*18. Ellen G. White, The Adventist Home (Nashville, Tenn.: Southern Publishing Association, 1952), pp. 231-239*

*19. Ellen G. White, Spiritual Gifts, vol. 2, pp. 88, 128, 129*

*20. SDA Encyclopedia, art. "White, James Springer"*

*21. Sidney Brownsberger, usually listed as the first president, served under White at first (See Vande Vere, Wisdom Seekers, p. 27)*

*22. The Battle Creek Church [of SDA], Defense of Elder James White and Wife (Battle Creek, Mich.: Steam Press of the Seventh-day Adventist Publishing Association, 1870), pp. 111, 112*

*23. Ellen G. White, Testimonies, vol. 1, p. 613*

*24. "Interview with Ellen G. White re Early Experiences"; manuscript release no. 310*

*25. Vindication of the Business Career of Elder James White (Battle Creek, Mich.: Steam Press of the Seventh-day Adventist Publishing Association, 1863) 480*

*26. In Memoriam, p. 55*

*27. Review and Herald, November 1, 1853, p. 133*

*28. Ellen G. White, Letter 125, 1898; cf. idem to F. M. Wilcox, in Jemison, A Prophet Among You, pp. 338, 339*

*29. See SDA Encyclopedia, art. "White, James Edson"; also Ron Graybill, E. G. White and Church Race Relations (Washington, D.C.: Review and Herald Publishing Association, 1970) and Mission to Black America (Mountain View, Calif.: Pacific Press Publishing Association, 1971)*

*30. Ella M. Robinson, "Stories of My Grandmother," Junior Guide, January 2, 1963, and "Hymns My Grandmother Loved," Youth's Instructor, May 22, 1951; Arthur L. White, Messenger, p. 108*

*31. Ellen G. White, Life Sketches, p. 449*

## SURA YA 26
## MAAZIMIO YA FURAHA, TAKATIFU NA YENYE AFYA.

Alikufa kwa Diptheria (dondakoo). Jessie Alvira, mwenye umri wa miezi 10 na siku 15. Huyu ni mtoto wa pili ambaye Bw. na Bibi Ross walikuwa wamempoteza ndani ya wiki moja kwa ugonjwa wa Diptheria... Tanzia iliyosomwa! Dorcas Z., mke wa Alfred Hurlburt, mwenye umri wa miaka 31. Anaacha mume na watoto wadogo watano wakiomboleza kifo chake……[1] Matangazo ya vifo vya watoto wachanga, vijana, na wazazi wachanga kwa ujasiri huacha wazazi kutabasamu kupitia machozi yao kwamba Yesu atakuja na kifo kitakoma.

Kwa takribani, kila toleo la Review ya karne ya 19 lilifafanua mara nyingi maelezo ya ugonjwa, kujitolea kwa marehemu kwa maneno, "amelala katika Bwana," kulingana na viwango vya kisasa, ambayo yote hayalingani na ukubwa wa vuguvugu la Waadventista - yanatusadikisha kwa urahisi kwamba jambo fulani halikuwa sawa.

Hakika Mungu angependelea watoto Wake wanaomwamini waishi, kamwe wasilale ndani ya Yesu wakiwa wadogo hivi. Nuru juu ya kazi ya Kristo katika Patakatifu pa Patakatifu sana, ikisimama karibu na Amri Kumi akizifuta dhambi, iliwasadikisha haraka waanzilishi wa Waadventista Wasabato kwamba Yesu alitaka wafuasi wake wawe watakatifu na kwamba kwa neema Yake wangeweza kushirikiana katika utakaso kwa kuzishika na kuzitii kanuni na sheria za maadili. Kufahamu kwamba

mbingu ilitayarishwa pia kuwasaidia kuwa na afya njema kupitia kuzishika sheria za asili za kimwili kulichukua miaka mingi kueleweka.

Tayari tumeona jinsi John Andrews na James White walivyokuwa wagonjwa nyakati fulani. Hawakuwa peke yao katika changamoto hii. Imesemekana kwamba kiongozi pekee ambaye alitunza afya yake vizuri sana alikuwa Joseph Bates. Alikuwa mgonjwa siku chache tu katika maisha yake yote, bila kuhesabu ugonjwa wake mfupi wa mwisho, yaani kabla tu ya kufa. Na alijua kwanini alikuwa na afya njema. Hakunywa chai au kahawa, alikula chakula kidogo cha mboga-mboga yaani vegeterian, na alitumia muda wake mwingi nje ya nyumba, akipata hewa bora, aliposafiri kuwaongoa wenye dhambi na kuwaongoza katika maisha ya utakatifu.

Lakini, unasema, lazima walijua jambo hilo la afya mbaya na kwamba tatizo lilikuwa wao wenyewe, kwa hiyo kwa nini hawakufanya jambo fulani kuhusu tatizo lao? Jibu ni kwamba  wao wenyewe hawakujua tatizo ni nini.[2] Hata madaktari siku hizo hawakujua ni nini kilisababisha ugonjwa huo. Makala katika shajara ya Angeline Andrews ni ya kuelimisha: "Carlos Beeman alikufa asubuhi ya leo karibia saa 11 asubuhi. Alikuwa na Diptheria/dondakoo kwa siku kadhaa. Jana alichanwa, chanwa na wembe ili atoke damu na ugonjwa utoke, na akafikiri angepumzika vizuri usiku (walichanwa chanwa na wembe watoke damu, wakifikiri ndiyo itasaidia ugonjwa kupona—blood letting—, hata Rais wa kwanza George Washington alikufa kwa matibabu haya ya blood letting-kuachilia damu itoke kwa uhuru, wakifiri inaondoa magonjwa).

Alikula chakula cha jioni kwa furaha.  Takriban saa tano usiku mke wake alimpa dozi ya morphine ambayo daktari alikuwa ameamuru apewe na Mara moja akalala, ambapo hakuamka tena.[3] Nadharia ya bakteria ilikuwa bado haijavumbuliwa katika siku hizo. Hadi kufikia miaka ya 1840 baadhi ya madaktari bado waliwatoa damu wagonjwa wao, wakiamini kwamba damu nyingi mwilini ilisababisha magonjwa kama Afyuni/bangi, calomeli, zebaki, arseniki, na strychnine zilitumika kwa kawaida "kuupunguza nguvu ugonjwa" katika miaka ya 1850. Kwa njia kama hizo, madaktari wanaweza kuwa wameua wagonjwa zaidi kuliko ambavyo wangekufa ikiwa wangeachwa peke yao bila madaktari.

Elimu ya Upasuaji ilikuwa bado changa, huku dawa za ganzi zikianza kutumika. Hakukuwa na mionzi ya Xray, antibiotics, au antihistamines. Kwa kweli hakuna mtu "aliyekwenda hospitali," hospitali zilikuwa hazipatikani kwa urahisi. Hata aspirini ilikuwa bado haijulikani. Watu wengi walikula na kunywa chochote kilichopatikana na kuwavutia, mara nyingi kwa kiasi kikubwa kilichowekwa viungo vingi mno kama pilipili, saa yoyote ya mchana au usiku. Hawakuona uhusiano wowote kati ya chakula chao na maradhi yao. Walifunga madirisha kwa kuhofia kuwa wangepatwa mafua au kikohozi (magonjwa ya mapafu). Walifunga mapazia ili kuepuka kupauka

kwa samani zao. Walioga mara chache tu. Walifanya kazi kupita kiasi au kufanya mazoezi ya chini kwa kadiri walivyojisikia au ulazima ulivyowagusa.

Karibu wote walishindwa kuona kwamba njia yao ya maisha ilikuwa njia ya kifo. Kama mmoja wao alivyokiri baadaye: "Tulikuwa na "mawazo machache juu ya maumivu ya kichwa, dyspepsia [kuvimbiwa tumbo], kichefuchefu, homa, n.k, tukiamini kwa sehemu kubwa kwamba haya yalikuwa nje ya uwezo wetu na ... yaliamriwa na mkono wa Mungu, yaani ni mapenzi ya Mungu-God's act."[4] Waadventista hawakuruhusu kamwe pombe, bila shaka, na katika miaka ya 1850 walitambua kabisa uovu wa tumbaku.

Zaidi ya muumini mmoja alitupa kiko chake cha tumbaku ndani ya jiko au kukizika kwenye mtaro. Lakini jaribio la wanandoa wanaopenda malumbano katika 1858, walitaka kulazimisha kanisa changa kuacha nyama ya nguruwe jambo ambalo lilileta Shuhuda kutoka kwa Dada White kwamba malaika walikuwa wakiongoza kanisa kwa kasi zaidi kuliko walivyokuwa wanadamu na hekima ya kuendana na wakati, na kwamba watu binafsi wanaotangulia mbele ya kanisa, inabidi warudishe hatua zao nyuma. "Mungu anaongoza watu,na sio watu wachache tofauti, hapa na pale, mmoja anaamini jambo hili, na mwingine lile," alisema.[5]

Suala kuu lililokabili harakati mnamo 1858 lilikuwa kuanzisha mfumo wa taasisi. Inaonekana Mungu alitaka ndugu waunganishwe kama timu, wakiaminiana katika nyadhifa za uongozi, kuunganishwa kama kitu kimoja katika Kristo, kabla hajaanzisha nuru hii zaidi. Lakini mara tu taasisi ya Konferensi Kuu ilipoanzishwa, malaika kwa hakika walielekezwa kwamba ilikuwa ni wakati wa kushughulikia jambo la ulaji nguruwe na kuzungumza kuhusu mwisho wa kula nguruwe, na kuhusu mambo mengi yanayohusiana pia.

Taasisi ilianzishwa siku ya Alhamisi, Mei 21, 1863. Nuru juu ya sheria za afya ilikuja katika maono siku kumi na tano baadaye, Ijumaa usiku, Juni 5, katika jumba dogo la shambani mwa Ndugu A. Hilliard kando ya barabara ambayo ingali inapita huko mpaka leo- Green meadowland katika eneo linalozunguka kwa upole magharibi mwa Otsego, Michigan, kama maili thelathini kaskazini-magharibi mwa Battle Creek.

Merritt Cornell na R. J. (si Horace) Lawrence walikuwa wakiendesha mikutano ya makambi katika kijiji cha Otsego. Mahudhurio yalikuwa hafifu, labda kwa sababu ya wasiwasi wa jumla juu ya Vita vya wenyewe kwa wenyewe-Civil War iliyohusu utumwa, ambavyo vingefikia kilele chake huko Gettysburg, mapema Julai. Familia ya White na wengine wachache waliamua kuendesha gari mwishoni mwa juma ili kwenda kusaidia kuhubiri na kuwachangamsha makutano waliohudhuria. Walifanya ibada ya machweo katika eneo la Hilliard.

Karibu na mwisho wa msimu wao wa maombi, Ellen aliweka mikono yake juu ya James na kumsihi Mungu kwa ajili ya afya yake. Mara moja alitoa mshangao wake wa kusisimua, "Utukufu! Utukufu! Utukufu!" maneno ambayo yalitangaza maono mengine. Kundi hilo lilichukua viti vyao na kusubiri matokeo. Dakika arobaini na tano baadaye, baada ya maono hayo kuisha na kushusha pumzi ndefu, walimtaka aeleze alichoonyeshwa lakini alichoweza kusema kilikuwa cha ajabu sana, nao wasingeweza kuelewa yote kwa  mara moja. Maono yalijumuisha orodha pana ya vitu.

Ripoti ya Ellen White iliyoandikwa wakati fulani baadaye,[6] na ikiwezekana kuongezwa na maudhui ya maono yaliyofuata, ilianza na maelezo ya Adamu na Hawa katika uzuri wao wa Edeni. Ilishutumu kwa dhati kabisa "chakula cha wanyama" (nyama) kama sababu kuu ya kuzorota kwa jamii ya wanadamu. "Nyama ya nguruwe" ililaumiwa haswa, lakini aina zingine zote za nyama pia zililaumiwa. Maono hayo yalizungumza dhidi ya utumiaji wa vinywaji vyenye kileo, viungo (pilipili na vyote vinavyokera tumbo), na vitu vya sukari vilivyojaa virutubisho visivyo muhimu—Keki, maandazi, halua, kalimati, vitumbua.

Tumbaku ililaaniwa kama "sumu ya aina ya udanganyifu na mbaya zaidi kama kansa tu," na chai na kahawa, kuwa na athari "sawa na zile za tumbaku" lakini kwa kiwango cha chini. Kula kupita kiasi hata chakula kizuri, na vitafunio kati ya milo au kabla tu ya kwenda kulala, kulionyeshwa kuwa jambo lisilofaa kabisa kwa afya. Kufanya kazi kupita kiasi kulionyeshwa kama uovu mkubwa. Na kwa ajili ya tiba/matibabu ya magonjwa, Ellen White aliagizwa kugonga kengele ya tahadhari dhidi ya matumizi ya dawa za hospitali "dawa/prescription" - arsenic, strychnine, calomel, nk – kama jinsi neno lilitumiwa siku hizo.

Kujiepusha na vyakula, mazoea, na maagizo haya yasiyo ya hekima bila shaka kungesaidia mwanadamu yeyote kuishi vizuri zaidi; lakini kulikuwa na ushauri wa upande mzuri pia: kunywa maji mengi, kufanya mazoezi mara kwa mara nje ya malango kwenye hewa safi, kuleta jua na hewa safi ndani ya nyumba, na kuoga kila siku. Yote haya yalikuwa ya busara! Ni vigumu leo kuelewa kwa nini hakujua jinsi ya kuielezea njozi hii mwanzoni. Si kwamba kila kitu alichoona katika maono yake juu ya maisha yenye afya kilitambulishwa kwanza kwa ujuzi wa wanadamu kupitia mafunuo yake! Waadventista  hawatoi dai kama hilo.

Jarida la Dr. Russell T. Trail la Water Cure Journal lilikuwa likisomwa na baadhi yao kwa miaka mingi (tiba ya maji, au uponyaji wa maji), na angalau John Loughborough, Annie Smith, J. P. Kelloggs, na J. N. Andrews walifahamu kwa kiasi fulani "mbinu za busara" za tiba ya maji (au "hydrotherapy"). Hata Familia ya White walikuwa wamejaribu matibabu machache ya maji na kwa muda walikuwa

wameacha madirisha yao wazi usiku. James White alikuwa ameanza upya kuchapisha mfululizo wa nakala kuhusu afya katika gazeti la Review.

Athari za kiafya za kukanda mwili kwa maji ya moto na baridi, moto kisha baridi kwa mara kadhaa (hot and cold fomentation), baada ya yote, tiba hizi zilijulikana sana na kuthaminiwa sana wakati wa utawala wa Kirumi, mamia ya miaka kabla! Arnold wa Villanova, ambaye tulikutana naye wakati wa kujadili siku 2300, alifundisha tiba ya maji na mboga-mboga (vegeterianism) katika jumba la papa la Avignon, Ufaransa, katika karne ya 15, na Luigi Cornaro alifundisha mawazo sawa huko Italia katika karne ya 16. Mashauri ya John Wesley kuhusu afya yaliheshimiwa na wafuasi wake katika karne ya 18 na mwanzoni mwa karne ya 19.

Hata katika vuguvugu la Wafuasi wa Miller, Dr. L. B. Coles alieleza mawazo mengi, yaliyofanana na yale Ellen White aliyoyaeleza baadaye; na hata hatujamtaja mla mboga-mboga (vegeterian) maarufu Sylvester Graham. Kwa kifupi, kupitia ushawishi wa sauti nyingi za watu wa awali na wa kisasa, tiba ya maji, mboga-mboga —vegeterianism, matumizi ya mkate wa ngano isiyokobolewa, na matengenezo mengine mengi ya afya yalikuwa yamepata wafuasi katika Amerika kabla ya 1863. Ellen White alipoanza kusoma kwa upana zaidi juu ya somo hili baada ya maono yake ya 1863, alivutiwa na ulinganifu kati ya kile alichokuwa akisoma na kile alichokuwa ameonyeshwa, na katika kitabu chake, “How to Live—jinsi ya kuishi,” alichapisha idadi ya makala za wanamatengenezo wengine pamoja na sura za makala alizoziandika mwenyewe.

Ni dhahiri alitarajia kwamba kufanana kungekuwa kama aina ya uidhinishaji katika kusaidia watu kukubali maono yake. Lakini bila maono muundo haukuwa wazi. Ujuzi ambao Waadventista mmoja mmoja walikuwa wameuchukua ulikuwa umegawanyika kidogo. Na pamoja na mawazo mengi mazuri yaliyochochewa na wanamatengenezo wa kitaalamu kulikuwa na mawazo mengi, yaliyotetewa kwa bidii sawa na kuonyesha Ukweli, kwamba tangu wakati huo sayansi ya kisasa imethibitika kuwa ya uongo. Hata Dr. Trail, ambaye alikuwa na hekima ya mbingu katika tiba kwa njia ya maji na chakula bora, alipiga kabisa marufuku chumvi na sukari juu ya sababu kwamba chumvi ilikuwa "sumu ya madini-mineral poison" na sukari, "sio chakula kabisa."[7]

Ellen White, akitegemea mafunuo yake, aliepuka mitego kama hiyo. Madai ambayo Waadventista Wasabato hutoa kwa ajili ya maono ya afya ya Ellen White ni kwamba:

(a) Maono haya yalitoa mapendekezo vyakula vizuri na taratibu nzuri tu, na matokeo ya kupuuza au kuonya dhidi ya mambo mabaya, na

(b) Yalitoa msukumo wa kidini wenye akili, ufaao, wenye uwiano katika kuwaelekeza mamilioni kwenye msawaziko wa kuzingatia afya bora, kupitia afya bora na kwenda kwenye ushindi mkubwa zaidi wa kiroho.

Akiongea na Waadventista Wasabato kama mmoja wa wainjilisti na mwanatheolojia wao mashuhuri, J. H. Wagoner mapema mwaka 1866 alitoa hoja kwamba "hatudai kuwa waanzilishi katika kanuni za jumla za matengenezo ya afya. ... Lakini tunadai, "aliendelea, "kwamba kwa njia ya chaguo la Mungu," maono ya Ellen White yahusuyo "kanuni za afya yamefunua kwa uwazi zaidi na kwa nguvu zaidi, na hivyo kuleta matokeo makubwa," na kurithishwa kwa ujumla kwa kanuni hizi na Waadventista Wasabato"ambako hatukuweza kuitazamia kwa njia nyingine yoyote." Maono hayo, Wagoner aliendelea, "Yamemweka simba aliye hai na mwenye afya katika kiwango cha zile Kweli kuu za ujumbe wa malaika wa tatu" kama "njia ambayo kwayo watu wanyonge wanaweza kufanywa kuwa na nguvu kushinda, na kupata sifa na stahiki kwa ajili ya kutwaliwa kwenda mbinguni.[8]

Katika istilahi za wakati huo, mtindo mpya wa maisha uliitwa "health reform— matengenezo ya afya." Neno "Reform" lililomaanisha Matengenezo lilikuwa maarufu. Marekebisho mengine mengi yalikuwa yakitetewa au yalikuwa yakifanyiwa promosheni hivi karibuni huko Amerika Kaskazini: matengenezo au mageuzi ya magereza, matengenezo ya nyumba za kuhifadhi wagonjwa wa akili, matengenezo ya kilimo, matengenezo ya elimu, matengenezo ya ndoa, na mengineyo. Ilikuwa ni "Enzi ya Matengenezo," wakati ambapo Horace Greeley aliweza kuandika, "Kutokuwa mwanamatengenezo sio kuiishi ile Kweli." Kama matengenezo ya afya yangekuja nuruni mwa watu karne moja baadaye, katika miaka ya 1960, "mageuzi" yangeonekana kama "mapinduzi," na dhana nzima kama "mapinduzi ya afya."

Ni dhahiri ilikusudiwa na Bwana kubadilisha maisha ya watu kuwa bora, kuwasaidia kuwa na afya njema na watakatifu zaidi, na hivyo kuwa na furaha zaidi pia.

*Vidokezo:*

*1.Slightly adapted from Review and Herald, June 30, 1863, p. 39, and June 23, 1863, p. 31*

*2. Many matters dealt with in this chapter have been presented earlier in Dores Eugene Robinson, The Story of Our Health Message (Nashville, Tenn.: Southern Publishing Association, 1943, 1955), and Ellen G. White Estate, A Critique of Prophetess of Health (Washington, D.C.: Ellen G. White Estate, 1976)*

*3. Angeline Andrews, Diary, entry for September 14, 1860*

*4. J. N. Andrews, in Ellen G. and James White, Christian Temperance and Bible Hygiene. (Battle Creek, Mich.: Good Health Publishing Co., 1B90), p. 263. Cf. J. N. Andrews to James White, February 1877*

*5. Ellen G. White, Testimonies, vol. 1, p. 207*

*6. Ellen G. White, Spiritual Gifts, vol. 4a, pp. 494 120-151*

*7. R. T. Trall, "Hog Milk for Humans," Health Reformer, October 1869, p. 76, in Ellen G. White Estate, "Ellen G. White and Health Reform" (Washington, D.C.: Ellen G. White Estate, 1975), p. 32*

*8. Review and Herald, August 7, 1866, pp. 76, 77*

## SURA YA 27
## ZAWADI YA KRISMASI

Mwaka 1865 Msisitizo mpya wa afya kwa kweli ulikuwa ni "fitness revolution-mapinduzi ya afya imara," au "mapinduzi ya utimamu wa mwili," lakini yalikusudiwa kutimiza zaidi ya kujiboresha mwenyewe au maboresho binafsi. Thamani yake ilikuwa katika kuwasaidia watu kujisikia vizuri, si tu ili wawe wazuri bali pia ili waweze kufanya mema.[1] Ilihusiana moja kwa moja na misheni ya kanisa kupeleka

injili kwa "miji yote, na katika vijiji vyote," ili kuuambia ulimwengu. Matengenezo ya afya yalikuwa kwenye mzizi wa "kazi ya umishenari wa tiba."

Kazi ya umishenari wa tiba katika harakati ya Waadventista Wasabato imekuwa mambo mengi kwetu kama waamini. Kwa upande mmoja ni chuo cha tiba kilichoidhinishwa kisheria (accredited) kinachotoa madaktari walio na utaalam mbalimbali. Kwa upande mwingine ni mlei wa Kikristo anayemtendea jirani yake wema kwa matumaini ya kumwondolea dhiki yake na kumwongoza kwa Kristo—(huduma isiyo na ubinafsi-disinterested benevolence, neno lililoanza kutumiwa mwaka 1897). Bibi White alifanya mazoezi ya kazi ya aina hii kama kazi ya umishenari wa tiba muda mwingi wa maisha yake, mara kwa mara akiwapeleka wagonjwa kuwapa watoto wao matibabu ya nyumbani au kuwaletea chakula cha kuvutia kwa watu wazima ambao hawakuwa wanakula vizuri au walikosa hamu ya kula.[2]

Mnamo 1902 aliandika, "Tumefika wakati ambapo kila mshiriki wa kanisa anapaswa kushikilia kazi ya umishenari wa tiba."[3] Wangeweza kufanya hivyo, alieleza katika makala mbalimbali na shuhuda, kwa kuwafundisha watu jinsi ya kupika na kuvaa kwa akili na jinsi ya kutoa tiba rahisi nyumbani kama vile tiba ya maji (hydrotherapy); pia kwa kusali nao walipokuwa wagonjwa.

Katika Mkutano Mkuu wa General Konference wa 1901 alihimiza kwamba kazi ya umishenari wa tiba na kazi ya umishenari ya injili "kamwe, haziwezi kutenganishwa.[4] Kwa ufupi, kazi ya umishenari wa tiba ni injili kwa vitendo, upendo kwa vitendo, kumsaidia mtu kwa uhalisia kwa matendo. Ni kuwatendea wengine wema katika kuonyesha upendo wa Mungu. Ni fadhili zinazohusisha akili, na zinazoelekezwa kuwasaidia watu si tu kukabiliana na hali ya dharura ya ugonjwa au umaskini bali pia kuishi maisha bora zaidi hata baada ya hapo, naam uzima wa milele. Na lengo lake kuu ni kuwafanyia wengine wema mkuu na wa hali ya juu kabisa (ultimate good); yaani, kuwaleta kwa Kristo.

Muhimu kama vile huduma za Sanitarium—nyumba za afya za tiba rahisi, hospitali, na vyuo vya tiba ni wazi vinafanya kazi ya umishenari wa tiba, sio sifa muhimu zaidi za programu. "Si taasisi nyingi, majengo makubwa, au maonyesho makubwa ndiyo ambayo Mungu anataka, lakini tendo la mapatano/maelewano la watu wa kipekee, watu waliochaguliwa na Mungu na wa thamani. Kila mtu anapaswa kusimama katika sehemu yake na mahali pake, akiwaza, akizungumza na kutenda kupatana na Roho wa Mungu."[5]

Nuru hii mpya, kwa bahati, ilithibitisha kuleta manufaa maalum kwa Ellen White na familia yake mwenyewe. Kwa mfano, miaka michache kabla ya kifo chake akiwa na umri wa miaka 87—jambo ambalo halikuwa baya kwa mtu ambaye, akiwa na miaka

kumi na saba, alikuwa amepewa miezi mitatu ya kuishi—Arthur W. Spalding, msimuliaji wa visa na mwanahistoria, alipokuwa akitembelea "Elmshaven," nyumbani kwake Ellen huko California, alitoa ofa mwishoni mwa mahojiano kumsaidia kupanda ngazi. "Oh, hapana asante," alijibu kwa msisitizo. "Mimi nina uwezo mkubwa wa kupanda ngazi peke yangu. Kwani, mimi ni mwepesi kama nilipokuwa msichana." "Kama nilipokuwa msichana? La!" Alishangaa. "Sipaswi kusema hivyo! Nilipokuwa msichana, nilikuwa mgonjwa na dhaifu na mwenye afya mbaya. Lakini sasa Bwana amenifanya kuwa mzima na mwenye nguvu, na mimi ni bora, bora zaidi, kuliko nilipokuwa msichana."[6]

Miaka ya mapema katika ndoa yao yeye na James waliteseka zaidi kwa ugonjwa wao, kwa kuwa walifanya kazi kwa bidii sana, walilala kidogo sana, na walikula kidogo sana. Walifanya hivyo kwa sababu waliona mzigo wa kazi hiyo na kupokea msaada mdogo sana kutoka kwa kundi lililotawanyika. Baada ya muda walikuja kuona kwamba Mungu hakutarajia dhabihu hizo zilizopitiliza kiasi.[7] Kando na hayo, Ellen alipatwa na magonjwa mengi zaidi kuliko kawaida yake kwa sababu, kama mjumbe wa pekee wa Mungu, yeye pia alikuwa shabaha iliyochaguliwa na Shetani. Alijifunza hili hasa kuhusiana na maono ya "Pambano Kuu" ya 1858 huko Ohio.[8]

Katika miaka yake ya awali mara nyingi aliponywa papo hapo. Katika miaka yake ya baadaye alidumisha imani yake wakati ambapo nyakati fulani Mungu alichagua kutotenda muujiza. Baadhi ya vifungu bora zaidi kutoka katika kitabu cha Tumaini la Vizazi Vyote viliandikwa alipokuwa "akimtegemea Mungu alipokuwa akiteseka" kutokana na ugonjwa wa yabisi-kavu huko Australia. Njozi ya matengenezo ya afya ya Juni 5, 1863, haikumpa afya bora bila yeye kufanya mabadiliko makubwa katika njia yake ya maisha. Alikuwa mla nyama nyingi, na hakuweza kustahimili ladha ya mkate wa kahawia isiyokobolewa (brown bread). Lakini alitaka sana mwili wenye afya ili amtumikie Mungu kwa matokeo yenye ufanisi zaidi, naye akaamua kutii.

Alitayarisha chakula cha mboga-mboga na kuoka mkate wa ngano isiyokobolewa. Lakini vyakula hivi vilionekana kumchukiza sana kula, maana alifikiri mkate wa ngano isiyokobolewa haukuwa mtamu. Na hivyo, alipokuwa akisimulia hadithi mwenyewe, alikunja mikono yake kwenye mapaja yake, karibu na tumbo na kusema, "Tumbo langu, wewe unaweza kusubiri mpaka uweze kula mkate huu usiokobolewa. Mimi nitakula chakula rahisi, au sitakula kabisa."[9] Baada kukosa MLO wa pili au wa tatu angeweza kula. Na huko baadaye alibakia kuwa mlaji wa mboga-mboga maisha yake yote, isipokuwa pale alipokula nyama mara chache sana, hasa wakati wa kusafiri, hadi 1894. Baada ya 1894 hakula nyama tena katika miaka ishirini na moja iliyobaki ya maisha yake hata akiwa safarini na hii ni baada ya kushawishika kutokana na nuru aliyopokea kwamba haikuwa busara kula nyama.[10]

Mzee James White alichaguliwa kuwa mwenyekiti wa Konferensi Kuu mwaka wa 1865. Vita vya wenyewe kwa wenyewe vilikuwa vinakaribia mwisho na hivyo pia, kwa wakati huo, alikuwa amehifadhi nguvu zake kwa namna ya ajabu. Kiharusi kilimfanya apooze kiasi. Wazee Loughborough na Uriah Smith pia walikuwa wagonjwa kwa wakati mmoja, na pamoja na Familia ya White walifunga safari yao hadi "Nyumbani kwetu Hiffside," kituo cha afya kinachoendeshwa na Dk. James C. Jackson na kujengwa kando kabisa ya kilima huko Dansville, New York. Familia ya White walijua vya kutosha sasa kuhusu kutotegemea madaktari wa kawaida, na Dk. Jackson alitoa matibabu bora zaidi ya maji na jua yanayopatikana nje ya mji.

Uriah Smith alipona baada ya muda mfupi, na Loughborough pia alikuwa mzima muda si mrefu kiasi cha kutosha kurejea kazini. Lakini James White, ambaye hali yake ilikuwa mbaya zaidi tangu mwanzo maendeleo yake yalikatisha tamaa. Zaidi ya hayo, Ellen White alizidi kuwa na wasiwasi kuhusu baadhi ya mbinu za Dk. Jackson. Dk. Jackson aliwataka wagonjwa wake wapumzike kwa kucheza dansi na kucheza karata, na akawaambia waondoe akili zao mbali kabisa na dini au mambo yoyote ya Biblia, na wasifanye kazi yoyote. Kwa mtu mwenye kanuni za hali ya juu, mwenye bidii, mwenye dini kama Mzee White hii ilikuwa mabadiliko ya kutisha sana.

Katikati ya dhoruba ya Desemba Familia ya White waliondoka, wakitumaini kwamba angepata nafuu haraka zaidi nyumbani kwa marafiki wengine huko Rochester. Baada ya wiki mbili za maombi maalum kwa niaba ya Mzee White, waumini wa Rochester waliiadhimisha Desemba 25, Siku ya Krismasi, 1865, ikiwa ni siku kamili ya kufunga na kuomba kwa ajili ya kurudishiwa kwake afya. Mungu alijibu kwa kuwapa zawadi ya ajabu ya Krismasi. Katika maono ya siku hiyo Ellen White alionyeshwa kwamba tiba ya kupumzika tu-bila-dini au mionjo ya kiroho ilikuwa mbaya kabisa, na kwamba Waadventista wanapaswa kuanzisha taasisi yao ya tiba ya maji na mboga-mboga ambapo kozi ya matibabu iliyosawazishwa ipasavyo na inayomcha Mungu (water treatment and vegeterian diet) ingeweza kupatikana si kwa Waadventista tu bali kwa umma kwa ujumla, na ambapo hawakuweza tu kutibiwa kwa tiba zenye busara bali pia kufundishwa “jinsi ya kujitunza na hivyo kuzuia ugonjwa."[11]

Matokeo mawili ya haraka ya maono haya makubwa ya "taasisi ya afya" yalikuwa (1) maono ya kutia moyo katika Familia ya White kuhusu kile ambacho mwanamke anaweza kufanya katika kumuuguza mume mgonjwa.[12] Na (2) uanzishwaji wa Taasisi ya Matengenezo ya Afya ya Magharibi (Western Health Reform Institute) katika nyumba ya zamani iliyokarabatiwa huko Battle Creek mwaka wa 1866. Mtu ambaye alifanya mengi zaidi kuijenga Taasisi hii ya Matengenezo ya Afya, na, kwa hakika, mwanamume aliyehusika katika kukuza matengenezo ya afya katika sehemu kubwa ya dunia kwa miaka mingi iliyofuata, alikuwa ni daktari mfupi (5'4"), mwenye maamuzi thabiti, na mahiri kwa jina la John Harvey Kellogg. Huyu anastahili kupata muda wetu mchache ili kuangalia kazi yake.[13]

John Harvey Kellogg alizaliwa katika familia ya watoto 16 katika mwaka huo huo wa 1852, ambao baba yake, J. P. Kellogg, aliikubali imani ya Waadventista Mwaka 1855. Bw. Kellogg alitoa robo ya fedha zilizohitajika ili kuweka kiwanda kidogo chenye mashine za mkono, za kuchapisha magazeti hapo Review and Herald, na mwaka wa 1856 alihamisha familia yake hadi Battle Creek, ambako alifungua kiwanda cha kuchapisha vitabu kwa mkono na baadaye alianzisha duka la ufagio.

Katika umri wa miaka kumi John Harvey alikuwa kazini katika biashara ya baba yake na mwaka 1866, akiwa na umri wa miaka kumi na minne, alikuwa mhakiki wa makala kwa ajili ya Jumba la uchapishaji la Waadventista Wasabato. Huu ulikuwa mwaka ambapo Taasisi ya Matengenezo ya Afya ya Magharibi ilizinduliwa, huku J. P. Kellogg akitoa mchango wa kwanza na mkubwa zaidi wa $500 kwa ajili ya taasisi hiyo. Baba Kellog na mwanae John, hawakuona mbele kuhusu kazi ambayo John angekuja kuifanya kupitia taasisi hiyo katika siku za mbele. Matarajio yake wakati huo yalikuwa kuwa mwalimu wa shule.  Kwa hakika, John alifundisha shule kwa mwaka mmoja; lakini mustakabali wake ulikuwa mahali pengine.

Mnamo 1872 alianza kusomea udaktari katika Chuo cha Dr. Trall's Hygeio Therapeutic College huko New Jersey, na baadae kidogo akahamia chuo cha tiba huko Ann Arbor, Michigan, na hatimaye Chuo cha tiba cha Bellevue huko New York City, chuo bora zaidi katika taifa. Kwa namna fulani Mzee James White alifanikiwa kupata dola 1000 za kumsaidia John katika masomo, na kijana Kellogg alitumia sehemu kubwa ya fedha hiyo kuajiri wataalamu wa kitivo cha afya kumfundisha kwa faragha nje ya darasa. Hamu yake ya kusoma haikutosheka/haikukinai. Akiwa na shahada ya juu ya Utabibu, Dk. Kellogg alirudi Battle Creek mwaka 1875 na mwaka mmoja baadaye akafanywa kuwa msimamizi wa tiba katika Taasisi ya Matengenezo ya Afya ya Magharibi. Kulikuwa na wagonjwa ishirini waliosajiliwa wakati huo.

Habari zilipoenea kuwa daktari kijana, wa miaka ishirini na minne anachukua nafasi hii ya usimamizi, inasemekana wagonjwa sita kati ya wale waliokuwa wamelazwa waliinuka na kuondoka. Vitanda vyao vitupu vilijazwa kwa upesi. Wagonjwa wengi sana walimiminika Battle Creek kuchukua fursa ya ujuzi wa kipekee wa  mkurugenzi huyu mpya wa tiba na washirika wake waliochaguliwa kwa uangalifu kwamba karibu mpango wa haraka wa ujenzi endelevu ulihitajika katika miaka ishirini illiyofuata. Jina lilibadilishwa haraka na kuwa Battle Creek Medical and Surgical Sanitarium, ikafafanuliwa kama mahali ambapo watu "hujifunza kuendelea kuishi vizuri-kwa afya njema."

Kufikia wakati majengo yake makuu mawili yalipochomwa moto mnamo 1902, hata hiyo ilikuwa na vyumba vya wagonjwa mia kadhaa (labda elfu au zaidi). Dk. Kellogg alikuwa na kipaji na akili mahiri. Daima aliendana na maendeleo ya kitiba kwa kusoma majarida ya hivi karibuni katika lugha mbalimbali na kwa kusafiri mara kwa

mara hadi Ulaya ili kujifunza chini ya madaktari wakuu huko. Aliandika vitabu hamsini kadhaa vikiwa vikubwa na vya tiba. Alianzisha chuo cha tiba-Medical School. Alifanya oparesheni nyingi (upasuaji), akifunga majeraha ya upasuaji kwa uzuri sana kiasi kwamba "kovu la Kellogg" likawa alama mahususi.

Daima alikuwa na soko la kutoa mihadhara ya umma, akiitwa huku na kule. Aligundua aina nyingi za vifaa vya tiba, kadhaa kati ya hivi, bado kuna vingine ambavyo vinatumika ulimwenguni kote. Na alifanya ubunifu wa vyakula vingi, kati ya hivyo, vile ambavyo ndiyo maarufu zaidi, ni kama cornflake, alibadilisha mazoea ya mlo wa kifungua kinywa cha taifa na kumfanya kaka yake Will (W. K. Kellogg) kupata utajiri mkubwa baada ya kuasili utengenezaji wake wa cornflakes mnamo 1906.

Madai kwamba daktari huyo ndiye aliyeanzisha matumizi ya siagi ya karanga yanatia mashaka, hasa kwa vile Wahindi wekundu katika nchi za Amerika ya Kusini walikuwa wamefurahia kwa muda mrefu kuweka goober yaani siagi ya njugu kwenye chakula ambayo kiuhalisia haina tofauti sana na siagi ya karanga (peanut buttera). Lakini hakuna shaka kwamba Kellogg alichangia kwa kiasi fulani kukuza umaarufu wa siagi yetu ya karanga kwa ujumla-(peanut butter).[14] Na pia inaonekana kuwa kweli kwamba alibuni neno "Granola," ambalo lilitumika sana katika miaka ya 1970. Baada ya moto mbaya Mnamo Februari 1902 Dk. Kellogg alijenga upya jumba la tiba rahisi liitwalo Sanitarium.

Hasa katika miaka ya 1910 na 1920 ilipata neema ya kutembelewa na wengi. Rais Coolidge, Henry Ford, Percy Grainger (mpiga kinanda), na Homer Rhodeheaver (mwandishi wa nyimbo za injili) walikuwa wachache tu, miongoni mwa wageni wake mashuhuri. Admiral Byrd alishauriana na Kellogg mara kwa mara kuhusu lishe kwa wagunduzi wake wa Polar (Aktiki na Antaktika). Watu wengine wengi mashuhuri walikuja mara kwa mara, wengine kila mwaka. Ingawa Battle Creek Sanitarium walifanya upasuaji wa kitaalamu na kulaza watu katika hospitali kubwa ya wagonjwa wenye hali mbaya sana, ilikuwa maarufu zaidi kama mahali ambapo watu walikuja kupunguza uzito, kupumzisha mishipa yao ya fahamu, na kupata nguvu kwa ujumla.

Mazingira ya chumba cha usafi yalikuwa ya hotelini zaidi, kuliko ya hospitali. Akiwa amevalia (katika miaka yake ya baadaye) katika suti nadhifu nyeupe, shati jeupe, tai nyeupe, soksi nyeupe, na viatu vyeupe, daktari huyo alikusanya umati katika chumba cha Sanitarium kila juma ili kutoa hotuba ya kuburudisha kuhusu maendeleo ya leo ya tiba. Kusudi kuu la kazi ya umishenari wa tiba lilikuwa kufundisha watu jinsi ya kuishi vizuri.

Mnamo mwaka wa 1907 Dk. Kellogg aliachana na kanisa, hatua ambayo huenda aliifikiria mapema kama mwaka 1890.[15] Kulikuwa na sababu kadhaa. Tofauti za kiasili na uongozi wa madhehebu juu ya sera za utawala zilizidishwa kwa bahati mbaya, na kule kusita kwa baadhi ya wachungaji kutekeleza vipengele fulani vya matengenezo ya afya. Kellogg, ambaye mwenyewe hakupatana kabisa na kanuni za afya, kwani alifanya kazi hadi kuchoka (ambayo kwake ilimfanya apitie hatua fulani katika haiba yake), na hii ilimfanya kuwa mtu mwenye kuudhika kirahisi. Theolojia pia ilichangia.

Dhana ya kibiblia kwamba mwili wa Mkristo ni "hekalu la Roho Mtakatifu" (1 Wakorintho 6:19), aliibeba hadi kupitiliza  katika aina ya imani ya kidini iitwayo Pantheismu, ambayo ilimfanya aseme kuwa nafsi ya Mungu inakaa katika kila kiumbe hai, katika wanyama, wadudu. na mimea, na hata kumtambulisha Mungu kwa uvutano na mwanga wa jua na siyo nafsi tena. Msimamo kama huo ulidhoofisha fundisho la msingi la Waadventista wa Kristo katika Patakatifu pa mbinguni na kuweka msingi uliomwezesha kuwa na ushupavu na utovu wa maadili kama vile uasherati (kwa msingi kwamba ikiwa Mungu akinijaza, jambo lolote ninalotaka kufanya lazima liwe sawa, hitimisho ambalo Kellogg mwenyewe hakufikia kamwe).

Kellogg alicheza-cheza na mawazo yake ya pantheismu kwa muongo mmoja au zaidi, akipokea barua nyingi za dhati na za kina kutoka kwa Dada White ambaye alikuwa kama mamaye, maana aliishi kwake. Alipochapisha nadharia yake ya The Living Temple (1903), kuachana kikamilifu na kanisa likawa suala la muda. Kimsingi zaidi, kujitenga kwake na madhehebu kulitokana na yeye kukataa uhalisia kwamba Ellen White ni mjumbe maalum wa Bwana. Alithamini sana shauri lake alipokuwa kijana na hata aliishi kwa muda nyumbani mwake Mama White. Lakini alipomwonya dhidi ya nadharia ya Pantheismu, kufanya kazi kupita kiasi, na matamanio ya ukuu, na kumsihi azingatie sana roho na miili ya wagonjwa wake, alienda mbali zaidi na ushawishi wake.

Yeyote anayesoma barua zake pamoja naye na rufaa zake zilizochapishwa kwa watumishi kwa niaba yake anajua jinsi kuondoka kwake kulivyoumiza moyo wake mama White. Endapo Kellogg angebaki na vuguvugu, ni mafanikio ya kiasi gani yangefannywa zaidi katika kutangaza ujumbe Wake kwa ulimwengu. Tuseme, kwa talanta na ushawishi wake, angekuwa amemshawishi Henry Ford au Rais Coolidge kushika Sabato na kukubali tumaini la ujio wa pili wa Masihi, lingekuwa jambo lenye mafanikio kwa kiasi gani kwa injili! Huku kujitenga kwa Kellogg na kanisa kukiwa katika mwaka 1903 na matumizi ya shule yake Kellog ya udaktari yakawa hayafai tena.

Ellen White, ambaye sasa alikuwa na umri wa kati ya miaka sabini, na akaanza kuzindua shule mpya ya matibabu kusini mwa California iitwayo Loma Linda. Pia

alilemewa na huduma za ziada za Sanitarium katika eneo hilo. Kellogg alikuwa ameanzisha safu ya vituo ishirini na saba au zaidi vya Sanitarium kote ulimwenguni, kwa mafanikio makubwa. Kwa kawaida, kila moja imebobea katika tiba ya kimwili ambayo ni mbadala na rahisi (matibabu ya maji, mazoezi, masaji, n.k.) pamoja na kutoa inapowezekana baadhi ya tiba za hospitali za jumla.

California ilikuwa na sanitarium moja pekee ya Waadventista hadi sasa, iliyo karibu na Saint Helena katika Wilaya ya Napa (sasa Deer Park). Ellen White alisisitiza kwamba nyumba mpya lazima ziwepo nje ya miji mikubwa. "Msijenge nyumba za Sanitarium mijini," alionya katika Mkutano Mkuu wa 1903.[16] Kwa usaidizi wa John A. Burden na wafuasi wengine waaminifu, alipata jengo sanitarium huko Glendale, kijiji kilicho umbali wa maili chache kutoka Los Angeles. Majengo mengine yanayofaa yaligunduliwa katika mji unaoitwa National City, maili chache kusini mwa San Diego, na huko Loma Linda, umbali kidogo kutoka kila moja ya miji mitatu ya Riverside, Redlands, na San Bernardino.

Walipokuwa wakiomba, bei za ardhi/mali hizi ziliteremka chini. Mjumbe mzee wa Bwana aliwashawishi ndugu waliosita kuidhinisha ununuzi wao. Michango iliyohitajika ilikuja—mara moja kutoka kote nchini siku ile ile ambayo mkopo wa nyumba ungehitimishwa. Kuhusu chuo kipya cha tiba, Ellen White aliwaandikia akina ndugu kwamba Bwana alitaka taasisi ambayo wahitimu wake wangeweza kufaulu mtihani wowote ufaao katika nchi. Na hivyo katikati ya milima na mashamba ya michungwa huko Loma Linda, Chuo cha Wainjilisti wa tiba kikazaliwa, kilio chake cha kwanza cha imani, pumzi yake ya kwanza ilikuwa sala. Leo shirika la awali linawakilishwa na shule za uuguzi na tiba katika Chuo Kikuu cha Loma Linda, na wakati huo huo shule ya madaktari wa meno, afya ya umma katika kuzuia magonjwa, yaani Public Health, na zingine.

Mnamo 1975, Waadventista Wasabato walifungua shule ya pili ya tiba huko Montemorelos, Mexico. Katika miaka ya 1970, ili kusaidia kuwafanya watu wawe na furaha, afya njema, na utakatifu, Waadventista Wasabato waliendesha vyuo viwili vya tiba vya mamilioni ya dola, ukanda wa viwanda vya chakula cha afya, kundi dogo la uzinduzi wa matibabu, ndege za kuchukua wagonjwa (medical aviation relief airplanes), na mtandao wa kimataifa wa hospitali na zahanati zaidi ya mia tatu (Leo kuna chuo kikuu cha Tiba pale Rwanda Adventist University of Central Africa, na Babcok University Nigeria, na Ufilipino ina chuo cha Madaktari wa Meno na Peru, Brazil, na Argentina zina vyuo vikuu vya tiba pia madaktari wenye shahada ya MD-medical doctors).

Ushirika wa maelfu ya madaktari, madaktari wa meno, wauguzi, na wahudumu wengine wa afya huwezesha yote—bila kuzungumzia juu ya wasimamizi, waweka hazina, wahandisi, makatibu na walezi. Dhehebu kwa ujumla, ambalo sasa lina

nguvu zaidi na watu zaidi ya milioni 22, nalo linathamini sana dhana ya utimamu wa mwili kama fursa ya kiroho na mazoezi ya "kazi ya umishenari ya matibabu" kama jukumu la kidini. Nani angefikiria kweli kwamba mengi yangezuka kutokana na wazo ambalo liliibuka kwa mara ya kwanza Ijumaa jioni mnamo Juni 1863 katika jumba lisilo na uzuri, la mashambani maili chache magharibi mwa Otsego, Michigan? Au kutoka kwa "zawadi ya Krismasi" iliyofunguliwa kwa machozi na maombi ya kufunga, yenye mateso huko Rochester mnamo 1865?

*VIDOKEZO:*

*1. Ellen G. White, Testimonies, vol. 9, pp. 158, 159*

*2. Review and Herald, July 26, 1906, p. 8*

*3. Review and Herald, July 29, 1902, p. 7*

*4. General Conference Bulletin, 1901, p. 205*

*5. Ellen G. White, Testimonies, vol. 6, p. 293*

*6. Spalding, Origin and History, vol. 1, p. 407, note for p. 351*

*7. Ellen G. White, Testimonies, vol. 1, pp. 205, 206; The Desire of Ages, pp. 359-363*

*8. Ellen G. White, Life Sketches, pp. 162, 163*

*9. Ellen G. White, Testimonies, vol. 2, pp. 371, 372*

*10. Ellen G. White, Counsels on Diet and Foods (Washington, D.C.: Review and Herald Publishing Association, 1938), pp. 173-178, 491*

*11. Ellen G. White, Testimonies, vol. 1, p. 494*

*12. For a fascinating episode in this story see 514 Spalding, Origin and History, vol. 1, p. 363*

*13. For the paragraphs dealing with Dr. Kellogg, see Richard W. Schwarz, John Harvey Kellogg, M.D. (Nashville, Tenn.: Southern Publishing Association, 1970)*

*14. F. Roy Johnson, The Peanut Story (Murfreesboro, N.C.: Johnson Publishing Co., 1964), pp. 90, 91, 158-173*

*15. Schwarz, Kellogg, p. 69*

*16. Review and Herald, April 14, 1903, p. 19*

# SURA YA 28
# KWA FURAHA YA HUDUMA

Hakukuwa na kosa kubwa la kumkasirisha mdhamini wa kitivo kuliko kurusha tabasamu hadharani au faraghani kwa mtu wa jinsia tofauti; Na kila mara nilijiuliza, na kushangaa na hakika nitashangaa maisha yangu yote—Jinsi nilipokuwa chuo kikuu wakati wa mbalamwezi, nilivyofanikiwa kupata mke. Lakini jambo moja kulikuwa na uhakika, ambalo sasa ninaona wazi sana. Kwamba kanuni hizi zote ngumu, kwa kweli zilikuwa baraka kwangu.[1]

Takriban kila mtu ambaye amehudhuria chuo cha Waadventista Wasabato anaweza kutambua kwa moyo wote hekima hii ndogo na anaweza kumsifu Mungu kwa kuzingatia "kanuni ngumu" (msichana na mvulana wasikae wenyewe gizani au mahali pa maficho) - na karibu kila kitu kingine isipokuwa hicho- ndicho ambacho kilifanya chuo chake cha Kikristo kuwa tofauti. Inaweza kusaidia kupitia tena, jinsi tofauti hii ilivyotokea. Macho yote yakamgeukia Sidney Brownsberger. Ellen White, hivi karibuni, akiwa na mumewe kutoka California baada ya kuanza gazeti la Signs of the Times, alikuwa amemaliza tu kusoma Shuhuda ya kina inayofichua maadili ya Mungu kwa elimu ya Waadventista.

Taasisi ya kwanza ya Waadventista Wasabato ya elimu ya juu, Chuo cha Battle Creek, ilikuwa katika mchakato wa kuzaliwa, ujenzi wake wa darasa ulikuwa ukiendelea, na baraza la wadhamini lilikuwa linakutana ili kuendeleza mipango na kusikia neno kutoka kwa Bwana. Mwalimu mkuu wa kwanza, Profesa Sidney Brownsberger, A. (Chuo Kikuu cha Michigan, 1869), alikuwa amealikwa kuhudhuria kwa kuzingatia umuhimu wake wa dhahiri kwa mafanikio ya mradi huo. "Vema, Ndugu Brownsberger," mmoja wa wajumbe wa bodi aliuliza, "tunaweza kufanya nini kuhusu maagizo haya ambayo Dada White ametupa?" Kila mtu alingojea majibu yake. Walichosikia kilikuwa cha kweli: "Sijui chochote kuhusu uendeshaji wa shule kama hiyo."[2] Haikuwa njia nzuri ya kuanza. Hata hivyo, huu haukuwa mwanzo kabisa wa elimu ya Waadventista.

Mnamo 1852, wazazi walipokuwa wakipuuza elimu ya watoto wao kwa msingi kwamba "Kristo alikuwa anakuja upesi" kwamba hawakuweza kutimiza mengi hata hivyo, James White aliwakemea. Mchango wake mwenyewe James kwa vijana, ulikuwa gazeti la kwanza la dhehebu, kwaajili ya vijana, liitwalo, Youth Instructor

au Mwalimu wa Vijana. Mnamo 1853 na 1854 idadi kubwa ya familia za Waadventista zilianzisha shule ndogo za kutwa katika nyumba zao. Inayojulikana zaidi kati ya hizi ilikuwa ile iliyoendeshwa na Martha Byington, aliyekuwa mwenye umri wa miaka kumi na tisa Katika mji wa Bridge ya Buck, New York. Katika mwaka mmoja au miwili, shule hizi zote za nyumbani zilikufa. Hili ni jambo la kusikitisha, kwani matokeo yake vijana wanaoshika Sabato katika shule za serikali walipata dhihaka kubwa kwa sababu ya mawazo yao "ya kipekee." Na ingawa wengi walivumilia, wakitazamia Yesu kuja dakika yoyote na kuwachukua mbinguni, wengine wengi walikata tamaa na kupoteza malengo yao.[3]

Miaka michache baada ya Familia ya White kuhama kutoka Rochester hadi Michigan mnamo 1855 na ofisi ya Review and Herald kuhama nao, Waadventista walianza shule ya kanisa huko Battle Creek, ambayo waliendesha chini ya safu ya waalimu tofauti kwa takriban miaka sita. Ilitelekezwa wakati shule mpya nzuri ya serikali ilipoanza maeneo ya karibu. Familia za Waadventista inaonekana zilipeleka watoto wao kwenye shule hii ya msingi ya serikali peke yake, huko Battle Creek. Vijana wao walipata kazi, wengi wao kwa kadiri iwezekanavyo wakienda kufanya kazi katika jumba la uchapishaji lililokuwa linapanuka kwa kasi na Taasisi ya Western Health Reform Institute.

Ilikuwa ni katika siku moja alipokuwa akifanya kazi kwenye Review ambapo Edson White aliona mtu asiyemjua akipasua magogo yaliyoleta rundo la kuni ambalo lilirushwa kwenye moto uliokuwa na njaa ambao ulipasha moto boiler zilizotoa mvuke ulioendesha mashine kwenye mashine za uchapaji. Baada ya saa za kazi Edson na rafiki yake, George States, na baadhi ya wenzake walizungumza na mgeni huyu na kujua kwamba jina lake lilikuwa Goodloe Bell. Miaka kadhaa kabla, Bw. Bell aliwaambia wavulana, kwamba alikuwa amesoma Chuo cha Oberlin huko Ohio, ambayo wakati huo ilikuwa mojawapo ya shule za matengenezo zaidi nchini.

Ilikuwa shule ya kwanza kutoa elimu kwa mchanganyiko wa jinsia yaani wavulana na wasichana. Ilisisitiza haja ya kuwa na kazi za viwandani na mashambani ziambatane na masomo rasmi ya darasani. Pia ilikuwa taasisi ya kidini sana. Bell aliendelea kusema kwamba alikuwa amefundisha shule katika maeneo mbalimbali kwa miaka kadhaa, na kwamba wakati kazi nyingi zilimfanya awe mgonjwa, alikuwa amefurahishwa kusikia kuhusu Taasisi mpya ya Western Health Reform Institute huko Battle Creek. Ilikuwa ni taasisi ya kidini sana. Mantiki ya taasisi hii ilikuwa ya kuleta matengenezo na mageuzi kama na Oberlin alivyo mwana mageuzi.

Bila shaka, badala ya kumtia dozi kwa dawa ya calomel na strychnine, madaktari wa hapa walikuwa wameagiza tiba ya kukanda mwili kwa maji ya moto na baridi na kumpatia huduma ya kupona ili aendelee kufanya kazi za mikono nje ya nyumba. Bell alisema aliipenda Taasisi ya matengenzo ya Afya na kwamba alipenda kile

alichojifunza kuhusu Uadventista wa Sabato. "Je! ungependa pia kufundisha shule ya usiku kwa baadhi ya wenzetu, Bw. Bell?" wavulana hawa waliuliza kwa shauku. Inawezekana tena mapema sana, alijibu. Katika jioni ndefu za joto za majira ya joto ya 1868 Goodloe Bell aliendesha "masomo yaliyochaguliwa" kwa vijana kumi na wawili wa Kiadventista ikiwa ni pamoja na, wavulana wote wa White, wana wawili wa J. P. Kellogg - John Harvey, daktari maarufu duniani wa baadaye, na Will. K., mfalme wa baadaye wa cornflake.

Lilikuwa kundi la wanafunzi wa ajabu. Na Bw. Bell alikuwa mwalimu mzuri, aliyekuwa na mbinu za kisasa sana katika kufundisha. Aliwaambia wanafunzi wake wajifunze masomo yao kwa uthabiti, lakini si kwa kukariri. Aliwataka wayaelewe vizuri ili waweze kujieleza hata kwa kushtukizwa. Shule ilienda vizuri sana kiasi kwamba katika majira ya kupukutisha majani, wavulana wengi zaidi waliomba kujiandikisha. Iliamuliwa kwamba Bw. Bell angeweza kutumia jengo dogo la awali ambalo J. P. Kellogg na wengine walikuwa wamelitenga ili kuweka mtambo wa kuchapa wa Review mwaka wa 1855.

Ili kutengeneza makao kwa ajili ya mke wake na watoto wanne, Bell aliweka viraka kwenye kuta zake za chini zilizochakaa. Wanafunzi wake walipanda ngazi za nje kuhudhuria madarasa katika chumba kirefu, chenye dari ndogo hapo juu. Kufikia 1872 Kamati ya Konferensi Kuu ilikuwa imeshawishika sana kuhusu uwezo wa Bell kiasi kwamba walipiga kura kufadhili shule aliyoichagua kama shule ya kwanza rasmi ya Waadventista Wasabato. Mwaka wa 1872 haufahamiki kwa kuidhinishwa tu kwa mtoto huyu wa Profesa Bell-(mtoto ilivyowekwa hapa ni elimu), lakini pia kwa kuzaliwa kwa Shuhuda za Ellen White juu ya asili ya elimu ya Kweli.  Kuhusiana na hili, ya kwanza kati ya mamia ya kurasa zake nyingi kuhusu somo hilo ilionekana mwaka huo katika Shuhuda Na. 22.[4]

Shuhuda Na. 22 huanza na sentensi hii: "Kazi nzuri zaidi kuwahi kufikiriwa na wanaume na wanawake ni ile ya kushughulika na akili za vijana." Kazi "nzuri zaidi". Sio nzuri zaidi kwa maana ya utamu au furaha zaidi, ingawa kufundisha kunaweza kuwa hivi wakati mwingine; lakini nzuri zaidi katika matumizi ya neno la karne ya kumi na tisa: "inayohitaji uchaguzi wa kina, kuchukuliana nayo kwa busara, kuzingatia kwa uangalifu, au mwenendo sahihi na wa uangalifu.”[5]

Alichomaanisha Ellen White ni kwamba elimu sio burudani au njia tu ya kufanya muda uende kwa walimu wasio na ujuzi na wazazi wasio na sifa, bali ni kazi ya juu inayohitaji maandalizi ya kina na kujiweka wakfu na kujitolea sana. Sentensi ya pili katika ushuhuda inaweka wazi hili: "Tahadhari na uangalifu mkubwa zaidi inapaswa kuchukuliwa katika elimu na malezi ya vijana ili kubadilisha namna ya mafundisho na kutangaza uwezo wa juu na adhimu wa akili." Tafadhali soma tena. Je, ni aina

gani ya mafundisho haya ambayo alihisi lazima yazingatiwe ikiwa "nguvu kuu na akili" zitatumika vya kutosha? Jibu lake linafuata.

Mwalimu Mkristo mwaminifu anapaswa kupendezwa vile vile “na elimu ya kimwili, kiakili, kimaadili na kiroho ya wanafunzi wake." Kufundisha ni kazi "nzuri zaidi" kwa sababu lazima ishughulike kwa msawaziko/balansi na "ukamilifu" wa kila mwanafunzi na wakati huo huo ikizingatia hulka na haiba anuwai ya kila mtu. Ni lazima izingatie uangalifu wa upembuaji mkali (1) kwa ajili ya wokovu wa wanafunzi, (2) kwa afya zao, (3) kwa ujuzi wa vitendo wanaopaswa kupata ili kuwa na manufaa katika kilimo, biashara, kazi za nyumbani, au katika kazi yoyote wanayofanya, juu ya kazi yoyote wanayoenda kuishughulikia (4) kukuza uwezo wao wa kutafakari kwa njia ifaayo. Na ni lazima (5) iwaongoze wanafunzi kuelekea huduma iliyowekwa wakfu na iliyojitolea kwa ajili ya wengine.

Kwa kuwa aina hii ya elimu ni muhimu, ni wazi haiwezi kufungiwa ndani ya darasa tu. Kwa hivyo wazazi na walimu mara nyingi hurejelewa katika ushuhuda huu. Wazazi wanapaswa kuufanya wokovu wa watoto wao kuwa "kipaumbele chao cha kwanza na cha juu." Wanapaswa pia kuifanya "huduma yao ya kwanza na shughuli yenye umakini endelevu" ili kuona kwamba watoto wao wana miili yenye afya. “pointi  mbili za kwanza zinapewa uzito sawa, kwa sababu afya ya kiroho inathiriwa sana na afya ya kimwili. Kwa kuzingatia majukumu yao, akina mama wanapaswa kuzingatia kazi zao za nyumbani kuwa "takatifu," na kuwa muhimu zaidi kuliko kazi ya katibu muhstasi anaye nakili taarifa (stenographer—mnakili") au mwanamuziki.

Hakika hakuna "ajira muhimu zaidi" kuliko ile ya kuumba na kutunza nyumba-(homemaker). Shule iliyopangwa kwa mikakati vizuri (inayorejea sasa kwenye jukumu la walimu) kwa hakika inahitajika kutoa "taasisi za kilimo na utengenezaji wa bidhaa" ambapo wanafunzi wanapaswa kujitolea "sehemu ya wakati kila siku" kwa kazi zenye utendaji hai za kushughulisha mwili. Na haitoshi kwa wanafunzi kuwekeza tu wakati, katika kazi zao. Lazima wapewe "elimu ya kina na kamili" katika aina tofauti za kazi ili waweze kupata kile chenye thamani yenye ubora kabisa. Wanapaswa "kufundishwa kazi na sayansi."

Kusoma Biblia, bila shaka, kunapaswa kuchukua nafasi muhimu/kuu zaidi, lakini si kwa kuachilia mbali sayansi. Na ni nini kusudi la elimu hii yenye balansi/msawaziko na yenye kujumuisha mambo haya manne? "Lengo kuu la elimu ni kutuwezesha sisi wanadamu, kutumia uwezo ambao Mungu ametupa kwa namna ambayo itawakilisha vyema dini ya Biblia na kuendeleza utukufu wa Mungu." "Kweli za Neno la Mungu zinaweza kuthaminiwa vyema zaidi na Mkristo mwenye akili. Kristo anaweza kutukuzwa vyema zaidi na wale wanaomtumikia kwa akili."

Baadaye, Ellen White alitoa muhtasari na kupanua falsafa yake kwa maneno haya maarufu: "Elimu ya Kweli ina maana zaidi ya kufuatilia kozi fulani ya masomo. Inamaanisha zaidi ya kujitayarisha kwa maisha haya yaliyopo sasa. Inahusiana na kiumbe kizima, na kwa kipindi chote cha uwezekano wa uwepo wa mwanadamu. Ni ukuaji wa upatanifu wa nguvu za kimwili, kiakili, na za kiroho huduma pana zaidi katika ulimwengu ujao."[6] Elimu ya Kweli si elimu ya kawaida; wala si kitu kilichojitenga na Kanisa la Waadventista Wasabato. Kanisa linapaswa kuundwa na wanaume na wanawake wanaoelewa, wanaoamini, na kuuishi ujumbe maalum wa Mungu wa siku za mwisho na wanaoungana ili kutimiza utume wao wa kuuambia ulimwengu kwamba Yesu alikuja na kufa kwa ajili yetu na Atakuja hivi karibuni.

Kwa ubora zaidi, elimu ya Waadventista Wasabato imekuwa njia kuu ya kanisa kufikia lengo hili. Inatafuta sio tu kuwafanya wahudumu, madaktari, wauguzi, na walimu, bali kuandaa kila mwanafunzi kuwa mwongoaji wa roho mwenye akili, bila kujali wito wake au taaluma. "Lengo moja kuu la shule zetu ni mafunzo ya vijana kushiriki katika huduma katika taasisi zetu na nyanja tofauti ya kazi ya injili;" lakini watoto wote wa Kiadventista wanapaswa kujipatia manufaa ya elimu ya Kikristo, wawe wameajiriwa na dhehebu au la, ili waweze kujaza "mahali pa wajibu katika maisha binafsi na yale ya umma." "Elimu ya Kweli ni mafunzo ya kimishenari. Kila mwana na binti wa Mungu ameitwa kuwa mmishenari."[7]

Muda mfupi baada ya General Konferensi kupitisha shule teule ya Bell, iliunda jumuiya ya elimu na kuanzisha mipango ya pamoja ya chuo kikuu na shule ya upili. Ardhi lazima ihifadhiwe. "Hebu kuwe na ardhi ya kutosha kwa ajili ya viwanda na kilimo," Ellen White alishauri kama msemaji wa Bwana. Alipendelea kuhamia eneo la kando ya ziwa maili chache nje ya mji. Uwanja wa maonyesho wa wilaya pia ulikuwa sokoni—ekari 50. Angeweza kubaki na kuridhika na kipande hiki cha ardhi. Familia ya White walishika gari-moshi kuelekea California na kuwaacha ndugu wafanye mpango huo (dili). "Laiti kama viwanja vya maonyesho vingekuwa karibu na Taasisi ya Matengenezo ya Afya," mjumbe wa bodi mwenye woga alihofia siku moja, "basi ingekuwa rahisi kwa wanafunzi kupata kazi huko." (Kwa kweli umbali ulikuwa ni kuvuka barabara moja tu na kwenda kwenye barabara nyingine!) "Ikiwa tutapata shule mbali sana, itabidi tuhamishe Taasisi. Fikiria hiyo gharama!" Na Battle Creek yenyewe ilionekana kijijini vya kutosha. Barabara hazikuwa na lami, na vinjia vilikuwa vya mbao.

Katika msimu wa kupukutisha majani, batamzinga walisikika wakigumia kwa sauti za juu kwenye misitu iliyo karibu. Kama vile Lutu alipoamriwa kukimbia maisha ya jiji, ndugu walitazama Battle Creek kama Soari na wakasihi kwa dhamiri zao, “Je, kwa nini usiseme tukae kwenye mji huu mdogo?” Ghafla Erastus Hussey alijitolea kuuza ekari zake 12 kando tu ya barabara kutoka Taasisi ya Afya! Bodi ya taasisi ya afya

ilinunua kwa haraka - kisha ikauza ekari tano, ikabakiza saba, na kujipongeza kwa kiasi gani cha pesa, walikuwa wameweka akiba kwa Bwana.

Ellen White alitafakari ni kwa kiasi gani mapenzi ya Bwana walikuwa wameyakataa. Lakini, akificha huzuni yake, alionekana kwenye mkutano wao wa bodi katika msimu wa kupukutisha majani na kueleza tena mipango ya Mungu kwa ajili ya shule Yake. Ni katika hafla hiyo ambapo kila mtu alimsikia Profesa Brownsberger akisema hajui chochote kuhusu kuendesha taasisi kama hiyo. Bw. Bell alikuwa anapatana na kanuni hizo mpya, lakini kipaji chake kilionekana kuelemea zaidi katika kufundisha kuliko katika utawala,[8] kwa hiyo labda hawakuwa na chaguo lingine. Kwa vyovyote vile ilionekana kuwa muhimu kuwa na mwanamume mwenye shahada ya chuo kikuu. Brownsberger aliteuliwa kuwa mkuu wa chuo, na huku James White akijaza nafasi kwa jina tu, kama rais au mkuu wa chuo.

Brownsberger, ingawa alijitolea, upesi alithibitisha maneno yake mwenyewe, kwamba kwa kweli hakujua jinsi ya kufanya kazi ambayo Mungu alitaka ifanywe. Elimu yake ilikuwa katika Classics za Kigiriki na Kilatini. Sio tu kwamba alipuuza viwanda vya uzalishaji na kilimo, lakini hata hakutoa masomo kwenye darasa la Biblia. Kulikuwa na kozi ya Biblia, yenye sauti lakini yenye kuchosha kwa kiasi fulani ya Mhariri Uriah Smith ambayo labda mmoja kati ya wanafunzi watano alihudhuria, na ibada za kanisa zilitumiwa mara nyingi kufundisha Biblia. Wanafunzi wengi walichukua kozi “za kawaida,” na matokeo yake, wakawa walimu wa shule za msingi wa umma.

Wengine, wakijitayarisha kuwa wahudumui/wachungaji au watumishi wa kanisa au kujaza kazi katika ofisi za Konferensi na vyama, walikubali mwito mara tu mtu alipokuja kuwaita, hata katikati ya muhula. Mungu aliwabariki. Alifanya alivyoweza na chuo ambacho watu wake walikuwa wamezindua. Mara kwa mara kundi la wanafunzi walipata uamsho wa kusisimua na mamia kadhaa ya vijana wa Kiadventista walipata kwa pamoja hisia mpya za umoja kutokana na hali ilivyokuwa.

Mnamo mwaka 1881, changamoto ziliongezeka na kumfadhaisha na Rais kijana Brownsberger akaona aibu (vice chancellor). (Alikuwa amefanywa mkuu wa chuo kamili mwaka wa 1880). Kwa sababu hiyo, alijiuzulu kimyakimya na kuelekea kaskazini huko Michigan ili kuchukua kazi za ukataji miti na kufundisha. Lakini mnamo 1882 Konferensi ya California ilimwita kuongoza Chuo chao kipya cha Healdsburg. Alikubali, akapanga mara moja mipango ya viwanda vya uzalishaji na masomo ya Biblia, na kuthibitisha upesi kwamba katika miaka michache ile kule Battle Creek, alikuwa amejifunza mengi kuhusu kuendesha aina ya shule yenye misingi ya Mungu.[9]

Katika kuchagua rais-mkuu wa chuo wake ajaye, Battle Creek ilimwacha tena Bell na kumchagua mzungumzaji anayependwa na mwenye roho ya kirafiki aliye na jina la kupendeza la Alexander McLearn. Japokuwa hakuwa Mwadventista Wa Sabato! Aliishika Sabato na kuhudhuria kanisani, naye alikuwa na shahada—katika theolojia, hakika maajabu. Alidumu mwaka mmoja na, baada ya kugawanya kundi la wanafunzi Mara mbili, aliondoka na kujiunga na chama cha Marion.[10] (Kijana mmoja aliyekasirika anasemekana kuwa alimrusha Profesa Bell chini ya ngazi). Chuo cha Battle Creek  kilifunga malango yake mwezi Juni na kuchukua mwaka mzima kufikiria mambo yote upya (1882-1883). Kwa mwaliko wa S. N. Haskell, Bell aliondoka kusaidia kuanzisha Chuo cha Lancaster Kusini (Baadaye kiliitwa Chuo cha Atlantic Union huko karibu na Boston, Massachusets, ila sasa kimefungwa).

Mgogoro uliofikia kilele kwa kufungwa kwa shule ya Battle Creek ulikuwa na matokeo mazuri. Bodi, wakufunzi, na baraza la wanafunzi walifikiria upya kuzingatia kwao kanuni za elimu. Mitazamo ilibadilika. Madarasa yalipoanza tena katika msimu wa  kupukutisha majani wa 1883, kulikuwa na roho tofauti kabisa katika kumbi—na kanisa lilikuwa na shule tatu badala ya moja: shule ya sekondari huko Massachusetts, na vyuo viwili, kimoja huko Michigan na moja huko Golden West.

Rais mpya wa chuo katika Battle Creek alikuwa W. H. Littlejohn, mchungaji kipofu ambaye G. I. Butler, mwenyekiti wa Konferensi Kuu, aliomba kuhudumu hadi ampate mtu wake ambaye aliona anafaa kwa wakati. Mtu wake aligeuka kuwa William Warren Prescott. Prescott alikuwa na Shahada ya chuo kikuu. Pia alikuwa na uzoefu kama mhariri na mwandishi wa habari. Alikuwa na njia ya kuwatia moyo vijana kulinda hadhi-binafsi na kuwajengea uwezo wa kujitawala wenyewe. Alikuwa Msabato mzuri. Na alitamani sana kufuata maadili yaliyovuviwa ya Ellen White. Alifanya Biblia kuwa mashuhuri zaidi, akashiriki katika uamsho kadhaa wa ajabu, na kwa kweli alizindua idadi ya viwanda vidogo. Lakini mnamo 1889, wakufunzi walipiga kura ya kuondoa viwanda vya uzalishaji tena! Punde si punde Ellen White alikuwa akionya dhidi ya hatari katika burudani na michezo ya ushindani ambayo ilikuwa ikijaza mahali ambapo kazi ya mikono ingepaswa kuchukua.[11]

Mnamo 1891 Nebraska Union college kilifunguliwa huko Nebraska na, mnamo 1892, Chuo cha Walla Walla, huko Washington. Prescott aliwahi kuwa mkuu wa vyuo vyote vitatu - kwa wakati mmoja. Mnamo 1891, pia, Prescott alimsaidia Ellen White na wengine kuendesha huko Petoskey, Michigan, taasisi ya kwanza ya kitaifa ya walimu Waadventista Wasabato. Takriban waumini mia moja wanaofundisha katika shule za Waadventista waliotawanyika na katika shule za umma walikusanyika kuweka kambi kwenye mahema na kujadili, kwa mara ya kwanza, "elimu ya Kikristo." Hii ilikuwa ni alama ya kihistoria.

Mnamo 1894 Prescott aliitwa kusafiri kuzunguka ulimwenguni, na Profesa G. W. Caviness alirithi nafasi yake katika Chuo cha Battle Creek. Pengine Caviness, pia, alitaka kuwa mwanamatengenezo; lakini, kama ni hivyo, kama watangulizi wake, hakujua jinsi gani afanye hilo—na angeweza kufanya nini hata hivyo kwenye chuo kilichowekewa vikwazo vingi kama hivyo? Alihitaji kila mtu achukue angalau darasa moja la Biblia. Lakini Ellen White aliandika kutoka Australia kwamba kadiri ambavyo wanafunzi wanachukua muda mfupi kukaa hapo shuleni Battle Creek chini ya hali ya sasa, ndivyo itakuwa bora zaidi. Mwezi mmoja baadaye aliandika tena. Ikiwa Mungu na Biblia vingepewa nafasi kuu katika elimu waliyopaswa kuchukua, basi wanafunzi wangeweza kuendelea na masomo yao kadiri walivyotaka.[12]

Sasa kulikuwa na wanaume wachache katika kanisa ambao hawakutaka tu kurekebisha elimu ya Waadventista Wasabato bali walikuwa na mawazo ya jinsi ya kufanya jambo hili na nishati ya kuifanya. Dk. John Harvey Kellogg alikuwa mmoja wa hawa. Percy Magan, mwenye umri wa miaka ishirini na nne na mfanyakazi wa chuo, alikuw mwingine. Ed Sutherland, pia mchanga kwa umri, alikuwa wa tatu. Wakati akifundisha historia katika Chuo cha Battle Creek mwaka wa 1892 Sutherland alikuwa amewahamasisha wanafunzi kuondoa nyama kwenye mlo/menyu za chuo. Huo ulikuwa ubunifu wa hali ya juu! Sasa alikuwa rais wa Walla Walla yaani mkuu wa chuo hicho, akianzisha viwanda, akitia moyo shauku ya kidini, na kuwatia moyo wanafunzi wake wajitolee kwa unyoofu kwa ajili ya utumishi wa Mungu.

Huko Australia, Ellen White alikuwa akionyesha kivitendo kwamba shuhuda zake zilimaanisha nini, huko Avondale akijenga chuo cha mfano hata katika hali ya umasikini, akitumia mikaratusi. Katika Mkutano Mkuu wa General Konferensi wa 1897 Ed Sutherland alipigiwa kura kama mkuu mpya wa Chuo cha Battle Creek, na Percy T. Magan kama mshauri wake (Dean). Kellogg alifurahi. Mabadiliko yalifanyika! Mafunzo ya Classics yalitolewa nje. Shahada ziliondolewa. Kozi zenye mwelekeo wa utume zilikuwa zimeingizwa. Biblia ikawa kitabu cha kiada muhimu kuliko vingine vyote; ilitumika hata katika madarasa fulani ya hesabu.

Katika ishara za mchoro au alama ilikuwa kwamba wakati Sutherland alipokuwa akishikilia usukani wa kuendesha, Magan aliiongoza timu, na Profesa Lamson mwenye uzito wa pauni 220 aliketi kwenye boriti, utawala huu mpya ulilima uwanja wa michezo kwa kuutayarisha kupanda mazao ya chakula. Ekari themanini kwa kuongezea zililimwa kwingine; Wanafunzi walijiandikisha katika kozi za huduma na ushuhudiaji kwa uinjilisti wa vitabu na katika mitaala mingine inayoongoza kuelekea uuguzi wa kimishenari na udaktari wa kimishenari, pamoja na kilimo cha umishenari na biashara za kimishenari, na kadhalika. "Umishenari" ilimaanisha kujitolea bila ubinafsi, nia na uwezo wa kujitegemeza, na shughuli za kudumu katika kuleta roho kwa Kristo.

Wanafunzi wengi pia walijiandikisha katika kozi ya "kawaida" ya mwaka mmoja--lakini hawakuwa na lengo tena la kufundisha shule za serikali. Wakiongozwa na maagizo ya Ellen White kwamba kila kanisa lolote lenye angalau watoto sita au zaidi linapaswa kuwa na shule yake ya kanisa;[13] Sutherland na Magan waliwashawishi wanafunzi wao wa kawaida kujitolea kuwa walimu wa shule za kanisa la Waadventista. Kwa namna fulani walipata muda na nguvu ya kutafuta idadi kubwa ya wahitimu wa zamani wa chuo cha Battle Creek na Waadventista wengine ambao walikuwa wametawanyika kuzunguka eneo hilo, waliokuwa wakifundisha katika shule za serikali, na kuwasihi pia kuanzisha shule za kanisa.

Wengi waliitikia wito huo. Na wengi walijitolea kweli kweli. Msichana mmoja, alipojua kwamba kanisa la mtaa lililomtaka halingeweza kutoa malipo, chumba chake binafsi na faragha na walisema watamjengea choo cha nje (sio self contained room) alikataa wito. Lakini msichana mwingine alijaza mara moja nafasi yake. Alikuwa tayari kulala kwenye dari isiyo na joto ya nyumba ile ile alimofundisha shule na, kwa sababu hakukuwa na pesa za maktaba, alikubali kutumia kitabu cha Tumaini za Vizazi vyote na nakala za mitumba ya vitabu vya Mkufunzi wa Vijana kama vitabu vyake vya msingi/kiada kwa masomo Jiografia, na fasihi ya Kiingereza.

Aliwapenda watoto, na wao na wazazi wao walimpenda. Aliporudi msimu wa vuli uliofuata, jiko lilikuwa limejengwa kwa ajili yake, na kuta za darini zilikuwa zimeezekwa kwa karatasi za Wakufunzi wa watoto, zenye thamani.[14] Wanandoa wachanga huko Pennsylvania walizindua ndoa yao na kazi zao katika makao ya kale ambayo yaliwapa hifadhi sio wao wenyewe na chumba chao cha shule tu bali pia kwa wanafunzi wao tisa kati ya kumi na watano, wasaidizi wawili, na washiriki watatu wa bodi ya shule.[15] Kati ya 1897 na 1900 takriban shule 150 za msingi zilianzishwa, hasa na wanafunzi wa zamani wa Chuo cha Battle Creek, na kusajili watoto 4000.

Mnamo 1901, katiba ya chuo na Konferensi Kuu ilipiga kura ya kufunga chuo huko Battle Creek na kukihamishia kwenda nje ya mji. Sutherland na Magan walipakia baiskeli zao kwenye treni, wakapita hadi kwenye stesheni iliyo karibu na eneo walilokuwa wamelisikia, kisha wakasafiri kwa barabara na vinjia vya kusini-magharibi mwa Michigan wakitafuta eneo la mashambani ambapo wangejenga shule yao mpya. Siku moja baada ya kuendesha baiskeli maili ishirini na tano kuelekea kaskazini juu ya vinjia vya mchanga karibu na Ziwa Michigan huko South Bend, Indiana, walivuta pumzi zao chini ya ramani kubwa zilizokuwa kwenye bustani ya matunda ya Bw. E. F. Garland katika mji wa mapumziko wa Berrien Springs, Michigan.

Punde Chuo cha Misheni cha Emmanuel (sasa ni sehemu ya Chuo Kikuu cha Andrews) kikajengwa huko kwenye ekari 272. Masomo ya jioni yalifanyika mwaka wa kwanza katika jela na mahakama iliyoachwa ya wilaya ya Berrien, kwani bega kwa bega,

wanafunzi na walimu walitumia wakati wa mwangaza wa jua wa siku, kufanya kazi shambani au kujenga majengo ya mbao pamoja. Ellen White alisisitiza kwamba ushirikiano kama huo kati ya wakufunzi na wanafunzi ulikuwa sehemu ya elimu ya Kikristo kwamba "kwa namna yoyote" siyo wa kupuuzwa.[16]

Mitaala ilirahisishwa hadi ambapo wanafunzi walichukua kozi moja pekee katika muhula mmoja. Majengo makuu manne yalijengwa, matatu kati yake hayakuwa na joto, hata wakati wa majira ya baridi—ili wanafunzi waweze kujizoeza na maisha magumu-yote ya utume. Milo miwili tu kwa siku ilitolewa, na, bila shaka, hakukuwa tena na Shahada za kwanza. Nebraska Union college pia ilikuwa imejaribu milo miwili na kuweka nyumba zisizo na joto, lakini kilikuwa kikitoa Shahada kwa vijana wa Kiadventista wa Sabato ambao walizitaka; na mnamo 1903 Kellogg, aliliacha kanisa na alifungua tena Chuo cha Battle Creek.

Usajili wa wanafunzi Berrien Springs ulibakia kuwa mdogo. Ukosoaji ulikuwa mwingi. Sutherland na Magan walimwomba Ellen White kama wangeweza kuanzisha shule mpya Kusini, na wakapata kibali chake, na kuondoka, wakichukua baadhi ya wakufunzi pamoja nao. Sutherland na Magan walikuwa wamekwenda mbali zaidi. Kwa mfano, Ellen White hakuwahi kukosoa dhidi ya Shahada kama walivyosema; na wakati Chuo cha Wainjilisti wa tiba kilipoanza huko Loma Linda karibu 1910, alishauri haswa kwamba wahitimu wake waweze kukidhi kila sifa zinazofaa za kitaaluma (academic qualification).[17]

Alipendekeza milo miwili kwa siku, lakini kwa moyo mkunjufu aliwaruhusu wanafunzi wa Avondale kula milo mitatu, na kila mara alitoa mlo wa tatu kwa washiriki na wafanyakazi wake.[18] Lakini Sutherland na Magan walikuwa wamedhihirisha ujasiri wa ajabu, imani, na nguvu, na walikuwa wamefanya kazi nzuri. Walikuwa wamehamishia chuo hicho Kwenda mashambani. Walikuwa wameanza kilimo na viwanda kuhusiana na hilo. Walikuwa wameweka Maandiko na utumishi usio na ubinafsi katika umashuhuri wa hali ya juu. Walikuwa wameweka wakufunzi na wanafunzi kufanya kazi ya mikono pamoja. Walikuwa wamepanga mikutano ya kila wiki ya wakufunzi na wanafunzi kwa ajili ya kuandika na kutafsiri sheria.[19]

Walikuwa wamejenga majengo muhimu kwa mbinu zenye uchumi mzuri. Kwa jumla, walikuwa wamepata mafanikio ya kiwango cha daraja la kwanza. Wakuu wa chuo na wakufunzi waliowafuata katika Chuo cha Misheni cha Emmanuel walikamilisha mchakato huo. Chini ya Profesa Frederick Griggs (1918- 1925) mwongozo wenye msawaziko/balansi ulikamilishwa kwa kiasi kikubwa. Kilimo na viwanda vilileta mapato, mazoezi, ujenzi wa tabia, na ushirika wa wakufunzi na wanafunzi. Idara ya dini ilisitawi. Mitaala iliongoza kwa busara kwa digrii, na wakati huo huo kila shughuli ilielekezwa kwa uwazi kuelekea wokovu wa roho.

Wanafunzi walikuwa na shauku; nao wakaondoka, wakiwa wameelimika vyema, wakiwa na nia ya kumtumikia Bwana popote alipoita, ili waende “kuuambia ulimwengu injili na kwamba Yesu anakuja.” Mnamo 1896 mwenyekiti wa General konferensi O. A. Olsen alisaidia mwenyewe katika kazi ya mikono katika uanzilishaji wa Chuo cha Oakwood, katika shamba lenye mialoni sitini na tano kwenye shamba la ekari 360 karibu na Huntsville, Alabama. Ikijulikana mwanzoni kama Shule ya Viwanda ya Oakwood (Oakwood Industrial School), ilitoa fursa za uzoefu wa vitendo na kitaaluma tangu mwanzo.

Karibu wakati huo huo (1892) chuo kingine kilianzishwa Kusini kama Chuo cha Graysville, ambacho miaka kadhaa baadaye (1916) kilihamishwa kutoka Graysville, Tennessee, hadi Collegedale. Punde chuo hicho kilizidi hadhi ya chuo cha diploma na kuwa taasisi nyingine ya elimu ya digrii/shahada ya miaka minne chini ya jina la Chuo cha Southern Adventist College. Wakati huo huo vyuo vingine vingi vya Waadventista vilikuwa vimeanzishwa—nchini Canada, katika nchi mbalimbali za Ulaya, Afrika, Amerika ya Kusini, India, na kwingineko.

Nchini Marekani, Chuo cha Healdsburg kilikuwa kimehama kutoka katika mji mdogo uliokuwa karibu nacho na kujiimarisha tena kama Chuo cha Pacific Union college katika shimo la  moyo wa volkeno kwenye Mlima wa Howell. Karibu na ofisi mpya za General Konferensi huko Takoma Park Maryland, Chuo cha Wamishenari cha Washington kiliteuliwa kuwa shule rasmi ya kuandaa wafanyakazi wanaoenda nchi za ng'ambo. Katika mashamba ya michungwa kusini mwa California, Chuo cha Wainjilisti wa tiba (sasa ni sehemu ya Chuo Kikuu cha Loma Linda) kilitokea kuchukua mahali pa Chuo cha Wamishenari wa Kiamerika cha Dk. Kellogg cha Battle Creek na Chicago.

Mnamo 1874, mwaka ambao Chuo cha Battle Creek kilifungua milango yake, James White, akiwa na maono murua na yenye sura ya kipekee, alitoa wito kwa vyuo vingine vinne kufunguliwa kwa haraka iwezekanavyo, hivi mwishowe vilitapakazwa njia yote kutoka bahari ya Atlantiki hadi Pasifiki.[20] Kama James White angeishi hadi 1920 angeona ndoto yake ikitimizwa mara nyingi katika nchi zote zinazozunguka ulimwengu. Je, angefurahi kwa kiasi gani! Katika miaka ya 1920 baadhi ya vyuo vya Waadventista katika Amerika ya Kaskazini, ili kuipa Loma Linda nguvu na kuwa na mashiko kwa Jumuiya ya Madaktari ya Marekani-American Medical Association, ilipata kibali cha diploma kwa ajili ya chuo kikuu ili kuwe na programu ambayo wanafunzi watasoma kabla ya kuingia shule ya udaktari hapo Loma Linda Medical School University (premedical program).

Wakufunzi wachache waliokomaa na wenye uzoefu, walitumwa kwa madhumuni haya katika vyuo vikuu kupata Shahada za udaktari. Katika miaka ya 1930, baada ya kujichunguza moyo, vyuo kadhaa vilipata ithibati ya chuo kikuu. Pia katika miaka ya

1930, Chuo cha Pacific Union College kilisimamia kuzaliwa kwa taasisi ya General Conference ambayo baadaye ilikua Seminari ya Theolojia ya Waadventista Wasabato. Katika miaka ya 1940 mabadiliko makubwa yalitokea katika vyuo vya Waadventista nchini Marekani na kufurika kwa Wasichana—Wasichana waliokomaa kiakili, walioolewa, na wanaoendesha magari yao wenyewe—baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia.

Miaka ya 1950 ilijulikana kwa idadi kubwa kama miaka ambayo wakufunzi wa vyuo vikuu, kutumwa kwenye vyuo vingine ili kupata astashahada ya udaktari (PHD). Mapema miaka ya 1960, Chuo cha Wamishenari cha Emmanuel (Emmanuel Missionary College), kilipanuliwa na kuwa Chuo Kikuu cha Andrews; na Chuo cha Wainjilisti wa tiba kiliunganishwa na Chuo cha La Sierra na shule za uuguzi, udaktari wa meno, na vingine na kuwa Chuo Kikuu cha Loma Linda.

Hakuna dhehebu lingine linalofanya mengi kwa ajili ya vijana wake kama linavyofanya Kanisa la Waadventista Wasabato. Tangu 1852 kanisa limetoa machapisho ya vijana ambayo sasa yanaweka alama ulimwenguni. Shule yake ya Sabato na idara zake kwa watoto na vijana, Idara ya Vijana, na Idara ya Elimu zipo kwa kiasi kikubwa kwa ajili ya vijana. Na leo kanisa lina mfumo mkubwa zaidi wa Kiprotestanti wa elimu ya msingi na sekondari ulimwenguni (lina shule nyingi zaidi kuliko dhehebu lolote la Kiprotestanti). Katikati ya miaka ya 2023, Waadventista Wasabato walikuwa wanaendesha shule 9845, zikiwemo za msingi 6897 na sekondari 2793, na vyuo 116 na kuajiri walimu 111,360 wanaohudumia wanafunzi milioni mbili.

Leo hii dhehebu la Waadventista Wasabato linaendelea kumimina mamilioni ya dola katika programu zake za vijana, likiwa na hakika kwamba vijana wake ndio tumaini la maisha yao ya baadaye, na kwamba wanaume na wanawake wanapaswa kuelewa, kuishi, na kusema ukweli maalum wa Mungu kwa wakati huu.

*Vidokezo:*

*1. D. K. Nicola, in Everett N. Dick, Union College, Fifty Years of Service (Lincoln, Neb.: Union College Press, 1941), p. 45*

*2. Many unfootnoted data in this chapter are taken from E. K. Vande Vere, Wisdom Seekers. This work on the early history of SDA education in general and the history of 545 Andrews University in particular supersedes Spalding's history in Origin and History, vol. 2, ch. 6*

*3. Review and Herald, August 19, 1852, p.63; November 6, 1888, pp. 689, 690; July 7, 1927, p. 2*

*4. The material in the nine volumes of Testimonies for the Church is made up of thirty-seven individually numbered Testimonies, the first thirty-four of which were originally issued as*

*separate pamphlets. The section of Testimony no. 22 under discussion here now appears in Testimonies, vol. 3, pp. 131-160, and has been republished in Fundamentals of Christian Education (Nashville, Tenn.: Southern Publishing Association, 1923), pp. 15-46*

*5. Webster's Third New International Dictionary 6. Ellen G. White, Education (Mountain View, Calif.: Pacific Press Publishing Association, 1903, 1952), p. 13*

*7. Ellen G. White, Testimonies, vol. 6, p. 133; Counsels to Teachers, p. 44; The Ministry of Healing, p. 395 546*

*8. Ellen G. White, Testimony to the Church at Battle Creek, pp.1-8*

*9. Vande Vere, Wisdom Seekers, pp. 20-22; H. O. McCumber, The Advent Message in the Golden West (Mountain View, Calif.: Pacific Press Publishing Association, 1946, 1968), pp. 129-132*

*10. Review and Herald, August 14, 1883, p. 528. Later McLearn joined the Seventh Day Baptists*

*11. Ellen G. White, Fundamentals of Christian Education, p. 378*

*12. Ibid., pp. 334-367 (dated March 21, 1895) and pp. 368-380 (dated April 22, 1895)*

*13. Ellen G. White, Testimonies, vol. 6, p. 199*

*14. Youth's Instructor, February 21, 1956*

*15. Student (a publication of Battle Creek College), January 1898, p. 65*

*16. Ellen G. White. Counsels to Parents, Teachers, and Students (Mountain View, Calif.: Pacific Press Publishing Association, 1913, 1943), p. 211*

*17. Ellen G. White, Manuscript 7, 1910*

*18. Ellen G. White, Counsels on Diet and Foods, 547 pp. 173-178*

*19. Ellen G. White, Education, p. 290*

*20. Signs of the Times, August 13, 1874, p.44*

## SURA YA 29
## SUMAKU YA WEMA NA UCHESHI USIOLINGANISHWA WA KRISTO

Katika siku moja ya baridi kali mwaka wa 1868, John G. Matteson alibisha hodi kwenye mlango wa kibanda cha mhamiaji mwenzake wa Denmark aliyeitwa C. Nelson, mhubiri Mbaptisti. Matteson kijana aliuliza kama angeweza kuingia ndani ili waweze kuzungumza pamoja, lakini Mchungaji Nelson alisema, "Hapana." Hapo, Matteson anatuambia, "Nilimhurumia. Nikitoa Biblia yangu kimya kimya na huku nimesimama kwenye theluji, nilianza kusoma kutoka katika Maandiko kuhusu upendo wa Mungu na ushirika mtamu katika Kristo.

Mhubiri huyo aliguswa sana! Ndipo alinialika niingie. Tulilia na kusali, kisha tukajifunza Biblia." Jioni hiyo hiyo Nelson alikubali ujumbe wa Waadventista, kwa wakati ufaao akawa mchungaji wa Waadventista Wasabato.[1] Upendo wa Yesu uliowasilishwa na Ellen White alipokuwa akionyesha "utukufu wa ufalme wa Mungu

na upendo na ucheshi usio na kifani wa Mkombozi aliyesulubiwa" uliyeyusha moyo wa kijana Elbert Lane mnamo 1853, na kumwongoza katika maisha ya kumtumikia Mola Wake.[2]

Uwasilishaji wake wa mada hii mwaka wa 1858 kufuatia maono yake ya "Pambano Kuu," yalisisimua kutaniko la Battle Creek kuliko ilivyowahi kutokea hapo awali. Hata hivyo hili halikuwa la kushangaza. Harakati za Ujio wa Yesu kwa mara ya pili zilianzishwa kwa kuelekeza macho yake kwa Yesu. "Yesu Yuaja upesi" lilikuwa neno la kauli mbiu la Wafuasi wa Miller. "Yesu anafanya nini sasa?" lilikuwa swali lililofuata baada ya kukata tamaa Oktoba 22, 1844. “Ana kazi ya kufanya katika Patakatifu pa Patakatifu” ndilo jibu ambalo Edson na wengine waligundua na ambalo Waadventista wa Sabato walikusudia kuuambia ulimwengu.

Uadventista wa Sabato kimsingi ni ujumbe kuhusu Kristo na kile ambacho amefanya na anachoendelea kukifanya kuwaokoa wenye dhambi. Kinachoshangaza basi ni kwamba kufikia miaka ya 1880 Waadventista Wasabato kwa kiasi kikubwa walikuwa wamempoteza Mola wao, uoni wao ulikuwa umeghafilishwa. O. A. Olsen, ambaye hivi karibuni angekuwa mwenyekiti wa Konferensi Kuu, alihimiza mkutano wa kambi huko Lincoln, Nebraska, mwaka 1885 hadi wachukue utunzaji wao wa Sabato wa sasa wa kushika sheria kwa kupitiliza sana na kukumbatia upya, haki ya Kristo;[3] lakini Olsen alikuwa na tofauti.

Wachungaji wengine wengi—lakini si wote—walikuwa wakisisitiza wajibu wa Sabato mpaka walikuwa karibu kutojumuisha uhusiano wa kibinafsi na Bwana wa Sabato. Ellen White alizungumza mara kwa mara juu ya upendo wa Yesu, lakini maneno yake ambayo sasa yanajulikana, na yenye ufanisi sana katika miaka ya 1850, yalianguka kwenye masikio yaliyokufa ganzi. Waandishi wa Review walipozungumza kuhusu jinsi wanadamu wanavyookolewa, walikuwa waangalifu kusema mambo sahihi: Tumeokolewa na Kristo pekee; hakuna mtu awezaye kushika sheria kwa nguvu zake mwenyewe.

Lakini kuna kitu kilikosekana. Au tuseme, Mtu alikosekana. Kristo alikuwa fundisho, lakini hakuwa tena rafiki yao binafsi kwa Waadventista wengi kama alivyokuwa hapo awali. Kanisa lilikuwa linahitaji sana taswira mpya ya Kristo, iliyofafanuliwa na waasisi wapya waliojitolea. Watu waliokusudiwa kufanya kazi hiyo walizindua mpango kazi wao mpya katika kikao cha General Konferensi kilichofanyika mjini Minneapolis mwaka wa 1888. "Minneapolis." na "1888." Ni Maneno yanayoendana pamoja kama pacha katika historia ya Waadventista kama vile mume na mke.[4] Maneno haya yamehusika na vikao muhimu vya Konferensi Kuu, ni kama vile miaka ya 1863 na 1901 ilivyo na umaarufu.

Tofauti na vikao hivi vingine, hata hivyo, Minneapolis 1888 si maarufu kwa kupangwa kwa taasisi ama kuundwa kwa mfumo upya, lakini kwa kutangaza kwake haki kwa njia ya imani. Kikao cha Mkutano Mkuu wa ishirini na saba kiliitishwa kuanzia Oktoba 17 hadi Novemba 4, 1888, katika kanisa jipya kabisa la Waadventista Wasabato kwenye kona ya mtaaa wa  Ziwa na Nene hapo Minneapolis, Minnesota.

Halikuwa Kongamano Kuu kubwa kwa viwango vya kisasa. Washiriki wake ulimwenguni wakati huo walikuwa 27,000 tu. Idadi ya wajumbe waliohudhuria ilikaribia tisini. Maendeleo ya fildi mpya za utume, "mgawanyo wa kazi," uinjilisti wa majiji, meli ya kuhudumia Visiwa vya Bahari ya Kusini huko karibu na Visiwa vya Solomon (Solomon Islands), na vitu vingine vingi kama hivyo vilinakiliwa; lakini shughuli zote za kawaida za mkutano huu zimesahaulika kwa kiasi kikubwa leo (business ajenda zake zimesahauliwa). Kinachokumbukwa bado ni kwamba “Bwana katika rehema Zake kuu alituma ujumbe wa thamani sana kwa watu Wake kupitia kwa Wazee Wagoner na Jones.... Ujumbe huo Uliowasilishwa ni kuhesabiwa haki kwa njia ya imani katika Uhakika. Uliwaalika watu kupokea haki ya Kristo; ambayo inadhihirishwa katika kuzitii amri zote za Mungu."[5]

Kwa bahati mbaya, hata hivyo, haya sio yote yanayokumbukwa kuhusu Minneapolis 1888. Ellen White pia aliandika, "Nimeagizwa [na Mungu] kwamba tukio la kutisha katika Mkutano wa Minneapolis ni mojawapo ya sura za kusikitisha zaidi katika historia ya Waumini wa Ukweli wa leo.”[6] Minneapolis 1888 inasimama katika historia ya Waadventista kama fursa nyingine kuu, kama rufaa ya Walaodikia ya miaka ya 1850, wakati waumini walikubali ofa ya Mungu kwa sehemu tu na kuikataa kwa sehemu. Baba mwenye shauku aliachwa tena kusubiri kwa uvumilivu, watoto Wake waliositasita. Ahadi ya 1888, hata hivyo, bado inapatikana hadi leo.

Wanaume wawili ambao walitoa mchango bora zaidi katika Mkutano Mkuu huu walikuwa Alonzo T. Jones na Ellet J. Waggoner. Mzee A. T. Jones alikuwa amezaliwa Ohio mwaka 1850. Akiwa na umri wa miaka ishirini alijiunga na jeshi, ambako alihudumu kwa miaka mitatu mara nyingi, kwenye kambi karibu na Walla Walla. Ili kutumia vyema saa zake za ziada alisoma historia, Biblia, na maandishi ya Waadventista Wasabato aliyoyapata. Baada ya kutoka alibatizwa na I. D. Van Horn, Ndipo alimwoa shemeji yake Mtumishi Van Horn, na, baada ya muda, aliitwa kuungana na E. J. Wagoner kama mratibu wa gazeti la Signs of the Times.

Mnamo 1886 yeye na Wagonner wakawa wahariri pamoja wa American Sentinel, mtangulizi wa Liberty. Jones alipendezwa hasa na mahusiano ya kanisa na serikali na utimizo wa unabii. Mzee E. J. Wagoner alizaliwa mwaka 1855, alichukua shahada ya tiba kutoka Chuo cha tiba cha Bellevue huko New York (shule ile ile ambayo Dk. J. H. Kellogg alipata shahada yake), na aliwahi kuwa daktari katika Battle Creek

Sanitarium. Baada ya miaka kadhaa aliacha udaktari kwa huduma ya injili na mnamo 1884 alijiunga na wafanyikazi wa “Signs of the Times.”

Wakati huohuo, katika siku ya mawingu mnamo 1882, wakiwa kwenye mkutano wa kambi karibu na Healdsburg, California, Mzee Wagoner alifurahia tukio hili muhimu. Alipokuwa ameketi kwenye ukingo wa kutaniko. “Ghafla,” aliandika baadaye, “nuru ilimulika kunizunguka, na hema langu, likaangazwa kwa uzuri zaidi kuliko jua la mchana lilivyokuwa likiwaka, na nikamwona Kristo akining’inia msalabani, akisulubiwa kwa ajili yangu. Wakati huo nilipata ujuzi wangu wa kwanza, ambao ulikuja kama mafuriko makubwa, kwamba Mungu alinipenda, na kwamba Kristo alikufa kwa ajili yangu."[7]

Uhakikisho huu wa ajabu ulikuwa na athari, bila shaka, katika kazi yake yote ya baadaye. Wagoner na Jones walikuwa wanaume wenye hulka tofauti kwa njia dhahiri. Jones alikuwa mrefu na mwenye mwili mnene, Waggoner, mfupi na mwenye mwili mdogo. Wote wawili wakawa wasemaji wenye matokeo mazuri. Watu wawili hao pia, wakawa marafiki wa karibu sana kiasi kwamba walifikiri sawa. Wakati fulani, waliporatibiwa kuhubiri katika kanisa lilelile siku za Sabato mbili zilizofuatana, walishangaa baadaye kujua kwamba wote wawili walikuwa wamehubiri mahubiri yaleyale.[8]

Kwa muda kidogo tutaangalia ujumbe waliowasilisha huko Minneapolis kwenye General Konferensi ya 1888; kwanza, hata hivyo, tuulize kwa nini ujumbe wao haukukubaliwa na wajumbe jinsi ilivyopaswa kuwa. Jambo moja lilikuwa, kama tulivyoonyesha mwanzoni, msisitizo mpya juu ya Kristo, au angalau kufanywa upya kwa msisitizo kuhusu Kristo na wokovu zaidi ya sheria. Na haikuwa wazi kabisa kwa kila mtu kwamba ujumbe huo ulikuwa ni Ukweli kuhusu Yesu au ni mawazo yao tu. Mahubiri ya Waggoner (alikuwa mzungumzaji mkuu katika eneo hili) yalitungwa kama tafsiri ya "sheria" katika vitabu vya Warumi na Wagalatia.

Lengo lake lilikuwa kuonyesha kwamba wanadamu wanaokolewa kwa haki ya Kristo tu, si kwa kutii sheria. Kwa dhana hii ya msingi kila mtu alikubali. Lakini katika kuendeleza mada yake, Wagoner alifasiri baadhi ya mistari kama inarejelea sheria ya maadili ambayo Waadventista wengi walidhani inarejelea sheria ya maadhimisho ya sherehe au kaida. Wagalatia 3:24, 25, kwa mfano, inarejelea sheria kama "mwalimu" ambaye alituleta kwa Kristo lakini ambaye "hatuko chini yake tena" kwa kuwa sasa imani imekuja.

Kwa miaka mingi wainjilisti wa Kiadventista walikuwa wamefasiri hii kama sheria ya maadhimisho ya sherehe/kaida, lakini sasa Wagoner alisema ilikuwa sheria ya maadili, Amri Kumi. Pengine inaeleweka sasa, kwamba baadhi ya wasikilizaji, bila kujua mwanzoni alichokuwa akifikiria, walishuku kwamba Wagoner aliikanyaga chini

na kuidharau Sabato. Lakini hii haina udhuru kwa wao kuleta uhasama wao. “Wengi walikuwa wamepoteza kumwona Yesu,” Ellen White aliandika baadaye. "Kwa miaka mingi kanisa limekuwa likimtazama mwanadamu ... lakini lilikuwa halimtazami Yesu."[9]

Waggoner, hata hivyo, kuhusiana na kile alichosema kuhusu sheria kilikuwa na mengi ya kusema kuhusu Yesu. Wengi katika hadhira walihisi kuwa alisema mengi juu Yake. Ulimwengu ulihitaji kusikia juu ya Kristo, walikubali, lakini Ukweli wa sasa ulikuwa amri ya nne, na ikiwa hatusisitizi hilo, walisema, watu watafikiri wanaweza kwenda mbinguni bila hiyo. Kwa hiyo msisitizo wa Waggoner kwa Yesu (kuhusiana na sheria) haukuwa wa kawaida, nao ukazua shaka. Jambo lingine, hata hivyo, lilijulikana sana, nalo lilizua ugomvi. Hii ilikuwa roho ya midahalo. Midahalo ya kitheolojia ni nadra leo, lakini karne iliyopita ilikuwa maarufu. Nafasi ya wainjilisti wa Kiadventista siku ya Sabato na hali ya wafu baada ya kifo ilikuwa ya Kibiblia, na rahisi sana kuielezea kwa busara,  kiasi kwamba wangeweza kumshinda karibu kila mtu; na mijadala ilichochea mvuto katika jumuiya, ikivuta umati na kuongoza kwenye ubatizo. Lakini pia walikuza silika ya malumbano ya mijadala.

Katika wa mkutano mkuu wa Konferensi wa 1888 baadhi ya wajumbe, badala ya kujadiliana na Dk. Waggoner kimya kimya kuhusu mahubiri yake, walimpa changamoto ya kufanya naye mjadala wa hadhara. Yeye na Jones walikataa. Walisema, hawakuja kufanya mdahalo, bali kujifunza Biblia na kuzungumza juu ya Yesu. Mchungaji, hata hivyo, aliteuliwa kuchukua huduma na kuhubiri kinyume na msimamo wao. Katika ibada iliyofuata Wagoner na Jones "walijibu" kwa namna ambayo wajumbe wengi waliikumbuka siku zote. Hawakubishana. Badala yake Wagoner aliingia kwenye mimbari, akafungua Biblia, na kusoma kifungu kikubwa kilichofunua Ukweli na uzima wa msisitizo wake juu ya Yesu. Ndugu walidhani kwamba alikuwa akisoma Andiko la mahubiri yake na wakangoja bila subira ili apitie Andiko hili. Lakini alipomaliza kusoma kifungu hicho alikaa tu bila ya kuongeza neno lake.

Kisha A. T. Jones akainuka, akasoma kifungu kingine, na kuketi. Watu wawili hao waliendelea na haya kwa kubadilishana hadi waliposoma vifungu kumi na sita. Mkutano ulifungwa kwa maombi. Mioyo ya watu iliguswa kwa kina. Changamoto ya tatu katika mkutano huu, pamoja na roho ya mdahalo na msisitizo wa Yesu upya, kulikuwa tofauti ya umri kati ya wanaume wawili kutoka California na viongozi kutoka Battle Creek ambao waliwapinga. Wakati ambapo mwenyekiti wa Konferensi Kuu alikuwa na umri wa miaka hamsini na nne na Uriah Smith alikuwa na hamsini na sita, Jones alikuwa na thelathini na nane na Waggoner, thelathini na tatu tu. Lakini hatuhitaji kutumia muda mwingi kuangalia tofauti ya umri kati ya pande hizi mbili.

Bibi White, ambaye alichukua msimamo wake kwa uthabiti kando ya Wagoner na Jones, alikuwa mmoja wa watu wenye umri mkubwa zaidi kwenye kikao hicho. Alikuwa na miaka sitini! Lakini sababu nyingine moja ya kutokuelewana, ambayo hatupaswi kuipita kirahisi, ilikuwa kosa lililofanywa na Wagoner na Jones wenyewe. Uelewa wao wa haki kwa imani ulionekana kuwa wa kusisimua sana kwao kiasi kwamba hawakuwa na subira kuandika kitabu juu yake na kuchapisha makala juu yake katika gazeti la Signs of the Times kabla ya mkutano wa Minneapolis. Walijua vizuri sana kwamba walikuwa hawakubaliani na mwenyekiti wa Konferensi Kuu na Mhariri Uriah Smith, lakini walikuwa na Ukweli, Ukweli kuhusu Yesu, na waliona kwamba ni lazima waitangaze hii Kweli kwa umma bila kujali "mlinzi wa zamani au mlinzi mzee" huko Battle Creek angechukuliaje jambo hili.

Ikiwa wangeonyesha busara zaidi, wangeweza kuokoa matatizo mengi kwa ajili yao wenyewe na kwa ajili ya kanisa. Kwa jinsi ilivyokuwa, waliwafanya viongozi wakubwa kuwatazama kwa wasiwasi mkubwa—na hii inaeleza kwa kiasi kikubwa kwa nini wazee hawakuweza "kusikia" mambo mazuri waliyosema huko Minneapolis 1888. Bibi White alikuwa Ulaya. Wagoner na Jones walipochapisha maoni yao mapya. "Sina mashaka kusema mmefanya makosa hapa," aliandika. “Sasa mmeonyesha mfano kwa wengine kufanya kama mlivyofanya, kwamba wajisikie wako huru kuweka mawazo na nadharia zao mbalimbali na kuzifikisha mbele ya umma, na kwa sababu mmefanya hivi jambo hili litakuwa na matokeo ambayo hamkuwahi kuyafikiri."

Alihitimisha hivi: "Lazima tuweke umoja mbele ya ulimwengu. Shetani atashinda atakapoona tofauti kati ya Waadventista Wasabato.[10] Lakini si kila mtu katika Mkutano Mkuu wa Minneapolis aliukataa ujumbe huo. Si kwa njia yoyote ile. Kwa wengine ilikuwa hivyo mwanzo wa tukio jipya la kusisimua, kwa mfano, mjumbe mmoja alirudi katika kanisa lake huko Wisconsin akiwa amechangamka sana kuhusu kuokolewa kwa imani kiasi kwamba mkulima katika kutaniko lake alipata shauku yake, akauza shamba lake mara moja, na alitoa mchango mkubwa kwa dhehebu, na akakubaliwa katika huduma.

Mchungaji mmoja kijana aliyefika Minneapolis "akiwa amejawa na ubaguzi" (kutumia maneno yake mwenyewe) alishangazwa kabisa na uzuri wa mawasilisho ya kuokolewa kwa njia ya imani, hata akatoka nje kwenye msitu karibu na kanisa, hapa alikaa mchana na Mungu na Biblia yake, na hapo hapo akampata Kristo kama Mwokozi wake. Mzee S. N. Haskell, mwenyekiti, Mzee Louis Johnson, Mzee J. O. Corliss, na wengine pia walibarikiwa sana na wahudumu, nao wakang’amua kwamba uhusiano wao mpya na Yesu ulikuwa tofauti sana na ule wa zamani kiasi kwamba waliomba kubatizwa tena.

Zaidi ya hayo, katika miaka ya mapema ya 1890 baadhi ya wajumbe waliokuwa wamechukua msimamo mbaya katika mwaka 1888 kuhusu kuokolewa kwa njia ya imani, waliungama pamoja kutoka moyoni. Mzee Uriah Smith alikuwa mmoja wa hawa. Muda mfupi kabla ya Ellen White kuondoka kwenda Australia katika mwaka 1891, yeye sio tu aliomba msamaha kwake na kwa wengine kwa faragha, lakini pia alisimama mbele ya kutaniko kuu la Tabernacle na kukiri kosa alilofanya huko Minneapolis. Hilo lilihitaji ujasiri! Na wengi wenye vyeo, katika jeshi na mstari wa Bwana waliitikia ujumbe mpya kwa hamu na njaa kubwa. Mzee Waggoner, Mzee Jones, na Bibi White walitumia muda mwingi katika mwaka huo kufuatia kikao cha Minneapolis cha mwaka 1888 kuendesha ibada za uamsho katika makanisa mahalia mbalimbali, taasisi za huduma, na mikutano ya kambi kadhaa.

Katika mwaka huo mmoja kati ya vikao vya Konferensi Kuu, Ellen White, mara nyingi akiwa na mmoja wao au wote wawili kati ya watu hao wawili yaani Jones au Wagonner, alitembelea Battle Creek (mara saba), Potterville, Des Moines, Lancaster Kusini, Brooklyn, Washington, Williamsport (mara mbili), New York (mara mbili), Chicago, Ottawa, Wexford, Kalamazoo, Saginaw, jimbo la Colorado, Healdsburg, na Oakland. Haya hayakuwa mawasiliano ya kawaida bali matukio ya kazi ngumu, kuhubiri, kutoa wito, kushauri, kuhimiza, kuomba, hadi upinzani ukayeyuka, machozi yakatiririka, dhambi ziliungamwa, mikono iliwekwa tena katika urafiki, na nyuso zenye kung'aa zilithibitisha ushindi na kuzaliwa upya.

Siku ya Ijumaa usiku mwishoni mwa mahubiri mfululizo huko Lancaster Kusini, Massachusetts, huduma ya ushuhuda ilianza kwa hiari iliendelea kwa saa kadhaa. Ellen White alitoa maoni: "Sijawahi kuona kazi ya uamsho ikisonga mbele kwa ukamilifu kama hii na bado ibaki kuwa huru kutokana na msisimko usiofaa."[11] Mnamo Julai 1889 angeweza kusema, "Katika kila mkutano tangu mkutano mkuu wa Konferensi Kuu roho zimekubali kwa shauku ujumbe wa thamani wa haki ya Kristo kwa njia ya imani."[12] Na miezi michache baadaye: "Wao [watu wanaohudhuria Mkutano Mkuu wa General Conference 1889] wanasema kwamba mwaka uliopita umekuwa bora zaidi katika maisha yao."[13]

Mzee Jones alionekana kuwa ni mwanatheolojia mkuu katika dhehebu. Mzee Waggoner, akatumwa kama mmishenari Uingereza, naye pia aliheshimiwa sana. Ni ajabu sana, kwa hakika, mwitikio wa fundisho hili, ulikuwa kwamba idadi ya washiriki iliongezeka kwa kiwango cha wastani wa karibu asilimia 10 kwa mwaka, karibia mara tatu ya ile ya GC ya mwaka 1888 ilipofika mwaka 1901, licha ya matatizo ambayo tutapaswa kuyaangalia katika sura yetu inayofuata. Wengi walitazamia mvua ya masika kunyesha na kazi hiyo imalizike kwa muda mfupi.

Kwa hakika, Ellen White aliandika, "Kipindi cha historia ambacho tunaishi sasa ni ... kipindi cha Roho Mtakatifu. ... Ni wakati wa mvua ya masika."[14] Sasa kwa kuangalia

ujumbe wa 1888 yenyewe. Kama tulivyosema, mahubiri ya Waggoner huko Minneapolis yalilenga kwa Yesu Kristo. Ellen White kwa shauku na shukrani aliyafupisha mahubiri haya kama "upendo na mvuto usio na kifani wa Kristo The Matchless Charm of Christ."[15] Leo hatuna ujumbe halisi ambao Wagoner aliwasilisha katika hubiri. Hata hivyo, tunaweza kufika karibu nao ikiwa tutachunguza vitabu alivyochapisha kabla na baada ya mkutano. Mojawapo ya hiki kinaitwa ipasavyo, 'Kristo na Haki Yake.'

Kitabu kizima kinazungumza juu ya Yesu. Kristo ni Mwokozi wetu kwa maana kamili ya neno hili. Hakuna Jina lingine isipokuwa Jina Lake ambalo watu wanaweza kuokolewa kwalo. Yesu amejazwa na utimilifu wote wa Uungu, na anatamani kutujaza sisi pia na nguvu Zake za Kiungu. Wakolosai 2:9; Waefeso 3:19. Yesu huyu wa ajabu anatoa bure msamaha kwa dhambi zetu zote na kutuvika haki Yake. Na haki anayotaka kutupa si kitu cha kufikirika tu. Mungu hatusamehi na huku akituacha kama tulivyokuwa hapo awali. Mungu "haweki vazi la dhambi, bali huondolea mbali dhambi….. Msamaha wa dhambi ni kitu zaidi ya umbo tu, kitu zaidi ya kuingia tu katika vitabu vya kumbukumbu mbinguni…. ni Ukweli; ni kitu kinachoonekana, kitu ambacho kinaathiri mtu binafsi." Anaposamehewa, mwenye dhambi anakuwa kiumbe kipya.[16]

Lakini, Wagoner alipendekeza, "inawezekana kuwa wewe unajiona kwamba hufai, hata huwezi kuamini kwamba Mungu anaweza kukukubali wewe kama mtoto Wake." Ili kutatua tatizo hili aliuliza swali: "Je, mtu atakipokea kile alichonunua?" Je, mtu akienda dukani, Wagoner akauliza, "akaomba anunue kitu na kisha akalipia, je, atabadili mawazo yake ghafla na kuondoka mahali hapo bila kwenda nacho kitu hicho?" Bila shaka hatafanya hivyo. Ikiwa atalipia, atakichukua. Na kadiri anavyolipia kwa gharama kubwa, ndivyo anavyokuwa na uhakika zaidi wa kuichukua. Sasa, Yesu amelipa gharama kwa ajili yetu. Amelipa bei ya juu zaidi iwezekanavyo na inayoweza kununua, "damu ya thamani ya Kristo" (1 Petro 1:19)

Kwa kweli, 'alijitoa mwenyewe kwa ajili yetu (Tito 2:14). Hivyo, Wagoner alimalizia, kwa kusema, unaweza kuwa na hakika kwamba Yeye atakukubali wewe! Lakini kwa nini basi Alipe kiasi hicho kwa ajili ya mtu ambaye hafai sana? Wagoner akajibu "Naam, Yeye Alikununua kwa sababu wewe hufai, kiasi kwamba wakati Yeye amekubadilisha anaweza kukuleta na kukuwasilisha mbele za Baba Yake bila dosari mbele ya ulimwengu, aweze kufurahi juu ya mabadiliko ya ajabu Aliyofanya ndani yako.[17]

Lakini haki kwa imani ni zaidi ya msamaha; pia ni ushindi juu ya dhambi. Katika ubinadamu Wake Kristo aliishi maisha ya haki, "na wewe unaweza kuwa na uwezo uleule aliokuwa Nao, ukiutaka," Wagoner aliendelea. "Ni uwezekano wa ajabu ulioje kwa Mkristo! Haijalishi ni kiasi gani Shetani anaweza kupigana naye mtu huyo,

akimshambulia pale ambapo mwili ni dhaifu zaidi, mtu huyo anaweza kukaa chini ya kivuli cha Mwenyezi, na kujazwa na utimilifu wa nguvu za Mungu."

Kristo, ambaye ana nguvu zaidi kuliko Shetani, anaweza kukaa daima katika moyo wa Mkristo; "na hivyo mwanadamu, akitazama mashambulizi ya Shetani kama ngome yenye nguvu, yeye [Mkristo] anaweza kusema, 'Nayaweza mambo yote katika Yeye anitiaye nguvu.'"[18] Ingawa ni jambo linaloonekana la ajabu, Wakristo wengi hufikiri kwamba kuomba msaada wa kushinda dhambi zao huwaacha tu na mwelekeo wa kufanya mabaya zaidi, kuliko pale ambapo hawakuomba. Kwa nini? Wanafanya kosa gani? Wagoner alieleza "Wanafanya makosa, kumwambia Mungu matatizo yao kabla ya kumkumbusha ahadi Zake." Kuomba kuhusu matatizo huelekeza uangalifu/umakini wetu kwenye udhaifu wetu, na hivyo hutufanya kuwa dhaifu zaidi. Ili kupata msaada wa Kweli tunapaswa kuelekeza umakini wetu kwenye nguvu za Mungu na ahadi Zake.

Kwa uchache, Wagoner alisema, Mkristo aliyejaribiwa anaweza kukumbuka ahadi, "Kristo Yesu alikuja ulimwenguni kuokoa wenye dhambi." (1 Timotheo 1:15). Kwa hiyo anaweza kuanza sala yake kwa kunukuu ahadi hii na kukaza fikira zake juu ya Kristo na ahadi Zake; na akifanya hivyo, atakuwa na imani. "Basi," Wagoner aliendelea, "tunakumbuka kwamba ... ikiwa Mungu anatoa ahadi, ni sawa na imetimizwa tayari. Na kwa hivyo ... tunahesabu ushindi kuwa, tayari ni wetu, na kuanza kumshukuru Mungu kwa ajili ya ahadi kubwa sana na za thamani."

Imani yetu inaposhika ahadi hizi huzifanya kuwa za Kweli na za hakika kabisa. Ni hakika sisi hatuwezi kujizuia kumsifu Mungu kwa ajili ya upendo Wake wa ajabu sana.[19] Katika mawasilisho ya Waggoner Ellen White pia alizungumza mara kwa mara huko Minneapolis 1888. Mahubiri aliyohubiri mchana wa Sabato, Oktoba 13, yalikuwa ya manufaa hasa.[20] Andiko lake lilikuwa, "Tazameni, ni pendo la namna gani alilotupa Baba," na ujumbe wake ulikuwa kwamba tunapaswa kufanya hivyo; tunapaswa kuzoeza akili zetu "kuona," au kufikiria, upendo wa Mungu kwetu. Ilikuwa ni jambo lile lile alilosema Wagoner—kuhusu kufikiria ahadi za Mungu badala ya matatizo yetu wenyewe.

Je, maua ya yungiyungi kwenye maji machafu yanawezaje kuelea yakiwa safi na kuwa meupe juu ya takataka na uchafu wa ziwa? Aliuliza. Kwa sababu huchagua kutoka kwa mazingira yake tu kile kitakachofanya yungiyungi kuwa nyeupe na safi tu! Vivyo hivyo, aliwashauri wajumbe, "msiseme juu ya uasi na uovu uliomo duniani, bali inueni nia zenu na kumnena Mwokozi wenu….." Ikiwa uko chini katika sakafu ya kukata tamaa, alisema, usilalamike na kugumia juu ya giza. Kunung'unika hakutafanya taa ziwake au mwanga utokezee. Ondoka nje ya chumba chako cha chini pale pasipo na madirisha! "Toka gizani ndani ya chumba na kukaa juu ambamo nuru ya uso wa Mungu inang'aa sana."

Pia, usilalamike kuhusu miiba na michongoma ya maisha. Kusanya maua mazuri! "Tunataka kuwekeza mawazo yetu juu ya mambo ya kutia moyo." “Sauti na isikike ya kile ambacho Kristo amenifanyia,” Mzee Wagoner alionyesha kwamba haki kwa njia ya imani hutokea wakati Wakristo wanapodai ahadi za Mungu. Vile vile, Ellen White alisema, "Nataka uchukue ahadi nyingi za Mungu na uzitundike katika ukumbi wa kumbukumbu pamoja nawe. ... Oh, nataka ahadi za Mungu ziwe picha hai kwenye kuta za kumbukizi, ambazo unaweza kuzitazama. Ndipo moyo wako unaweza kujazwa na neema Yake na unaweza kumwinua Yesu."

Kusanyiko lilisikiliza kwa mioyo iliyoinuliwa na katika ukimya hadi alipofunga mahubiri yake: “Loo, nampenda Yeye. Ninampenda, kwa maana Yeye ni upendo wangu. Ninaona ndani Yake pendo lisiloweza kulinganishwa na ninatamani tuingie mjini kupitia malango Yake... Natamani mngeelimisha mioyo na midomo yenu kumsifu, kuzungumza juu ya uwezo Wake na utukufu ... Mungu atusaidie kumsifu zaidi na kupatikana bila dosari. Katika mahubiri mengine makuu,[21] Ellen White alizungumza juu ya Kristo akitenda kazi katika Patakatifu pa mbinguni, akifanya upatanisho kwa ajili yetu. Wakati anasafisha Patakatifu pa mbinguni, alisema, tunapaswa kutakasa “mahali Patakatifu pa roho” zetu wenyewe kwa kuingia katika Patakatifu pa mbinguni pamoja Naye, kuungama dhambi zetu, na kushika mkono Wake kwa imani.

Katika uhusiano huu na Yesu hakuna msamaha tu bali pia nguvu za kushinda. "Tunasikia visingizio vingi," nabii aliona katika mahubiri haya Watu wakisema, "Siwezi kuishi na kufikia kiwango cha hili au lile. Unamaanisha nini kwa hili au lile?" Aliuliza. "Je, unamaanisha kwamba ilikuwa ni dhabihu isiyo kamili ambayo ilitolewa kwa ajili ya jamii ya wanadamu iliyoanguka pale juu ya Kalwari, kwamba hakuna neema ya kutosha na uwezo tuliopewa ili tuweze kufanya kazi mbali na kasoro na mielekeo yetu ya asili?" (Ilikuwa vigumu kwa Waadventista wengi kuamini ahadi hii ya ajabu.

Miaka kumi na sita baadaye, katika mwaka wa 1904, Ellen White alilalamika hivi: “Katika maisha ya wengi ambao majina yao yako kwenye vitabu vya kanisa hapajakuwa na mabadiliko ya kweli. ... wanakiri kumkubali Kristo kama Mwokozi wao, lakini hawaamini kwamba atawapa wao uwezo wa kushinda dhambi zao."[22] Muda mfupi baada ya 1888 (kama tunaweza kuondoka Minneapolis) Ellen White alichapisha kitabu Steps to Christ. Ndani yake aliendelea kueleza haki kwa njia ya imani na jinsi inavyofanya kazi.

Kwa mfano, akizungumzia jinsi Mungu anavyosamehe dhambi kikamilifu na kwa namna ya ajabu, alisema, “Ikiwa utajitoa Kwake, na kumkubali kuwa Mwokozi wako, basi, maisha yako yaliyokuwa yenye dhambi, kwa ajili Yake wewe unahesabiwa haki. Tabia ya Kristo inasimama badala ya tabia yako, na unakubalika

mbele za Mungu kana kwamba hukufanya dhambi."[23] Hili ni ajabu; lakini sio yote. Sisi tunaweza kuendelea siku baada ya siku, tukijua kwamba Yeye anatupenda na anajali kuhusu wokovu wetu. (Njia ya wokovu ni haki kwa imani, si kujipatia haki kwa njia ya hofu, au wasiwasi au kuhangaika!) "Hatupaswi kujiingiza katika wasiwasi na woga kwamba je, tutaokolewa au la," aliandika.[24]

Je, hii ina maana hakuna kitu ambacho tunapaswa kufanya? Hapana, kuna kitu lazima tufanye. Na tena ni jambo lile lile ambalo Mzee Wagoner na Ellen White walisisitiza katika mwaka 1888. Ni lazima tuchague kufikiri na kuzungumza juu ya ahadi Zake. "Mkabidhi Mungu nafsi yako, na umtumaini. Zungumza na umwazie Yesu. ... Ondoa shaka yote; ondoa hofu zako .... Tulia kwa Yesu .... Ikiwa utajidondosha katika nafsi Yake, mikononi mwake, Yeye atakuleta kama mshindi na zaidi ya mshindi kwa Yeye aliyewapenda ninyi."[25]

Lakini je, Biblia haisemi kwamba Wakristo wanapaswa kukesha na kujitahidi na kuomba? Ndiyo, kama vile Mathayo 26:41 na Luka 13:24. Lakini Ellen White aliwaambia Waadventista mwaka 1892 kwamba hawakupaswa kuhenyeka sana dhidi ya dhambi ila kujitahidi kufikiria juu ya Yesu. "Hapa ndipo tunapohitaji kukesha, kujitahidi, kuomba, kiasi kwamba kusiwe na kitu kinachoweza kutushawishi kuchagua bwana mwingine; kwa maana sisi daima tuko huru kufanya hivyo. Lakini tuweke macho yetu kwa Kristo, Naye atatuhifadhi. Tukimtazama Yesu, tuko salama ... Kwa kumtazama daima, 'tunabadilishwa tufanane na sura ile ile toka utukufu hata utukufu, kama vile kwa Roho wa Bwana" (2 Wakorintho 3:18)"[26]

Ilikuwa ni upepo mpya, uliokuwa ukivuma kanisani, msisitizo huu juu ya upendo usio na kifani wa Kristo.

*MAELEZO:*

*1. L. H. Christian, Sons of the North (Mountain View, Calif.: Pacific Press Publishing Association, 1942), p. 130*

*2. Review and Herald, August 23, 1881, p. 143*

*3. Michael McGuckin, "The Lincoln City Mission: A. J. Cudney and Seventh-day Adventist Beginnings in Lincoln, Nebraska," Adventist Heritage, Summer, 1975*

*4. For further reading see especially Olson, Through Criss to Victory, and LeRoy Edwin Froom Movement of Destiny (Washington, D.C.: Review and Herald Pubhshing Association, 1971), p. 237-268. Unfortunately both of these present a somewhat more optimistic picture than the Ellen White testimonies warrant*

*5. Ellen G. White, Testimonies to Ministers, pp. 91, 92*

*6. Ellen G. White, Letter 179, 1902, in Olson, Through Crisis to Victory, p. 39*

*7. E. J. Waggoner, "Confession of Faith," p. 5, copy deposited in the Heritage Room, James 575 White Library, Andrews University*

*8. A. T. Jones, funeral sermon for E. J. Waggoner, The Gathering Call, November 1916, copy deposited in the Ellen G. White Estate*

*9. Ellen G. White, Testimonies to Ministers, pp. 92, 93*

*10. Ellen G. White, Counsels to Writers and Editors, pp. 75, 76*

*11. Review and Herald, March 5, 1889, p. 146*

*12. Review and Herald, July 23, 1889, p. 466*

*13. Ellen G. White, Selected Messages, bk. 1, pp. 361, 362*

*14. Ellen G. White, Testimonies to Ministers, pp. 511, 512*

*15. Ellen G. White, Manuscript 5, 1889, in Olson, Through Crisis to Victory, p. 48 16. E. J. Waggoner, Christ and His Righteousness (Oakland, Calif.: Pacific Press Publishing Company, 1690 [Facsimile reproduction, Nashville, Tenn.: Southern Publishing Association, 1972], p. 66. Another of Waggoner's works, The Glad Tidings, published originally in 1900, was republished in an edited edition in 1972 by the Pacific Press Publishing Association*

*17. Waggoner, Christ and His Righteousness, pp. 69-73*

*18. Ibid., pp. 29-31*

*19. Ibid., pp. 78-84*

*20. This sermon is printed in Olson, Through Crisis to Victory, pp. 246-256*

*21. Ibid., pp. 260-269*

*22. Ellen G. White, Review and Herald, July 7, 1904, p. 7*

*23. Ellen G. White, Steps to Christ (Mountain View, Calif.: Pacific Press Publishing Association, 1908, 1956), p. 62*

*24. Ibid., p. 72*

*25. Ibid. 576*

*26. Ibid. 577*

## SURA YA 30
## MIAKA KUMI NA SITA YA MGOGORO

"Nawapa neno langu la heshima," Mzee A. G. Daniells alirudia maneno haya kwa mafundi bomba, wapiga plasta na wafanyabiashara wa mbao huko Marekani, wakati hundi itawasili, tutakulipa mara moja.” Daniells hakutambua kesi, au ushindi, ambao maneno yake yangehamasisha .[1] Ilikuwa ni majira ya kuchipua ya 1899. Miaka mitano mapema mfululizo wa miujiza ya dhahiri ilikuwa imewatia moyo waumini katika nchi ya Australia kuanzisha chuo cha Avondale, ambacho kingetuma wamishenari ng'ambo kwa wakati ufaao kama vile vyuo vya Amerika vilivyoanza kufanya kazi.

Wazo hilo lilionekana kutowezekana, hata la kipumbavu, kwa washiriki waliohudhuria mkutano wa kambi ya Middle Brighton karibu na mji wa Melbourne mnamo Januari 1894 wakati Bibi White alipendekeza kwa haraka. Je, eneo la kuketisha watu 1000 tu lingewezaje kujengwa na kuendesha chuo? Ellen White alisonga mbele, na ndugu wakifuata kwa kusitasita. Hivi karibuni ekari 1450 zilichaguliwa na kwa bei nzuri ya takriban $3.00 kwa ekari. Lakini hata $4500 zilionekana kutoweza kupatikana. Kando na hilo, mtaalam wa serikali alisema udongo ulikuwa una tindikali, unyevu, na mchanga. "Ikiwa jambazi angejaribu kuivuka ardhi hii," aliongeza, "atalazimika kubeba chakula chake cha mchana pamoja naye kwani atakufa njaa."

Lakini katika maono yake Ellen White alijifunza kwamba Mungu angeweza kuifanya ardhi hii kuzaa zaidi kwa imani. Ili kusaidia kuwashawishi viongozi, alimwonyesha katika maono mtaro uliokatwa safi “urefu wa yadi mbili na kama robo ya yadi kwenda chini,” ukilimwa kwa njia ya ajabu katika msitu uliokuwa unafyekwa kwenye shamba hilo; na mnamo Mei 24, 1894, ndugu walitoka nje kwenda mahali hapo kutazama, mtaro huo wa kimiujiza ambao ulikuwa pale ili kuwasalimu!

Asubuhi iliyofuata walipokuwa wakitafuta mwongozo wa Mungu kwa bidii isiyo ya kawaida, Mzee Stephen McCullagh, akiwa karibu kufa kutokana na kifua kikuu, alihisi mshtuko ukipita katika mwili wake na akapona kabisa. Bado, mashaka yaliendelea; na bado Ellen White aliwasihi ndugu wamwamini Mungu na kununua ardhi. Kwa namna fulani walifanya malipo kadhaa. Kisha mnamo Januari 1895

washiriki wa familia ya Diamondrich Wessels (ambao tulikutana nao katika sura ya 23) walifika kutoka Afrika na walivutiwa na kutoa $5000.

Mnamo Machi 6 aina ya Chuo cha awali (diploma) kilifunguliwa na wanafunzi wachache. Mnamo Julai, ili kuonyesha imani yake katika mradi huo, Dada White alinunua ekari 66 kati ya hizo 1450 na kuanza kujenga makazi yake na wasaidizi wake na kuyaita "Sunnyside. Lakini muhula wa shule ulipofungwa mnamo Oktoba au Novemba, ambayo ni majira ya kuchipua mimea nchini Australia, mradi huo ulikaribia kukatika. Ili hali kuwa mbaya zaidi, wakili wao alipoteza kesi isiyo ya lazima kwa gharama ya kutisha ya $ 2000. Julai iliyofuata Ellen White katika ndoto alipokea hoja mpya za kuwasilisha kwa ndugu na kuwashawishi waanze tena ujenzi. Vijana na washiriki wazee walikata miti na kuitengeneza mbao. Walikausha madimbwi na kupanda bustani. Walifanya kazi hadi usiku, wengine wakiwa wameshika mishumaa huku wengine wakipigilia misumari.

Mapema mwaka wa 1897, baada ya ujenzi wa bweni la wasichana kukamilika na ukumbi wa kulia chakula ulikuwa umeanza vizuri na pesa zote zilizopatikana zikawa zimekwisha, Ellen White aliita watu wa kujitolea kufanya kazi bila malipo, na thelathini walikubali. Mnamo Aprili 1897 Shule ya Avondale kwa ajili ya Wafanyakazi Wakristo ilifunguliwa kwa ratiba, ikiwa na walimu wanne na wanafunzi kumi. Mahudhurio yalipanda kwa kasi. Hitaji lilikuzwa kwa ajili ya jengo la kanisa linalotosheleza ibada za Sabato. Wafanyabiashara wasiokuwa Waadventista walitoa vifaa, vibarua walichangia sehemu ya wakati wao, na punde jengo lilikuwa limemalizika.

Kufikia 1899 wanafunzi walioandikishwa walikuwa wameongezeka kufikia 100, na majengo zaidi yalihitajika ili kukamilisha mradi huo. Na, kwa mara nyingine, fedha zilikwisha. A. G Daniells, mwenyekiti wa jimbo la Australasia, alikuwa msimamizi wa kukusanya pesa. Kwa kutiwa moyo na Dada White aliomba General Konferensi huko Battle Creek imachi/ilingane na dola ya Australia kwa dola ya Marekani, na viongozi katika Amerika walikubali (Australia wakitoa moja, Wamarekani watatoa moja). Wakiwa wamehakikishiwa haya, Waadventista wa Australia walitoa tena, hadi senti yao ya mwisho, kisha wakaahidi hata zaidi. Walitaka vijana wao wapate elimu ya Kikristo kwa gharama yoyote ile. Hapo ndipo wajumbe walipokwisha kupita lengo lao, ndipo Mzee Daniells alipowataka mafundi bomba, wapiga plasta, na wafanyabiashara wa mbao kutoa vifaa na vibarua kwa mkopo na kuahidi kwamba angewalipa wote mara tu Konferensi kuu itakapotuma hundi yake ya ukarimu.

Mei. Siku ya Jumanne, ya pili ya Mei, 1899, bahasha iliwasili ikiwa na anwani ya mtumaji - General Konferensi ya Waadventista Wasabato, Battle Creek, Michigan. Ilifunguliwa kwa hamu iliyoje! Kwa mshangao kiasi gani ilibainika kuwa haina pesa! Daniells alipigwa na butwaa. Alisoma kwamba ndugu wa Marekani walikuwa

wanakabiliwa na mahitaji mengi nyumbani wakati mdororo wa kiuchumi ulipoendelea kulikumba taifa. Huzuni! Walikuwa na hakika kwamba waumini wa Australia wangeelewa. Na kama suala la ushauri unaofaa, wakijua kwamba Australia ilikuwa ikikabiliwa na ukame mkali, walipendekeza kwamba mipango ya ujenzi isitishwe hadi siku bora zaidi zitakapokuja.

Habari zilipoenea upesi, yaelekea mtu fulani alikumbuka jambo ambalo lilikuwa wamelisamehe kwa furaha na kusahauliwa; yaani, hii haikuwa mara ya kwanza kwa uongozi wa Marekani kuwaangusha. Huko nyuma katika mwaka 1894, walipokuwa wamehitaji pesa kwa haraka sana kununua ekari 1450, Ellen White katika jina la Bwana alikuwa amemwomba S. N. Haskell kutafuta wafadhili huko California. Alikuwa amejibu kwa kuongeza $10,000 kama ahadi, lakini wakati $1000 ya kwanza (na ya pekee) ilipoingia, msimamizi katika Pwani ya Magharibi, bila ubaya kabisa lakini pia bila kufikiria Australia, aliitumia pesa hiyo kwa mahitaji halisi ya Konferensi ya California.[2] Dada White alikuwa amejibu wakati huo kwa mawasiliano ya dhati, na msimamizi alikuwa amejaribu kurekebisha mambo. Lakini japo uongozi wa Marekani, bila kufahamu kikamilifu mahitaji ya eneo la mbali la misheni, waliwaangusha Australia, inaonekana kwamba Mungu hakufanya hivyo.

Mnamo 1895 aliigusa moyo familia ya Wessels kusaidia. Mnamo 1899 Alifanya maajabu kumsaidia Mzee Daniells. Usiku mzima baada ya pesa kushindwa kufika Daniells alitumia muda wake kufanya maombi chini ya miti ya mikaratusi. Aliomba mpaka mbingu ikapambazuka asubuhi na uhakika ukamjia kwani uhakika uliwahi kufika asubuhi na mapema kama ilivyokuwa kwa Hiram Edson, kwamba maombi yake yangejibiwa na kwamba Mungu atatatua tatizo lao. Saa mbili asubuhi siku hiyo Daniells alikuwa akielekea Sydney, Melbourne na Adelaide kwa ujasiri kutafuta pesa ambazo alijua tayari Mungu alikuwa ameweka akiba kwa ajili yake. Ni mara chache tu aliondoka wakati treni ilipowasili kutoka New Zealand ikiuliza ikiwa shule ingetumia $2500!

Kwa muda wa majuma mawili yaliyofuata Daniells alifurahia mfululizo wa sala zilizojibiwa. Kwa mfano, siku ya Alhamisi asubuhi akili yake ilivutiwa sana na maneno katika Danieli 6:16, “Yeye atakuokoa.” Katika ukingo aliandika, "7:30 am au saa 1:30 asubuhi, 5/4/99." Yeye na rafiki yake walipopita benki saa kumi alasiri hiyo, saa moja kamili baada ya muda wa kufunga, waliona mlango umefungwa. Waliingia ndani na kustaajabu kumkuta mwenye benki na makarani wake wakiwa wamezungukwa na rundo la fedha taslimu, dhamana na hundi, katika chumba cha kuhifadhia fedha, kikiwa wazi, na hakuna aliyesimama kwa ulinzi. Mfanyabiashara huyo akatazama juu na uso wake ukabadilika rangi, "Umeingiaje humu?" akagugumia. "Mlango ulikuwa wazi." "Lakini haiwezekani! Niliiufunga, nikageuza ufunguo, na kushika mnyororo kwa mikono yangu mwenyewe."

Ndipo akahisi kwamba wanaume hao lazima walikuwa na usaidizi usio wa kawaida, mfanyakazi wa benki akauliza kwa upole, "Je, kuna chochote ninachoweza kukufanyia?" Hakika kilikuwapo kweli! Saa moja baadaye mfanyakazi wa benki alikuwa akiwapa tabasamu na pauni 300 za Australia, zilizohesabiwa kuwa ni ‘Wafalme wa dhahabu wanaong'aa,’ walioridhika kutopokea rehani nyingine isipokuwa karatasi ya ahadi iliyoungwa mkono na neno lao la heshima. Jioni hiyo Mzee Daniells aliandika kando ya Daniel 6:16, "hili limetimizwa, 5:00 pm, 5/4/99." Pesa zaidi zilikuja chini ya hali nyingine za kushangaza, na ndani ya wiki mbili kila ‘jukumu la sasa’ lilikuwa limetimizwa.

Avondale iliendelea kuwa kila kitu ambacho Mungu alikuwa amesema kingekuwa: chuo bora, kituo cha mafunzo kwa mamia ya wamishenari, na shamba lenye ufanisi sana kiasi kwamba wataalamu walikuja kujifunza sababu ya kufaulu kwake. Lakini ni nini kilienda vibaya huko Amerika? Kwa nini haikuwa mara moja bali mara mbili katika miaka ya 1890 uongozi huko ulikuwa umeangusha jimbo na misheni changa yenye matumaini? Labda hakuna jibu rahisi katika vichwa vyetu, kitabu "Miaka Kumi na Sita ya Mgogoro (1888-1904)" kinaelezea upana wa shida.

"Mgogoro" unaweza kufafanuliwa kama kipindi ambacho maamuzi ya kimsingi yanafanywa na yanayathiri matukio yote yajayo, na kama hali ambapo vipengele vya upinzani vinapingana kwa ukali. Miaka ya 1890, kama tunavyoweza kutaja takriban miaka inayojadiliwa, yote miwili ilikuwa wakati wa maamuzi na mapambano kati ya yale ya kusikitisha na yale ya utukufu katika Kanisa la Waadventista Wasabato. Utukufu, kwanza.

Minneapolis 1888 ilianzisha msisitizo juu ya Yesu na haki kwa imani ya ajabu zaidi kuliko yoyote ambayo yalikuwa yametangulia katika historia ya kanisa; na kwa 1888 kuandaa njia, vikao vya Konferensi Kuu ya 1893, 1895, na 1897—bila kutaja mikutano mingi ya kambi, taasisi ya huduma, na uamsho wa ndani—zilikuwa na matukio ya hotuba za kusisimua hasa kwenye Moyo wa injili. Hapa kulikuwa na ujumbe wa kuuambia ulimwengu; kwa hivyo ilikuwa kwamba kadiri watendakazi wa ng'ambo katika vituo vya misheni walivyosoma ripoti katika Review na Majarida ya Kila Siku ya General Konferensi, ya kila siku, mioyo iliyookuwa imehama maelfu ya maili ilitiwa joto la ajabu na ahadi zao kwa Mungu zilifanywa upya. Jambo lisilohusiana na jambo hili lilikuwa ni kuonekana kwa kazi bora ya Ellen White, vitabu tunavyovijua leo: Tumaini kwa Vizazi Vyote (Desire of Ages); pia Hatua za Ushindi (Steps To Christ), Thoughts From the Mountain of Blessings (Mlima wa Baraka), na Christ's Object Lessons (Vielelezo vya Mafundisho ya Kristo).

Kama tulivyoona, maendeleo ya kielimu yalionekana katika kipindi hiki. Mnamo 1891, taasisi ya kwanza ya walimu nchi nzima ilizingatia "elimu ya Kikristo;” hivi karibuni elimu ya vyuo ilianza kuhamia kwa umakini nchini; na mnamo 1897 shule za

kanisa zilianza kuchipua kwa mamia. Kuingia katika ardhi nyingi mpya na vituo vya kwanza vya misheni kwa watu wasio Wakristo pia kuliashiria miaka ya 1890, kama vile kiwango cha pili cha ukuaji wa kila mwaka kwa asilimia 9.8 kwa muongo wote. Kwa kuongezea, marekebisho kadhaa ya matokeo yalitekelezwa, ambayo tutasikia katika sura inayofuata.

Kisha nini kilikuwa kibaya sana? Ikitazamwa kutoka kwa maoni fulani, hakuna chochote cha hakika! Hakuna Mwadventista mashuhuri anayejulikana katika kipindi hiki kuwa aliweka bomu kwenye sanduku la barua, au kuwashikilia polisi akiwa amewaelekezea bunduki, au kumteka nyara mrithi wa mtu tajiri. Mbali na pengine kufanya kazi Jumapili  hapa na pale kinyume na sheria za bluu (blue laws), bila shaka walikuwa raia wema; walakini, katika makala na barua ambazo zilichapishwa baadaye katika Testimonies To the Ministers, (Shuhuda kwa Wachungaji) nabii wao alisema mambo mazito sana kuwahusu.

Mara kwa mara katika mawasiliano haya Ellen White aliwasilisha uzuri wa hali ya juu wa Yesu Kristo na kisha, kinyume kabisa, ushahidi kwamba uongozi, waumini, taasisi, makongamano, nyanja za misheni, na kanisa kwa ujumla, walikuwa wakihitaji sana matengenezo. Tena na tena alisisitiza kwamba “si wachache, bali wengi” (sisitizo lake) wamekuwa wakipoteza bidii yao ya kiroho na kuiacha nuru. Kumekuwa na "kurudi nyuma vya kushangaza" kati ya watu wa Mungu.

Kanisa li "baridi," upendo wake wa kwanza umeganda/umepoa. Viongozi katika Battle Creek wamempa Bwana migongo; washiriki wengi wa kanisa pia wamekataa uongozi Wake na badala yake wamechagua Baali. Wenyeviti wa makonferensi wanatenda kama maaskofu wa zama za kati, huku "mikutano mizima" na "kila taasisi" ikipotoshwa kwa kanuni. Baadhi ya viongozi kwa kweli "hujisifu" kwamba hawatafuata shuhuda. “Upofu wa ajabu” umemjia mwenyekiti wa Konferensi Kuu kiasi kwamba hata yeye anafanya kinyume na nuru. Hali ni mbaya sana katika jumba la uchapishaji la Battle Creek kiasi kwamba "mbingu zote zimekasirika."

Hakika, Bwana "ana ugomvi na watu Wake," na hivi karibuni "atafanya mapinduzi katika taasisi zinazoitwa kwa Jina Lake."[3] Ilikuwa mfululizo mbaya wa mashtaka. Lakini ni nini hasa walikuwa wanafanya vibaya? Hapa kuna jibu kutoka kwa Testimonies to Ministers, ukurasa wa 441: "Ikiwa una kiburi, kujistahi, kupenda ukuu, majivuno, tamaa mbaya, manung'uniko, kutoridhika, uchungu, matukano, kusema uongo, udanganyifu, matusi, sio Kristo anayekaa moyoni mwako, na ushahidi unaonyesha kwamba una akili na tabia ya Shetani ... Unaweza kuwa na nia nzuri, msukumo mzuri, unaweza kusema Ukweli kwa ufahamu, lakini haufai kwa ufalme wa mbinguni."

Kusengenya. Kulalamika. Kumtilia shaka Mungu, ulaghai na kadhalika. Walikuwa wakitenda kama Wakristo wa kawaida, wakati walipaswa kushirikiana na Kristo katika kufuta dhambi, wakiakisi kwa ulimwengu uzuri wa Yesu, wakiangaza utukufu wa tabia ya Mungu katika utakatifu wa Sabato, na kujitayarisha wenyewe, kwa neema yake, kuwa vyombo safi kwa ajili ya kumwagwa kwa Roho Wake kwa ulimwengu katika mvua ya masika. Walikuwa wamepokea nuru kuu—mnamo 1888 na, kwa jambo hilo, tangu siku za Wafuasi wa Miller, walikumbushana kwa machozi ya furaha katika mikutano yao ya ushuhuda kwamba waliipenda nuru hii.

Lakini wengi wao hawakuiishi nuru. "Hebu wahudumu wetu na wafanyikazi watambue kwamba sio nuru iliyoongezeka wanayoihitaji ..., zaidi ya kuishi nje ya nuru ambayo tayari wanayo,"[4] alionya Ellen White. Bibi S. M. I. Henry alidadavua hali hiyo kwa njia nyingine ya General Konferensi ya 1899: "Kama vile vitu vitamu, vinapogeuka kuwa vichafu, vinakuwa vya kuchukiza zaidi, hivyo kugeuka dhidi ya nuru kuu na Ukweli ni kuanguka katika giza kuu na uovu. Watu hawa wamekuwa na nuru ya ajabu."[5] Imesemwa kwamba, kwa kuwa Bwana hawezi kuwajaribu watakatifu kwa uovu, Shetani huwapata kwenye mambo wanayopendelea. Wito wa Kibiblia wa kujitenga na ulimwengu (1 Wakorintho 6) ulipotoshwa na adui na kuwavuta Waadventista katika makundi makundi, hasa pale Battle Creek.

Mapema kama 1879, wakati Battle Creek ilihesabu waumini 700 au 800, uongozi ulichapisha katika Review kwamba si ruhusa kwa mtu mwingine yeyote kuhamia huko bila mashauriano ya awali.[6] Hii haikusaidia. Idadi iliongezeka kufikia miaka ya 1890 hadi 2000. Wakiwa wamejikusanya wote na kuishi mahali pamoja tu kwa kufanya koloni, badala ya kutawanyika kuuambia ulimwengu ujumbe, walionyesha wasiwasi wao juu ya mafanikio ya kusudi kwa kujadili makosa ya washiriki wengine. Karibu mwaka wa 1900 mithali ilipita kati ya watakatifu kwamba hata Gabrieli mwenyewe angetoa wito kwa Battle Creek, hata yeye hangeweza kuepuka lugha zao za kutikisika.

Tamaa ifaayo ya kuwaongoza watu kuufikiria vyema ujumbe wa Waadventista kwa kufanya mambo ambayo "yangeipa kazi hiyo tabia," ilisababisha ujenzi wa vituo vikubwa zaidi na ununuzi wa vifaa vya kisasa zaidi hadi, ukubwa wenyewe ukadhoofisha mwenendo wa kazi na wafanyakazi. Ofisi za Review zikawa na idara za uchapaji, idara ya kulainisha jalada za vitabu, idara ya kubana karatasi yaani Binding, na idara za ufungaji na mitambo hamsini ya mvuke, jumba kubwa la uchapishaji huko Michigan; lakini walishindwa kujiuliza ikiwa ni lazima kiwanda kuwa kikubwa hivyo.

Kilichokuja kuwa cha lazima, ili kuweka mitambo ya gharama kubwa iendelee na wafanyakazi wengi walioajiriwa, ilikuwa ni kuchapisha karibu kila kitu kilichokuja na riwaya za kawaida, ikiwemo matangazo ya pombe, na hata kazi ya umizimu

hazikukataliwa ili tu wajipatie fedha.[7] Ellen White alisema kwamba Mungu alitaka Dk. Kellogg awafanye wagonjwa wake kukutana na Yesu na Ukweli wa leo; lakini chumba cha Sanitarium, pamoja na ghorofa zake zote moja juu ya nyingine na majengo yake yote moja kando ya lingine, yalichukua muda mwingi wa daktari huyu. Pamoja na wingi kulikuja "sera ya kidunia" na kusababisha kushuka kwa malengo ya kiutume katika taasisi ya afya.

Baada ya 1897, Kellogg alisisitiza kwamba sanitarium yake ilikuwa "undenominational" Yaani isio ya kidhehebu. Katika Review hiyo, wasimamizi, hasa Kapteni Clement Eldridge mapema katika muongo huo na Archibald R. Henry baadaye, waliweza kujiongezea mishahara yao wenyewe huku wakipunguza mishahara ya wafanyakazi wengine. Katika Review ya siku za awali kila mtu alihisi kwamba alikuwa akijitoa kwa namna iliyo sawa. Ukosefu wa usawa ulileta kutoridhika, malalamiko na mashaka. Henry alipopata nafuu mwaka 1897, alifungua shitaka la madai ya $50,000[8]—tofauti kabisa na roho ya mtindo wa Rochester na kipindi cha kuanzishwa kwa Avondale.

Mojawapo ya dosari za Miaka Kumi na Sita ya Mgogoro ilikuwa, kwa kweli, mfululizo wa kesi miongoni mwa waumini. Katika uchungu Ellen White aliomba siku za kwanza za kujitolea na akamnukuu Paulo: "Kuna hatia kati yenu, kwa sababu mnashtakiana. Ndio maana mnadhulumiana na kudanganyana" 1 Wakorintho 6:7. Alionya pia, kama mjumbe wa Bwana, kwamba walikuwa wakimtukana Yehova na ingekuwa vyema pia "kuacha kusali kwa Mungu, kwa maana Yeye hatasikia sala zao."

Akirejelea angalau kesi moja ya nyakati hizo, Ellen White alikiri kwamba mshitaki huyo alidhulumiwa waziwazi lakini akasisitiza kwamba ukosefu wa haki haukuhalalisha kwenda mahakamani. Mungu atalipiza kisasi, alikumbusha. “Uwe na imani kwa Mungu; kwani Yeye ameahidi kwamba atasikia maombi ya imani.”[9] Kwa kiwango kikubwa zaidi, maneno ya Kristo yakiwaita kuwa na umoja (Yohana 17) yalipotoshwa na adui hadi kusababisha mambo mengi kufanywa na ofisi moja, inayojulikana na watu wa wakati huo kama "nguvu ya kifalme-au aina ya udikteta," ambayo ilichukua muundo wake kutoka kwa msingi wa muundo wa kanisa wakati huo.

Utakumbuka kwamba shirika la kwanza kupigiwa kura na Waadventista Wasabato lilikuwa chama cha uchapishaji. Miaka miwili baadaye General konferensi ikaanzishwa, ikiwekwa kielelezo cha katiba rahisi inayotekelezeka na kutengwa kisheria na chama cha uchapishaji. Wakati Taasisi ya Matengenezo ya Afya ya Magharibi ilipoanzishwa mwaka 1866, iliungwa mkono na chama kilichojitenga na General Konference. Hivi ndivyo wanachama walivyotaka. Kufikia mwishoni mwa miaka ya 1890 vyombo vya habari, ambavyo sasa vilikuwa vikubwa sana, vilikuwa vimejitenga; na Taasisi ya Afya, ambayo ilikuwa imekuwa na kuwa msururu wa

sanitariums ishirini na saba, ilisimamiwa na Shirika la Kimataifa la Wamishenari wa tiba na Wafadhili, lisilotegemea jimbo kuu la kanisa.

International Tract and Missionary Society na International Sabbath School Association, vyote vilitokana na Jumuiya ya Kimataifa ya Uhuru wa Kidini, iliyoanzishwa mwishoni mwa miaka ya 1860 na mwanzoni mwa 1870, pia ilikuwa na makao makuu tofauti na uongozi mkuu wa kanisa. Kwa maneno machache, kufikia miaka ya 1890 kulikuwa na mashirika madogo madogo mengi sana. Kulikuwa na uchache sana kwa kuwa vyama na jumuiya nyingi tofauti zilifanya kazi zaidi au kidogo kwa kujitegemea na wakati mwingine kwa kweli kushindana. Kulikuwa na changamoto nyingi mno kwa sababu maamuzi yote makuu na mengine mengi madogo yalifanywa huko Battle Creek, ama na General Konferensi au na uongozi ufaao wa "chama" au "jamii" iliyoishi huko. Uhuru mdogo tu wa kufanya maamuzi ndio ulioachwa kwa makanisa mahalia, miungano, jumuiya, au misheni. Mwelekeo ulikuwa, kwa kweli, kuzidisha nguvu ya utawala wa ofisi kuu.

Mapema miaka ya 1890 hatua zilianza kuunganisha nyumba mbili za uchapaji yaani Review and Herald na Pacific Press. Ellen White aliandika vikali akipinga uunganishwaji huo wa kitaasisi na akaokoa mambo na kufanikiwa. Alisema Bwana alitaka waumini wengi zaidi, si wachache, katika nafasi za kufanya maamuzi, na alitoa sababu tatu ni kwa nini: (1) kuzuia udhaifu wa mtu mmoja kudhoofisha kazi yote; (2) kukuza viongozi zaidi kwa kuweka wajibu kwa walio wengi zaidi; na (3) kuwafanya watu wengi zaidi wamtegemee Mungu badala ya mtu mwingine.[10]

Mnamo 1896 Ellen White aliandika kutoka Cooranbong, Australia: "Mpangilio kwamba pesa zote lazima zipitie Battle Creek na chini ya udhibiti wa watu wachache mahali hapo ni njia mbaya ya kusimamia .... Je, watu hawa wangejua ni nini mahitaji ya kazi ya Mungu katika nchi za nje?" Katika waraka huohuo alipendekeza kwamba mwakilishi wa General konferensi ateuliwe kufanya kazi katika kila nchi, ili maamuzi yaweze kufanywa mahali watu wanaishi. Aliongezea kuwa mwakilishi huyu, anaweza kuwa mlei na anapaswa kusaidiwa na timu ya washauri.[11] Desturi ya kufanya maamuzi yote hapo Battle Creek ilikuwa na madhara hasa kwa sababu kamati zilizofanya maamuzi zilikuwa ndogo sana.

Kwa mfano, kamati kuu ya Konferensi Kuu ya 1863 ya wajumbe watatu ilitosha wakati washiriki walikuwa 3500. Ilipanuliwa hatua kwa hatua, na kufikia watu 13 mwaka 1897, lakini kufikia wakati huo kanisa lilikuwa likienea duniani kote, na washiriki walikuwa zaidi ya 70,000. Ndivyo hali ilivyokuwa kiujumla nayo ikaelezea hali ya bahasha tupu iliyowasili Australia mnamo Mei 2, 1899. Hata hivyo, licha ya ukarimu wa uongozi mkuu kwa maeneo ya mbali ya misheni, hali ya kifedha haikuwa nzuri hapa nyumbani Marekani.

Kufikia 1901 General Konferensi ilisukumwa kukopa pesa hata kusaidia wamisionari wake. The Battle Creek Sanitarium ilikuwa na deni la $200,000. Shule na vyuo mbalimbali vilidaiwa $330,000. Na huko Ulaya, shirika la uchapishaji la Oslo (wakati huo Christiania), Norway, lilikuwa limefilisika na lilikuwa katika hatari ya kufungwa, kama lile la Czechowski, mikononi mwa wadai wake. Katika hali hiyo ya dharura, Ellen White aliwasihi watoto wa kanisa hilo waachane na zawadi zao za Krismasi na kuwaomba wazazi wao watoe pesa sawa na zile za zawadi, kwa ajili ya kusudi la injili.[12]

Mnamo Aprili 1901, akitazama kwa huzuni na kwa dhati katika nyuso za viongozi waliokusanyika kwa ajili ya kikao cha General Konferensi session, aliomboleza kwa machozi kwa sauti yake, “Ee, nafsi yangu imehuzunishwa na mambo haya. … watu wanapaswa kusimama mahali Patakatifu, kuwa kama sauti ya Mungu kwa wanadamu, kama vile tulivyoamini kuwa General Konferensi lingekuwa, Tunachotaka sasa ni kuundwa upya kujenga juu ya kanuni tofauti."[13]

*Maelezo:*

*1. The story of the founding of the Avondale school has been retold many times. See particularly Arthur L. White, "Prophetic Guidance That Launched a College," two parts, Review and Herald, April 3 and 10, 599 1958; A. G. Daniells, "Establishing the Australasian Missionary College," in Arthur L. White, ed., Notes and Papers (Washington, D.C.: Ellen G. White Estate, 1962), pp. 265, 276; A. G. Daniells, The Abiding Gift of Prophecy (Mountain View, Calif.: Pacific Press Publishing Association, 1936), pp. 315, 316*

*2. Ellen G. White, Letters 40, 41, and 64, dated 1894*

*3. Ellen G. White, Testimonies to Ministers, pp. 449, 450; 162-168; 89; 467; 362, 359, 372, 373; 327; 467; 372; 373*

*4. Ibid., p. 439*

*5. Henry, 'Women's Work," General Conference Bulletin, 1899, p. 174*

*6. Review and Herald, May 1, 1879, p. 140*

*7. ct. Ellen G. White, Testimonies, vol. 7, pp. 164-168*

*8. David Neff, "A. R. Henry and His Lawsuit" (term paper, Andrews University, 1973)*

*9. Ellen G. White, Letter 61, 1898, and Manuscript 72, 1898; manuscript release no. 334 600*

*10. Ellen G. White, Testimonies, vol. 7, pp. 171- 174; also Arthur L. White, "Confederation and Consolidation," manuscript deposited in Ellen G. White Estate*

*11. White, Testimonies to Ministers, p. 321*

*12. Ellen G. White, Manuscript 71,1900; manuscript release no. 419*

*13. Ellen G. White, opening address at the 1901 General Conference, General Conference Bulletin, 1901, p. 25*

## SURA YA 31
## MDUARA WA UPENDO

Viongozi wa Kanisa la Waadventista Wasabato hawakufanya maamuzi yenye busara kila mara katika miaka ya 1890, lakini kwa sehemu kubwa walikuwa watu waliohamasishwa sana, waliojitolea kutekeleza majukumu yao kama walivyoyatazama, walifanya kazi kwa muda mrefu, mara nyingi kwa faida ya makonferensi/majimbo yao wenyewe, wakijaribu kuunda kitengo chochote cha muundo wa madhehebu walichopewa.[1]

Msimamizi wa pwani ya magharibi ambaye alishindwa mara ya kwanza kutuma dola 1000 huko Australia hakuziweka pesa hizo mfukoni mwake! Hakika hakuwahi kufikiria jambo kama hilo. Lakini wala hakufikiria kuhusu mahitaji ya uwanja wa utume nchi nyingine, ingawa yalikuwa yameletwa kwake mara nyingi. Katika saa ambayo ilihitaji mipango mipana na imani kuu, rekodi ya uongozi wa kanisa ilimkatisha tamaa, si sana kwa sababu ya jinsi hali ilivyokuwa ila kwa sababu ya jinsi ingeweza kuwa.[2]

Ni nani mwenye haki vya kutosha na kisha aanze kutupa jiwe la kwanza ili kumpiga mtu mwenye dhambi? Ili kuhakikisha tathmini iliyo na msawaziko leo, inafaa kukumbuka tena maendeleo ya haraka yaliyoashiria Miaka Kumi na Sita ya Mgogoro - faida katika kuwa mshiriki, taasisi, na nchi zilizoingia, na katika "kumweka Kristo" katika mahubiri mengi na machapisho. Hakika Ellen White hakukata tamaa! Akijua vizuri zaidi ya mtu mwingine yeyote mapungufu na ubora wa viongozi wa kanisa, alitambua baadhi ya waliojaza nafasi zao za kamati kuu kuwa "watu wenye kiasi na wenye nia sawa."[3] Naye alitetea kwa uthabiti dhehebu kwa ujumla kutoka kwa wale waliotumia udhaifu wa dhehebu kuhalalisha upotovu wao wenyewe.

"Kanisa la Kristo," aliandika kutoka Australia—akirejelea kwa bidii kanisa ambalo lina imani ya Yesu na kushika amri za Mungu—"kanisa, japo ni lenye kudhoofika na lenye dosari jinsi liwezavyo kuwa, ndicho kitu pekee duniani ambacho Yeye hukipa heshima Yake kuu."[4] Aliweka maisha yake mahali alipoweka maneno yake. Wakati katika mwaka 1891 General Konferensi ilipomtaka aende Australia, yeye hakutaka kwenda. Alikuwa na umri wa miaka 63, mjane, na alikuwa akifanya kazi kupita kiasi. Lakini yeye alifanya uamuzi akaenda. Alipofika aliugua sana kutokana na ugonjwa wa baridi yabisi. Kama wamishenari wengi wapya, alitamani angerudi nyumbani na kujiuliza kwa nini amewahi kuondoka.

Mara nyingi usiku kuna wakati hakuweza kulala, alitaka kulia. Akipinga msukumo huo, alijisemea: "Ellen G. White, unamaanisha nini? Je, hujafika Australia kwa sababu ulihisi kwamba ilikuwa ni wajibu wako kwenda ambapo General Konferensi iliamua kuwa ni bora kwako kwenda? Je, haya hayakuwa mazoea yako?" Alijibu kila swali kwa uthibitisho na kuendelea. "Basi kwa nini wewe unahisi umeachwa na Bwana na kukata tamaa? Je, hii si kazi ya adui?" "Naamini ni kazi ya adui." Huku akifumba na kufumbua macho yake, alihitimisha, "Inatosha; sitaangalia upande wa giza tena. Ikiwa ni kuishi au kufa, naweka ulinzi wa roho yangu kwa Yeye aliyekufa kwa ajili yangu."[5]

"Nilifuata sauti ya General konferensi [kwa ujumla]," aliandika baadaye mwaka huo huo (1892), "kama nilivyowahi kujaribu kufanya wakati sikuwa na mwanga wazi mwenyewe. ... sasa niko Australia na ninaamini niko pale ambapo Bwana anataka niwe."[6] Hakika alikuwa sahihi. Akitumia mtaji wa kutengwa kwake na kituo kikuu cha kazi na viongozi wake ambao walikuwa wepesi sana wa kufanya mabadiliko, alikinyanyua chuo kutoka kwenye umaskini na mikaratusi ambacho kingekuja kuwa "kiwango na mwongozo" wa mapinduzi kwa vituo vya elimu ya Waadventista kwa siku zote zijazo. Watu walipokuja kutembelea Avondale na kuchunguza maendeleo yaliyokuwa yakifanywa, Dada White alizungumza kwa maneno yenye kung’aa na ya kuthamini zawadi ambazo Waadventista wa Marekani na Afrika walikuwa wametoa mara kwa mara kiasi kwamba wageni walivutiwa sana.

Alitoa somo kwamba kwa kuzingatia michango hii “tuko chini ya wajibu mkubwa, hapa Australia, kujitoa wenyewe kwa kazi ya Bwana, na kuelimisha na kuzoeza vijana wa kiume na wa kike ili waweze kufaa na kuwa tayari kumtumikia Bwana katika misheni za nyumbani na nje."[7] Katika masikio ya umma hakutoa malalamiko yoyote kuhusu ahadi ambazo hazijatekelezwa au mapungufu ya wasimamizi. Hata kwa watu wa ndani aliweza kuzungumza katika miaka hiyo akiwa na imani ya ajabu juu ya mustakabali unaoongozwa na Mungu wa harakati ambayo hadi sasa alikuwa amejitolea maisha yake.

"Hakuna haja ya kuwa na shaka, kuwa na hofu kwamba kazi haitafanikiwa," alitangaza kwa ufahamu wa kinabii. "Mungu Ndiye kiongozi wa kazi, na ataweka kila kitu katika utaratibu. Ikiwa mambo yanahitaji kurekebishwa katika ofisi kuu ya kazi, Mungu atashughulikia hilo, na kufanya kazi ya kurekebisha kila kosa. Hebu tuwe na imani kwamba Mungu anaenda kuibeba merikebu tukufu inayobeba watu wa Mwenyezi Mungu na kuifikisha bandarini salama."[8] Matukio, kama kawaida, yameelekea kuthibitisha haki Yake. Baadhi ya hatua zilikuwa tayari zimechukuliwa, na nyingine zilifanyika hivi punde, ili kurekebisha tatizo la kujilimbikizia madaraka na “mamlaka ya kifalme,” hatua ambazo leo bado zinaathiri kanisa siku zote.

Mnamo mwaka 1889 makonferensi huko Amerika Kaskazini yaliwekwa katika "wilaya" sita, kila moja chini ya "msimamizi" anayewakilisha ofisi kuu. Mnamo mwaka 1891[9] A. T. Robinson alitumwa kuandaa mkutano wa misheni nchini Afrika Kusini. Ilifikiriwa kuwa angeunda "jumuiya" na "vyama" vya kawaida. Lakini angewezaje? Alikuwa na watu wachache kwenye kamati nyingi sana. Aliamua kujumuisha vyama vyote katika muundo wa makao makuu kama "idara" za mtu mmoja. Aliomba ruhusa kutoka kwa Battle Creek, akisubiri majibu ya barua kwa mwezi mzima. Viongozi wakuu walipinga vikali mpango wake lakini kama kawaida walikuwa nyuma sana katika kazi yao.

Robinson alitafsiri kucheleweshwa kwao kama idhini na kusonga mbele. Hati yao ilipofika, mfumo mpya ulikuwa ukifanya kazi vizuri sana, hakuubadilisha. Wakati huo huo Australia ilikuwa imeteuliwa kuwa "Wilaya Na.7." Mnamo 1894 ilijipanga upya kama Union Konferensi ya Australasia, muungano wa kwanza. Nafasi ya msimamizi huyo ilichukuliwa na orodha ya maofisa wa utawala na kamati iliyowakilisha majimbo ya eneo hilo. Mnamo 1897 Robinson aliitwa kutoka Afrika Kusini kuwa mwenyekiti wa Konferensi ya Australia ya Kati na akakuta kundi la kawaida la jamii na vyama likimngoja alipofika. Alizivunja na kuziweka katika idara za makonferensi. A. G. Daniells na W. C. White waliogopa—hadi walipoona jinsi "mpango wake wa Victoria" ulivyofanya kazi; hapo ndipo waliposhawishi makonferensi yao mengine na Muungano mpya wa Australasia pia kujipanga upya katika idara.

Uzoefu na idara na vyama vya wafanyakazi katika ngazi ndogo ya eneo ulitoa ushahidi muhimu kwa General Konferensi ya mwaka 1901 kwamba programu ilikuwa nzuri. Mnamo 1897 kikao cha General konferensi, ambacho kilikutana katika Chuo Kikuu cha Union Nebraska, kilifanya kamati ya Konferensi Kuu kuwa na wawakilishi zaidi kwa kuipanua hadi kuwa na wawakilishi kumi na tatu. (Ilikuwa imepanuliwa kutoka wajumbe watatu hadi watano mwaka 1883, na kisha kufikia wajumbe saba katika mwaka 188). Kikao hicho pia kilirekebisha baadhi ya kamati, kikagawanya kazi za mwenyekiti kati ya watu kadhaa, na kutoa uhuru kiasi fulani wa mamlaka katika fildi za Ulaya na Australasia lakini pamoja na kwamba hili lilionekana la kuvutia lakini bado liliacha mahitaji fulani ya uboreshaji mkubwa unaohitajika ambao haukuguswa.

Mkutano Mkuu wa 1899 ulikuwa wa kawaida. Mkutano Mkuu wa 1901 ulipata maendeleo makubwa. Sio kwamba mtu yeyote alifikiria ingekuwa hivyo. Ellen White mwenyewe alisema baadaye "Sikutaka kuja Battle Creek. Niliogopa mizigo ambayo ningelazimika kubeba ambao ungegharimu maisha yangu." Viongozi walipomtaka kuhudhuria, alisema hawezi. Mungu alipomwambia aende katika maono, alitii.[10] Mnamo Aprili 1, siku moja kabla ya kikao rasmi kufunguliwa, Bibi White, aliwasili karibuni kutoka Australia, na  alikutana na viongozi katika maktaba ya chuo.

Alikuwa ameonyeshwa maisha ya ndani kabisa, ya wengi wao, alikuwa ameandika ushuhuda kwao, aliwajua vizuri zaidi kuliko walivyojijua wenyewe. Hawa walikuwa viongozi wa kazi ya Mungu, na kama mama wa kweli katika Israeli, aliwapenda wote. Kwa uthabiti aliwasilisha muhtasari wa jumbe ambazo angewapelekea hadharani kwa muda wa wiki kadhaa zijazo, ili waweze kupata manufaa ya kujua nini cha kutarajia. Kimya kimya wajumbe waliahirisha ili kutafakari shida au mzigo wake mzito. Asubuhi iliyofuata walikusanyika tena katika kanisa kubwa liitwalo Dime Tabernacle. Pamoja na mnara wake wa saa unaovutia, matakia yake mekundu, na vinara vyake vya kupendeza, maarufu "Dime Tabernacle,"[11] jengo kubwa zaidi katika Battle Creek na kwa hakika kanisa kubwa zaidi katika dhehebu, liliketisha zaidi ya watu 2500 bila kusongamana.

Katika tukio hili, wakiwa wamejazana kwenye ghorofa, inasemekana kuwa waliketi watu 4,000, bila shaka hawakuweza kukaa kwa starehe kwa sababu ya msongamano. Picha inayojulikana sana ya Ellen White akihubiri ilichukuliwa alipokuwa akizungumza katika kikao hiki cha General Konferensi. Ndani yake wajumbe wenye ugumu wa kusikia wanaweza kuonekana wakiwa wameketi kwenye ngazi zilizopanda kutoka jukwaa hadi kwenye balcony. Kuna piano kwenye picha kwa bahati, lakini hakuna ogani. Washiriki walikuwa wametamani ogani ya muziki, lakini kutoka Australia Ellen White alikuwa amewahimiza kuhifadhi pesa kwa ajili ya utume.[12]

Mwenyekiti Irwin alifungua mkutano kwa matamshi yanayofaa; kisha Ellen White akasonga mbele. Ulikuwa Mkutano wake Mkuu wa kwanza katika miaka kumi. Alitoa ushuhuda wa moja kwa moja kwa wajumbe.[13] "Huna haki ya kusimamia," alisema, "isipokuwa unasimamia kwa utaratibu wa Mungu!" "Mungu hajaweka mamlaka yoyote ya kifalme kati yetu." "Ili watu hawa wasimame mahali Patakatifu, hebu pawe sauti ya Mungu, ... " Nini basi kifanyike? "Tunachotaka sasa ni kupanga upya ... kwa kanuni tofauti."

Kanuni mpya ilikuwa "upendo." Upendo wa aina gani? Upendo kama vile Yesu alituonyesha, alieleza. Upendo unaofanya kazi katika faragha ya familia ya mtu. Mapenzi ambayo humfanya mtu asiseme na kulalamika anapokuwa kazini. Upendo unaochukua "jukumu la kutimiza agizo la Kristo, "Enendeni ulimwenguni mwote." "Wakati umefika ambapo watu hawa watazaliwa mara ya pili," alihimiza. Kisha akatazama kwa bidii kwenye bahari ya nyuso za watu mbele yake, basi alipokuwa akiangalia ukumbi mkuu, kibaraza/balcony, na ngazi, alisema, "Nataka kuwa na nyumba na waliobarikiwa huko mbinguni, nami nataka wewe uwe na nyumba huko. Ninataka kufanya kazi kwa kupatana na ninyi." “Acheni kila mmoja wenu aende nyumbani [kwenye nyumba zenu au vyumba vyenu ambamo mnakaa] si kuzungumza zungumza, bali kusali.”

Alipoketi chini, kutaniko kubwa sana lilinyamazishwa, likijawa na majuto ya matendo yao ya siku za nyuma, matumaini ya siku zijazo, na maazimio ya sasa. Mzee A. G. Daniells aliinuka, Alikuwa amefanya kazi na Ellen White kwa miaka mingi huko Australia na kupitia uzoefu mwingi alijifunza kuamini mwongozo wake. Katika hafla hii ilikuwa kwamba taratibu za kawaida na mipango ilikusudiwa kuwekwa kando, na kwamba kamati kubwa sana iteuliwe kufanya upangaji upya, unaofanya kazi chini ya kanuni za bunge kwa ajili ya "kamati nzima," utaratibu usio rasmi. Nia yake ilikuwa kutoa uhuru wa juu wa majadiliano ili Roho Mtakatifu apate nafasi ya kutosha ya kufanya kazi ambayo iliongeza zaidi maana ya dhamira ya kikao. Dk. Kellogg alitoa jumbe za kusisimua, akisisitiza jukumu la kazi ya umishenari wa tiba katika kuongoa roho.

Saa 11:30 asubuhi mnamo Aprili 3 Mzee Daniells aliwasihi wajumbe wakumbuke kwamba Marekani ni moja tu ya ishirini ya idadi ya watu duniani. "Nje ya nchi hii kuna kumi na tisa ya ishirini ya wanadamu!" "Hata hivyo kati ya waumini 75,000 wa ujumbe wa malaika wa tatu, karibu 60,000 wako hapa Marekani!" Alikiweka kidole chake kwa nguvu kuelekea ramani ya dunia iliyokuwa ukutani nyuma yake. "Katika ulimwengu leo kuna makafiri au wakana Mungu wapatao 1,000,000,000. Kati ya 1,400,000,000 wanaoishi, angalau theluthi mbili ni wapagani." (leo dunia ina watu bilioni nane na kati ya hao karibu bilioni nne hawajasikia kisa cha msalaba vema, hawa ni kama wale wa nchi 54 zinazoitwa dirisha la 10/40 kama Wahindi, Waislamu, Wayahudi, Budha, Hindu, Wakomunisti, Shintoism, Confusius na hata Secularists)[14]

Ellen White alikuwa amesimama kwa miguu yake tena na tena ili kuongeza uzito wa ushuhuda wake kwa changamoto za kutia moyo kama hizi. "Shamba ni ulimwengu," alilia. Lakini Je, Konferensi kuu imetambua hili? Aliuliza. Kwa uwazi akipitia uzoefu wake mwenyewe. "Nilimwambia Bwana kwamba nitakapokuja Battle Creek wakati huu, ningeuliza kwa nini umetunyima fedha kufanyia kazi huko Australia .... Tunatamani kwamba katika mkutano huu kazi iwe imara kiasi kwamba hakuna kitu kama hicho kitakachofanyika. Watu wawili au watatu, ambao hawajawahi kuona mashamba tasa ... hawapaswi kudhibiti mambo."[15]

Pia alitoa mwito tena na tena kwa madaktari na wahudumu kutotengana na kutojiruhusu kugawanywa na wivu, kutoelewana, na ugomvi. "Nataka kukuambia," alionya "kwamba hivi karibuni hakutakuwa na kazi itakayofanywa katika safu za wahudumu bali kazi ya umishenari wa tiba."[16] Wajumbe walilainishwa chini ya jumbe hizi. Mabadiliko makubwa yalifanyika, na mwishowe wengi walitamani kumsifu Mungu kwa ajili ya kazi ya kushangaza Aliyokuwa Ameifanya mioyoni mwao wakati wa mikutano kiasi kwamba huduma mbili za muda mrefu za ushuhuda zilihitajika.

Mabadiliko yaliyopatikana yanabaki kuwa muhimu sana hata leo. Kwa mfano, "wilaya" huko Amerika Kaskazini (huku kwenye uga wa Kusini ukiongoza) walianza kujipanga katika mikutano ya union kama ule mtindo wa Australasia. Matokeo yalikuwa kwamba vikundi vya makonferensi vilipata kipimo cha mamlaka ya kufanya maamuzi ambayo hayakujulikana hapo awali. Mpango huu wa kuweka mamlaka kwenye makonferensi ulipopanuliwa kwa ulimwengu wote, kama ilivyokuwa kwa wakati, mpango huo ulithibitika kuwa wa kusisimua na wa kuridhisha. Maeneo yaliyo mbali na makao makuu ya General Konferensi yaliachiliwa kufanya maamuzi yaliyoshughulikiwa hapo awali huko Battle Creek, na General Konferensi tu, na kanisa kuwekwa huru kutunza sera za kimsingi na uangalizi wa jumla.

Kisha, kamati ya Konferensi Kuu ilipanuliwa (wakati huo hadi kuwa na wajumbe ishirini na tano) ili kwamba kamwe wasije tena "watu wawili au watatu" kufanya maamuzi makuu kwa ajili ya kanisa zima. Hali hii mpya haikuwa tulivu. Kila mwenyekiti wa konferensi ya union alitangazwa kuwa mjumbe aliyetoka ofisini, na hii ilikuja kumaanisha kwamba watu waliosimamiwa kote ulimwenguni na waliochaguliwa katika maeneo ya ndani wangekuwa washiriki wa kamati ya Konferensi Kuu kama maafisa wanaoishi Marekani. Katika miaka ya 1970 wanachama katika kamati hii walikuwa zaidi ya 300! leo wapo zaidi ya 2000, na Afrika ina asilimia 51% ya washiriki wote duniani (zaidi ya nusu)

Maamuzi makubwa hayakuwahi kufanywa tena na watu waliofungiwa kijiografia katika Amerika Kaskazini tu. Sera pia zilizinduliwa mnamo 1901 ili kuhakikisha mkondo wa pesa kutoka katika maeneo yenye ustawi zaidi uende kwenye maeneo

yenye uhitaji zaidi wa kanisa. Mchakato ulianzishwa pia wa kujumuisha jumuiya na vyama mbalimbali (Shule ya Sabato, Kitengo cha Umishenari-Adventist Mission, n.k.) kama "idara" za konferensi zao (za mitaa, union, na division kwa jumla). Katika mabadiliko haya yote, ufahamu wa fildi za ulimwengu unaonekana. Idara na makonferensi ya union yalikuwa yameandaliwa awali katika maeneo ya utume. Na upangaji na mkakati mpya uliundwa ili kuwezesha usimamizi wa pesa uwe mzuri, watu, na kuwezesha kuwe na mamlaka kuelekea "kuuambia ulimwengu kwamba Yesu anarudi."

Kwa bahati mbaya, lilipokuja suala la idara, Jumuiya ya Wamishenari wa tiba na Wafadhili walisita. Ingawa hisia kati ya madaktari na wahubiri ziliboreka sana wakati wa kikao, hali ya kutoaminiana iliendelea kuwepo. Maelewano ya muda yalifanywa kwa kupiga kura kwamba wajumbe sita wa kamati ya Konferensi Kuu wachaguliwe kutoka kwa chama cha matabibu. Mkutano Mkuu wa General Conference, uliofuata ulifanyika mwaka 1903 huko Oakland, California (ambapo Pacific Press imefanya makazi, kabla ya kuhamia Mountain View). Mchakato wa kimsingi wa kuunda vyama vya watendakazi na idara ulikamilishwa, na umakini zaidi ulitolewa kwa kazi ya tiba.

Kwa bahati mbaya, kutoaminiana kati ya Dk. Kellogg na wachungaji kuliongezeka badala ya kupungua kwa muda huo. Hoja ilianzishwa ili kuziweka taasisi zote za Waadventista chini ya umiliki wa aidha konferensi ya ndani, Union, au Konferensi Kuu badala ya kuwa chini ya vyama vyao vilivyojitegemea- nusu-huru. Dk. Kellogg na idadi ya marafiki zake wa karibu walikataa mpangilio huo, lakini asilimia themanini ya wajumbe walipiga kura ya ‘ndiyo’. Ni nyumba moja tu ya sanitarium kule Battle Creek na moja kule Mexico ndizo ziliamua kubaki nje ya muundo wa Kimadhehebu.

Wakati huohuo (Februari 1902) jengo kuu la Battle Creek Sanitarium lilikuwa limeteketea kwa moto. Na wakati Dk. Kellogg alipokuwa katika harakati za kulijenga upya, jengo hilo la Sanitarium, Taasisi ya Uchapishaji ya Review and Herald pia liliteketea kwa moto (tarehe 30 Desemba). Ujumbe wa Ellen White kuhusu kuhama kutoka Battle Creek, sasa ukachukuliwa kwa umakini sana. General konferensi ya mwaka 1903 ilipendekeza kuhamisha ofisi zake na zile za Review and Herald mbali na Battle Creek. Marekebisho ya katikati ya hii njia yalikuwa yamekamilika sasa. Kanisa la Waadventista sasa lilikuwa limekata kamba iliyokuwa imeunganisha Battle Creek, Michigan, na Marekani. Na pale lilipohamia mji mkuu wa nchi yaani karibu na Washington D.C, pia lilisonga mbele katika maon ulioratibiwa ambao ulitoa uhuru bora wa kufanya maamuzi yenye usawa na uratibu bora wenye bidii (balansi).

Maendeleo mengine mawili mashuhuri ya upangaji upya wa miaka ya baadaye pia yanapaswa kutajwa. Katika uhamasishaji wa wafanyikazi huko Ulaya, kikao cha

Mkutano Mkuu wa 1913 kilianzisha ngazi mpya ya utawala, iitwayo "Divisheni," ambayo hata kufikia sasa tuna Divisheni kumi na tatu. Mgawanyiko huu unafikiriwa kuwa sehemu ya Konferensi Kuu unaofanya kazi katika sehemu mahalia ya ulimwengu. Wakati huo huo, kila mmoja anakumbatia idadi fulani ya vyama vya wafanyakazi. Kwa vile vyama vya wafanyakazi kwa upande wake vinaundwa na konferensi za mitaa na konferensi za mitaa za makanisa ya mtaa, nia ni kwamba hakutakuwa na kukatika kwa mawasiliano ya kiutawala kati ya mshiriki wa kanisa na ofisa mkuu wa Konferensi Kuu, na kwamba dhehebu litakuwa ni moja na lililounganishwa na likiendelea kuungana.

1. Kitengo kikuu cha pili cha utawala kilichoundwa tangu 1901-1903 kinapatikana kwa sasa tu Amerika Kaskazini nacho ni kitengo cha Waadventista weusi. Mwanzoni mwa karne kulikuwa na waadventista weusi mia kadhaa tu nchini Marekani. Kadiri washiriki wao walivyoongezeka, ndivyo idadi ya wachungaji wao ilivyoongezeka. Ellen White alihimiza kwamba sauti za watu weusi zisikike katika kamati wakilishi za dhehebu. Pamoja na ukuaji wa waamini weusi, ushauri huu ulifuatwa katika ngazi ya Konferensi Kuu. Kisha karibu mwaka 1940 majimbo kadhaa ya ndani yalifanya jambo la kujumuisha mhubiri mweusi kwenye kamati zao za mkutano ili kuwakilisha masilahi ya jamii ya watu weusi (Asilimia 51 ya Wasabato sasa huishi Afrika, na hii inaweza kufanya asilimia ya Wasabato weusi duniani kuwa 60% au zaidi, kwa vile kuna washiriki wa Carribean na America ya Kusini).

Mnamo 1944 sera mpya ilifungua njia kwa waumini weusi kuunda makonferensi yao wenyewe (yanayojulikana kwa njia tofauti kama makoferensi ya "rangi," "ya kikanda," au "maconference meusi"—colored or black conferences) ndani ya vyama vya wafanyakazi vilivyokuwepo, na isipokuwa tu katika Pasifiki Magharibi wengine wote walichagua kufanya hivyo. Matokeo yake weusi wengi wameletwa katika nyadhifa za uongozi, na ongezeko la ajabu la washiriki weusi limefanyika. Ukitazama nyuma katika vikao vya 1901 na 1903, Dada White alikuwa na sababu ya kufurahishwa na mabadiliko ya kiutawala. Naye alifurahishwa. Ingawa mara moja alisema kwamba siku ilikuwa imepita wakati Konferensi Kuu ilikuwa kama sauti ya Mungu, mwaka 1909 alijisikia huru na kusema, “Wakati,watu walipokusanyika katika Mkutano Mkuu, ilionekana kutoka sehemu zote za fildi kwa ajili ya shauri la ndugu utekelezwaji wa maamuzi mema ni lazima uzingatie uhuru binafsi na maamuzi binafsi na halipaswi kudumishwa kwa ushupavu na ubishi, bali kwa kutii amri...[17]

Mnamo mwaka 1913 aliongeza, "Ninatiwa moyo na kubarikiwa ninapotambua kwamba Mungu wa Israeli angali anawaongoza watu Wake, na kwamba ataendelea kuwa pamoja nao, hata mwisho.”[18] Lakini hakupendezwa kabisa na mwaka wa 1901. Wakati fulani baadaye katika maono ya adhuhuri, wakati yeye ameishika kalamu

yake tayari kujadiliana katika kikao kile, maono yalimbeba na kumrudisha kwa kile ambacho hakikutokea. Furaha ilifuata hapo awali katika kanisa au hema ya Dime (Dime Tabernacle). Maono yalielekea kufifia mawazoni mwake.[19] Kikao cha 1901 bila shaka kilikuwa ushindi mkubwa. Lakini hisia binafsi ziliendelea kutawala kati ya wahubiri/wachungaji na madaktari; na Dada White alipomfikiria Dk. Kellogg, moyo wake ulikaribia kuvunjika.

Alijisikia kama Daudi baada ya ushindi katika msitu wa Efraimu: "Ee Absalomu, mwanangu, mwanangu!" Lakini mpasuko katika idara ya utume kwa njia ya tiba, badala ya kupungua, ulinolewa na kupanuka zaidi baada ya kikao cha 1903. Ufuasi wa Kellog katika imani ya Pantheismu na kitabu chake cha The Living Temple na uhuru wake katika kikao cha mwaka 1903 uliwathibitishia wachungaji wengi katika kujitenga naye. Wakati huohuo, Ed Sutherland na Percy Magan, viongozi waelimishaji wanaofanya matengenezo, walikosa subira kwa wachungaji waliposhindwa kukubaliana na mawazo yao yote mapya katika Chuo cha Utume cha Emmanuel.

Katika "Mkutano wa Berrien Springs" wa mwaka 1904, Mkutano wa Michigan, uliofanyika kwenye chuo kikuu cha Emmanuel missionary college, suala la miaka Kumi na Sita ya Mgogoro lilikuwa kipaumbele. "Mama White," kama alivyojulikana kwa upendo wakati huo, alinyoosha mikono ya upatanisho kwa vikundi vyote vitatu. Lakini Sutherland na Magan, wakiwa wameudhiwa na wahubiri, walijiuzulu nyadhifa zao chuoni, huku Kellogg na wahudumu wa kanisa wakiendelea kuwa na misimamo ya zamani, na wagumu kuaminiana.

Alasiri moja wakati Kellogg alikuwa akitoa hotuba, aliona kwamba macho yote yalikuwa yameelekezwa kwa mtu nyuma yake. Alipogeuka tu, akamwona Mama White mzee akija kwenye jukwaa, na akampa mimbari. Hapo juu ya mimbari, huyu nabii mke alifungua moyo wake kwa sauti ya mama iliyosikika kwa kina ili kumwokoa daktari Kellog ikiwezekana. Kellogg alisogea kwenye ukuta wa nyuma. Ndugu yake Will alikuwa kwenye hadhira. Dada White alikumbuka siku ambayo mama yao, kabla hajalala usingizi wa mauti, alipomfanya Ellen aahidi kuwachukua wavulana wake pamoja naye katika ufalme wa mbinguni. Ndipo Will alilia. Na daktari Kellog yeye alisimama bila kuonyesha hisia yoyote- kisha akatazama saa yake, na kuona kwamba hakuwa na muda uliobakia ili kuiwahi treni ya kwenda Battle Creek, na hivyo alsogeza miguu yake kwa hatua za kwenda mbele na kutoka nje.

Kuondoka kwake kulileta picha fulani. Lakini Mama White hakukata tamaa. Kellogg kwa kweli hangeweza kurejea tena, lakini mama White katika uzee wake hakusita hasa lilipokuja suala la kazi ya kuwaokoa wengine. Alianzisha Chuo cha Wainjilisti wa tiba huko Loma Linda na kuhimiza uongozi wa huduma, kuajiri madaktari waliofunzwa huko Battle Creek. Daniels alijitoa mara moja, madaktari walijitoa, na

majeraha ya mpasuko wa zamani yakaanza kupona. Aliwafuata Sutherland na Magan kuelekea Kusini (kama tulivyoona), akawapa Shuhuda la karipio ambalo walilipokea kwa toba, hii ilipelekea uanzishwaji wa Chuo cha Madison na Sanitarium kupitia wao, naye akawa mshiriki hai wa bodi yao—wakati pekee aliowahi kuwa nao.

Aliketi kwenye bodi yao - na kuleta mshikamano katika kanisa na katika udugu mpana wa wafanyakazi wa Kiadventista. Miaka ya 1901 na 1903 ilikuwa ya msingi na muhimu. Mwaka 1904 pia Mama White alichukua nafasi yake katikati ya pembe tatu ya mgawanyiko na kuchora mduara wa upendo uliokuwa mkubwa vya kutosha kuchukua vyama vyote - na kuwaunganisha katika umoja wa kudumu.[20]

*Maelezo: 1.*

*1. On the topic of this chapter see C. C. Crisler, Organization (Washington, D.C.: Review and 624 Herald Publishing Association, 1938); Arthur L. White, "The Story of the General Conference of 1901," three parts, Review and Herald, March 29, April 5, and April 12, 1956; SDA Encyclopedia, art. "Organization"*

*2. General Conference Bulletin, 1901, p. 24*

*3. Ibid.*

*4. Ellen G. White, Testimonies to Ministers, p. 15*

*5. Ellen G. White, Selected Messages, bk. 2, pp. 233, 234*

*6. Ibid., p. 239*

*7. Review and Herald, October 18, 1898, p. 661*

*8. Ellen G. White, Selected Messages, bk. 2, p. 390*

*9. General Conference sessions were held annually through 1889, then biennially through 1905, approximately quadrennially through 1970, and are now described as "quinquennial."*

*10. General Conference Bulletin, 1901, p. 43*

*11. The name "Dime Tabernacle" came from the fact that Adventists all over the United States were asked to contribute one dime each per week for a year, and a fair part of the total cost of $26,000 was raised in this way. For one description see Arthur W. Spalding, Origin and History of Seventh-day Adventists, vol. 2, p. 112. Another "dime" project was the purchase of the missionary ship Pitcairn*

*12. Daily Bulletin of the General Conference, 1893, pp. 13-15*

*13. General Conference Bulletin, 1901, pp. 23-27*

*14. Ibid., pp. 48, 50*

*15. Ibid., pp. 84, 85*

*16. Ibid., p. 204*

*17. Ellen G. White, Testimonies, vol. 9, p. 260*

*18. Ellen G. White, Selected Messages, bk. 2, p. 406*

*19. Ellen G. White, Testimonies, vol. 8, pp. 104-106*

*20. For interpretation of the 1904 meeting I am indebted to Emmett K. Vande Vere, professor emeritus, Andrews University*

## SURA YA 32
## KUNG'AA KWA UTUKUFU WAKE

Siku ya Sabato asubuhi, Oktoba 21, 1944, siku iliyotangulia. miaka mia moja ya masikitiko makubwa ya kukatishwa tamaa kwa kuwa Yesu hakurudi kama walivyotazamia ile Oktoba 22, 1844, kundi la Viongozi wa Waadventista wa Siku ya Saba walifanya ibada ya ukumbusho kwa heshima ya waanzilishi wa ujumbe wa marejeo. Asubuhi iliyofuata, Jumapili, Oktoba 22, 1844 walifanya safari fupi ya kwenda kwenye kaburi la William Miller lililo karibu na nyumbani kwake. Miaka miwili kabla ya hili, “Sauti ya Unabii” ilikuwa imeenda pwani ya Atlantiki hadi pwani ya Pasifiki.

Ndugu walipofika mahali pale alipopumzika Miller, ulikuwa karibu wakati wa programu ya kila juma kuanza. Waliiacha redio ya gari imewashwa na vioo vikiwa chini wasije wakakosa hata kitu chochote cha mada ya ufunguzi wa kwaya ya King's Heralds. Katika jiwe la msingi la marumaru lililokuwa limechakaa kwa ajili ya hali ya hewa hapo waliandika jina la William Miller na tarehe ya kifo chake, 1849. Je, inaweza kuwa, lazima wangejiuliza kwa muda, kwamba kule kuchelewa kwa karne moja kulikuwa ni kuthibitisha kuwa tumaini la Miller ni la uongo kabisa? Kisha waliona moja ya aya zake alizozipenda, pia zilizochongwa kwenye uso wa jiwe uliochakaa: "Wakati wa mwisho uliowekwa utakuwa" Danieli 8:19.

Na walipokuwa wakitafakari juu ya uhakikisho wa unabii huu, sauti ya mtangazaji wa ‘Heralds of the King’ ilikuja ikielea angani: "Inueni tarumbeta na pigeni panda ya makelele, Yesu anakuja tena." Lisifuni Jina Lake! Yeye Anakuja tena. Lakini lini? Waadventista Wasabato kwa muda mrefu wamenukuu kifungu kutoka ukurasa wa 69 wa Kitabu cha Ellen White cha Christ's Object Lessons kilichochapishwa mwaka wa 1900: "Kristo anangoja kwa hamu kubwa kujidhihirisha Mwenyewe katika kanisa Lake. Wakati tabia ya Kristo itakapozaliwa kikamilifu katika watu Wake, ndipo atakapokuja kuwadai kama watu Wake."

Maneno hayo ni maelezo juu ya mojawapo ya ahadi za Yesu Kristo Mwenyewe: “kwanza jani, tena suke, kisha ngano pevu katika suke.." (Marko 4:28, 29) Wakati matunda yanapotolewa kwa maana mavuno yamekomaa. Wakulima hawavuni mashamba wakati machipukizi ya kijani yanapotokea, au wakati vichwa vya mbegu vinapoanza kuota. Wanatazama mchakato wa ukuaji kwa makini, wakipima unyevunyevu, rangi, na kila dalili nyingine za kuonesha hali ya mazao hadi kufikia

ukomavu mkamilifu zaidi. Kisha wanaleta mashine ya kuvunia na kuvuna mavuno, mara moja.

Yesu anangojea uzaliwaji kamili wa tabia Yake Mwenyewe ya neema, roho ya kusamehe, inayotoka ndani ya moyo na kugusa maisha ya wengine, uvumilivu, na ukarimu. Hakika! Kama Kuhani Mkuu katika Patakatifu pa mbinguni kwa zaidi ya karne amemwaga kwenye shamba la mavuno mng'ao wa utakaso wa Sabato; Kwa bidii amejishughulisha na "kufuta dhambi," sio tu kutoka katika kumbukumbu za mbinguni lakini pia kutoka katika maisha katika ulimwengu huu. Ni ajabu na la kufurahisha kiasi gani kufikiria kwamba siku moja ndoto Yake itatimizwa. Inasikitisha jinsi gani kwamba Amelazimika kungoja kwa muda mrefu sana.

Kifungu kingine katika Masomo kutoka kitabu cha  Christ's Object Lessons (ukurasa wa 419) kinahusiana na kile kilicho kwenye ukurasa wa 69. Kinasema, "Mbingu zote zinangoja mifereji ambayo kwayo mafuta matakatifu yanaweza kumwagwa ili kuwa furaha na baraka kwa mioyo ya wanadamu. Ukurasa huo huo unaongeza, "Ni upendeleo wa kila nafsi kuwa mfereji ulio hai ambao kwa huo Mungu anaweza kuwasilisha kwa ulimwengu hazina za neema yake, utajiri wa Kristo usiochunguzika. Hakuna kitu ambacho Kristo anatamani sana kama mawakala ambao wanawakilisha kwa ulimwengu roho na tabia Yake Kristo. Hakuna kitu ambacho ulimwengu unahitaji zaidi kama udhihirisho wa upendo wa Mwokozi kupitia ubinadamu.

Kungoja wahusika wakamilifu na kungoja njia za kuwasiliana na neema ya Mungu sio vitu viwili tofauti. Ni vipengele viwili vya kitu kimoja. Ni wazi kwamba Mungu anangojea watu ambao ni wakamilifu kwa kusudi fulani. Anawataka washinde dhambi si tu kwa furaha yao wenyewe bali pia kwa manufaa katika kuwakilisha kikamilifu tabia Yake nzuri kwa wenye dhambi walio mbali na karibu. Ni bora jinsi gani Waadventista Wasabato “wangeweza kuuambia ulimwengu kuhusu Masihi”—kwa kila mji, kila kijiji, na kila mtu ulimwenguni—kwa kuuishi upendo Wake kila siku katika nyumba zao wenyewe, vitongoji, mahali pa kazi, na popote pengine duniani kote? Je, Mungu atasubiri hadi lini?

Mapema mwaka 1884 Ellen White aliandika hivi: “Kama wote walivyofanya kazi kwa umoja katika mwaka 1844 wangepokea ujumbe wa malaika wa tatu na kuutangaza kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, Bwana angefanya kazi kwa nguvu na juhudi zao. Nuru ingaliiangazia dunia miaka mingi iliyopita wakazi wa dunia wangekuwa wameonywa, kufungwa kwa kazi kungekwisha kamilika, na Kristo angekuja kwa ajili ya ukombozi wa watu Wake[1] "miaka iliyopita," kabla ya 1884. Ni ndoto ya ajabu iliyoje! Tuseme kwamba Waadventista waliokuwa Wafuasi wa Miller laki moja huko Marekani na maelfu ya Waadventista huko Ulaya na kwingineko wangekubali na kutangaza ujumbe wa Sabato na Patakatifu.

Kulingana na kifungu hiki Kristo angeweza kuja kabla ya Vita vya wenyewe kwa wenyewe Marekani vya Mwaka 1861-1865! Kikosi cha Pickett inaweza kuwa kisingeenda kuandamana hadi wanajeshi kufa huko Gettysburg. Wanaume milioni moja wasingehitaji kuteseka kwenye matope huko Verdun katika vita vya kwanza vya dunia. Hiroshima na Nagasaki wangeweza kuponyoka mabomu ya atomiki katika vita vya pili vya dunia. Jinsi Mwenyezi Mungu anavyoshiriki huzuni ya kila mjane na yatima, jinsi ambavyo Bwana angetamani sana kumtuma Yesu kabla ya vita hivyo kupiganwa! Na ni dhahiri Yeye kama Baba—Baba anayewatarajia watoto wake, akiwasubiri watoto lakini, watoto walikuwa wenye kusitasita.

Kwa Waadventista wachache waliokubali ujumbe wa malaika wa tatu, barua ya Laodikia ilikuja kwa nguvu katika miaka ya 1850. Yesu alionekana kwenye milango ya mioyo yao akitafuta mlango wa kuingia nayo Mvua ya masika ya Roho Mtakatifu ilisubiri kwa umakini, tayari kutiririka kupitia kwao hadi kwenye ulimwengu wenye uhitaji. Ushindi wa mwisho ulikuwa mikononi mwao. Mungu alitoa "muda wa ujumbe kufanya kazi yake." Walisonga mbele kidogo, kisha wakapumzika wakiwa wameridhika.

Baba mwenye matarajio akisubiri lakini watoto wanasitasita. Katika Konferensi Kuu ya Minneapolis mwaka 1888 Roho Mtakatifu alizunguka kwa karibu akisubiri utayari wa watu. Kwa mara nyingine tena ulikuwa "wakati wa mvua ya masika." Faida ziliongezeka kwa kila mkono. Lakini badala ya “kuingia Patakatifu pa Patakatifu pamoja na Yesu,” waumini wengi sana walichagua Miaka Kumi na Sita ya Mgogoro wa kuhusiana na mada ya kuokolewa kwa njia ya Imani.

Kisha "Mama White," inaonekana akinena kwa niaba ya Kristo, Bwana akachora duara la upendo kubwa vya kutosha kuchukua watoto hawa wote wanaositasita. Mduara wa upendo umedumu, umeimarishwa na Ukweli wa Biblia na Shuhuda kwa Kanisa na kupanuka kama wimbi mwaka baada ya mwaka ili kuzingira na kujumuisha sehemu zinazopanuka za Kanisa la Waadventista. Tofauti huingia, lakini maelewano yanatawala. Wajumbe 1700, weusi na wa manjano, wekundu na weupe, walichangamana katika kikao cha Konferensi Kuu cha mwaka 1975, mada za karibu kila itikadi ya kisiasa duniani. Nilikaa na kamati ya uteuzi yenye wajumbe 173 Niliona, nikasikia, na kuhisi chini ya mawimbi madogo ya mabishano, ulivyotiririka mkondo wa imani na maelewano.

Katika simulizi hili la kitabu cha sasa kuhusiana na kisa cha Waadventista Wasabato tumekuwa tukiangalia tu "Kusudi" la kanisa lilivyoanza. Mianzo ni kwa makusudi maalum ya kanisa lao la dunia nzima la leo. Ugunduzi wa mapema wa Ukweli kuhusu Yesu na usadikisho, ujasiri, na ukarimu wa waanzilishi wao hufafanua vyema zaidi kile kinachofanya vuguvugu hilo liendelee kukua. Laiti tungekuwa na nafasi ya kutendea haki karne ya ishirini, kwa kusimulia visa vya imani na dhabihu na takwimu

za ukarimu na ukuaji zingeweza kuongezeka karibu kila mara. Hata uvumbuzi wa nuru iliyoongezeka zaidi unaweza kuchukua sura mpya.

Hapa na pale tayari tumerejelea baadhi ya maendeleo ya karne ya ishirini katika utume, kazi ya tiba, shirika, na elimu.

Tungependa kusema mengi; watenda kazi wenye mioyo mikubwa, wakitoa maisha yao, wakati mwingine kutoa maisha yao, kubeba ujumbe katika maeneo magumu.

Ikawa kwamba W. R. Smith Mmishenari wa Korea, anatembea, akiendesha baiskeli, akiendesha farasi, wakati mwingine mchana na usiku kwenye matope, mvua, na theluji, akiganda mikono na miguu, akiteleza kwenye ukingo wa korongo gizani, miadi ya mikutano, kuharibu afya yake, kuendeleza shule na makanisa.

Naye J. P. Anderson, mtendakazi wa China katika maisha yake yote, akichagua kubaki wakati majeshi ya adui yalipomshinda Canton, akitumaini kwa maombi, busara, na ujasiri kuilinda hospitali ya misheni dhidi ya waporaji—na kurudisha taasisi hiyo kwa kanisa miaka mingi baadaye bila kupoteza taulo au shuka la kitanda.

Uadventista wa karne ya ishirini umekuwa wa C. C. Crisler akiimba kwa upole, "Njiani Mwokozi Huniongoza," alipokuwa amelazwa akifa kwa homa ya mapafu (Pneumonia) huko Chona katika maeneo ya ndani ya Uchina na kufa. Na W. H. Anderson akiwa safarini, na akizinduka kutoka katika kupoteza fahamu wakati wa shambulio baya la ugonjwa wa kuhara damu ili kusikia wabebaji wake waongofu wa Matebele wakiimba, "No, Never Alone/Hapana hautakuwa peke yako" na kupata nafuu. Na G. McLaren, chombo chake kilichozungukwa na Solomon Islanders wenye ukatili, wakiimba, "Popote Na Yesu Ninaweza Kwenda" - na kutua salama.

Beni Tavondi, mzaliwa wa Fiji, alikuwa mwongofu wa kwanza, baada ya miaka kumi ya kazi ya taabu huko Papua, na huyu mwongofu wake wa kwanza wa Kiadventista alipokuwa amelala akifa kutokana na kuumwa na nyoka. Naye Bi. Fika Mitieli, mmishenari mwingine wa Kifiji aliyeishi Papua, akiwafundisha wanawake na watoto vijijini, akinyakua mikuki kutoka kwa wapiganaji kwenye njia za msituni, akishiriki kwa mafanikio Ukweli juu ya Yesu katika Patakatifu.

Naye Billiat Sapa, mzaliwa wa Afrika, akisimamia kazi katika bonde lenye majimaji huko Nyasaland, akiishi na mke wake na watoto wawili kwenye jukwaa kwenye mti kwa sababu wanakijiji walikataa kuwakaribisha; akishuhudia watoto wote wawili wakifa, yeye na mke wake wakikataa kurudi nyuma; akiangalia mke wake akifa, na yeye akikataa kugeuka nyuma; hatimaye akawasadikisha wanakijiji kwamba anawapenda na kwamba Mungu aliwapenda, na kufanikiwa kuanzisha shule kadhaa.

Leo, bila shaka, watoto hutazama TV katika Afrika  na Fiji na pia katika Ulaya na Amerika Kaskazini, hivyo misheni ya Waadventista katika karne ya ishirini imelazimika kupima mambo ya teknolojia ya kisasa katika nchi za kale. Lakini hata katika nyakati za kisasa majanga ya zamani bado yanatokea, na Uadventista wa karne ya ishirini umekuwa na watu kama L. H. Christian ambaye katika njaa kuu ya Urusi ya 1920, akijua kwamba homa ya matumbo iliambukiza idadi kubwa ya watu, alienda Urusi kwa wiki tatu zilizoonekana kuwa ni ndefu, ili kuwatia moyo waumini, huku watu wa nyumbani wakiomba na kufunga. Na mkuu wa chuo asiyeweza kushindwa, huku akijawa na maumivu makali na kuwajibika kwa wanafunzi 1000, alitafuta mchele wa kutosha kulisha wanafunzi katika njaa ya miaka ya 1970.

Tusemeje basi, pale ambapo tungeangalia maelfu ya vijana katika vita vibaya zaidi vinavyojulikana katika historia, ambapo vijana wenye ujasiri wa kutosha kufuata dhamiri zao kuhusu kusimama kwaajili ya imani, na huku wakipigwa risasi kwa wakati mmoja, ikiwemo wanaume kumi na wanne waliofungwa sehemu tofauti katika gereza la kijeshi, kila mmoja akiarifiwa kwamba marafiki zake wote walikuwa wameikana Sabato, ili kuleta woga. Watu ambao walikuwa wakiimba kwa sauti za chini sana wimbo wa sala ya jioni huku jua likitua na kuwasikia wengine wote, wakiwa peke yao katika vyumba vyao kumi na tatu wakijiunga na wimbo huu.

Naye Desmond Doss, asiyepigana kwa ajili ya dhamiri yake (Conscience Objector) huko Okinawa Japan, aliyepata Nishani ya Heshima ya Bunge (Congress) kwa kuwaokoa watu sabini na watano waliojeruhiwa huku kikosi cha adui kikimkabili kwa risasi, makombora na mabomu ya kutupa kwa saa kadhaa.

Katika Uadventista wa Siku ya Saba katika karne ya ishirini, kumekuwa wenyeviti wa Konferensi Kuu, kama vile W. A. Spicer (1922-1930), waliopendwa sana, wakisafiri kila mahali, wakijua kila mfanyakazi kwa jina, wakipeana zawadi kidogo kwa watoto wa wamishenari, na kila mara wakinunua tiketi za kusafiria katika daraja lililo nafuu zaidi (3rd class). Wakati fulani wenyeji wake walipopinga kwamba mtu muhimu sana amefika kwa treni kwenye daraja la tatu, aliomba msamaha kwa upole, "Samahani; sikujua kulikuwa na daraja la nne." Na J. Lamar McElhany (1936-1950), pia mpendwa aliyeshika Uenyekiti wa Konferensi Kuu, akilia baada ya kuchaguliwa tena kwa mara ya pili, akiwa amezidiwa na ukubwa wa kazi yake ambayo kwa kiasi kikubwa zilikuwa kazi kubwa miongoni mwa viongozi waliowekwa wakfu.

Uadventista katika karne ya ishirini umejitolea kuwa  sio wa watu wa kawaida—kama askari hodari waliotajwa hivi punde, kama vile maelfu katika Inter-Amerika na Ufilipino ambao wameongeza kasi ya ukuaji wao kwenye rekodi za dunia, na hakika ni idadi isiyohesabika, washiriki wanaofundisha na kusimamia shule za Sabato, kushona nguo za maskini, kufundisha shule, au kuendesha taasisi za Waadventista Wasabato kwa ujumla.

Walei wengi wametoa michango ya pekee, kama vile Jasper Wayne, mkuza mimea wa Iowa, ambaye wakati fulani alijadiliana na mke wake nini zaidi wangeweza kufanya kwa ajili ya Bwana, Mkewe alipendekeza kwamba waagize nakala 100 za toleo maalum la 'Signs of the Times,' nayo ingekuwa sawa. Naye akiwaza kuwa nakala ishirini na tano zaidi ingefaa zaidi, walikubaliana kuagiza nakala hamsini. Mwendelezo huu huadhimishwa kila mwaka wakati wa mikutano.

Baadhi ya waumini wa Kiadventista katika karne ya ishirini wamefurahia mwongozo wa ajabu kutoka kwa bwana Charles Ashcroft wa Carmel, Australia, alijiuliza mnamo 1906 kama angetoa shamba lake kubwa la tufaha kwa ajili ya shule ya sekondari. Aliomba Mbinguni ishara: mvua ya radi kutoka anga ya bluu safi, ndani ya wiki moja. Katika muda wa juma moja wingu jeusi lilitokea kwenye anga ya bluu, likapanda juu ya kilima hadi kwenye bonde lake, likatoa mng'aro mkali na mngurumo juu ya nyumba yake, kisha likateleza chini kwenye bonde hilo. Kaka yake alikimbia kutoka shamba la karibu huku akipiga kelele, "Je umeona kilichotokea?! "Ndiyo nimeona," alijibu Charles; "ni ishara kwangu kutoa ardhi yangu kwa Bwana." Chuo cha Carmel kimesimama kwenye ardhi hiyo leo.

Takwimu zinathibitisha maendeleo ya kutia moyo. Michango imeongezeka kutoka dola nusu milioni mwaka 1895 hadi milioni 300 mwaka 1975 [Na sasa ni zaidi ya bilioni tatu duniani]. Usajili katika shule za Waadventista Wasabato umeongezeka kutoka takriban wanafunzi 1300 mwaka wa 1890 hadi takriban 400,000 na sasa ni zaidi ya milioni mbili.

Mnamo 1853 mashine ndogo ya uchapaji ya Washington huko Rochester ilitoa nakala moja kwa dakika, karatasi sitini kwa saa, kwa bidii kubwa kiasi kwamba vijana walioendesha baada ya miezi michache waliugua. Katika karne ya ishirini gazeti la "These Times" limefikisha idadi ya nakala 200,000 kila mwezi, gazeti la "Signs of The Times" nakala 350,000, gazeti la "Liberty" limefikia nakala 500,000. Matangazo ya redio na televisheni yameongezeka kote ulimwenguni. "The Quiet Hour" pekee hutumia zaidi ya stesheni 300, "Voice of Prophecy," zaidi ya ya nakala 800 [na bado kuna zoom, YouTube, Facebook, Instagram, email na simu za mikono].

Vitabu milioni sitini vya "Uncle Arthur" S. Maxwell vimebeba maadili ya Kikristo na ujumbe wote wa Biblia kwa familia zinazozungumza lugha thelathini na mbili tofauti [Na sasa inabidi tuendelee kuandika vitabu vya watoto kwa Kiswahili pia! Net Events zimeleta watu wengi kwa Bwana, mamilioni wamebatizwa kwa net events]. "Steps To Christ" imechapisha nakala milioni mia moja na kutafsiriwa katika lugha zaidi ya 100.

Takwimu za ongezeko la waumini pia zinavutia, kwa kiasi fulani. Katika mwaka 1863 kulikuwa na Waadventista 3500 katika idadi ya watu duniani ya bilioni. Huo ulikuwa

uwiano wa muumini mmoja kwa watu milioni tatu. Kufikia mwaka wa 1975, wakati ulimwengu ulikuwa umefikia bilioni nne, uwiano ulikuwa umeboreshwa na kufikia muumini mmoja kati ya watu 1600. Ikiwa kasi ya ukuaji ingebaki tu kwa sasa asilimia 5.5 kwa mwaka hadi AD 2000, wakati ulimwengu utakuwa na watu bilioni 6.5, panapaswa wawepo washika Sabato milioni 9, au mmoja kwa kila nafsi 700 [hata leo tuna waumini zaidi ya milioni 23. Ni maendeleo mazuri, Bwana asifiwe, lakini haitoshi [kwani tuna watu bilioni nane sasa].

Ni kweli mwendo ni  polepole sana. Kama kanisa lingeendelea kukua kila mwaka tangu 1880 kwa kiwango cha asilimia 11.1 cha miaka ya 1870, lingeweza leo kuhesabu si washiriki 2,500,000 bali washiriki 275,458,110! "Mbingu yote" imekuwa "ikingoja" kwa muda mrefu sana. Kazi lazima ishike kasi na "kuenea kama moto kwenye makapi ya ngano" na itafanya hivyo, kulingana na Ellen White, "wakati nguvu za Bwana zinapounganishwa na juhudi za kianadamu."[2] "Mungu atafanya kazi ikiwa tutampa vyombo yaani sisi wenyewe."[3]

Mnamo 1845 Ellen akiwa binti mdogo, aliona jets za mwanga zikitokea mahali baada ya mahali hadi zikajaza ulimwengu mzima.  Hizi ziliwakilisha ahadi katika Ufunuo 18:1, “Nikaona malaika mwingine akishuka kutoka mbinguni, mwenye mamlaka kuu;” Na bila shaka utukufu wa malaika unaangazia utukufu wa Mungu. Malaika huyu wa Ufunuo 18, kama malaika watatu wa Ufunuo 14:6-12, ni mfano wa watu wanaobeba ujumbe (Angelos katika Kigiriki maana yake ni mjumbe. “Utukufu wa Mungu” kimsingi ni tabia Yake tukufu, iliyojaa neema na Ukweli (Tazama Kutoka 33 na 34). Kwa hiyo dunia inapaswa kuangazwa kwa utukufu wa Mungu wakati kanisa la Mungu litakapojazwa na nguvu za Mungu na kuzalisha kikamilifu tabia ya Mungu.

Utukufu ambao Ellen aliuona uking'ara kutoka kwa Sabato katika Patakatifu pa Patakatifu sana, mfano wa utakatifu wa upendo wa Mungu Mwenyewe, siku moja utang'aa kutoka kwenye nyuso na maisha na midomo ya watu wa Mungu wanaoitunza Sabato. Kuitunza Sabato takatifu, kwa wanaume na wanawake, wavulana na wasichana, kutawafanya wenyewe kuwa watakatifu.[4] "Dunia 'itaangazwa kwa utukufu Wake,” anaeleza Ellen White. "Roho wa Bwana kwa neema atabariki vyombo vilivyowekwa wakfu vya kibinadamu kiasi kwamba wanaume, wanawake, na watoto watafungua midomo yao na kutoa sifa na shukrani, wakijaza dunia ujuzi wa Mungu, na utukufu Wake usio na kifani."[5]

Kushiriki katika kilele hiki kitukufu cha vuguvugu la marejeo ya Yesu, hakutafungwa kwa washiriki wake wa sasa. Sivyo kabisa! Inapatikana kwa kila mtu anayepumua. Nchi na vyote viijazavyo ni mali ya Bwana. Mungu ni Baba wa kila mtu, na punde tu mtu yeyote anaposikia neno, yeye pia, anaweza kushiriki furaha ya kupata nguvu yake ya kubadilisha na furaha kubwa zaidi ya kuipitisha kwa wengine. “Roho wa Mwenyezi anatembea juu ya mioyo ya watu, na wale wanaoitikia mvuto wake

wanakuwa mashahidi wa Mungu na ukweli wake, njia ya wokovu kwa njia ya Kristo na wanapoendelea kuiacha nuru yao iangaze, kama walivyofanya wale waliobatizwa kwa Roho siku ya Pentekoste, wanapokea zaidi na zaidi nguvu za Roho dunia itaangazwa kwa utukufu wa Mungu."[6]

"Watumishi wa Mungu, nyuso zao zikiwa zimeangazwa na kung'aa kwa utakaso mtakatifu, wataharakisha kutoka mahali hadi mahali ili kutangaza ujumbe kutoka mbinguni. Kwa maelfu ya sauti, duniani kote, onyo litatolewa. Miujiza itatendeka, wagonjwa wataponywa, na ishara na maajabu zitafuatana na waaminio ... ".....  Miale ya nuru itapenya kila mahali, Ukweli utaonekana katika uwazi wake, na watoto waaminifu wa Mungu watakata kamba zilizowashikilia… ... Ukweli ni wa thamani zaidi kuliko vyote. Ijapokuwa mashirika yakiunganishwa dhidi ya Ukweli, idadi kubwa husimama upande  wa Bwana."[7]

Ukweli ni wa thamani zaidi kuliko yote. Ukweli muhimu kuhusu Yesu, kuhusu kile ambacho amefanya zamani na kile anachofanya sasa. Lazima iwe ni Ujumbe wa malaika wa kwanza kuhusu injili ya milele ya msalaba wa Yesu na ujumbe kwamba Saa ya hukumu Yake imekuja, na ujumbe wa malaika wa pili, akiwaita watu wajitenge na kila sanamu inayowazuia, na ujumbe wa malaika wa tatu, unaoonya dhidi ya mifumo ya ibada ya uongo, kuwageuza watu na kuwaelekeza kwenye amri za Mungu na imani ya Yesu, na Haki kwa imani.

Tangu Oktoba 22, 1844, Yesu katika Patakatifu pa Patakatifu amekuwa akielekeza uangalifu wa watu kwenye Sabato, si kwa sababu tu ni siku ya saba bali kwa sababu inawakilisha njia ya pekee ya maisha kama ya Kristo, kigezo kikuu zaidi. kutenganisha mema na mabaya katika siku za mwisho. Yesu anafanya kazi ya kufuta dhambi, si tu katika vitabu vya mbinguni bali pia katika maisha ya watoto Wake, ili waweze kuwa washindi, watakatifu, kama Kristo. Kupitia kwa mwakilishi wake, Roho Mtakatifu, anabisha juu ya mioyo ya wafuasi wake, akitafuta kuwasaidia kutanzua maisha yao katika viwango vya ndani zaidi na kutamani kuwajaza na Roho Mtakatifu.

Anajua bado ni "vyombo vya udongo" ambavyo bado vinahitaji kuoshwa; Naye Anaviosha kwa "sabuni ya kuoshea" mpaka ziwe zenye harufu nzuri na safi, kwa sababu anataka kuvijaza. Lakini hataki kuvijaza kama vyungu na sufuria lakini maji chini ya shinikizo hujaza na bomba la bustani na kutiririka ndani yake kuleta "furaha na baraka kwa mioyo ya wanadamu." Kama vile mwanga unavyojaza balbu ya umeme na kuangaza nuru katika pande zote nje yake, ndivyo Yeye Anavyotaka watu safi ambao kupitia kwa macho na midomo na mikono na miguu Yeye anaweza, kuruhusu, bila kizuizi, kuangaza kwa ulimwengu utukufu Wake.

Nihuishe kwa Pumzi ya Roho Wako Bwana, Mpaka niwe Wako kabisa, Mpaka hadi sehemu yangu hii ya dunia langaze kwa moto Wako wa mbingu/Kiungu. Wakati wa marejeo ya pili ya Yesu kila mtu ambaye bado Yuko katika kupenda dhambi lazima aangamizwe. Hata hivyo, bila kutamani kwamba yeyote aangamie, Mungu anamwalika kwa bidii kila mtu anayeelewa Ukweli wa siku hizi kuhusu Yesu Kristo kuuishi na kuwaambia wengine. Yeye Anawataka wajenge shule ambazo zinaweza kufundisha vijana wapate mafunzo ya uzima; kuanzisha mitambo ya uchapishaji na vituo vingine vya mawasiliano ambayo yanaweza kuchapisha na kusambaza ujumbe wa marejeo; kudumisha taasisi za tiba/matibabu ambapo huruma ya Kristo inaweza kuonyeshwa hasa na watu wanaoweza kujifunza jinsi ya "kujisikia vizuri ili waweze kuwa wazuri na wema."

Waadventista Wasabato wanaamini kwamba wameitwa kuutangaza ujumbe wa mwisho wa Mungu. Kwa kiwango cha kuvutia wamejitolea kufanya kazi kwa miaka mingi, na inaonekana Mungu amebariki kazi yao kwa ishara nyingi za majaliwa Yake na miujiza ya neema. Lakini huo muujiza mkuu ambao kanisa lao liliitiwa kuwepo, yaani ujio wa pili wa Kristo, bado unangojewa. Kizazi cha sasa cha waumini, hebu na kimpokee Yesu maishani mwao, na kisha, midomo yao iwake moto kwa Roho Mtakatifu, maisha yao yawake moto na kutoa mng'ao wa utukufu Wake, ili injili isonge mbele hadi kufika hata kwa mtu aliye mbali zaidi duniani. Na kwa haraka "Wauambie ulimwengu kuhusu ujio wa Masihi" ili Yesu Kristo aje hatimaye.

*Vidokezo:*

*1. Ellen G. White, Roho ya Unabii, gombo 4. (Battle Creek, Mich.: The Steam Press of the Seventh-day Adventist Publishing Association, 1870-1884), vol. 4, uk. 291; cf. Pambano Kuu, uk. 458*

*2. Ellen G. White, Selected messages, bk. 1, uk. 118*

*3. Ellen G. White, Testimonies, vol. 9, uk. 107*

*4. Ellen G. White, The Desire of Ages, uk. 283*

*5. Ellen G. White, Comments, Seventh-day Adventist Bible Commentary, vol. 7, uk. 984*

*6. Ellen G. White, The Acts of the Apostles, uk. 54*

*7.Ellen G. White, Pambano Kuu*